Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

# BUNGE LA TANZANIA

## MKUTANO WA KUMI NA MBILI

**Kikao cha Kumi na Tatu – Tarehe 27 Juni, 2008**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

## D U A

*Naibu Spika (Mhe. Anne S. Makinda) Alisoma Dua*

## MASWALI NA MAJIBU

Na. 114

**Ukosefu wa Barabara - Ipera**

**MHE. GRACE S. KIWELU (K.n.y. MHE. HALIMA J. MDEE)** aliuliza:-

Kwa kuwa Vijiji vya Mang'aliza, Nzugilo, Vikundi, Idodoma na Malolo vilivyopo Wilaya ya Mpwapwa Jimbo la Kibwake Kata ya Ipera ni miongoni mwa Vijiji vinavyozalisha mahindi, maharage, vitunguu na viazi ulaya kwa wingi sana na kwa kuwa ukosefu wa barabara ndio chanzo kikuu kinachorudisha nyuma Maendeleo ya wakazi wa maeneo husika:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kuisaidia Halmashauri ya Wilaya ya Mpwapwa kutengeneza barabara ya Chilando, Kambarage, Sokoine hadi Kinusi, Nzugilo, Vikundi, Ipera hadi Kinusi na Idodoma, Malolo hadi Ipera?

(b) Je, Serikali ina mpango gani wa kuvipeleka vijiji hivyo Mikoa ya Iringa au Morogoro kama utengenezaji wa barabara hizo hauwezekani kwa kuwa mpaka leo wananchi wa vijiji husika hupata huduma zao zote za kijamii kutoka Mikoa hiyo?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Halima James Mdee, Mbunge wa Viti Maalum lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba vijiji alivyovitaja Mheshimiwa Mbunge vinahitaji barabara ili kurahisisha mawasiliano pamoja na huduma nyingine za kijamii, kisiasa na kiuchumi. Serikali inatambua umuhimu wa barabara kama kiungo muhimu cha uchumi kwa wananchi wake.

Hatua mbalimbali zimekuwa zikichukuliwa katika kuhakikisha kuwa barabara za Wilaya zinatengenezwa kwa kutumia fedha za kutoka Serikali Kuu na kuhamasisha wananchi kutengeneza barabara za vijiji kwa kutumia nguvu zao wenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na umuhimu wa barabara ya Makose-Malolo-Idodoma yenye urefu wa kilomita 79, Serikali imekuwa ikichukua hatua kwa awamu katika kufungua mawasiliano katika barabara hiyo kwa kutenga Bajeti.

Kwa mwaka wa fedha 2007/2008, Serikali ilitenga kiasi cha Sh. 95.5m/= kufanya matengenezo ya maeneo korofi ya barabara hii na hivi sasa Mkandarasi anaendelea na kazi. Serikali itaendelea kufanya matengenezo ya barabara hizo kulingana na upatikanaji wa fedha.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu rai ya Mheshimiwa Mbunge kuvihamishia Mkoa wa Iringa na Morogoro vijiji alivyovitaja , suala la msingi hapa ni kuboresha huduma mbalimbali za kijamii zikiwemo barabara ili kuwavutia wananchi kuendelea kuishi katika vijiji hivyo.

Aidha, Serikali ina utaratibu wake wa kugawa mipaka ya Wilaya Mpya pale inapoona inafaa kwa kutumia vigezo maalum vya kitaalam na hasa baada ya kufanya utafiti wa kina juu ya kugawa mipaka hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sasa Serikali haina mpango wa kuvihamisha vijiji hivyo vya Wilaya ya Mpwapwa kwenda Mikoa ya Iringa na Morogoro.

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa nina maswali ya nyongeza. Kwanza, nimshukuru sana kwa jibu lake zuri kwa sababu jukumu la kugawa Vijiji na Kata ni jukumu la Serikali na siyo Mheshimiwa Mbunge kuomba vijiji vipelekwe mkoa mwingine kutoka katika Wilaya ya Mpwapwa.

Sasa kwa kuwa Serikali imetenga Sh. 768m/= kwa ajili ya kutengeneza barabara za Wilaya za Mpwapwa ikiwemo barabara hii ya Mang'aliza-Nzugilo, barabara za Kata ya Mima, Matomondo. Je, Mheshimiwa Naibu Waziri atakubaliana nami kwamba kwa kuwa fedha inayotengwa ni kidogo, asilimia thelathini tu ndiyo zinakwenda Serikali za

Mitaa na asilimia sabini zinabaki *TANROAD*. Je, sasa atakubaliana na ushauri wangu kwamba asilimia arobaini au hamsini ya fedha ambazo zinatengwa katika Halmashauri zetu zipelekwe huko badala ya asilimia thelathini ambayo kwa kweli ni fedha ambazo hazitoshi na barabara nyingi zimeharibika hapa nchini?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote kwamba naomba nichukue fursa hii kwa niaba ya Serikali na kwa niaba ya Waziri Mkuu kumshukuru Mheshimiwa Mbunge kwa shukrani ambazo amezitoa hapa.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, Mheshimiwa Lubeleje anazungumzia kuhusu fedha ambazo zimetengwa kwa ajili ya Wilaya yao ya Mpwapwa. Suala la kupeleka asilimia thelathini au arobaini au hamsini linategemeana na mpango ambao wamejiwekea katika Halmashauri yao. Kwa hiyo, suala la kipaumbele mara nyingi linatokana na mpango ambao wamejiwekea wao wenyewe katika Halmashauri ya Wilaya ya Mpwapwa. Kwa hiyo, hatuoni tatizo lolote lile kama wao watafika mahali wakaona kipaumbele kinahitaji kupelekwa kwenye barabara yoyote ile wanaweza kufanya hivyo ili mradi iwe ni ndani ya Bajeti yenyewe.

**NAIBU SPIKA:** Hapana hujajibu. Yeye anachokisema mgao wa sasa hivi asilimia thelathini katika *Road Fund* inakwenda Halmashauri, asilimia sabini inabakia Serikali Kuu. Yeye anapendekeza kwamba mgao wa asilimia thelathini uongezeke, hilo ndiyo swali. (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kufafanua swali lake nilikuwa sikumpata vizuri. Sasa hili litakuwa ni suala la bajeti maana yake siwezi nikazungumza hapa kwamba zinaweza kuongezeka. Hili ni jambo ambalo linazungumzika, tutakwenda, tutakaa lakini kwa sasa hivi Bajeti hii itabaki hivyo hivyo kama ilivyo. (*Makofi*)

**MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri nilitaka kwanza kabisa kwa ajili ya kuweka rekodi sawasawa nifanye masahihisho ya muuliza swali maana yake eneo linalozungumzwa ni eneo lililopo katika Jimbo langu la Kibakwe.

Sina kijiji kinaitwa Chilando, Kambarage, Sokoine na wala jiografia katika mtiririko wa vijiji vilivyotajwa hapa hauko sawasawa. Swali, tumeomba barabara hii kwa sababu ya umuhimu si kwa utaratibu uliotajwa hapa bali kwa umuhimu wake maana ya kutoka Malolo kwenda Ruaha Mbuyuni na Serikali ilikuwa imekubali kwamba italifikiria wazo hili.

Je, katika Bajeti ya mwaka huu barabara imezingatiwa kupandishwa daraja na kuwa ya mkoa ili tuweze kusaidiwa kwa sababu Halmashauri ina uwezo mdogo?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa naomba nimshukuru kwa kusahihisha kwa sababu yeye anatoka Kibakwe anavijua vijiji hivi vizuri zaidi. Kwa hiyo, kwa vile inaingia kwenye *Hansard* sisi ndio tunachukua hayo ndiyo majina hasa yaliyo kule Kibakwe.

Kuhusu suala la kwamba, wameomba barabara hii ipandishwe daraja ili iweze kuingia katika *TANROADS* suala hili linapitia katika mchakato wa Wilaya yenyewe halafu unakwenda *TANROADS* kama tulivyojibu hapa na baadaye linakwenda katika mamlaka kuu kwa maana ya kufanya uamuzi huo.

Nitapenda baadaye nicheki kujua hii imepewa hiyo *status* lakini ninavyojua kwa sasa hivi iko katika mchakato na kama wameomba itakuwa katika mpango wa kuhakikisha kwamba inawekwa katika daraja hilo wanalolizungumzia.

Na. 115

**Gari Kituo cha Afya cha Engarnaibor**

**MHE. BENEDICT N. OLE-NANGORO (K.n.y. MHE. MICHAEL L. LAIZER)** aliuliza:-

Kwa kuwa Kituo cha Afya Engarenaibor kinahudumia Kata za Matale, Mundarara, Gilaylumbwa na kwa kuwa kituo hicho kiko mbali na hospitali ya Wilaya ambayo zamani ilikuwa Monduli:-

(a) Je, ni lini Serikali itakipatia kituo hicho gari la wagonjwa ili kunusuru maisha ya wagonjwa hususan akina mama wajawazito na watoto wanaopata rufaa kwenda hospitali ya Wilaya Mkoani Arusha?

(b)Je, ni lini Serikali itapeleka watumishi wa kutosha kama Madaktari/Waganga na wauguzi kwenye kituo hicho?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu naomba kujibu swali la Mheshimiwa Michael Lekule Laizer, Mbunge wa Longido lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatambua tatizo la usafiri wa wagonjwa linaloikabili Halmashauri ya Wilaya ya Longido hususan Kituo cha Afya cha Engarnaibor. Halmashauri ya Wilaya ya Longido ina magari mawili aina ya *Land Cruiser Hardtop* yanayotumiwa kwa ajili ya shughuli za Afya Wilayani.

Wagonjwa kutoka katika zahanati zilizo katika Vijiji vya mbali na Kituo cha Afya hukodisha magari ya watu binafsi kwenda kutafuta huduma katika Kituo cha Afya cha Engarnabor, Longido ama hospitali ya Rufaa ya Kibongoto.

Kimsingi kila Kituo cha Afya kinapaswa kuwa na miundombinu mizuri ya mawasiliano kwa maana ya uwepo wa angalau gari moja kwa ajili ya kusafirisha wagonjwa, barabara zenye kupitika nyakati zote pamoja na mawasiliano ya simu ama redio ya upepo (*Radio Call*).

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali pia inatambua umuhimu wa kuwa na usafiri wa uhakika katika Vituo vya Afya kwa ajili ya kusafirisha wagonjwa ikiwa ni pamoja na Kituo cha Afya cha Engarnaibor. Tatizo kubwa linaloikabili Serikali ni ufinyu wa bajeti. Serikali inashauri Halmashauri ya Wilaya ya Longido iweke kipaumbele cha kununua gari hilo katika Bajeti yake ya mwaka 2009/2010.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, kulingana na ikama ya watumishi wa Kituo cha Afya, Kituo kinapaswa kuwa na watumishi wapatao 29 wa kada mbalimbali za afya wakiwemo Madaktari Wasaidizi wawili, Maafisa Tabibu watatu, Wauguzi kumi, wahudumu wa Afya wanne na watumishi wengine wapatao kumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kituo cha Afya cha Engarnaibor kina watumishi nane tu ambao kati yao watumishi wawili wako masomoni. Kwa mwaka wa fedha 2007/2008, Serikali ilipeleka watumishi watano wa Afya katika Halmashauri ya Wilaya ya Longido ambapo hadi sasa ni Mtumishi mmoja tu (Afisa Tabibu) aliyeripoti katika kituo cha kazi. Halmashauri pia imewasilisha mahitaji ya watumishi katika Ofisi ya Katibu Tawala Mkoa ili taratibu za kuomba kibali cha watumishi hao ziweze kufanyika.

**MHE. BENEDICT N. OLE-NANGORO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kwanza nimshukuru Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri lakini naomba niulize swali la nyongeza. Hali ya watu wa Engarnaibor na maeneo yaliyotajwa kwa kweli kiafya ni mbaya sana huduma hazipo Je, Naibu Waziri kabla ya Wauguzi na Waganga kupatikana na gari hilo la wagonjwa, anaweza kunihakikishia kwamba wenyeji wa vijiji hivyo wanapata huduma za msingi hasa chanjo kwa watoto na huduma za akinamama kabla ya huduma hizo za kudumu kupatikana? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** Mheshimiwa Naibu Spika, jambo ambalo Mheshimiwa Ole-Nangoro analizungumzia hapa linalohusu chanjo kwa ajili ya watoto ni jambo la msingi sana ambalo kwa kweli hatuwezi kukataa hapa kwamba hatutasaidia katika jambo hilo.

Tatizo lililopo hapa kubwa ni usafiri ulioko pale lakini vipo vituo vya afya ambavyo viko karibu pamoja na zahanati. Kwa hiyo, tutahakikisha kwamba huduma hii ya kupata chanjo kwa ajili ya watoto inapatikana. (*Makofi*)

**MHE. SIJAPATA F. NKAYAMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi. Kwa kuwa Mheshimiwa Waziri Mkuu kabla hajawa Waziri Mkuu alipata nafasi na kwenda kutembelea Mkoa wa Rukwa, alitoa amri akasema kuwa ni marufuku kwa Halmashauri yoyote kutotoa mafuta kwa Vituo vya Afya lakini katika kijiji cha Bitare kuna Kituo cha Afya ambacho wagonjwa wakipata rufaa kwenda Hospitali ya Maweni huwa wanajinunulia mafuta kwa ajili ya kupata usafiri. Je, Mheshimiwa Naibu Waziri anawaambia nini viongozi waliopo katika Halmashauri hiyo? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa naomba niseme hapa kwamba kama Mheshimiwa Waziri Mkuu alikuja na akatoa maelekezo kwamba Vituo hivi viwe vinapata mafuta na mafuta yapatikane bila kuhitaji kwenda kwa wananchi, hayo ni maelekezo na maagizo ya Serikali lazima yatekelezwe. Hilo la kwanza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, kwamba nasema nini katika Halmashauri hii nadhani anazungumzia Halmashauri ya Kigoma, maelekezo ambayo tunatoa hapa ni kwamba, huduma hizi ambazo zinatolewa kwa ajili ya watoto wadogo wale wenye vifua vikuu na wale wengine ambao umri wao umepita sera yetu inatamka waziwazi kwamba huduma hizi watapata bure. Kwa hiyo, maelekezo ambayo nayatoa hapa ni kwamba Halmashauri ihakikishe kwamba mafuta yanapatikana ili majokofu yaweze kufanya kazi kama inavyotakiwa.

Na. 116

**Ujenzi wa Daraja la Mto Bubu**

**MHE. DAMAS P. NAKEI** aliuliza:-

Kwa kuwa ujenzi wa Daraja la Mto Bubu sehemu ya Udagati ni ombi la siku nyingi la wananchi wa Jimbo la Babati Vijijini na kwa kuwa Serikali ilikwishaahidi kulijenga daraja hilo:-

Je, kwa nini Serikali inaona vigumu kutoa fedha kwa awamu ikianza na fedha za usanifu ili hatimaye kujenga daraja hilo ili kuondoa tatizo hilo?

**NAIBU WAZIRI WA TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu naomba kujibu swali la Mheshimiwa Damas Pascal Nakei, Mbunge wa Babati Vijijini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kuwa Halmashauri ya Wilaya ya Babati katika mwaka wa fedha 2007/2008 iliwasilisha maombi ya fedha ya Sh. 134,498,100/= kwa ajili ya ujenzi wa daraja la Mto Bubu lililoko katika barabara ya kutoka Hanang – Bubu - Duru hadi Riloda. Fedha zilizotolewa kwa ajili ya matengenezo ya barabara kwa Halmashauri ya Wilaya ya Babati kwa mwaka 2007/2008 ni Sh. 238.93m/= kutoka kwenye Mfuko wa Barabara na Sh. 29,848,338/= kutoka program ya usafiri katika Halmashauri.

Kwa mwaka wa fedha 2008/2009 Halmashauri ya Wilaya ya Babati imetengewa jumla ya Sh. 405.71m/= kutoka Mfuko wa Barabara. Kati ya fedha hizo Sh. 265.71 kwa ajili ya matengenezo ya barabara zenye urefu wa kilomita 179 na makalvati Sh. 140m/= kutoka Program ya Usafiri katika Halmashauri (*Local Government Transport Programme)* kwa ajili ya matengenezo ya maeneo korofi. Nashauri Halmashauri ya Wilaya ya Babati kuweka katika vipaumbele yake ujenzi wa daraja la Mto Bubu.

**MHE. DAMAS P. NAKEI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza. Nianze kwa kumshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri ya swali langu. Swali la kwanza, kwa sababu fedha zilizotolewa sasa hivi hazijaainisha kama daraja hilo ni sehemu ya Bajeti hiyo. Je, Serikali itatoa kibali ili sehemu ya fedha zilizotolewa tuweze kulipangia matengenezo au ujenzi wa daraja hilo?

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, kwa kuwa ombi hili la wananchi wa vijiji vya Halmashauri ya Wilaya ya Babati Vijijini ni la siku nyingi tangu mwaka 2003 na kwa kuwa leo tunapitisha Bajeti ya Wizara hii. Je, Serikali kwa uwezo ilionao na kwa huruma yake inaweza kupokea ombi langu maalum ambalo nalitoa sasa hivi ili kwa uwezo ilionao ikatoa kiasi cha fedha ambazo zinaweza kuanza ujenzi wa daraja hili mwaka ujao wa fedha? (*Makofi*)

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, jukumu la kupanga vipaumbele vya fedha za barabara ni jukumu la Halmashauri husika. Kwa hiyo, ni Halmashauri yenyewe ambayo inaweza kutoa kipaumbele kwa hilo daraja la Bubu kwa sababu ni muhimu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ombi lake la pili, kwamba anatoa sasa hivi ombi maalum, niseme tu hata katika maandiko matakatifu wanasema aliyenacho huongezewa. Kwa hiyo wenyewe kama watatenga fedha kidogo kwa ajili ya daraja hilo sisi kama Serikali Kuu tunaweza kuangalia uwezakano wa ku- *top up* ili daraja hilo liweze kujengwa. (*Makofi*)

**MHE. FELISTER A. BURA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo tu la nyongeza. Kwa kuwa tatizo la daraja la Mto Bubu katika Wilaya ya Babati Vijijini ni sawa na tatizo la daraja la Mto Kolo katika Wilaya ya Kondoa na katika barabara inayotoka Kondoa kwenda Babati.

Naomba sasa ni lini daraja hilo litatengenezwa kwa sababu sio ombi la kwanza katika Bunge lako Tukufu na daraja hili ni tatizo la muda mrefu zaidi ya miaka mitano sasa?

**NAIBU SPIKA:** Lakini ukishataja daraja maalum Waziri akaweza kulijua sasa hivi atakuwa *computer* kweli kweli. Hebu jaribu. (*Kicheko*)

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kabisa kwamba, hapa siwezi kutamka hapa tutafanya nini kwa sababu cha kwanza ni kwamba kama kweli anavyosema wamekuwa wanaleta katika maombi na kama hili daraja la Kolo Kondoa litakuwa limo katika mpango huu wa Bajeti, basi maana yake ni kwamba leo tutamwomba Mheshimiwa Bura atupitishie Bajeti hapa ya Waziri Mkuu ili liweze kuwa *taken care of.*

Lakini kama halipo maana yake ni kwamba, watatakiwa walete kwenye mpango wao wa barabara na liingie katika utaratibu kama ambavyo tunaeleza hapa. (*Makofi*)

Na. 117

**Uchangiaji Huduma za Matibabu**

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA (K.n.y. MHE. BERNADETA K. MUSHASHU)** aliuliza:-

Kwa kuwa huduma ya matibabu ni muhimu kwa kila mgonjwa na hivyo ni wajibu wa Serikali kuhakikisha kuwa kila mgonjwa anapata huduma hiyo na kwa kuwa watu hutakiwa kuchangia gharama za matibabu:-

(a) Je, ni utaratibu gani wa kuchangia matibabu uliopo kwa sasa na ni kwa kiasi gani mgonjwa anapaswa kuchangia?

(b)Kwa kuwa wazee ni watu muhimu na wametumikia Taifa kwa muda mrefu na Serikali iliamua wapatiwe huduma ya matibabu bure. Je, ni wazee wa umri gani wanapata huduma hiyo?

(c)Je, ni kwa nini wazee wote wasipewe huduma hii bure?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Bernadeta Mushashu, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a), (b) na (c) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inasimamia Mifuko mitatu ya wananchi kuchangia huduma za matibabu kama ifuatavyo:-

(a)Mfuko wa papo kwa papo – huu ni Mfuko ambao mgonjwa huchangia kulingana na huduma atakazopewa kwa mfano dawa, vipimo na maabara na kulazwa. Kima cha mchango kinatofautiana kati ya Zahanati, Vituo vya Afya na Hospitali. Serikali imetoa mwongozo kwa Halmashauri wa jinsi ya kutekeleza uchangiaji huu, vigezo vya kuwasamehe wasio na uwezo wa kulipa, makundi yanayostahili msamaha na kadhalika.

(b) Mfuko wa Afya ya Jamii – katika Mfuko huu Halmashauri inawashirikisha wananchi katika Halmashauri zao na kwa pamoja kupanga kima cha kila Kaya kuchangia. Viwango vinatofautiana Halmashauri na Halmashauri lakini ni kati ya Sh. 5,000/= mpaka 10,000/= kwa matibabu yote kwa mwaka.

(c) Bima ya Afya ya Taifa – Mpango huu ulianza mwaka 2001 kwa Sheria iliyopitishwa na Bunge na kundi lililohusika katika huduma hii lilikuwa waajiriwa wa Serikali Kuu, baadaye wafanyakazi wa Serikali za Mitaa pia wakajumuishwa na hivi sasa juhudi zinafanywa ili sheria ibadilishwe kupanua wigo la wanufaika. Katika Mfuko huu mtumishi huchangia asilimia tatu ya mshahara wake na mwajiri huchangia asilimia tatu kwa ajili ya matibabu ya mtumishi na wategemezi wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuliarifu Bunge lako kwamba fedha zinakusanywa katika Mifuko hii mitatu zinatumika katika kituo zinapokusanywa.

Kwa hiyo, kila kituo kinawajibika kusimamia makusanyo na matumizi ili kuboresha huduma katika sehemu zao za kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu swali la kifungu (b) na (c). Wazee wanaopatiwa huduma za matibabu bila malipo ni wazee wote wenye umri wa miaka 60 au zaidi na ambao wamethibitika kuwa hawana uwezo wa kuchangia.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii imetokana na kwamba wazee kama ilivyo kwa makundi mengine katika jamii hutofautiana katika vipato vyao. Kwa hiyo, wazee wenye

uwezo wa kipato wanatakiwa kuchangia matibabu yao.  Msingi wa uchangiaji ni kipato na siyo kulitumikia Taifa kwa muda mrefu.

Aidha, watumishi wa sekta ya afya wameelekezwa kuwa, hakuna mgonjwa wa aina yoyote atakayenyimwa huduma ya afya kwa sababu ya kukosa uwezo.

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza.  Kwa kuwa katika maeneo mengi ya nchi yetu bado hauna zahanati wala hospitali ambazo zinamilikiwa na Serikali, hivyo kumekuwa na hospitali ama zahanati za watu binafsi na hospitali na zahanati hizo haziwakubalii wazee hao kutibiwa bure.  Je, Serikali inasema nini katika hali ya namna hiyo?

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, kwa kuwa hata Mifuko hii ambayo wafanyakazi na wananchi wamekuwa wakichangia Bima zao za afya wakati mwingi wanapokwenda hospitalini hawapati dawa zote na matibabu yote yanatakiwa ingawa tayari wameshachangia michango yao katika Mifuko hiyo na wanapotakiwa kupata dawa wanaambiwa wakazitafute dawa nje ya hospitali walizokwishachangia Mifuko ya Bima za Afya.

Je, Serikali inasema nini katika hali hiyo inayojitokeza mara nyingi na kusababisha matatizo makubwa kwa wazee na Watanzania wengine pia?  (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA AFYA  NA USTAWI WA  JAMII:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kabisa kwamba, misamaha hii au utaratibu huu wa kuchangia unapatikana katika hospitali za Serikali lakini kuna sehemu ambazo hakuna hizo hospitali za Serikali, katika vituo vya dini wale ambao wamepata misamaha kwa mfano watoto na wazee wanatakiwa kutibiwa bure kwa sababu Serikali huwa inachangia asilimia fulani ya dawa katika sehemu husika.

Lakini katika hospitali binafsi bado mpaka sasa hivi hakuna utaratibu wa wazee, watoto au wale wenye misamaha kuweza kutibiwa bure.

Hivyo, nawashauri wananchi ambao wanatibiwa katika maeneo yale waende katika hospitali za Serikali zilizo jirani au za dini zilizoko pale ambapo sisi huwa tunaruhusu waweze kutibiwa na Serikali huwa inafidia.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kuna malalamiko kwamba wale ambao wanakatwa fedha zao katika Mfuko wa Bima za Afya wengine huwa hawapati huduma hizo kwa sababu aidha hawapati sehemu zile au inabidi wasafiri.

Napenda kusema kwamba Serikali inaliangalia hii na kuhakikisha kwamba katika mpango tunaohakikisha kwamba huduma zitakuwa zinafika, tutahakikisha kwamba dawa zitakuwa zinapatikana na kufikia kule kote ambako wananchi wanachangia.*(Makofi)*

Lakini vilevile, katika yale maeneo kama nilivyosema katika jibu langu la msingi kwamba fedha zinazokusanywa pale zinatumika katika maeneo husika. Kwa hiyo, nataka niwaagize wale ambao wanakusanya fedha hizo wahakikishe kwamba vile vituo ambapo wananchi wanahudumiwa kule wananunue zile dawa waweke katika maeneo yao kwa sababu fedha wanazochangia zinatakiwa zitumike katika yale maeneo husika kule wanakopatikana, na wale ambao wanatakiwa kwenda kwa Rufaa basi wakapate kwa mtiririko wa rufaa na kule wanatakiwa wapatiwe zile dawa zao.

**MHE. LEDIANA M. MNG'ONG'O:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kuniona. Kwa sababu tatizo la wazee na watoto wanaotakiwa kupata msamaha wa kutibiwa bure wamekuwa wakipata matatizo makubwa. Serikali inaonaje kama itatoa vitambulisho na hivyo vitambulisho viwawezeshe kutibiwa kwenye hospitali yoyote. Kwa sababu matibabu wanapata lakini tatizo linakuja wakati ule ambapo dawa zinakuwa hazipo.

Je, Serikali itakuwa tayari kutoa vitambulisho maalum ambavyo vitawawezesha hao wazee na watoto waliopo chini ya miaka mitano kupata dawa katika sehemu yoyote?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Naibu Spika, utaratibu wa kuwatambua wazee na watoto ni kama ufuatao. Mtoto chini ya miaka mitano huwa anatambulika popote pale anapokwenda anapokuwa na kadi yake ya kliniki. Kwa maana hiyo kama atakuwa na kadi ya kliniki hicho ni kitambulisho tosha kitakachomwezesha mtoto aweze kupatiwa matibabu bure kama Serikali ilivyoagiza.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la wazee ni kwamba mzee anapokuwa pale ni kwamba anatambuliwa kwa umri wake, lakini vilevile anatakiwa awe anathibitishwa katika ile sehemu anayoishi. Kwa hiyo, kwa sasa hivi hakuna utaratibu wa kwamba tutengeneze vitambulisho, lakini mzee ni mzee anafahamika.

Lakini pia nilikwishasema kwamba yule ambaye atakosa huduma basi atakosa kujulikana kwamba ni mzee au umri wake hautoshi, anaweza akatibiwa hata kama hana fedha za kuchangia. *(Makofi)*

Na. 118

**Malipo ya Wastaafu wa Afrika Mashariki**

**MHE. AZIZA SLEYUM ALLY** aliuliza:-

Kwa kuwa, kero ya wastaafu wa Afrika Mashariki inashughulikiwa na Serikali licha ya kuwa bado kuna matatizo:-

(a) Je, Serikali itakubaliana nami kuwa, wapo wastaafu walio ripotiwa kuwa, wamefariki na warithi wao bandia kulipwa fedha hizo?

(b) Je, Serikali inashauri nini kwa wastaafu hao ambao wapo na hawajalipwa haki yao?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. OMAR YUSSUF MZEE)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Uchumi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Aziza Sleyum Ally, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, utaratibu unaotumika wa kuwalipa mafao warithi wa iliyokuwa Jumuiya ya Afrika ya Mashariki ni kwa wahusika kukamilisha taratibu zote za mirathi na hatimaye Shirika alilofanyia kazi mhusika kuthibitisha vielelezo vyote kuwa ni sahihi.

Kutokana na kwamba kumbukumbu za wafanyakazi wa iliyokuwa Jumuiya ya Afrika Mashariki hazikuwa na picha za wafanyakazi husika, pamoja na kubadilika mara kwa mara kwa viongozi wa Mashirika ya Jumuiya ya Afrika ya Mashariki, ni dhahiri kwamba upo uwezekano wa kujitokeza wananchi na kudai mafao au mirathi wakati yameshalipwa. Hata hivyo, utaratibu wa malipo kwa sasa umeboreshwa, ili tatizo hili kwa siku za baadaye lisijitokeze tena.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inawashauri wastaafu husika wawasiliane na Shirika walilofanyia kazi ambao ndio waliowathibitisha waliolipwa, kwa lengo la kufahamu anayestahili kulipwa ili waajiri hao waone namna ya kuwalipa na ofisi yangu itakuwa tayari kusaidiana nao.

**MHE. AZIZA SLEYUM ALLY:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kwanza nitoe shukrani na pongezi kwa Serikali kuandaa utaratibu mpya ambao hautokuwa na tatizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, la kwanza, kutokana na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha na Uchumi, inaonekana kwamba Serikali haitokuwa inadaiwa tena na wale wastaafu ambao walipata malipo kama warithi bandia. Je, Serikali imejiandaaje

sasa hivi kukaa na Mashirika yale ambayo yana wastaafu hao ili kuweza kutatua tatizo hilo ambapo inaonekana Mashirika hayo ndiyo yaliyoidhinisha wale watu bandia waweze kwenda kulipwa fedha za wastaafu hao ambao ni halali na wenyewe wakawa bado hawajafa? *(Makofi)*

La pili, Mheshimiwa Naibu Waziri, nilikuwa naomba aweze kutufahamisha je, tatizo la wastaafu wale ambao wanalala *station* pale Dar es Salaam tatizo lao litakwisha lini na ufumbuzi uweze kupatikana ili wastaafu wale wapate fedha zao na tatizo sugu la ulipaji wa fedha hizo liweze kupatikana na warudi makwao haraka iwezekanavyo? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. OMAR YUSSUF MZEE):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, nakubaliana na ushauri wake kwamba Wizara yangu itakaa na Mashirika hayo ili kuona kwamba hayo matatizo yanamalizika.

La pili, Mheshimiwa Naibu Spika, nakumbuka katika kikao kilichopita nililitangazia Taifa mbele ya Bunge lako Tukufu kwamba wastaafu wa iliyokuwa Jumuiya ya Afrika Mashariki wote wanaoidai Serikali fedha zipo, na nikawaomba waje wanione mmoja mmoja pamoja na vigezo vyao.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nikuthibitishie kwamba kuanzia mwezi Aprili, 2008 waliokuja kuniona ni kumi na nikazungumza nao na matatizo yao tuliweza kuyatatua. Walioajiri ni mmoja mmoja siyo makundi, na Dar es Salaam sasa hivi lazima tukubali kwamba imekua, wajanja wamekuwa wengi.

Mimi ninawaomba wahusika fedha zipo waje mmoja mmoja na vielelezo vyao na hayo matatizo lengo letu sisi yamalizike. *(Makofi)*

**MHE. MOHAMMED RAJAB SOUD:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa, taratibu zote wakati mtu anapoajiriwa zinakuwepo, picha pamoja na mambo mengine yote. Huu usumbufu wote unaotokea hivi unatokea wapi?

**NAIBU SPIKA:** Kwa sababu wanakuja kwa makundi. *(Kicheko)*

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. OMAR YUSSUF MZEE):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kama nilivyoeleza wastaafu wa Afrika Mashirika walipoajiriwa mafaili hayakuwa na picha. Kwa hiyo, kuthibitisha kwamba huyu ndiye kunatakiwa ufanye utaratibu na busara nyingi sana. Vinginevyo utamlipa mtu aliyekuwa siye.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kama ulivyosema huwezi uka-*deal* na kundi, kila mmoja ana kesi yake, kila mmoja akaajiriwa tarehe yake, kila mmoja ameajiriwa

kwenye Shirika lake. Mimi ninaomba sana tena waje mmoja mmoja na hayo matatizo yatakwisha.

**MHE. DR. WILBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa, ndani ya Bunge hili Serikali imekwishatoa majibu mengi; na kwa kuwa leo Naibu Waziri amerudia tena kwamba fedha zipo ila anataka waende mmoja mmoja; na kwa kuwa matatizo ya wastaafu hawa ni pamoja viwango ambavyo hawajakubaliana na Serikali.

Je, Mheshimiwa Naibu Waziri atakubaliana nami kwamba utaratibu mpya wa kutaka mmoja mmoja ni utaratibu wa kuwadhoofisha ili wasije na nguvu ya pamoja ya kudai haki zao? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. OMAR YUSSUF MZEE):** Mheshimiwa Naibu Spika, utakubaliana nami kwamba haki za mfanyakazi kama zilivyoainishwa katika Sheria za Utumishi ni haki ya mtu mmoja mmoja siyo haki ya kundi. Bado naendelea kusema kwamba sikuwadhalilisha wastaafu hao kwa kutaka waje mmoja mmoja.

Bado naendelea kusema kwamba waache waje mmoja mmoja na kila mtu atapata haki yake kwa mujibu wa taratibu zilivyowekwa. *(Makofi)*

Na. 119

**Sheria ya Ukomo**

**MHE. JUMA H. KILLIMBAH (K.n.y. MHE. RAMADHANI A. MANENO)** aliuliza:-

Kwa kuwa, Sheria ya Ukomo (*Law of Limitation Act*) Na. 10 ya mwaka 1971 imepitwa na wakati, na kwa kuwa kuna malalamiko mengi kutoka kwa wananchi yanayohusu madai ya fidia kwenye maeneo yao yanayochukuliwa na kampuni na taasisi; na kwa kuwa; wananchi wengi vijijini hawajui sheria:-

Je, kwa nini Serikali isiifanyie sheria hiyo marekebisho ili kusiwepo na ukomo wa kufungua kesi za madai kama ilivyo kwa kesi za jinai?

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ramadhani Athuman Maneno, Mbunge wa Chalinze, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kila shauri linapopelekwa mbele ya Mahakama huwa linahusu pande mbili, yaani mdai na mdaiwa. Kwa msingi huo, Sheria aliyoitaja Mheshimiwa Mbunge huweka ukomo wa muda wa kufungua mashauri ili kuhakikisha kuwa haki inakuwepo kwa pande zote zinazohusika. Ni kweli kwa upande uliokosewa unayo haki ya kufungua shauri. Hata hivyo, upande mwingine nao unayo haki ya

kutokubaki kuisubiri kesi kufunguliwa muda wowote. Shauri lolote lile ni lazima lifike mwisho ili mdaiwa aendelee na maisha yake bila ya hofu. Hivyo, ni muhimu pawepo na ukomo wa muda wa kufungua mashauri Mahakamani.

Pia msingi wa Sheria hii ni sababu za kiushahidi. Kuruhusu kufungua mashauri ya madai wakati wowote ule kunaweza kuleta madhara kwa mdaiwa ambaye iwapo madai yangewasilishwa kwa muda muafaka, angeweza kutoa utetesi wake kwa kuwasilisha ushahidi ambao anao. Kwa mdai kuchelewa kufungua kesi, mdaiwa anaweza kupoteza ushahidi wake kutokana na kupitwa na muda. Uwekaji ukomo sio tu kwamba unamlinda mdaiwa bali pia na mdai mwenyewe kwani madai ya muda mrefu hukosa ushahidi thabiti.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na sababu hizo Serikali inaona kuwa kuna umuhimu wa kuendelea kuwa na Sheria ya Ukomo wa kufungua mashauri. Hivyo Sheria hii ni muhimu na bado haijapitwa na wakati.

**MHE. JUMA H. KILLIMBAH:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Pamoja na majibu ya Mheshimiwa Waziri, nina swali la nyongeza. Kwa kuwa Sheria hii inakizana na Katiba ya Nchi Ibara ya 24(2).

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niinukuu hii inayosema: "Bila kuathiri masharti ya Ibara ndogo ya kwanza ni marufuku kwa mtu yeyote kunyang'anywa mali yake kwa madhumuni ya kutaifisha au madhumuni mengineyo bila idhini ya Sheria ambayo imeweka masharti ya kutoa fidia." Kama kweli sheria hii jinsi inavyozungumza Katiba jinsi inakizana wale waliothirika kupitia Sheria hiyo ambayo nimeitaja Sheria namba 10. Sasa Serikali inasemaje juu yao?

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya Katiba ambayo Mheshimiwa Mbunge ameinukuu kwa hakika haina mahusiano yoyote na Sheria hii ya Ukomo wa Madai. Sheria ya Ukomo wa Madai inahusiana na kesi zilizofunguliwa kulingana na aina ya kesi yenyewe. Kwa mfano, katika madai ya Mikataba ukomo wake ni miaka sita. Kama una kesi ya madai ya mikataba na hujadai ndani ya miaka sita basi kesi hiyo hairuhusiwi kudaiwa tena baada ya kipindi hicho. Na kama una madai ya kesi inayohusu ardhi kama hujadai ndani ya kipindi cha miaka 12 basi huruhusiwi kufungua kesi tena baada ya miaka 12. Kwa hiyo, haihusiani na suala nzima la kutaifisha mali ya mtu.*(Makofi)*

**MHE. PONSIANO D. NYAMI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize swali moja la nyongeza. Kwa kuwa, Kimataifa huwa waathirika wanaodai fidia mbalimbali huwa pia wanachukua miaka mingi. Kwa mfano, wanaodai masuala ya utumwa labda mauaji ya kimbari. Kwa nini sheria hii sasa inaweka ukomo kwamba anayedai fidia ni lazima awe katika miaka kadhaa na kwa nini hizo Sheria za Kimataifa haziwezi ukomo huo. Je, Serikali haioni kwamba inakiuka Sheria za Kimataifa.

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria ya Ukomo inaweka ukomo wa kuanzisha madai siyo kuendeleza madai. Unaweza ukafungua kesi yao ya madai leo ukaidai kwa muda miaka 300 kama inawezekana hiyo kesi ikaendelea kwa muda huo.

Lakini huwezi ukaianzisha kama jambo lililotokea muda wake umezidi miaka 6 haujadai ndani ya kipindi hicho, baada ya miaka 6 ukaanza kudai kwa mfano. Hicho ndicho kinachozuiwa si kuendelea na kesi ila kufungua kesi mpya katika kipindi kinachohusika. *(Makofi)*

Na. 120

**Mpango Shirikishi wa Uhifadhi wa Maliasili**

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA** aliuliza:-

Kwa kuwa, mpango shirikishi wa uhifadhi wa maliasili ni mpango mzuri unaowapa wananchi fursa ya kushiriki kikamilifu kulinda na kuhifadhi rasilimali zao; na kwa kuwa, ni wajibu wa Serikali kuhakikisha kuwa, raslimali zinalindwa kikamilifu kwa Maendeleo ya wananchi:-

(a) Je, hadi sasa ni maeneo mangapi ya hifadhi za jamii ya wanyamapori (WMA) yaliyoainishwa na yapo wapi?

(b) Kwa kuwa, kikwazo kimojawapo kilichokuwa kinakwamisha maeneo hayo kupata hadhi ni kukosekana kwa mpango wa matumizi ya ardhi kwenye maeneo husika. Je, Serikali inachukua jukumu gani la dhati kuhakikisha maeneo hayo yanapimwa ili rasilimali zilizopo zitumike kibiashara kuinua uchumi wa wananchi wanaozunguka maeneo hayo?

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Magdalena Sakaya, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, kanuni za Maeneo ya Jumuiya ya Hifadhi ya Wanyamapori za mwaka 2005 ziliainisha maeneo 16 ya majaribio ya Jumuiya ya Hifadhi za wanyamapori (*Pilot Wildlife Management Areas*). Hadi kufikia Juni 2008 maeneo kumi yameidhinishwa kuwa maeneo ya Jumuiya ya Hifadhi za wanyama (WMAs) kama ifuatavyo:-

| **Eneo** | **Wilaya** |
|---|---|

| | |
|---|---|
| 1. Ipole | Sikonge, |
| 2. Uyumbu | Urambo |
| 3. Burunge | Babati |
| 4. Ngarambe/Tapika | Rufiji |
| 5. 5 Enduiment | Longido |
| 6. Ikona | Serengeti |
| 7. Idodi/Pawaga | Iringa |
| 8. Wami-Mbiki | Morogoro, Mvomero na Bagamoyo |
| 9.Tunduru | Tunduru |
| 10.Songea | Namtumbo |

(b)Kwa mujibu wa kanuni za maeneo ya Jumuiya ya Hifadhi ya Wanyamapori 2005, uanzishwaji wa WMAs huamuliwa na wanavijiji wenyewe, baada ya kupata elimu kuhusu uanzishaji na uendelezaji maeneo ya Jumuiya ya Hifadhi ya wanyamapori.

Kwa kuzingatia hilo, Wizara yangu ina jukumu la kutoa elimu kwa wanavijiji ili kuanzisha *WMAs.* Aidha, Wizara yangu kwa kushirikiana na Kamisheni ya mipango ya Matumizi Bora ya Ardhi (*Land use Planning Commission*) imekuwa ikiziwezesha Halmashauri zenye vijiji ambavyo vinataka kuanzisha *(WMA)* kuandaa mipango ya matumizi bora ya ardhi kulingana na uwezo wa bajeti ya Serikali. Vilevile Wizara yangu kwa kushirikiana na wahisani, *NGOs,* na sekta binafsi huwezesha vijiji hivyo kuandaa mipango ya matumizi bora ya ardhi.

**MHE MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba niulize maswali mawili madogo ya nyongeza.

La kwanza, kwa kuwa, mengi ya maeneo haya ambayo ni Hifadhi za Jamii yameanzishwa kwa uguvu za wananchi na misaada ya wafadhili na wahisani; na kwa kuwa baada ya kusubiri kwa muda mrefu baadhi ya wafadhili walijitoa na kuachia wananchi wenyewe wakiendeleza; na kwa kutambua uwezo wa Halmashauri zetu zimeshindwa kuwasaidia wananchi kuweza kukamilisha taratibu za matumizi bora ya ardhi?

Je, Serikali sasa haioni umuhimu wa kuweka juhudi za kutosha bila kutegemea Halmashauri kuhakikisha kwamba maeneo hayo yanafanyiwa matumizi bora ya ardhi mapema ili kuendelea kutunza rasilimali ambayo imetunzwa kwa muda mrefu?

La pili, kwa kuwa Askari wa Wanyamapori wa vijiji vinavyozunguka maeneo hayo wamekuwa wanafanya kazi ngumu kwa muda mrefu na wamenyimwa kutumia silaha; na kwa kuwa Askari hawa wana vitambulisho vinavyotoka Idara ya Wanyamapori na wamepata mafunzo kwenye Vyuo vya Wanyamapori ambavyo vinatambulika lakini wanashindwa kutumia silaha. Je, Idara ya Wanyamapori au Wizara ni sababu zipi zinazowafanya wawazuie wakati wanawatambua na vitambulisho vyao?

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, sababu zinazochelewesha ukamilishaji wa *Pilot Areas* kama nilivyosema zinatofautiana. Kwa kweli kutoka eneo moja hadi lingine. Ni nia ya Wizara kutoa msaada kila unapohitajika kuhakikisha kwamba mchakato unakamilika. Kuna maeneo kwa kweli mchakato unachelewa kutokana na wananchi wenyewe. Kuna baadhi ya maeneo kwa mfano, Ntwantwa kule Kilosa, wananchi wenyewe ambao wanahusika kwenye vile vijiji wanakuwa hawaelewani. Baadhi yao wanakubali na wengine wanakataa.

Kwa hiyo, yanapotokea mazingira ya namna hiyo inakuwa ni vigumu kwa Wizara kuwaingilia. Lakini pale ambapo wananchi wote wamekubaliana tumekuwa hatuna matatizo na tumekuwa tukisaidia. Hata nje ya maeneo haya 16 bado kuna maeneo ambayo yameanzishwa kwa mfano, eneo la Makaho kule Meatu wao wenyewe wameanzisha na hawakuwemo kwenye *Pilot Project*. lakini tumewapokea na tumewasaidia na sasa wapo kwenye hatua za mwisho kabisa za kumaliza. Kwa hiyo, tulikuwa tunaomba tu wananchi wakubaliane sisi tuko tayari kuwasaidia.

Kuhusu kuruhusu Askari kutumia silaha. Utaratibu wa utumiaji na umiliki wa silaha unaeleweka. Watumishi wa Wizara ambao *authorise* ndiyo wanaoruhusiwa kutumia silaha za Wizara. Hao waliopo kwenye maeneo ya *open areas* wengi wao wanakuwa wamepata mafunzo ya muda mfupi.

Kwa mfano, yale mafunzo yanayotolewa kule Kwesimenganga ambayo yanawezesha tu kushiriki katika *process* nzima ya Uhifadhi. Lakini mafunzo yanayohusu utumiaji na umiliki wa silaha wanakuwa bado hawajafikia. Kwa hiyo, nilikuwa naomba kusisitiza kwamba pengine si vizuri kulegeza utaratibu wa utumiaji na umiliki wa silaha kutokana na madhara ya kiusalama yanayoweza kutokea.

**MHE. MGANA I. MSINDAI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize swali moja la nyongeza. Kwa kuwa, *WMAs* haziwezi kufanya kazi mpaka Sheria ya Wanyamapori iletwe hapa Bungeni; na sasa hivi ni zaidi ya miaka minne hiyo Sheria haijaja ni kikwazo gani kinazuia sheria hiyo kuja na itakuja lini? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria ya Hifadhi ya Wanyamapori Sura 283 inaruhusu uwindaji au umiliki wa maeneo ya *open areas* kwa wananchi. Kwa hiyo, kisheria haizuiliwi isipokuwa kuna upungufu mwingine wa kiujumla wa kisheria ambao tumekuwa tukiupitia; na kwa taratibu ambao tunao Wizarani tunategemea katika muda mfupi ujao tutakamilisha mchakato wa kupitia sheria hii upya. Lakini si kikwazo cha uanzishaji wa WMAs kama nilivyosema karibu kati ya 16 zimekwishakamilika na sasa hivi zipo kwenye hatua za mwisho kabisa za kuruhusu uwindaji wa wananchi kwenye hayo maeneo. Kwa hiyo, sheria hairuhusu ndiyo maana hayo maeneo 10 tayari yapo kwenye hatua za mwisho.

**MHE. VITA R. KAWAWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii ya kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa, sheria ya uvunaji wa

wanyamapori moja ya vifungu vyake vinasema asilimia 25 ya mapato ya mavuno ya *quarter* ya wanyama ya msimu zinatakiwa zilipwe katika Halmashauri inayozunguka kitalu au vitalu; na kwa kuwa mapato halisi huwa Halmashauri hatuyafahamu hasa ya Namtumbo na mgao unatoka katika Idara ya Wanyamapori huwa kama hisani badala ya kufuata sheria.

Je, Wizara inaweza kuwa inatuletea *quarter* za wanyama watakaovunwa katika msimu huo na thamani yake katika Halmashauri zetu ili tuweze kuweka katika hesabu zetu kama *revenue projection* kwa msimu huo husika katika Bajeti zetu? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Naibu Spika, mapendekezo anayoyatoa Mheshimiwa Mbunge ni mazuri, nafikiri ni sahihi kwamba Halmashauri ziwe zinapata taarifa ya wanyama ambao tumepanga kuwawinda. Pendekezo hili ni nzuri isipokuwa upungufu ambao umekuwepo ni kwamba mara nyingi unaweza ukatoa *quota* fulani ya wanyama kuwinda na wasiwindwe wote. Sasa ikitokea hivyo tulikuwa tukihofu kwamba inaweza ikaleta mzozo kidogo.

Kwa mfano, mwaka jana tulitoa *quota* ya kuwinda mamba 1,600, lakini wanyama waliowinda ni 1,585, simba tulitoa *quota* 478 lakini waliwindwa 226 sasa katika mazingira kama hayo tuna hofu kwamba inaweza ikaleta tatizo kati ya Bajeti au *quota* na *actual* ya wanyama ambayo wanakuwa wamewindwa. Lakini pendekezo nzuri tutalifanyia kazi.

Na. 121

**Mikesha ya Mbio za Mwenge Kueneza UKIMWI**

**MHE. JUMA SAID OMAR** aliuliza:-

Kwa kuwa UKIMWI ni janga la Taifa na unapoteza vijana wengi ambao ni nguvukazi ya Taifa:-

(a) Je, Serikali inajua kwamba, mikesha ya mbio za Mwenge inachangia kueneza UKIMWI kutokana na ngono zembe zinazofanyika katika mikesha hiyo?

(b) Kwa kuwa mikesha hiyo hufanyika katika mashule ambapo wanafunzi wa rika mbalimbali hukusanyika. Je, Serikali haioni kuwa hali hiyo inaweza kuchangia watoto wadogo kushiriki katika tendo la ndoa wakiwa wadogo na hivyo kuchangia kuenea kwa UKIMWI?

**WAZIRI WA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Juma Said Omari, Mbunge wa Mtambwe, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Serikali inajua kwamba mikesha ya mbio za Mwenge haichangii kabisa katika kueneza UKIMWI badala yake mikesha hiyo ni Vituo vya kuelimishana na kukumbushana juu ya matendo yanayoeneza UKIMWI likiwemo na tendo la ngono zembe. *(Makofi)*

Mwenge wa Uhuru ambao hukimbizwa nchi nzima Tanzania Bara na Visiwani kila mwaka kinabaki kuwa chombo chake pekee kinachofikisha ujumbe mbalimbali za Kitaifa na Kimataifa ana kwa ana kwa watu na kwa muda mfupi.

Tangu janga la UKIMWI likumbe Taifa letu, Mwenge wa Uhuru umekuwa ndio chombo ambacho hutoa ujumbe wa Vita dhidi ya UKIMWI ambao ni madhubuti katika maeneo yote mijini na vijijini. Kwa kipindi cha miaka 10 iliyopita, ujumbe wa Vita dhidi ya UKIMWI umekuwa ni ujumbe wa kudumu unaotolewa na kutiliwa mkazo katika mbio za Mwenge wa Uhuru kila mwaka.

Aidha, Mwenge wa Uhuru umekuwa ni chombo cha kuleta mshikamano miongoni mwetu bila kujali tofauti za kisiasa, kidini au kikabila. Pia umeimarisha Muungano na kukuza tabia ya ushindani wa kimaendeleo kwa kushindanisha Wilaya zote nchini na washindi kutunukiwa vyeti na Mheshimiwa Rais.

Mwenge pia umewezesha kuanzisha wiki ya vijana yenye fursa za kubadilisha uzoefu katika nyanja za uzalishaji mali na pia kujadili masuala mbalimbali ikiwa ni pamoja na UKIMWI.

(b)Mheshimiwa Naibu Spika, wakati wa mbio za Mwenge wanafunzi hushiriki katika ratiba ya Mwenge ambayo hufanyika wakati wa mchana tu tena chini ya usimamizi wa walimu wao. Aidha, watoto wadogo na wanafunzi kwa ujumla hawaruhusiwi kubaki na kushiriki katika mikesha ya Mwenge na endapo wapo wanaobaki, basi ni jukumu la wazazi wao kuwadhibiti.

**MHE. JUMA SAID OMAR:** Mheshimiwa Naibu Spika, sijaridhika bado na majibu ya Mheshimiwa Waziri. Naiomba Serikali ifanye utafiti wa kina na inipatie jawabu muafaka. Ahsante.

**MHE. HAFIDH ALI TAHIR:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Baada ya majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania hivi sasa tupo katika vita vya kupigana na ugonjwa huo wa UKIMWI. Kule Zanzibar kuna ngoma moja inaitwa Msewe, ngoma hiyo inapendwa sana kupigwa kule Kisiwani Pemba na huwa inakusanya vijana, wazee na rika zote.

Je, Mheshimiwa Waziri atakubaliana nami kwamba hivi sasa umekwishafika wakati muafaka wa kuishauri Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kupunguza kupiga ngoma hiyo ili kuzuia UKIMWI? *(Makofi/Kicheko)*

**WAZIRI WA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kule Pemba kuna ngoma inaitwa Msewe na sehemu zingine kuna ngoma mbalimbali, ngoma hizi huchezwa mchana na nyingine huchezwa usiku ni kuwadhalilisha wananchi wa nchi hii kudhani kwamba kila wanapokutana usiku shughuli ni moja tu. Ndiyo maana tunasema kazi kubwa tunayoifanya ni kuelimisha wananchi. Lakini kudhani kwamba watu hawa wanapokutana madhali kuna giza basi shughuli ni kushughulikiana tu, si sahihi. (*Kicheko*)

**NAIBU SPIKA**: Waheshimiwa Wabunge muda wa maswali umeisha na maswali yameisha. Haya mengine mnayafanya kuyazulia tu. Tabia za watu ni za watu iwe kwenye ngoma, iwe kwenye mwenge, tabia za watu ni watu tu. Ni vizuri mkajichukulia suala hili kwa makini sana kwa sababu ni shida, kabisa. Baada ya kusema hivyo Waheshimiwa Wabunge mimi naomba niwapongeze kwa dhati Waheshimiwa Mawaziri kwa majibu yao mafupi yanayolenga kwenye hoja. Nyie wenyewe mnaona kabisa tukiwa namna hiyo mnakuta Bunge linakuwa changamfu sio anatuhutubia mtu mmoja mpaka tunalala usingizi. Sasa hii mimi nawapongeza sana kuna maendeleo makubwa kabisa na mfanye vizuri zaidi ya hapo. Kasoro ipo wauliza maswali wanauliza maswali wakati mwingine gazeti zima. Mnajua hatari ya kufanya hivyo. Wakati tunakaa hapa redio inatangaza moja kwa moja. Sasa swali lako likiwa refu mtangazaji atalisomaje lote swali refu mno? Maana unapouliza unasema naomba swali langu namba fulani lipatiwe majibu. Lakini mtangazaji analazimika kulisoma kusudi wananchi wajue uliuliza nini. Sasa wewe umeuliza *page* nzima mtangazaji atakuwa na muda kweli wa kusoma *page* hiyo na akaenda na wakati? Hiyo ndiyo hasara ya kuuliza maswali marefu na tunataka yaishe saa nne kwa sababu ikifika saa nne redio inazima. Kwa hiyo wanaouliza baada ya saa nne hawatangazwi *live*. Kwa hiyo, ndiyo maana tunataka ku-*stic* kwenye maswali mkiuliza mafupi, mkajibiwa kifupi na maswali ya nyongeza yakawa mafupi wote mtakuwa *covered*. Lakini nawapongeza Mawaziri kwa safari hii. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, matangazo ya wageni. Leo Naibu Spika hana matatizo ya kusoma vikaratasi ana karatasi rasmi. Wageni walioko Bungeni asubuhi hii. Kwanza kuna wageni wa Mheshimiwa Dr. Wilbrod Slaa, ambao ni Wajumbe 36 wa Kamati Kuu ya Taifa ya CHADEMA, wakiongozwa na Mwenyekiti wa Taifa Mheshimiwa Freeman Mbowe naomba wasimame wajumbe wote. Mzee wetu Mheshimiwa Edwin Mtei yupo, nadhani bado yupo safari. Halafu kuna Balozi Christopher Ngaiza, kuna Profesa Mwesiga Baregu na baadhi ya Wakurugenzi wa Sekretarieti Kuu ya Chama. Wote hao wapo hapa mjini Dodoma kwa ajili ya Mkutano wa Kamati Kuu ya CHADEMA. Hawa wengine nimewataja hawakuonekana inaelekea bado wapo safarini wanakuja.

Tunao pia wageni wa Mheshimiwa Mtutura Abdallah Mtutura, ni Ndugu Said Zubeir Makandu, Mwenyekiti wa Taasisi isiyo ya Kiserikali inaitwa *HEDEFO*, karibu

sana. Halafu tuna Ndugu Maulid Kalambo Maulid, Katibu wa Mbunge Tunduru. Karibuni sana wageni kutoka Tunduru.

Tuna wageni wa Mheshimiwa Charles Keenja, wako Madiwani 15 wa Kamati ya Mipango mji wakiongozwa na Mwenyekiti wao Mheshimiwa Diwani Rajabu Hasani na Mheshimiwa Diwani Ahmed Mwilima ambaye ni Naibu Meya wa Jiji la Dar es Salaam. Naomba Naibu Meya asimame na hawa wengine wote naomba wasimame, nadhani wengine wamechelewa kidogo. Halafu tuna wageni wa Mheshimiwa Fatma Othman Alli ni watoto wake watatu naomba wasimame na Madiwani sita kutoka Mkoa wa Mjini Magharibi Zanzibar, naomba wasimame walipo. Karibuni sana Waheshimiwa Madiwani. (*Makofi*)

Tuna wageni wa Mheshimiwa Celina Kombani Waziri katika Ofisi ya Waziri Mkuu anayehusika na Mambo ya TAMISEMI. Yupo Mr. S.K. Pongolani ambaye ni mume wake, karibu sana mkeo anafanya kazi nzuri. Pamoja naye ni watoto wake Shaban. Karibuni sana sisi Mheshimiwa Kombani tunamtegemea sana katika harakati zetu.

Mheshimiwa Hoogan ana wageni wake yupo Profesa Gati Andrew. C*an you please stand up, I don't who is?* Huyu ni *Director* kwenye Cancers African Studies Centres pia ni mzungumzaji wa lugha ya Kiswahili. Yupo yule pale karibu sana nasikia wewe ni mzungumzaji mzri wa Kiswahili. Halafu tuna wageni wa Mheshimiwa Benedict Ole Nangoro, ni wanafunzi 20 na walimu wawili kutoka shule ya sekondari ya Kiteto karibuni sana naomba msimame wote.

Tuna wageni wa Mheshimiwa Mwanawetu Zarafi, ni Bwana Suleman Bungala jina maarufu anaitwa Bwege ndiye mume wake. Bwana Bwege karibu sana mume wake na Mheshimiwa. Yupo Bwana Deo Chaurembo Mkurugenzi wa Siasa *CUF* Wilaya ya Kilwa, karibu sana na mdogo wake Salum Mayanga, karibuni sana. (*Makofi*)

Tunao wageni wengine ambao ni Wanafunzi wa Udaktari wa Binadamu kutoka *The Herbert Kairuki Memorial University Dar es Salaam* wako 35 wanaweza kusimama walipo. Ok karibuni sana Madaktari tunawategemea kwa siku zijazo karibuni sana. (Makofi)

Tuna wanafunzi 50 kutoka Shule ya Sekondari Jamhuri, Dodoma. Karibuni sana na Bunge lipo katika eneo lenu kwa hiyo ni haki yenu kuja kila wakati. Halafu tuna Ndugu Lucas Kisasa Katibu wa Yanga na nadhani wale wapenzi wa mnamjua huyu, karibuni sana. Kwa hiyo, Kisasa unaona ulivyo na wanachama wengi humu ndani. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge nawashukuru kwa kuleta majina kwa utaratibu huu yanasomeka kwa urahisi. Sasa matangazo ya shuguli za leo kwa Kamati mbalimbali.

Mheshimiwa Issa Khatib Mwenyekiti wa Kamati ya Viwanda na Biashara anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati hiyo kwamba leo tarehe 27 kutakuwa na Kikao cha Kamati. Kikao hicho kitafanyika saa tano asubuhi katika ukumbi namba 227 jengo la utawala. Mheshimiwa Jenista Mhagama, Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii anawatangazia Waheshimiwa Wenyeviti, Makamu Wenyeviti na Waheshimiwa Wabunge wote walioandikiwa barua kuhudhulia mjadala baina ya Wajumbe wa Kamati za Kudumu za Bunge na Asasi za Kiraia. Mjadala huo utafanyika Jumapili tarehe 29/6/ kuanzia saa tano asubuhi katika Ukumbi wa Pius Msekwa. Kwa hiyo, mtakutana siku ya Jumapili saa tano.

Mheshimiwa Dr. Raphael Chegeni, Mwenyekiti wa *CPA, Tanzania Branch,* anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati ya Utendaji ya *CPA* tawi la Tanzania kuwa kutakuwa na Kikao cha Kamati katika chumba namba 219 ghorofa ya pili katika jengo la utawala leo saa saba mchana.

Kuna tangazo la kongamano, kesho Jumamosi tarehe 28 Juni, 2008kutakuwa na Kongamano kwa Waheshimiwa Wabunge wote litakaloanza saa tatu asubuhi katika Ukumbi wa Msekwa. Kongamano hilo linahusu usalama na ubora wa chakula kwa watunga sera na wenye kutoa maamuzi nchini. Waandaji wa kongamano hilo ni Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Viwango Tanzania. (Makofi)

Mheshimiwa Jenista Mhagama, Mwenyekiti wa Kamati ya Tafrija anaomba kuwatangazia wajumbe kwamba tarehe 28 Juni, 2008 kesho kutakuwa na burudani iliyoandaliwa kwa jina la usiku wa ki-Zanzibar itakayofanyika katika ukumbi wa tafrija za Bunge. *Basement Area* kuanzia saa moja jioni.

Waheshimiwa Wabunge wote mnakaribishwa ili waburudike na burudani zifuatazo. Kuna mziki wa dansi ya kiarabu, taarab, muziki mchanganyiko muziki wa zamani, Bongo flava na tenzi. Hapa si Wabunge tu na hata watu wa nje wanakaribishwa maana dansi hamuwezi kucheza peke yenu inabidi mcheze na watu wengine.

Baada ya kusema hivyo Waheshimiwa Wabunge tulikubaliana toka jana kwa sababu leo tunapenda kuhitimisha hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu na kama mnavyojua mmeshachangia kwa muda wa siku hizo tano na kwa Wabunge wengi sana wameandika michango yao kwa maandishi. Kwa sababu jioni tutaingia kwenye Kifungu kwa Kifungu na hiyo kunakuwa na Ofisi ya Waziri Mkuu yenyewe, Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za MIkoa na Serikali za Mitaa nafikiri kuna mafungu kama matatu.

Sasa ili kutoa muda mzuri kwa watu kupata nafasi nzuri kwa hiyo tunaingia moja kwa moja katika wachangiaji. Nafikiri tuanze na Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za MIkoa na Serikali za Mitaa.

**MWONGOZO WA SPIKA**

**MHE. MASOUD ABDALLA SALIM:** Mwongozo wa Spika.

**NAIBU SPIKA:** Mwongozo wa Spika, Mheshimiwa Masoud Abdalla Salim, Kanuni gani.

**MHE. MASOUD ABDALLA SALIM:** Mheshimiwa Naibu Spika, Kanuni ya 68 (7).

**NAIBU SPIKA:** Inasemaje?

**MHE. MASOUD ABDALLA SALIM:** Mheshimiwa Naibu Spika, Kanuni ya 68 (7), Mbunge anaweza kusimama wakati wowote ambapo hakuna Mbunge mwingine anayesema na kuomba Muongozo wa Spika kuhusu jambo ambalo limetokea Bungeni mapema ili Spika atoe ufafanuzi kama jambo hilo linaruhusiwa au haliruhusiwi kwa mujibu wa Kanuni na Taratibu za Bunge na majibu ya Spika yanatolewa papo hapo na baadae kadri atakavyoona inafaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati jana nikichangia hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu niligusia suala zima la bomoa bomoa Mjimwema Chang'ombe na baada ya hapo nilieleza kwamba kuna baadhi ya walionyanyaswa na Polisi na nilitakiwa kutoa uthibitisho na Waziri mhusika Mheshimiwa Marmo. Nilimpelekea majina kama alivyotaka, jina la mama aliyekuwa na kichanga na wale ambao walinyanyswa na Polisi. Hata hivyo akaniambia majibu hayatoshelezi na naaahidi kumpa mashirikiano ya hali ya juu. Naomba nimpe mashirikiano hayo kama ifuatavyo:-

**NAIBU SPIKA:** Ngoja kwanza Mheshimiwa Mbunge. Wakati unachangia jana uliombwa kuhusu utaratibu na muongozo wa Spika kwamba. Je, kuna ushahidi wa majina hayo? Kiti tukakwambia upeleke majina hayo kwa Waziri anayehusika wakati anajibu aweze kuwa ameyafanyia kazi majina hayo.

Sasa huwezi kuanza kujibu sasa hivi. Wewe subiri ajibu atakapokuwa hajajibu kwa kuridhisha ndiyo tunaingia kwenye vifungu baadaye jioni. Sasa huwezi kuanza kujibu sasa hivi itakuwa kama tunaingia kama *club* ya wazungumzaji tu.

Wewe jana ulizungumza nikakuagiza kwamba baada ya kutoa muongozo wa Spika kwa Waziri aliyekuwa anataka mwongozo kuhusu wewe kama una majina hayo mpelekee mtoa hoja.

Lengo letu lilikuwa akapate muda wa kutafuta majibu hayo. Wakati atakapokuwa anajibu kuanzia yoyote atakayeanza kujibu watajibu.

Wewe hujaridhika tutaingia kwenye vifungu wakati wa mchana utasimama kwamba sijaridhika na majibu kutokana na maelezo yako utakayokuwa nayo wakati huo. Kwa sasa ulivyopeleka umefanya vizuri. Tunaendelea. Katibu endelea na *Order Paper.*

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI)**: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa vile hii ni mara yangu ya kwanza kusimama hapa kwa ajili ya kuchangia hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu na kwa vile ningependa iingie katika rekodi, ningependa tena kwa mara ya pili kuchukua nafasi hii kumshukuru sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, ambaye alinipa mimi na wananchi wa Siha heshima kubwa ya kuwa Naibu Waziri katika Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI).

Naomba niseme hapa kwamba nitaendelea kushirikiana na Mheshimiwa Rais pamoja na Viongozi wote akiwemo Waziri Mkuu kutoa ushirikiano wangu na kumsaidia katika kazi zake kwa kadri Mwenyezi Mungu atakavyonijalia. Naomba nichukue fursa hii pia kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kuteuliwa kwake kuwa Waziri wetu Mkuu katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Ninapenda kusema kwamba tunamshukuru kwa kadri ambayo amekuwa anatulea tangu nilivyoingia katika Ofisi nimepata msaada mkubwa sana na amekuwa akinielekeza na kuniongoza. Ninachoweza kusema kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu nitaendelea kushirikiana naye kwa karibu sana na kumsaidia ili kazi yake iweze kuwa nyepesi.

Hivyo hivyo napenda kutoa salamu na shukrani zangu kwa Mheshimiwa Celina Kombani na kwa kweli kumpongeza kwa kuchaguliwa kuwa Waziri wa Nchi katika Ofisi ya Waziri Mkuu. Toka nimeingia katika Ofisi hii amenisaidia sana katika majukumu yangu na amenilia vizuri na anaendelea kushirikiana na mimi.

Ninachoweza kumhakikishia Mheshimiwa Kombani ni kwamba nitaendelea kushirikiana naye kuhakikisha kwamba kazi ambazo anazifanya za kulijenga taifa letu zinafanyika kwa umakini mkubwa. Napenda kuwashukuru pia Katibu Mkuu Mama Maimuna Tarishi pamoja na Ndugu Mbonde Msaidizi wake pamoja na Wakuu wa Idara wote katika Wizara yetu ambao tumekuwa tukishirikiana katika majukumu mpya na katika upya wangu huu imenisaidia sana.

Kipekee napenda kuwashukuru wananchi wangu wa Siha pamoja na familia yangu ambayo walinienzi sana na kunipa fursa hii ya kuja hapa. Bila wananchi wa Siha kufanya maamuzi ambayo waliyafanya mimi naamini kabisa kwamba isingeliwezekana nikawa nimesimama hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nimekuwa upande huu sasa na nimejaribu kuangalia mambo ambayo tumekuwa tunayafanya toka mwanzo tulipoanza na Wizara ya Fedha na mpaka tulipofika hapa tulipofika. Jambo moja kubwa sana ambalo limejitokeza

katika mijadala yetu miwili, huu wa Waziri ya Fedha na huu wa Waziri Mkuu ni suala ambalo Wabunge wengi wamelizungumzia hapa la kuhakikisha kwamba tunakuwa na Bajeti ya kujitegemea. Mimi naamini kwamba kama tutakwenda hivyo tunavyokwenda itatusaidia sana katika nchi yetu kwa sababu hatuwezi tukakaa hapa tunawategemea Wahisani kwa ajili ya kuendeleza nchi yetu.

Mimi nafikiri ni vizuri sasa tukaingia kwenye huo mkondo wa kufikiri kwamba sisi wenyewe ndani tufanye nini ili kuweza kuwaletea Maendeleo kwa ajili ya nchi yetu. Badala ya kukaa tunawategemea wahisani. Kwa kuanza naomba nichukue fursa hii kuunga mkono Hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu asilimia mia moja na kwa vile muda niliopangiwa hapa ni mfupi sana nitaomba niende haraka yale masuala yanayohusu sekta nyingine na Wizara nyingine tumewaomba wale wenzetu watusaidie. Mheshimiwa Waziri Mkuu atakapokuja atazungumza zaidi lakini sisi tutajikita zaidi kwenye maeneo yanayotuhusu na mengine tumemwachia Mheshimiwa Waziri Mkuu ayajibu na Mheshimiwa Marmo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wa kwanza uliokuwa unahusu maslahi ya Madiwani na viongozi wengine wa ngazi za mwanzo na mawazo haya yaliletwa na Mheshimiwa George Lubeleje ambaye ni Mwenyekiti wa Katiba na Sheria, Mheshimiwa Jacob Shibiliti, Mheshimiwa Wilbrod Slaa, Mheshimiwa Kabuzi Rwilomba, Mheshimiwa George Simbachawene, Mheshimiwa Stephen Galinoma na Mheshimiwa Abbas Mtemvu na ningependa tu kusema kwamba suala hili la maslahi ya Madiwani linashughulikiwa kama ilivyoonyeshwa katika Hotuba ya Waziri Mkuu, ukurasa wa 62 aya ya 102 kwamba Serikali imekubali kuboresha maslahi ya madiwani kuhusu posho, matibabu, kiinua mgongo na kuwapatia vyombo vya usafiri na kutoa unafuu wa kodi. Kwa mwaka 2008/2009 jumla ya shilingi bilioni 4.8 zimetengwa kwa ajili ya posho ya mwezi kwa ajili ya Waheshimiwa Madiwani.

Aidha marekebisho ya Sheria yatafanyika ili kuwawezesha Waheshimiwa mbalimbali kulipwa posho zao za matatibu, kiinua mgongo na kuwapatia vyombo vya usafiri na kutoa unafuu wa kodi. Sheria ilivyokaa sasa hivi haituwezeshi kufanya hivyo lakini tunasema kwamba tutafanya haraka iwezekanavyo kuhakikisha kwamba sheria inakaa kwa namna ambayo Madiwani wanaweza wakapata hizi huduma. Suala la maslahi ya viongozi ambao wapo katika ngazi za vijiji na kuna kilio kikubwa sana hapa kwamba wenyeviti wa vijiji nao tungewaangalia na wale watendaji wengine walioko kwenye zile ngazi za chini kwa maana ya ngazi za msingi. Hili nalo linafanyiwa kazi na wakati mufaka utakapofika tutahakikisha kwamba tunatekeleza kama ilivyoelekezwa hapa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja ya pili ambayo ililetwa na Mheshimiwa George Malima Lubeleje ambayo inazungumzia Waheshimiwa Wabunge waelimishwe juu ya maboresho ya Serikali za Mitaa awamu ya kwanza na awamu ya pili. Katika awamu ya kwanza ya maboresho Serikali ilitoa elimu kwa wadau mbalimbali wakiwemo Waheshimiwa Wabunge. Katika awamu ya pili Serikali itaendelea kutoa elimu ya maboresho awamu ya kwanza na ya pili kwa Wabunge wote kadri ya uwezo wa fedha utakavyoruhusu. Tutaangalia uwezekano wa awamu hii ya pili kwa kufanya semina

katika Bunge mwezi Novemba 2008. Huu ni ushauri ambao umetolewa hata tulipokutana katika Semina na ilishauriwa kwamba Wabunge waweze kupata semina kwa ajili ya maboresho, tunaangalia uwezekano huo na tunaangalia kipindi hiki cha Bajeti haionekani kama itawezekana lakini ahadi tunayoitoa hapa ni kwamba mwezi Novemba tutajitahidi kuhakikisha semina hii inafanyika.

Mheshimiwa George Lubeleje pia alizungumzia Mikoa iangalie uwezekano wa kujenga ofisi, nyumba mpya endapo gharama za kukarabati zinakaribia zile za ujenzi na Wabunge wengi wamezungumzia jambo hili. Tumelitafakari, tumeliangalia tumeona kwamba kweli takwimu zinaonyesha kwamba kuna maeneo ambayo watu tunakwenda tunakarabati nyumba lakini ukiangalia gharama za ukarabati zinazidi hata zile za kujenga nyumba mpya. Kwa hiyo, ushauri huu tumeukubali na tumeuchukua na tutaufanyia kazi. Serikali itenge fedha za ujenzi wa jengo la Mkuu wa Mkoa wa Dodoma.

Mawazo haya pia yameletwa na Mwenyekiti Mheshimiwa George Lubeleje. Katika mwaka wa fedha wa 2008/2009 Serikali imetenga kiasi cha shilingi bilioni 1.2 kwa ajili ya kuanza kujenga jengo la Ofisi ya Mkuu wa Mkoa na Serikali itaendelea kutenga fedha kwa ajili ya ujenzi huo. Mheshimiwa Lubeleje pia alizungumzia hali ya jengo la Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Pwani litazamwe upya ili kulingana na hali ya udongo. Tunachosema hapa ni kwamba tunafanya tathimini ya kitaalam ili kubaini tatizo lililopo. Matokeo ya tathimini hiyo yatasaidia Serikali katika kufanya uamuzi sahihi. Kwa hiyo hili tunalifanyia kazi tumeliona na tutapeleka wataalam pale ili waweze kufanya utafiti wa kufanya lakini baadaye tuhakikishe kwamba linatekelezwa. Mheshimiwa Lubeleje pia alisema Kamati inashauri mbinu za ushirikishaji wananchi katika shughuli za maendeleo. Huu ni mfumo ambao unatumika katika upangaji mipango, tunatumia mfumo huo huo kwa fursa na vikwazo kwa maendeleo. Hizi ni *O* and *OD* na mambo mengine kama hayo. Kwa hiyo hili tunalichukua moja kwa moja suala la *oppotunities and obsticles to development.*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sana anasema taarifa za Bajeti za Mikoa ziainishe mafanikio na matatizo. Ushauri huu tunauzingatia na tumeuchukua. Mheshimiwa Wilbrod Slaa, Mbunge wa Karatu na Mheshimiwa Jacob Shibiliti, Mbunge wa Misungwi amezungumzia ujazaji wa nafasi wazi za uongozi katika ngazi za vijiji na vitongoji. Jibu ni kwamba nafasi wazi zinapaswa kujazwa katika siku sitini toka Mkurugenzi wa Halmashauri kupokea taarifa ya kuwepo nafasi wazi. Hata hivyo Ofisi yangu itafuatilia kilichotokea maeneo hayo hadi uchaguzi ukachelewa kufanyika hadi sasa na kurekebisha kasoro hiyo. Kwa Mheshimiwa Slaa na Mheshimiwa Shibiliti tunataka tufuatilie jambo hili kuona kwamba nini kilichotokea mpaka ikawa hivyo lakini kama nilivyosema utaratibu unataka kwamba katika siku sitini uchaguzi uwe umeitishwa.

Mheshimiwa Slaa amezungumzia pia kuzuiliwa kwa shughuli za maendeleo kwenye vijiji vinavyoongozwa na vyama vya upinzani. Azma ya Serikali ni kusimamia maendeleo ya Watanzania bila kujali itikadi zao. Uchaguzi ukimalizika pale na kumpata Mwenyekiti pale, hatuna tena habari ya itikadi inakuwa imekwisha na tunachoangalia pale tunaangalia itikadi ya nchi kwa maana ya Ujamaa na Kujitegemea.

Kwa hiyo, kiongozi yoyote anapokuwepo pale, ndiyo katika Katiba ya Nchi hii tunazungumza habari za ujenzi wa Ujamaa na Kujitegemea. Kwa hiyo tunapoingia pale kazi inayofanyika pale ni kuhakikisha kwamba tunaleta maendeleo kwa ajili ya wananchi wetu kuhakikisha kwamba wanapata huduma muhimu. Hili jambo kama linafanyika kweli kama alivyosema Mheshimiwa Slaa tutalifanyia uchunguzi lakini tunataka kusema kwamba msimamo wetu ni huo kwamba kiongozi wetu akishachaguliwa pale anakuwa ni kiongozi kwa ajili ya Maendeleo ya watu wote bila kujali itikadi zao. *(Makofi)*

Serikali, ikipatia gari la wagonjwa kituo cha afya Malya. Hili wazo lilikuwa la Mheshimiwa Richard Ndassa wa Sumve. Majibu yake ni kwamba kituo cha afya cha Malya ni miongoni mwa vituo mbalimbali nchini vinavyohitaji magari ya wagonjwa. Katika mwaka wa fedha 2008/2009 Serikali ina mpango wa kununua magari 100 kwa ajili ya vituo vya afya na hospitali za Wilaya. Kutokana na ufinyu wa Bajeti Serikali imeshindwa kutenga fedha kwa madhumuni haya. Hivyo Halmashauri ya Wilaya ya Kwimba inashauriwa kutafuta vyanzo vingine vya fedha ili kununua gari hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Savelina Mwijage, Mbunge wa Viti Maalum, alizungumzia Hospitali ya Mkoa wa Kagera iboreshwe kwa kuongezewa fedha na vifaa. Ninaomba kujibu kama ifuatavyo. Upo mpango wa Serikali wa kuboresha Hospitali zote nchini. Kutokana na mpango huo Hospitali zote za Mikoa zitakuwa za Rufaa kwa Mikoa husika na za Wilaya zitakuwa za Rufaa kwa Wilaya husika. Kutokana na Mkakati huo wa Serikali uboreshaji uliopo ni pamoja na kuziongezea hospitali hizo fedha na vifaa. Kwa mwaka 2008/2009 Hospitali ya Mkoa wa Kagera imetengewa kiasi cha shilingi milioni 140.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Mwijage pia alizungumzia kuhusu hospitali ya mkoa ina upungufu wa madaktari na wataalam licha ya kuwepo kwa vifaa vya *X ray* na kadhalika. Majibu yake ni kwamba Serikali inao wajibu wa kuboresha vituo hivyo vya kutolea huduma za afya zikiwemo Hospitali za Mikoa. Kwa mujibu wa Ikama Hospitali za Mikoa kama Kagera inatakiwa iwe na Madaktari 19. Madaktari waliopo kwa sasa ni 14 na upungufu wa madaktari ni wa tano. Hivyo Hospitali ya Mkoa wa Kagera inaonekana kuwa na hali nzuri ikilinganishwa na Hospitali nyingine za Mkoa. Hata hivyo Ofisi yangu itawasiliana na Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii ili kupunguza tatizo la upungufu wa Madaktari katika Hospitali za Mikoa.

Mheshimwia Lucy Fidelis Owenya alizungumzia kuhusu mgawanyo wa rasilimali katika Mikoa uzingatie ukubwa wa Mikoa na Wingi wa watu. Ushauri huu umepokelewa na tutaendelea kuuzingatia katika utendaji wake.

Majengo mapya na marefu yaangaliwe ili yaendane na mfumo wa maji taka. Ushauri huu ulitolewa vilevile na Mheshimiwa Owenya na tunasema hapa kwamba sisi tunaukubali ushauri huu umezingatiwa na utafanyiwa kazi.

**HOJA ZA SERIKALI**

**Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2008/2009**
**Ofisi ya Waziri Mkuu na Tawala za**
**Mikoa na Serikali za Mitaa**

*(Majadiliano yanaendelea)*

**MICHANGO KWA MAANDISHI**

**MHE. HERBERT JAMES MNTANGI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu pamoja na wote waliomsaidia kuandaa hotuba hii nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa napenda kutoa maoni na mapendekezo yangu katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, nina hoja inayohusu Wabunge kutohudhuria vikao vya Kamati za Fedha na Baraza la Madiwani. Licha ya malalamiko ya Wabunge wengi, Ofisi ya Waziri Mkuu haijatoa Mwongozo kama ilivyoahidi Bungeni mara kwa mara, kwani Wabunge hawana nakala zozote za mwongozo.

Hapa Bungeni katika mchango wangu, nilinukuu kauli ya Mkurugenzi Mtendaji Muheza kwamba: "Sifuati kauli na maagizo ya Bunge ila Mwongozo wa Maandishi toka TAMISEMI." Pamoja na hayo, wahusika hawakufanya lolote. Hivi karibuni baadhi ya Wabunge wametoa mapendekezo kwamba Wabunge wasiwe Wajumbe katika vikao vya Halmashauri. Hili linatokana na Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI kutojali hoja za Waheshimiwa Wabunge kwa miaka mingi kuhusu somo hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mwenyekiti wa Halmashauri kuwa na madaraka zaidi ya Mbunge katika Halmashauri: Uteuzi wa Madiwani mmoja miongoni mwa Madiwani wa Kata 20 za Jimbo kuwa Mwenyekiti kunamfanya Diwani huyu na nafasi ya Madaraka zaidi kwenye Halmashauri kuliko Mbunge ambaye ndio mwenye Jimbo lenye Kata zote.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wenyeviti ndio wanashinikiza na kuendesha mikutano wakati vikao vya Bunge vikiendelea kwa uchu huo wa Madaraka na kupitisha hata maamuzi yanayomkera mwenye Jimbo (Mbunge), hasa matumizi mabaya ya Fedha za Halmashauri. Ni vyema utaratibu huu ukaangaliwa upya. Kwa msingi huo huo, Mkurugenzi huchukua ushauri wa Mwenyekiti wa Halmashauri na kumshauri kukubali mambo ambayo Mbunge asingeyaafiki, bila kumshirikisha Mbunge aliyesimama kutoa Ahadi za Serikali na za kwake katika Kata.

Mheshimiwa Naibu Spika, wenyeviti wamekuwa wakiwagawa Madiwani kwa kutumia nafasi zao kupanga Madiwani katika Kamati ya Fedha kwa kushirikiana na Mkurugenzi kukiuka taratibu na kanuni za Uchaguzi wa viongozi katika Kamati za Halmashauri. Tutaendelea hivyo mpaka lini?

Akaunti nyingi za fedha katika Halmashauri sio rahisi kusimamia fedha zinazopitia akaunti nyingi tofauti na kuwa na watia saini benki watu wengi, (kila Mkuu wa Idara) matokeo yake na ubaya wake ni kama ifuatavyo:-

(a)Kamati ya Fedha kutojulishwa fedha zinazoingia katika Idara mbalimbali kutoka Serikali Kuu. Kwa uthibitisho, Ombeni taarifa za Kamati ya Fedha, Halmashauri ya Muheza katika vikao vyote vya mwaka 2008 pekee, mtaona ninalosema. Mhojini Mwenyekiti wa Kamati ndogo Elimu, Maji na kadhalika, mtaona kama anazo taarifa hizo.

(b)Mkurugenzi anakuwa na mahusiano ya karibu na Idara inayopata fedha nyingi na mara nyingi Mkuu huyo wa Idara anapewa nafasi ya kukaimu Mkurugenzi anaposafiri.

(c) Wakuu wa Idara wanatengeneza vitabu vyao kwa ajili ya kutoa *Profoma Invoinces* "tatu" ili kuweza kununua vifaa vya miradi kupitia maduka yenye mahusiano nao na hivyo kuingiza vifaa hewa wakati fedha nyingi zinatolewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Idara ya Ukaguzi wa Ndani kudhoofishwa. Mpango wa Idara ya Ukaguzi wa Ndani ulilenga vizuri kumsaidia Mkurugenzi Mtendaji kuthibiti matumizi ya fedha katika Idara mbalimbali.

Hata hivyo, kutokana na Mkurugenzi Mtendaji kujenga mahusiano ya karibu na baadhi ya Wakuu wa Idara kwa nia ya kuhujumu fedha, dhana hiyo imebadilika na kuleta madhara yafuatayo:-

(a) Mkurugenzi Mtendaji anaagiza Mkaguzi wa Ndani kufuta baadhi ya taarifa za ukaguzi zinazoonyesha matumizi mabaya na hata upotevu wa fedha ili kuwalinda au yeye mwenyewe kujilinda;

(b) Mkurugenzi Mtendaji anatoa mapendekezo ya adhabu kwa Wakaguzi wa Ndani ili kuwatia hofu wasiandike wanayoona. (Haya yote yametokea ndani ya Halmashauri ya Wilaya ya Muheza). Tuangalie utaratibu wa mfumo imara ili kutoa uhuru wa vifaa vya utendaji kwa ukaguzi wa miradi ndani ya Halmashauri na katika Kata zote. Wanahitaji usafiri na kinga za usalama wao.

Mheshimiwa Naibu Spika, fedha za miradi na matumizi ya Ofisi za Wabunge kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu, Ofisi za Mikoa na Wilaya fedha hazifiki kwenye miradi yote inayoelezwa. Katika maeneo machache, fedha zinakotolewa, Mbunge ambaye ndiye anapendekeza kusaidiwa kwa miradi hiyo hashirikishwi katika kukabidhi na kusimamia utekelezaji wake. Pia maombi ya vifaa vya Ofisi ya Mbunge kutoka Ofisi za *DAS* Wilayani, hayatekelezwi. Fedha hizo kama zinapelekwa huko zinabaki huko huko. Mnaweza kuthibitisha hili kwa Muheza iwapo mtapenda.

Kwa maelezo hayo machache, wote tutaona umuhimu wa kuyathibitisha na njia pekee na muhimu ni kukubali kuwa na utaratibu wa kuunda Kamati Teule ndani ya Halmashauri za Wilaya kuibua na kuthibitisha malalamiko ya kweli kama nilivyoeleza hapo juu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na mapungufu hayo yanayohitaji muda kuyarekebisha, naunga mkono hoja.

**MHE. FATUMA A. MIKIDADI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa bajeti nzuri ambayo imezingatia jamii, hasa pale ilipotenga pesa kwa ajili ya kumalizia shughuli za umeme wa kituo cha Somanga Fungu, kwani kelele za Kilwa sasa zitapungua. Ahsante sana.

Kusudi la kuhoji, kwa nini bajeti ya mwaka huu haijatenga pesa za elimu ya ufundi kwa ajili ya Kituo cha Lindi Mkoa *VETA*? Kwa miaka ya nyuma tuliambiwa tutumie Kituo cha Mtwara *VETA*.

Tumefanya hivyo, lakini sasa watu ni wengi na watoto ni wengi, hatuwezi kutumia *VETA*/Ufundi ya Mtwara tu. Ajabu ni kwamba, Mikoa mingine sasa wanajengewa *VETA* za Wilaya wakati sera inasema kila Mkoa utajengewa Shule ya *VETA* ya Mkoa kwanza, ndipo twende kujenga Wilaya. Sisi je?

Mheshimiwa Naibu Spika, katika nchi ilizoendelea, hututhamini sana Shule za Ufundi ili watu wao waweze kujiajiri. Lakini sisi Lindi tutaendelea kuitwa wamachinga, kwani watoto wakimaliza darasa la saba tu, basi huenda Dar es Salaam; kwani hawaendi Sekondari na hakuna *VETA, VETA* ya Mtwara haitoshi. Tusaidieni jamani.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine, tunaomba kupata taarifa ya Tume iliyotumwa kwa ajili ya kuchunguza masuala mazima ya migogoro ya mifugo juu ya uhamishaji wa mifugo kutoka Ihefu kwenda Mikoa mingine kama Lindi, Mtwara na kadhalika. Hali ilikuwaje?

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni barabara zilizosaidiwa na msaada wa *HIPIC,* bado hazijaisha mpaka leo mkoani Lindi. Tunaomba nguvu ya ziada.

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho ni Maji. Lindi suala la maji ni taabu. Miaka kadhaa sasa wananchi wananunua maji kwa ndoo Sh. 1,000/= kila siku. Je, Ule mradi vipi?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa, napenda kupongeza bajeti hii ambayo imezingatia kuwasaidia Madiwani. Kwa kweli Madiwani inabidi wasaidiwe kwani wanafanya kazi nzuri sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kusudi langu ni kuendelea kuchangia maoni yafuatayo:-

Kwanza ni mgawanyo wa Utawala/Maeneo: Vitongoji, Majimbo, Vijiji, Mikoa, Kata, Manispaa, Tarafa, City na Wilaya.

Maeneo hayo sasa yamelemewa na watu wengi, inabidi sasa yagawanywe ili viongozi wahusika waweze kutawala vizuri. Utawala bora unaendana na kiasi cha watu wa kuwatawala na kiasi cha eneo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni upungufu wa fedha wa ajili ya Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya. Pesa wanazotengewa katika *OC* kwa ajili ya mafuta, matengenezo ya magari na posho za safari ni kidogo sana, hazitoshi. Wao kama Wakuu wa Utawala sio vizuri wapite wakiomba omba kwa ma-*DED* au watu wengine, inashusha heshima. Sasa hivi wenye pesa ni ma-*DED*. Kuna safari nyingine nyingi zinatokea za ghafla ambazo hazikupangwa ndani ya *OC* ile. Kwa hiyo, pesa ziongozwe kwa ajili ya dharura. *OC* ya *RC* na *DC* ziongezwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho linahusu suala la Mheshimiwa Mwanawetu - Mbunge wa Kilwa *(CUF),* kumsema *RC* wa Lindi juu yake kuhusu utendaji wake wa kuhamasisha Shule ya Sekondari na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi wananchi wa Lindi kwa masikitiko makubwa sana tunamsikitikia Mheshimiwa Mbunge kusema maneno yale bila kufanya utafiti.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nimwambie Mheshimiwa Waziri Mkuu kuwa, Mkuu wa Mkoa wa Lindi - Ndugu Sadiki ni Mkuu ambaye yupo karibu na wananchi katika kutenda kazi Lindi. Alipohamia Lindi, alikuta Shule za Sekondari 18 tu, lakini sasa ameweza kushirikiana na wananchi na yeye mwenyewe kutafuta misaada kwa wafadhili kwa ajili ya kujengea sekondari hizo. Sasa hivi kuna shule za sekondari 96. Ni Mkuu wa Mkoa ambaye anatembelea hadi Vijijini kuhimiza maendeleo ya Mkoa wa Lindi. Kwa kweli ni Mkuu ambaye anahimiza kazi, pia michezo na mambo kadhaa ya maendeleo. Vile vile ni kada wa CCM mzuri sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi binafsi na wananchi kadhaa tunasema, maneno ya Mheshimiwa Mwanawetu hayana ukweli ndani yake. Hivi sasa Mkuu huyo anasimamia, kufufua masuala mazima ya Kilimo cha Umwagiliaji maji na shughuli za utalii. Siku hizi kumekuwa kwa kweli na maendeleo kuliko zamani. Tunasema kumekucha. Kwa hiyo, usemi wa Mheshimiwa Mwanawetu haueleweki kwa umma wa Lindi, kwani bado wanamhitaji *RC* huyo kwa maendeleo zaidi ya Lindi. Ahsante sana.

**MHE. JUMA ATHUMANI KAPUYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nianze na kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kuteuliwa kwake na Mheshimiwa Rais na hatimaye kuthibitishwa kwa kishindo na Bunge. Nampa hongera sana. Sisi wananchi wa Urambo Magharibi tumefurahishwa sana na uteuzi wake na tunamhakikishia ushirikiano wetu wa moja kwa moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa hotuba yake nzuri na iliyo makini. Imeainisha maeneo yote na vipaumbele vya Serikali ya awamu ya nne kwa ufasaha sana wenye kuashiria utekelezaji utakaoleta mabadiliko

makubwa ya Watanzania kwa ujumla, lakini hatimaye kuzaa maisha bora kwa kila Mtanzania mmoja mmoja. Hongera sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa muda mrefu sasa tumekuwa tukiomba Jimbo letu la Urambo Magharibi sasa lipatiwe hadhi ya Wilaya iwe Wilaya Kaliua. Sababu za kuomba Wilaya hii mpya ni katika kutimiza azma ya Serikali ya kusogeza madaraka kwa wananchi na kwa hiyo, kusukuma maendeleo kwa ari mpya, nguvu mpya na kasi mpya. Wilaya mama ya Urambo ina ukubwa wa eneo la kilomita za mraba 25,595. Hili ni eneo kubwa sana na inakuwa vigumu kutawanya huduma za maendeleo na pia kuzisimamia kwa ufanisi.

Sababu ya pili ni wingi wa watu baada ya ndugu zetu kuhamia kwa wingi sana Wilayani Urambo, hivi sasa ongezeko la watu Wilayani Urambo ni karibu asilimia 4.9 . Kasi hii ya kuongezeka kwa watu kumeifanya Wilaya yetu kuwa na watu takriban 700,000. Idadi hii inatosha kabisa kuigawa Wilaya hii kuwa na Wilaya ya pili ya Kaliua.

Sababu ya tatu ni miundombinu iliyopo. Tunao umeme, shule nyingi za sekondari ikiwemo na ya *"A" Level,* tuna Chuo cha *VETA*, tuna Vituo vya Afya viwili vikubwa sana kiasi kwamba kimojawapo kinaweza kuwa Hospitali teule ya Wilaya mpya. Pia tunacho kiwanja cha ndege. Mawasiliano yameenea, tunazo barabara, reli na simu. Raslimali za Jimbo hili ni nyingi. Ukianza na ari ya watu wake ya kujituma kwa kazi, tunayo mazao mengi ya kilimo kama vile Tumbaku, Pamba, Karanga, Mawese, Alizeti na kadhalika.

Vilevile tuna asali nyingi sana na maeneo fulani fulani yana wachimbaji wadogo wadogo wa madini. Hawa wamedumu hapa karibu miaka 20 sasa. Isitoshe tuna misitu mingi ambayo baadhi yake imetengwa kuwa hifadhi na mingine imezaa vitalu vya uwindaji. Hivi sasa viwanda vimeanza kujengwa Kaliua kama ile *ginnery* ya pamba.

Sababu ya tano ni ari ya wananchi wa eneo hili kuomba wawe na Wilaya yao, nasi hii itarahisisha sana ujenzi wa Wilaya hii kwani nina hakika shughuli nyingi zitafanywa kwa kujitolea.

Kwa kifupi Mheshimiwa Waziri Mkuu, Kaliua ina uhusiano wa kiasili na wananchi wa Ugalla na Mpanda. Pia Mpanda hutegemea kwa kiasi kikubwa kupata maslahi yake toka Tabora. Lakini tunalo tatizo la barabara yenye kutuunganisha toka Kaliua hadi Ugalla. Kwa bahati nzuri barabara ya Mpanda hadi Ugalla inasimamiwa na Mkoa. Kwa hiyo, matengenezo yake yamekuwa ya uhakika sana. Barabara ya Ugalla hadi Kaliua yenyewe bado iko chini ya Halmashauri ya Wilaya ya Urambo. Mgao wa Halmashauri kuhusu fedha za barabara ni ndogo sana na kwa hiyo, barabara hii ambayo ni muhimu sana kwa wananchi wa mikoa yetu hii miwili, haipati matengenezo ya kutosha na kwa hiyo, kuifanya kupitika kwa muda tu.

Ombi letu, tunaomba barabara ya Ugalla hadi Kaliua sasa iwe chini ya *Tanroad* ili ipate matengenezo ya kuaminika. Barabara hii ni mkombozi wa kiuchumi na pia kwa

mateso wanayopata akina mama ambao hupata shida wakati wa masika, reli ya Mpanda inakuwa na matatizo ya mafuriko.

Baada ya kusema hayo, narudia kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa hotuba yake nzuri sana na naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. Namtakia mafanikio mema katika utekelezaji wake.

**MHE. CHARLESI O. MLINGWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Ofisi ya Waziri Mkuu kwa uratibu na usimamizi mzuri wa utekelezaji wa Ilani ya CCM ya mwaka 2005 na mengineyo.

Kwa muda wa utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2005 unakaribia mwisho:-

(a) Naomba bajeti zijazo zitenge fedha ya kutosha kwa ujenzi wa barabara za lami na madaraja katika Manispaa ya Shinyanga kwa kiwango kisichopungua fedha ya kutosha kilomita tano (5) ndani ya Mji wa Shinyanga. Barabara za lami ilikuwa pia ni ahadi za Mgombea Urais ambaye sasa ni Mheshimiwa wetu.

Naomba Manispaa ipewe fedha za ujenzi wa soko bora la Mji wa Shinyanga. Hii ni ahadi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu iliyotolewa Agosti 2006; tayari andiko la mradi huo tulikwishawasilisha Ofisi ya Waziri Mkuu. Nitawasilisha tena kwa kumbukumbu ili ahadi isisahaulike. Shinyanga mjini ni Makao Makuu ya Mkoa, hivyo soko la kisasa ni stahili pia.

Ofisi ya Waziri Mkuu naiomba isikubali upotoshaji wa baadhi ya Wakaguzi wa uendeshaji wa Halmashauri unaoweza kusababisha Halmashauri kukosa fedha ya Ruzuku ya Maendeleo, kama ilivyojitokeza kwa Manispaa yetu.

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nachukua nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mawaziri wa nchi na Naibu Waziri katika ofisi yake pamoja na wataalam wote kwa maandalizi ya hotuba nzuri. Baada ya pongezi hizo naomba sasa nichangie katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Serikali inagharimia ununuzi wa samani katika Ofisi za Wabunge na ujenzi wa ofisi hizo; naiomba pia Serikali kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu igharamie pia uendeshaji wa ofisi hizo kama vile chai, kahawa, sukari na kadhalika.

Aidha, naomba kufahamu Majimbo ambayo Ofisi za Wabunge zinajengwa/zitajengwa kwa miaka ya 2007/2008 na 2008/2009.

Mheshimiwa Naibu Spika, gharama za mafuta zimekuwa zikipanda kila kukicha na kuna dalili zote kwamba gharama za mafuta zitaendelea kupanda. Kupanda huko kwa mafuta kumekuwa na athari kubwa sana kiuchumi, kama vile kupanda kwa bei za bidhaa

mbalimbali pamoja na huduma. Naomba mamlaka zinazohusika, usimamizi wa nishati ya mafuta iweke mikakati madhubuti ya usimamizi wa bei ya nishati hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, bei kubwa za mafuta zimewaathiri hata Waheshimiwa Wabunge. Naomba viwango vya sasa vya pesa zinazolipwa kwa Waheshimiwa Wabunge kwa ajili ya mafuta virekebishwe ili kuwawezesha kufanya shughuli zao kwa ufanisi zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kufuatia mzigo mkubwa walionao Wabunge katika kuchangia/kuhamasisha Maeneo Majimboni, Wabunge waliomba uanzishwe mfuko wa Maendeleo ya Jimbo *(Constituency Development Fund).* Mfuko huo ungesaidia sana kuwapunguzia mzigo Wabunge, yaani kutoa pesa zao mfukoni, kwa ajili ya kuchangia shughuli za maendeleo. Kwa kuwa suala hili ni la muda mrefu sasa, naomba Mheshimiwa Waziri Mkuu alitolee maelezo suala hili. Tatizo ni nini?

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Serikali itimize ahadi yake kwa wakulima; lakini pia itimize yale yaliyoandikwa kwenye Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya 2005. Kilimo kitengewe sio chini ya asilimia 10 ya bajeti ya Serikali. Hilo lilikuwa ni lengo la Wakuu wa Nchi za Jumuiya ya Kusini mwa Afrika – *SADC*.

Mapinduzi ya Kilimo au *Green Revolution* itabakia kuwa ndoto ambayo haitaweza kutimizwa. Watu tunao, ardhi tunayo, kinachokosekana hapa ni dhamira ya kweli. Wananchi wapewe pembejeo za kilimo, kama vile mbolea na mbegu bora kwa wakulima kwa wakati na bei wanaoweza kumudu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kwamba Madiwani wanalipwa posho, lakini bado posho hizo hazitoshi. Naiomba Serikali itekeleze mapendekezo ya Tume ya Mheshimiwa George Lubeleje ambayo ilitoa mapendekezo mazuri sana. Hata hivyo bajeti ya mwaka 2008/2009 imetimiza mengi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wenyeviti wa Serikali za Vijiji wanafanyakazi nzuri na muhimu sana kwa taifa hili. Wenyeviti wa Vijiji ndiyo wanaofanyakazi na *VEOs*, ndiyo Wenyeviti wa Kamati za Maendeleo ya Vijiji, Wenyeviti hao hutumia muda wao mwingi sana kwa shughuli za Maendeleo ya Vijiji. Pamoja na kazi nzuri sana inayofanywa na Wenyeviti hao, bado hawalipwi posho ya aina yoyote.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama CCM inapeleka posho ya Sh. 5,000/= kwa mwezi, hivi Serikali inashindwa nini kuwalipa Wenyeviti wa Vijiji hata posho ya Sh. 5,000/= kwa mwezi? Kwa kuwa Wenyeviti wengi wa Vijiji wamekata tamaa sana kufuatia kutolipwa posho na hivyo kudhoofisha moyo wa kufanya kazi, naishauri Serikali ilitafakari sana suala hili kabla athari kubwa zaidi hazijajitokeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. JANET B. KAHAMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, napongeza sana juhudi zilizofanywa na Wizara ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukuaji wa mji wa Dodoma ni muhimu sana, kwani ni urithi wa Baba wa Taifa kwa Watanzania. Mji wa Dodoma ndio mji ulianzishwa kuwa ni Makao Makuu ya Nchi ya Tanzania. Fedha nyingi zimetumika katika utayarishaji wa *Master Plan* na ujenzi kwa ujumla wa huduma za ugani *(Extension Services).* Ni mji ambao haupati mafuriko ya maji wakati wa mvua za masika kutokana na kuwa na mifereji mikubwa ya maji na kadhalika.

Ni mji uliotengewa na kutengenezewa *Oxidation Pond*, ili maji machafu yamezwe kuchujwa na kuhifathiwa katika madimbwi ya maji ambayo baadaye yatatumika kwa sehemu ya kufanya mazoezi ya mitumbwi *(boating sporting).* Dodoma imetengenezewa barabara nzuri na inapata maji ya kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, Dodoma ni mji uliotengewa maeneo mengi ya nafasi za wazi *(open space)* kwa ajili ya mandhari nzuri za majani na maua na pia kwa ajili ya michezo kwa watoto na kupumzika. Kwa bahati mbaya kabisa au kwa kutokujali na kuheshimu taratibu za mpango wa *Master Plan, Open Space* hizo zimevamiwa na Mafisadi wa Mamlaka ya Ustawishaji wa Makao Makuu ambao ni watumishi husika wa mamlaka hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mji wa Dodoma mjini, kumegaiwa maeneo katikati ya makazi ya watu, kujengwa kwa Minara ya simu kama vile *TIGO, VODACOM* na kadhalika. Sio kweli kama minara hiyo haina madhara, baadaye madhara yataonekana.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mji wa Dodoma hauna majina katika Mitaa mingi ikiwemo Mitaa ya Area *'C'* na *'D'* na kadhalika. Hii inasabasisha wakazi na wageni kubabaika wakitafuta maeneo mbalimbali. Kuna umuhimu wa kufuatiliwa watumishi wanaokiuka taratibu hizi zilizowekwa kwa manufaa yao wenyewe.

Aidha, bustani ya miti na maua ya *CDA* imerudi nyuma, haina miti ya kutosha. Eneo hili ni muhimu sana kutokana na kuwa mbegu na aina mbalimbali za miti na maua yaliyotoka nchi nyingine, mbegu hizo zimepotea. Kuna umuhimu wa Serikali kuinusuru Dodoma na Makao Makuu ya Tanzania.

**MHE. JACOB DALALI SHIBILITI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua fursa hii kukupongeza wewe kwa uongozi wako bora na pia Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa taarifa yenye ufafanuzi wa kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Serikali kwa kazi nzuri ya ujenzi wa barabara wa Mkoa hasa katika Jimbo langu la Misungwi, barabara ya Mwanangwa – Misasi – Inonelwa imetengenezwa vizuri sana. Bajeti hii tunategemea kama watakuwa

na bajeti nzuri waendelee kutoka Inonelwa – Bulingo – Kabale – Busongo – Mwagiligili hadi Mwawile. Yapo baadhi ya madaraja ni hatari, mfano Mwakashu na Mwamagembe. Tunaiomba Serikali iyaone haya ili tusije kuleta ajali hapo baadaye.

Mheshimiwa Naibu Spika, upande wa barabara kuu, Serikali itajenga kwa lami toka Sengerema – Usagara. Tunashukuru bado ipo ahadi ya siku nyingi ya barabara ya Kisesa, Usagara, *Bypass* upembuzi yakinifu umekuwapo kwa muda mrefu sasa watu wameshindwa kuendeleza maeneo yao kwa kuhofia ramani ya barabara hiyo. Tunaomba taarifa juu ya hilo wananchi wajue cha kufanya. Ni lini kazi hiyo itafahamika mipaka yake na kuanza kazi?

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hotuba yake Mheshimiwa Waziri Mkuu amesema Serikali imetenga kiasi cha Shilingi bilioni 23 kwa ajili ya MMAM ili kuanza ujenzi wa Zahanati na ukarabati wa Hospitali za Wilaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya ya Misungwi ilianzishwa 1997 inatumia majengo ya Kituo cha Afya kwa huduma za Hospitali ya Wilaya yapo mapungufu mengi.

Waziri Mkuu amesema Halmashauri baadhi zitanufaika na mpango huo. Namwomba sana Waziri Mkuu na Waziri wa Afya waione Misungwi kuwa inahitaji huduma hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hotuba ya Waziri Mkuu Sekta ya Nishati pia itafaidika na msaada wa Serikali ya Marekani kupitia *Millenium Challage Corporation (MCC),* Dola 206 milioni zitatumika kuboresha miundombinu ya umeme, lakini mikoa iliyotajwa ni Mbeya, Iringa, Morogoro, Dodoma na Tanga. Hali ya Mkoa wa Mwanza ni mbaya, ni kwa nini Mkoa wa Mwanza haumo katika MCC wakati hotuba mbalimbali za Mheshimiwa Rais zimegusia kuwa Mwanza itanufaika na *MCC*?

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba ufafanuzi kwa jambo hilo. Hii ni pamoja na Vijiji vilivyoathirika na nguzo zilizokuwa ziende kwenye chanzo cha Maji Ihelele. Vijiji hivyo ni Buhingo, Seeke, Nyamayinza, Mbalama, Isesa hadi Ihelele (Nyang'homango).

Mheshimiwa Naibu Spika, nakubaliana na Mheshimiwa mtoa hoja kwamba ili kupata mavuno mengi ya uhakika, ni vyema tukaimarisha kazi hii ya kujenga skimu ili wakulima watumie wakati wa kiangazi au mvua kidogo inayopatikana. Wilaya ya Misungwi ni kati ya Wilaya kame nchini. Serikali imejenga skimu mbili, ziko tayari na faida imeonekana kwa wakulima wa maeneo ya Igongwa (Mabuki), Nyambeho (Lubiga), japo tatizo ingefaa yakajengwa mabwawa ya kutunza maji wakati wa masika ili maji hayo yatumike wakati wa kiangazi. Pia zipo skimu mbili zinazojengwa. Moja, iko Nyang'homango na ya pili tayari mkandarasi amekabidhi iko Nyasidala. Tatizo ni kwamba hadi leo hajalipwa. Hali hii ni hatari sana kwa mitaji ya hawa Makandariasi Wazalendo kwani malipo yao huchelewa na riba za Benki hukata mitaji. Swali, ni lini atalipwa na ni sababu zipi zilicheleweshsa malipo? Je, atalipa na riba?

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwa na mauaji ya kinyama ya *albino* na wasioona ambayo Serikali kwa ujumla wake imelikemea sana jambo hili. Pia hali hii kwa Wilaya yetu ya Misungwi tumejipanga kukabiliana na tatizo hilo. Matatizo tunayokumbana nayo ni upungufu wa vyumba vya kulala wanafunzi ambao ni *albino* na wasioona waliopo katika shule maalum ya Mitindo iliyopo Misungwi. Naomba Serikali itoe fedha na kuiona shule hiyo maalum inahitajika sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ahadi za Mawaziri kutembelea Majimbo, niikumbushe Serikali kuwa Bunge lililopita, Waziri wa TAMISEMI aliahidi kutembelea Wilaya ya Misungwi na kujionea hali ya shida niliyoieleza hapa Bungeni juu ya tatizo la barabara ya Mwaniko – Misungwi yenye urefu wa kilomita 28. Barabara hii inahitaji zaidi ya Shilingi milioni 300. Kwa bahati nzuri wakati akiwa Mwanza tayari kwa safari ya Misungwi aliteuliwa na Mheshimiwa Rais kuwa Waziri kamili wa TAMISEMI. Nampongeza sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba barabara hiyo ya Mwaniko - Nguge hadi Misungwi ijengwe. Hali ni mbaya sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja mia kwa mia.

**MHE. KABWE ZUBERI ZITTO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nimeona katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, taarifa kuhusu *TIC* na *TNBC*. Napenda kufahamu kama *TIC* na *TNBC* sasa zipo katika ofisi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Mimi nadhani hapa kuna tatizo kidogo. Vyombo hivi havitapata msukumo stahili hata ukizingatia kuwa Kamati ya Bunge ya sheria na utawala ndio itapitia utendaji wa *TIC* na *INBC*.

Napenda kusema kuwa vyombo hivi ni *"specialized",* hivyo sio sawa kuwa katika ofisi na Kamati ya Bunge iliyo *general*. Suala hili liangaliwe kwa umakini mkubwa sana. Kuna tatizo kama hilo kwa Tume ya Mipango chini ya Ofisi ya Rais. Ninadhani ni bora kuwa na Waziri wa Nchi wa Mipango ili vyombo hivi viwe chini yake ili pia vishughulikiwe na kamati ya Bunge ya Fedha na Uchumi. *Approach* ya Tume ya Mpango *shall be very different, otherwise it will kill the purpose*. Naomba Mheshimiwa Waziri Mkuu aliangalie hilo. Kwa mfano, katika Ibara 137 za hotuba ya waziri Mkuu ni ibara mbili tu (0.015%) ndio zimevutia uwekezaji. Hivyo umuhimu wa *TIC* ndani ya ofisi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ni 0.15% tu. Hii ni hatari.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati najadili (kwa maandishi) Muswada wa Sheria ya Umeme, nilishauri kuhusu kuwapo kwa Gridi nyingine ya Taifa kwa ajili ya usalama wa Taifa. Nimefurahi sana kuwa upembuzi yakinifu wa mradi *Noth-west Grid* (uk. 33, ibara 47) umekamilika. Ninaipongeza Serikali kwa hili. Hata hivyo, gridi hii ni vyema iwe Mikoa ya Kigoma, Kagera, Rukwa, Tabora, ihudumie Shinyanga na Mwanza. Eneo hili ni *sleeping giant* wa uchumi wa Taifa letu. Nishati ya umeme katika eneo hilo itasaidia sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu barabara ya Mwandiga – Manyoni, nashukuru sana kwamba sasa barabara hii inajengwa. Umuhimu wa babarara hii kwa uchumi wa

Mkoa wa Kigoma ni mkubwa. Nitashirikiana na Serikali kuhakikisha kuwa barabara hii inajengwa kwa ubora. Wananchi wa Jimbo la Kigoma Kaskazini wamefurahi sana kupata habari hii njema. Ninaomba Mheshimiwa Waziri Mkuu aje aweke jiwe la msingi la ujenzi wa barabara hiyo. Sasa ni jukumu la Halmashauri ya Kigoma kwa msaada wa Serikali kujenga barabara za Vijiji ili kuunganisha Vijiji na barabara kuu *(feeder roads).* Mfano barabara kutoka Kalinzi kwenda Buganda mpaka Mwagongo itasaidia sana kusafirisha samaki aina migebuka kwenda katika soko la Burundi na pia mji mdogo wa Kalinzi. Ofisi ya Waziri Mkuu itatusaidia kupata utaalam kupima barabara hii ya Kalinzi – Bugamba – Mwamgongo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna tatizo kubwa sana la ardhi Mkoani Kigoma. Mashamba ya wananchi wa Mwandiga yamegawiwa kwa watu binafsi bila ya ridhaa ya wananchi na kuwaacha wananchi *landless*. Kisingizio ni mji mdogo, huduma za mji mdogo hazitolewi lakini ardhi inagawiwa hovyo. Napenda ofisi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu iingilie kati mara moja tatizo la ardhi ya wananchi wa Mwandiga. Lazima tuwalinde wananchi wetu na sio kuwapokonya kidogo walichonacho.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kijiji cha Nyambande, Baraza la Ardhi kwa kushirikiana na Serikali ya Kijiji wamewanyang'anya wananchi ardhi yao. Mzee Aron amenyeng'anywa ardhi yake bila huruma pamoja na wananchi wengine wa Nyambande. Ofisi yako ifuatilie suala hili kwani ni baya sana kwa wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ofisi ya Waziri Mkuu ni vyema sasa ifuatilie suala la miji midogo iliyotangazwa. Kigoma Kaskazini miji midogo ni Kalinzi, Kagunga, Mwandiga, Mahembe na Bitale iliyotangazwa, lakini hakuna lililofanyika isipokuwa pale ambapo maafisa Ardhi wanataka ardhi. Hatuwezi kutekeleza mamlaka ya miji midogo kwa upande wa ardhi tu. Kama mamlaka hazijawa tayari ardhi ibakie kuwa mali ya Kijiji. Huko Uvinza tatizo hili ni kubwa sana. Fuatilia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu muundo wa Serikali za Mitaa, utakumbuka mwezi Novemba, 2006 nilipokuwa nachangia Muswada wa mabadiliko ya Sheria ya Serikali za Mitaa nilizungumzia kwa kina suala la kuangalia upya muundo wa Jiji la Dar es Salaam. Ni hatua nzuri sana. Hata hivyo ni vyema kuangalia upya muundo wa Serikali za Mitaa na Mikoa upya ili kuleta ufanisi kupeleka *parliamentary democracy* katika ngazi ya Tawala za Mikoa. Ni muhimu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kikao cha *RCC* Mkoa wa Kigoma kiliamua kuishauri Serikali kuanzisha Wilaya mpya ya Uvinza na Halmashauri yake. Vile vile *RCC* ya Kigoma ilitoa ushauri mzuri sana na *innovative* kuhusu muundo wa Manispaa ya Kigoma. Tulipendekeza kuwa Manispaa ya Kigoma iwe na muundo wake tofauti na Manispaa nyingine nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumependekeza kuwe na Halmashauri ya Manispaa Kigoma (sio Kigoma –Ujiji); Manispaa iwe na *satellite towns* (tuiite *Township Authorities as provided for by the law*) za Ujiji, Kalinzi, *Satellite towns* hizi ziendeshwe kama Halmashauri za Wilaya lakini *mandate* yake kisheria iwe chini ya Manispaa. Hii

itasaidia sana kuhakikisha kuwa mpango wa kanda maalum ya uchumi *(SEZ)* Unapangwa vizuri. Vile vile Kigoma itaweza kuwa ni *Commercial Capital* ya *Great Lake Region.* Tunataka Kigoma iwe na *Port* ya *DRC* na Burundi kwa maana ya kwamba Dar es Salaam iwe ni *transit port.*

Bila muundo maalum wa Manispaa ya Kigoma itakuwa ni vigumu sana kufikia changamoto hizi za maendeleo. Mimi ninashauri, inaweza kuwa jambo geni, lakini ni *innovative,* tuwe na *Separate Acts* za Dar es Salaam na Kigoma (Dar es Salaam - *Metropolitan Act* na Kigoma - *Special Municipal Act*).

Mheshimiwa Naibu Spika, nadhani ukiangalia Dar es Salaam na Kigoma *within the context* ya sheria za sasa yaweza kuleta utata mkubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la kuongoza Halmashauri ya Kigoma Ujiji kwa mseto kati ya CCM na CHADEMA ni la Kihistoria.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, zaidi ya hapo, suala hili ni letu mimi na wewe. Unakumbuka wakati wa mgogoro wa Kigoma nilikwambia "hatuwezi ongoza pamoja" hatimaye tukawa mseto. Hata hivyo, hotuba yako ime-*playdown* suala hili. Ni suala la ukomavu wa kisiasa Mheshimiwa Waziri Mkuu. Ni muhimu kulisemea kwamba mwaka huu umeya unatoka Chama kimoja kwenda Chama kingine. Kumbuka *we had to amend Local Government Laws fuatila experience* ya Kigoma. Tafadhali lisemee hili na kwamba sasa zamu ya CCM imefika.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda kutoa maelezo ya ziada kuhusiana na sababu za kuiweka *TIC* (Tanzania Investment Centre) chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu. Asilimia 75 ya miradi yote ya *TIC* inaelekea Dar es Salaam, Kilimanjaro, Arusha, Mwanza na Shinyanga kwa sababu ya Madini tu. Tufanyeje ili kuandikisha miradi ya uwekezaji inakwenda kwa nchi nyingine tofauti na zote za kawaida.

Mheshimiwa Naibu Spika, Viongozi wa Vyama vya Siasa ni viongozi muhimu sana katika Taifa, lakini hawapewi hadhi inayostahili. Viongozi wa vyama wanadharauliwa sana na maafisa wa Serikali. Ninatoa mfano.

Mheshimiwa Naibu Spika, viongozi wa Vyama vya Siasa vyenye Wabunge hawana haki kuingia *VIP Lounges* katika viwanja vya ndege hapa nchini. Hii sio haki wala sio vizuri kuhusiana na ahadi ya viongozi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, wiki iliyopita Mwenyekiti wa CHADEMA - Mheshimiwa Freeman Mbowe alipokuwa ametoka safari ya Moshi, aliingia Uwanja wa Ndege wa Dar es Salaam (Julius Nyerere). Alipokuwa amekaa pale *VIP*, walikuja Maafisa Usalama na kumtoa tena kwa bugudha. Hivi hawa Maafisa Usalama wanatumwa na nani kumdhalilisha Mwenyekiti wa Chama cha Siasa chenye Wabunge 11? Tena Wabunge makini kabisa wenye michango yenye manufaa kwa nchi!

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nadhani ni suala la msingi kabisa kuhakikisha kuwa viongozi wa Vyama vya Siasa angalu wenye Wabunge wanapewa hadhi stahiki kwani hawa ni viongozi wenye kuheshimika ndani ya jamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu hakugusua kabisa suala la Sheria mpya ya Tume ya Uchaguzi *(NEC Act).* Kumekuwa na mapendekezo ya muda mrefu ya kuandika sheria hii ili kuifanya Tume kuwa huru na iweze kuendesha chaguzi kwa uhuru ili kuendeleza amani katika Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna umuhimu mkubwa sana kufanya marekebisho ya Sheria ya Uchaguzi ili kuifanya Tume kuwa huru. Vilevile ninashauri kuangalia upya mfumo wetu wa Uchaguzi ili kupanua zaidi mfumo wa uwakilishi wa uwiano *(PR)* ili kupanua demokrasia na kuimarisha vyama vya siasa. Vile vile turuhusu mfumo wa uchaguzi wa watu binafsi kugombea. *I wish all the best.*

**MHE. BRIG. GEN. HASSAN NGWILIZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, katika Jimbo la Mlalo Wilayani Lushoto, wananchi, kupitia Halmashauri ya Wilaya wamekuwa wakiomba kibali kutoka Wizara ya Maliasili ili wajenge barabara kutoka Kata ya Mbaramo hadi Mlalo ili kurahisisha mawasiliano na Makao Makuu ya Wilaya Lushoto. Kimsingi Serikali (TAMISEMI) ilikubaliana na hoja ya wananchi kwani ilitenga fedha Shilingi milioni 60 ili kuunga mkono nguvu za wananchi mwaka 2005/2006.

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wa Kata ya Mbaramo hivi sasa wanaendelea kupata mateso kwa sababu barabara ilipo hivi sasa inayounganisha MBARAMO na Kata ya Mnazi ina mwinuko mkali ambao mabasi na malori hayawezi kupanda isipokuwa magari yenye *four wheel drive*. Aidha, inabidi wananchi wazunguke kilometa 170 kwenda Makao Makuu ya Wilaya (Lushoto) badala ya umbali wa kilometa 50 tu iwapo barabara ya Mbaramo – Mlalo – hadi Lushoto itaunganishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, msimamo wa Serikali wa kufanya *Environmental Impact Assessment* kwanza kabla ya kibali, kinadharia ni sahihi, lakini barabara zote Wilayani Lushoto zipitie kwenye Misitu ya asili. Kisingizio cha kuokoa vyanzo vya maji kinawashangaza wananchi kwa sababu barabara hiyo haitaingilia vyanzo vya maji bali itatambuka *(cross),* vijito ambavyo vitawekewa *culverts* kama ilivyofanyika katika barabara nyingine Wilayani Lushoto. Wananchi wa Jimbo la Mlalo wanaona Serikali yao haiwatendei haki kwa kusitisha maendeleo yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, Waziri Mkuu (na Serikali kwa ujumla) anaombwa aingilie kati suala la barabara ya Mbaramo/Mlalo kwa sababu inahusu kero na maendeleo ya wananchi. Waziri Mkuu atawapa faraja wananchi ya Mlalo iwapo atawahakikishia kuwa Serikali yao ni sikivu na itatoa kibali kilichoombwa.

**MHE. MBARUKU KASSIM MWANDORO:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutoa pongezi zangu za dhati kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu pamoja na Mawaziri wa nchi, Naibu Waziri, Makatibu Wakuu wa Mikoa na Wilaya, wataalam wao

na viongozi wote wa taasisi za Ofisi ya Waziri Mkuu kwa Hotuba nzuri iliyotoa taarifa murua ya utekelezaji wa kazi za Serikali kwa mwaka 2007/2008 na mwelekeo wa kazi za Serikali kwa mwaka 2008/2009. Ni hotuba elekezi na yenye kuleta matumaini makubwa. Naunga mkono Hoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, hotuba hiyo imeeleza kwa ufasaha mkubwa jitihada zilizofanywa na zinazotarajiwa kufanywa na Serikali katika kufanikisha utekelezaji wa malengo ya dira ya maendeleo ya 2025, malengo ya milenia 2015, MKUKUTA na Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya 2005. Ni jambo la faraja kubwa kwamba mkazo umewekwa katika kuhimiza wajibu wa Serikali kuimarisha usimamizi na ufuatiliaji pamoja na utoaji taarifa wa mara kwa mara wa mipango yetu ya maendeleo kwa misingi ya mbinu shirikisihi na hivyo kuongeza uadilifu na uwajibikaji. Hakika haya yakizingatiwa na kutekelezwa ipasavyo, Tanzania itaweza kuzikabili changamoto zote zinazoikabili na kusonga mbele kimaendeleo kwa kasi kubwa endelevu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Serikali kwa jitihada zake za kujenga Ofisi za Wabunge. Naomba jitihada hizi ziendelezwe ili mapema iwezekanavyo azma ya Wabunge kuwa na ofisi stahili ikamilike.

Aidha, ipo haja kubwa ya kuwa na utaratibu ulio wazi zaidi kuhusu fedha zinazotengwa na Serikali kwa ajili ya matumizi ya kawaida na hatimaye *CDF* zinazopitishwa kupitia Tawala za Mikoa. Aidha, naiomba Ofisi ya Waziri Mkuu na Serikali kwa jumla ikamilishe na kutekeleza Mfuko wa Maendeleo wa Jimbo *(CDF)* kama ilivyopitishwa na Bunge hili Tukufu katika bajeti ya 2007/2008.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu uwezeshaji wa wananchi kiuchumi, zaidi ya yaliyoainishwa katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, ipo haja ya kudumisha na kuboresha mifuko na mifumo ya kuwapatia mikopo wananchi hasa walengwa wanyonge ambao mpaka sasa hawajafikiriwa kwa kiwango cha kuridhisha licha ya hamasa kubwa waliyoipata. Matumaini makubwa waliyonayo yaliyowasukuma kujiunga katika *SACCOS* na vikundi vingine vya maendeleo ya kiuchumi na kijamii, pamoja na mambo mengine, mafunzo ya ujasiriamali, ulegezaji zaidi wa masharti ya mikopo na uboreshaji wa utendaji wa wahudumu na viongozi husika ni muhimu kwa mafanikio bora zaidi. Vile vile ipo haja ya kuimarisha *SIDO* kwa karibu zaidi kama taasisi ya mafunzo ya ujasiriamali na taasisi ndogo ya fedha ya kupitishia mikopo hasa kwa mfuko wa mabilioni ya *JK* zaidi ya MKUKUTA.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sehemu kubwa ya mafanikio katika uwezeshaji wananchi kiuchumi na kufanikisha mipango mbalimbali ya maendeleo kunategemea sana umahiri, umakini, uadilifu na uwajibikaji wa viongozi na Watendaji katika ngazi mbalimbali. Zaidi ya kuendeleza mifumo ya kazi na kuwanoa viongozi na Watendaji katika ngazi mbalimbali, kuna umuhimu mkubwa wa kuhakikisha utekelezaji wa *OPRAS* na mfumo *Clients Chartor* kwa dhati zaidi. Aidha, ili kusisimua ufanisi na tija, utaratibu mzuri wa kuweka malengo, kushindanisha na kuzawadia ngazi mbalimbali za utendaji kutoka kaya, Vijiji, Wilaya, Mikoa hadi Taifa ufikiriwe kuanzishwa na kushamirishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni muhimu kusisitiza umuhimu wa Wabunge katika kushiriki kwa ufanisi zaidi katika bajeti zake na utekelezaji wake. Pamoja na Serikali Kuu kuhimiza, mara nyingi sana Wabunge wanakosa fursa za kushiriki katika Mabaraza ya Halmashauri, Kamati za Halmashauri, *DCC, RCC, Road Board* na vikao vingine vya maendeleo na ushauri katika ngazi ya Wilaya na Mkoa, kwani vikao vingi hivyo hufanyika sambamba na vikao vya Bunge. Ipo haja ya kuchukua hatua thabiti kutekeleza sera hii kwa dhati.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile ipo haja ya kuwahusisha Wabunge kwa njia ambayo itaonekana inafaa katika hatua za maboresho ya Serikali za Mitaa. Kadhalika, ipo haja ya kufafanua kuhusu madaraka na uwajibikaji kati ya Serikali Kuu na Serikali za Mitaa katika ngazi mbalimbali ili kuepusha mwingiliano na migogoro isiyokuwa ya lazima.

Mheshimiwa Naibu Spika, mfumo wa stakabadhi za mazao ghalani umeonyesha mafanikio mazuri katika maeneo ambako umetekelezwa. Nashauri Serikali ifanye jitihada ya kuufikisha mfumo huo kwa sehemu nyingine za nchi ambako haujafikishwa, mapema iwezekanavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, inatia moyo sana kwamba hatimaye barabara ya Tanga - Horohoro inatarajiwa kujengwa kwa kiwango cha lami chini ya miradi ya *MCC*. Hata hivyo, sio vyema kuiacha barabara hiyo hadi kuharibika kama ilivyokuwa hivi karibuni wakati tukisubiri utekelezaji wa miradi ya *MCC*. Naomba tuendelee na matunzo ya barabara hiyo ya changarawe hadi hapo utengenezaji kwa ngazi ya lami utakapoanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni jambo la faraja kwamba barabara inayotarajiwa kuunganisha Makao Makuu ya Wilaya ya Mkinga na Tarafa ya Maramba imetengewa fedha kwa ajili ya usanifu. Kwa kuwa barabara hii ni muhimu sana na ambayo kujengwa kwake kutaondoa kero kubwa na kuongeza ufanisi na tija katika shughuli za kiuchumi na kiutawala, ipo haja kubwa za kuipatia barabara hii fedha za kutosha kukamilisha ujenzi wa barabara hii mapema iwezekanavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kero ya maji bado ni kubwa sana kwa Wilaya ya Mkinga. Hata Vijiji vinne vilivyobainishwa kupata maji chini ya mpango wa Benki ya Dunia bado unasusasua. Kwa mipango ijayo, Wilaya ya Mkinga ifikiriwe kwa kipaumbele maalum katika kupatiwa miradi ya maji ya umwagiliaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wa Mkinga wanafarijika kwamba Vijiji vyao vya Daluni, Gumbero na Kwale vimo katika mpango wa kuwekewa umeme chini ya miradi ya *MCC*. Vile vile inatarajia kukamilisha uwekaji wa umeme Mkinga. Litakuwa jambo la faraja kubwa haya yote yakitekelezwa kama inavyotarajiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya ya Mkinga ni miongoni mwa Wilaya za pembezoni zilizo nyuma kimaendeleo. Kwa bahati nzuri Wilaya ya Mkinga ina raslimali nyingi na hali nzuri ya hewa pamoja na ardhi kubwa yenye rutuba nzuri, ukanda mrefu wa mwambao wa bahari, mabonde na milima mingi na hivyo kuwa na nafasi nzuri ya maendeleo ya kiuchumi wa kilimo, viwanda, mifugo, uvuvi na Madini.

Ombi letu ni kwamba, Wilaya hii isiwe mojawapo ya maeneo ya nchi yaliyo nyuma kimaendeleo na kupewa kipaumbele maalum katika kupatiwa raslimali, wataalam na vitenda kazi ili Wilaya hii iweze kupata kasi nzuri ya maendeleo endelevu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya ya Mkinga, ambayo ni ya mpakani ina nafasi nzuri ya kuendeleza biashara ya utalii na shughuli nyingine za kiuchumi na nchi jirani. Kwa kungatia hili, kuna umuhimu mkubwa wa kuimarisha na kuboresha masoko na minada iliyopo Horohoro, Machimboni na kwingineko Wilayani Mkinga.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama Wilaya ya Mpakani, Wilaya ya Mkinga inastahili kuboreshewa miundombinu na vitendea kazi kwa ajili ya kuimarisha ulinzi na usalama ikiwa ni pamoja na barabara ya mpakani itokayo Jasini kupitia Jotohovu, Duga, Mwakijembe na kuunganika na Vijiji vya Wilaya ya Lushoto kando kando ya mto Umba. Kadhalika, kuna umuhimu mkubwa wa kuongeza idadi ya Vituo vya Polisi, idadi ya askari Polisi, magari na vitendea kazi vingine ikiwa ni pamoja na vifaa vya mawasiliano. Vile vile upo umuhimu mkubwa wa kuweka na kuimarisha doria katika Bahari ya Hindi na mipakani yote.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Serikali iendelee na jitihada za kutafuta kutumia gesi asilia na mafuta ya petroli ambayo yanaaminika kuwepo katika Wilaya ya Mkinga.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja asilimia mia.

**MHE. AL-SHYMAA J. KWEGYIR:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa nampongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa hotuba nzuri na kwa kweli imelenga mambo muhimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitaanza na suala la elimu. Naipongeza Serikali kwani shule nyingi zimejengwa. Kikubwa ni kuboresha Elimu ya Msingi na Elimu ya Sekondari. Hivyo basi, nitalenga upande wa watu wenye ulemavu. Naomba walimu wa taaluma ya kufundisha wasioona, viziwi na wenye ulemavu wa viungo wapewe nafasi ya kusoma ili waongezeke, kwani waliopo hawatoshi, kwani elimu ndiyo ufunguo wa maisha. Kwa upande wa maalbino wapewe fursa pamoja na Wasioona kutokana na tatizo la macho *(Short sighted)*. Pamoja na kupata elimu hiyo, watu wenye ulemavu wapewe kipaumbele kwenye ajira. Mlemavu akienda kwenye *interview* anaonekana hafai kuajiriwa kutokana na mapungufu aliyonayo. Naiomba Serikali ilione hilo.

Kwa upande wa afya, naiomba Serikali kwamba zahanati ziongezeke Vijijini ili kuwapa unafuu wanavijiji kupata matibabu kina mama wajawazito na watoto.

Mheshimiwa Naibu Spika, napongeza Waziri Mkuu wa kuboresha maslahi kwa Madiwani kuhusu posho, matibabu na unafuu wa kodi katika vyombo vya usafiri kwani kulikuwa na ugumu wa kufanya kazi ya kusimamia maendeleo.

Kwa upande wa Ulinzi na Usalama, nalipongeza Jeshi la Polisi kwa kushirikiana na wananchi kwa lengo la kukomesha uhalifu. Wananchi wameanza kufahamu umuhimu wa mpango wa ulinzi shirikishi ambao kwa kiasi kikubwa imepunguza uhalifu. Kwa upande wa mauaji ya Maalbino, Vikongwe, kuchuna ngozi na mauaji ya watoto wadogo, naomba Serikali iwachukulie hatua kali hawa wauwaji, washirikina kwa kupelekwa Mahakamani na kuhukumiwa. Hii itakuwa fundisho kwa wengine na balaa hili linaweza kupungua au kumalizika kabisa kwa viumbe wa Mwenyezi Mungu wasio na hatia.

Mheshimiwa Naibu Spika, namalizia mchango wangu kwa kusema naunga mkono hoja. Ahsante.

**MHE. PROF. IDRIS ALI MTULIA:** Napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mawaziri wote katika ofisi yake na Makatibu Wakuu kwa hotuba nzuri yenye kutia matumaini kwa wananchi. Ninaunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niishukuru TAMISEMI kwa kuendeleza ukarabati wa Boma la Utete.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Serikali itimize ahadi ya Rais ya kuifufua barabara ya Kibiti – Mkongo – Utete pamoja na ununuzi wa Kivuko *(ferry)* kipya cha Utete.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Serikali kutathmini maendeleo ya Wilaya zake kisha kuwapelekea Wakuu wa Wilaya wachapakazi na *Developmental Oriented*. Wale Ma-*DC*, wanasiasa wapelekwe katika Wilaya za mijini wafanye kazi ya Itifaki *(protocol),* huko kwetu Vijijini muwapeleke Ma-*DC* wachapa kazi.

Aidha, kuna tabia ya kuwahamisha maafisa wasioweza kazi na kuwapa adhabu ya kupelekwa Wilaya zilizo nyuma kimaendeleo kwa mfano Rufiji. Afisa Kilimo bora aliyekuwa Rufiji, ndugu Mshana ambaye ni mfanya kazi sana, ghafla amehamishwa na kutuletea Afisa Kilimo *reject* kutoka Kibaha. Kesi hii nimeshaizungumza na viongozi wa TAMISEMI pamoja Katibu Mkuu wake anafahamu.

Naomba ahadi aliyoitoa Mheshimiwa Pinda alipokuwa Waziri wa TAMISEMI, pamoja na Ndugu Tarishi - Katibu Mkuu wa TAMISEMI waitimize kwa kuturudishia Afisa Kilimo Mahiri - Ndugu Mshana aje achape kazi Rufiji na huyu aliyeletwa kama *reject* mumpeleke sehemu mnayotaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, naunga mkono hoja. Naiombea Ofisi ya Waziri Mkuu ufanisi katika utekelezaji wa majukumu yake.

**MHE. MWINCHOUM ABDULRAHMAN MSOMI:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote naomba kutoa pongezi kwa Waziri Mkuu, Waziri wa Nchi TAMISEMI, Naibu Waziri TAMISEMI pamoja na Katibu Mkuu wa Ofisi ya Waziri Mkuu kwa kuleta mbele yetu hotuba ya bajeti yenye uchambuzi wa kutosha na yenye matumaini kwa Watanzania. Hongereni sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hayo, katika Jimbo la Kigamboni kuna umuhimu wa kuangalia uwezekano wa kuijenga kwa kiwango cha lami barabara itokayo Kibada – Tungi – Vijibweni Hospitali. Barabara imepuuzwa/imeachwa kwa muda mrefu bila ya kufanyika matengenezo yoyote. Ni muhimu sasa kujenga kwa kuzingatia mahitaji ya wananchi kwa kufuata matibabu Hospitali ya Vijibweni. Barabara hiyo imeungana na barabara kuu ya Kongowe – Feri.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na juhudi za Serikali kuitengeneza Pantoni/Kivuko cha M.V. Alina Dar es Salaam, bado tunaiomba Serikali kuchukua hatua ya kuifanyia matengenezo makubwa M.V. Kigamboni ambayo ni kivuko kikubwa zaidi kuliko M.V. Alina. Kivuko hicho hakina budi kuwekewa mashine nne mpya, kugongwa na kupakwa rangi upya pamoja na kuchomwa upya sehemu ya chini na kuifanyia marekebisho milango yake ambayo kwa sasa hainyanyuki.

Aidha, ni muhimu sana kuwapa motisha mafundi wa vivuko pale Feri – Kigamboni kwa kuzingatia kazi kubwa wanazozifanya kuzifanyia matengenezo mara kwa mara vivuko vilivyopo ambavyo vimechoka. Naishauri Serikali kuwapatia posho maalum.

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wa Jimbo la Kigamboni wanaiomba Serikali kuendelea kuimarisha huduma za Mawasiliano ya simu za mkononi kwa kuwachajisha Makampuni ya simu za mikononi kuweka minara zaidi ya *Celtel, Tigo, Vodaccom* na *Zantel* katika Kata ya Somangila, Kimbiji na Pemba Mnazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wa Jimbo la Kigamboni wanafurahishwa sana na zoezi la Serikali la kupima ardhi chini ya mpango wa mradi wa viwanja 20,000. Hii inasaidia kuokoa tatizo la ujenzi holela katika maeneo ya Jiji.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuishauri Serikali kuwa na utaratibu wa kujenga maeneo maalum ya kilimo badala ya utaratibu wa sasa wa kupima maeneo yote kwa ajili ya makazi. Kutengwa kwa maeneo hayo kutasaidia kulimwa kwa mazao muhimu na mboga mboga kulisha eneo hilo au biashara kama miji mingine inavyofanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni vyema leseni za uvuvi zibakishwe mbili, yaani leseni ya chombo cha uvuvi na leseni ya mvuvi. Leseni za aina ya uvuvi zifutwe kwa kuwa zinamkandamiza mvuvi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja asilimia mia.

**MHE. ANNE S. MAKINDA:** Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa hotuba hii kwa sababu imetoa majumuisho ya shughuli ambazo Serikali imefanya kwa mwaka uliopita na nini kitafanyika mwaka mwingine. Maombi yangu ni kama yafuatavyo:-

(i) Suala zima la kugawa Mkoa wa Iringa ili upatikane Mkoa wa Njombe utakaojumuisha Wilaya za Ludewa, Makete na Njombe limefikia wapi?

(ii) Katika mchango wake Mheshimiwa Jenista Mhagama, katika hotuba hii ya Waziri Mkuu alizungumzia ombi la ujenzi wa daraja ambayo itaunganisha Vijiji vya Mawezo upande wa Halmashauri ya Songea Vijijini na Mikongo upande wa Halmashauri ya Mji wa Njombe. Hii ni ile barabara ya zamani ya Songea – Njombe.

Sasa hivi barabara hii inakoma Maweso na Makoma - Mikongo. Lakini Vijiji hivi vyote viko mbali sana kutoka barabara kuu ya sasa ya Njombe – Songea. Vijiji hivi vina uchumi mkubwa sana wa mazao ya kahawa, ndizi, matunda, na sasa wanaanza kulima chai. Lakini usafiri wao ni wa taabu, kwani haujaunganishwa na daraja hilo. Hali ya maisha ya watu katika Vijiji hivi ni duni sana, kwani wako kwenye mwisho kabisa na hawajaunganishwa. Daraja hilo likijengwa Vijiji hivi vitakuwa njiani na hivyo uchumi wao utakuwa mkubwa sana. Naomba sana Serikali itusaidie

(iii) Mheshimiwa Spika, suala la mbolea ya *DAP* ni suala la uhai wa watu wa Njombe hususani Njombe Kusini. Nafahamu ni mbolea ambayo imepanda sana bei na kwamba Serikali itakuwa na shida kubwa sana kutoa ruzuku kwenye mbolea hiyo. Nakubali hoja zake hizo za Serikali. Mbolea ya *DAP* ni mbolea inayotumika kukuzia mahindi na kupandia viazi katika sehemu hii. Katika nchi hii watumiaji wakubwa wa mbolea hii ni Njombe Kusini na Imalinyi, Njombe Magharibi. Viazi hivi hulimwa mara tatu katika mwaka na ndiyo chanzo kikubwa cha kipato kwa wananchi hao. Viazi hivyo huuzwa Dar es Salaam, Songea, Mtwara, Dodoma na nchi za Kenya na Comoro. Naomba Serikali ijitahidi kwa vyovyote vile kuhakikisha kuwa mbolea hiyo inapatikana tena kwa wingi.

Mahindi kule Njombe huchukua miezi kumi na moja tokea yanapandwa mwezi Novemba na kuvuna mwezi Oktoba wa mwaka unaofuata (miezi kumi na moja). Hiki sio chanzo kizuri cha mapato ya chakula. Viazi ndiyo nguzo kubwa ya watu hao.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii.

**MHE. DR. LUKA JELAS SIYAME:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya wananchi wa Wilaya ya Mbozi, hususan wale wa Jimbo la Mbozi Magharibi, naomba nitoe pongezi kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu binafsi, Mawaziri, Naibu Mawaziri, Makatibu Wakuu, Naibu Makatibu Wakuu, Wakuu wa idara, Watendaji na Wafanyakazi

wote wa Ofisi yake kwa hotuba iliyotayarishwa kwa umahiri mkubwa wa kutoa kipaumbele kwa masuala mbalimbali kama ilivyoanishwa kwenye Ilani ya CCM ya Uchaguzi Mkuu wa CCM 2005.

Napenda pia nitamke kuwa naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Mbozi Magharibi, Wilaya Mbozi Mkoani Mbeya, naomba nianze kwa kuomba Jimbo hili lichukuliwe kuwa duni kimaendeleo na kiuchumi na hivyo kupewa upendeleo maalum kama ilivyo kwa sehemu za pembezoni za mikoa ya nchi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, sababu ya kuomba Jimbo hili kupewa upendeleo maalum kama unaopewa mikoa ya pembezoni ya nchi hii ni kufuatana na maeneo yafuatayo:-

(1) Uduni wa huduma za jamii na miundombinu:-

- Barabara kukosekana kati ya Kata, Vijiji na Vitongoji vya Jimbo hili na pia ukosefu wa barabara kutoka Majimbo mengine kuja Jimboni;

- Ukosefu wa Mawasiliano ya simu Jimboni;

- Uchache wa huduma za Afya Jimboni;

- Ukosefu wa walimu wa shule za msingi na sekondari pamoja na wananchi kujenga shule hizi; na

- Ukosefu wa maji safi na salama Vijijini na Mji Mdogo wa Tunduma.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na jitihada za Serikali kupitia programu mbalimbali za usambazaji maji na wadau mbalimbali wa maendeleo, hususan kwenye Kata za Ivuna, Kamsamba, Chilulumo, Chitete, Tunduma, Myunga na Kapela; mwaka 2007/2008, bado kuna mahitaji makubwa ya maji safi na salama katika Kata nyingi za Jimbo hili hususan Kata za Chiwezi, Chitete, Msangano, Tunduma, Nkangamo, Myunga, Ndalambo na Kapele.

(2) Uduni wa Huduma za Maendeleo ya Uchumi:-

- Kilimo cha Enzi ya Ujima (Jembe la Mkono) na ukosefu wa mbolea;

- Utegemezi wa Kilimo cha mvua. Pamoja na Jimbo hili kuwa na maeneo makubwa ya umwagiliaji, mradi wa umwagiliaji wa sehemu ya Naming’ongo ulisombwa na mafuriko kabla ya kukabidhiwa wananchi, sehemu za umwagiliaji za Iyendwe na Chilangu zimetekelezwa kabla ya kumalizika ujenzi; na

- Ukosefu wa Nishati ya umeme. Kati ya Vijiji zaidi ya 75 Jimboni ni Kijiji kimoja tu cha Katete (Mpemba) na mji mdogo wa Tunduma pekee ndiko kuna umeme ambao hata hivyo una matatizo makubwa kwani unakatikakatika na una nguvu hafifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, matatizo ya Kiutawala na uwiano mbaya wa rasilimali na huduma za maendeleo kutokana na ugumu wa miundombinu, jiografia na eneo kubwa la Jimbo la Mbozi Magharibi. Eneo la Wilaya ya Mbozi ni kilomita za mraba 9,679 kati ya hizo 6,275 ni Jimbo la Mbozi Magharibi ambalo hukaliwa na wananchi zaidi ya 200,000 kati ya 600,000. Hali ya UKIMWI – Tunduma na Vijijini: Kutokana na maelezo hayo mafupi, wananchi wa Jimbo la Mbozi Magharibi wanaandaa mambo yafuatayo:-

(1) Wilaya ya Mbozi igawanywe na kuwa Wilaya mbili kufuatana na Majimbo *(constituencies)* zilizopo sasa, yaani Wilaya ya Mbozi Magharibi yenye Makao Makuu yake Msangano na Wilaya ya Mbozi Mashariki yenye Makao Makuu yake Vwawa, kama ilivyopendekezwa na Baraza la Madiwani *(Full Council)* ya Halmashauri ya Wilaya ya Mbozi tarehe 14 Mei, 2006 na kufuatiwa na uamuzi wa kujenga Ofisi za Bunge Msangano na Vwawa kwa ushauri wa Kikao cha *CMT* (Mbozi) cha tarehe 7 Desemba, 2007 na kufuatiwa na kukubaliwa na kikao cha Baraza la Madiwani *(Full Council)* kilichofanyika kati ya tarehe 17 na 21 Desemba, 2007.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutekelezwa kwa ombi hili kutaharakisha kupeleka maendeleo haraka Jimboni Mbozi Magharibi, ambako hivi sasa kutokana na ukosefu wa miundombinu ya msingi kabisa zikiwemo barabara, mawasiliano ya simu, umeme, huduma za Afya, Maji na Elimu ndogo ya Maisha Bora kwa kila Mtanzania yanawezekana maendeleo kuwa hadithi ya kufikirika.

Mheshimiwa ukiondoa mji mdogo wa Tunduma, toka tupate Uhuru, ukiondoa Mheshimiwa Hayati Mwalimu Nyerere (1981) na Mheshimiwa Fredrick Sumaye (1997) hakuna kiongozi yeyote wa juu Serikalini, kuanzia ngazi ya Mawaziri ambaye amewahi kupelekwa kuzungukia Jimbo langu kutokana na barabara mbaya. Hivyo huishia barabara kuu tu Tunduma.

(2) Barabara ya Kazozi – Kapele- Ilonga km 54 ambayo *TANROADS* wamekwishafanya makisio ya gharama zake kuwa Sh. 1,405,365,990.00 na barabara ya Chapwa – Chindi – Msangano – Chitete – Chilulumo- Kamsamba km 123 (ambayo sehemu ya kwanza ya Chapwa – Chindi – Msangano (km 46) inakisiwa kugharimu TSh. 3,220,630,008.75) kwa mujibu wa barua ya Meneja wa Mkoa *TANROADS* Mbeya ya tarehe 27 Februari, 2008, zitengenezwe, kwani ndizo pekee zenye manufaa kwa wananchi wa Jimbo la Mbozi Magharibi. Ili kuhakikisha uwepo wa barabara hizi, tunaomba zipandiwe hadhi na kuwa barabara za mkoa kama ilivyoombwa na Mkurugenzi Mtendaji wa Wilaya ya Mbozi kwa barua Kumb. Na. MDC/DE/RG/10/172 kufuatia kikao cha Bodi ya Barabara cha Mkoa wa Mbeya cha 8 Mei, 2008.

(3) Huduma za jamii ziboreshwe. Vituo vya Afya na Zahanati zilizopo zipewe vitendea kazi na watumishi kwani mpaka sasa kuna upungufu mkubwa. Wananchi wamekwishaanza matayarisho ya utekelezaji wa Vituo vya Afya kila Kata na Zanahati, kila Kijiji ili kutekeleza azma ya Serikali kuhusu uboreshaji wa huduma hizo.

-Walimu wapelekwe katika shule za msingi na sekondari Jimboni, kwani kwa sasa kuna upungufu mkubwa, kutokana na walimu wanaopangwa huko kutoripoti kutokana na hali ngumu ya miundombinu ya barabara.

-Huduma za maji safi na salama zienezwe kulingana na vipaumbele vyao. Tunaishukuru Serikali na wadau wa maendeleo kwa kasi waliyoonyesha kwa mwaka 2007/2008.

(4)Mradi wa Umwagiliaji wa Naming'ongo, Kata ya Chitete, ulioharibiwa na mafuriko tarehe 21/12/2006 ujengwe upya; na miradi ya Iyendwe na Chilangu imaliziwe.

(5) Huduma za Kinga, Tiba na Ushauri Nasaha ziongezwe Jimboni kwani kutokana na Jimbo hili kwa mpakani na nchi za Zambia na Malawi, hali ya Maambukizi ni mbaya.

**MHE. MGANA I. MSINDAI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakupongeza sana wewe, Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu Mheshimiwa Kombani, Mheshimiwa Marmo - Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Bunge), Mheshimiwa Mwanri - Naibu Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI), Mr. Mrisho - Katibu Mkuu Ofisi ya Waziri Mkuu, Ndugu M. Tarishi, Manaibu Katibu Wakuu, Watendaji wote kwa kazi nzuri za kila siku wanazofanya na pia kwa kutuletea bajeti nzuri yenye nia ya kuwakomboa wananchi hasa wakati huu ambao tunapeleka madaraka kwa wananchi *(D by D).*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nishauri machache ambavyo kwa kweli ni jukumu la ofisi yako kuyashughulikia ili kuondoa kero hiyo kwa watumishi wa Serikali. Watumishi kwa kawaida wanatakiwa kupelekewa mishahara yao kwenye vituo vya kazi, lakini kutokana na sababu mbalimbali, watumishi hao hubidi kufuata mishahara *NMB* au benki nyingine zilizopo Wilayani. Watumishi hao hutumia nauli na mara nyingine hulazimika kulala huko wakisubiri malipo yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa umefika wakati wa kuwahurumia watumishi hawa na kuanza utaratibu wa kuwarudishia fedha wanazotumia.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo lingine kubwa ambalo linaleta matatizo makubwa kwenye Halmashauri zetu za Wilaya ni watumishi kukaa kituo kimoja cha kazi kwa miaka mingi au mtumishi kuajiriwa kituo hicho hicho na kuanza kupandishwa vyeo hapo hapo. Kwa vyovyote, mtumishi aliyeajiriwa na kukaa kituo hicho miaka mingi anatawaliwa na mazingira ya eneo hilo inawezakana kabisa anaanza kushindwa kutoa maamuzi sahihi kwa sababu walioko hapo waliajiriwa nao na wamezoeana sana. Nashauri tena watumishi wote ambao wamekaa kituo kimoja kwa miaka mingi wahamishwe haraka sana na wale ambao wameajiriwa kituo kimoja na kukaa muda

mrefu wahamishwe haraka pia. Ninayo mifano hai na baadhi ya wasaidizi wako na Watendaji wanajifahamu, nisingependa malumbano juu ya mambo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wetu wanaumia sana na asilimia 20 ambayo wanatakiwa wapelekewe akaunti zao zinazotokana na ruzuku ya kodi ya maendeleo. Ruzuku hiyo haiwafikii walengwa kwa sababu sehemu ya fedha hizo hukatwa huko huko Hazina kulipia madeni ya *LAPF, NSSF* na *NIC* ambako huko nyuma Wakurugenzi walikuwa wanakata fedha hizi lakini hawawasilishi kwenye mashirika yaliyotajwa hapo juu.

Hivi kwa nini wananchi wabebeshwe mzigo wa kukatwa haki yao kwa makosa ya watu wengine? Pia fedha zinazobaki zikifika Wilayani haziingizwi kwenye akaunti ya Vijiji. Naomba ofisi yako itafute orodha ya Halmashauri zinazodaiwa fedha hizi na zilipe haraka sana kwenye akaunti za Vijiji na Watendaji waonywe waache tabia ya kuzinyima haki Serikali zetu za Vijiji.

Mheshimiwa Naibu Spika, bado fedha za UKIMWI zinatumika vibaya kwenye Halmashauri nyingi za Wilaya. Ushahidi upo maana mambo haya tunayagundua kwenye Kamati yetu ya *LAAC*. Mpaka leo ofisi yako haijatoa mwongozo kama ule wa *Basket Fund* ambao unaonyesha wazi jinsi fedha hizo zinazotakiwa kutumika. Kama mwongozo huo upo, basi uletwe Bungeni kwenye Kamati ya *LAAC*. Kamati iliwahi kugundua matumizi mabaya kwenye Wilaya ya Mwanga, Nzega, mpaka *CAG* akaagizwa afanye *Special Audit* ambayo nakala zake zilitumwa kwako.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka huu fedha za *VTTP* zimetolewa tena kwenye Wilaya zilizochaguliwa Wilaya ya Iramba ikiwa kati ya hizo Wilaya. Fedha zilizotolewa kipindi cha nyuma maeneo (Wilaya) mengi hazikufanya kazi nzuri kutokana na usimamizi mbovu Wilaya ya Iramba barabara za Mwangeza, Ikolo na Mingela, Dolomoni ndizo zilihusika, lakini kazi haikuwa nzuri kabisa. Kamati yetu ya *LAAC* ilitembelea baadhi ya Wilaya zilizopewa fedha hizi. Fedha za *VTTP* zilifanya kazi nzuri sana Wilaya ya Mheza, wananchi walishirikishwa kikamilifu na mpaka leo barabara hizo bado nzuri na zinatunzwa na wananchi wenyewe. Naomba kwa awamu hii, ofisi yako ifuatilie kwa karibu sana matumizi ya fedha hizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, narudia kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kazi nzuri unayofanya na naunga mkono hoja mia kwa mia.

**MHE. VICTOR K. MWAMBALASWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa naunga mkono hoja. Baada hapo napenda nieleze jambo moja ambalo ni kero sana kwa mapato ya Serikali. Kwa upande wa mafuta yanayoingizwa nchini, Serikali ilifanyie kazi nzuri ya kuiagiza Wizara ya Miundombinu kuweka bandarini vifaa vinavyoitwa *"Flow meters"* vifaa hivi vinasaidia sana kukadiria kodi ya kulipa. Mwaka wa kwanza wa kazi ya vifaa hivi, kodi itokanayo na mafuta ilipanda toka Shilingi bilioni saba mpaka Shilingi bilioni 19. Lakini sasa vifaa hivyo ni mwaka wa pili sasa

vimeharibika. Mamlaka ya Mapato *TRA* iko Wizara ya Fedha na Mamlaka ya Bandari *THA*, iko chini ya Wizara ya Miundombinu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sana Ofisi ya Waziri Mkuu iwakutanishe Watendaji wa *THA* na *TRA* ili vifaa hivi vitengenezwe na kuzidi kuongeza mapato ya Serikali.

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa mchango wangu kwa kumshauri Mheshimiwa Waziri Mkuu namna bora ya kushughulikia mambo ambayo yana maslahi kwa Taifa na wananchi lazima wayaelewe kinaganaga; yakiwekwa uwanjani kwa kiasi fulani yanaboa na kudhalilisha Taifa letu na yasipopata majibu kwa wakati, yaliyo ya kweli yataendelea kuwa mjadala ndani ya Bunge, nje ya Bunge na hata kwa wahisani wetu na hivyo kusababisha hata nchi yetu na uongozi wake kupungua hadhi yake.

Hivyo naomba kushauri kuwa kwa kupitia Kamati ya Uongozi ya Bunge, mambo yote ambayo yatakuwa na athari nilizozielezea hapo juu, ni vyema hasa haya ya ufisadi yaletwe katika Kamati ya Uongozi kwa madhumuni ya kuyachambua yale yenye majibu ambayo ni vyema wananchi wayaelewe. Kamati ya Uongozi ielekeze kamati inayohusika iyatolee maelezo Bungeni, yale ambayo ni nyeti, kamati iishauri Serikali namna ya kuyashughulikia na yale yanayohusu kuchukuliwa hatua za kisheria au kiutawala. Cha msingi ili hatua hizi zifanye kazi, Serikali isirudi tena kuchambua yaliyoshauriwa, kwani matatizo haya yatakuwa yanalundikana, hivyo Kamati nayo itaonekana kutotimiza wajibu wake. Ushauri huu utaipunguzia mzigo na lawama Serikali na pia Serikali itakuwa imelishirikisha Bunge katika utekelezaji wa mambo ambayo ni agenda kwa umma wa Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na Awamu ya Nne kuendelea kuboresha utendaji Serikalini, bado Serikali haiamui kwa wakati muafaka hata pale sheria inapoagiza hivyo. Matokeo yake kwa visingizio visivyo na sababu Wakuu wa Taasisi na Serikali wanaonekana kuwa juu ya sheria. Mfano ni pale *TIC* inapompa *Certificate* ya uwekezaji anapewa idhini ya kuwekeza halafu mwekezaji tena anatakiwa aende kwenye Taasisi ambayo inatoa leseni. Huku ni kukiuka madhumuni ya kuanzisha *TIC* na pia kutokuheshimiwa sheria iliyopo. Hivyo kuleta usumbufu na hasara kwa wawekezaji. Je, nini msimamo wa Serikali kufikia kusimamia utekelezaji wa sheria, kanuni katika kutoa maamuzi kwa muda uliowekwa?

Mheshimiwa Naibu Spika, Watanzania wote haki zao zinalindwa na Katiba ya nchi na sheria zinazotokana na katiba hiyo. Migogoro mingi ya kisiasa hapa nchini ni kwa Serikali kushughulikia jambo moja kwa namna tofauti. Kwa mfano, matatizo ya ardhi kwa ndugu zetu Wahadzabe, wamekwenda *UN* kushitaki, wao hawakupelekwa Polisi na wala hawakusumbuliwa, lakini wazee wao wengi wengine kusumbuliwa kwa madai yao mbalimbali na hata kuwekwa ndani kama mimi mwenyewe ambaye pamoja na wenzangu tulikaa ndani miaka mitatu. Kwa hili, naishauri Serikali isiwabague

Watanzania wakati wanaposhughulikia matatizo mbalimbali ya wananchi *(double standards).*

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kutokujibu barua na malalamiko yao kwa wakati, Mawaziri wengi hawajibu kwa wakati kwa mfano Mambo ya Ndani hadi leo wameshindwa kumpatia pasi ya kusafiria Bwana Sherali alioko London pamoja na Ubalozi. Mimi mwenyewe katika kipindi cha zaidi ya mwaka sasa hajajibiwa. Aidha, Wizara ya Ardhi pamoja na ahadi za miaka mitano hadi leo wameshindwa kumpatia faili lake halijapatikana (Waziri wa Ardhi anaelewa na kadhalika) Serikali ijibu kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kilimo: Wakati wa kuamua malengo ya kila Mkoa kutupa chakula cha kutosha umefika mbali na zile programu zilizopo. Kila mkoa upewe malengo ya kuzalisha chakula 50,000 MT. mbali na zile za sasa (50,000 x 21= 1,050,000) kiwango hiki kinaweza kufikiwa kuwa kuwashirikisha JKT, Magereza vyuo vya kilimo na kadhalika, mikoa iwe na maghala ya kuhifadhi mazao sio chini ya 100,000 =MT.

Tatu, tuandae masoko ya mazao yetu nje, kwenye bei kubwa wakati huu suala la pembejeo na ugavi, kila mkoa uwe na *centre* ya uhakika ya pembejeo. Tusingoje Serikali Kuu, Halmashauri zikae na wadau wanaoweza kuleta pembejeo ambao wana uwezo wa kuleta pembejeo kwa bei muafaka, nayo ni kununua pembejeo kwa kiwango kikubwa kwa mfano ukiagiza mbolea tani 200,000 bei yake ni tofauti na bei ya tani 50,000 na kadhalika. Utaratibu huu waliotumia Egypt kabla hawajajitosheleza kwa mbolea yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, Fedha hii ya *one billion* kwa kila Mkoa inunuliwe matrekta na zana zake zote na kila mkoa upewe mgao wake. Kuliko wa utaratibu wa kuzitoa kama sadaka hivi sasa. Hatua hii ninayoshauri itasaidia sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kupunguza umasikini, kuongeza uzalishaji na kuwapunguzia kina mama muda wa kukaa mashambani.

Naomba irudishwe fedha na uchumi, iliko hakuna utaalamu, hata Kamati inayosimamia haina utaalam *TIC* ndiyo tunayoitegemea kuingiza fedha *FDI*. Hivyo Wizara ya Fedha na Uchumi ndio Wizara muafaka kusimamia Taasisi hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tume ya Mipango Katika muundo wa Serikali, ni vyema ikawa chini ya Rais, lakini aweko Waziri wa Nchi ama Wizara ya Fedha na Uchumi au kwa Rais Mwenyewe, vinginevyo Wizara ya Fedha itatoa uzito mdogo kwenye mipango.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninashauri gharama ya kuendesha Serikali ipunguzwe, kila mabadiliko ya Serikali, Mawaziri, wananunua magari mapya, ofisi inatengenezwa upya na kadhalika, hizi gharama ambazo sio za lazima zipunguzwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Viwanda na Biashara hivi sasa inalipa pango Shilingi milioni 700 kwa mwaka. Ni bora ijenge lao.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. PHILEMON NIKOL SARUNGI:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa hotuba yake yenye msingi, upeo na mwelekeo ya kuimarisha na kusukuma kwa kazi uchumi wa Taifa letu. Napenda kutamka kuwa naunga mkono Hoja.

Nampongeza Mheshimiwa Celina Ompeshi Kombani, Waziri wa nchi Ofisi ya Waziri Mkuu TAMISEMI, kwa kuteuliwa kwake na Rais kuwa Waziri. Nampongeza Mheshimiwa Philip Sang'ka Marmo – *"chief whip"* kwa uteuzi wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na pongezi hizo, sasa napenda kuchangia hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu katika maeneo yafuatayo kwa lengo la kuboresha.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika ukurasa wa 43 – 44 Mheshimiwa Waziiri Mkuu amezungumzia kuhusu hali ya chakula nchini. Tanzania imebarikiwa na Mungu kuwa na ardhi yenye rutuba, mabonde makubwa, maziwa na mito mikubwa isiyokauka.

Wilaya ya Rorya ni mojawapo ya sehemu ya nchi yenye mabonde makubwa, Ziwa Victoria, miti mikubwa, Mara na Mori. Mpango wa miradi ya umwagiliaji ikielekezwa kama ilivyoidhinishwa, Wilaya ya Rorya inaweza kuzalisha tani 6,373 ya zao la mpunga badala ya tani 861 zinazozalishwa sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, maombi la wananchi wa Wilaya ya Rorya ni kama ifuatavyo:-Kwanza, Miradi ifuatayo ya umwagiliaji ifanyiwe ukarabati:-

(a)Mradi wa Chereche - hekta zinazofaa kwa kilimo cha umwagiliaji ni 250. Zinazolimwa sasa ni hekta 110. Mavuno ni tani 435, mavuno yatakayovunwa tani 1,640;

(b)Ochuna Hekta 60 Mavuno tani 225;

(c)Bariki Hekta 50 inayolimwa 35 tu. Mavuno ni tani 164 itakayovunwa iwapo Hekta 50 italimwa ni Tani 308; na

(d)Irienyi Hekta 130 inayolimwa Hekta 8, mavuno ni tani 37 tu. Mavuno yatakayopatikana baada ya kulima Hekta 130 ni tani 853.

Mheshimiwa Naibu Spika, Miradi mipya ni kama ifuatavyo:-

(a)Rwangenyi, Hekta inayofaa 120 inalimwa 0, mavuno yatakayopatikana ni 787;

(b)Nyathorogo Hekta inayofaa (Hekta 400 inayolimwa) mavuno yatakayopatikana ni tani 1,640; na

(c)Kirogo Hekta Inayofaa ni 300 inayolimwa mavuno yatakayopatikana ni tani 787.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya ya Rorya iwezeshwe ili iweze kuchangia ghala la Taifa kwa lengo la kupambana na upungufu wa chakula nchini. Naomba Mheshimiwa Waziri Mkuu aweke Wilaya ya Rorya kama eneo muhimu la kuchangia kilimo cha umwagiliaji nchini.

Kama nilivyotangulia katika ukurasa wa kwanza, Wilaya ya Rorya ina uwezo wa kuvuna tani 6,373 ya mpunga badala ya tani 861 inayovunwa sasa. Wilaya ya Rorya iko tayari iwapo itawezeshwa kwa kuboresha miundombinu ya mabwawa yaliyopo na mabwawa mapya.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Mheshimiwa Waziri Mkuu ahakikishe Kilimo cha Umwagiliaji Wilaya ya Rorya kipewe kipaumbele.

**MHE. HEMED MOHAMED HEMED:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni vyema nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kufika hapa hali nikiwa mzima. Pia naipongeza hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ambayo imeonyesha nia ya Serikali kumgomboa Mtanzania katika maisha yasiyo na uhakika.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo, sasa naomba nitoe mchango wangu katika hotuba hii. Nianze na suala la bomoa bomoa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi yetu ni muda mrefu kunatokezea ghasia za wananchi wetu juu ya kupanga maamuzi ya Serikali kubomoa nyumba zao. Kwa dai la Serikali wananchi wamevamia maeneo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni majuzi tu wananchi wa Mji wa Dodoma walionyesha hasira zao juu ya *CDA* kwa dai la kuwabomolea nyumba zao. Wananchi hawa walijilinda na silaha za jadi kama vile mapanga, visu mishale na kadhalika. Taaluma ya kuwafanya wananchi wawe tayari kwa kupambana na dola ni dosari kubwa kwa Serikali. Nani mkosa kati ya Serikali na wananchi? Ni wapi Serikali haipo? Iweje watu kuingia maeneo na kujenga majumba na kufanya sehemu hiyo ni Kijiji? Hili linaitia hasara Serikali kila leo. Kwa nini iwe hivyo?

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Mahakama ya Kadhi. Ni Kitendawili juu ya Serikali kuwa na maamuzi ya kusuasua juu ya kuwepo mahakama ya kadhi nchini. Kwa kuwa watanzania wana dini zao na iko sheria ya ruhusa ya kuabudu. Waislamu wanahitaji Mahakama inayoweza kutoa haki. Katika hili Zanzibar iko Mahakama ya Kadhi na inafanya kazi zake kama kawaida. Ni kitu gani kinachozuia kuwepo Mahakama ya Kadhi katika Serikali ya Muungano?

Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba Waziri Mkuu atupatie ufumbuzi wa suala hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kuvunjika kwa muafaka kati ya *CCM* na *CUF,* kwa kuzingatia kauli ya Rais wetu, juu ya mkono wake wa kuwepo mpasuko wa kisiasa kati ya Unguja na Pemba ilikuwa na maeneo muhimu ya kuthaminiwa na kutekelezwa. Pamoja na kuundwa kwa Kamati ya Muafaka, hatimaye kuvunjika, kitendo cha kuvunjika kwa muafaka ni vyema Serikali isisite kufanikisha kauli ya Mheshimiwa Rais kwani azma ya Rais Kikwete ni kuinusuru nchi katika migogoro ya wenyewe kwa wenyewe. Ni vyema kuzingatia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu madawa ya kulevya nchini, nchi yetu ina usalama mipakani mwetu. Maeneo ya bandari zetu pamoja na nyanja za ndege inaonekana maeneo haya ndio njia zinazotumika kupitisha madawa hayo. Tuseme Serikali imeshindwa kuzuia madawa hayo ambayo yanasababisha nguvukazi ya nchi yetu kuathirika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu miundombinu ongezeko la Kipato cha nchi yetu ni kuwepo kwa barabara za uhakika. Ni vyema Serikali iandae mikakati mahususi ili iweze kuzikarabati barabara zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ongezeko la mahitaji ya umeme linaongezeka siku hadi siku. Kwa kuzingatia hili, ni vyema Serikali ipange mipango ya kuondoa tatizo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kuhusu Utawala Bora. Inafahamika cheo cha Mkuu wa Mkoa sio cha kisiasa. Kumfanya Mkuu wa Mkoa kuwa mwanasiasa ni kasoro, kwani kunaweza kuufanya Mkoa kukosa maendeleo. Nchi yetu ni ya mfano wa vyama vingi. Kuna baadhi ya viongozi hao ni wanasiasa. Jambo ambalo hupelekea Mkuu huyo kushindwa kuzungumza na Wapinzani. Ni vyema Serikali isimamie suala hili ili Watanzania waweze kuiletea nchi yao maendeleo.

Baada ya maelezo yangu hayo nasita hapa. Ahsante.

**MHE. JOHN PAULO LWANJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri Sera nzuri itungwe ili kufidia wakulima kwa eka na mifugo inayoharibiwa na wanyamapori. Kifuta jasho cha Sh. 100,000/= kwa hekta sio sahihi, ni kubeza juhudi za wakulima na kuwadhalilisha kwa kubaki ombaomba wakisubiri uponi kutoka Serikalini. Pia fidia halisi tuiweke Sh. 10,000,000/= kwa kila mtu anayeuawa na mnyama mkali ili watoto waweze kuanza maisha mapya baada ya kufiwa. Kifuta jasho cha Sh. 200,000/= sio lolote wala chochote; hakina utu ndani yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, Jimbo la Manyoni Magharibi lina mbuga za hifadhi ya Rungwa na Mhesi na Chaya; zaidi ya *12,000* $km^2$, Makampuni zaidi ya 12 ya uwindaji lakini pamoja na mapato makubwa yatokanayo na uwindaji, hakuna cha maana kinachorudi kuendeleza Jimbo hilo. Pia mbao, asali na nta ni mazao muhimu, pamoja na tumbaku. Lakini nini kinakuwa *"ploughed back"* Jimboni? Hakuna. Serikali iangalie

jambo hili. Naiomba Serikali ianzishe Wilaya kamili ili kusimamia vyema raslimali za Jimbo hili muhimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwakani, kipaumbele cha Serikali iwe barabara ili barabara za vijijni zitengenezwe kwa makini zaidi ili zipitike. Barabara zikiwa nzuri, watu watajiajiri wenyewe katika kilimo na biashara. Uganda na Kenya kila mara ziko mbele yetu kiuchumi kwa sababu barabara nyingi nchi hizo ni za lami hadi Vijijini. Bila barabara, hakuna fursa ya maendeleo. Mwaka jana tu Jimboni kwangu, hata shule zilifungwa baada ya mvua kunyesha na kuharibu barabara.

Mheshimiwa Naibu Spika, nishati ya umeme ihimizwe ili tupate viwanda vidogo vidogo vya kusindika mazao mbalimbali. Naiomba Serikali iwekeze kusaidia kwenye nishati hiyo kama kipaumbele cha pili baada ya barabara.

Mheshimiwa Naibu Spika, naishauri Serikali ianzishe Bodi ya Asali na Nta ili kusimamia mazao haya muhimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, taasisi za fedha zinazokopesha wafanyakazi zimezuka kama uyoga. Kuna zenye riba hadi asilimia 50, wameingia mikataba ya kijanja na wafanyakazi na kuwafilisi. Hawana tena mishahara kutokana na makato yanayofanywa ku-*service* mikopo hiyo.

Matokeo yake ni kwamba walimu na watumishi wengine hawafanyi kazi wanatangatanga kutafuta namna ya kujikimu na kuwakwepa wafilisi baada ya kushindwa kulipa madeni. Anayeumia sasa ni wanafunzi. Naishauri Serikali ichuke mzigo wa madeni hayo.

**MHE. GIDEON A. CHEYO:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, napongeza Mheshimiwa Mizengo Peter Pinda (Mb) kwa kuteuliwa kuwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Amekwishaonyesha uwezo mkubwa wa kuongoza, namtakia mafaniko mema. Aidha, napenda kumpongeza Mheshimiwa Kombani kwa kuteuliwa kuwa Waziri wa Nchi TAMISEMI na Mheshimiwa Aggrey Mwanri kwa kuteuliwa kuwa Naibu Waziri (TAMISEMI). Wote nawatakiwa mafanikio mema.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa hotuba yake nzuri ambayo imegusia maeneo mengi ya msingi katika maendeleo ya nchi yetu. Katika lengo la kuunga mkono hoja hii naomba kuchangia maeneo machache.

Naipongeza Serikali kwa programu ya uendelezaji Mifumo ya Masoko ya mazao ya Kilimo. Wilaya yangu ya Ileje imo katika programu hii, tunaomba maeneo zaidi yaongezwe katika programu hii ili wakulima wengi zaidi waweze kufaidika. Aidha, kwa kuwa kuna mpango wa kujenga soko pale ISongole mpakani na nchi jirani ya Malawi, naiomba Serikali ikubali na kuteleza ombi letu la kupandisha hadhi barabara ya kutoka Mpemba (Mbozi) hadi Isongole (Ileje) kuwa ya Taifa. Barabara hii ikijengwa kwa

kiwango cha lami itakuwa imara zaidi, usafiri utaboreshwa, biashara kati ya nchi yetu na Malawi itaongezeka. Wenzetu wa Malawi nao wanaimarisha barabara ya upande wao kwa kiwango cha lami.

Naipongeza Serikali kwa uamuzi wa kuboresha maslahi ya Madiwani. Nashauri maboresho ya maslahi yaende sambamba na maboresho ki-uongozi na kitaaluma kwa Madiwani ili waweze kuongoza na kusimamia kwa ufanisi zaidi shughuli zote za Halmashauri zao.

Aidha, ratiba za vikao vya Halmashauri zinazowataka Wabunge kushiriki, ziendelee kuboreshwa ili kusiwe na mgongo na ratiba ya mikutano ya Bunge. Ni muhimu sana kwa Wabunge kushiriki vikao vya Halmashauri vinavyowahusu. Hii italeta mshikamano kati ya Wabunge, Madiwani na Watendaji.

Naipongeza Serikali kwa kuanzisha utaratibu wa kutoa taarifa kwenye magazeti kuhusu uwasilishaji wa fedha katika Halmashauri zetu.

Nashauri Wabunge wawe wanapewa taarifa hizo kwa urahisi wa ufuatiliaji. Pengine hili lingehusu Wizara zote zinazowasilisha taarifa muhimu kwenye Halmashauri, Wabunge wapate nakala ya taarifa hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kukumbushia maombi yetu ya tangu awamu ya tatu kuhusu Tarafa mpya na Kata mpya. Kutokana na jiografia ya Wilaya yetu, tuliomba tuwe na Tarafa nne (4) badala ya mbili za sasa na Kata mpya ya Kalembo.

Aidha, maombi machache ya nafasi za Watendaji wa Vijiji yamewasilishwa ofisini TAMISEMI kwa idhini. Tunasubiri kibali.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumalizia kwa kuwapongeza Watendaji wote ngazi ya Wizara, Mkoa, Wilaya na Halmashauri kwa juhudi zao na maandalizi ya bajeti hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. DR. CYRIL AUGUST CHAMI:** Kwanza, nikupongeze Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa hotuba yako ambayo kama unavyoona, inapongezwa na Waheshimiwa Wabunge wote, hata wale wa upinzani. Napenda pia kuwapongeza Waheshimiwa Mawaziri, Naibu Waziri, Makatibu Wakuu, Naibu Makatibu Wakuu na Watendaji wengine wote wa ofisi yako kwa maandalizi mazuri ya hotuba hii ya Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nina ombi moja na pendekezo moja. Kwanza, mapato ya Mlima Kilimanjaro yakatwe sehemu fulani (tuseme japo 10%) kuendeleza Halmashauri zinazozunguka mlima Kilimanjaro, hasa katika nyanja za elimu, afya,

barabara na Kilimo. Jambo hili sio geni hapa kwetu Tanzania na linafanyika kwa maeneo yanayozunguka vivutio mbalimbali vya utalii au maeneo ya migodi.

Mheshimiwa Naibu Spika, bado Mlima Kilimanjaro una nafasi kubwa zaidi ya kuliingizia Taifa letu mapato kama Wizara ya Maliasili na Utalii itawahamasisha wawekezaji wawekeze katika *crane tourism*, ili wapenda mazingira (watalii) wanaopenda kufika kileleni au hata urefu wa aina fulani lakini hawana uwezo wa kupanda mlima wenyewe waweze kupandishwa kwa *crane* hizo kwa kulipia fedha. Aina hii ya uwekezaji imefanikiwa sana *Cape Town (Table Mountains)* na China.

**MHE. EMMANUEL LUHAHULA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyochangia kwa kuzungumza, nampongeza tena Mheshimiwa Waziri Mkuu na timu yake yote. Napenda kuchangia yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuishauri Serikali ifanye utaratibu mahususi wa kuwakusanya watu wanaozagaa mijini bila kazi. Serikali ifungue/ianzishe mashamba ya umwagiliaji, hawa watu wapelekwe huko, kwani kwa kufanya hivyo tutapunguza kundi la watu wasiozalisha na kuongeza pato la Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ikumbukwe kwamba miaka iliyopita, Baba wa Taifa - Hayati Mwl. J.K. Nyerere aliwahi kufanya hivyo kwa kuwachukua wasio na kazi Dar es Salaam na kuwapeleka Kigamboni.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali naomba barabara zifuatazo zingaliwe kwa karibu sana.
Kwanza ni Isako – Kahama – Bukombe – Rusumo. Barabara hii inasaidia sana kusafirisha mizigo kwenda nchi jirani Rwanda, Burundi, Congo na Uganda.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niulize: Je, barabara hili itafanyiwa kazi? Mheshimiwa Naibu Spika, wakati wa ziara ya Mheshimiwa Rais Wilayani Bukombe tarehe 23 Agosti, 2007 waliahidi kutengeneza barabara ya Ushirombo – Buselesele kwa kiwango cha Moramu. Je, imefikia wapi?

Mheshimiwa Naibu Spika, iko barabara iliyoahidiwa kujengwa kwa kiwango cha lami barabara la Runzewe –Bwanga.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya ya Bukombe kiusalama sio shwari sana. Naomba uwepo mpango mahususi wa kuweka ulinzi maeneo yote ya barabara ya Bukombe Ruzewe – Nyakanazi – Lusahunga na kuendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba tujifunze jirani, zetu Burundi na Rwanda sehemu zote zenye matatizo ya usalama kuna ulinzi kila baada ya kilometa kadhaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango Mheshimiwa Pesambili Mramba ulikuwa mzuri sana. Badala ya kumtafuta Mbunge mmoja mmoja, naomba Mheshimiwa Waziri Mkuu aandae muda mzuri ili Mheshimiwa Mramba atoe semina.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuishauri Serikali ifanye utaratibu wa kupata maelezo toka kwa kila Mbunge nini mahitaji ya Jimbo lake. Serikali ikijua tatizo la kila eneo toka kwa Mbunge, itasaidia sana kupanga bajeti yake. Mfano: Bukombe tunahitaji umeme, kutenga maeneo ya utawala, ina maana Serikali itaandaa bajeti kufuatana na matakwa hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba umeme Bukombe. Fanyeni kila liwezekanalo ufike huko, vinginevyo mambo magumu.

Mheshimiwa Naibu Spika, utafiti wa Madini wa muda mrefu unachosha wananchi wa Bukombe, nisaidieni. Kwa mfano *Resolute Co. Ltd* wapo muda mrefu. Nashukuru sana Serikali kupitia Wizara ya Nishati na Madini kuonyesha mweleko wa kuwasidia wachimbaji wadogo wadogo wa Bukombe.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli ziara ya Mheshimiwa Adam Malima - Naibu Waziri alisaidia sana. Mungu Ambariki.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. PROF. RAPHAEL MWALYOSI:** katika kifungu No. 33 ukurasa wa 25, yanaainishwa masoko yaliyojengwa na kukamilika nchini ikiwa ni pamoja na soko la Mlangali (Ludewa). Soko hilo limekuwa linajengwa kwa miaka miwili sasa na halijakamilika na kukabidhiwa. Mategemeo ya wananchi wa Ludewa yalikuwa kuanza kutumia soko hilo katika msimu huu wa mwaka 2008 wa mauzo. Naomba nielezwe kwa nini soko hilo halijakamilika na kwa sababu gani na ni lini litakamilika?

Katika Kifungu Na. 46 ukurasa wa 32 Serikali inaeleza kuwa imenunua kivuko cha Mto Ruhuhu chenye uwezo wa kubeba tani 50. Ni kweli kivuko tumepata lakini kuna matatizo. Kwanza, kilikosa mwendeshaji (dreva) na hakikutumika kwa muda mrefu kwani dereva alitoroka. Baadaye aliwekwa dereva asiye mzoefu akakigongesha kivuko na hadi leo hakijatengenezwa na hakitumiki. Napendekeza kuwa, wapewe mafunzo watu wanaotoka Manda au Mbinga (Lituhi) ili waendeshe kivuko hicho badala ya kuleta madereva kutoka nje ya Manda na Lituhi. Mbadala wake ni kuanza kufikiria ujenzi wa daraja katika eneo hilo la kivuko.

Katika kifungu 47 ukurasa wa 34 inasemekana kuwa *TANESCO* imekamilisha kazi ya kuweka nyaya za kuwambaza umeme kutoka Mji wa Ludewa. Ahadi ya Serikali ya maandishi ilikuwa kukamilisha mradi huu Desemba, 2006. Hadi leo tunaelekea kumaliza kipindi cha miaka mitano, mradi huu bado kukamilika. Naomba maelezo kwa nini mradi haujakamilika na lini utakamilika?

Mwaka 2007 Wizara ya Maliasili na Utalii iliendesha mafunzo kwa wavuvi wa Ludewa na Mbinga kutoka Ziwa Nyasa ambao ni endelevu kwa kutumia ndoana katikati ya ziwa na hivyo kutumia boti za kisasa na injini *(Motorized boat).*

Aliyekuwa Waziri wa Maliasili na Utalii wakati huo Prof. Jumanne Maghembe, aliwaahidi wananchi wavuvi wa Ludewa kutoka Ziwa Nyasa boti ya kisasa na injini yake kwa ajili ya kuendeleza mafunzo hayo endelevu kwa vikundi vya wavuvi. Tayari vikundi kadhaa vya wavuvi vimeundwa kwa kujiandaa na mafunzo hayo na kisha kupata mikopo ya maboti na injini kwa ajili ya uvuvi endelevu. Naomba Waziri wa sasa wa Mifugo na Uvuvi - Mheshimiwa John Magufuli atimize ahadi aliyoitoa Waziri mwenzake kwa wananchi wavuvi wa Ludewa.

Utekelezaji wa mkakati wa kuhifadhi mazingira ya Ardhi na vyanzo vya maji (Kifungu 114 ukurasa wa 77) hauwezi kuwa na tija. Kwa vile nielewavyo mimi, nadhani hakuna *Baseline Data* iliyotayarishwa kutumia kama msingi wa kuperemba mabadiliko ya mazingira ya ardhi na vyanzo vya maji nchini. Naomba ushahidi kwamba *Baseline report* ipo.

**MHE. CHARLESI N. KEENJA:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kwanza nimpongeze Waziri Mkuu - Mheshimiwa Pinda kwa hotuba yake ya Bajeti ya kwanza ambayo imeyatendea haki maeneo yote yaliyoko chini ya uongozi wake. Naunga Mkono hoja hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi yetu ina muundo mzuri sana wa uongozi na utawala ambao unashuka hadi karibu sana na wananchi katika ngazi ya nyumba kumi. Kama muundo huu ungewezeshwa, maendeleo yetu yangekuwa ya kasi kubwa sana. Kwa bahati mbaya mfumo huu hasa katika zile ngazi muhimu za Kata na kushuka chini, haufanyi kazi. Kwa maana hiyo, mpango wa *D by D* umeishia kwenye ngazi ya Wilaya au Mji na bila kushuka kwenda ngazi za chini zaidi, matatizo ya maendeleo yaliyopo yataendelea kuwepo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo kubwa ni kwamba mamlaka na rasilimali za Serikali za Mitaala hazikukasimiwa kwa ngazi za chini. Kamati za maendeleo za Kata zinatakiwa kuandaa makadirio ya matumizi ya kila mwaka lakini hazijulishwi ni nini kilichokubalika au kilichoshindikana. Kunapokuwapo mradi au shughuli ya kufanya katika Kata au Mtaa, utekelezaji hufanywa na Mamlaka inayohusika bila kushirikisha Kata au Mtaa unaohusika. Hali hii inafanya Kata na Mitaa wajione kwamba hawathaminiwi na hawana shughuli za kufanya. Chombo pekee ambacho kinafanya kazi na ngazi hizo za chini ni *TASAF* na wamepata mafanikio makubwa katika kutekeleza shughuli zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa mfumo wetu wa utawala haufanyi kazi chini ya ngazi ya Wilaya/Mji, hakuna maandalizi yaliyofanywa katika ngazi hizo. Viongozi hawapewi mafunzo juu ya kazi zao, hawana ofisi wala samani, hawana sehemu

za kuhifadhia fedha na makabati ya kuweka kumbukumbu na kadhalika. Kwa hali hiyo, hawako tayari kupokea madaraka na majukumu yaliyowahusu. Jitihada za Serikali zimekuwa zinahamisha mamlaka na rasilimali kutoka Wizarani na Mikoani na kuzilundika kwenye Halmashauri za Wilaya na Miji na haijahakikisha kwamba uwezo huo unapelekwa kwa wananchi kupitia kwenye Kamati zao za Maendeleo ya Kata na Viiji au Mitaa.

Kutokana na hali hii, shughuli zote za maendeleo na kutoa huduma zinaachwa kuisubiri Serikali ikazifanye. Hata pale ambapo uongozi ungeweza kutumia raslimali zilizopo, haifanyiki hivyo. Moyo wa kujitolea umekufa kabisa na madhara yake ni makubwa sana kwa kuwa Halmashauri za Wilaya na Miji hazina uwezo wa kufanya kila kitu kila mahali, pia haziwezi kuwa kila mahali kila wakati. Inabidi hatua zichukuliwe kuandaa ngazi za Kata na Mitaa/Vijiji ili ziweze kuchukua majukumu yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi sasa, vikao vya Kata na Mitaa havifanyiki kwa kuwa wajumbe wa vikao hivyo hawaoni umuhimu wa kukutana. Hata hivyo, ngazi hiyo hukusanya mapato ambayo yanapotezwa bila ya kuwa na manufaa kwa wananchi. Kwa mfano kila anayeuza nyumba, shamba au kiwanja, hulipishwa asilimia ya bei ili Kata au Mtaa utoe idhini na kupiga mihuri na saini kwenye kumbukumbu husika. Fedha zinazokusanywa hufujwa na wanaohusika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inapaswa kuendelea na mpango wa kurekebisha Serikali na Mitaa ili kufikiria ngazi zilizoko karibu na wananchi. Vinginevyo *D by D* haina maana iliyokusudiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, narudia kuunga mkono hoja.

**MHE. JUMA KILIMBAH:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu kunipa afya njema na hata kupata fursa hii kuchangia hoja ya bajeti ya Makadirio na Matumizi ya Waziri Mkuu na Taasisi zake kwa mwaka wa fedha 2008/2009.

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue nafasi hii kutoa shukurani kwa Waziri Mkuu -Mheshimiwa Mizengo Peter Kayanza Pinda, Mheshimiwa PhilIp Sankl Marmo - Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Uratibu na Bunge), Mheshimiwa Celine Ompeshi Kombani – Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI) na Mheshimiwa Aggrey Mwanri - Naibu Waziri wa TAMISEMI.

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue fursa hii tena nitoe shukrani kwa Katibu Mkuu Ofisi ya Waziri Mkuu na wasaidizi wake kwa kazi nzuri ya maandalizi ya hotuba hii ambayo Ofisi ya Waziri Mkuu ndiye Mtendaji Mkuu wa shughuli zote za Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa mchango kuhusu TAMISEMI. Wizara hii ni Mtambuka, kwani baada ya shughuli zote za Serikali Kuu kuwa mikononi mwao kwa maana ya kupitia Halmashauri za Wilaya, Miji, Manispaa na Jiji. Ni dhahiri fedha nyingi sana za ruzuku zinapelekwa moja kwa moja kama vile *Capital Development Grant*

*(CDG), Global fund, Road fund,* fedha za maji na kadhalika. Utaratibu wa Serikali Kuu ni mzuri sana kwani unafanya urahisishaji wa utekelezaji wa shughuli za maendeleo moja kwa moja kwa mamlaka ya wananchi wenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na dhamira nzuri za Serikali, lipo tatizo kubwa ambalo linazikabili Halmashauri zetu kama vile *capacity* ndogo ya utendaji, wizi wa fedha za miradi, utawala mdogo wa Madiwani, pia ushirikishwaji wa wananchi kwa miradi inayotekelezwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili tuweze kupiga hatua za haraka za maendeleo ni vyema basi katika mwaka wa fedha 2008/2009 masuala haya yarekebishwe hasa kwa kuwa na ikama ya watendaji wenye sifa kwa idara mbalimbali kama vile Kilimo, Maji, Barabara (ujenzi), Afya na kadhalika. Wataalam hawa pia wawe na sifa za uadilifu kiutendaji. Kadhalika, semina za usimamizi wa Fedha za Halmashauri zinazotoka Serikali Kuu zitolewe kwa Madiwani wote na isiwe kwa upande wa ile Kamati ya Fedha peke yake. Uelewa wa Madiwani juu ya Mapato yanayoingia katika Halmshauri yatasaidia kwa kiwango kikubwa kuepusha ubadhirifu wa fedha za Halmashauri, pia kutasaida usimamizi wa miradi kuwa madhubuti *(value for money)* na hivyo kuondoa tatizo la mradi mmoja kutekelezwa mwaka hadi mwaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na Halmashauri kuwafanya *participatory Research Assesment (PRA)* wanachi, bado utaratibu huu haukidhi malengo na matarajio ya ushirikishwaji bado semina za *PRA* ni za kustukiza, maandalizi ni madogo mno, lugha inayotumika bado inatatizo wananchi wengi, suala la *ownership* ya miradi kwa wananchi halieleweki. Katika utaratibu huu napendekeza juu ya maandalizi ya kutosha kwa kuwaandaa wananchi, ili kushiriki ipasavyo, lugha nyepesi itumike ili wananchi kuelewa miradi na mali yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue nafasi pia kuelezea suala la wajibu wa viongozi na wananchi, juu ya kuzungumzia suala la Mkakati wa kuondoa umaskini na kukuza uchumi (MKUKUTA). Mkakati huu ni muhimu sana kwa dhamira ya kweli. Kama utatekelezwa kwa ukamilifu, basi Taifa letu litakuwa ni Taifa la watu wenye uelewa na utekelezaji wa majukumu kiufanisi na hivyo nchi yetu kuwa na maendeleo endelevu.Eneo hili la MKUKUTA, suala ya utawala bora limo, kwa maana hiyo, kila kiongozi kuelewa wajibu wake wa utekelezaji shughuli za maendeleo ni muhimu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika eneo hili nasisitiza juu wa wajibu wa viongozi katika kila kada na kwa kuwa Ofisi ya Waziri Mkuu ndio msimamizi Mkuu wa shughuli za Serikali, basi iwe ni wajibu ili kutekeleza yale yote yaliyomo kwenye MKUKUTA.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nizungumzie suala la mgawanyo wa Kata na Vijiji, kwa hivi sasa maeneo ya kiutalwa ni makubwa sana hivyo utekelezaji wa majukumu ya Serikali kupitia Watendaji wa Kata na Vijiji unakuwa ni mdogo hii ni kutokana na kukosa nyenzo za kufanyia kazi, naomba Ofisi ya Waziri Mkuu TAMISEMI izingatie maombi ambayo tayari yamewasilishwa kwao kwa ajili ya mgao wa Kata za Shule ili kupatikana Kata ya Mgongo,Kata ya Kuselya ili izaliwe Kata ya Mwandoigembe, Kata

ya inampanda ili izaliwe Kata ya Maluga, Kata ya kiombi ili izaliwe Kata ya *Old Kiomboi*. Pia Vijiji vya Songambele kipatikane Kijiji cha Luzilukulu, Kijiji cha Kizonzo kipatikane Kijiji cha Msansao, Kijiji cha Masagi kizaliwe Kijiji cha kinkungu na kadhalika. Maeneo ya Kata na Vijiji, hivi ni makubwa sana hivyo naomba Waziri Mkuu atoe baraka zake ili zoezi la kuvigawa litekelezwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na ukweli kwamba hali ya siasa ya nchi yetu ni nzuri, hasa katika mfumo wa vyama vingi, lakini Ofisi ya Waziri Mkuu iwe makini na utoaji ruzuku kwa vyama ambavyo ni dhahiri uendeshwaji wake ni wa ubabaishaji na havionyeshi mahesabu kwa mujibu wa taratibu ya daftari la Msajili wa Vyama.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. DR. WILBROD PETER SLAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuchangia katika eneo lifuatalo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa vile kwa muda mrefu sasa tumekuwa tukiedhesha mpango wa maboresho wa Serikali za Mitaa *(Local Government Reform Program)* na kwa kuwa mpango huo unafikia mwisho wake mwaka 2008 Je:-

(a)Tumekwishafanya tathmini ya mpango unaoendelea na kufahamu tumefanikiwa wapi na tumekwama wapi katika malengo yaliyowekwa? Waheshimiwa Wabunge wanaweza kupata nakala ya tathmini hiyo kama imefanyika na kama haijafanyika kuna utaratibu gani kufanya tathmini hiyo?

(b)Kwa kuwa mpango ulioko unakwisha: Je, tuna mpango gani wa kuendelea na mpango huo, na kama majadiliano yamekwisha na wadau waliokuwa wakifadhili mpango huo na kama wapo ni nchi zipi zinakubali kusaidiana nasi katika maboresho haya?

Mheshimiwa Naibu Spika, natanguliza shukrani za dhati, naunga mkono hoja nikitumaini kupata maelezo ya kina.

Naomba kupata ufafanuzi ufuatao:-

Kwa vile Mheshimiwa Philip Marmo - Naibu Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu ametangaza kwa kuomba mwongozo wa Spika, 26 Juni, 2008 kuhusu Wabunge wanaopata nyaraka za Serikali, napenda Waziri Mkuu atupe ufafanuzi wa kina:-

(a)Je, kwa mujibu wa sheria ya Nyaraka za Serikali, ni nyaraka zipi hasa zinatakiwa kuwa za siri?

(b)Je, upo waraka umeandikwa *"siri",* lakini unakwenda kinyume na maadili ya uendeshaji bora wa Serikali? Unaokwenda kinyumbe na maslahi ya Taifa? Una vigezo

vyote vya ufisisadi? Waraka huo bado una kinga ya waraka wa Serikali wenye hadhi ya usiri na hivyo kulindwa na sheria ya Nyaraka za siri za Serikali?

Mheshimiwa Naibu Spika, iwapo Serikali imegubikwa na matatizo ya kuficha uchafu: Je, Mbunge ana kosa gani kuwa na waraka wa aina hiyo ambao Watanzania wenye uchungu na nchi yao wamemkabidhi Mbunge ili atimize wajibu wake wa kuisimamia Serikali kikamilifu?

Mheshimiwa Naibu Spika, Waziri anayetaka kutumia vyombo vya dola, badala ya kutafuta ukweli wa Taarifa hiyo, yeye anataka uchafu ufunikwe na kufichwa, katika kipindi hiki cha kusafisha uchafu katika Serikali yetu ni kwanini asijiuzulu? Kama hayuko tayari kujiuzulu kwa nini asifukuzwe kazi? Kwani dhahiri hana dhamira ya kupambana na ufisadi, uwizi wala uchafu ndani ya Serikali yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hili nisipopata maelezo na majibu ya kina nitatumia kifungu cha kuondoa shilingi.

Natanguliza shukrani za dhati.

**MHE. KABUZI F. RWILOMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na maelezo mazuri ya Bajeti, napenda kuulizia kwamba Mheshimiwa Waziri Mkuu ametaja ujenzi wa Ofisi za Wabunge: Je, katika mpango huo Jimbo la Busanda limefikiriwa? Mimi sina ofisi popote pale, naomba Mheshimiwa Waziiri Mkuu aje unitembelee aone mwenyewe. Hakuna ofisi! Haipo!

Mheshimiwa Naibu Spika, fedha za Ruzuku nimesoma kitabu cha fedha zinazopelekwa kwenye Halmashauri, inakuwaje *Municipal* zinapewa pesa zaidi ya ruzuku ya kilimo kuliko Halmashauri za Vijiji? Wanafanya kazi gani ya kilimo? Naomba wakazi wa mijini wapewe pesa za barabara na sio za kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nasikitika kutoa taarifa kuwa Geita tumepokea barua ya mwanasheria toka ofisi yako inayotuzuia tusitoze *Service Levy* wa kuwa wanaishi Dar es Salaam au Mwanza. Wanaishi huko lakini *operations* zao ziko Geita na zinatuathiri sisi, hivyo sio busara kulipa Mwanza.

Naomba suala hili la *Service Levy* liwekwe wazi kwa nini *service levy* isimamishwe Wilaya ya Geita. *Head office* zao zisiwe tatizo, kwani wengine wana *Head Office* Nairobi, Afrika Kusini na Lusaka, hawa hawatalipa *service levy*? Barua hiyo iliandikwa tarehe 18 Juni, 2008 na Ndugu Luanda kwa niaba ya Katibu Mkuu.

Tunaomba mgao mpya wa Vijiji utoke haraka. Halmashauri zinamwangusha Mheshimiwa Waziri Mkuu. Ni wezi sana! Unda mkakati.

**MHE. DR. MAUA D. DAFTARI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. Nampongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mheshimiwa Celina Kombani, Mheshimiwa Prof. Peter Msolwa na Mheshimiwa Mwanri kwa kuteuliwa kwao kushika

nafasi mbalimbali. Nawatakia mafanikio mema katika utekelezaji wa majukumu yao. Nampongeza Katibu Mkuu na Watendaji wenzake wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru Waziri Mkuu na viongozi wote kwa kushirikiana kikamilifu katika mazishi ya mume wangu na kunifariji pia.

Mheshimiwa Naibu Spika, natoa hongera kwa hoja ya Waziri Mkuu iliyogusa maeneo mengi kwa kina. Ninayo maoni yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la ujasiriamali linahitaji sana kuvaliwa njuga, kuwekewa mikakati maalum na ufuatiliaji ili kwa kiasi kikubwa waweze kuchangia uchumi wa nchi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi ninapoandika mchango huu, fedha zilizotolewa na Mheshimiwa Rais Kikwete na Rais Karume kule Pemba haijatoka kutokana na urasimu. Sina hakika iwapo zitawafikia wale ambao tayari wameshaelimishwa juu ya ujasiriamali na wako tayari. *Bureacracy* zinadumaza maendeleo yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala la ulinzi na mipaka yetu, upo umuhimu wa kufanya makusudi ya ununuzi wa boti za doria ili ziwasaidie walinzi wetu kutekeleza vyema majukumu yao. Visiwa vyetu maeneo makubwa viko wazi, watu wanaingia katika maeneo ya panya bila kujulikana. Wakati wa uchaguzi walifika hadi wageni toka Mombasa kuja Pemba kupiga kura. Sasa ni wakati muafaka kuimarisha maeneo nyeti ya bahari yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Mheshimiwa Waziri Mkuu afanye kwa makusudi kusukuma *Head quarters* za Polisi Pemba zikarabitiwe na yale majengo mabovu yabomolewe na kujengwa upya. Maeneo hayo yanaitia aibu sana Serikali. Hakujatenga fedha za marekebisho. maeneo yafuatayo yanahitaji msukumo wa Serikali Kuu.

1. Polisi *Head Quarters* – Chake chake
2. Ofisi za fundi magari - Wete Polisi
3. Ofisi ya Polisi - Mtambile na Mkoani

Mengine, nina hakika Wizara ya Mambo ya Ndani watashughulikia ila maeneo hayo hayajaonwa na yanahitaji msukumo toka juu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ya Muungano isaidie kwa makusudi upatikanaji wa umeme wa uhakika Pemba. Serikali ya Mapinduzi Zanzibar isaidiwe hataka kwa *SMT* kuongea na wafadhili. Ahadi ni nyingi za muda mrefu, matokeo ni sifuri. Naelewa umeme sio suala la muungano ila hili lazima *SMT* lisaidie ili kudumisha ulinzi na usalama nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, lazima tufike mahali, suala hili la kuwa kila mtu ni fisadi liishe. Ufafanuzi utolewe basi kwa kuelimisha wananchi ili waweze kuelewa kwa

kina. Nina wasiwasi, upinzani sasa wanatu-*engage* tuache kunayofanya muda wote tuanze kushutumiana. Ujanja huu ni vyema ueleweke. Mafisadi wapigwe vita kwa nguvu zote ila tusi-*over do!!*

**MHE. BENSON M. MPESYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naomba nianze kwa kusema naunga mkono hoja hii kwa nguvu zote na kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri Mkuu na Wasaidizi wake wote kwa kazi nzuri ya maandalizi ya bajeti bila kuwasahau Mawaziri wafuatao: Mheshimiwa Celina Kombani, Mheshimiwa Philipo Marmo na Mheshimiwa Aggrey Mwanri, wamekuwa ni msaada kwetu Wabunge unapoleta kero za wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, naomba nieleze mchango wangu katika maeneo makubwa yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ukubwa wa Jimbo la Mbeya Mjini, naomba Serikali iliangalie upya na upokee mapendekezo yangu ya kuligawa Jimbo la Mbeya Mjini na kupata Majimbo mawili ambayo takriban kila Jimbo litakuwa na karibu watu 200,000 kwa sababu zifuatazo:-

(i) Jiji la Mbeya limepanuka mno katika kipindi cha miaka 20 iliyopita, kwa kuwa na ongezeko kubwa la idadi ya watu takriban watu 400,000 ina karibia mno na idadi hiyo;

(ii) Pamoja na idadi hiyo, zipo Tarafa mbili tu, Sisimba na Iyunga, ni vema tungepata Tarafa nne, ambapo kila Tarafa ingekuwa na takriban watu 50,000;

(iii) Jimbo langu lina Kata 36 na Waheshimiwa Madiwani 51. Napendekeza kama kila Jimbo lingekuwa na Kata 18 na Madiwani wasiopungua 25 kwa kila Jimbo, hii ingerahisisha shughuli za maendeleo za Jiji la Mbeya.

(iv) Shughuli za wakazi wake (anuai) – wakati Kata 16 zina sifa zote za wakazi wa jiji na 20 ni *peri-urban* ambapo shughuli zao kubwa ni kilimo, wakati kati ya Jiji ni biashara na huduma.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Serikali ituhurumie watu wa Jiji la Mbeya. Lengo langu ni kutoa hduma zinazostahili. Pia Kata mbili za Iyela na Iwambi zinastahili kugawanywa, kwani Kata kama ya Iyela ina taribani watu 30,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri viongozi walioteuliwa na Rais katika ngazi ya Mkoa na Wilaya wasiwe chanzo cha migogoro na kuwagawa wananchi kwa kuendekeza matakwa yao binafsi. Muda mwingi unatumika kwa malumbano badala ya shughuli za maendeleo. Hivi ni kweli Serikali yenye mkono mrefu, imeshindwa kuliona hili? Hivi ni halali au ni maadili ya kiongozi, *DC* au *RC* kuwa sehemu ya makundi ya kisiasa, tena kwa kushiriki katika kampeni na kuacha shughuli za msingi za kusimamia maendeleo na *monitoring* ya shughuli za Serikali.

Hili likipuuzwa litaleta wakati mgumu kisiasa. Wananchi wanasema hajawahi kuona viongozi wa namna hii. Hivi sasa *DC* wa Mbeya ana ugomvi na Meya wa Jiji na hata Mbunge ambao ni Wawakilishi wa wananchi. Kisiasa hatukuwa kambi moja. Tarehe 21 Juni, 2008 *DC* alikuwa sehemu ya kundi lililofanya Mkutano *Holiday Hotel* kufanya maandalizi ya viongozi anaohitaji baadaye huko Mbeya mjini. Hivi muda huu si angeutumia kwa kazi za Serikali?

Inawezekana *DC* alikuwa bora sana huko alikotoka, lakini kwa Mbeya amepoteza uelekeo. Kuwatisha viongozi wenzake katika Wilaya sio busara. Hivi karibuni amemwandikia Meya wa jiji la Mbeya, eti ajieleze kwake ajibu tuhuma. Ni sheria ipi inayompa madaraka hayo? Yeye ni mshauri na kazi yake ni *monitoring and valuation* ya utekelezaji. Pia *role* yake ni ya *facilitation,* sheria ya Uhimili ilishafutwa, akumbushwe.

Kazi za maendeleo hazifanyiki ila malumbano. Kwa nini Mbeya tunapuuzwa? Mimi ni kipindi changu cha pili, haya mambo ni mageni ya kutunishiana misuli katika Wilaya. Heri Yanga na Simba wanacheka sio sisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja iliyowasilishwa na Waziri Mkuu kwa mwaka wa fedha 2008/2009.

Hoja yangu naomba niielekeze kwenye suala zima la barabara za miji yetu mikubwa, lilikuwepo jiji la Mbeya. Katika mwaka wa fedha wa 2007/2008, Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI) na kwa ahadi ya Waziri Mkuu mwenyewe pia ahadi ya uchaguzi ilikuwa ni kutengeneza barabara ya *Airport* – Iyela kwa kilometa moja kwa kiwango cha lami. Iyela ndiyo Kata kubwa ndani Jiji la Mbeya, ina watu takriban 30,000. Pia ni eneo lenye taasisi nyingi za Serikali na za watu binafsi. Lakini hawana usafiri wa uhakika na kisha kuwa kero mno, kwani wakati wa masika/mvua watu huhamishwa kwa mikokoteni maana maji hujaa sana. Naiomba sana Serikali itimize ahadi hii kama ilivyoahidiwa 2007/2008 kuwa imetenga Shilingi milioni 300 kwa ajili ya barabara hii. Naomba hili litekelezwe tafadhali.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. SIJAPATA F. NKAYAMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nianze kabisa kwa kumpongeza Waziri Mkuu - Mheshimiwa Mizengo Peter Pinda kwa kuteuliwa kwake na Rais - Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, vile vile niwapongeze na walioteuliwa na Rais, Mheshimiwa Celina Kombani kuwa Waziri wa Ofisi ya Rais (TAMISEMI) pamoja na Mheshimiwa Mwanri kwa kuteuliwa kuwa Naibu Waziri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa watoto wanasomeshwa na Halmashauri kwenda Kidato cha kwanza na kuendelea, wale watoto wanaosomeshwa na Halmashauri hizo ambao ni wale watoto yatima na wale wasiojiweza, watoto hao wamekuwa wakisumbuka katika masomo yao kwa kutolipiwa na Halmashauri hizo mpaka watoto wamesimamishwa masomo. Je, pesa hiyo ni ya *DED* au ni haki ya wale watoto?

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2003 – 2004 Serikali Kuu iliamua kulipa watumishi wa Afya malimbikizo ya likizo, *on call allowance*, matibabu lakini kuna watumishi ambao hawakulipwa wakati huo walisahaulika, lakini mimi niliweza kufuatilia malipo yao, lakini mpaka leo bado mwaka 2006 nilileta majina hayo TAMISEMI Dodoma, 2007 nikampelekea majina na idadi ya pesa wanayoidai. Majina hayo yalipelekwa kwa Mheshimiwa Peter Pinda akiwa bado ni Waziri, alipopandishwa cheo na kuwa Waziri Mkuu, baada ya uteuzi wake niliamua tena kupeleka majina hayo kwa Mheshimiwa Waziri aliyekuwa ameteuliwa, Mheshimiwa Wasira.

Mheshimiwa Naibu Spika, mpaka leo hakuna chochote au lolote linalozungumzwa hapo. Majina hayo yamewekwa pembeni: Je, hao watumishi ambao hawajalipwa malipo hayo mpaka sasa miaka mitano, hao watumishi watakuwa na mori wa kufanya kazi? Nilikuwa naomba Serikali iwaonee huruma ili watumishi hao waweze kufanya kazi kwa ari mpya, kasi mpya na nguvu mpya.

Mheshimiwa Naibu Spika, marehemu hawatendewi haki na warithi vilevile hawatendewi haki hata mara moja. Kuna askari mmoja jina lake ni P/C Hasan Mluya *Force No. E5552* alifariki tarehe 27 Mei, 2000. Mirathi No. 48/1/2001 mpaka leo bado mrithi wake hajalipwa. Nimetembea kwenda Makao Makuu Polisi Dar es Salaam – Hazina Dar es Salaam, jina lake lilionekana Hazina kuwa aliorodheshwa tangu tarehe 22 Julai, 2002, lakini mpaka sasa mrithi huyo hajalipwa. Je, Serikali inasemaje kuhusu malipo ya marehemu huyo?

Mheshimiwa Naibu Spika, katika swali la msingi lililojibiwa na Naibu Waziri wa Usalama wa Raia bado hajawa Mkuu wa fedha alisoma Bungeni swali na kujibu kuwa Vita vya Kagera mwaka 1978 kuwa walilipwa fidia. Mheshimiwa Naibu Spika, sikubaliani na majibu hayo kwa sababu si kweli kama walilipwa baadhi na wengine walibakia bila kulipwa. Kwa kuwa ushahidi Askari *EX5299 P/C* hamisi alipigana vita vya Kagera na alikuwa katika kikosi cha *26 K Brigade 207* ya Marehemu *Walder (Brack Mamba)* akiwa Luteni Kanali Bayeke Mkuu wa *Support* akiwa *Cap*. Msabaha – waliokuwa wakubwa walilipwa fidia hizo na waliokuwa wadogo hawakulipwa fidia bali walilipwa malimbikizo ya mishahara yao tu. Kwa hiyo, nilikuwa naomba wale askari ambao bado hawajalipwa fidia hiyo walipwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hotuba ya Waziri wa Fedha alisema, maji hayakutengewa pesa. Wanawake waliopo Kigoma Vijijini vile vipara vyao kuongezeka katika kujibu swali Bungeni mwaka 2007 Mheshimwa Shamsa Mwangunga wakati akiwa bado Naibu Waziri wa Maji alisema kuwa mwaka huo hautakwisha bila kupata maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa akina mama wanazidi kusumbuka, nilikuwa naiomba Serikali kuwatupia jicho la huruma.

**MHE. BERNADETA K. MUSHASHU:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa hotuba yake nzuri, iliyotoa mwanga mzuri

wa utekelezaji wa Ilani kwa kipindi kilichopita na kwa mwaka ujao wa fedha 2008/2009. Nawapongeza Waziri wa TAMISEMI, Naibu Waziri, Makatibu Wakuu na Watendaji wote walioandaa Hotuba hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, hotuba ya Waziri ni nzuri, inaleta matumaini. Maisha bora kwa kila Mtanzania yatawezekana kama tutaboresha Kilimo. Wenye hotuba ya Waziri wa Fedha, nilizungumzia kwa kina mapendekezo ya kuboresha kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi wananchi wanavuna. Juzi nilikwenda Kongwa, kuna mazao mengi na kwa wingi watu wanaendelea kuwauzia walanguzi. Wakulima wanaendelea kupata fedha kidogo na hivyo kuendelea kuwa maskini. Naomba Waziri Mkuu atueleze ni lini mfumo mzuri wa kununua mazao ya wakulima wenye tija utaanza ili kuwanusuru wakulima hawa waondokane na umaskini?

Mheshimiwa Waziri Mkuu, nakupongeza kwa kuboresha maslahi ya Madiwani. Madiwani ndio walio karibu na wananchi. Wao ndio wanaosimamia fedha za Halmashauri, wengine maeneo wanayosimamia ni makubwa sana, hawawezi kuyatembelea yote kwa mguu. Hivyo nakupongeza kwa uamuzi huo. Kilio changu kikuu kwa Mkoa wa Kagera ni uwanja wa ndege. Wananchi wanasikitishwa na kuona badala ya kwenda mbele wanarudi nyuma. Hawawezi kuendelea bila kuwa na miundombinu muhimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri Mkuu aje atutembelee Bukoba, kukuonyesha hayo matatizo na atueleze ni lini basi uwanja huu utatengewa fedha, ili upanuliwe na kutengenezwa kwa kiwango cha lami?

Mheshimiwa Naibu Spika, wanafunzi wengi, hasa mijini kama Dar es Salaan wanapata matatizo makubwa sana kwa sababu Serikali imeshindwa kutekeleza jukumu lao la kuwapatia wanafunzi usafiri. Watoto hawa wanatoka nyumbani asubuhi sana (usiku) na kurudi nyumbani usiku sana wakiwa wamechoka. Je, ni lini Serikali itaanza kununua mabasi ya wanafunzi hasa kwenye mji mkubwa kama Dar es Salaam?

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. DR. RAPHAEL CHEGENI:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na pongezi kwa hotuba ya bajeti hii, napenda kuomba masuala yafuatayo yatekelezwe na Serikali katika mwaka huu wa fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba tusaidiwe kugawa Wilaya ya Magu. Mkoa wa Mwanza ili kupata Wilaya mpya ya Busega. Jimbo la Busega limetimiza vigezo vyote vya ku-*warrant* Wilaya muda mrefu uliopita na kwamba ni muda sahihi wa kufanya maamuzi ya msingi. Sambamba na ombi hili ni pamoja na kugawa Kata za Mkula, Kalemera, Malili na Ngasamo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkoa wa Mwanza umekuwa ni mkubwa sana kwa vigezo vyote na kwamba hatua yoyote ya kuchelewesha kuugawa mkoa huu sio tija kwa wananchi wa Taifa. Namwoma Mheshimiwa Waziri azingatie ukubwa wa eneo, idadi ya watu, Wabunge na hali ya kiuchumi. Katika misingi sahihi ya utawala bora ni vyema Serikali ikatekeleza maombi haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, vikao vyote muhimu kwa ngazi zote vimeridhia mapendekezo ya kugawa Wilaya ya Magu kupata Wilaya mbili za Busega na Magu na pia kuugawa Mkoa wa Mwanza.

Naomba Serikali itoe msukumo wenye kipaumbele kwa maslahi ya wananchi wa maeneo haya na kukidhi azma ya utawala bora.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii.

**MHE. SAVELINA S. MWEAJAGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa nimeshachangia kwa kuongea. Sasa naomba nichangie tena kwa maandishi. Nawapa pole Mkuu wangu wa Mkoa Enos Mfuru pamoja na kamanda wa Polisi kwa kazi ngumu ya majambazi ambao hawapungui pori la Kimisi, Kasindaga, Buligi. Naomba Serikali kuongeza Polisi. Pili, kuhusu uwanja wa ndege, kweli tutaendelea kulia na usafiri mpaka lini, miezi yote mpaka mwishoni mwa mwaka?

Naipongeza Serikali kwa kutoa pesa za ujenzi wa Ofisi ya Mkuu wa Mkoa, nashukuru sana. Kuhusu wafanyakazi wa Hospitali ambao wako hapa Mirembe wanasoma, mbona wanazungushwa kulipwa pesa? Hata juzi walikuwa wameambiwa hawatafanya mitihani mpaka walipe pesa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanini Serikali haiweki mikakati ya mbolea angalau wakulima wa Karagwe, Ngara, Muleba ili na wenyewe waweze kuwa na nguvu za kulima? Naomba wananchi warudishiwe baiskeli na pikipiki zao. Kama kushtakiwa washitakiwe kuliko kukaa zimelundikana, huo ni unyanyasaji mkubwa! Kuna viongozi wanaopata uongozi ikiwa chanzo cha kunyanyasa watu.

Kwa mfano, kuna mwekezaji mfugaji aliyeko Bubale Mishenye Kyaka; mwananchi wa pale amezaliwa pale pale wanaleta mwekezaji wanaambiwa muhame bila kuonyesha pa kuanzia! Mtu mwenyewe amezaliwa pale pale! Unategemea aende wapi pamoja na uzee ule? Mheshimiwa Rais alivyokwenda pale alitoa uamuzi, lakini mpaka sasa hivi bado huo uamuzi haujatekelezwa. Ni kwa nini waendelee kupata shida na ni watanzania? Nitaomba kujua utaratibu huo. Naomba nipatiwe majibu mazuri ya michango yangu. Asante.

**MHE. BALOZI ABDI HASSAN MSHANGAMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mawaziri, Naibu Waziri, Makatibu Wakuu na Wataalam wote wa Wizara kwa hotuba nzuri sana. Naunga mkono hoja.

Natoa maoni na ushauri na pia nitaomba ufafanuzi na mwongozo wa Wizara katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya 19: Uamuzi wa wapi zijengwe Ofisi za Wabunge, lini, michoro ipi, utafanywa na nani?

Mheshimiwa Naibu Spika, bado kuna tatizo sugu la vikao hivyo muhimu kupangwa na kufanyika bila ushiriki wa Wabunge kwa sababu waandaaji wa vikao hivyo hawazingatii ratiba za vikao vya Bunge. Kila Wabunge wa Mkoa wana mwenyekiti wao. Ni vyema basi Wakuu wa Mkoa watakiswe kushauriana na Wenyeviti wa Wabunge wa Mikoa husika wanapoitisha vikao vya Bodi ya Barabara, *RCC* na kadhalika, kuhakikisha ushiriki wa Wabunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, je, Serikali haioni ubora na umuhimu wa kugawa fedha za Uwezeshaji za J.K. kiwilaya kwa uwiano wa idadi ya watu– *prorata to population* badala ya mfumo wa sasa wa bilioni kila Mkoa?

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya 31, ni lini vikundi vya wazalishaji, wafanyabiashara na wasindikaji wa mboga na matunda vitaanzishwa Lushoto?

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya 41: Barabara ya Mlalo – Ngwelo – Mlola – Makanya – Milingano – Korogwe ina umuhimu mkubwa kwa vile barabara hiyo ni barabara ya mpakani na hivyo ni barabara ya ulinzi katika mpaka wetu na Kenya. Pia barabara hii ni kiungo muhimu kati ya Tarafa za Umba, Mlola, Mgwashi na Bandari ya Tanga. Ni vyema isimamiwe Kimkoa na *Tanroads*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya 47: Wakazi wa Kata za Malibwi, Ngwelo, Mlola na Makanya, wamenituma nipate uthibitisho wa Serikali ni lini mtandao wa umeme utawafikia kutoka vituo vya Mlalo na Kwemakame. Vile vile umemenuru?

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya 51: Kuhusu mfuko wa mawasiliano Vijijini, Kata za Mlola, Malibwi na Makanya zina watu wengi na taasisi nyingi lakini hakuna Mitandao ya simu. Naiomba Serikali izihimize kampuni za *TIGO, CELTEL* na *VODA* waharakishe kujenga minara katika maeneo hayo yenye wateja wengi sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya 66: Umwagiliaji: Tarafa ya Mlola Wilaya ya Lushoto ina miti mingi na mabonde mazuri sana ya kilimo cha umwagiliaji, kama vile Mshangai, Mbwei, Mdando, Masashai, Kweulasi na kadhalika kinachohitajika ni mabwawa, miundombinu, mafunzo kwa wakulima, na uwezeshaji. Naomba Tarafa hii ijumuishwe katika huo mpango kabambe wa Taifa wa umwagiliaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya 72: Madini: ziko taarifa za kuwepo aina nyingi na akiba kubwa za madini Wilayani Lushoto. Naomba Serikali itufafanulie aina hizo za madini na kuwashauri wananchi wa maeneo husika namna bora ya kuvuna madini hayo kwa vikundi vya wachimbaji wadogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya 89: Maji Vijijini. Upatikanaji wa maji mengi safi na salama kwa wakazi wote wa Wilaya ya Lushoto ni kero namba moja. Vyanzo vipo, ni vingi havikauki. Tunaomba Serikali itusaidie wataalam na kugharamia uhakika wa vyanzo vyote kuandaa michoro ya miundombinu stahiki na makadirio ya gharama shrikishi za utekelezaji kufikisha maji Vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya 91: Zahanati kila Kijiji ifikapo 2010: Tamko hili zuri la Serikali linahitaji ufafanuzi wa kina hasa kuhusu michoro, watumishi, vifaa na mgawanyo wa majukumu ya utekelezaji na gharama kati ya Kijiji, Halmashauri na Wizara ya Afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya 102: Maslahi ya Waheshimiwa Madiwani na Wenyeviti wa Vijiji: Naipongeza Serikali kuafiki kilio cha Wabunge kwamba mafao ya Waheshimiwa Madiwani yaboreshwe. Tunahimiza Serikali ikubali kuwapa posho Wenyeviti wa Serikali za vijini 2008/2009.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, tunatoa Hongera sana PM naunga mkono hoja.

**MHE. DR. SAMSON F. MPANDA:** Awali ya yoto Naunga Mkono Hoja mia kwa mia. Yafuatayo yangetiliwa mkazo katika Bajeti hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wa Kilwa Kaskazini ambao wanaishi mbali na Kilwa Masoko ambako kuna Benki ya (NMB) kwa kweli wana wakati mgumu sana hasa wakati wa masika inawalazimu watembee km 80 kwa miguu au baiskeli. Tunaomba Serikali iwaangalie wananchi hawa kwa jicho la huruma, angalau wangepata japo tawi moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, Hivi tunasema maji ni uhai, - maana yake ni nini? Wakati wakala wa uchimbaji na Mabwawa (DDCA) ambayo ni wa kizalengo tunawaacha wa kidola tu maana yake nini, sasa tunategemea nini hata hii miradi ya World Bank ya Quick wing tumechimba visima bila kuweka pamp hao wananchi watawezaje kupata hayo maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ningependa kujua barabara ya Ndundu – Somanga (60 km) ambayo ingekuwa chachu ya maendeleo kwa wananchi wa mikoa ya kusini. Mbona inacheleweshwa na wananchi wanazidi kuumia kiuchumi kutokana na kipande hicho cha barabara. Daraja la Kigamboni vipi?

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho naipongeza Serikali kwa kusimamia uuzaji wa korosho katika mikoa ya Lindi na Mtwara kwa kuuza katika Vyama vya Ushirika. Hata

hivyo wananchi wanategemea na zao la ufuta lifanyike hivyo hivyo ili mapata ya mkoa yapande na uweze kuendelea kama Ilani ya Chama cha Mapinduzi CCM isemavyo:

Mheshimiwa Naibu Spika, hii tabia ya walanguzi kununua mazao yakiwa bado mashambani tena kwa bei ya chini tunaomba Serikali iwachukulie lhatua watu hao ikiwezekana wapelekwe kwenye Vyama vya Ushirika.

Mheshimiwa Naibu Spika, maunga Hoja mia kwa mia.

**MHE. MWANTUMU S.B. MAHIZA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza hotuba nzuri ambayo kwa hakika imeonesha mafanikio makubwa .

Naomba kuchangia yafuatayo:-

(1) Naomba sana askari wa jiji la Dar es Salaam wasitumike kupokonya mali za wafanyabiashara wadogowadogo na kuzichukua wao na kuzigawana kitendo chao hicho ni **dhuluma** hata kama wafanyabiashara hao wamekosa kwanini wasiruhusiwe kuzikomba biashara zao? Aidha, askari hao watumie zaidi kulinda amani na kuhakikisha biashara hazifanyiki holela.

(2) Kinamama/wafagiaji wa barabara katika Jiji la DSM ndicho chanzo cha kuziba kwa mifereji kwani wanapofagia hsukumia michanga ndani ya mifereji na hivyo kusabisha kuziba, ushahidi mkubwa upo hawana usismamizi na hivyo hufanya wapendavyo.

(3) Nakerwa sana na utaratibu wa kuweka vibanda vya biashara katika maeneo ya shule ndani ya jiji la DSM- maduka na biashara zinazofanywa huko si salama na kubwa ziko taarifa za uhakika wa kiusalama kwamba baadhi ya vibanda huusa dawa za kulevya, bangi na kuberi. Je kuna ulazima gani wa biashara hizo kufanyika katika maeneo hayo? Aidha, matendo ya kudhalilisha wanafunzi wadogo hufanyika katika maeneo hayo, nashauri agizo lilitoka Ofisi ya Rais Utawala Bora litekelezwe haraka iwezekanavyo.

(4) Walimu wengi kubaki katika orodha ndefu ya kungojea hali yakuwa maeneo mengine haya walimu katika Manisaa ya Jiji la DSM. Nashauri Maafisa Elimu na Wakurugenzi wa Manispaa hizo za Ilala, Temeke na Kinondoni wawapangie kazi walimu kwa uwiano mzuri badala ya kuwalundika katikati ya jiji tu.

(5) Vyombo vya usafiri kwa Wakuu wa Idara katika Wilaya mpya. Karibu Wilaya nyingi mpya kama vile Mkinga, Bahi, Nanyumbu n.k. hazina kabisa vyombo vya usafiri kwa Wakuu wa Idara - naomba katika vipaumbele nao wafikiriwe.

(6) Kivuko na Gati kwa maeneo ya Delta – Rufiji na Mkuranga. Naomba sana Serikali tuone huruma kwa wananchi wa maeneo hayo ni hatari sana kwa maisha ya wananchi na ndio maana hata walimu na watumishi wengine hawako tayari kwenda kufanya

kazi huko. Hivi ni lini tutaona umuhimu wa kuwapatia kivuko – Boti wananchi wa maeneo hayo?

(7) Wakandarasi wasio na uwezo wa kufanya kazi za barabara za Vijijini wanalipwa fedha kwa kuweka vifusi vya tope kwa fedha nyingi sana na mara mvua zikianza barabara hazipitiki mifani ni Kilindi – Handeni – Korogwe na Chanika – MKata. Anomba umakini uwepo katika zabuni hizo.

(8) Handeni ni Wilaya yenye kupata mateso makubwa ya maji naomba ukamkini uwepo na pia wananchi wapatiwe utaalam wakuvuna maji ya mvua kama inavyofanyika katika Halmashauri zingine.

Naunga mkono hoja.

**MHE. HAJI JUMA SEREWEJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kuniruhusu kuchangia kwa maandishi hotuba ya Bajeti ya Waziri Mkuu.

Kabla sijaanza kuchangia naomba kwanza naunga mkono asilimia mia moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli naipongeza hotuba hii kwa jinsi iliyo nzuri na ambayo imeelezea kwa uwazi kabisa yale yote ambayo yatafanikiwa kwenye mikoa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nitazungumzia kuhusu fedha ambazo za miradi kwa wananchi wenye biashara ndogo ndogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mfuko huu unaojulikana kwa jila la Fedha za Mheshimiwa Kikwete, kwa upande wa Zanzibar bado kabisa wananchi hawajfaidika nao hata kidogo kwa sababu nathubutu kusema fedha hizi hazijatoka kwa hata mmoja, sijui fedha hizi zitaanza kupelekwa lini kwa wananchi hao.

Mheshimiwa Naibu Spika, nafsi yangu napongeza kwa dhati kabisa Serikali kusikia kilio cha Waheshimiwa Wabunge kuhusu Madiwani kupatiwa posho katika Bajeti hii ya 2008/09. kwa sababu Madiwani ni kiungo kikubwa sana wa kufanikisha na kufuatilia kazi kwenye Majimbo na Kata. Nategemea na Zanzibar wafuate nyayo hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na magari kuendeshwa ubabe na kusababisha msongamano wakati mwngine si wa lazima. Mheshimiwa Waziri Mkuu ameataka askari wa usalama barabarani wasimamie kikamilifu sheria hii. Ushauri wangu mimi naomba Serikali iwapatie vitendea kazi askari wa usalama barabarani kama vile pikipiki ili askari hao waweze kufanya doria kwenye barabara hizo. Kwani utakuta askari wanakaa sehemu za keepleft tu na sehemu nyingine za barabara hazina doria yoyote. Kwa hivyo madereva huwa hawan wasiwasi wa kufanya huo ubabe wao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu elimu naipongeza Serikali kwa kuipa kibaumbele elimu.

Mwisho kabisa nazidi kuunga mkono hotuba hii asilimia mia kwa mia.

**MHE. MGENI JADI KADIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuweza kunipa nguvu kuweza kuchangia hoja hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumpongeza Waziri Mkuu kwa hotuba yake nzuri na yenye kuwapa faraja watanzania, iwapo yatatekelezwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kilimo ndio uti wa mgongo wa Tanzania lakini kilimo cha jembe la mkono tayari kimepitwa na wakati lazima tubadilike.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunahitaji sasa ifunguliwe benki ya wakulima ili waweze kupata mikopo waweze kukopeshwa trekta wapate madawa, mbolea wapate wataalam ili wapate kufahamu ukulima wa kisasa wapate mazao ya kutosha na wapata kuhifadhi fedha zao kwa kujiwekea akiba.

Mheshimiwa Naibu Spika, Elimu ni ufunguo wa maisha kila binadamu anahitaji elimu na kweli Serikali inafaa kupongezwa kwa kuliona hilo kutoa kipaumbele kwenye bajeti na mengineyo kwa kweli shule zimejengwa nyingi sana Msingi, na sekondari lakini lakusikitisha shule hizo hazina vikalio, na hazina walimu wa kutosha hasa walimu wa somo la Sayansi kwa hiyo ni tatizo, na vile vile shule za Vijijini kuna upungufu wa nyumba za walimu, waalimu wengi wanabakia mijini kwa tatizo hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile wale walimu wapya wanaoajiriwa wapate mishahara yao mapema wasicheleweshwe au wakapata usumbufu wakiwa wako Wilaya hii wakambiwa mshahara wako uko Wilaya nyingine mpaka inafika miezi 6 hajapata maslahi yake na maslahi yao walimu waongezwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, haki za binadamu kwa kweli nimeguswa na sala la mtoto yatima Mbeya hivi karibuni mtoto huyo baada ya kufiwa na wazazi wake alichukuliwa na jamaa zake wa karibu lakini la kusikitisha mtoto aliuza kwa mfanyabiashara wa hoteli kwa Sh. Milioni 5 ili akachunwe ngozi ati kwa kupata utajiri kwa njia ya ushirikina, kwa bahati wasamaria wema wakapeleka taarifa Polisi na mtuhumiwa akatiwa mbaroni

Mheshimwa nataka kujua mtoto huyu baada ya kupata mtihani huo alifishwa kwa jamaa zao au Serikali imemuhifadhi kwa kumpa malezi ya matumaini ili aishi kama watoto wengine au yuko wapi?

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya mchango wangu namtakia Waziri Mkuu afya njema na maisha marefu na amkinge kwa kila shari isimfike. Mungu Ibariki Tanzania.

**MHE. ERNEST GAKEYA MABINA:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutoa pongezi kubwa kwa uteuzi wa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuweze kutuchagulia kiongozi mahiri naye si mwingine bali ni Waziri Mkuu aliyeweza kuwaslisha bajeti yake mbele ya Bunge hili kwa umakini mkubwa ambayo inaungwa mkono na pande zote mbili zilizoko ndani ya ukumbi huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nalazimika kuwapa pia hongera kwa Waziri wa TAMISEMI Mheshimiwa Celina Kombani (Mb) pamoja na Naibu Waziri Mhe. Aggrey Mwanri (Mb) bila kuwasahau Katibu Mkuu, Wakurugenzi na Wafanyakazi wote wa TAMISEMI kwa kazi kubwa wanayoifanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa nishukuru kwa maelezo mazuri haya yanaweza yakasaidia sehemu zingine lakini Wilaya ya Geita ina matatizo mengi ningeomba haya yafuatayo yafanyiwe kazi.:-

(1) Mji wa Geita hauna maji salama kwa matumizi ya binadamu pamoja na mifugo, hivyo tunaomba Serikali iangalie katika kutatua tatizo hili kubwa la maji katika mji huu.

(2) Kutokana na jiografia ilivyokuwa Wilaya ya Geita imekaa vibaya sana hiyo tuliomba kwamba igawanywe ili iwe na Wilaya mbili pia kuwe na utaratibu wa kuongeza Majimbo hii inatokana na kuongezeka kwa idadi kubwa ya watu.

(3) Uandikishaji wa Vijiji na Kata Geita ipewe Kipaumbele ili kuweza kurahizisha kuleta utawala bora kwa uongozi wa Vijiji na Kata ambazo ni kubwa mno.

(4) Hali ya usalama ni ndogo mno, kumekuwa na matukio ya kuvamiwa walimu kiasi ambacho kunasababisha walimu wengi kuhama kwenye shule na kudidimiza elimu Wilayani Geita.Tunaomba:-

- Polisi Geita wapewe vitendea kazi kama magari kama matano (5) pikipiki (20) ishirini na hata baiskeli.
- Uhamisho ufanyike kwa askari waliokaa muda mrefu kwa kuwa kumekuwa na mahusiano makubwa kati Askari na Majambazi.
- Tuongezewe maaskari wengi kulingana na idadi ya watu.

(1) Kuwe na utaratibu wa kuwanyang’anya wachimbaji wakubwa ambao wamepata Secial Mining Licence na wamepewa tena *Properting Mining Licence* basi maeneo yote yaliyonayo ya *Prospecting Minding licence* wapewe wachimbaji wadogo wadogo.

(2) Serikali ifanye mazungumzo na Serikali ya Kenya na Uganda kuweza kulinda Ziwa Victoria ambako sasa limevamiwa na Wawekezaji wakubwa ambao wananunua samaki usiku na mchana. Serikali hizi zifanye utaratibu wa kuwa na vyombo

maalumu au misimu ya uvuvi kuliko kuacha uvuvi holela ambao unafanyika hivi sasa.

**MHE. JUMA SAID OMAR:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia uzima na afya na hivyo kuweza kushiriki katika kikao cha leo.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kukupongeza wewe, Naibu Spika, Wenyeviti wa Bunge pamoja na viongozi wa kambi ya upinzani kwa kutuongoza vizuri katika mambo mbalimbali kuhusiana na shughuli zetu za Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, usafiri wa majini umekuwa ukisababisha vifo vya wananchi wengi kila mwaka katika maeneo mbalimbali kutokana na kukosekana kwa vyombo vya uokoaji. Je, Serikali haioni wakati umefika sasa kuwa na speed boat katika bandari zetu kuu na angalau helkopta moja vikiwa vimekaa standby ili ikitokea ajali ya chombo kuzama viweze kuokoa maisha ya wananchi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwafaka baina ya CCM na *CUF* unahitaji kupatiwa ufumbuzi wa kudumu katika muda huu tulionao ili usije ukaleta maafa makubwa iwapo utaachwa hivi hivi bila ya kupatiwa ufumbuzi. Ni matarajio yetu kwamba hatua za dharura zitachukuliwa ili kuinusuru Zanzibar isijeikaingia katika balaa litakalohitaji gharama kubwa hasa ikizingatiwa na ahadi nyingine iliyotolewa na Mheshimiwa Rais Jakaya Kikwete aliyoitoa hivi karibuni alipohojiwa huko Uingereza.

Mheshimiwa Naibu Spika, Muungano wetu ni wa muda mrefu, lakini kuna kero mbalimbali ambazo hadi sasa bado hazijapatiwa ufumbuzi. Je, Serikali haioni kwamba kuna haja ya kuchukua hatua za muda mfupi kumaliza kero hizo badala ya utaratibu wa hivi sasa ambao utachukua muda mrefu kumaliza kero hizo huku zikiendelea kuathiri pande mbili za Muungano.

Mheshimwa Spika, tume za uchaguzi za Zanzibar na Muungano zinahitaji kufanyiwa marekebisho ili zisionekane kukandamiza haki za wananchi kushiri katika chaguzi zilizo huru na za haki. Hii ni kutokana na matatizo mbalimbali yanayojitokeza wakati wa uandikishaji katika daftari la kudumu la wapiga kura pamoja na uchaguzi wenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi yetu imeingia katika Mageuzi ya Kisiasa, Kiuchumi na Kijamii. Pia hivi sasa ni wakati wa ukweli na uwazi, (Truth and Transparency). Hivyo wakati umefika sasa kuwa na katiba mpya inayoendana na wakati yenye kubadilika (flexible constatiction) badala ya kuendelea na katiba ya hivi sasa ya 1977 ambayo haibadiliki (rigid constitution) ili matatizo mbalimbali ya kikatiba na mengineyo yanayoikabili nchi yetu yaweze kuondoka.

**MHE. PAULO P. KIMITI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ya yote naomba nitumie nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Mizengo Peter Pinda kuteuliwa na Mheshimiwa Jakara M. Kikwete (Rais wetu) kuwa Waziri Mkuu. Pia nampongeza kwa

jinsi alivyowasilisha hoja yake kwa ufasaha na umakini wa hali ya juu. Nawapongeza Wasaidizi wake wote Wakuu na Watumishi kwa kuiandaa vizuri hotuba hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeona niyaweke haya yafuatayo kwa maandishi kwa kuwa mengine katika utawala bora huwezi kuyasema hadharani. Namwomba Mheshimiwa Waziri Mkuu ayazingatie haya yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Manispaa ya Sumbawanga kwa bahati mbaya ilianza na Watendaji wenye uwezo, uzoefu na hata taaluma hafifu kulingana na majukumu ya Manispaa yenyewe.

Tukianza na Mkurugenzi Mwenyewe, alikuja moja kwa moja toka Wilayani ambako alikuwa akifanya kazi kama Afisa Ushirika. Hakuwahi kuwa hata Mkurugenzi wa ngazi nyingine yoyote ya Wilaya. Sijui vigezo gani vilitumika kumteua.

Mheshimiwa Naibu Spika, tangu afike, Manispaa imekumbwa katika tatizo la kukosa fedha za ruzuku ya Maendeoeo kwa kukosa hati safi mfululizo kwa zaidi ya miaka mitatu. Hasara hii ilitokana na ubovu wa usimamizi wa Wakuu wake husika.

Pili Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kipindi chote amekuwa akipambana na wakuu wake wa Idara pamoja na Madiwani ambao kwa viako vingi vya Kanseli, kumekuwa na maandalizi hafifu ya vikao hibyo na kufanya view vinarudishwa na kuahirishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ujumla katika mazingira kama hayo, hata Mkuu wa Mkoa Rukwa analielewa suala hili. Hivi karibuni nilipata nafasi ya kuzungumza naye mwenyewe (Mkurugenzi wa manispaa) na kweli mwenyewe amekiri kuwa hali ya mazingira ya kufanya kazi katika Manispaa hii (siyo conducive at all), hali hii inaonyesha kuwa naye amesalimu amri - na siyo vizuri kuendelea naye katika hali hii- mambo yanaweze kuwa mabaya. Naomba Waziri Mkuu usaidie kurekebisha hali hii.

Pamoja na hilo, Mkurugenzi huyu kwa sasa yuko masomoni – Mzumbe University - jambo ambalo ungozi unaona kuwa fedha ndogo zinazoletwa kwa maendeleo, zinatumaika pia kwa ngarama nyingine za masomo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo jingine ambalo ninamwomba Mheshimiwa Waziri Mkuu ni kuchukua hatua madhubuti kuanzia sasa wakati bei ya mafuta imepanda:-

(i) Awatake Wakurugenzi wasisafiri bila kibali cha Wakuu wa Mikoa

(ii) Misafara ya kutembele miradi wakati wa viongozi wakuu wanapotembelea mikoa iratibiwe na misururu isiwe mirefu sana. waende wanaohusikatu na wapakieane kwenye magari machache. Wakati wa kuendesha, magari mengi kwa jambo la kawaida uachwe mara moja.

(iii) Waheshimiwa Wabunge wawekwe kwenye orodha ya Wakuu wa Wilaya na Wakurgenzi – pamoja ili kujenga umoja kwenye uongozi wa Wilaya, wakati wa ziara za viongozi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa mwaka huu kuna dalili za upungufu wa chakula na kwa kuwa Mkoa wa Rukwa karibu unaaza kuvuna mahindi, nashauri

(i) Tani 19,00 za mahindi zilizomo kwenya maghala ya SGR Sumbawanga yaanze kusafirishwa kwenda sehemu zenye upungufu ili kutoa nafasi kwa mahindi ya mwaka huu kununuliwa.

(ii) Ununuzi wa mahindi uanze Sumbawanga ili kabla ya mvua kunyesha iwe kazi hiyo imekamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho namwomba Mheshimiwa Waziri Mkuu afuatilie kwa karibu sana juu ya fedha za *MCC* ili masharti waliyoyatoa yasikwamishe kazi ya ujenzi wa barabara mwaka huu wa fedha, angalau tuone tenda zimetangazwa kwa sehemu ndogo ndogo za km 60/60/60/60 – ili barabara kwa kufikia 2010 tujivunie hatua kubwa ya kujip;atia sifa za utekelezaji ILANI ya uchaguzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii kwa asilimia zote.

**MHE. MWAJUMA HASAN KHAMIS:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni vema nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia kuwa hai na ni mzima.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nampongeza Waziri Mkuu kwa hotuba yake ilio na sura ya MAISHA BORA KWA KILA MTANZANIA. Baada ya maelezo yangu hayo, sasa naomba nitoe mchango katika hotuba hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mahakama ya Kadhi katika nchi yetu

Kwa kuwa muda mrefu sana, waislamu hapa nchini wanadai kuwepo Mahakama hiyo. Mtazamo wa wengi wamegundua Serikali suala hili walipiga danadana, jambo ambalo linatoa sura mbaya kwa waislamu hapa nchini. Ni vema Serikali ielewe kwamba kuna baadhi ya haki za keski hukumu yake ni lazima ihukumiwe kidini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano ndoa na mirathi. Makosa haya yanapotokea hukumu yake ni lazima yapatikane katika vitabu vya kidini. Je, ni lini Serikali itaamua kuanzisha mahakama hiyo iloi waislamu wapate haki zao?

Mheshimiwa Naibu Spika, Watanzania haki yao ya kuishi imo ndani ya nchi yao, mara nyingi tunaona kuvamiwa wananchi hao na Serikali kubomolewa nyumba zao. Katika hili nani mkosa. Serikali ama wananchi. Mwananchi ameanza mpaka amemaliza Serikali ilikuwepo wapi hata eneo likajengwa lote na kuwa Kijiji.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kuhusu Madawa ya Kulevya, kwakuwa nguvu kazi ndio waathirika wakubwa katika nchi yetu, ni vema Serikali iandae mpango mahususi kuzuia Madawa haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo yangu hayo nasema ahsante.

**MHE. JOYCE N. MACHIMU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa nafasi hii ili na mimi niweze kuchangia hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuzungumzia kuhusu kilimo. Naomba kuzungumzia mambo mawili makuu katika Mkoa wangu wa Shinyanga.

(1) Kuwainua wakulima wa pamba kulingana na soko la dunia kuhusu bei ya pamba. Iwapo katika soko la dunia bei iko juu, kwa nini Serikali iwe na kigugumizi kuwapa wananchi bei kubwa ili wapunguze kuvimba misuri na kuendelea kuzeeka bila mafanikio! Tunaomba Serikali ikae upya na Bodi ya Pamba ili iongeze bei ya pamba, kwani Mkoa huu ndio zao pekee wananchi wanalolitegemea.

(2) Mheshimiwa Naibu Spika, tunaomba utaratibu uliotumika kuwainua wananchi wa Kusini (Korosho), itumike pia kwa wakulima wa pamba hasa Shinyanga ambako tayari kuna SACCOS zimeundwa na zimekubali kutumia utaratibu huo lakini tatizo lililopo ni vyombo vya fedha (benki) kutowapatia mikopo ya ununuzi wa pamba ya wananchi hawa kwa sababu zisizoeleweka. Taasisi hizi zilizokubali kutumia utaratibu wa stakabadhi ya mazao, zimenyimwa fedha na wananchi hawa nao hawajauza pamba yao, Je, Serikali inatoa kauli gani kwa benki ya *CRDB* kutoa mkopo kwa taasisi hiyo ili utaratibu huu uimarike hatimaye watu wote wasiibiwe na wafanyabiashara wasio waaminifu? Taasisi hizi ninazozizungumzia ziko Wilayani Bukombe (Kampuni ya SIBUKA).

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Serikali ichunguze vyema vyombo vyetu vya fedha visilalie kwa wafanyabiashara tu, waone uchungu wa wananchi wetu. Tafadhali sana, utaratibu wa stakabathi ya mazao, umeonekana ni mzuri hata mwaka jana Wilayani Bukombe ulitumika. Chondechonde, *CRDB* itoe fedha haraka ili kuepuka *"risk"* ya kukaa na pamba ndani kwani ni hatari, ahsante.

**MHE. MARTHA M. MLATA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya wananchi wa Mkoa wa Singida, napenda kutoa pongezi zangu za dhati, kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa hotuba yake nzuri, inayoleta matumaini mapya kwa wananchi wa Tanzania.

Pamoja na pongezi hizo, pia naomba nichukue nafsi hii, kwa niaba ya wananchi wa Singida, kupitia Bunge lako Tukufu, kutoa shukrani zetu za dhati, kwa Mkuu wetu wa Mkoa, kwa uchapakazi wake na mapenzi makubwa aliyonayo kwa Mkoa wa Singida na hatimaye matunda ya uchapakazi wake yameonekana.

Aidha, tunaishukuru Serikali kwa jitihada zake katika kukamilisha ujenzi wa barabara itokayo Dodoma - Shelui.

Pamoja na shukrani hizo, wananchi wa Mkoa wa Singida, wanaoomba Serikali kuweka nguvu zake zote ili kuweza kukamilisha kipande cha barabara kutoka Chikuyu - Isuna, kwani kusuasua kwa ukamilikaji wa barabara hiyo, kumewanyima wananchi wa Mkoa wa Singida haki ya msingi katika kuchangia maendeleo ya Mkoa huu. Aidha wamejisikia kama vile Serikali imewatenga kwa kutowajali kwa adha wanazopata katika barabara hii hasa kipandi cha masika.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine, ni Uwanja wa Ndege wa Singida Mjini. Kwa juhudi za Mkuu wa Mkoa, kwa kushirikiana na wananchi, wameshajitahidi kuanza ujenzi wa kiwanja hiki. Hivyo, ombi letu Mkoa wa Singida kwa Serikali ni kwamba, Serikali itoe fedha ili kuweka lami katika kiwanja hiki kwani ndio kichocheo cha maendeleo ya Mkoa wa Singida hasa pale Mkoa unapotafuta wawekezaji kwani wengi wao huuliza kama ndege zinatua Singida. Tunaomba Serikali iungane nasi katika kusukuma gurudumu la maendeleo na kumpatia Mtanzania maisha bora.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ninalopenda kulizungumzia ni suala la "utumishi wa umma".

Mheshimiwa Naibu Spika, bajeti ya mwaka 2008/2009, iliwasilishwa Bungeni, pia hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ya makadirio ya matumizi ya fedha, ni dhahiri imekuwa ya kumkomboa mwananchi kwa kiwango kizuri, lakini yote hiyo inategemea uadilifu wa watumishi wa umma na uzalendo wao. Pia kuwa makini katika kusimamia na kuhakikisha kila fedha iliyotengwa inafanya kazi iliyopangwa bila uzembe wowote ili kuhakikisha hazirudi Hazina au kupotea. Swali langu kwa Serikali ni je, imeweka mkakati gani kuhakikisha fedha zilizotengwa zinatumika kama zilivyopangwa na bila kuzirudisha Hazina?

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Waandishi wa Habari. Hapa nchini kipo chuo kimoja kinachotoa Degree ya kwanza tu, Waandishi wanapotaka kujiendeleza zaidi inabidi waende nje ya nchi kupata *Degree* ya pili au zaidi. Jambo hili limekuwa ni kikwazo kikubwa sana kwa Waandishi wetu kuendelea zaidi kutokana na gharama kubwa. Je, Serikali haioni kwamba kuna ulazima wa kutenga fungu na kuweka mikakati ya kuwasomesha Waandishi wetu nje ya nchi walio na sifa za kusoma *Degree* ya Pili au zaidi, angalau kuanzia watano kila mwaka? Je, Serikali pia haioni kuwa ni vema kutenga fungu la fedha ili kuwawezesha Waandishi wa Habari kuweza kufika maeneo ya Vijijini ili kuweza kuibua matatizo au maendeleo katika maeneo mbalimbali?

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala la afya, je, Serikali inachukua hatua gani za makusudi na za haraka, ili kupunguza vifo vya wanawake vitokanavyo na ujauzito au uzazi baada ya kujifungua na kabla ya kujifungua?

Mheshimiwa Naibu Spika, mikakati ya Kitaifa inaonyesha kuwa vifo vya wanawake vitokanavyo na ujauzito au uzazi kabla na baada ya kujifungua vinaweza

kupungua kama tukiwa na wahudumu wenye uzoefu na ujuzi. Wahudumu hao, ni lazima wawe na mafunzo yakiwemo ya ukunga, mazingira mazuri ya kufanyia kazi, vifaa na madawa pia usafiri (miundombinu). Je, Serikali inasema nini juu ya uwiano huo ukilinganisha na takwimu za wanawake wajawazito na vituo vya Afya? Kwa maana nyingine mahitaji halisi kufanikisha mikakati hii. Naomba maelezo ya kina kwa nini bado kuna wanawake wanaokufa kwa kukosa huduma bora au usafiri muafaka?

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri, fedha nyingi zinazotengwa kwa ajili ya vituo au kwa ajili ya mkakati wa kupunguza vifo hivi, pesa hizi huwa hazitumiki ipasavyo na hatimaye kurudishwa Hazina eti kwa kisingizio cha kwamba vituo vingine vilikosa wahudumu kwa sababu ya miundombinu au maeneo duni.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wangu ni kwamba, fedha hizo zisirudishwe, ni vema zikatumika kutatulia tatizo mojawapo katika zahanati hiyo au kituo hicho. Aidha kwa kuboresha mazingira ili kuwavutia wahudumu a kununua hata gari aina ya *Pickup,* itumike kama *ambulance* ili kuokoa maisha ya mama na watoto hata jamii nzima.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumzie suala la Watendaji wa Kata na Vijiji. Kumekuwa na tabia ya Watendaji wa Kata yaani *VEO* na *WEO,* kuwanyanyasa wananchi kwa kutumia vibaya vyeo vyao, hasa katika suala la michango mbalimbali. Mheshimiwa Waziri Mkuu amekuwa akikemea Watendaji hao wasiwatese na kuwaweka watu rumande kwa ajili ya michango hasa katika kipindi cha masika ambapo ndio muhula wa kazi wa mwananchi huyo lakini kuna maeneo bado watu wanateswa. Je, Serikali inatambua kwamba kuna watu bado wanateswa na hatimaye kubambikizwa kesi na kufungwa jela kutokana na kukamatwa kwa kosa la kutokulipa michango hiyo? Je, Serikali inatambua kwamba kuna watu wamekuwa wakimbizi ndani ya nchi yao kwa kuzikimbia familia zao na kuzitelekeza kwa kuogopa kufikishwa Mahakamani? Je, Serikali inajua kama kuna wanawake wajawazito ambao wamekuwa wakikamatwa na kuwekwa rumande hadi uchungu kuwajia wangali washtakiwa? Mambo haya yote ni Kata ya Ndago/Iramba.

Mheshimiwa Naibu Spika, Je, Serikali inachukua hatua gani kwa Watendaji hao? Je, Serikali ina mikakati gani kuhakikisha mambo haya hayatokei tena? Je, Serikali ina mkakati gani wa kutafuta mbinu nyingine ya kuwabana wanaokwepa kulipa michango au ni kutokana na hali ngumu ya maisha waliyonayo?

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuitangaza nchi yetu katika ngazi ya Kimataifa, ni vema kuanza na ubora na unadhifu wa Balozi zetu (Ofisi) kwani kuna ofisi nyingi za Balozi zetu majengo hayako katika hali nzuri na ya kuweza kuijengea heshima nchi yetu na kuwa ni chanzo cha kuwavutia hata wawekezaji hata watalii kuja Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama vile Ubalozi wa Paris ni kama kijiwe tu, kwani wanapanga kwenye jengo la Uganda, hii imeishushia nchi yetu heshima. Serikali itenge fungu la kuboresha Ofisi za Balozi zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna jengo la Tanzania ambalo lilianguka London, Uingereza na sasa ni kiwanja tu kimekaa, hakijafanyiwa kazi yoyote. Katika dodoso zangu kwamba kwa nini wasitumie kiwanja hicho kujenga jengo zuri kubwa ambalo itakuwa ni kitega uchumi kizuri kwa nchi yetu, nikaambiwa wanasubiri kibali toka Serikali ya Tanzania ili wapatiwe mkopo kwenye Benki za UK ambapo walishakubaliwa, je, hilo jibu la kibali linatoka nini?

Mheshimiwa Naibu Spika, leo naomba kuishia hapa na wenzangu watazumgumzia mengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja, ahsante.

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutumia nafasi hii, kwa njia ya maandishi, kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mheshimiwa Mizengo Pinda, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera na Uratibu, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI Mheshimiwa Celina Kombani, Naibu Waziri, Mheshimiwa Aggrey Mwanri, Makatibu Wakuu na Watendaji wote walioshiriki kuandaa bajeti hii yenye mikakati madhubuti ya kuendeleza Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya pongezi hizi kwa Serikali, nitakuwa mchoyo wa fadhila kwa Mkuu wa Mkoa wetu, Mheshimiwa Parseko Kone, Mtendaji Mkuu, Ndugu Husein Katanga na Watendaji wote, kwa juhudi kubwa na mshikamano wao kwa kuiendeleza Singida yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema hivi nikiwa na mifano hai kupitia ujenzi wa shule za sekondari kwani hadi 2005 tulikuwa na shule za Serikali 18 na za binafsi 12 jumla shule 30, lakini hadi sasa zipo shule za sekondari mpya 90 na kufanya jumla ya shule 120. Kweli tuna kila sababu ya kumpongeza Mkuu wa Mkoa wetu. Vilevile mara nyingi mambo ya kimaendeleo amekuwa akitushirikisha sisi Wabunge wa Mkoa huo pamoja na Madiwani wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya pongezi hizi, sasa nianze kuchangia bajeti hii kama ifuatavyo:-

A: REDIO TBC NA TVT - Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuikumbusha Serikali maombi ya wananchi wa Mkoa wa Singida juu ya kuletewa Redio *TBC* pamoja na TVT kwani sasa ni muda mrefu sana toka tumeanza kuahidiwa. Tumekuwa tukitembelewa na Mawaziri wa Habari na Michezo toka mwaka 2003. Alikuja Mheshimiwa Ramadhani Mapuri, kisha alitutembelea Mheshimiwa Seif Khatibu na juzi alikuja Mheshimiwa Mkuchika, wote hawa wamekuwa wakiahidi kutuletea Redio *TBC* na *TVT*. Namwomba Mheshimiwa Waziri Mkuu, wakati wa majumuisho, atueleze ili wananchi wa Singida wapate matumaini. Tunapenda nasi tuwe tunasikiliza hotuba na kuona televisheni ya Taifa wakati Rais anapohutubia kila mwisho wa mwezi.

B: WATU KULIWA NA SIMBA - Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli usiofichika kuwa hili ni tatizo kubwa linaloikera jamii yetu juu ya Simba kula watu hasa Singida Kusini na Manyoni Magharibi. Pamoja na juhudi kubwa za Mkoa na Wilaya za kuwasaka samba hao bado tumegonga mwamba. Naiomba Serikali kuingilia kati tatizo hili hata kuleta helkopta ipite angani kuwasaka hawa samba, tutakuwa tumenusuru sana wananchi hawa hasa vijana ambao ndio wanaliwa zaidi.
C. ADHA YA AKINAMAMA WANAPOJIFUNGUA - Mheshimiwa Naibu Spika, kuna tatizo la wanawake wasio na uwezo wanapopata ujauzito wakati wa kujifungua wakiwa hawana vifaa vya kuwapa Wauguzi mfano *gloves*, Wauguzi hukataa kuwazalisha. Naiomba Serikali ikemee hali hii kupitia bajeti hii pamoja na kupeleka taarifa ya maandishi kwa kila Halmashauri.

D: KUINUA KILIMO - Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza sana Serikali kwa jinsi inavyojitahidi kuinua uchumi wa nchi kupitia kilimo cha mazao ya chakula na biashara. Vilevile, napongeza uongozi wa Mkoa wa Singida kwa jinsi ulivyojitahidi kuhimiza kilimo Mkoa wa Singida hatimaye mwaka huu Singida tumevuna zaidi ya asilimia mia. Hata hivyo, tungeweze kuvuna zaidi kama kila Kata ingekuwa na Maafisa Kilimo. Ninaiomba Serikali kwa kuwa sasa inasomesha Maafisa Kilimo basi mara watakapohitimu, Singida tuwepe kipaumbele. Wakati tunasubiri Maafisa hawa, Serikali ianze kuandaa vitendea kazi hasa usafiri wa pikipiki, ofisi na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuieleza Serikali kuwa, Maafisa Tarafa wanafanya kazi kubwa sana huko Vijijini za Idara zote kwa sababu Idara nyingi hazina Watendaji wa Kata mfano Maafisa Kilimo, Maafisa Mifugo, Maafisa Maendeleo ya Jamii na kadhalika, kwa kweli wanafanyakazi kama trekta. Naiomba Serikali sasa iwasaidie hawa Maafisa Tarafa wapate pikipiki kwani walizonazo ni za miaka mingi sana tokea miaka ya tisini na zimechakaa sana. Vile vile wapewe mafuta ya kuendeshea pikipiki zao kwani wanazitumia kwa kuombaomba tu, mara kwa *DC* au *DED,* jambo ambalo ni kikwazo cha utendaji kazi wao.

E. MIRADI YA MAENDELEO KWENYE HALMSHAURI ZETU - Mheshimiwa Naibu Spika, ni ukweli usiojificha kuwa utekelezaji wa miradi hii sio mzuri mfano ujenzi wa shule za msingi. Zipo shule ambazo zilipata pesa lakini shule hazikujengwa au zimejengwa kwa kiwango cha chini sana *(value for money)*. Naomba kila Halmashauri iwe na Mkaguzi wa Ndani kusimamia fedha hizo ili ziweze kufanya kazi iliyotarajiwa na Serikali. Vile vile, Wakaguzi hawa wasiwe chini ya Wakurugenzi kwani watashindwa kufichua ubadhirifu wa fedha hizi.

F: MADAWA YA KULEVYA - Mheshimiwa Naibu Spika, ni ukweli usiojificha kuwa wapo vijana wetu ambao wanajihusisha na uuzaji wa madawa ya kulevya na hatimaye kutumia wenyewe. Wengi wao wameathirika vibaya sana kufikia hatua wazazi wao kushindwa kuwalea na kuwa kero kubwa kwa familia.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Serikali iendelee kupambana na wale wanaoendeleza biashara hii haramu. Pia Serikali ijenge vituo ambavyo vitatumika kwa

kuwalea na kuwafundisha vijana hawa ambao ni kero sana katika familia na jamii kwa ujumla. Sasa hivi, wanapelekwa Hospitali ya Mirembe wakati wao sio vichaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza sana Serikali kwa kusikia kilio cha Waheshimiwa Wabunge, juu ya kuongeza maslahi ya Madiwani. Nina matumaini itasaidia kuwapa ari Madiwani ya kusimamia matumizi ya Halmashauri pamoja na miradi mbalimbali. Kwani umaskini unaweza ukamshawishi kiongozi kupokea rushwa kwa Watendaji au Wakandarasi wanaopata tenda kwenye Halmashauri.

G: MWISHO - Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nimalizie kwa kuunga mkono hoja hii kwa asilimia mia kwa mia.

**MHE. MAGARET S. SITTA:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchangia kama ifuatavyo:-

(1) Hali ya usafiri wa Reli ya Kati, inahitaji hatua za haraka kwani ndiyo njia inayotumiwa na wananchi wengi wenye uwezo mdogo.

(2) Barabara ya Manyoni – Tabora, iimarishwe ili kupunguza msongamano wa wanaotegemea reli ambayo kwa sasa ina matatizo mengi.

**MHE. JAMES P. MASALIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, yapo Makampuni ambayo yamekuwa yakifanya shughuli mbalimbali katika Wilaya zetu (Halmashauri za Wilaya).

Chini ya Sheria ya *Local Government Finance Act No. 9* ya mwaka 1982, ushuru ni mojawapo ya mapato ya Halmashauri unaotajwa katika Kifungu 7(i)(a) ya Sheria hii;

Chini ya Sheria hii, Sehemu ya 7, Halmashauri ya Wilaya ya Geita imetunga Sheria Ndogo ya *"Service Levy"* ya mwaka 2004; na ilichapwa kwenye gazeti la Serikali No. 423 la tarehe 15/10/2004;

Chini ya Sheria hii, Makampuni yanayofanya shughuli zake katika eneo la Halmashauri yetu zinapaswa kulipa *"Service Levy'* ya asilimia 0.3 ya *"annual turnover",*

Yapo Makampuni yanayofanya shughuli zake Wilayani Geita wakiwa pia na ofisi zao Jijini Mwanza kama – *Kaserkandis Construction Company (KASCO),* ambayo inafanya kazi za *"Earth Works"* mbalimbali katika mgodi wa *GGM*, Geita na Kampuni ya *HYSPEC (AFRICA) TANZANIA LIMITED,* Kampuni ambayo hufanya shughuli za *drilling* katika mgodi huo wa *GGM* wa Geita pamoja na Makampuni mengine.

Kwa bahati mbaya na kwa tafsiri potofu ya Sheria hii, Halmashauri ya Jiji la Mwanza imedai kulipwa *"Service Levy"* katika Jiji la Mwanza badala ya Geita wanakofanyia kazi. Kwa mshangao wa Wabunge wa Geita, hata Afisa wako mmoja, anayeitwa K.M. Luanda, kwa niaba ya Katibu Mkuu, TAMISEMI, katika barua yake ya

Juni 28, 2008 kwa Kampuni ya *Stanley Drilling Services (T) Ltd*. wanaofanya kazi zao katika Halmashauri ya Geita, Mgodini GGM, inaelekea kutotoa tafsiri sahihi ya Sheria hii. Sisi Wabunge wa Geita, kwa Sheria yetu Ndogo hapo juu, tunaomba utoe maelekezo ili Makampuni hayo yalipe *"Service Levy"* hiyo katika Halmashauri ya Wilaya ya Geita.

**MHE. MARIA I. HEWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, pongezi kwa hotuba ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa Mizengo Peter Pinda, (Mb), kuhusu mapitio na mwelekeo wa kazi za Serikali na makadirio ya matumizi ya fedha ya Ofisi yake. Pia pongezi kwa Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa na Ofisi ya Bunge ya mwaka 2008/2009, kwa kazi nzuri wanazozifanya pamoja na wataalamu wao.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kutupa matumaini makubwa na kupewa Manispaa mbili za Ilemela na Nyamagana, katika muundo wa Halmashauri ya Jiji la MWANZA. Kuhusu ugawaji wa ardhi, pamoja na maelekezo mazuri ya Ofisi ya Waziri Mkuu, naomba kutoa ushauri kama ifuatavyo:-

(1) Katika bajeti zijazo, ofisi izidi kufikiria kuongeza pesa za kutosha upande wa elimu kwa wafugaji ya jinsi gani wanaweza kupunguza Idadi ya mifugo yao walau 5% ya idadi ya mifugo yao kila mwaka ili ardhi iweze kuwatosha kwa sababu ardhi haiongezeki.

(2) Katika bajeti zijazo kuwe na orodha kwa Halmashauri zote zitakazoshindwa kutimiza zoezi la kutenga maeneo ya wafugaji na wakulima wakubwa kama agizo lilivyoelekeza. Orodha hiyo iletwe Bungeni kwa maamuzi zaidi kwa Halmashauri zenye kukiuka agizo la Ofisi ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu elimu ya msingi, Elimu ya Msingi Tanzania, ni nzuri na ninawapongeza. Napendekeza yafuatayo:-

(1) Kuwepo na makusudi mazima ya Wizara /Halmashauri kuwaunga mkono wazazi katika suala zima la madawati. Ni aibu sana kuwaona watoto katika karne hii eti bado wanakaa chini darasani. Kukifanyika *operation* maalum kikidhi haja hii, inawezekana ili watoto wakae juu ya madawati.

(2) Elimu ya masomo ya sayansi yatiliwe mkazo toka shule za msingi. Walimu wenye taaluma hiyo, watawanywe kila shule ya msingi.

**MHE. FLORENCE E. KYENDESYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa hotuba nzuri ambayo imegusa maeneo yote muhimu na hasa yanayoshughulikiwa na Manispaa, Majiji na Halmashauri nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na mwonekano wa hotuba hiyo, sasa napenda kusema kuwa naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia kwa mia.

Hata hivyo, napenda kutoa mchango wangu katika maeneo yafuatayo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Uwanja wa ndege wa Songwe Mbeyanapenda kuelezea jinsi gani ujenzi huu wa Ndege Songwe unayokwenda taratibu wakati kazi kubwa imeshafanyika kwa kutumia fedha nyingi za Serikali. Naomba msukumo mkubwa wa kukamilisha ujenzi huo uwekwe na hasa ikizingatiwa kuwa awamu ya kwanza na ya pili ilikwishakamilika kama ilivyopangwa.Ili kukamilisha awamu ya tatu, Mhandisi Mshauri alipatikana tarehe 15/6/2006 na mkopo wa Dola za Kimarekani millioni 11.6 zilipatikana Oktoba 2006, kwa hali hiyo, kazi ilipangwa kuanza Novemba 2007 ili mradi ukamilike baada ya miezi 19 lakini mpaka sasa hakuna kinachofanyika. Je, Serikali imepata hasara kiasi gani tangu mradi usimame kwani hadi sasa wapo walinzi, maji na umeme vinatumika.

(b)Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Kuboresha huduma kwa wavuvi katika Ziwa Nyasa – Huko Kyela. Uvuvi unaofanywa katika Ziwa Nyasa, ni wa kutumia njia za kizamani. Naiomba Serikali iwasaidie wavuvi wanaojipatia kipato chao kwa njia hiyo ili kuboresha uvuvi wa kisasa kwa maana ya kutumia vyombo vya kisasa.

(c) Mbali na hali hiyo, pia naiomba Serikali kuweka kivuko cha kuaminika kutoka Kyela hadi Manda Ziwani kwa sababu ni njia ya mkato kwa Wilaya hizo zinazolizunguka ziwa Nyasa.

(d) Kupanda kwa bei ya mafuta, kumesababisha chakula na nauli kupanda kiholela. Naomba Serikali ilisimamie suala hili na kuwabana wamiliki wa vyombo vya usafiri ili wafuate na kuheshimu Sheria za Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawasilisha, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

**MHE. ELIETTA N. SWITI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na hotuba iliyotolewa na Waziri Mkuu, napenda kuchangia kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kilimo kama uti wa mgogo wa Taifa letu, kinapaswa kuongezewa fedha na pembejeo ili tupate chakula cha kutosha na pia zisambazwe mbegu bora kwa madhumuni hayo hayo. Mikakati ya Serikali katika Kilimo, iongezewe nguvu. Wakati tukilima chakula cha kutosha kwa nchi yetu; iko kila sababu ya kulima mazao yatakayozalisha *bio-diesel.* Tusishawishike kuacha kilimo hicho maana tunaona wazi hata nchi zenye akiba kubwa ya mafuta kama Marekani wanatumia mahindi kutengeneza *bio-diesel.*

Mheshimiwa Naibu Spika, kitu ambacho sikubaliani nacho, ni kuwamilikisha wageni ardhi yetu ili walime jatropha na kadhalika bali waingie ubia na wananchi au Serikali kulima mazao hayo, au walete mitambo ya kukamulia. Kutengwa kwa shilingi bilioni 3.5 kwa ajili ya mikopo kwa wakulima, ni hatua inayofaa sana. Hivyo, nashauri Serikali iendelee kuhamasisha kilimo cha mbegu za *bio-diezel,* kama jatropha na mengine kama hayo ili kuiwezesha nchi yetu kuwa na dizeli na mafuta mbadala ya taa.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la chakula liende sambamba na kilimo cha mbegu za mafuta kwa manufaa ya Tanzania nzima. Licha ya agizo la Serikali, wapo Wabunge ambao hawaelewi jatropha na faida zake, lakini wako wale walioelewa na kutoa hamasa nyingi katika Mikoa yao ikiwemo Mbeya, Kagera, Rukwa na Arusha, kwa miaka miwili iliyopita walipoagizwa Bungeni. Mkoa wa Rukwa kwa mfano, tayari kiwanda kinajengwa Mpanda. Hii ni hatua nzuri kwa Rukwa ambayo haina zao la kudumu la biashara lenye tija kwani tumbaku hailimwi Mkoa mzima na kule inakolimwa imesababisha uharibifu wa misitu tena haina tija kwa wakulima. Naamini jatropha itaiondoa Rukwa katika dimbwi la umaskini wa kipato, kwa kuacha kutegemea mvua/ukame wa Mwenyezi Mungu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue fursa hii, kuihakikishia Serikali kuwa wana-Rukwa, ni wakulima waadilifu wa chakula cha Watanzania; wenye kutumia plau kwa kilimo. Hivyo, wakilima jatropha kama zao la biashara, itawawezesha kutunzia mashamba ya chakula, kulipa ada za shule na viingilio vya *SACCOS,* tiba na mambo mengine "watajikomboa na dimbwi la umaskini". Wana – Rukwa, wangependa kufurahia kilimo cha kudumu kama ambavyo Kusini watu wanafurahia Korosho, Kagera, Mbono na Vanilla lakini pia Mbeya Kahawa na Arusha Mbono. Wachaga walifurahia Kahawa japo waliing'oa na kulima nyanya, kwa hiari yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, hekta 11,352 za umwagiliaji na mradi wa kusaidia wakulima unaofanywa na Serikali ya Tanzania kwa kushirikiana na *FAO* na Serikali ya Japan, usiishie Ziwa Victoria bali ufike pia katika Mikoa inayozalisha chakula ambayo ina mabonde yanayofaa kwa umwagiliaji mfano bonde la Ziwa Rukwa, bonde la Ulumi, Jimbo la Kalambo na mabonde ya Wilaya ya Mpanda, Mkoani Rukwa. Miundo mbinu, niseme tu kuwa Serikali inatupenda sana wananchi wake ila tu wezo mdogo. Pamoja na uwezo huo mdogo, naiomba Serikali ielekeze macho yake katika yafuatayo:-

(1) Kutengeneza barabara ya Kaengesa – Mwimbi – Zambia kwa lami maana barabara hiyo inaunganisha Tanzania na Zambia. Kuachwa kwa barabara hiyo kubaki ya vumbi (moramu), ni aibu kwa nchi yetu. Naikumbusha Serikali kwamba kama imedhamiria kuunganisha nchi yetu na nchi jirani kwa barabara ya lami, ishughulikie barabara hii.

(2) Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Reli ya Kati, naomba reli hii ikarabatiwe ili itowe huduma zitakazotujengea heshima. Mabehewa yana kunguni, panya, mende na mashuka hayafuliwi baada ya mteja kuyatumia (mfano toka Dar es Salaam - Kigoma) mashuka hayo hupewa mteja mwingine bila kufuliwa au toka Kigoma hadi Tabora au Dar.

Mheshimiwa Naibu Spika, *Baffet Car,* huishia Tabora na kufika Mwanza, Kigoma na Mpanda waishie kula mihogo na vitumbua njiani.

Mheshimiwa Naibu Spika, zaidi ya hapo, mabehewa hayatoshi, watu hujaa sana na kusababisha watu kupanda kwenye *engine* na wakati mwingine kusababisha vifo.

Mheshimiwa Naibu Spika, wafanyakazi wa *baffet car* na wa reli, wote wanadai madeni ya mishahara yao miezi 3 - 5. Mshahara wa wafanyakazi wa *baffet,* ni Sh. 60,000/= kwa mwezi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. MWADINI A. JECHA:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, naomba nichukue nafasi hii, kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa kuweza kuwasilisha hotuba yake ndefu iliyosheheni mambo mengi.

Aidha, nichukue nafasi hii kuchangia suala zima la kuanzishwa Mahakama ya Kadhi Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, imekuwa ni jambo la kushangaza kwamba hadi hii leo suala la kuanzishwa kwa Mahakama hii, imechukua sura ya malumbano ndani ya jamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la kuanzishwa kwa Mahakama ya Kadhi, sio tu limetajwa katika Ilani ya Uchaguzi wa CCM, lakini Mahakama hii ni dai la muda mrefu sana la Waislamu wa Tanzania Bara kuwa na chombo chao ambacho kitasimamia ndoa za Kiislamu, mirathi katika misingi ya Kiislamu na talaka kwa wanandoa wa Kiislamu.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati wa Awamu ya Tano ya Uongozi wa Zanzibar, aliyekuwa Rais wa Zanzibar, Mheshimiwa Dr. Salmin Amour, alichukua uamuzi wa Zanzibar kujiunga na *(OIC) Organization of Islamic Community.* Madhumuni makubwa ya Zanzibar kujiunga na *OIC*, ilikuwa ni kufungua milango ya kiuchumi lakini kwa bahati mbaya Serikali ya Jamhuri ya Muungano iliiamrisha Serikali ya Zanzibar kujitoa *OIC*. Serikali ya Zanzibar ililazimika kutii amri ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano, Zanzibar ikajitoa *OIC*. Lakini Serikali ya Jamhuri ilitamka wazi kwamba ikiwa Zanzibar inaona kuna umuhimu wa kujiunga na *OIC* basi Jamhuri ya Muungano ndio ambayo itajiunga na Jumuiya hiyo.

La kusikitisha na kustaajabisha ni kuwa hadi hii leo, suala hili halijazungumzwa tena ilhali bado Serikali ya Zanzibar inaona upo umuhimu wa kujiunga na *OIC* ili kupanua wigo wake wa kupata misaada ya kiuchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue nafasi hii, kuiomba Serikali ama ijiunge na *OIC* kwa niaba ya Zanzibar au Zanzibar iruhusiwe kujiunga tena na *OIC* moja kwa moja vinginevyo tupewe maelezo yanayoingia akilini.

**MHE. ALI KHAMIS SEIF:** Mheshimiwa Naibu Spika, miongoni wa Majimbo yanayotarajiwa kupata ofisi ya Mbunge, ni Jimbo langu la Mkoani. Ushirikishwaji juu ya zoezi hilo, ni mdogo sana. Badala ya kushirikishwa, hutoa fedha Sh.180,000/= ikiwa ni gharama ya upimaji wa kiwanja, sielewi hatua yoyote iliyofikiwa. Nadhani licha kuwa niko kwenye Upinzani lakini napaswa kuelewa hali inavyoendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hali hii, ninatamka rasmi, udhaifu wowote utakaotokezea, ieleweke wazi mimi sitohusika.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuzindua Bunge, mnamo tarehe 30/12/2005, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, alisema anasononeshwa sana na mpasuko uliopo baina ya Unguja na Pemba, mazungumzo baina ya vyama viwili yalifanyika kwa muda mwa miezi 14 kwa vikao 21.

Mheshimiwa Naibu Spika, matokeo ya mazungumzo hayo, *CCM* wakaja na msimamo wa kura za maoni. Hii inaonyesha wenzetu wanajifanya kama kwamba hawaelewi chanzo cha mgogoro huo kuwa ni uchaguzi. Sasa haiwezekani mgogoro wa uchaguzi, utatuliwe kwa uchaguzi (kura za maoni). Nasema tusiendelee kuichezea amani tuliyonayo kwani ikikutoka ni taabu kuipata.

Mheshimiwa Naibu Spika, inavyoonekana, nchi hii haina wala rushwa wakubwa kwa kuchukua kesi zilizoko Mahakamani. Wanaokula rushwa ni Askari wa barabarani, Mahakimu wa Mahakama ya Mwanzo, mahakamani hakuna kesi za rushwa kubwa kubwa. Watu wa chini wakishutumiwa, huwa wanapandishwa Mahakamani lakini wakubwa bado utaambiwa uchunguzi unaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, hatuwatendei haki Watanzania kuhusu hili suala na ipo haja ieleweke kwamba madaraka tuliyonayo, ni mtihani, pasipo na haki, uwezekano wa kuvunjika amani ni mkubwa mno. Ipo haja Serikali kuchukua hatua muafaka kuhusu suala hilo kwa sababu haiaminiki kuwa wakubwa hawali rushwa.

**MHE. DR. ZAINAB A. GAMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitoe mchango wangu wa nyongeza katika bajeti ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi Dr. Zainab A. Gama, Mkurugenzi wa Mji wa Kibaha, Kamanda wa Kikosi cha Nyumbu, tulikwenda kumwona Waziri wa TAMISEMI ambaye sasa ndiye Waziri Mkuu, kumwomba atusaidie kupata pesa za kutengeneza barabara ya Kwamathias – Nyumbu - Msongoni km. 12.6 yenye thamani ya Tsh. 573.500 za ujenzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri Mkuu ambaye wakati huo alikuwa Waziri wa TAMISEMI, aliona umuhimu wa barabara hii na kusema haiwezekani gharama kubwa kama hiyo kupata pesa kutoka kwenye michango ya wananchi, akaahidi kumwomba Waziri Mkuu aliyekuweko wakati huo, ili aweke kipaumbele na atafute pesa za kujenga barabara hii. Kwa bahati nzuri, hivi sasa Mheshimiwa Pinda amekuwa Waziri Mkuu, hana haja ya kwenda kumwomba Waziri Mkuu, Waziri Mkuu ni yeye mwenyewe. Je, pesa hiyo inaweza kupatikana? Katika bajeti hii ya 2008/2009, haikuwekwa, je, atakuwa na mkakati mwingine wa kupata hizo pesa?

Mheshimiwa Naibu Spika, Halmashauri ya Mji wa Kibaha, tuliomba maombi maalum ili kutengeneza barabara hii kwa kiwango cha changarawe. Pia tuliomba fedha TSh.617,000,000/= kwa ajili ya uendelezaji wa Kituo cha Afya Mkoani ili kiweze kufikia Hospitali ya Wilaya kama alivyoahidi Rais Jakaya Mrisho Kikwete.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hayo, ninaomba nipate maelezo juu ya eneo kubwa linalozunguka Kiwanda cha *TAMCO,* limebakia pori linalofuga majambazi, je, Serikali ina mkakati gani kuliondoa hili pori linalohatarisha maisha ya watu na hasa wanawake.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutoa shukrani kwa Serikali kutupatia pesa za kuendeleza Hospitali ya Tumbi. Pia nimearifiwa kuwa Serikali imetenga shilingi milioni 300 ili kujenga/kutengeneza kidogo kidogo barabara ya Mkoani.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka huu, nilikuwa na dhamira ya kushika shilingi katika Wizara ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa na sababu kubwa iliyotaka kunifikisha hapo, ni tabia ya Wizara kuchukulia mambo yanayoikabili Wilaya ya Kibaha kimzaha mzaha na kumfanya Rais aonekane si mkweli, kwa kutoa hadi asizozitimiza. Masuala hayo ni:-

(1) Serikali kushindwa kuufanya mji wa Kibaha kuwa na hadhi ya Makao Makuu ya Mkoa wa Pwani;

(2) Kuwaachia watu binafsi kugawa viwanja zaidi ya themanini bila Halmashauri kuwachukulia hatua na Wizara ikiambiwa haifanyi chochote;

(3) Kuwaachia *Town Planner* na Maafisa Ardhi, wakiendelea na hujuma ya kutokupanga mji wa Kibaha na kugawa maeneo kiholela jambo lililosababishi mji huu kuendelea kujengeka kiholela;

(4) Wizara kutochukuwa hatua za dharura za kuingilia kati mgogoro wa fidia wa wananchi wa mtaa wa Sofu; na

(5) Kutosimamia utekelezaji wa ahadi za Rais ambazo ni:-

(a) Kuufanya mji wa Kibaha usiwe maficho ya Mkoa wa Dar es Salaam. Pia ameahidi kuleta viwanda. Hivi sasa hakuna eneo la viwanda lililotengwa, majibu ya swali langu kuwa Zegereni ni eneo lililotengwa kuwa eneo la viwanda, lilikuwa sio jibu sahihi. Nilipomuuliza Mkurugenzi ni lini tulitenga Zegereni (ambalo ni shamba la *Holm*) kuwa eneo la viwanda na yeye alionekana kushangaa. Hivi sasa tunakubaliana na jibu la Bunge lionekane kuwa sahihi ili kuficha ulaghai uliofanywa na *Town Planner*, Maafisa Ardhi na *RAS*.

(b) Pia Rais aliahidi kuwa barabara za mji wa Kibaha zitajengwa mpaka sasa Halmashauri haijaandaa hata michoro ya barabara. Mitaa mingi inayoonekana, ni ile iliyoanzishwa na njia za miguu zilizoanza Kiholela. Je, huyo Rais atajenga au kutengeneza barabara zilizoanzishwa kiholela? Ombi langu kwako Mheshimiwa Waziri Mkuu ni yale yote uliyotamka katika hotuba yako ya bajeti kuhusu masuala ya ardhi, uhakikishe TAMISEMI na Halmashauri ya Kibaha Mjini wanayatekeleza. Maafisa wote

watakaoshindwa kutekeleza, naomba waadhibiwe kwa aidha, kuhamishwa, kuteremshwa cheo au kufukuzwa kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, *Ref. Pg*. 36, kif.36. Pg.37, kif.54, kuanzia mstari wa nne kutoka chini. *Pg.* 38, kif. 55 – 56, Tume ya Mipango majukumu yake na ikiwezekana Tume iwe na ofisi katika ngazi za Mikoa na Wilaya. Naomba wadau mbalimbali washirikishwe katika upangaji wa matumizi ya ardhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Pg. 39, kif. 58, kuanzia mstari wa sita kutoka chini, sentensi inayoelekeza Halmashauri zitenge fedha za kutosha kwa ajili ya utayarishaji wa mipango ya matumizi bora ya Ardhi. Swali, hivi sasa tayari Halmashauri zimeshapanga bajeti zao. Je, hizo pesa kuwa ajili ya utayarishaji ya Mipango Miji watapata wapi?

Mheshimiwa Naibu Spika, *Pg*. 40, kif. 58, Tume ya Mipango ya Matumizi Bora ya Ardhi itaimarishwa, yote haya uliyaeleza katika hotuba yako hii ya bajeti 2008/2009, yakitekelezwa, mimi na wewe ugomvi hatuna. Haiwezekani Makao Makuu ya Mkoa kuwa na sura ya Kijiji.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kushukuru kwa kutenga pesa kwa ajili ya kupanua Hospitali ya Tumbi. Ombi langu, mwagize Waziri wa Afya, azungumze na Hospitali ya Muhimbili na Moi, wawe wanaleta wanafunzi wao katika Hospitali ya Tumbi. Kitendo hiki kikifanikiwa, kitawahamasisha na kuwapa ari wafanyakazi wa Hospitali ya Tumbi wawe *Modernized* katika shughuli zao. Hii ni sababu Muhimbili ni *Consultant Hospital, Training Centre* na *Research Centre*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu *SACCOS,* nashukuru uhamasishaji wa *SACCOS* umefanya wananchi wengi kujiunga. Ombi langu kwa Halmashauri ya Mji wa Kibaha, ukiacha *SACCOS* zilizoanza zamani, *SACCOS* nyingi zilizoanzishwa baada ya tamko la bilioni moja, zimekufa au zimesimama, haziendelei. Hii ni kwa sababu Wana–*SACCOS* wengi walifikiri zitapata mkopo huu, zilipokosa hivi sasa zimesinzia. Kwa kuwa Afisa Ushirika wangu siyo *aggressive,* kuzisukuma/kuzihamasisha ziendelee, naomba msaada na ushauri wa Wizara.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi sasa nina lawama kubwa kwa wana *SACCOS*. Hamasa niliyoitoa kwa wananchi kuanzisha *SACCOS*, ni kubwa. Nimesimamia mpaka hata kusajili *SACCOS* zao pale walipopata matatizo ya kusajili, mimi sio mtaalamu wa kuendeleza *SACCOS* hizo. Naomba Wizara wanisaidie watu wangu wana moyo lakini *aggressiveness* ya Afisa Ushirika, haipo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu maji, kutatua tatizo la maji, ni moja ya ahadi ya Chama cha Mapinduzi katika Ilani. Wananchi wa Kibaha Mjini wanashangazwa, hawapati maji japokuwa bomba linalopeleka maji Dar linapita kwenye maeneo yao. Tumeambiwa *consultant* aliteuliwa DAWASA, alikuja kufanyia *survey* mji wa Kibaha na Mlandizi katika mradi unaofadhiliwa na *World Bank*. Lakini mtaalamu hajawahi hata kupita ofisi ya Halmashauri ya mji kujitambulisha au kushirikiana na *Engineer* wa Maji, Ofisi ya Halmashauri ya Mji haikuwa na taarifa, ila mimi Mbunge nilipokwenda DAWASA ili nifahamu mikakati ya DAWASA kutekeleza Ilani katika Jimbo langu,

nikaambiwana hivyo na *Engineer* wa Maji, DAWASA, Mr. Kassiga. Je, huu mpango ni wa kweli au ni maneno tu?

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu *TASAF*, naomba niwashukuru *TASAF*. Tumepata mgao wa *TASAF* na umetusaidia kujenga shule tano za 2nd za Kata. Pia tumepata mradi wa mbuzi wa maziwa kwa wanaoishi na virusi vya UKIMWI.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu umeme, Mji wa Kibaha ni Makao Makuu ya Mkoa wa Pwani pia ni mji ulioko karibu na Jiji la Dar es Salaam. Utashangaa nikikuarifu kuwa, maeneo mengi ya Mji wa Kibaha hayana umeme na cha kusikitisha zaidi hata baadhi ya mitaa iliyoko barabara kuu ya Morogoro, hayana umeme. Tunaomba *TANESCO*, watusaidie kupata umeme. Jibu tuliopata *TANESCO* haina pesa kama kuna mitaa au mtu binafsi anataka kupata umeme agharamie kwa 100%. Mbona baadhi ya Halmashauri zimetengewa bajeti? Je, sisi Kibaha tunamkosi gari?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, Pg.33, Kif. 47, Serikali imeendelea na mipango ya kusambaza umeme kwa wananchi, maeneo kama Ludewa, Mbinga, Kilolo, Mto wa Mbu, Bahi, Uyui, Mkinga, Simanjiro, Kilindi na kadhalika. Je, imekuwaje Halmashauri ya Mji wa Kibaha, tuambiwe tujilipie wenyewe? Sehemu kubwa ya Kibaha imepata umeme wakati Mbunge wake alipokuwa Waziri wa Wizara husika. Je, hii ina maana kwamba kama siyo Waziri, hupati huduma?

Mheshimiwa Naibu Spika, bajeti shirikishi, kwa taratibu tunazoambiwa na Serikali, maandalizi ya bajeti ni lazima yawe shirikishi kuanzia ngazi ya Vijiji, mitaa, Vitongoji, hata na Wizara. Je, imekuwaje Halmashauri ya Mji wa Kibaha, hakuna ushirikishwaji wa maandalizi ya bajeti kama tunavyoelekezwa na Serikali?

Mheshimiwa Naibu Spika, Februari 2008, nilikuwa nafanya ziara ya kukutana na viongozi wa Serikali za Mitaa katika kila Kata na wajumbe wa Halmashauri ya CCM, Kata. Nia ya ziara hii ni kukumbusha usimamizi na utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi wa CCM katika uchaguzi wa 2005. Katika ziara hii, nimegundua kuwa, mwezi huo wa Februari, Maafisa wa Halmashauri ya Mji wa Kibaha walikuwa katika maandalizi ya bajeti. Maandalizi haya yameanza baada ya Mkurugenzi na Mwenyekiti wa Halmashauri kutoka Dodoma walikoitwa kwa ajili ya suala la bajeti.

Mheshimiwa Naibu Spika, kilichonishangaza, Kata zangu saba kati ya nane na mitaa, zilikuwa hazijapeleka mapendekezo yao Wilayani, hii ni pamoja na Kata ya Mwenyekiti wa Halmashauri. Nilipouliza Halmashauri je, bajeti wanayoitengeneza, wameshirikisha wananchi? Walijibu ndiyo lakini kwa kuthibitisha jibu hilo si sahihi, Mwenyekiti wa Halmashauri alitamkiwa na Viongozi wa Kata yake kuwa hatujapeleka na yeye alikuja kukiri hata *WDC* haijaketi kujadili mapendekezo ya Bajeti katika Kata yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, matatizo ya kutoshirikishwa viongozi wa chini nilifikiri yako katika Jimbo langu tu lakini nilipata bahati kwenda Serengeti, Kata ya

Machochwe. Kata ambayo Mwenyekiti wa Halmashauri ya Serengeti anatoka walikiri mbele ya Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti pia alikubaliana nao bado hawajakaa kwenye *WDC* kujadili mapendekezo ya bajeti katika Kata yao. Kwa maeneo mawili tu niliyoyasema, nina wasiwasi ushiriki wa wananchi katika kuandaa bajeti, haifahamiki vizuri, naomba Wizara iwaelimishe na kama inawezekana, waarifiwe ratiba ya vikao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ushiriki wa Wabunge katika Vikao vya Halmashauri, Wabunge wengi wamelalamikia suala hili. Waziri Mkuu aliyepita alitoa maagizo, tatizo hili lisiwepo na Watendaji washirikiane na Mbunge katika kupanga ratiba ya vikao. Agizo hili bado utekelezaji wake unasuasua kwenye Halmashauri yangu, siarifiwi vikao hata kama niko Jimboni. Ni mara nyingi nimekwenda Halmashauri kwa masuala fulani fulani, ninakuta kuna kikao kinaendelea, ukiuliza kwa nini hamkuniarifu, wanatoa sababu za uongo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mbaya zaidi, hata wageni wanaotoka Taifa na Mkoani, siarifiwi. Mara nyingi ninashtushwa na wananchi, kwa kushangaa mbona hawanioni. Hata hivi karibuni, Waziri Mkuu wa Sweeden alipokuja, niliuona msafara unaelekea Dar. Nilipouliza, nikaambiwa ugeni huo unatoka Wilayani Kibaha. Nimeshawahi kumlalamikia Waziri Mkuu aliyepita lakini tabia hiyo inaendelea. Hata ratiba za Rais nimeshirikishwa kwa kulazimisha. Nikimuuliza *DC* anasema, yeye sio jukumu lake. Nikimuuliza *Town Director,* anasema jukumu ni la Mkuu wa Wilaya. Nikilalamika kwa Mkuu wa Mkoa, *DC* analalamika, ninamchongea na kumgombanisha na Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa. Waziri Mkuu naomba ushauri wako, nifanye nini ili nishirikishwe vikaoni na ziara za viongozi mbalimbali wanaokuja Jimboni kwangu?

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ni suala la 50/50, mbona katika hotuba yako hukusema chochote? Je, hii inatuonyesha picha gani? Inaonekana Serikali hamtaki kutekeleza suala hili la Ilani? Inafahamika kuwa kama tusipolishughulikia mwaka huu 2008 au mwanzoni mwa mwaka 2009, utekelezaji wake hautakuwepo. Nakuomba Mheshimiwa Waziri Mkuu, lisimamie suala hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, mgogoro wa ardhi Sofu, Wizara ya TAMISEMI na Ardhi, inadharau kuingilia kati mgogoro wa kulipwa fidia wananchi wa Sofu. Wananchi wa Sofu hawajaridhika na fidia waliyopewa, hawakushirikishwa katika mkakati wa kupima viwanja katika eneo lao. Malalamiko haya, wameyapeleka Halmashauri ya Mji wa Kibaha lakini hakuna lililofanyika. Wamepeleka Mkoa, Mkoa ikashauri waunde Kamati itakayoshirikisha wananchi. Kamati ilimalizia kazi kwa kushirikisha wananchi wakati wa upimaji wa viwanja, wakati wa kulipwa, Kamati haikushirikishwa. Wananchi walikwenda Wizara ya Ardhi, TAMISEMI, kutoa malalamiko yao, hakuna hatua iliyochukuliwa. Wananchi hawa walikwenda pia Mahakamani.

Mheshimiwa Naibu Spika, niliposikia suala hili, nikaombwa nisaidie kuingilia kati. Vikao viwili vilivyofanyika vya wananchi wa Sofu na Mkurugenzi, Madiwani na Maafisa Ardhi, vyote viliishia kwa Halmashauri kushindwa kuwapatia majibu wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilizungumza na Waziri wa TAMISEMI aliyekuwapo, akaniambia niandike barua. Nimeandika barua nakala nikampelekea Waziri wa Ardhi. Nilituma nakala kwake kwa sababu nilipoomba ushauri kwake, aliomba nimpatie nakala, kwa kuwa yeye ndiye mwenye kufanya *valuation* lakini mpaka sasa sijapata majibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa masikitiko, Mkuu wa Wilaya, anadiriki kutamka kuwa mimi ndiyo ninaowadekeza. Je, kosa langu kuwasikiliza na kutafuta suluhisho kwa njia ya kusikilizana? Je, niwaache wananchi hawa waende Mahakamani?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa taarifa, wananchi hawa wana Sheria ya Ardhi na *Hansard* ya Mheshimiwa Magufuli, akielezea Bunge kuhusu suala zima la fidia. Pia baadhi ya wananchi wa Sofu walikuwepo kwenye mkutano wa Mheshimiwa Magufuli (aliyekuwa Waziri wa Ardhi) na wananchi wa Kiluvya akiwa anatafuta suluhu ya mgogoro wa fidia.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, barabara ya *TAMCO* - Mapinga, Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba nifahamishwe kama barabara hii imepandishwa daraja kuwa barabara ya Mkoa chini ya *TANROAD.* Je, inategemewa kupangiwa pesa za matengenezo katika bajeti ya mwaka gani?

**MHE. HADIJA SALEH NGOZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa, natoa pongezi zangu za dhati, kwa Mheshimiwa Mizengo Peter Pinda, (Mb), kwa kuteuliwa kwake kuwa Waziri Mkuu. Pia nampongeza kwa hotuba yake nzuri ambayo imewapa matumaini mema Watanzania. Ninaomba tukubaliane kuwa, hotuba hii ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, ni kielelezo kizuri cha ubora wa CCM.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nijikite katika suala zima la Malaria. Ugonjwa huu unachangia sana vifo hasa kwa watoto wachanga na hata kudhoofisha nguvu ya kupambana na maradhi kwani ni ungonjwa ambao unarudia mtu mara kwa mara. Hivyo, Serikali za Mitaa, zihakikishe kwamba mipango ya maendeleo shirikishi na pia Kamati za Afya na za Mazingira katika ngazi zote mpaka Vijijini zihakikishe kila mara zinakagua mazalio ya mbu na kufanya usafi ili kuhakikisha kwamba hakuna mazali mengi. Tukifanya hivyo, ugonjwa huu wa malaria tunaweza kuudhibiti. Kamati hizo zipo kwa ajili ya kuhakikisha kwamba wanakuwa kweli na maneno ya kuwashauri na kuwasimamia wananchi katika kujitahidi kuboresha mazingira hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda kutoa ushauri kwamba jitihada zifanyike kuhakikisha kwamba vifaa vya upimaji wa Malaria vinapatikana hata Vijijini na pia hivi vipimo vifanyike bila gharama yoyote.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ishirikiane na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar ili kupata maelekezo jinsi gani wameweza kutokomeza ugonjwa wa Malaria kwa asilimia mia ili kuokoa maisha ya Watanzania wanaokufa kila siku kwa maradhi haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ni kuhusu madawa ya kulevya. Madawa ya Kulevya ni tatizo sugu. Ninapenda nitoe ushauri kwa Serikali kuwa, pamoja na kutoa elimu juu ya madhara ya dawa za kulevya, Serikali iunde au ilete Sheria itakayomdhibiti mletaji na mtumiaji wa madawa hayo ya kulevya ikiwemo bangi kuliko kuiachia Tume ya Kuratibu Udhibiti wa dawa hizo, kutoa elimu juu ya madhara yake, Tume hiyo inafanya kazi nzuri.

Pia tutakuwa tumeokoa vijana wetu ambao bado hawajajiingiza katika ulevi huo na tutakuwa tumeokoa vizazi vijavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri mwingine, Jeshi letu zuri la Kujenga Taifa tunalo, hebu tufanye *operation* maalum kwa kila kijana atakayeonekana anatumia madawa hayo ikiwemo bangi, Tanzania nzima, wachukuliwe na kupelekwa katika Jeshi hilo pia watasaidia kutoa taarifa nzuri za nani hasa mhusika mkuu wa madawa hayo. Vijana hao pia watakuwa katika udhibiti mzuri na kufanya kazi za kujitegemea na pia za kujenga Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania bila madawa ya kulevya, inawezekana. Kuna baadhi ya Mikoa ikiwemo Dodoma, vijana wetu bado hawajaathirika sana. Tusikubali kupoteza vijana wetu ambao ndiyo nguvu kazi ya Taifa kwa suala ambalo jamii ikishirikiana na Serikali, tunaweza kufanikiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ni Kuhusu UKIMWI. Katika kutimiza azma yetu hii ya kudhibiti UKIMWI na magonjwa mengine, ni lazima tumuunge mkono Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete kwa juhudi zake ambazo yeye mwenyewe amekuwa mfano mzuri kwa Watanzania kwa kujitolea kupima na familia yake *VVU* hadharani bila woga. Ameonyesha njia nzuri na mfano wa kuigwa kwa kila Mtanzania na hatimaye takwimu zimeonyesha kupungua kwa maambukizi hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia kwa mia.

**MHE. DR. ALI TARAB ALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ninamshukuru Waziri Mkuu, kwa hotuba yake nzuri.

Pili, tatizo kubwa kila mahali nchini kwetu ni ukosefu wa maji. Ukimuuliza mtu yeyote hasa Vijijini, atathibitisha kuwa jambo la kwanza *(priority)* ambayo wanahitaji, ni maji. Hivyo, kuipatia Sekta ya Maji 6% ya mgao wa bajeti, ni jambo lisiloridhisha hata kidogo na hata pale ambapo maji ya bomba yanapatikana, huwa sio maji salama, hivyo, yanaweza kuleta mlipuko wa maradhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu, nasikitika kuwa hatukuitumia vizuri taarifa ya upungufu wa chakula duniani. Tunamshukuru Mwenyenzi Mungu, katujalia nchi kubwa yenye Maziwa na Mito mingi, nashangaa kilimo tumekipa sehemu ndogo ya bajeti yetu.

*This is a loser opportunity.* Tungewekeza huko na kupata chakula cha kutosha ili kikatutosheleza sisi na tukauza cha ziada.

Mheshimiwa Naibu Spika, nne, elimu ni nuru na kigezo muhimu katika kuleta maendeleo popote pale ingawaje, tusijitahidi tu kujenga mabanda, lakini pia shule hizi zipate Walimu. Watoto wetu hawawezi kupata *quality education* ikiwa shule hizo hazina *trained Teachers*. Walimu waliofunzwa ipasavyo, ni muhimu kwa kusomesha kizazi kijacho. Mbali na Walimu, shule zipatiwe vitabu, maktaba na maabara. Hatuwezi kuwa na Wanasayansi mahiri kama shule zetu hazina Maabara. Hii ni muhimu hasa tukizingatia kuwa wanafunzi wengi siku hizi huwa hawachukui masomo ya sayansi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tano, nchi yoyote haiwezi kuendelea ikiwa hakuna amani na mshikamano. Jambo hili ni muhimu sana kwa sababu tukilea manung'uniko yoyote, hatimaye yanaweza kuleta madhara makubwa nchini. Nasema hivi kwa sababu, ni muda mrefu mgogoro wa Zanzibar uliopewa jina "Mpasuko wa Kisiasa Zanzibar" umekuwa ukifukuta. Ni vyema tukamaliza kwa haraka mpasuko huo kwa kutekeleza yale yote yaliyokubalika katika vikao vya *CUF* na CCM.

Mheshimiwa Naibu Spika, sote hatukutizamia yaliyotokea nchi jirani ya Kenya, hayo hayo ndio yanayotokea Zimbabwe hivi sasa na haya yote, ni matokeo ya kulea manung'uniko kwa kipindi kirefu. Hivyo, tufanye haraka kumaliza mgogoro huu na tumwombe Mwenyezi Mungu atuepushie mbali maafa kama yanayotokea kwa majirani wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hatimaye, tunaipongeza Serikali kwa kuboresha maslahi ya Madiwani. Ni vema katika bajeti ijayo tukawafikirie pia Wenyeviti wa Vijiji na Vitongoji, ahsante.

**MHE. DR. MZERU O. NIBUKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nianze na wachimbaji wa madini wadogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, wachimbaji hawa wanateseka sana kwa uchimbaji madini katika mazingira magumu na ya hatari. Hii yote inatokana na sera ya Madini kwamba haiwasaidii sana wachimbaji wadogo wadogo kwa sababu wachimbaji hawa, hawana nyenzo za kufanyia kazi, wanatumia mikono na masululu, majembe na vyuma duni kwa ajili ya kuvunjia mawe makubwa kitu ambacho ni kigumu sana. Nashauri Serikali iandae utaratibu wa kuweza kuwanunulia vifaa vya kuchimbia madini hayo ili na wao wajikwamue na uchumi na dhiki ya uchimbaji duni.

Mheshimiwa Naibu Spika, vyombo hivi havina gharama ya kutisha. Naomba nitoe mfano wa vyombo vichache ambayo ni:-

(i) *Escavetor*
(ii) *Compressor*

(iii) *Shaking table*
(iv) *Water pump (ext)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ni suala tu la kununua vyombo hivyo na kuwapa vijana katika vikundi ili walio wengi, wafaidike. Au njia nyingine ni kuwa, Serikali ianzishe maduka makubwa ambayo yatauza vyombo vya kuchimbia madini.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuwasaidia wachimbaji hawa, watainufaisha sana Serikali kwa kuzalisha madini mengi na ya kutosha na hivyo basi kuliongezea tija (pato kubwa) Taifa letu. Pia wapangiwe utaratibu wa jinsi ya kulipia vyombo hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini jambo lingine linalowarudisha nyuma vijana hawa, ni jinsi Serikali inavyotoa mwanya wa kuwaruhusu watu wenye uwezo mkubwa ambao huchukua maeneo makubwa mno kiasi kwamba wachimbaji wadogo hawapati sehemu za kuchimba. Kibaya zaidi, watu hao wanaochukua maeneo hayo makubwa, kwanza si watu wa maeneo hayo na pengine hawatoki katika Mkoa huo.

Lakini pia wengine si wachimbaji bali wanahodhi tu ardhi, ili baadaye wawauzie wawekezaji, hata hivyo watu hao hawachangii chochote katika maendeleo ya Vijiji husika vinavyozunguka eneo hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri, Serikali isitishe na isikubali kuruhusu jambo hili la sivyo vitaleta umwagaji wa damu kwa sababu wananchi hawatakubali wakati eneo wanaloliona halifanyiwi kazi lakini linaambiwa la mtu fulani ambaye wananchi wenyewe hawamjui kabisa. Hii ni kuwanyima fursa na haki ya kupata maendeleo. Hivyo, kwa mtu yeyote anayeomba eneo basi apewe *plot* kuanzia 1 – 20 lakini sio mtu mmoja kupewa eneo kubwa kabisa kiasi wananchi wengine wakose maeneo ya kuchimba. Hii si haki kabisa na nashauri kwamba hata wale ambao wameshapewa lazima wayarudishwe ili yagawiwe kwa wananchi wengine ili watu wote wafaidi matunda ya rasilimali hii katika nchi yao. Mimi naamini uongozi wa juu wa Wizara ya Nishati na Madini, chini ya vijana makini sana na wasikivu, watakuwa wamenielewa vizuri, nawatakia kheri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu usalama barabarani, Maaskari wa Usalama barabarani wameweka vituo vingi sana barabarani kiasi kwamba sasa imekuwa kero kubwa. Nitoe mfano mdogo tu, kutoka Morogoro mpaka Dodoma, kipo kituo pale Kihonda, Maili 11, Maili 20, Wami Dakawa, Dumila, Njia Panda ya Berega, Gairo, Kibaigwa, Njia panda ya Kiteto, Mbande, Njia panda ya Chamwino, Kisasa na Njia Panda kwenda Area D, vituo 13.

Mheshimiwa Naibu Spika, hebu angalia kama kila kituo gari litasimamishwa kwa dakika 5 tu (5 x 13 = 65) dakika hizo zinapotea kwa kusimamishwa tu na kama atasimamishwa dakika 10 kila kituo, basi maana yake atatumia dakika 130 = 2.10 masaa. Naomba sana vituo vipungue ili kupunguza adha kwa wananchi, mbona pamoja na vituo vyote hiyo lakini hakuna hata gari linaloshikwa? Inakuwa ni mradi kwa watu fulani.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumpongeza kwa dhati kabisa, Mheshimiwa Mizengo Peter Pinda, Waziri Mkuu, kwa hotuba yake nzuri sana. Hotuba iliyoandikwa vizuri, iliyojaa maelezo ya kina na takwimu muhimu na zinazoeleweka. Nampongeza tena na naunga mkono hoja yake kwa asilimia mia moja.

Aidha, nawapongeza Mawaziri wa Nchi wa Ofisi hiyo, Waheshimiwa Marmo na Kombani. Pia nampongeza Naibu Waziri, Mheshimiwa Mwanri. Wote hawa wamemsaidia Waziri Mkuu, kwa uaminifu na ufanisi na kumwezesha kuwasilisha hotuba bora zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande mwingine, nawapongeza Makatibu Wakuu, Bwana Mrisho na Bibi Tarishi, pamoja na wasaidizi wao kwa ushirikiano waliowapatia viongozi wao na kufanikisha hotuba hiyo ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hotuba ya Waziri Mkuu, imepongezwa na wananchi wa Jimbo la Bumbuli kwa ubora wake na uwazi. Naunga mkono tena kwa niaba yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na yote hayo, nakumbushia barabara mpya ya Mashewa – Bumba ya km. 5. Imetolewa maelezo na maelekezo mengi ya namna ya kuihudumia na Waziri Mkuu (alipokuwa Naibu Waziri TAMISEMI). Fedha za barabara zinatolewa kwa zilizopo tu, hii inahitaji msaada maalum. Nakuletea mchoro tena!

Mheshimiwa Naibu Spika, nazidi kuunga mkono hoja hii.

**MHE. MOHAMED ALI SAID:** Mheshimiwa Naibu Spika, naanza kuchangia kuhusu afya. Kwa vile kila mwanadamu anahitaji afya nzuri katika mwili wake kwa maisha yake yote na ili tuwe na Taifa lenye nguvu, amani na utulivu, basi ni lazima wananchi wetu wawe na afya bora.

Mheshimiwa Naibu Spika, ingawa bajeti ya afya imepewa kipaumbele, lakini bado haijapewa pesa za kutosha. Wizara hii imepewa 11.1% ya bajeti ambapo hiki ni kiasi kidogo sana. Wizara hii angalau ingepewa 16% ya bajeti yote.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na kiasi hicho kidogo cha bajeti katika Wizara hii, Wizara hii haiwezi kufanya yale mambo muhimu, kwa mfano, kuwalipa wafanyakazi (Madaktari) mishahara mizuri ambayo itaweza kuwakimu kimaisha, kununua zana za kufanyia kazi Hospitalini, kujenga majengo ya Hospitali na Zahanati, hasa Vijijini, kununua madawa, vyandarua na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naomba nichangie kuhusu Mpasuko wa Kisiasa Zanzibar. Kutokana na uwezo mkubwa alio nao Rais wetu, Mheshimiwa J. Kikwete,

Umoja wa Nchi za Afrika, umemchagua kuwa Mwenyekiti wa Umoja huo. Hii ni kutokana na busara, hekima alizonazo Rais wetu. Haya yote ameyaonyesha wakati alipokwenda kuutatua mgogoro ambao ulikuwa tayari umeshindikana ule wa Kenya lakini yeye kwa hekima zake, akautatua mara moja mgogoro huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile katika kuijali demokrasia, aliweza kuutatua mgogoro wa Kisiwa cha Nziwani huko Komoro na sasa hivi Kisiwa cha hicho ni Kisiwa cha Kidemokrasia kilicho huru.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi anashughulikia mgogoro wa Zimbabwe, ambapo tunategemea sana kwamba nao atautatua.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa tunamwomba Mheshimiwa Rais wetu, atumie uwezo wake, hekima na busara zake zote, atatue huu Mpasuko wa Kisiasa ulioko Zanzibar ambao ni mgogoro uliomo ndani ya nyumba yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunamwomba sana Rais wetu Mpendwa, auondoshe Mpasuko huu, ili Tanzania iwe na amani ya kweli.

Mungu Ibariki Tanzania
Mungu Ibariki Afrika
Mungu Ibariki Dunia. Amina!

**MHE. DR. LUCY S. NKYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mawaziri wote wa Ofisi ya Waziri Mkuu na Watendaji wao wote kwa kutayarisha hotuba nzuri sana.

Aidha, napenda kuchukua fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa kuteuliwa na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kuwa Waziri Mkuu. Mwenyezi Mungu ambariki na kuendelea kumpa hekima ya kumsaidia Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia napenda kumpongeza Mheshimiwa Celina Kombani, kwa kuteuliwa kuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI na Mheshimiwa Philip Marmo kwa kuteuliwa kuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Uratibu na Bunge.

Aidha, ninampongeza Mheshimiwa Mwanri, kwa kutekuliwa kuwa Naibu Waziri katika Wizara ya TAMISEMI. Mwenyezi Mungu awaongeze na kuwapa hekima ya kumsaidia Mheshimiwa Waziri Mkuu. Baada ya kutoa pongezi hizo, kwa nia ya kuboresha, ninapenda kutoa ushauri ufuatao:-

(i)Ninaomba Serikali iangalie uwezekano wa kuweka umeme wa mionzi ya jua katika Zahanati za Vijijini. Kukosekana kwa umeme, kunachangia sana kuongezeka kwa vifo vya akinamama na watoto. Usiku bila mwanga, siyo rahisi kumhudumia mama anayejifungua;

(ii)Kuongeza wahudumu wenye uwezo katika Zahanati zetu kwani nyingi hazifanyi kazi kutokana na ukosefu wa Watendaji. Mkoa wangu wa Morogoro, una upungufu mkubwa wa Watendaji wa Afya Vijijini;

(iii)Wilaya ya Morogoro Vijijini, haina Hospitali ya Wilaya. Ninaomba kituo cha Afya cha Dulumi, kipandishwe daraja kuwa Hospitali ya Wilaya;

(iv)Elimu, pamoja na jitihada kubwa za ujenzi wa madarasa, ninaomba Serikali iangalie namna ya kujenga Maabara angalu moja katika shule moja ya kila Tarafa hatua kwa hatua;

(v)Chanjo, ninashauri kituo cha kutengeneza chanjo cha Mabibo, kifufuliwe kwani kilikuwa kinapunguza gharama za chanjo hapa nchini. Pamoja na kutumia chanjo hizo hapa nchini, kuna uwezekano wa kuuza nje tupate hela za kigeni;

(vi)Huduma kwa waathirika wa UKIMWI ziangaliwe upya kwani kuna upungufu mkubwa sana. Pamoja na kutoa *ARV's,* wagonjwa wanaomba huduma ya lishe. Aidha ninaomba sana watoto wanaoishi na virusi vya UKIMWI, waanzishiwe Huduma Maalum *(Holistic Care),* kwani wengi ni yatima na wanatunza na wazee (bibi na babu) ambao hawana nguvu na uwezo wa kuzalisha chakula na kulipia huduma za afya.

(vii)Viwanda, napenda kuomba Serikali iviangalie Viwanda vya Morogoro. Viwanda vingine vimebinafishwa lakini wawekezaji wamebadili matumizi ya viwanda hivyo. Vitendo hivi, vimepunguza fursa ya ajira na upatikanaji wa vitendea kazi na mahitaji mengine; na

(viii) Miundombinu, ninaomba kukumbusha ahadi za Mheshimiwa Rais kuhusu ujenzi wa Madaraja ya Mto Kilombero na Ruvu, eneo la Magogoni pamoja na barabara ya Ubena – Ngerengere – Mvuha mpaka Kisaki.

Aidha ujenzi wa barabara usiwe chanzo cha uharibifu wa mazingira kama Shule ya Sekondari ya Ifakara iko kwenye hatari ya kukumbwa na mafuriko kutokana na uharibifu wa mazingira uliosababishwa na Mkandarasi wa barabara ya *TANROAD* ya Ifakara. Hivi sasa kuna mashimo ambayo yamejaa maji na kutengeneza mabwawa makubwa. Yana athari kwa sababu ni mazalia ya mbu na ni hatari kwa watoto. Ninaomba ofisi husika zikumbushwe kuingilia kati suala hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuunga mkono hoja hii kwa moyo wangu wote.

**MHE. CLEMENCE B. LYAMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kupata nafasi hii ya kushiriki kuchangia katika hoja hii.

Kwanza, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa kuwasilisha hotuba yake katika mfumo na lugha nyepesi, iliyoeleweka vizuri na wananchi wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nawapongeza Mawaziri wote na Wataalam/Watendaji walio katika Ofisi yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza sana Serikali kwa kukubali kuwaongeza posho Madiwani na kuwapunguzia ushuru kwenye vyombo vya usafiri watakavyonunua kwa matumizi ya kikazi. Maamuzi haya, yanaonyesha usikivu wa hali ya juu kwa mapendekezo ya muda mrefu ya Wabunge na kutambua thamani ya mchango mkubwa wa Madiwani katika kuhimiza, kuhamasisha na kuwasimamia wananchi kujiletea maendeleo ya kiuchumi katika maeneo yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili mnyororo wa viongozi ulioungana, usiwe na pengo katika kusimamia na kuhamisisha ushirikiano wa wananchi kujiletea maendeleo yao ya kiuchumi katika ngazi za Vijini na Vitongoji, napendekeza kuwa Serikali ifikirie pia kuwapa posho ndogo Wenyeviti wa Vijiji na Vitongoji ili kudhihirisha inavyothamini kazi zao nyingi katika ngazi zao za utawala kulikogubikwa mfululizo wa matatizo mengi.

Napendekeza, posho hii kwa mfano TSh. 10,000/= kila baada ya miezi 3 kwa Wenyeviti wa Vijiji na TSh. 5,000/= kila baada ya miezi 3 kwa Wenyeviti wa Vitongoji. Viwango hivi, katika maisha ya Vijijini, vitawapa motisha ya Wenyeviti hawa kutekeleza kazi zao kwa kujituma zaidi kwa kuona kwamba wamethaminiwa. Vyanzo vya malipo haya, nategemea vitokane na fedha itakayookolewa kutokana na udhibiti mzuri zaidi wa matumizi ya fedha nyingi za Serikali, ambazo siku za nyuma zilikuwa zikitumika vibaya kwa kufujwa na baadhi ya Watendaji na viongozi ambao sio waaminifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wengi nchini wanaichukia Serikali katika ngazi za Vijiji pale ambapo mapato na matumizi hayasomwi kwa wakati. Kwa hiyo, ili kuongeza imani na ushiriki wa wananchi katika kuchangia mipango na mradi ya maendeleo, Serikali ifanye utafiti wa kina kubaini sababu kubwa za kucheleweshwa au kutosomwa mapato na matumizi ya fedha za miradi ya Vijijini.

Aidha, napendekeza Serikali iandae *standard form* maalum za kila *classification* ya miradi inayojulikana kwa mfano ujenzi wa Madarasa, Zahanati, Visima vya Maji, visambazwe Vijijini ili vijazwe na Watendaji katika ngazi zao na kutoa agizo la kuwahimiza kusomwa Mapato na Matumizi si zaidi ya mwezi mmoja au miwili tangu mradi wowote kuanza. Pia Serikali ipange adhabu za kutoa kwa wale watakaokiuka maagizo ya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, Watendaji katika Halmashauri nchini, wahamasishwe kujiepusha na ubadhirifu na matumizi mabaya au ufujaji wa fedha. Ni budi Serikali itafute mfumo wa utawala kwa kushirikiana na Mkaguzi Mkuu wa Serikali *(CAG)*, utakaowapa Wakaguzi wa Ndani madaraka na maamuzi huru zaidi na yenye nguvu za kujitegemea na kuheshimika zitakazotumika kudhibiti, kuhoji na kutoa ripoti kuhusu

matumizi ya fedha yaliyo nje ya kanuni, utaratibu au sheria za matumizi ya fedha. Mfumo huo, unapaswa kutoa maelekezo bayana kwa Mkurugenzi Mtendaji, hatua anazopaswa kuzichukua hata kama masuala mengine yatamhusu yeye mwenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mtindo huu, Watendaji wengi watawaheshimu zaidi Wakaguzi wa Ndani na kuogopa kukumbwa na ghasia zitakazowakuta watakapofuja au kukiuka kanuni za matumizi ya Fedha za Halmashauri.

Mheshimiwa Naibu Spika, ubadhirifu mkubwa unatokea katika Halmashauri zetu, ni kutokana na udhibiti hafifu wa taratibu za kutoa zabuni kwa Wakandarasi mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukweli ni kuwa, kutoshiriki kwa Madiwani katika *Tender Committee,* kumeongeza zaidi ukiukwaji na ufujaji wa fedha za zabuni kuliko ilivyokuwa wakati Madiwani walipokuwa wakishiriki katika *Tender Committee.*

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuzuia au kupunguza kwa kiasi kikubwa uhuru wa Watendaji kutumia mbinu mbalimbali za kufuja fedha za zabuni, naishauri Serikali kwa kushirikiana na *PPRA* na *CAG* na taasisi nyingine inayoona inafaa, itafute mfumo mbadala wa kutoa zabuni mbalimbali katika Halmashauri zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, napendekeza uwezekano wa kuwepo kwa hatua mbili za utoaji zabuni. Hatua ya kwanza, iwe ni ile ya Watendaji peke yao kutoa zabuni ya awali yaani *Pre-qualification* na kueleza vigezo vyote vilivyozingatiwa kuwateua au ku-*short list* walioomba *tender* husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, hatua ya pili ya kutoa tenda ya maamuzi ya mwisho iwashirikishe baadhi ya Madiwani pamoja na Watendaji. Njia hii itaweza kusaidia kuondoa ukiritimba wa maamuzi uliotokana na vigezo vilivyotathminiwa na Watendaji peke yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya mchango huu, naunga mkono hoja hii.

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nampongeza Waziri Mkuu kwa hotuba yake nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, matumizi mabaya ya madaraka kwa viongozi waliyopewa dhamana ya kuhudumia wananchi. Viongozi hawa kwa mfano Wakuu wa Wilaya, Wakurugenzi wa Wilaya, wamekuwa wanawatendea wananchi kinyume na taratibu na sheria kwa mfano:-

(i) Kutengua matokeo ya uchaguzi pale wanapobaini nafasi ya Mwenyekiti wa Kijiji au Kitongoji imeshikwa na Chama cha Upinzani;

(ii) Nafasi kama hizi pamoja na za Madiwani zinapotokea kuwa wazi, wanachukua muda mrefu sana kutoa taratibu za kuziba pengo; na

(iii)Mahali pengine wanaziba kinyemela kwa kumweka mtu kutoka Chama cha Mapinduzi bila uchaguzi kufanyika. Mifano ipo mingi kutoka maeneo mengi mojawapo Wilaya ya Urambo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu elimu kwa watoto wanaotoka familia maskini/duni, Serikali imetangaza wazi kwamba itawasaidia kwa kuwapatia elimu bure na upo utaratibu unaofanyika kwenye Wilaya zetu kuwatambua, watoto hawa walengwa na fungu linatolewa kwa ajili yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, yapo malalamiko mengi sana kutoka kwa wananchi kwamba wanaonufaika na fursa hii, ni watoto wa familia zenye uwezo na wale wasio na uwezo kuikosa na kuendelea kubaki bila elimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, watoto hawa wamekuwa wakifuatilia Wilayani hadi wanachoka na ukizingatia hata nauli ya kwenda huko Wilayani ni shida. Wanaofaidika na nafasi hizo, wengi wao ni watoto wa watumishi wa Halmashauri.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali iangalie utarabitu mwingine mzuri utakaowawezesha walengwa kunufaika na fungu hili linalotolewa na Serikali pia kuinua familia za hali ya chini.

Mheshimiwa Naibu Spika, mawasiliano ya *TBC* na Radio Tanzania, bado kuna maeneo ambayo hawapati habari zinazoendelea hapa Tanzania, wanasikiliza redio Kenya na Radio Zanzibar na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya ya Urambo Mashariki, kuna Kata ambazo hawajui nini kinaendelea mfano Kata ya Usoke, Kiloleni na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la ujenzi/upanuzi wa Kiwanja cha Ndege Tabora. Kiwanja hiki ni muhimu sana kwa maendeleo ya Mkoa wa Tabora na Wilaya zake. Serikali ituambie, ni lini kiwanja hiki kitapanuliwa?

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ujenzi wa barabaraqa ya Manyoni – Itigi – Tabora – Kigoma, Mheshimiwa Waziri Mkuu, tunaomba sana, barabara hii ni kiungo muhimu sana sana kwa Mikoa yote ya upande wa Magharibi. Kwa kufungua barabara hii, tutakuwa tumefungua njia ya maendeleo ya wananchi wote wa Mikoa hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala la mazingira, hali ya maisha ya wananchi, imekuwa ngumu, vitu vimepanda bei na wananchi wengi wamejikita kwenye uchomaji mkaa, ukataji magogo na ukataji mbao usiozingatia taratibu na Sheria. Gunia la mkaa mjini ni Sh. 15,000/- mpaka Sh.30,000/=, umeme ni ghali, uwezo wa gesi na majiko ya gesi, wengi wanashindwa kumudu, mafuta ya taa Tsh. 1,500 – 1,600/=,

wananchi wa kawaida ategemee wapi? Serikali itupie macho suala hili vinginevyo nchi itakuwa jangwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la usalama wa nchi yetu, kumekuwepo matukio ya kutisha, yanayotishia amani na usalama wananchi maeneo mengi. Silaha nzito na kubwa zinamilikiwa na watu binafsi, hali hii ni hatari sana. Maeneo ya mipakani wanakoingilia wakimbizi, ndio hatari zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tukio la hivi karibuni lililotokea Urambo, Mkuu wa Wilaya na Kikosi cha FFU kutimuliwa kwa risasi na kikundi cha watu wanaojificha msituni, kifanyiwe kazi na kubaini wahusika. Ikiwa Serikali haitachukua hatua za haraka kwenye matukio kama haya, kwanza tunawajengea wananchi hofu ya kuishi. Pili, tunawapa fursa wahusika kujijenga na tatu, tutashindwa kuwadhibiti huko mbele ya safari.

Mheshimiwa Naibu Spika, maoni, wakimbizi watakapokuwa wanaingia kwenye mipaka yetu, wakaguliwe kwa sababu silaha nyingi wanaingia nazo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru.

**MHE. USSI AME PANDU:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, naomba kuchukua nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu, pamoja na Mawaziri wake na Watendaji wake wote wa Wizara hii, kwa hotuba yake ambayo ni nzuri na imekidhi matakwa ya Watanzania lakini pia ni bajeti itakayotuwezesha kutekeleza kikamilifu Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2005.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, muungano, nchi hii, ni ya mfano Barani Afrika kwa kuweza kuendelea kudumisha Muungano wetu kati ya Tanzania Bara na Tanzania Visiwani (Zanzibar) kwa ushirikiano mzuri tunaouonyesha katika kujenga mustakabali wa nchi yetu na vizazi vijavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kasoro ndogo ndogo zinazojitokeza, ni imani yetu kwamba baada ya muda ujao, kasoro hizi zitamalizika.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, ahadi ya Rais Mstaafu Awamu ya Tatu, wakati wa Kampeni ya Uchaguzi wa mwaka 2005, Rais Mstaafu wakati anafungua barabara ya Amani – Mtoni, katika Jimbo langu, kwa awamu ya kwanza ya ujenzi wa barabara hiyo. Mheshimiwa Rais aliahidi ujenzi wa barabara hiyo kwa awamu ya pili yenye *kilometer* nne na ataimaliza kabla hajaondoka madarakani. Mheshimiwa Waziri Mkuu, utekelezaji wake mpaka leo bado haujatekelezwa. Je, Mheshimiwa Waziri Mkuu, wananchi pamoja na wanachama wetu ambao walisikia ahadi hiyo, watatuelewaje kwa Serikali ya Muungano kushindwa kujenga kilomita hizo nne (4) ambazo Rais aliahidi? Naomba jibu.

**MHE. ANASTAZIA J. WAMBURA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kutoa mchango wangu kwa maandishi.

Kwanza, ninampongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa hotuba yake nzuri inayoonyesha mikakati ya utekelezaji wa sera za nchi katika sekta zote.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia naipongeza Serikali kwa kazi nzuri inayofanya kwa kupitia mikakati mbalimbali zikiwemo program za *TASAF*, *ASDP* na *MACEMP,* kwa nia ya kuboresha maisha ya wananchi. *TASAF,* imefanya kazi mzuri sana katika Mikoa yetu ya Tanzania kwa upande wa elimu, afya, maji na uwezeshaji wa wananchi kiuchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la kushangaza, ni pale ambapo kwa miaka zaidi ya miwili sasa tangu kuanzishwa kwa miradi hii ya *ASDP* na *MACEMP,* bado wananchi hawazitambui program hizi kabisa kutokana na kusuasua kwake kwani wavuvi na wakulima wanalalamika mbona hawatazamwi? *MACEMP* wanasuasua wakidai kwamba wanafanya utaratibu ili pesa za mradi zisimamiwe na *TASAF.* Kwa mtazamo wangu, naona *TASAF* watarundikiwa mambo mengi kiasi cha kushindwa kumudu kazi zote. Kwa ujumla, proramu zote tatu nilizozitaja awali, ni kubwa na kama utekelezaji wake utafanyika kama ilivyopangwa, Watanzania hasa jamii za Vijijini zitaendelea haraka sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wangu ni kwamba, wasimamizi wa programu hizi na nyinginezo, washirikiane na hasa kwa kuzingatia maslahi ya wananchi ili fedha za miradi ziwafikie walengwa inabidi *MACEMP,* wajiamini na kuomba ushauri kwa *TASAF* juu ya jinsi gani fedha zinaweza kuwafikia wananchi ili waweze kuitekeleza programu hii bila ucheleweshaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, wazee wa nchi yetu, wake kwa waume, wamekuwa na msaada mkubwa katika ujenzi wa Taifa tangu enzi za ujana wao na sasa kama waelekezi na wafafanuzi wa mambo ya kihistoria, wapo wazee wastaafu wanaothaminiwa na wastaafu wengine hawathaminiwi. Lakini wapo wazee ambao walikuwa wakulima siku zote na sasa nguvu zinawaishia pasipo msaada wowote. Naomba wazee hawa wasaidiwe kwa ukaribu kuhusu teknolojia za kuharakisha shughuli za kilimo. Wapewe *power tiller,* katika vikundi vyao, mashine za kupukuchulia mahindi, mtama, karanga pamoja na mikokoteni ya kubebea mazao yao kutoka mashambani.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Ofisi ya Waziri Mkuu, kwa kuwaongezea Madiwani wetu maslahi. Napendekeza waendelee kujengewa uwezo kwa namna mbalimbali zikiwemo semina na *study tour,* ili waweze kufanya ufuatiliaji na usimamizi mzuri katika mpango wa *D by D*.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile kwa kuwa miundombinu ya barabara, ni hafifu na bei ya mafuta inapanda mara kwa mara, ninashauri Halmashauri ziwapatie

Madiwani zile pikipiki za matairi manne ambazo zinatumia mafuta kiasi cha lita moja kwa kilomita 100 ambapo Madiwani wataweza kuzungukia Kata zao kwa muda mfupi na kwa gharama nafuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Watanzania wapatao milioni 17.5, wanaishi katika umaskini uliokithiri wa kipato cha chini ya Shilingi 1000/= kwa siku. Wengi wao wanao uwezo wa kufanya biashara isipokuwa hawana elimu ya ujasiriamali na pengine kukosa fursa za mikopo.

Napendekeza kuwa *SIDO* itoe mafunzo ya ujasiriamali kwa watu wa aina hii bure ili waweze kukopesheka. Nalisema hili kwani mimi mwenyewe nimejaribu kutoa mafunzo ya ushonaji, utengenezaji batiki, ufyatuaji tofali, kilimo cha uyoga na kuvipatia vikundi hivi kiasi kidogo sana cha mitaji na wameonyesha kuridhika na kuendelea kupata faida na kukuza mitaji yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, maji ni hitaji la msingi kwa viumbe hai ambavyo ni binadamu, wanyama na mimea na maji yanapokosekana kabisa viumbe hufa. Uhaba wa maji, ndiyo kero ya kwanza katika nchi yetu ambapo tatizo hili lina athari zifuatazo:-

(1) Uchumi, kwa kupunguza muda wa nguvu kazi katika shughuli za kiuchumi;

(2) Afya, kwa kuwa ni vigumu kuwepo na usafi wa kuridhisha bila kuwa na maji na matokeo yake ni milipuko ya maradhi ya kuhara, minyoo na kipindupindu;

(3) Lishe duni kwa watoto wa chini ya umri wa miaka mitano kwani akina mama hukosa muda wakutosha kutayarisha idadi ya milo inayotakiwa kwa watoto wao na kuzingatia ubora; na

(4) Elimu kwa watoto wetu huathirika kwani nao pia hushiriki katika zoezi la utafutaji wa maji wakitumia muda mrefu ambao ungetumika kujisomea, Walimu pia hawataki kwenda kufanya kazi katika maeneo yasiyokuwa na maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, tukisubiri wahisani, tutachelewesha maendeleo ya nchi yetu ambapo waathirika wakubwa ni jinsi ya kike.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninalo pendekezo moja ambalo nina hakika kuwa litawezekana. Watanzania wote wenye kipato, waombwe kuchangia kwa kutumia utaratibu mzuri lakini isiwe lazima bali hiyari. Vijiji vitakavyochangia fedha nyingi na kwa muda mfupi zaidi, vipatiwe kipaumbele cha kwanza. Majina na kiasi kilichochangiwa, viwekwe kwenye ubao wa matangazo wa Kijiji. Wabunge tulichangia timu ya Taifa Stars na benki ya Wanawake, tunaweza pia kuchangia maji. Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya, Wakurugenzi, Watumishi wote wa Serikali na wasio wa Serikali, wachangie. Wafanyabiashara wachangie kupitia benki na majina yao yapelekwe kwenye ubao wa matangazo wa Halmashauri. Makampuni mbalimbali kama *Vodacom, Celtel, Tigo* na wawekezaji wakubwa, wote waombwe kuchangia, ikiwezekana tuombe

ofisi za Ubalozi na Mashirika ya Kimataifa, yatuunge mkono. Suala hili, linawezekana, ahsante.

**MHE. ENG. CHRISTOPHER K. CHIZA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imefanya uamuzi mzuri wa kupeleka rasilimali zake kwa wananchi kupitia Halmashauri za Wilaya kwa mtindo wa *D by D.* Fedha hizi ni nyingi, tunahitaji kupata *"Value for Money"*, nashauri tuwe na mfumo unaowezesha Wizara zinazopeleka fedha Wilayani kufanya yafuatayo:-

(1) Ukaguzi wa kazi *(Physical progress)*

(2) Ukaguzi wa fedha *(Financial Progress)*

(3) Kuna visingizio vya ugumu na urasimu wa *Procurement Act,* mimi siamini. Halmashauri zijali kwanza maslahi ya wananchi kuliko kuung'ang'ania utaratibu wa manunuzi na kuchelewesha kazi hata pale ambapo thamani ya kazi ni ya shilingi milioni mbili tu.

**MHE. KIUMBWA MAKAME MBARAKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninamshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa uzima na kunipa uwezo wa kuchangia hotuba hii.

Pia nawashukuru wapiga kura wangu, wanawake wa Mkoa wa Kusini Unguja kwa ushirikiano wanaonipa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimpongeze Waziri Mkuu, Mawaziri wake, Mheshimiwa Marmo na Mama Kombani, Naibu Waziri, Katibu Wakuu na Maofisa wote wa Wizara, walioshirikiana na kuleta bajeti ndani ya Bunge letu Tukufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, bajeti ya Waziri Mkuu, iliyo mbele yetu, ni bajeti ya ukombozi na utekelezaji wa Ilani ya Chama chetu cha Mapinduzi na imezingatia utekelezaji wa Malengo na Dira ya Maendeleo 2025.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kuchangia masuala ya Muungano. Muungano wetu ni mzuri sana na umeleta upendo na matumaini mema miongoni mwetu. Nimefurahi sana katika Kitabu cha hotuba ya Waziri Mkuu, kimezungumzia kuratibu masuala ya Muungano, kufanya utafiti na kutoa elimu kwa umma pamoja na mgawanyo wa mapato. Masuala haya yote, ndio yanayosababisha migogoro na migongano katika nchi yetu na kuonekana kana kwamba Muungano wetu haufai.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba mambo yetu haya yaliyoelezwa, mazungumzo yaongezwe *speed* ili yaishe ili Muungano wetu uwe imara na wale wenye tamaa ya fisi kuwa mkono utaanguka na wale wanaodhani Muungano wetu utavunjika, waone ukiimarika zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, migomo ya wanafunzi katika vyuo vikuu. Kumekuwa na mtindo wa wanafunzi wa vyuo vikuu kugoma, hali ambayo ni kinyume na utaratibu na kusababisha usumbufu kwa wengine ambao hawahusiki na mgomo huo. Pia husababisha hasara kubwa kwa Taifa.

Mheshimwa Naibu Spika, umefika wakati sasa kukomesha vitendo hivi kwa Serikali kutoa adhabu kali ikiwemo kuwafukuza kabisa wale wote wanaoanzisha migomo. Wazee wanasema "mtoto hanyei kiganja na mkono ukaukata" lakini mtoto huyo huyo, ukicheka naye sana kuna siku atakuvua nguo mbele ya watu. Kwa hiyo, Serikali imewaachia sana wanafunzi na ndio maana kila siku wanaendelea na migomo. Kwa hiyo, adhabu kali inahitajika bila ya kumwonea huruma mtu yeyote na bila kujali mtoto wa nani na anatokea wapi. Serikali yetu ina mambo mengi ya kuyashughulikia na si vyuo vikuu pekee.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mchango wangu huu mdogo, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. WILSON M. MASILINGI:** Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wa Jimbo la Muleba Kusini, wanaridhishwa na jitihada za Serikali yao ya CCM katika kupambana na umaskini, kuwahudumia na kuharakisha maendeleo yao kwa kuendeleza utawala bora na kusisitiza elimu.

Aidha, wanaamini matatizo ya utendaji ngazi ya Wilaya, Kata na Vijiji, yataendelea kushugulikiwa kwa uzito unaostahili ili kuwaondolea kero. Baadhi ya Watendaji sio waadilifu kwa kutokuwa wazi katika kuwajibika kwa kutoa taarifa ya mapato na matumizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, baadhi ya Wenyeviti wa Vijiji wamekuwa sio waadilifu kwa kushirikiana na Watendaji katika ubadhirifu wa rasilimali za umma. Nitaendelea kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu, kuhakikisha viongozi na Watendaji wote wahalifu, wanakamatwa na kufikishwa mbele ya vyombo vya sheria kabla ya mwezi wa kumi mwaka huu. Wananchi wanaomba ushirikiano wa Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI.

Mheshimiwa Naibu Spika, naungana na Wabunge wenzangu, kuishukuru Serikali yetu kwa kuwa sikivu na kuahidi kuboresha mazingira ya kazi ya Waheshimiwa Madiwani. Nashauri ahadi hii, itekelezwe haraka iwezekanavyo. Aidha, nashauri Serikali ifikirie kwa pamoja na posho za Wenyeviti wa Vijiji na Vitongoji kwa sababu wanafanya kazi ngumu ya kisheria. Kusimamia miradi ya maendeleo vijijini ni kazi ya Serikali ya Kijiji.

Aidha, kuhakikisha kuna amani na kuheshimu sheria vijijini, Wenyeviti wetu wa Vijiji na Vitongoji wanatumia muda mwingi kutekeleza mambo hayo. Sioni mantiki, kupeleka fedha nyingi Vijijini kwa ajili ya maendeleo bila kutenga fedha kwa ajili ya posho zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kufafanuliwa Ibara ya 40 ya hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, barabara ya Kagoma – Muleba – Biharamulo – Lusaunga, haikutajwa na ujenzi ulisimama kutokana na upungufu wa Wakandarasi mwaka huu, je, itaendelea kujenga mwaka wa fedha 2008/2009?

Mheshimiwa Naibu Spika, Jimbo langu la Muleba Kusini, lina watu wapatao 300,000 (laki tatu). Tumeanza michakato ya kuomba Muleba iwe na Wilaya mbili au tatu kwani vigezo vyote vipo. Naahidi kwenda kusukuma ugawaji wa Kata na kuongeza Tarafa katika maandalizi ya kupata Wilaya. Wananchi wanaomba ushirikiano na Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. VEDASTUSI M. MANYINYI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naendelea kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa jinsi anavyoendelea kushughulikia matatizo ya wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, jana, nilipokuwa nikichangia hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, muda wa kuwasilisha maombi yangu ulikuwa mdogo sasa, naomba yaliyobakia niwasilishe kwa maandishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuboresha wafugaji watoke kwenye uchungaji wa kizamani, naomba *Ranch* zetu kama Kongwa, Ruvuma, Mpwapwa na kwingineko, zitumike kuzalisha madume kama *Boran* na Serikali iyagawe kwa wafugaji kama ruzuku. Madume hayo yakipandishwa kwa ng'ombe wetu kama Zebu, wataweza kupatikana ng'ombe bora zaidi na tutawafuga kwa muda usiozidi miaka minne na kuwauza kuliko ilivyo sasa tunafuga hadi miaka kumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la waendesha baiskeli, naamini kila mmoja wetu analielewa vizuri na hili tumelizungumza toka mwaka jana na mwisho Serikali ilikubali kuwa Muswada ungeletwa Bungeni tokea mwanzoni mwa mwaka huu. Kwa bahati mbaya, tunaona Serikali kama inalisahau. Namwomba Mheshimiwa Waziri Mkuu, alitolee ufafanuzi suala hili la waendesha baiskeli na pikipiki.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja.

**MHE. MOSSY SULEIMAN MUSSA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, napenda kuunga mkono hoja hii ya Waziri Mkuu. Pamoja na kumpongeza na kumwombea ufanisi mzuri wa madaraka yake mapya, imani ya Watanzania kwake ni kubwa kwa sababu ya rekodi yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nachukua fursa hii, kumpongeza Waziri Mkuu, kwa uwasilisho wa hotuba yake ambayo ilichukua muda wa masaa mawili *(2 hrs)* bila kuonyesha udhaifu wowote, hivyo kuonyesha mfano mzuri kwa Mawaziri wanaomfuata.

Mheshimiwa Naibu Spika, bado naendelea kuiomba Serikali ifungue ofisi ndogo ya Waziri Mkuu, Zanzibar kwani yapo masuala ya Watanzania Zanzibar ambayo yanataka msaada kutoka Ofisi ya Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, wapo baadhi ya Wabunge ambao wanapotosha umma wa Watanzania kwa kutaka usawa ndani ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kwa kisingizio cha kutokuwepo usawa kwa sababu ambayo inaweza kuwa sawa na ukabila, binafsi siungani na hoja hiyo kwa sababu Zanzibar haikaliwi na watu wa Unguja na Pemba pekee kwani wapo wale wanaoitwa Wazanzibara na wao mbona hawana uwiano kama wanavyodai wengine ambao wanataka nafasi za uongozi kwa usawa?

Mheshimiwa Naibu Spika, nadhani tuache mambo ya kitoto, tujenge nchi yetu na kufuata usia wa Marehemu J.K. Nyerere, ili tuweze kutokomeza fitina, dharau, uroho, ubinafsi na tujikite katika mambo ya kuimarisha uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kwamba tumepata uhuru na kuendesha shughuli zetu sisi wenyewe katika nyadhifa mbalimbali nyeti, lakini mimi namwomba Mheshimiwa Waziri Mkuu, awe mkali kidogo katika kuhimiza ufanisi katika ofisi zetu kwani nidhamu zinapungua siku hadi siku. Uwajibikaji haupo sawa sawa hivyo kupelekea kufanya kazi kwa maneno ya mdomoni zaidi kuliko ki-utendaji. Aidha, katika ofisi zetu, kila mtu ni mkubwa kiasi cha kwamba ufanisi unashuka, inaudhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, yapo maeneo ambayo yanaweza kuwekewa mkazo katika kukuza uchumi wa nchi yetu hasa bahari. Pamoja na kwamba Serikali haimo katika biashara lakini ina uwezo wa kutoa msukumo wa pekee katika Sekta ya Uvuvi katika kuwavutia wawekezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, sekta ya elimu inapaswa ipewe kipaumbele zaidi ya hapa na zaidi katika shule za vijijini kwani kutokufanya hivyo, kutaleta utofauti kati ya shule za Serikali na *Private*, shule za Vijijini na Shule za Mijini, hivyo kutafanya baadaye nafasi za kazi Serikalini kuhodhiwa na baadhi ya watu fulani kutokana na *background* zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kuhamia Dodoma, nahisi Serikali inataka kufanya hivyo lakini inajisahau. Mfano zipo taasisi muhimu ambazo bado zinajengwa Dar es Salaam badala ya Dodoma. Lakini mfano mzuri, ni ule wa kujenga Vyuo vikuu hapa Dodoma, huo ni mfano wa kuigwa.

Mheshimwa Naibu Spika, mikakati ya maandalizi ya Hopitali ya Rufaa kwa Dodoma ni muhimu sana. Hivyo, namwomba Mheshimiwa Waziri Mkuu asisitize kupatikana kwa eneo kubwa na mipango ya baadaye ya Ujenzi ianze mapema kwa umuhimu wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, suala la kuboresha Majeshi yetu lipewe umuhimu kila siku, hasa mishahara, sare, magari, masomo, ufundi hasa kikosi chetu cha *Navy,* ahsante.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. FUYA G. KIMBITA:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, ni pongezi za dhati kabisa kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mawaziri na Manaibu, katika Ofisi yake pamoja na Watendaji wengine wote kwa hotuba nzuri tuliyoitarajia, yenye kugusa maeneo ya kipaumbele katika nchi yetu kwa wakati huu. Hongereni sana na Mwenyezi Mungu awabariki sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaipongeza Serikali kwa takwimu zinazoonyesha ukuaji wa uchumi kwa kiwango cha 7.1%. Rai yangu hapa, ni ukuaji huu wa uchumi sasa utafsiriwe kwa vitendo kwa maana ya kumgusa mwananchi pamoja na kufanya mengine yote. Muhimu sana, ni usimamizi mzuri na wa wazi wa rasilimali zetu na uwajibikaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaweka msisitizo zaidi katika *SACCOS* kwani ni dhahiri hizi *SACCOS* ndizo zitakazokuwa mkombozi wa wananchi wetu kote nchini kwa kuzaa Benki Kata.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapendekeza fedha kidogo tulizonazo katika mipango ya miundombinu, tuendelee kuboresha barabara zetu za Wilayani na Vijijini na zile barabara kuu na za Mikoa tukakope nje au kutumia utaratibu *"BOT"* ili tuweze kuharakisha maendeleo yetu kwani pasipo miundombinu bora ya uhakika, ni ndoto kuendela.

Mheshimiwa Naibu Spika, usafiri katika Jiji la Dar es Salaam, ni tatizo kubwa sana ambapo tunapoteza muda na pesa nyingi sana katika tafsiri zote. Ninapendekeza barabara zilizopo ziwe zinapatiwa ukarabati wa uhakika, kuzifungua na kujenga barabara zote za mzunguko *(ring roads)* na zile za *shortcuts* pamoja na uzibuaji wa mitaro ya maji machafu pamoja na kuziba mashimo mara yatokeapo barabani. Ninapendekeza upanuzi wa barabara ya kutoka Mwenge hadi njia panda ya kwenda kiwanda cha cementi cha *Wazo Hill* ufanyike.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye sekta ya nishati, ninaipongeza Serikali kwa jitihada inayofanywa lakini nako lazima tutumie vyanzo vyote tulivyonavyo kwani hata tukizalisha ziada tuweze kuwauzia majirani zetu na hapa ninasisitiza kufufuliwa kwa Kituo kidogo cha KIKULETWA kule Wilayani Hai.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika sekta ya ardhi, ni muhimu sana kufuatwa kwa sheria zilizopo ili kuepusha migogoro inayotokea au itakayotokea, mfano kutenga maeneo rasmi kati ya wakulima na wafugaji, ujenzi holela mijini na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, ile ardhi yetu nzuri kwa kilimo cha mazao ya chakula, tusilime jatropha (mimbono) kwani Jatropha haihitaji maji mengi na inastawi kwenye maeneo kame yenye maji kidogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kilimo kwa ujumla, mapinduzi makubwa ni ya lazima na hapa ninasisitiza wasomi wetu wazalengo, ni muhimu kuwapa kipaumbele pasipo kusahau mbolea na bei yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, umwagiliaji kwa ujumla wake, ni muhimu sana na ndiyo kilimo cha uhakika, nikikumbushia yale maeneo ya Pambarare kule Wilayani kwangu Hai na hata milimani.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushirika ni muhimu sana lakini tatizo kubwa sana ni utendaji wa viongozi wa Ushirika nchini, wengi wao sio waaminifu na hivyo kuwakatisha tamaa wana Ushirika yaani wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika sekta ya madini, jamani uzalendo ututawale kwani yanayofanyika huko, ni aibu. Mfano hakuna sababu yoyote ya msingi ya kuendelea kuwaruhusu wageni kuwa kwenye Madini ya Vito kama *Tanzanite*, Rubi na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, maadam sasa duniani, tunajulikana na kufahamika kwa kuwa na dhahabu, almasi na kadhalika ni muhimu tuwe na *Blue Prints* za mikataba ya Madini yote hivyo kila mwekezaji anayekuja akae akifahamu wazi anakuja kuingia kwenye mikataba ya aina gani ambayo uzalendo kwa maana ya kulinda maslahi ya Taifa letu, utazingatiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika sekta ya viwanda, nako panahitajika mapinduzi ya lazima kabisa, huku kunahitajika viwanda vidogo vya kati na vile vikubwa vilivyobinafishwa ambao hawajaweza kuviendesha, wanyang'anywe.

Mheshimiwa Naibu Spika, sekta ya utalii, bado kabisa hatujaitumia vya kutosha kwani bado kuna aina nyingi sana za utalii ambazo hatujazitumia au kuzitambua na ili tufanikiwe ni muhimu kuwepo na Mfuko wa Utalii ambao utasaidia katika kutambua na kutangaza vivutio vyote vya zamani, vya sasa na vipya tulivyojaliwa na Mwenyezi Mungu.

Mfano katika Mlima Kilimanjaro, kuna utalii wa *Summit Tourism of Mount Kilimanjaro, Eco and Cultural* ambapo mapato kwa Serikali na kwa wananchi, yangeongezeka. Kwa kuanzia, njia ya ahadi ya Mheshimiwa Rais, katika Jimbo la Hai ya kutoka Kwasadala kwenda Masama, ni mojawapo ya aina mpya ya utalii kwenda katika mlima Kilimanjaro.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika sekta muhimu ya elimu, tunahitaji kuongeza uwezo zaidi kwa maana ya bajeti pamoja na elimu ya vitendo ili tuwe na wanasayansi pamoja na watu wa kufanya kazi viwandani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ujumla, huduma zote za kijamii, ni muhimu sana kwa mfano maji, afya na kadhalika ambapo ni vema kuongeza fedha kwenye bajeti zake.

Mheshimiwa Naibu Spika, mapambano dhidi ya rushwa, ni lazima tuongeze wigo mpana zaidi kwani kila kukicha Watendaji wanakuja na mbinu mpya za kudai kupokea rushwa na hasa kwenye Halmashauri zetu tunakopeleka pesa nyingi sana kwa mtindo wa *D by D*. Ni muhimu kutolewa kwa elimu kwa wananchi wetu ili wajue jinsi ya kufuatilia utekelezaji wa miradi yao haswa Waheshimiwa Madiwani wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaipongeza Serikali kwa kukubali kuboresha maslahi ya Madiwani, hii itawaongezea moyo wa kuwahudumia wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapongeza jitihada zinazoendelea za mapambano dhidi ya UKIMWI lakini tunahitajika uratibu zaidi matumizi ya fedha za wafadhili kwani kuna malalamiko kuwa waathirika wanatumiwa tu lakini hawafikiwi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaunga hoja mkono.

**MHE. GAUDENCE C. KAYOMBO:** Mheshimiwa Naibu Spika, Kwanza, namshukuru Mungu kwa kutuwezesha tena kukutana katika mkutano huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia kuishukuru sana Serikali kwa yafuatayo yanayohusu maendeleo ya Mbinga:-

(1) Upatikanaji wa fedha kujenga barabara ya Songea – Mbinga;

(2) Majenereta yaliyoahidiwa na Serikali kwa ajili ya mji wa Mbiga, yamewasili na sasa ni sherehe tupu Mbinga. Kipekee namshukuru Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Jakaya Kikwete, kwa msukumo mkubwa alioutoa hasa kuhakikisha fedha zinapatikana;
Pia namshukuru Mheshimiwa Lowassa aliyekuwa Waziri Mkuu kwa kufuatilia kwa karibu suala hili;

(3) Soko la nafaka limejengwa pale Mbinga, nawashukuru sana Waziri na Watendaji wake Wizara ya Viwanda na Biashara; na

(4) Nawashukuru *DC* wa Mbinga, Mkurugenzi na Afisa Kilimo, kwa kushirikiana na wananchi wa Kata ya Mkumbi katika kutokomeza ugonjwa ulioiathiri sana kahawa ya eneo hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa napenda kuzungumzia maeneo ya jumla kama ifuatavyo:-

(1) Huduma kwa wananchi. Serikali inafanya mambo mengi mazuri lakini hayo yote, yameharibiwa na tabia ya kutokuwa chanya na kutochukua hatua zinazofaa kwa wakati. Njoo kesho, bado ni nyingi sana. Maamuzi yanachukua muda mrefu kutekelezwa na hivyo gharama kuongezeka kwa mfano:-

(a) Kuhamia Dodoma;

(b) Vijana waliojenga Mahakama Kata ya Ruanda, miaka 2 iliyopita, bado kulipwa mpaka leo;

(c) Watumishi 29 wa Idara ya Afya, Wilaya ya Masasi walioshiriki katika *Campaign* ya kipindupindu mwaka 2003/2004, bado hawajalipwa mpaka leo; na

(d) Watendaji Kata – *Scheme of Service* yao haifahamiki, aliyeacha kazi miaka ya 1999, eti analipwa Sh. 90,000 sawa na *VEO* aliyeacha kazi hivi karibuni. Kuna tatizo gani, barua yao ya tarehe 29/9/2007, mpaka leo haijapata majibu kulikoni. Mambo haya hayashughulikiwi kikamilifu na hivyo kuleta chuki kwa Serikali. Haijalishi ni Serikali ipi ya Mitaa au Kuu kwa mwananchi zote ni Serikali.

(2) Mheshimiwa Naibu Spika, uwezeshaji wananchi kwa mfano:-

(a) Mwananchi *Empowerment Fund,* haijapewa fedha kabisa. Huu ndio mpango wa kumwezesha mwananchi, kwa nini fedha hazikutengwa?

(b) Taasisi tulizonazo, hazitumiki ipasavyo kama *DIT, GST*, Nyumbu, *TIRDO*, *SIDO*, *CARMATEC, IRDP* na kadhalika.

(3) Kilimo, njaa inainyemelea dunia. Serikali ina mpango gani kuhusu Mikoa inayolima nafaka kwa wingi maana wakulima wataendelea kulima kawaida tu *inceative* zipi zimewekwa ili walime zaidi?

Mheshimiwa Naibu Spika, matatizo ya Jimbo la Mbinga Mashariki ni kama ifuatavyo:-

(1) Naomba *Mbinga Farmers Cooperative Union* ifufuliwe kama ambayo ilifanyika kule Lindi na Mtwara. Ikiwezekana ushirika ununue Kahawa mwaka huu;

(2) Bodi ya Kahawa imetakiwa na Sheria ya 2001, ifanye *registration* ya wakulima wa Kahawa, jambo hili halijafanyika. Ni lini *TCB* watafanya hivyo? Serikali ichukue hatua zifaazo kufanikisha jambo hili;

(3) Sheria hiyo ya Kahawa inakataza wanunuzi kununua matunda shambani lakini jambo hili linaendelea. Naomba Serikali ichukue hatua zifaazo.

(4) Serikali iliahidi mwaka 2005, kulipa madeni ya ushirika waliowakopa wananchi. MBIFACO inadaiwa na wakulima Sh. 106.6 milioni. Serikali ilikwishafanya tathimini na kuhakiki madeni hayo mwaka 2006. Naomba wakulima hawa walipwe;

(5) Katika hotuba ya Waziri Mkuu, uk. 48, imeainisha maeneo ya wachimbaji wadogo yaliyotengwa. Maeneo ya Makoro na Ngembambili Jimboni kwangu, hayajatajwa. Serikali itafanya lini shughuli hiyo?;

(6) Serikali iliahidi kuendeleza mradi wa umeme na Nakatate (barua ninayo), nini maendeleo mpaka sasa?;

(7) Ninaomba sasa tuwe na Halmashauri ya Mji ya Mbinga, nipewe hatua za kufuata ili 2009 tufikie lengo;

(8) Kama nilivyoarifu mwaka jana, *DC* Mbinga, hana jengo lake na hii ni Wilaya ya siku nyingi;

(9) Maji katika miji ifuatayo ni tatizo:-

(i) Mbinga mjini;
(ii)Kigonsera;
(iii)Maguu;
(iv)Matiri; na

(10)Umeme Vijijini, ninaomba Mjasiriamali, Ndugu Andoye, anayejaribu kupata umeme wa maji asaidiwe.

Ninaomba pia *REA*, watoe fedha kwa *DIT* ili wafunge mitambo midogo ya umeme vijini vya Mbinga. Mradi huu ukifanikiwa, Serikali inaweza kueneza sehemu nyingine. Hii ni taasisi yetu, ni vizuri tukaithamini.

Serikali izumgumze na *DIT* ili waweze kutengeneza vifaa kwa wachimbaji madini wadogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja kwa 100%.

**MHE. OMAR ALI MZEE:** Mheshimiwa Naibu Spika, hali ya kisiasa sio nzuri kama tunavyofikiri, ingawa hali hii haiko dhahiri lakini bado kuna viashiria ambavyo kama havitatiliwa maanani, vinaweza kusababisha kuvunjika kwa amani ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali tete ya kisiasa ya Zanzibar ambayo inaendelea kuwepo kila mara na hasa wakati wa uchaguzi, inachafua sifa ya nchi yetu. Hivyo ipo haja ya kuchukua tahadhari juu ya suala hili ili kuyakinga majanga yatokanayo na uchaguzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, uchaguzi ulio huru na wa haki, unategemea kuwepo na Daftari la Wapiga Kura ambalo limehakikiwa kikamilifu na kuwaondoa wale wote ambao wamefariki na kuwaingiza wale waliofikia umri wa kupiga kura na wale ambao wamejiorodhesha zaidi ya mara mbili au tatu kuwachukulia hatua zinazofaa ili kuwepo na haki na uaminifu na kuelewana katika suala zima la uchaguzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, bado ziko kero nyingi za Muungano ambazo hazijachukuliwa hatua za kufaa ingawa tunaambiwa kuna hatua zimechukuliwa kutatua kero hizo. Hivyo basi, sasa wakati umefika wa kutatua kero hizo ili kuondoa dhana mbaya zilizoko juu ya Muungano wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Bunge ni taasisi muhimu, hivyo ipo haja ya kuliangalia Bunge na Wabunge wake ili waweze kumudu shughuli zao za kiutendaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuipongeza Serikali kwa mpango wake wa kuwawezesha wananchi kiuchumi lakini ninapenda kuelewa Sh.600,000,000/-, zilizotengwa kwa wananchi wa Visiwani, mgao wake ukoje ili na mimi nifahamu jinsi wananchi wangu wanavyoweza kutumia fursa hiyo, ahsante.

**MHE. RAYNALD A. MROPE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nawapongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mawaziri wake na Katibu Mkuu, kwa hotuba nzuri na utekelezaji mzuri wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM.

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wangu, utajikita zaidi katika sula la uanzishwaji wa Wilaya/Jimbo jipya katika Wilaya ya Masasi Mkoani Mtwara. Suala hili ni la siku nyingi toka Awamu ya tatu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwanzoni Halmashauri ya Wilaya, ilipitisha mapendekezo kuwa iwepo Wilaya mpya ya Ndanda kutokana na wingi wa watu katika sehemu hiyo (ilikadiriwa kuwa na watu 268,000 mwaka 2004). Mji mdogo wa Ndanda, una vigezo vingi vya kuanzisha Wilaya.

Ndanda ina Hospitali kubwa ya Misheni Katoliki ambayo inatumika kama Hospitali ya Rufaa kule Kusini, kuna shule ya Sekondari ya Kidato cha V na VI, yenye wanafunzi zaidi ya 1,000, kuna vyuo vya ufundi vinavyotoa Diploma ya Useremala, Uashi, Makenika na Ufundi Umeme. Ndanda ina benki ya *NBC*, yenye *deposits* zaidi ya Sh.500,000,000/-. Pia kuna umeme na maji ya kutosha. Je, Serikali itaanzisha lini Wilaya inayojitegemea ya Ndanda?

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwa pia na mawazo, kuwa kama Wilaya ya Ndanda ingeanzishwa basi Wilaya hii ingekuwa ni Jimbo la Ndanda ambalo lingezaliwa kutoka Jimbo kubwa la Masasi. Mipaka yake ipo kihistoria, yaani toka Nanganga (mpakani kati ya Lindi na Masasi) mpaka Liloya (mpakani kati ya Jimbo la Masasi na Jimbo la Lulindi). Kiutawala, eneo hili lenye watu zaidi ya 200,000 lingeweza kuhudumia watu hawa kwa ubora zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. VITA R. KAWAWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Waziri Mkuu, Mheshimiwa Pinda, kwa kuwasilisha vema hotuba yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nianze na ushirika. Tunaishukuru Serikali kwa kuwafutia au kupunguza baadhi ya madeni ya Vyama vya Ushirika vya Wakulima wa Korosho. Lakini ili kuondoa tofauti baina ya wakulima wa mazao yanayotupatia fedha za kigeni na ushuru kwa Taifa, tunaomba Vyama vya Wakulima wa Tumbaku, nao walipiwe deni lao la Sh.1.8bn tu kwa nchi nzima.

Mheshimiwa Naibu Spika, zao la tumbaku linalimwa katika Mikoa 10 ya Tanzania Bara na linachangia pato la Halmashauri zake kwa wastani wa Sh.2.6bn kama *District Cess* na limekuwa la pili kwa miaka mingi kuchangia fedha za kigeni kwa mazao makuu na pato la Taifa. Kwa mwaka 2007, imelipa kodi kupitia sigara Sh.90bn na imeuza nje tumbaku ya dollar milioni 89,986,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, fedha hizo zote, ni kwa uzalishaji wa tani (54,000) tu na ili kuongeza uzalishaji moja ya vikwazo ni deni kwa vyama nililotaja hapo juu. Wamebanwa na Makampuni yanayonunua tumbaku, wanashindwa kununua mbolea kutoka katika *source* nyingine sababu Makampuni yanawadai hivyo kuwauzia mbolea kwa bei ya juu ili kukata madeni yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii ina wanyong'oneza wakulima kujiunga katika Ushirika kuogopa kukatwa madeni ya zamani yasio yao na hivyo kufanya kuchelewa kupanda uzalishaji wa tumbaku. Tunaamini kuwa uzalishaji ukiongezeka na mapato yataongezeka kwa nchi na wakulima. Tunaomba Serikali itulipie kama mazao mengine ya pamba na korosho vyama vyake vilivyolipiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mkopo wa wajasiriamali, Namtumbo, ni Wilaya iliyokosa awamu ya kwanza ya fedha (maarufu Mabilioni ya JK) na awamu hii tutapata mgao kupitia mtandao wa *SACCOS* za Dunduliza Sh.100,000,000/=. Lakini Naibu Waziri wa Miundombinu wakati akijibu swali kwa niaba ya Waziri wa Kazi, alisema Wilaya zilizokosa awamu ya kwanza wamepewa Sh.200,000,000/=. Sisi hatukupata Sh.200,000,000/=, tumepata Sh.100,000,000/=.

Sasa tunaomba kama ni hivyo tupewe *balance* ya Sh.100,000,000/= kwani wananchi wanahoji, tumeisikia Sh.200,000,000/= mbona tunaambiwa na Dunduliza *SACCOS* Sh.100,000,000/=? Ili kuondoa *confussion* hii, naomba hiyo Sh.100,000,000 iliyobakia.

Mheshimiwa Naibu Spika, umeme, tumeahidiwa na Wizara ya Nishati na Madini, kuwa tutapata umeme wa Gridi kwa fedha za *SIDA* lakini 2008/2009 katika hotuba ya Waziri Mkuu, haikutamkwa. Naomba ufafanuzi kuhusu suala hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. ZAYNAB M. VULU:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, napenda kuchukua nafasi hii, kukupongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa hotuba yako ambayo imekidhi na kukonga nyoyo za Watanzania.

Vilevile, nawapongeza Mawaziri C. Kombani, Waziri Marmo na Naibu Waziri A. Mwanri kwa ushirikiano wanaokupa katika kutimiza majukumu kwa Taifa letu. Baada ya pongezi hizo, napenda kutoa michango yangu kwa maandishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika maeneo yetu mengi ya Mkoa wa Pwani, tunakabiliwa na matatizo mengi, naanzia sekta ya afya, hatuna Wauguzi wa Afya na madawa ya kutosha.

Vilevile kutokana na miundombinu ya Mkoa, unakuta Kituo cha Afya kiko mbali sana hivyo kupeleka wagonjwa hasa akina mama wajawazito, hupata taabu ya kusafirishwa na hatimaye kujifungulia njiani. Hivyo basi, ni vema kuwe na magari ya wagonjwa kwenye kila Kituo cha Afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo lingine ambalo inabidi lipewe mtazamo wa kipekee, ni suala la Walimu. Hili ni tatizo sugu. Ni vema wachukuliwe Walimu wanaotoka Mkoa husika ambao watakuwa na mazoea na mazingira ya Mkoa huo na pia idadi yao iongezwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika ulimwengu huu wa sasa, shule zetu zinahitaji kupatiwa Walimu wa kutosha wa masomo ya sanyansi na maabara. Hivyo, msukumo kutoka Serikalini uongezwe ili kuwa na maabara na kupata Walimu wa masomo ya sayansi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna haja ya Serikali kuongeza nguvu kwa wananchi ili kuweza kuwa na hosteli katika shule zetu na hii itapunguza matatizo wanayopata watoto wa kike na hasa tutakuwa tumepunguza tatizo la mimba.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nimpongeze Mheshimiwa Rais, kwa juhudi zake za kupambana na UKIMWI. Kampeni yake ya Kitaifa ya kupima UKIMWI, imeleta mafanikio makubwa sana. Hali kadhalika, juhudi zako Mheshimiwa Waziri Mkuu, katika kuhimiza jamii kupima, imeleta mafanikio. Hivyo kuna haja Watanzania tuwe na siku yetu ya UKIMWI na ile ya UKIMWI Duniani iwepo. Tarehe ambayo Mheshimiwa Rais alizindua kampeni ya Taifa ya kupima VVU, ndiyo iwe siku ya UKIMWI Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hilo, naomba Mheshimiwa Waziri Mkuu, utoe wito kwa jamii na hasa viongozi popote wanapohutubia mwisho au mwanzo mwa hotuba, wazungumzie suala ambalo ni sugu kwa watoto wetu juu ya mimba za watoto wa shule.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. ATHUMANI S. JANGUO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Waziri, Mawaziri wawili, Naibu Waziri, Makatibu Wakuu wawili na Wasaidizi wote, kwa hotuba nzuri yenye mwelekeo na inayogusa maeneo yote muhimu ya kiutawala na kiuchumi wa nchi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza hotuba hii zaidi kwa mambo matatu yaliyotekelezwa na Serikali ambayo ni:-

(1) Kwa Serikali kutimiza ahadi yake ya kulipa madeni ya Vyama vya Ushirika kwa kiwango cha Sh.2.5bn lakini nashauri Serikali ihakikishe kuwa vyama hivyo sasa vinaongozwa na Watendaji hodari na waaminifu ili visianze kulimbikiza madeni mapya na viwe vina mafanikio;

(2) Kwa kuamua kuboresha posho za Madiwani, kuwaingiza Madiwani kwenye Bima ya Afya na kuwaondolea kodi kwa vyombo vya usafiri; na

(3) Kwa kuharakisha utoaji wa mbolea ya ruzuku tani 74,503 sawa na asilimia 83 ya lengo katika kipindi cha miezi mitano ya awali mwaka huu. Hapa nashauri mambo mawili yafuatayo:-

(a) Kuhakikisha kuwa ruzuku hiyo inawafikia walengwa, isiishie mikononi mwa wafanyabiashara.

(b) Mbolea iwafikie wakulima ndani ya msimu ili itumike kabla ya msimu haujapita.

Mheshimiwa Naibu Spika, madukuduku ya wana – Kisarawe ni kama ifuatavyo:-

(a) Tatizo la Maji Kisarawe Mjini. Kwa mujibu wa Ibara 88 ya hotuba hii, Serikali inatambua kuwa "maji ni miongoni mwa huduma muhimu kwa wananchi wote" lakini hotuba ya Bajeti mwaka huu, haionyeshi kuthibitisha kauli hii. Kwani mwaka 2007/2008, Sekta ya Maji ilitengewa Sh.306,000,000,000/=, mwaka huu kiwango kimeshuka hadi shilingi Sh.260,000,000,000/-. Sasa umuhimu uko wapo? Wazaramo wanasema "Zilongwa mbali zitendwa mbali".

Mheshimiwa Naibu Spika, nilipochangia kwenye hotuba ya bajeti, nilieleza adha ya wakazi wa mji mdogo wa Kisarawe kuhusu maji. Wakati mwingine wananyang'anyana maji kidogo yaliyoletwa kwenye magari kutokea Dar es Salaam. Kwenye Bajeti hii, wameomba Sh. 300,000,000 tu wanunue mitambo na matanki ili waondokane na balaa hili. Wapi! Ombi halikukubaliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hasira, wamenituma, nisiiunge mkono bajeti iwapo hakuna jibu la kuridhisha. Lakini nikawa mwana – CCM, sikulitekeleza agizo hilo. Sasa Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa jinsi ninavyofahamu, utawashuri Waheshimiwa Mkulo na Prof. Mwandosya, wafanye kila wanaloweza kutenga hizo pesa kidogo za Sh.300,000,000/= ili tuepushe adha na malumbano.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, maji vijijini, Wilaya ya Kisarawe, ina shida kubwa ya maji vijijini. Vima vifupi ama havitoi maji au maji hukauka muda mfupi baada ya kuchimbwa. Kuna visima virefu *(boreholes)* vichache tu. Tumechimba malambo sita lakini kwa Wilaya yenye eneo la kilomita za mraba 3,335 malambo hayatoshi, isitoshe, baadhi yao tayari yamekauka.

Kwa muda wa takriban miaka 10 sasa, ndani ya Bunge hili nimekuwa nikiomba Serikali itimize ujenzi wa mabwawa makubwa mawili kule Gumba na Titu. Pia irejee katika kuukamilisha mradi wa maji ya bomba ya Mzenga tokea Mto Ruvu. Wapi! Sijasikilizwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, zimetolewa ahadi nyingi tu na Wizara ya Maji na yako kabla ya uteuzi wako. Lakini ahadi zote hizo zilikuwa za kutuliza wananchi wa Kisarawe.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukaribu na Dar es Salaam, umetuponza maana wengi ndani ya Serikali wanaamini kuwa Wilaya yetu imehudumiwa kama ilivyo Dar es Salaam. Ukweli ni kwamba kiuchumi na kimaendeleo, sisi ni wa pembezoni.

Mheshimiwa Naibu Spika, utawala, naomba nikukumbushe suala la kuigawa Kata ya Masahi kwa kuunda Kata mpya ya Msimbu. Sina haja ya kueleza mengi kwani wewe mwenyewe katika kutusaidia suala hili, umeliweka kimaandishi. Sababu ulizotupa tumeridhika nazo. Sasa, kwa kuwa tunaenda kwenye uchaguzi wa Serikali za Mitaa mwakani, tunaomba basi suala la Kata ya Msimbu liamriwe kabla ya uchaguzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na ombi la Kata, Halmashauri ilileta ombi lingine la kutaka Vitongoji vifuatavyo ambavyo vilikwishatimiza masharti yote ya kuwa Vijiji navyo ni:-

1. Kitongoji cha Mwanzo Mgumu;
2. Kitongoji cha Kidugalo cha Kanga;
3. Kitongoji cha Malangalanga; na
4. Kitongoji cha Kilangali.

Mheshimiwa Naibu Spika, magari ya wagonjwa, Wilaya ya Kisarawe yenye Hospitali moja ya Wilaya, vituo vitatu vya Afya na Zahanati zaidi ya 10, haina hata gari moja la kusafirishia wagonjwa baina ya Zahanati na vituo vya Afya kwa upande mmoja na Hospitali ya Wilaya. Matokeo yake tunapoteza maisha ya watu na mara nyingi wajawazito kuhudumiwa na Wauguzi/Wakunga wa jadi au kujifungulia kwenye mabasi wakielekea vituoni na Hospitali ya Wilaya. Tunaomba sana tupatiwe angalau *ambulance* moja. Wapi ! Hali hii haikubaliki.

Mheshimiwa Naibu Spika, miundombinu, Wilaya ya Kisarawe, ina barabara kuu mbili za Mkoa, moja yenye Km 96 (Pungu – Vikumburu) na nyingine km 65 (Mlandizi – Mzenga – Maneromango). Lakini hakuna hata barabara moja yenye lami isipokuwa km sita toka Pugu hadi Kisarawe. Hata hivyo, lami haifiki Bomani. Hizo km sita

zimepatikana baada ya mvutano mrefu Bungeni na ahadi ya Rais Mstaafu. Barabara hiyo ina mambo matatu muhimu ambayo ni:-

(a) Inaunganisha Wilaya ya Kisarawe na Rufiji lakini kuna km 65 za mpakani ambazo haipitiki kabisa;

(b) Ndiyo njia fupi kuliko zote zinazounganisha Jiji la Dar es Salaam na Mbuga ya Selous ambayo inavuta watalii wengi; na

(c) Ni barabara muhimu ya kusafirishia vyakula toka Vijijini hadi soko la Dar es Salaam.

Mheshimiwa Naibu Spika, yote haya hayazingatiwi na Serikali katika kuiboresha barabara hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mambo ya sheria na utawala bora, kwa mujibu wa Ibara 108 (b) ya Ilani ya CCM ya Uchaguzi wa 2005, Serikali inahimizwa kulipatia ufumbuzi suala la kuanzishwa kwa Mahakama ya Kadhi Tanzania Bara. Kabla ya mwaka 2005 wakati wa Kampeni za Uchaguzi wa 2000, CCM na Serikali ililivalia njuga suala hili lakini baada ya uchaguzi likasahauliwa. Mwaka 2005 hasa kabla ya uchaguzi suala hili likafufuliwa baada ya uchaguzi "ziii".

Mheshimiwa Naibu Spika, huko mitaani Waislamu wanang'unika na wanasema azma hii ya CCM ni danganya toto (Waislam ili zipatikane kura zao). Sasa wamechoka kudanganywa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa Bungeni ziliundwa Tume mbili kwa nyakati mbalimbali (ya Ntagazwa na Janguo). Zote zimetoa mapendekezo ambayo yamebaki kwenye makabati. Mwaka jana, Waziri wa Sheria, alitangaza kulipeleka suala hili kwenye Tume ya Kurekebisha Sheria, hadi sasa kimya. Waislam, wanasubiri ulitolee kauli, vinginevyo utulivu utatoweka.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri Mkuu.

**MHE. GAUDENTIA M. KABAKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, hotuba imegusa sehemu zote zinazohusu maisha ya kila siku ya Mtanzania na inatekelezeka na inakidhi utekelezaji wa Ilani ya CCM ya Uchaguzi ya 2005 – 2010.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naomba nichangie kidogo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna malalamiko kutoka kwa Waheshimiwa Madiwani, kuna muda wa siku moja uliotengwa kujadili bajeti zao, hautoshi kutokana na kutaka kuijadili bajeti hiyo kwa kina kuliko inavyofanyika hivi sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, rai hii niliipata katika Halmashauri za Mkoa wa Ruvuma wakati tumeenda huko kuelezea bajeti ya Serikali ya 2007/2008. Aidha, suala hilo hilo limezungumzwa katika vikao vya Halmashauri vya Mkoa wangu Mara na pia katika vikao visivyo rasmi na Waheshimiwa Madiwani mbalimbali hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na hilo, nashauri muda huo kama inawezekana utazamwe upya na kuongezwa kadri inavyohitajika ili Madiwani hawa wazijadili bajeti zao kikamilifu na kujiridhisha katika mchakato mzima wa bajeti hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja, tena nampongeza sana Mheshimiwa Mizengo Pinda kwa uteuzi wake na namwombea Mungu amjalie afya, hekima, amani na yote anayohitaji ili kutenda kazi hii muhimu kwa Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pongenzi nyingi kwa Mheshimiwa Celina Kombani, kwa kupandishwa na kushika Wizara hiyo ya TAMISEMI lakini naomba nimpongeze Mheshimiwa Mwanri (rafiki), kwa uteuzi wake na kwa umahiri wake wa kujibu maswali yanayoihusu Wizara yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, nimpongeza Mheshimiwa Marmo kwa nafasi hiyo ya U-*chief Whip* ambao ni halali yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawaombeeni kheri na baraka za Mwenyezi Mungu katika kazi zenu na nawaahidi ushirikiano wangu kama Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi hasa hasa kwenye muungano wetu wa kushughulikia elimu ya nchi hii kwa ufanisi na kwa maendeleo ya nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawasilisha.

**MHE. RAMADHANI A. MANENO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa, ninamshukuru Waziri Mkuu, Mheshimiwa Mizengo Pinda na Mawaziri katika Wizara zilizo chini ya Ofisi yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia kuipongeza Wizara kwa ujumla, kwa maandalizi na mpangilio mzuri walioutumia katika kuandaa bajeti hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze na barabaraba. Kwa kweli uti wa mgongo wa uchumi wa Mtanzania ni barabara, Wizara itenge fedha kwa makini na usimamizi mzuri kuhusu ujenzi wa barabara maana hazipitiki.

Mheshimiwa Naibu Spika, TAMISEMI wakati umefika kuwafungia na kuwanyima kazi Wakandarasi wabovu, upo uzembe, Wakandarasi wanaharibu kazi lakini wanapewa kazi nyingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nizungumzie afya, tulisema ifikapo mwaka 2008, kila Kijiji kitakuwa na Zahanati. Tumefika Vijijini tumehamasisha, wananchi wanasubiri Zahanati.

Mheshimiwa Naibu Spika, madawa kwenye Vituo vya Afya, hakuna. Waganga hawatoshi, hali hiyo inakatisha tamaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, elimu, Walimu, bado ni tatizo kubwa. Pia upendeleo Wizara ya Elimu, kuhusu mgao wa Walimu, ukomeshwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, likomeshwe tatizo la migogoro mashuleni, vyuoni, ni aibu. Tafuteni kinga mapema kabla ya kuponya.Tunapata matatizo, tumesema kuhusu *(CDF)* mbona kimya? Imefikia mahali Wabunge wanaichukia Serikali kwa majibu ya mkato.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ni kuhusu itifaki za Wabunge. Wapo baadhi ya Ma-*RC*, Ma-*DC*, wanatudharau sana. Hii hali isiporekebishwa, ni hatari katika ufanisi wa kazi zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, uchaguzi wa wanafunzi kuingia vyuo vikuu, hali si nzuri, rushwa bado ipo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kilimo, Serikali isaidie suala hili la Kilimo kama ilivyofanya kwenye elimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, naishukuru Serikali, imesikia kilio chetu kuhusu Madiwani, japo kidogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. MCHUNGAJI DR. GERTRUDE P. RWAKATARE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kuungana na Wabunge wenzangu kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa hotuba yake nzuri na inayokidhi mahitaji ya Mtanzania.

A. Elimu Tanzania - Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba Mheshimiwa Waziri Mkuu na Serikali, ipongeze juhudi kubwa za wawekezaji kwenye sekta ya elimu. Juhudi hizo:-

(1) Zimekuza na kuinua kiwango cha elimu;
(2) Zimeokoa fedha za Kigeni;
(3) Zimepunguza matengano ya watoto wadogo na wazazi wao kwa kigezo cha kusaka elimu bora;

(4) Kutunza historia, Jografia na Mila za Kitanzania badala ya watoto kusoma historia, Jografia au mila za nchi jirani na nje;

(5) Kurudisha heshima ya nchi yetu kwa kurudisha watoto wadogo kusoma nchini; na

(6) Lugha ya Kiingereza imepanda na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo, shule zisizo za Serikali, zichukuliwe kama ni huduma kama shule za Serikali kwa sababu zinatoa elimu kwa watoto wa Tanzania kama shule za Serikali. Lakini Serikali imezibagua shule za *private,* imeziacha kabisa kama biashara wakati ni huduma kwa kuwa:-

(a) Inatoza kodi kubwa sana, *Corporation Tax,* Kodi za Majengo ya Shule, *VAT, Income Tax, NSSF, PPF* na kadhalika;

(b) Serikali haitoi hata vitabu au vifaa vya Maabara vya misaada;

(c) Serikali zichangie hata elimu za kozi fupi za Walimu, wasibague;

(d) Waondoe masharti magumu ya kupata Walimu wa nchi jirani, eti lazima awe na *Degree*;

(e) Serikali ichangie hata mishahara ya Walimu wachache;

(f) Ruzuku inayoimbwa hatuioni na ni Sh. 10,000/= kila mwaka; na
(g) Serikali isipange ada za *Private Schools* kwa sababu gharama ni kubwa. Kiwanja unanunua pengine milioni mbili (2) – 1 Billioni na kadhalika. Ujenzi, bilioni 1 – 2, *furniture,* mishahara, usafiri – *buses, Meals* (chakula), michezo, *medical, books, stationery*, daftari na kadhalika, hailipi kabisa, shule ni huduma tu.

B. Mpango wa uwezeshwaji wananchi kiuchumi kwa kutoa mikopo kupitia benki au SACCOS - Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, ijulikane kwamba Benki sio rafiki wa maskini ipo kutegeneza faida *to the Maximu*m! Ushauri, wangu ni kama ifuatavyo:-

(1) Serikali itoe pesa za mitaji kwa *SACCOS* au vikundi badala ya Benki – *SACCOS* – Mjasiriamali. Benki itatoa riba – SACCOS, itaweka ripa, hivyo mjasiriamali atatozwa riba mara mbili;

(2) Wajasiriamali wawezeshwe hata kimafunzo *(social capital)* ili kwajengea kujiamini na kuthubutu. Tengeni fedha za mafunzo;

(3) Balozi zote zina *Women Desk* na kuna pesa za mitaji kwa wanawake. Tuombe pesa hizo ambazo ni *grants* zitunishe *SACCOS* za wanawake ili zikopeshwe kwa riba ya 5% - 7%;

(4) *Exchange Programs,* ni elimu itakayofungua macho ya wajasiriamali ili kufanya kwa bidii. *Study Tours* nchini hata nchi jirani ni muhimu; na

(5) Tuwajengee uwezo, tuwaonyeshe *opportunities* kwa mfano *AGOA Programs,* uwezekano wa kila Mtanzania kuwa tajiri, upo.

C. UTALII - Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania tuna vivutio vingi vya kujivunia, tuna Mlima Kilimanjaro, Maziwa makubwa, Mito ya ajabu, Mbuga za Wanyama nyingi, chemchem zinazotoa Maji ya Moto na kadhalika, kwa nini hatupati watalii wengi? Nashauri tufanye yafuatayo:-

1. Tujitangaze vya kutosha;
2. Tuwe na Mawakala Ulaya na Marekani;
3. Kuboresha hoteli, vyoo na usalama wetu; na

4. Hoteli zetu ziwe *lively* kwa kuwa na vikundi vya ngoma na kadhalika.

**MHE. MWANTUMU S.B. MAHIZA:** Naipongeza hotuba nzuri ambayo kwa hakika imeonesha mafanikio makubwa . Naomba kuchangia yafuatayo:-

Naomba sana askari wa jiji la Dar es Salaam wasitumike kupokonya mali za wafanyabiashara wadogowadogo na kuzichukua wao na kuzigawana kitendo chao hicho ni dhuluma hata kama wafanyabiashara hao wamekosa kwanini wasiruhusiwe kuzikomba biashara zao? Aidha, askari hao watumie zaidi kulinda amani na kuhakikisha biashara hazifanyiki holela.

Kinamamama/wafagiaji wa barabara katika Jiji la DSM ndicho chanzo cha kuziba kwa mifereji kwani wanapofagia hsukumia michanga ndani ya mifereji na hivyo kusabisha kuziba, ushahidi mkubwa upo hawana usismamizi na hivyo hufanya wapendavyo.

Nakerwa sana na utaratibu wa kuweka vibanda vya biashara katika maeneo ya shule ndani ya jiji la DSM- maduka na biashara zinazofanywa huko si salama na kubwa ziko taarifa za uhakika wa kiusalama kwamba baadhi ya vibanda huusa dawa za kulevya, bangi na kuberi. Je kuna ulazima gani wa biashara hizo kufanyika katika maeneo hayo? Aidha, matendo ya kudhalilisha wanafunzi wadogo hufanyika katika maeneo hayo, nashauri agizo lilitoka Ofisi ya Rais Utawala Bora litekelezwe haraka iwezekanavyo.

Walimu wengi kubaki katika orodha ndefu ya kungojea hali yakuwa maeneo mengine haya walimu katika Manisaa ya Jiji la DSM. Nashauri Maafisa Elimu na Wakurugenzi wa Manispaa hizo za Ilala, Temeke na Kinondoni wawapangie kazi walimu kwa uwiano mzuri badala ya kuwalundika katikati ya jiji tu.

Vyombo vya usafiri kwa Wakuu wa Idara katika Wilaya mpya. Karibu Wilaya nyingi mpya kama vile Mkinga, Bahi, Nanyumbu n.k. hazina kabisa vyombo vya usafiri kwa Wakuu wa Idara - naomba katika vipaumbele nao wafikiriwe.

Kivuko na Gati kwa maeneo ya Delta – Rufiji na Mkuranga. Naomba sana Serikali tuone huruma kwa wananchi wa maeneo hayo ni hatari sana kwa maisha ya wananchi na ndio maana hata walimu na watumishi wengine hawako tayari kwenda kufanya kazi huko. Hivi ni lini tutaona umuhimu wa kuwapatia kivuko – Boti wananchi wa maeneo hayo?

Wakandarasi wasio na uwezo wa kufanya kazi za barabara za Vijijini wanalipwa fedha kwa kuweka vifusi vya tope kwa fedha nyingi sana na mara mvua zikianza barabara hazipitiki mifani ni Kilindi – Handeni – Korogwe na Chanika – MKata. Anomba umakini uwepo katika zabuni hizo.

Handeni ni Wilaya yenye kupata mateso makubwa ya maji naomba ukamkini uwepo na pia wananchi wapatiwe utaalam wakuvuna maji ya mvua kama inavyofanyika katika Halmashauri zingine. Naunga mkono hoja.

**MHE. HAJI JUMA SEREWEJI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kuniruhusu kuchangia kwa maandishi hotuba ya Bajeti ya Waziri Mkuu. Kabla sijaanza kuchangia naomba kuunga kwa mkono asilimia mia moja.

Mheshimiwa Spika, kwa kweli naipongeza hotuba hii kwa jinsi iliyo nzuri na ambayo imeelezea kwa uwazi kabisa yale yote ambayo yatafanikiwa kwenye mikoa.

Mheshimiwa Spika, mimi nitazungumzia kuhusu fedha ambazo za miradi kwa wananchi wenye biashara ndogo ndogo.

Mheshimiwa Spika, mfuko huu unaojulikana kwa jila la Fedha za Mheshimiwa Kikwete, kwa upande wa Zanzibar bado kabisa wananchi hawajfaidika nao hata kidogo kwa sababu nathubutu kusema fedha hizi hazijatoka hata mmoja, sijui fedha hizi zitaanza kupelekwa lini kwa wananchi hao.

Kwa nafsi yangu napongeza kwa dhati kabisa Serikali kusikia kilio cha Waheshimiwa Wabunge kuhusu Madiwani kupatiwa posho katika Bajeti hii ya 2008/2009. kwa sababu Madiwani ni kiungo kikubwa sana wa kufanikisha na kufuatilia kazi kwenye Majimbo na Kata. Nategemea na Zanzibar wafuate nyayo hizo.

Mheshimiwa Spika, kutokana na magari kuendeshwa ubabe na kusababisha msongamano wakati mwngine si wa lazima. Mheshimiwa Waziri Mkuu ameataka askari wa usalama barabarani wasimamie kikamilifu sheria hii. Ushauri wangu mimi naomba Serikali iwapatie vitendea kazi askari wa usalama barabarani kama vile pikipiki ili askari hao waweze kufanya doria kwenye barabara hizo. Kwani utakuta askari wanakaa sehemu za keepleft tu na sehemu nyingine za barabara hazina doria yoyote. Kwa hivyo madereva huwa hawan wasiwasi wa kufanya huo ubabe wao.

Kuhusu elimu Mheshimiwa Spika, naipongeza Serikali kwa kuipa kibaumbele elimu.

Mwisho kabisa nazidi kuunga mkono hotuba hii asilimia mia kwa mia.

**MHE. MGENI JADI KADIKA:** Mheshimiwa Spika, kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuweza kunipa nguvu kuweza kuchangia hoja hii.

Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza Waziri Mkuu kwa hotuba yake nzuri na yenye kuwapa faraja watanzania, iwapo yatatekelezwa.

Mheshimiwa Spika, kilimo ndiyo uti wa mgongo wa Tanzania lakini kilimo cha jembe la mkono tayari kimepitwa na wakati lazima tubadilike.

Mheshimiwa Spika, tunahitaji sasa ifunguliwe benki ya wakulima ili waweze kupata mikopo waweze kukopeshwa trekta wapate madawa, mbolea wapate wataalam ili wapate kufahamu ukulima wa kisasa wapate mazao ya kutosha na wapate kuhifadhi fedha zao kwa kujiwekea akiba.

Mheshimiwa Spika, Elimu ni ufunguo wa maisha kila binadamu anahitaji elimu na kweli Serikali inafaa kupongezwa kwa kuliona hilo kutoa kipaumbele kwenye bajeti na mengineyo kwa kweli shule zimejengwa nyingi sana Msingi, na sekondari lakini lakusikitisha shule hizo hazina vikalio, na hazina walimu wa kutosha hasa walimu wa somo la Sayansi. Kwa hiyo, ni tatizo. Vile vile shule za Vijijini kuna upungufu wa nyumba za walimu, waalimu wengi wanabakia mijini kwa tatizo hilo.

Mheshimiwa Spika, vile vile wale walimu wapya wanaoajiriwa wapate mishahara yao mapema wasicheleweshwe au wakapata usumbufu wakiwa wako Wilaya hii wakambiwa mshahara wako uko Wilaya nyingine mpaka inafika miezi 6 hajapata maslahi yake. Na maslahi yao walimu waongezwe.

Mheshimiwa Spika, haki za binadamu kwa kweli nimeguswa na suala la mtoto yatima. Huko Mbeya hivi karibuni, mtoto baada ya kufiwa na wazazi wake alichukuliwa na jamaa zake wa karibu lakini la kusikitisha mtoto aliuza kwa mfanyabiashara wa hoteli kwa Sh. Milioni 5 ili akachunwe ngozi ati kwa kupata utajiri kwa njia ya ushirikina, kwa bahati wasamaria wema wakapeleka taarifa Polisi na mtuhumiwa akatiwa mbaroni. Nataka kujua mtoto huyu baada ya kupata mtihani huo alirudishwa kwa jamaa zao au Serikali imemhifadhi kwa kumpa malezi ya matumaini ili aishi kama watoto wengine au yuko wapi?

Mheshimiwa Spika, baada ya mchango wangu namtakia Waziri Mkuu afya njema na maisha marefu na amkinge kwa kila shari lisimfike. Mungu Ibariki Tanzania.

**MHE. ERNEST GAKEYA MABINA:** Mheshimiwa Spika, napenda kutoa pongezi kubwa kwa uteuzi wa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuweze kutuchagulia kiongozi mahiri naye si mwingine bali ni Waziri Mkuu aliyeweza kuwasilisha Bajeti yake mbele ya Bunge hili kwa umakini mkubwa ambao inaungwa mkono na pande zote mbili zilizoko ndani ya ukumbi huu.

Mheshimiwa Spika, nalazimika kuwapa pia hongera kwa Waziri wa TAMISEMI Mheshimiwa Celina Kombani (Mb) pamoja na Naibu Waziri Mheshimiwa Aggrey

Mwanri (Mb) bila kuwasahau Katibu Mkuu, Wakurugenzi na Wafanyakazi wote wa TAMISEMI kwa kazi kubwa wanayoifanya.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa nishukuru kwa maelezo mazuri haya yanaweza yakasaidia sehemu zingine lakini Wilaya ya Geita ina matatizo mengi ningeomba haya yafuatayo yafanyiwe kazi.:-

Mji wa Geita hauna maji salama kwa matumizi ya binadamu pamoja na mifugo, hivyo tunaomba Serikali iangalie katika kutatua tatizo hili kubwa la maji katika mji huu.

Kutokana na jiografia ilivyokuwa Wilaya ya Geita imekaa vibaya sana hiyo tuliomba kwamba igawanywe ili iwe na Wilaya mbili pia kuwe na utaratibu wa kuongeza Majimbo hii inatokana na kuongezeka kwa idadi kubwa ya watu.

Uandikishaji wa Vijiji na Kata Geita ipewe Kipaumbele ili kuweza kurahisisha kuleta utawala bora kwa uongozi wa Vijiji na Kata ambazo ni kubwa mno.

Hali ya usalama ni ndogo mno, kumekuwa na matukio ya kuvamiwa walimu kiasi ambacho kunasababisha walimu wengi kuhama kwenye shule na kudidimiza elimu Wilayani Geita.Tunaomba:-

- Polisi Geita wapewe vitendea kazi kama magari kama matano (5) pikipiki (20) ishirini na hata baiskeli.

- Uhamisho ufanyike kwa askari waliokaa muda mrefu kwa kuwa kumekuwa na mahusiano makubwa kati Askari na Majambazi.

- Tuongezewe askari wengi kulingana na idadi ya watu.

(1) Kuwe na utaratibu wa kuwanyang'anya wachimbaji wakubwa ambao wamepata Secial Mining Licence na wamepewa tena *Properting Mining Licence* basi maeneo yote yaliyonayo ya *Prospecting Mining licence* wapewe wachimbaji wadogo wadogo.

(2) Serikali ifanye mazungumzo na Serikali ya Kenya na Uganda kuweza kulinda Ziwa Victoria ambako sasa limevamiwa na Wawekezaji wakubwa ambao wananunua samaki usiku na mchana. Serikali hizi zifanye utaratibu wa kuwa na vyombo maalum au misimu ya uvuvi kuliko kuacha uvuvi holela ambao unafanyika hivi sasa.

**MHE. JUMA SAID OMAR:** Mheshimiwa Spika, kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia uzima na afya na hivyo kuweza kushiriki katika kikao cha leo.

Mheshimiwa Spika, napenda kukupongeza wewe, Naibu Spika, Wenyeviti wa Bunge pamoja na viongozi wa kambi ya upinzani kwa kutuongoza vizuri katika mambo mbalimbali kuhusiana na shughuli zetu za Bunge.

Mheshimiwa Spika, usafiri wa majini umekuwa ukisababisha vifo vya wananchi wengi kila mwaka katika maeneo mbalimbali kutokana na kukosekana kwa vyombo vya uokoaji. Je, Serikali haioni wakati umefika sasa kuwa na *speed boat* katika bandari zetu kuu na angalau helkopta moja vikiwa vimekaa *standby* ili ikitokea ajali ya chombo kuzama viweze kuokoa maisha ya wananchi wetu.

Mheshimiwa Spika, mwafaka baina ya CCM na CUF unahitaji kupatiwa ufumbuzi wa kudumu katika muda huu tulionao ili usije ukaleta maafa makubwa iwapo utaachwa hivi hivi bila ya kupatiwa ufumbuzi. Ni matarajio yetu kwamba hatua za dharura zitachukuliwa ili kuinusuru Zanzibar isijeikaingia katika balaa litakalohitaji gharama kubwa hasa ikizingatiwa na ahadi nyingine iliyotolewa na Mheshimiwa Rais Jakaya Kikwete aliyoitoa hivi karibuni alipohojiwa huko Uingereza.

Mheshimiwa Spika, Muungano wetu ni wa muda mrefu, lakini kuna kero mbalimbali ambazo hadi sasa bado hazijapatiwa ufumbuzi. Je, Serikali haioni kwamba kuna haja ya kuchukua hatua za muda mfupi kumaliza kero hizo badala ya utaratibu wa hivi sasa ambao utachukua muda mrefu kumaliza kero hizo huku zikiendelea kuathiri pande mbili za Muungano.

Mheshimwa Spika, Tume za Uchaguzi za Zanzibar na Muungano zinahitaji kufanyiwa marekebisho ili zisionekane kukandamiza haki za wananchi kushiri katika chaguzi zilizo huru na za haki. Hii ni kutokana na matatizo mbalimbali yanayojitokeza wakati wa uandikishaji katika daftari la kudumu la wapiga kura pamoja na uchaguzi wenyewe.

Mheshimiwa Spika, nchi yetu imeingia katika Mageuzi ya Kisiasa, Kiuchumi na Kijamii. Pia hivi sasa ni wakati wa ukweli na uwazi*, (Truth and Transparency).* Hivyo wakati umefika sasa kuwa na katiba mpya inayoendana na wakati yenye kubadilika *(flexible constatiction)* badala ya kuendelea na katiba ya hivi sasa ya 1977 ambayo haibadiliki *(rigid constitution)* ili matatizo mbalimbali ya kikatiba na mengineyo yanayoikabili nchi yetu yaweze kuondoka.

**MHE. PAUL P. KIMITI:** Mheshimiwa Spika, kwanza ya yote naomba nitumie nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Mizengo Peter Pinda kuteuliwa na Mheshimiwa Jakaya M. Kikwete (Rais wetu) kuwa Waziri Mkuu. Pia nampongeza kwa jinsi alivyowasilisha hoja yake kwa ufasaha na umakini wa hali ya juu. Nawapongeza Wasaidizi wake wote Wakuu na Watumishi kwa kuiandaa vizuri hotuba hii.

Mheshimiwa Spika, nimeona niyaweke haya yafuatayo kwa maandishi kwa kuwa mengine katika utawala bora huwezi kuyasema hadharani. Namwomba Mheshimiwa Waziri Mkuu ayazingatie haya yafuatayo:

Mheshimiwa Spika, Manispaa ya Sumbawanga kwa bahati mbaya ilianza na Watendaji wenye uwezo, uzoefu na hata taaluma hafifu kulingana na majukumu ya Manispaa yenyewe.

Tukianza na Mkurugenzi Mwenyewe, alikuja moja kwa moja toka Wilayani ambako alikuwa akifanya kazi kama Afisa Ushirika. Hakuwahi kuwa hata Mkurugenzi wa ngazi nyingine yoyote ya Wilaya. Sijui vigezo gani vilitumika kumteua.

Mheshimiwa Spika, tangu afike, Manispaa imekumbwa katika tatizo la kukosa fedha za ruzuku ya Maendeoeo kwa kukosa HATI SAFI mfululizo kwa zaidi ya miaka mitatu. Hasara hii ilitokana na ubovu wa usimamizi wa Wakuu wake husika.

Pili Mheshimiwa Spika, kwa kipindi chote amekuwa akipambana na wakuu wake wa Idara pamoja na Madiwani ambao kwa vikao vingi vya Kanseli, kumekuwa na maandalizi hafifu ya vikao hivyo na kufanya viwe vinarudishwa na kuahirishwa.

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla katika mazingira kama hayo, hata Mkuu wa Mkoa Rukwa analielewa suala hili. Hivi karibuni nilipata nafasi ya kuzungumza naye mwenyewe (Mkurugenzi wa manispaa) na kweli mwenyewe amekiri kuwa hali ya mazingira ya kufanya kazi katika Manispaa hii (siyo *conducive at all),* hali hii inaonyesha kuwa naye amesalimu amri - na siyo vizuri kuendelea naye katika hali hii. Mambo yanaweze kuwa mabaya. Naomba Waziri Mkuu usaidie kurekebisha hali hii.

Pamoja na hilo, Mkurugenzi huyu kwa sasa yuko masomoni, *Mzumbe University,* jambo ambalo ungozi unaona kuwa fedha ndogo zinazoletwa kwa maendeleo, zinatumaika pia kwa ngarama nyingine za masomo hayo.

Mheshimiwa Spika, jambo jingine ambalo ninamwomba Mheshimiwa Waziri Mkuu ni kuchukua hatua madhubuti kuanzia sasa wakati bei ya mafuta imepanda:-

Awatake Wakurugenzi wasisafiri bila kibali cha Wakuu wa Mikoa.

Misafara ya kutembelea miradi wakati wa viongozi wakuu wanapotembelea mikoa iratibiwe na misururu isiwe mirefu sana. Waende wanaohusika tu na wapakiane kwenye magari machache. Wakati wa kuendesha, magari mengi kwa jambo la kawaida uachwe mara moja.

Waheshimiwa Wabunge wawekwe kwenye orodha ya Wakuu wa Wilaya na Wakurgenzi – pamoja ili kujenga umoja kwenye uongozi wa Wilaya, wakati wa ziara za viongozi.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa mwaka huu kuna dalili za upungufu wa chakula na kwa kuwa Mkoa wa Rukwa karibu unanza kuvuna mahindi, nashauri:-

Tani 19,00 za mahindi zilizomo kwenya maghala ya *SGR* Sumbawanga yaanze kusafirishwa kwenda sehemu zenye upungufu ili kutoa nafasi kwa mahindi ya mwaka huu kununuliwa.

Ununuzi wa mahindi uanze Sumbawanga ili kabla ya mvua kunyesha iwe kazi hiyo imekamilika.

Mwisho Mheshimiwa Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri Mkuu afuatilie kwa karibu sana juu ya fedha za MCC ili masharti waliyoyatoa yasikwamishe kazi ya ujenzi wa barabara mwaka huu wa fedha, angalau tuone tenda zimetangazwa kwa sehemu ndogo ndogo za km 60/60/60/60 – ili barabara kwa kufikia 2010 tujivunie hatua kubwa ya kujipatia sifa za utekelezaji ILANI ya uchaguzi. Naunga mkono hoja hii kwa asilimia zote.

**MHE. MWAJUMA HASAN KHAMIS:** Mheshimiwa Spika, ni vema nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia kuwa hai na ni mzima.

Mheshimiwa Spika, pia nampongeza Waziri Mkuu kwa hotuba yake ilio na sura ya MAISHA BORA KWA KILA MTANZANIA. Baada ya maelezo yangu hayo, sasa naomba nitoe mchango katika hotuba hii. Sasa ni kuhusu mahakama ya Kadhi katika nchi yetu.

Kwa kuwa muda mrefu sana, Waislamu hapa nchini wanadai kuwepo Mahakama hiyo. Mtazamo wa wengi wamegundua Serikali suala wanalipiga danadana, jambo ambalo linatoa sura mbaya kwa waislamu hapa nchini. Ni vema Serikali ielewe kwamba kuna baadhi ya haki za kesi hukumu yake ni lazima ihukumiwe kidini.

Kwa mfano NDOA NA MIRATHI. Makosa haya yanapotokea hukumu yake ni lazima yapatikane katika vitabu vya kidini. Je, ni lini Serikali itaamua kuanzisha mahakama hiyo ili waislamu wapate haki zao?

Mheshimiwa Spika, kuhusu ubomoaji holela wa majumba Watanzania haki yao ya kuishi imo ndani ya nchi yao, mara nyingi tunaona kuvamiwa wananchi hao na Serikali kubomolewa nyumba zao. Katika hili nani mkosa. Serikali ama wananchi. Mwananchi ameanza mpaka amemaliza Serikali ilikuwepo wapi hata eneo likajengwa lote na kuwa Kijiji

Kuhusu Madawa ya Kulevya na kwa kuwa, kwa nguvu kazi ndio waathirika wakubwa katika nchi yetu, ni vema Serikali iandae mpango mahususi kuzuia Madawa haya.

Baada ya maelezo yangu hayo nasema ahsante.

**MHE. KHADIJA SALUM ALLY AL-QASSMY:** Mheshimiwa Spika, kwanza sina budi kushukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia nikawa mzima na kuweza kuchangia hoja hii ilioko mbele yetu ya Waziri Mkuu. Mheshimiwa Spika, vile vile

napenda kumpongeza Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani kwa hotuba yake nzuri ambayo kaitoa kwa ufasaha mkubwa. Mheshimiwa Spika, nachukua nafasi hii kumpongeza Waziri Mkuu kwa hotuba yake ambayo kwa mara ya kwanza imemgusa mwananchi, naomba yasiwe maeneo tu kwenye vitabu iwe inatekelezwa.

Kwanza napenda kuchangia kuhusu Jiji la Dar es Salaam. Jiji hili ni jicho la nchi yetu ambalo limejaa majengo makubwa mazuri na marefu, lakini cha kusikitisha barabara hasa *Feeder roads* ni mbovu sana na hazina hadhi ya yale majengo. Mheshimiwa Spika, namwomba Waziri Mkuu watenge pesa za kutosha ili kuliondosha jiji hilo na aibu. Jiji hilo lina adha ya kila aina ya taka, maji safi, mvua ikinyesha ni adha na hata msongamano wa magari ambalo kwa maoni yangu utatuzi wake ni kujenga *"flying over"* tu.

Mheshimiwa Spika, pili napenda kuchangia kuhusu suala la Mahakama ya Kadhi naomba Serikali jambo hili walishughulikie kwa kina ili liweze kufanikisha kwa sababu waislamu wanasheria zao ambazo wanahitaji chombo hicho ili kiweze kuwasimamia.

Mheshimiwa Spika, jambo jingine ambalo napenda kulichangia ni suala la *SACCOS* kwa kujibu hotuba ya Waziri Mkuu amesema kwamba Zanzibar kumepelekwa Sh. Milioni 500 kwa ajili ya wananchi wa Zanzibar Je! Pesa hizo zimepelekwa lini? Maana hatujaona hata harufu ya pesa hizo. Bado Zanzibar kila kitu kinafanywa kisiasa. Je! Kuna taratibu gani za kufanya ili wananchi wote wahakikishe kama wanaweze kupata?

Mheshimiwaa Spika, jambo jingine ni suala la madawa ya kulevya. Bado vijana wengi wanaathirika na tunamwomba Waziri Mkuu atueleze Serikali imechukua hatua gani ya makusudi ili kuhakikisha wanathibiti hali hiyo?

Mheshimiwa Spika, jambo la mwisho ni kuhusu bomoabomoa. Serikali haioni kama inachezea amani katika nchi kutokana na kuwaacha wananchi wajenge mpaka wamalize na watu wanaishi kwa miaka halafu wanakuja kuwabomolea. Je, hawaoni kama hiyo wanafanya si haki na kusababisha vurugu? Je! Serikali inakuwapo wapi watu hao wanapojenga?

Mheshimiwa Spika, jambo jingine ni kuhusu Mgambo ambao wengi wananyanyasa wananchi na kuwapiga na kuwanyang'anya mali zao Je! Serikali na hili wanalichukuliaje? Wananchi wa kawaida watafanyaje?

Mheshimiwa Spika, nashukuru Ahsante.

**MHE. FATMA OTHMANI ALI:** Kwanza napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa hotuba nzuri yenye uelewa kwa wananchi wa Tanzania pili naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Kwa upande wa Muungano wetu naomba jitihada zifanyike kwa kunasua hizi kero katika Serikali yetu ya Muungano hasa kwenye *TRA* hili kero la *TRA* kuhusu magari yanayotoka Zanzibar kuja Tanzania Bara bado lina utatanishi mkubwa

ningeomba kikao cha Waziri Mkuu na Waziri Kiongozi kitakapokaa pamoja suala hili lizungumzwe kwa kina kabisa.

Suala la usafiri bado ajali za barabarani zimekuwa zikitisha hasa kila siku unaposikia ajali hizo zinauwa watu 8 chini ya watano ingekuwa vyema haya mabasi ya abiria yanayosababisha ajali zaidi ya mara mbili wanyang'anywe kibali cha kuchukua abiria na dereva huyo anyang'anywe leseni yake. Kuhusu Usalama wa Raia na Mali zao ninalipongeza sana Jeshi la Polisi kwa kupunguza kwa kasi kubwa wimbi la ujambazi.

Lakini bado Jeshi la Polisi lina upungufu wa vitendea kazi hasa kwa upande wa Jeshi hilo huko Zanzibar kwani kuna Vituo vya Polisi ambavyo vipo kwenye maeneo muhimu kama Kituo cha Polisi Mazizini ambacho kipo njiani kuelekea uwanja wa ndege pia kipo kwenye majumba yanayoishi viongizi wetu kituo hicho hakina gari, pikipiki wa *Radio Call.* Wakati hivyo vyote ni vitendaa kazi muhimu.

**MHE. COL. FETEH SAAD MGENI:** Mheshimiwa Spika, kwa heshima kuwa ninaomba kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kuteuliwa kushika Wadhifa huo na *Inshaalla* Mwenyezi Mungu atakusaidia.

Mheshimiwa Spika, naipongeza hutoba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu jinsi ilivyo nzuri na imeguza maeneo yote ya nchi yetu. Aidha ninawapongeza Mawaziri wake pamoja na Watendaji wake wote wa ofisi yake. Ninaomba kuchangia maeneo yafuatayo ambayo Waziri Mkuu ameyaeleza kwa vizuri sana. Bali kwa upande wangu ninayatilia mkazo na kuunga mkono Bajeti hiyo.

Mheshimiwa Spika, saula la Elimu lazima sasa bidii ya hali ya juu ichukuliwe kuanzia Elimu ya Msingi hadi ya Vyuo Vikuu. Aidha Elimu ya Sayansi na Mambo ya Ufundi ichukuliwe bidii zaidi. Mheshimiwa Spika, Tanzania iko njiani katika kujiunga na Afrika Mashariki na baadaye Muungano wa Bara la Afrika, kwa maana hiyo tujiandae vizuri katika soko la ajira.

Mheshimiwa Spika, uchumi, lazima sasa tuimarishe sana miundombinu yetu, kuanzia Barabara, bandari zetu kuu, ambazo ni Tanga, Zanzibar, Dar es Salaam, Mtwara na Mafia tuziangalie sana. Lazima tuimarishe viwanda vyetu vilivyopo na kujenga vingine ili tuwe na uwezo wa ushindani katika soko la Afrika Mashariki, hivi sasa bado soko hilo hatujakuwa na ushindani mzuri. Kwa kweli bado Sekta ya Uvuvi hautjaitumia ipasavyo tunaeneo kubwa la ukanda wa Bahari, ambapo bado hatuja wekeza vizuri ambapo sote tunaamini kwamba kuna utajiri mkubwa baharini na katika maziwa yetu makuu.

Mheshimiwa Spika, katika ulimwengu wa leo katika nchi nyingi katika Utalii inaonekana wanafaidika katika Sekta hiyo. Tanzania ina utajiri sana wa mambo ya Kale, maumbile mbalimbali ya kiajabu kama vile milima, mbuga za wanyama mbalimbali, Sokwe wa Ajabu huko Kigoma, Historia za Bagamoyo, Soko la Watumwa, Historia za Kisultani na Maorofa kongwe ya ajabu huko Zanzibar na mambo kadhaa wa kadhaa.

Mheshimiwa, Spika, ninashauri sana tutumie kwa umahiri mzuri fursa hii ya biashara ya Utalii. Nina heshima kuwasilisha mchango wangu huu mdogo ambao Mheshimiwa Waziri Mkuu amezungumza katika hotuba yake, mimi ninautilia mkazo na kuunga mkono.

Mheshimiwa Spika, kwa niaba yangu na wananchi wa Jimbo langu la Bubwini tunaunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa asilimia mia moja.

**MHE. AMEIR ALI AMEIR:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa ninamshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia uzima na kuniwezesha kuchangia hotuba hii ya Waziri Mkuu. Ninawashukuru Wapiga kura wangu wa Jimbo la Fuoni Zanzibar kwa kuniamini na kuendelea kuniunga mkono nami nawaahidi niko tayari kushirikiana nao.

Mheshimiwa Spika, nimpongeze Mtoaji wa Hotuba hii Mheshimiwa Waziri Mkuu pamoja na Watendaji wote walioandaa hotuba hii, hotuba ambayo ni utekelezaji wa Ilani ya Chama Tawala CCM.

Mheshimiwa Spika, Bajeti ya Ofisi zilizo chini ya Waziri Mkuu ni nzuri naikubali hasa kwa ilivyo jali matakwa ya Watanzania wa ngazi zote.

Mheshimiwa Spika, nina mchango mdogo tu hasa kwa kuwa sikuona likizungumziwa nalo ni Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo *(CDF)*. Fedha hizi ni muhimu sana na kilio cha muda mrefu kwa Waheshimiwa Wabunge kupatiwa mfuko huu. Lakini bado kitendawili sijui Serikali imekwamia wapi, wakati Wabunge waliambiwa muswada utaletwa Bungeni kujadili mfuko huo. Mheshimiwa Spika, kutekelezeka kwa mfuko huu ndio utakaoleta Maendeleo ya uhakika na kutekelezeka ahadi za viongozi wa Kitaifa, na za Mbunge katika Jimbo husika kuliko kusubiri Fedha za Halmashauri kwa sababu Halmashauri ina mambo mengi na haihudumii Jimbo moja. Serikali yetu iliyoko madarakani ni ya CCM, Wabunge wengi ni CCM na hali hii itaendelea kwa vipindi vyote Serikali hii kuwa ya CCM hakuna haja ya Serikali kuwa na kigugumizi kutoa fedha kwa Maendeleo ya Jimbo. Wale wanaozuia lazima Serikali ijuwe wanakataa kwa misingi gani na kwanini. Kwa maoni yangu hawa wanaopinga hawakitakii mema Chama chetu na kuturudisha nyuma katika kuwaletea maendeleo ya haraka wananchi wetu wanataka siku zote tuwe nyuma na kuendelea kuwa tegemezi.

Mheshimiwa Spika, kutolewa mfuko huu kwa Wabunge Bajeti zetu za mbele, zitatuwezesha kupunguza chini hii kuwa na bajeti tegemezi. Kwa hiyo, namwomba Waziri Mkuu ambaye ni msimamizi Mkuu wa Serikali akae na Kamati zake kwa makusudi ya kujadili suala hili ili fedha zipatikane kwa kipindi hicho cha Bajeti. Tanzania itajengwa na Watanzania wenyewe.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

**MHE. JANETH MAURICE MASSABURI:** Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa hotuba nzuri yenye kukidhi matarajio na

matumaini ya watanzania wengi. Natoa pongezi kwa timu nzima iliyoshiriki kuandaa bajeti hii.

Mheshimiwa Spika, naomba nitoe maoni yangu machache kama ifuatavyo:-

*Computerized Magnetic Number Plates for Transit Vehicles*. Mfumo huu utasaidia Serikali kupata chanzo kipya cha mapato na pia kitasaidia kudhibiti upotevu wa mapato hasa kwa magari ya mafuta ambayo husingizia kana kwamba yako *On Transit* na kiwa kuishia mikoa ya humu nchini.

Kwa mfano, inakadiriwa magari 4000 huvuka katika mipaka yetu *(Transit Vehicles)* kila mwezi. Kwa kukadiria kwa kiwango cha chini *TRA* inaweza ikatoza (Dola 25 kwa *Transit number plate* na Dola 15 kwa *Transit card)*. Kwa mwaka *TRA* itaweza kukusanya kiasi cha dola 1.920,000.00 kiasi hiki kitaweza kusaidia kuchochea Maendeleo ya nchi hii.

Mfumo *Carbon Tax* umelenga kupata mapato na pia utasaidia kuhifadhi mazingira kwa kila Halmashauri hapa nchini. Maeneo yatakayohusishwa na utoaji wa hewa chafu ni kama ifuatavyo:-

- magari na vyombo vya moto;
- mitambo mbalimbali;
- mashine;
- viwanda (vikubwa na vidogo);
- magereji;
- petroli stations;
- usafiri wa anga;
- usafiri wa majini (meli, boti na kadhalika)
- treni na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, chanzo hiki cha mapato si kigeni hapa nchini na hasa katika nchi za Kiafrika. Kinatumika maeneo kama Zambia, Afrika Kusini, Zimbambwe , *DRC*, Dubai na India.

Mheshimiwa Spika, kwa kutoza (magari pekee) kiwango cha chini kabisa, Serikali itaweze kupata kiasi cha sh. 700 bilioni kwa mwaka. Kiasi ambacho kitaweza kukidhi Bajeti nzima ya wizara inayohusika na uhifadhi wa mazingira, kiasi kingine kitakwenda kusaidia Sekta nyingine kama Miundombinu katika Kilimo Vijijini.

Kuhusiana na ajisra kwa vijana, naomba Serikali itenge maeneo maalum kwa vijana wa Mkoa wa Dar es Salaam kwa uzalishaji mali na kuwapatia mikopo ya vifaa kama mashine za kutengenezea chaki na majiko yanayohifadhi mazingira kwa kila Wilaya. Wilaya za Ilala, Temeke na Kinondoni ili vijana hawa waweze kutoa mchango wao kwa taifa. Vijana wengi wanahitaji mafunzo hayo na soko la bidhaa hizo lipo, tatizo ni ujuzi, Vifaa, eneo. Naiomba sana Serikali iwasaidie vijana wa Mkoa wa Dar es Salaam na kuwatambua vijana wa *camps* kama ni *scheme* ya nguvu kazi ya taifa isiyotumika. Mimi kama Mbunge wa Mkoa huo niko tayari wakati wowote kushirikiana

na Serikali kuwasaidia vijana hao. Nakumbusha tena mahitaji muhimu kwa vijana (faida itakayopatikana).

1. Mafunzo (ya muda wa siku 5 tu) *TIRDO/SIDO;*
2. Vifaa (Vitendea kazi);
3. Eneo la kufanyia kazi kwa kila Wilaya (3);
4. Soko la chaki ni shule zetu (Halmashauri);
5. Faida - Ajira itapatikana;
   - wazururaji watapungua;
   - umaskini utapungua;
   - uchumi wa wananchi utapanda;

Kwa hayo machache ninakushukuru sana na ninaunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. BAHATI ALI ABEID:** Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu pamoja na Watendaji alioshirikiana nao kuandaa hotuba hii nzuri yenye mambo ya Maendeleo kwa Watanzania.

Mheshimiwa Spika, kuhusu uvuvi. Wavuvi wanamchango mkubwa wa ukuaji wa uchumi kwa taifa letu kwani hutoa ajira kwa vijana wetu wa kike na wa kiume. Kwa hiyo, Serikali imelina hilo na ndio maana serikali ikauleta mradi wa uhifadhi mazingira ya bahari ambao ni MASEMPU. Lakini mradi huu umeanza kwa majaribio kwa baadhi ya Wilaya za Tanzania Bara na Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, mradi huu una wataalam na una fedha nyingi na una ofisi zake na unafanya kazi. Ni kwanini mradi huu haumalizi mambo yake wenyewe mpaka uishie kwenye *TASAF* na wakati huo mradi huu uko kwenye majaribio kwa baadhi ya Wilaya.

Mheshimiwa Spika, wananchi ambao ni wavuvi walidhani mradi huu ukiwa unajitegemea peke yake utakuwa unawanufaisha wavuvi kwa haraka zaidi kuliko ilivyo sasa.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa mradi huu umeanza kwa majaribio basi iwaeleze wananchi mafanikio ya mradi huu kuwa wamefaidika wavuvi wengi au la.

Mheshimiwa Spika, sasa ni kuhusu Ulinzi na Usalama. Napenda kulipongeza Jeshi la Wananchi na Askari wetu wa Vikosi vyote kwa kufanya kazi kwa moyo na kwa uzalendo mkubwa ndani ya nchi na nje ya nchi inapotakiwa kufanya ulinzi.

Mheshimiwa Spika, wenzetu hawa wanafanya kazi kubwa ya kulinda raia na mali zao usiku na mchana. Askari wetu hawa kama Polisi ni kidogo sana na inwabidi kufanya kazi kubwa bila ya kuwa na muda mbadala wa kufanya shughuli nyingine za kuwaletea kipato zaidi ambacho kingeweza kuwasaidia kupambana na maisha.

Mheshimiwa Spika, mcheza kwao hutunzwa, sasa wakati umefika kwa makusudi kuangaliwa kwa makini na huruma ndugu zetu hawa waongezewe mishahara hasa askari wangazi ya chini ili na wao waweze kukabiliana na maisha ya kila siku.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. Ahsante sana.

**MHE. BENITO W. MALANGALILA:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa napenda kutoa maoni yangu kuwa naunga mkono hoja ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, pia, napenda nianze mchango wangu kwa kueleza uchungu mkubwa uliomo moyoni mwangu kuhusu Vijiji vya Kihanga na Mninga hautopitiwa umeme wakati umeme umepita juu ya nyumba zao kwa zaidi ya mwaka sasa, huku sisi pia ikikumbukwa kuwa Kijiji cha Kihange, Kwepalogwe na Mninga na Kijiji cha Kihanga ndicho Kijiji kilichotoa ardhi kwa mwekezaji ili azalishe nguzo za umeme ambazo shirika la ugavi wa umeme *TANESCO* linaumiliki toka kwa huyo mwekezaji, ni jambo la kusikitisha zaidi kuwa wakati mwekezaji huyo akivutiwa umeme wananchi hao waliishia tu kufanya vibarua vya kuchimba mashimo na kubeba nguzo za kusimika nguzo wakati wao wenyewe hawana umeme.

Pia ikumbukwe kuwa ni jambo lililowazi kuwa vijini hivi viwili ni vikubwa na vina nyumba nyingi nzuri na uchumi wa wananchi ni mzuri sana, kwa maoni yangu hii ni nafasi pekee kabisa kwa *TANESCO* kuvuna fedha nyingi na za kutosha.

Pia *TANESCO* wamefanya tathmini ya gharama za usambazaji umeme katika Vijiji hivyo viwili, gharama yake haizidi Sh. Sabini milioni *(70 million only)* hivyo basi kwa kuwa kiasi hiki si kikubwa naamini ofisi yako itaktoa maelekezo kwa Waziri wa Nishati na Madini ili tumalize tatizo hili ambalo mimi kama Mbunge wa eneo hilo nimehangaika na Jimbo hilo kwa zaidi ya mikakati kumi na zaidi hadi sasa.

Mheshimiwa Spika, jingine ni kero kubwa Wilayani Mufindi nihamishie Watendaji wa Kata wasiofaa toka Kata moja kwenda Kata nyingine, mfano yuko mtendaji mmoja jina lake anaitwa Mhelela, ndugu huyu aliajiriwa kama Mtendaji wa Kata, Mbalamaziwa alikoharibu. Akahamishiwa Kasanga, akaharibu, akahamishiwa Malangali napo ameharibu sasa amehamishiwa Kata ya Isilivenu, pale Malangali aliwafunga mahabusu wanawake chumba chenye ukubwa wa mita 2 kwa siku sita (6 days) na miongoni mwa mahabusu hao alikuwepo mama mja mzito, kwa maoni yangu huyu adhabu inayomtosha ni kufukuzwa kazi mara moja.

**MHE. SUSAN LYIMO:** Mheshimiwa Spika, miundombinu ni kielelezo cha maendeleo. Ni jambo la kusikitisha kuona kuwa pamoja na juhudi kubwa ya wakulima kuzalisha mazao mengi lakini wanashindwa kuyafikisha sokoni. Hii imefanya mkulima aone ni nafuu kununua bidhaa kuliko kulima kwani bei ni ndogo kuliko gharama zake.

Pamoja na ujenzi wa barabara za Wilaya bado za Vijiji ni muhimu zaidi ili mazao yafikike lakini tatizo ninaloliona katika barabara ni kutokuwa na vipaumbele au

kutokuwa na uamuzi wa kujenga walau barabara moja na ikakamilika halafu tuhamie kwingine ili walau ionekane. Lakini kusambaza vibarabara nchi nzima ni kutokukamilisha hata moja hivyo kuonekana tunatwanga maji katika kinu. Ni lazima tu-*concentrate* katika barabara moja.

Mheshimiwa baba wa Taifa alisema ili tuendelee tunahitaji mambo manne – watu, Ardhi, siasa safi na uongozi bora. Ardhi ni muhimu sana na moja ya raslimali kuu ya nchi yoyote kwani bila ardhi tusingekuwepo. Ni jambo la kusikitisha kuona mabonde yetu yenye ardhi yenye rutuba yameachwa na kuwa na eneo la mifugo. Hali hii ni mbaya na italeta vurugu sana kati ya wakulima na wafugaji.

Uwekezaji ni muhimu sana katika nchi yetu lakini naamini kituo cha uwekezaji kiwekwe chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu. Kinaweza kuwa na changamoto nyingi kuliko ilivyokuwa katika Wizara ya Mipango na Uchumi.

Mheshimiwa Spika, Utawala Mkoa wa Dar es Salaam una idadi kubwa ya watu wapatao milioni 4. idadi hii kubwa ya watu wa ufinyu wa miundombinu unafanya hali iwe ngumu sana kiutawala. Ni matumaini yangu kuwa kama suala la utawala litashughulikia, basi mambo yatakuwa mazuri. Kwa mfano, sehemu kama Tegeta, Mbagala, Kivukoni kuwa na miji na hivvyo huduma zote za kijamii zikiwemo, Hospitali, masoko, maduka zitaweza kufanya miji hiyo ikue na hivyo kupunguza misongomano isiyo ya lazima.

Kuhusiana na Ujenzi holela, mwaka 2006 aliyekuwa Waziri Mkuu, Mheshimiwa Lowasa aliunda tume ya wataalam wa ujenzi baada ya kuanguka kwa jengo pale Temeke, cha kushangaza hadi leo ripoti hiyo haijaletwa mbele ya Bunge au popote pale. Lakini baya zaidi juzi jengo lingine la ghorofa kumi limeanguka kwa kile kiitwacho ujenzi holela. Je, Serikali ilikuwa na maana gari kuunda tume iliyotumia fedha nyingi na bado matatizo yako pale pale? Tutakuwa na uhakika gani kama halitaanguka tena jingo lingine.

Mawasiliano katika dunia ya sasa ni muhimu sana hasa simu na *internet* ni jambo la kusikitisha kuona nchi kama Kenya ina wateja zaidi ya millioni 14 wakati Tanzania iliyoanza zamani ina wateja milioni 9 tu.

Hii ni kutokana na kodi kubwa na kipato cha wananchi, Serikali kutaka kuongeza gharama ni kuwanyima wananchi habari ambayo ni haki yao ya msingi. Naiomba Ofisi ya Waziri Mkuu ione umuhimu wa kutoongeza kodi toka 7% - 10%.

Pamoja na nyongeza za posho za Madiwani bado hatujafafanuliwa ni kiasi gani kila Diwani atafaidika nacho.

**MHE. YONO STANLEY KEVELA:** Kwanza nampongeza sana kwa dhati pamoja na Watendaji wote. Naipongeza sana *TANROAD* kupitia Waziri Mkuu barabara ya Makete/Njombe kupitia Igagala, Usalule na Kipengere imetengewa fungu Bajeti na Mkandarasi amepatikana tunaomba Serikali itilie mkazo na iwe ya lami.

Pia kuhusu miundombinu naomba Serikali ijenge daraja la Wangutwa/Uhambule Wilaya ya Njombe ni tatizo kubwa sana. Ni muhimu sana kwa uchumi na watoto wa Shule ya Sekondari ya Wanging'ombe na Tom Nyimbo Sekondari.

Daraja la Dulamu/Kanani Kata ya Usuka Wilaya ya Njombe. Daraja hili nalo ni tatizo kubwa sana, wananchi wa Vijiji hivi wanashindwa mawasiliano daraja hili halipitiki kabisa; akina mama na watoto wanateseka sana. Naomba Serikali haya madaraja yapatiwe uvumbuzi wa kudumu.

Barabara za Kata za Saja zimesahaulika, Vijiji kama Idenyimembe, Isimike, Itengelo,Ikulimambo, Uhenga, Igenge. Igomba na Saja; naomba sana barabara na madaraja yajengwe. Naishukuru sana barabara moja ya Makambako kwenda Saja – Halmashauri wameikumbuka kidogo. Napongeza sana.

Maji katika eneo la Jimbo la Njombe Magharibi kuna miradi miwili ya kitaifa moja ni ule wa Maji wa Wanging'ombe uliofadhiliwa na *UNICEF* mwaka 1986. mradi huu unapewa Bajeti ndogo sana. Naomba tupewe fedha walau millioni 300 hii kwa kuanzia,. Napongeza sana Serikali kwa kunisaidia Bajeti kidogo tulipewa na matatizo ya Vijiji vya Lyandebwe na Lyamluki – Kata ya Wanging'ombe Njombe. Naashukuru huu mradi ulikuwa unatumika kisiasa sasa toka ahamishwe yule Mhandisi Kiboko, Tatizo la Maji limepungua sana; wananchi wanafuraha sana. Mhandisi Eng. Adam ni mzuri sana amekomesha tatizo la maji, pamoja na Eng. Mkalimoto wa Wilaya wanafanya kazi nzuri.

Pia nashukuru sana kwa mradi wa Maji wa Tove –Mwiramba Njombe unaofadhiliwa na Serikali ya Italy na Serikali yetu.

Naomba mradi huu wenye thamani ya 3.5 bilioni wa Mwiramba Njombe uko Jimboni kwangu Njombe Magharibi tuwe Bodi ya Maji nzuri yenye wataalam na katika uundaji wa Bodi nishirikishwe kwani nimehamasisha watu wajitolee kuchimba mifereji pamoja na Father Kamilo wa Kanisa Katoliki Kipengere Njombe.

Naomba Serikali pale bandarini na *TRA* wafadhili hawa wasitozwe kodi kabisa kwani wanatoa msaada kwa wananchi wetu.

Serikali ikazie *"A" Level* katika Jimbo langu/Njombe wananchi wanajitolea ujenzi wa Shule za Kitaifa za *"A" level* pala Wanging'ombe, Wanike na Makoga.

**MHE. PINDI HAZARA CHANA:** Mheshimiwa Spika, napongeza kazi nzuri inayofanywa na ofisi hii. Suala la barabara ya Iringa – Dodoma tunaomba itengewe fedha. Mradi wa Mchuchuma na Liganga bado umekuwa ni kitendawili *plus* wananchi wanaoishi maeneo karibia na hapo waliambiwa wasiendeleze wanapaswa kuhama lakini bado hawajalipwa fidia.

Mheshimiwa Spika, naomba katika majibu pia tuzingatie Madiwani posho na usafiri. Naomba kuwasilisha . naunga Mkono hoja. Maisha ya mtanzania yamekuwa Ghali – Gharama:-

Kwa nini Serikali haikemei upandishwaji ovyo wa bei ya Consuer products mfano sukari, bei ya nauli za mabasi ya mikoani na *town buses.* Vyombo vya Habari vipewe *limitation* wanapoandika habari za uongo bila uthibitisho.

Mheshimiwa Spika, naomba katika majibu hayo yaliyoulizwa yazingatiwe.

**MHE. VUAI ABDALLAH KHAMIS:** Mheshimiwa Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri Mkuu na Mawaziri wote wanaomsaidia pamoja na Watendaji wote wa Kamati ya Bunge na Wizara kwa mashirikiano na kuweza kuwasilisha Bajeti nzuri nasema naiunga mkono hoja ipitishwe.

Mheshimiwa Spika, pamoja na uzuri wa Bajeti Mheshimiwa Waziri Mkuu ikipitishwa nakuomba usimamizi wa matumizi kwa Wizara zote na Sekta zake.

Mheshimiwa Spika, kusimamiwa na kwenda kinyume na maadili yake hatua zifuate na pia mwenyewe uwe mwepesi kufuatilia kama ulivyo.Uchumi bila miundombinu mizuri haukuwi. Kwa hiyo, naomba Serikali barabara, Viwanja vya Ndege, Reli, Majengo na kadhalika fedha ya mambo yote hayo izidishwe kwa mara nyingine makisio yake yawe makubwa au utafutwe ufadhili au wahisani.

Mheshimiwa Spika, Afya, kwa kwa wananchi ni muhimu. Bila wananchi kutopata afya. Basi hata kazi zote za Serikali au za binafsi, haziwi. Naomba kuangaliwa Hospitali zote na dawa ziwepo na kukimu maslahi yetu.

Mheshimiwa Spika, raslimali za nchini kwetu. Naomba zitumike za barabani, za nchi kavu na nyingi bado hatujazitafuta wa kujali. Naomba tuzinduke tuweze kuzitumia.

Mheshimiwa Spika, elimu tunajitahidi sana lakini bado elimu ni muhimu na elimu haina mwisho. Kwa hiyo, bado tuongeze juhudi watoto wetu tusomeshe na wataalam tuongeze kuwapo kwa elimu kwa kila fani yote.

Mheshimiwa Spika, Kilimo uti wa mgongo. Juhudi ziwepo kupata matrekta, mbolea, elimu, tuondokane na umaskini na tuongeze ajira. Wazalendo wawezeshwe waweze kuendesha biashara za kileo. Pia *SIDO* shirika hili nalo liwezeshwe kifedha na mambo mengi kwa faida ya nchi.

Mheshimiwa Spika, Tanzania ilikuwa ingine *OIC.* Je bado? Kwa nini, na kuna utaratibu upi mpaka leo? Bado basi tufahamishwe. Na baada ya yote namwomba Mwenyezi Mungu atubariki Tanzania, Wabunge na Wananchi wote tuwe na hekima tuongoze nchi yetu kwa Amani, na kwa niaba ya wananchi wa Magogoni na mimi mwenyewe naunga mkono hoja asilimia zote.

**MHE. MAIDA H. ABDALLAH:** Mheshimiwa Spika, kwanza napenda kuchukua nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu, vile vile kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa hotuba yake nzuri ambayo inaleta matumaini kwa wananchi.

Ikiwa yatafuatiliwa vizuri na kutekelezwa kwa vitendo yale yote yaliyoainishwa na Mheshimiwa Waziri Mkuu ndani ya hotuba yake, basi nchini hakutakuwa na kero za wananchi walio wengi na mwaka 2010 tutaweza kuishinda CCM kwa kura nyingi sana sababu tumeyatekeleza yale yote yaliyo katika Ilani 2005.

Mheshimiwa Spika, Wakulima wengi nchini ardhi wanayolima imechoka hivyo wanahitaji elimu zaidi katika kilimo, ili kiweze kuwa endelevu. Mbolea ya ruzuku kama ilivyoelezwa ni vizuri zikawafikia wakulima kwa wakati pia kuweko na ufuatiliaji katika sula la kuafikia wakulima kwani mara nyingine huwa inapita njia za panya na malalamiko kwa wakulima kubaki pale pale.

Ni vema Serikali kuandaa utaratibu mzuri katika Halmashauri husika ili kuwafikishia wananchi mbolea kwa urahisi.

Mheshimiwa Spika, ili kumpunguzia mkulima mzigo mzito ni vema Serikali ikaliweka vizuri suala la matrekta ili kumsaida mkulima kuweza kumega muda wa kupata mapumziko na kufanya masuala mengine ya kumletea Maendeleo.

Mheshimiwa Spika, sasa ni kuhusu usajili wa Magari ya Zanzibar kuingia Tanzania Bara. Utakumbuka kuwa mnamo tarehe 20.6.2008 Mheshimiwa Waziri wa Fedha alipokuwa anafanya majumuisho ya michango ya Waheshimiwa Wakuu kuhusu Bajeti ya Wizara ya Fedha na uchumi. Alisema sheria ya Zanzibar ni tofauti na Sheria za Tanzania Bara, ndiyo maana magari yanapofika yanatakiwa kusajiliwa upya. Hivyo naomba niulize hivi ni kweli sheria za Tanzania bara na Visimani ni tofauti. Lakini mbona magari kutoka nchini Kenya kuwa hayasumbuliwi au sheria zake zinalingana Kenya na Tanzania Bara? Ni vizuri suala hili likangaliwa upya ili wananchi wa Zanzibar tusiwasumbue ikwani hii nayo inaleta kero katika masuala ya Muungano.

Mheshimiwa Spika, sasa ni kuhusu sekta ya afya. Kila ifikapo mwezi Juni huwa tunapitisha Bajeti za Wizara mbalimbali, tukiwa na lengo la kuleta ufanisi na utendaji kazi katika Wizara. Tunapokaa kupitisha Bajeti ya Wizara ya Afya tunafahamu kuwa, utendaji kazi wa Wizara na idara utafanikiwa kwa kiwango kikubwa. Vile vile madawa na vifaa katika Hospitali kununuliwa, na kuwahudumia wananchi walio mijini na Vijijini.

Mheshimiwa Spika, kinachosikitisha ni kuwa wananchi walio wengi huwa wanapata shida sana wanapofika katika vituo vya afya na wakati mwingi bila mafanikio. Hivyo hizi fedha tunazozipitisha hapa huwa zinatumika kwa kitu gani? Au ni mishahara tu?

1. Baadhi ya wahudumu wa afya hawatekelezi majukumu yao.

2. Hata ukienda mwanzo wa mwezi dawa hakuna.
3. Mama na watoto wanapoteza maisha kwa uzembe.

Mheshimiwa Spika, ni sheria zipo zilizomo humu, mhudumu wa afya kama hakutekeleza majukumu yake na kama ipo hukumu inayomhusu inatekelezwa kwa kiasi gani pindi ukitokea uzembe.

Mheshimiwa Spika, Sekta ya Elimu fedha zilizopangwa katika Sekta hii ni nyingi, tunaiomba Serikali kuweka msimamizi katika matumizi ya fedha hizo. Kwa kuangalia vigezo vifuatavyo:-

1. Upungufu wa Walimu, mashuleni hasa Vijijini.
2. Kuweka Maabara katika shule husika.
3. kuongeza wataalam wa michezo mashuleni (wachezaji bora).
4. kuangalia upungufu na madawati mashuleni.

Mheshimiwa Spika, utakumbuka Mheshimiwa Waziri Mkuu alipokuwa anawasilisha Bajeti yake alisisitiza kusimamia utekelezaji wa MKUKUTA. Ni lazima usimamizi ufanyike katika ngazi zote, ingawa fedha zilizotengwa hazitoshelezi mahitaji yaliyopo lakini tutimize wajibu wetu ili ifikapo mwaka wa fedha ujao tujue pakuendeleza, vinginevyo wananchi daima wataendelea kuponda Serikali.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, naunga mkono hoja.

**MHE. CASTOR R. LIGALLAMA:** Awali ya yote napenda kuunga mkono hoja hii:-

Hospitali ya Mtakatifu Francis ya Mjini Ifakara Wilayani Kilombero ni *District Designated Hospital.* Hospitali hii huendeshwa na Kanisa Katoliki huku wakiendelea kupata ruzuku ya Serikali katika azma ya kusimamia utekelezaji wa sera ya Afya na kuimarisha kiwango cha utoaji wa huduma za afya.

Hivi karibuni Hospitali hii imepandisha viwango vya gharama ya kutoa huduma zake kiasi cha kuleta manunguniko makubwa kwa wananchi wa Wilaya hii.

Tunaomba Serikali iingilie kati kwa kuongeza ruzuku kwa Hospitali hii ili gharama zirudi kama zilivyokuwa au kujenga Hospitali ya Wilaya ya Serikali ili Hospitali hiyo ya *St. Francis* ibaki kuwa Hospitali ya rufaa, kwa vile wana madaktari Bingwa.

Sasa ni Mgawano wa Wilaya. Wilaya ya Kilombero ina Kata 19, Vijiji 81 na Vitongoji 365. Kutoka mwanzo wa Wilaya ya Kidatu mpaka mwisho wa Wilaya Kijiji cha Tanganyika (Kata ya Taweta) na Kijiji cha Uchindile (Kata ya Uchindile) ni takriban kilometa 300.

Wilaya hii imepokea wageni wengi kutokana na wananchi wengi kuvutiwa na ardhi yake, mvua za uhakika kwa ajili ya shughuli za kilimo. Katika sensa ya mwaka 2002 katika Mkoa wa Morogoro Wilaya iliyokuwa na watu wengi ni Kilosa (watu 488) ikifuatiwa na Kilombero (324).

Pamoja na uongezekaji wa kawaida wa asilimia 2.9% kwa idadi nilizotaja bado kuna ongezeko hilo na mpangilio *(random)* kwa wakulima waliohamia Wilaya Kilombero kwa malengo ya kuja kufanya shughuli za kilimo. Sasa hivi idadi ya watu katika Wilaya inakadiriwa kuwa na watu zaidi ya laki tano (500,000). Tunaomba Wilaya hii igawanywe ili huduma za jamii ziendane na idadi ya watu.

Sasa ni kuhusu barabara. Katika Wilaya ya Kilombero kuna barabara kuu mbili kubwa. Kuna barabara ya kitaifa *(trunk road)* ya kutoka Kidatu hadi Ifakara (km 75) na barabara ya Mkoa *(Regional road)* ya kutoka Ifakara hadi Taweta (km. 225). Barabara nyingine zote ni za Halmashauri.

Serikali iliishaahidi hapa Bungeni na wananchi walishangilia ahadi hiyo ya kujenga barabara ya Kidatu – Ifakara - Mahenge kwa kiwango cha lami kuanzia mwaka 2006/2007 mpaka 2010/2011. Je, ni lini basi ahadi hii itanza kutekelezwa? Barabara ya Ifakara – Mlimba – Taweta (km.225) ambayo ni barabara ya Mkoa inapita kwenye maeneo ambayo ni mashamba makubwa ambayo yataendelezwa na wawekezaji.

Shamba la *(Korea Tanzania Cooperation (KOTACO)* limepata mwekezaji wa kulima mpunga. Shamba la Ruipa, limo katika mchakato wa kupimwa (kuwa *surveyed)* ili hati ipelekwe *TIC* kupata mwekezaji wa kulima miwa kwa ajili ya kweka kiwanda cha Sukari katika Kijiji cha Namwawala. Shamba hili lilikuwa limetengwa na *SUDECO* miaka ya 70 kwa madhumuni hayo. Kutokana na shughuli hizo za uchumi, bila shaka patatokea ajira nyingi kwa wananchi wetu. Barabara hufuata bidhaa na itakuwa vizuri sasa kama Serikali itaimarisha barabara hii ili bidhaa zitakazozalishwa ziweze kusafirishwa na kuwafikia walaji kwenye masoko yaliyo nje ya Wilaya.

Wilaya yangu ina migodi miwili yenye kufua umeme (Kidatu na Kihansi). Niliwahi kuuliza katika Bunge hili. Kwa nini Serikali isiwe na mpango wa makusudi wa kupeleka umeme toka Kihansi kwenda Chita JKT, shamba la *KOTACO* na *RUIPA* ili wawekezaji wakija waanze mara moja kushughulikia uzalishaji.

Mheshimiwa Waziri Mkuu ameeleza kwenye hotuba yake kuwa Sekta hii ya Nishati itafaidika na msaada wa Serikali ya Marekani kupitia *Millenium challenge Corporation (MCC).* Kiasi cha Dola za Marekani 206 kutoka *MCC* kitatumika kuboresha miundombinu ya usafirishaji na usambazaji wa umeme katika mikoa mbalimbali. Mkoa wa Morogoro ukiwa mmojawapo.

Naomba Serikali, iingize Wilaya yangu katika mpango kama nilivyopendekeza katika ripoti yangu ambayo niliiwasilisha Wizara ya nishati na madini kupitia kwa Waziri Mkuu aliyejiuzulu Mheshimiwa Edward Ngoyai Lowassa. Katika *Feasibility Study* ile, nieleze sababu ya kiuchumi na kijamii za kuweka umeme Vijiji vya Wilaya yangu.

Inasikitisha sana kwa wananchi wa Wilaya hii kuendelea kuwa walinzi wa *pylons* zinazosafirisha umeme wa *grid* ya Taifa, huku wao wakibaki gizani. Inaleta pia manung'uniko kiasi kwa sababu hapo Kihansi kwa mfano kuna kila kitu. Kwa maana ya *feeder* za njia tatu ambayo ingeweza kupeleka umeme kutoka Kihansi kwenda Udagaji, Chita, Mchombe, Mkangawalo, Njage, Mbingu, Namwawala, Idete hadi Ifakara. *Feeder* nyingine ingeanza Kihansi mpaka Chisano, Kalengakero, Mlimba, Mpanga, Utengule, Ngalimira, Taweta. *Line* hii pia inaweza kuendelezwa na kupeleka umeme katika Jimbo la Ulanga Magharibi kupitia Vijiji vya Malinyi, Sofi, Mtimbira, Itete, Iragua mpaka kuungana na *grid* ya taifa kutoka Kidatu pale Lupiro.

**MHE. DR. JAMES ALEX MSEKELA:** Mheshimiwa Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa hotuba yake ambayo pamoja na kupangiliwa vizuri, imetoa ufafanuzi na mwelekeo mzuri wa utekelezaji wa Bajeti kwa kipindi cha 2008/2009. Ni matumani yangu kuwa haya yatasimamiwa vizuri ili tufikie malengo ya Bajeti hii na ya nchi kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, kuwa na Bajeti nzuri ni suala moja, lakini kuitekeleza kwa ufanisi ni jambo muhimu zaidi. Hapa watumishi wa Serikali watatakiwa kuongeza nidhamu ya kazi na kufuata taratibu hasa za fedha, katika utendaji wao.

Mheshimiwa Spika, muundo wa *organization* wa Serikali yetu haushabihiani sana na uwingi wa wananchi kadri unavyokwenda ngazi ya Kitongoji kutokea ngazi ya Taifa. Hii angalau husababisha usimamizi wa moja kwa moja wa Serikali ibakie na pengo kubwa.

Hili linajidhihirisha katika usimamizi duni wa Sekta mbalimbali katika ngazi ya Kata, Kijiji na Kitongoji kiasi cha ufanisi na tija kuendelea kuwa haba katika mpango na utekelezaji wake. Hata pale ambapo pia inakuwa imepelekwa ruzuku.

Mheshimiwa Spika, katika hali hii cha kufanya ni kujikita zaidi katika ung'atuaji wa madaraka, nyenzo *(resources)* pamoja na watumishi. Lakini pia itakuwa ni muhimu ufanyike uwekezaji mpana zaidi ili Mabaraza ya Maendeleo ya Kata na Vijiji pamoja na Halmashauri zao waweze kuchangia zaidi na kuongeza ufanisi katika usimamizi.

Mheshimiwa Spika, ninashukuru sana kwa mpango wa Serikali kupeleka umeme Wilaya ya Uyui kupitia Bajeti hii ili itusaidie kuharakisha Ofisi mpya ya *DC* wa Uyui na pia ofisi ya Halmashauri ya Wilaya kwanza kutoa huduma karibu na wananchi kama iilivyodhamiriwa. Napenda hapa pia niombe Mheshimiwa Waziri Mkuu na Wizara ya Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi waje wajenge nyumba za watumishi wa Wilaya na Halmashauri ya Wilaya. Majengo mawili ya ghorofa yaliyojengwa Chalinze ni aina nzuri ya Majengo tunayoyahitaji pale Isikizya yalipo Makao Makuu ya Wilaya ya Uyui. Mheshimiwa Spika, pia nikumbushe haja ya kuongeza na kuharakisha upatikanaji wa maji ya kutosha pale Isikizya – Makao Makuu ya Wilaya.

Mheshimiwa Spika, hapa pia nikumbushie hoja ya kubadilisha jina la Halmashauri ya Wilaya ya Tabora ili sasa itambulike kwa jina la Halmashauri ya Wilaya ya Uyui. Hili litatuondelea usumbufu na mkanganyiko wa kushabihiana kwa majina ya Halmashauri ya Wilaya ya Tabora (iliyopo Wilaya ya Uyui) na Halmashauri ya Manispaa ya Tabora. Mheshimiwa Spika, hapa sioni ugumu wa kubadili jina ili sote *to upate* urahisi wa kuondokana na Mkanganyiko usio wa lazima.

Mheshimiwa Spika, nitoe pongezi kwa Serikali na hususan kwa Waziri wa Kilimo Mheshimiwa Stephen Maatu Wasira kwa kufanikisha uanzishwaji na utekelezaji wa mafaniko ya utaratibu wa sheria ya stakabadhi katika maghala katika kumsaidia mkulima kupata bei nzuri kwa mazao yake na vile vile kuweza kupata *"bridging finance"* kutokana na mazao yake huku akisubiri bei nzuri. Mafanikio haya yameonekana katika Mikoa ya Mtwara na Lindi kupitia zao la korosho.

Mheshimiwa Spika, katika mafanikio haya pia Vyama vya Ushirika vimeimarika na napata yameongezeka kwa Halmashauri husika kutokana na Korosho. Haya yamefanikiwa kwanza kabisa kutokana na juhudi binafsi za Mheshimiwa Waziri wa Kilimo na msukumo mkubwa wa Serikali Kuu. Hili ndilo ninaloliomba kwa wakulima wa tumbaku Mkoani Tabora na pia kwa wakulima wa Pamba, hususan katika Mkoa wa Mwanza.

Mheshimiwa Spika, nimejifunza vikwanzo na upinzani uliowafika wenzentu wa Mikoa ya Mtwara na Lindi katika mwaka wao wa kwanza. Ugumu huo nauona hivi sasa na ninatarajia utaongezeka katika Mkoa wa Mwanza, hasa kuwa kuwa tayari tumetangaza nia ya kuanzisha utekelezaji wa sheria ya stakabadhi kwenye masoko kuanzia msimu wa mauzo ya pamba baada ya huu wa sasa ulioanza hapo tarehe 16 Juni, 2008. Hivyo basi ningependa kumsihi Mheshimiwa Waziri Mkuu na Waziri wake wa Kilimo wajizatiti na walete nguvu ya Serikali Kuu kuanzia msimu huu ili tuimarishe vyama vya msingi vya ushirika na pia *NCU (1984) Ltd* tayari kwa utekelezaji wa sheria hii ya Stakabadhi kwenye maghala kuanzia msimu wa mauzo ya pamba mwaka 2009/10. Baada ya hayo, napenda kutamka kwamba Naunga mkono Hoja ya Mheshimiwa Waziri Mkuu.

**MHE. FAIDA MOHAMEDI BAKAR:** Mheshimiwa Spika,kwanza napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa Hotuba yake yenye kuleta mategemeo ya maendeleo mazuri katika nchi yetu. Napenda pia kutoa pongezi kwa Waziri wake na Naibu Waziri kwa ushirikano mzuri.Naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Spika, naomba kuchangia yafuatayo:-

Napenda kuusifia Muungano wetu ambao uliasisiwa na viongozi wetu waasisi Mhe. Hayati Mwalimu J.K. Nyerere na Mhe. Hayati Sheikh Abeid Amani Karume. Muungano wetu umetuunganisha wananchi wa Tanzania Bara na Visiwani Zanzibar na umeleta maendeleo makubwa sana ya kiuchumi na kijamii. Napenda Serikali iendelee kuweka zawa kwa kuondosha kero za Muungano zilizobakia ili Muungano wetu udumu milele na milele maana Muungano wetu huu una manufaa sana hasa kwa sehemu ya pili

ya Muungano – Zanzibar ingawa kuna baadhi ya watu hasa kwa upande wa upinzani wanauchukua sana Muungano lakini pia wananchi walio wengi wanaupenda Muungano wetu. Namwomba Mungu aendelee kuulinda Muungano wetu.

Mheshimiwa Spika, sasa ni hali ya kisiasa hapa nchini. Hali ya kisiasa inaendelea kuwa nzuri katika nchi yetu na naipongeza Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na ile ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kwa kudumisha AMANI katika nchi yetu. Licha ya matatizo madogo madogo yanayojitokeza. Nashauri viongozi wetu wazidi kuwa na busara katika kuendeleza AMANI NA UTULIVU uliopo hapa nchini.

Kama tunavyojua kwamba kilimo ni uti wa mgongo wa taifa letu. Napenda kushauri Serikali iweze kutoa mikopo na msaada wa matrekta kwa wakilima pamoja na mbolea kwa wakati hasa kwa wakulima akimama walioko Vijijini kama tunavyojua kwamba wanawake wa Tanzania ndio wakulima wazuri sana. Lakini wana tatizo kubwa la vitendea kazi na wengi wamebakia kuliuma kwa majembe ya mkono. Serikali inapowapatia wakulima vitendea kazi vizuri mikopo mbolea na kutafutiwa soko la uhakika ya bidhaa zao. Basi wananchi pamoja na nchi yetu itaondokana na umasikini.

Mheshimiwa Spika, napenda kupongeza Serikali kwa kuanzisha shirika la TBC lakini kwa hiki ni chombo cha Serikali kinatakiwa kienee taifa lote kuliko kuacha Mashirika ya Habari ya Binafsi kuweza kuenea nchi mzima lakini taasisi ya Serikali ikawa haionekani wala kusikika nchi nzima. Nashauri serikali *T.B.C.* ienee nchi nzima mpaka Vijijini. Maana wananchi wanapendelea kujua au kupata taarifa kutoka Serikali yao.

Mheshimiwa Spika, sasa ni kuhusu maslahi ya madiwani, napenda kuishukuru na kuipongeza Serikali kwa kuamua kuongeza posho kwa Madiwani. Ahsante Mheshimiwa Spika.

**MHE. LUDOVICK J. MWANANZILA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Fedha za Bajeti zisichelewe kutoka baada ya kusoma mapato na matumizi ili Miradi ianze kutekelezwa mapema katika Wilaya na Mikoa yetu. *Experience* fedha huanza kutolewa mwezi wa Oktoba au Novemba, hali hii haikubaliki.

Magharibi yote ifunguliwe kwa miundombinu ya barabara, reli na ndege ili tuchume kutokana utajiri wa Congo.

Naomba maombi yangu ya Wilaya Mpya ya Kalambo yasisahaulike, ikiwa ni pamoja na Wilaya Mpya ya Katavi iliyopitishwa na *RCC* Rukwa.

Kilimo Rukwa ni kufa na kupona, tupewe mbolea ya kutosha mapema kabla ya mvua ili tuzalishe zaidi. Umwagiliaji upewe kipaumbele ili tuongoze uzalishaji.

Uvuvi katika Ziwa Tanganyika haujatiliwa maanani. Nimesema hili kwa miaka yote kuwa Mji wa Mpulungu Zambia, hupokea samaki toka Tanzania bila kuliingizia taifa letu ushuru wowote.

Umeme katika Jimbo la Kalambo ushughulikiwe mwaka huu wa fedha. Hadithi za nishati na madini hazieleweki sasa ni kero.

Maji Vijijini bado hatujafanikiwa ipasavyo, Miradi ya *World Bank* ni kichekesho ifutwe tu. Serikali iwekeze fedha zake yenyewe.

Biashara za mipakani zitatusaidia sisi wa Jimbo la Kalambo kama Serikali itaandaa mazingira muafaka. Hakuna juhudi za Wizara ya Viwanda na Biashara kuwekeza katika Mipaka ya Kasesya, Kasanga, Kipili, Kirando na Karema.

**MHE. SAID A. ARFI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumpongeza na kumshukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa hotuba yake nzuri; hata hivyo, nahitaji kupata maelezo ya ziada kuhusu dhana ya Madaraka kwa Wananchi kama inatekelezeka kama inavyokusudiwa. Kwa kuwa Wawakilishi wa Wananchi katika Serikali za Mitaa ni Madiwani, ambao hufanya maamuzi kwa niaba ya Wananchi; inakuaje maamuzi yanayofanywa na Madiwani katika vikao halali vya Halmashauri, yanabatilishwa na Watendaji wa mhimili mwingine (dola), bila kijali na kuthamini maoni na maamuzi ya Madiwani?

Mheshimiwa Naibu Spika, niliweke bayana jambo ambalo nakusudia kulielezea, ni juu ya ujenzi wa Makao Makuu ya Halmashauri ya Mji wa Mpanda. Tulikuwa na Kikao cha Halmashauri ya Mkoa wetu wa Mpanda, ambapo Wabunge wawili tulihudhuria na ajenda ya kujenga Makao Makuu ya Halmashauri ilijitokeza kujadiliwa kwa mapana na kidemokrasia, hatimaye maamuzi yalitolewa kwa kupiga kura na waliotaka yajengwe zilipo ofisi za sasa walishinda. Hayo ndiyo maamuzi ya wananchi ni lazima yaheshimiwe.

Naomba maelezo kwa maandishi; kwa nini maamuzi hayo yamepuuzwa na kupingwa na kuamua kujenga katika eneo ambalo watawala wanataka?

Wananchi wa Mpanda Mjini wanahitaji mji wao upanuke kwa kuwa na majengo mapya ya kisasa kila eneo ili iwe kichocheo cha kuboresha makazi na ujenzi wa majengo bora, badala ya kuweka huduma zote za Kiserikali eneo moja ambalo ni adha na usumbufu kwa wahitaji huduma.

Maoni ya watu yaheshimiwe na ndio maana ya dhana ya madaraka kwa wananchi itakuwa na maana. Vinginevyo, iwe wazi kwamba Viongozi wa Dola wataamua kwa niaba yao.

Haitoshi, hata pale wananchi walipoamua katika Miradi ya *TASAF* kutokana na vipaumbele vyao mfano maji au mifereji, vimepuuzwa na pesa zote za *TASAF* zimeelekezwa katika madarasa; si jambo baya hiyo ilikuwa ajenda ya Serikali kujenga

shule na kuwaambia wananchi kuibua miradi ilikuwa ni hadaa. Wananchi wanahitaji huduma za kijamii ziboreshwe, hasa upatikanaji wa maji na kuwa na Mamlaka za Maji katika miji yetu hazina uwezo na mitandao yao ya maji ni chakavu na ya muda mrefu; wameshindwa kufikisha huduma kwa walaji ambao wanaongezeka kwa kasi kubwa katika miji. Naiomba Serikali isaidie katika eneo hili na kuondoa kero ya maji kwa wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuiomba sasa Serikali iangalie suala la Watendaji wa Vijiji, ambao hadi sasa hawajaingizwa katika mfumo wa malipo ya Serikali. Nina maana kwamba, mishahara yao kupitia benki kwa wale ambao mpaka sasa wanahangaika kwenye madirisha ya Wahasibu wa Halmashauri, wakisubiri makusanyo; wanapata tabu na gharama, pia ni usumbufu; waaidiwe watu hawa ili watekeleze wajibu wao ipasavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, suala la Wakimbizi ambao wapo Katumba na Mishamo, nimesikia watakaoondoka ni wachache kuliko watakaobaki na hatimaye kupewa uraia. Naomba mambo yafuatayo yaangaliwe kwa kina; athari zake kisiasa, kiuchumi na kiusalama.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimelazimika baada ya kupata taarifa za ziada toka katika Jimbo langu la Mpanda Kati, nichangie kwa maandishi. Mji wa Mpanda ni miongozi mwa miji inayokua haraka na kupewa hadhi ya Halmashauri ya Mji, ambayo tunatakiwa tuibadilishe sura ya Mpanda ifanane na mji kama miji mingine nchini.

Napenda kuishukuru Serikali kwa kutupatia mgao kutokana na Mfuko wa Barabara *(Road Fund)*, lakini fedha tunayopata haitoshelezi mahitaji halisi ya kuboresha miundombinu ya maji kwa maeneo ya barabara na mifereji. Miji wa Mpanda umezungukwa na mito na vijito; hivyo, kuna njia za maji kuelekea katika mito na vijito hivyo ambazo zinapita katika makazi ya watu. Kwa hiyo, mifereji inahitajika sana kuboreshwa na kuimarishwa ili kunusuru makazi ya watu hasa mji wa zamani, Makanyagio, Mji Mwema na Kotazi. Fedha inayopokelewa ni kidogo na haitoshelezi.

Mheshimiwa Spika, naomba kuleta ombi kupitia kwako kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mji wa Mpanda unahitaji huruma ya Serikali kwa kuongezewa fedha za ziada kwa ajili ya ujenzi wa mifereji.

Mheshimiwa Spika, tunadhani ipo haja Mji wa Mpanda kuwa na barabara za lami ili kubadili sura ya mji. Tunafanyaje pesa inayotengwa ni kidogo sana? Naiomba tena Serikali itusaidie katika eneo hili angalau kwa kilomita chache za kuanzia kwa Mji wa Mpanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilisema katika mchango wangu mapema juu ya tatizo la umeme Mpanda. Ufumbuzi wa tatizo la umeme Mpanda ni pamoja na kupata jenereta mpya na zilizopo zitengenezwe. Aidha, kuna utafiti juu ya umeme wa upepo, nasikia tafiti za kule Usevya (Mpimbwe) zilionyesha kuweza kuzalisha umeme kwa kiasi fulani.

Naomba utafiti huo uendelezwe kuona uwezekano wa kupata umeme kwa Mji wa Mpanda na Vijiji vya Tarafa ya Mpimbwe - tujaribu Mheshimiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo la maji ni kubwa katika nchi yetu, pia Mji wa Mpanda tunahitaji kupunguza kero hiyo hata kwa kuchimba visima virefu katika Vitongoji vya Kampuni, Milupwa, Itogolo, Mapinduzi, Ilembo na Kasimba. Visima vilivyopo kati ya mji havitoshi katika Kata ya Kawajembe na Nsemlwa. Kwa kusaidia eneo hilo, tutakuwa tumepunguza kero na kutimiza wajibu wetu kama tunajali shida zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kero nyingine ambayo inahitaji sana kushughulikiwa ni malimbikizo ya madeni ya watumishi hasa Walimu, Askari Polisi na Magereza, Wauguzi na Madaktari. Watu hawa wanafanya kazi katika maneo yasiyo na mvuto ya pembezoni, tusiwakatishe tamaa walipwe madeni yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, napenda kuiomba Serikali kama ilivyofanya kutoa kibali cha kuajiri walimu wastaafu kwa ajili ya shule za sekondari, bado tunao upungufu pia katika shule za msingi, ili kupunguza tatizo hilo hasa katika Mkoa wa Rukwa, tupewe kibali cha upendeleo cha kuajiri walimu wastaafu katika shule zetu za msingi katika Mkoa wetu wa Rukwa ili tupunguze tatizo hili la upungufu wa walimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana.

**MHE. ASHA MSHIMBA JECHA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naanza kwa kumpongeza Waziri Mkuu, Mawaziri, na Watendaji wa Ofisi yako, kwa kutuletea hotuba hii iliyozungumzia Sekta zote na kuonyesha azma kubwa ya Serikali katika kuwaletea wananchi maendeleo endelevu. Huu ni mwanzo mzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kilimo ndio uti wa mgongo wa Taifa letu. Serikali yetu ichukue jududi za dhati, kuwapatia mikopo wananchi wetu wanaojishughulisha na kilimo. Taasisi za fedha zielekezwe kwa makusudi kuwa na fungu la kuwakopesha wakulima.

Tatizo la UKIMWI linaendelea kukua licha ya juhudi mbalimbali zilizochukuliwa Kitaifa na Kimataifa na kuathiri vijana mbao ndio nguvu kazi ya Taifa letu. Nashauri Serikali, Taasisi, *CBOs,* nguvu zao wazielekeze moja kwa moja kwa jamii wakiwemo walioathirika, familia zinazowahudumia waathirika hao na watoto mayatima ambao wazazi wao wamefariki kwa maradhi hayo. Aidha, watoto mayatima wapatiwe elimu na kuendelezwa.

Serikali kupitia Wizara ya Afya ichukue juhudi za makusudi, kuwapatia matibabu bure, wananchi wake wale ambao wanaugua na hawana uwezo wa kujitibu, hata kufika kwenye vyombo vya habari kuomba msaada kwa Watanzania wenzao; inasikitisha sana. Ahsante.

**MHE. LUCAS L. SELELII:** Mheshimiwa Naibu Spika, Wafanyakazi au Watumishi wa Umma ni Wanachama wa Mifuko ya Pensheni ya *NSSF/NPF/PPF.* Mifuko hii inafanya kazi nzuri ya kuwekeza katika majengo ili kuongeza mapato ya mashirika haya.

Nashauri ni vyema masharika haya yawe na mpango wa kuwakopesha wafanyakazi ambao ni Wanachama wao, mikopo ya kuwawezesha kujiandaa katika maisha yao ya baadaye baada ya kustaafu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ilikubali mapendekezo yote 23 ya Bunge, kuielekeza Serikali kuchukua hatua za utekelezaji wa Kamati ya *Richmond.* Muda wa Serikali kutekeleza ilikuwa ni siku 90. Ajabu tangu wakati huo, bado Serikali haijatoa majibu ya hatua gani zilizochukuliwa! Naelewa yapo mambo yanayohitaji muda mrefu, kati na mfupi, lakini ni inavyoelekea Serikali imekaa kimya kwa maelekezo yote. Pamoja na ugumu huo, naomba jambo moja Serikali ikubali; ni lile la kusitisha ulipaji wa *capacity charges* kwa makampuni ya kuzalisha umeme kuendelea kulipa *capacity charges.* Huku ni kuwakomoa au kuwapa adhabu wananchi ambayo inasababisha hasara kwa fedha za Serikali/TANESCO.

Kila mwaka, Makampuni haya yanalipwa shilingi bilioni 240. Kipengele hiki cha *capacity charge* kifutwe mara moja tena haraka sana. Hizo pesa zinazolipwa, zipelekwe kuwekeza umeme Vijijini (hasa katika maeneo yaliyosahaulika). Naomba hili lisichukue muda mrefu katika kulifanyia uamuzi.

**MHE. MOHAMED A. ABDULAZIZ:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, napenda kuunga mkono hoja.

Naomba nizungumzie suala moja tu la Mahakama ya Kadhi. Kwanza kabisa, mimi nakubaliana na Ahadi ya ki-Ilani ya kuwepo kwa Mahakama ya Kadhi. Ningependa kutoa ushauri kwamba, Mahakama ya Kadhi ianzishwe na iwe inashughulikia masuala yafuatayo: Kuonekana kwa mwezi; mirathi; ndoa; na talaka. Hii ni kwa waumini wote ambao ni Waislam na wameoana Kiislam.

Gharama za uendeshaji wa Ofisi ya Kadhi ziwe ni juu ya Waislam wenyewe, isipokuwa sheria zetu zirekebishwe zionyeshe wazi kuwa kesi za mirathi, ndoa na talaka zitashughulikiwa na Mahakama ya Kadhi. Serikali isijiingize katika kugharamia gharama za uendeshaji wa Ofisi za Kadhi. Kikao cha pamoja cha Madhehebu, Taasisi na Jumuia za Waislamu kikutane na kuchagua Kadhi Mkuu na Kadhi Mkuu naye atawachagua Makadhi wa ngazi za chini. Hili litapunguza kabisa malalamiko ya wote wanaopingana na kuwepo kwa amri hiyo.

**MHE. PROF. FEETHAM F. BANYIKWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naanza kwa kutoa pongezi kwa Waziri Mkuu, kwa kutoa hotuba nzuri inayoleta

matumaini.  Baada ya pongezi hizo, ningependa kuchangia hotuba ya Waziri Mkuu kama ifuatavyo:-

Jimbo la Ngara limevamiwa na majambazi wenye silaha kutoka nchi za jirani, katika Kata za Kabanga, Mabawe, Mugoma na Kilushya.  Watu wengi wamehama kutoka kwenye makazi yao kwa sababu wanavamiwa usiku.  Vijiji vya Muruvyagira na Mabawe vimevamiwa kwa kasi kubwa hivi karibuni.  Tunaiomba  Serikali iweke jitihada katika kukabiliana na huo uvamizi wa majambazi wenye silaha.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunashukuru kupewa umeme katika Mji wa Ngara, kwa sasa tunaomba usambazwe katika Vijiji na Miji ya Kabanga na Rulenge.

Mgodi wa Kabanga Nickel utakuwa mgodi mkubwa wa *nickel* katika Afrika.  Ili mgodi huu uanze kujengwa unahitaji umeme MW 45.  Huu umeme ni mkubwa, hauwezi kupatikana Ngara.  Tunaomba umeme mkubwa wa gridi usambazwe mpaka Kabanga Nickel, ili tuweze kuanza kujenga Mgodi wa Kabanga Nickel.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wananchi wa Ngara wanaomba Barabara ya Murugalama - Keza -Nyakahura ijengwe kwa Kiwango cha lami ili iwe kichocheo cha maendeleo ya wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wananchi wa ngara wanaomba shule za Sekondari za Ngara Mjini na Kabanga ziwe sekondari zenye Kidato cha Tano na Sita.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wananchi wa Ngara wanaomba Hospitali ya Myamiyaga iwepe hadhi ya Hospitali ya Wilaya.  Kwa kuisaidia, Halmashauri ya Wilaya ya Ngara ipatiwe pesa za kuboresha majengo yaliyopo katika Hospitali hii.

**MHE. FELISTA A. BURA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua fursa hii, kumpongeza Waziri Mkuu, Mheshimiwa Mizengo Pinda; Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa Celina Komani; Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Uratibu na Bunge), Mheshimiwa Philip Marmo; Naibu Waziri wa Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Mheshimiwa Aggrey Mwanri; pamoja na Watendaji wote wa Ofisi ya Waziri Mkuu, kwa kazi nzuri wanayoifanya katika kuiendeleza nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Jengo/Ofisi ya Manispaa ya Dodoma ilichukuliwa na Wizara ya Kilimo na Ushirika, kwa muda mrefu sasa jengo hilo halijarudishwa kwa Manispaa.  Manispaa ya Dodoma inafanya kazi katika Majengo ya Shule ya AghaKhan.  Jengo ambalo Manispaa hawawezi kuliongeza au kubadilisha kitu chochote.  Ofisi nyingine za Manispaa zimo ndani ya kilichokuwa choo.

Mheshimiwa Naibu Spika, je ni haki Wizara ya Kilimo na Ushirika kuendelea kung’ang’ania Jengo la Manispaa?  Kama Wizara ya Kilimo na Ushirika wanalipenda Jengo hilo la Manispaa, waijengee Manispaa jengo lingine ili Manispaa waache kufanya shughuli zao ndani ya majengo ya shule.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imetenga Sh. 1.6 bilioni kwa ajili ya Ujenzi wa Kiwanja cha Ndege Msalato Dodoma kwa mwaka ujao wa fedha 2008/2009.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujua kama kiasi hicho kilichotengwa na Serikali kinatosha katika ujenzi na kuwalipa fidia wananchi wanaoishi eneo la Msalato? Ili kuepuka migogoro kati ya Serikali na Wananchi, naiomba Serikali iwalipe fidia Wananchi wanaoishi katika eneo litakalojengwa Uwanja wa Ndege kabla ya ujenzi wa uwanja huo kuanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeshtushwa na uamuzi wa Serikali kuendesha mjadala wa Kitaifa, kuhusu uamuzi wa Serikali kuhamia Dodoma au la.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi Wananchi wa Dodoma, tunaamini kabisa kuwa, Makao Makuu ya Chama na Serikali ni Dodoma na ndio maana kila awamu ya uongozi wa nchi inapoanza, tuaandaa mapokezi rasmi kwa Uongozi wa Kitaifa katika Kijiji cha Chamwino Ikulu. Hayati Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, alitangaza kuhamia Dodoma rasmi na pia Rais Mstaafu, Mheshimiwa Ali Hassan Mwinyi naye katika uongozi wake, alilitangazia taifa kuwa, amehamia Makao Makuu Dodoma.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama Dodoma siyo Makao Makuu ya nchi, ina maana Hayati Baba wa Taifa na wenzanke waliofuatia nyuma yake waliwadanganya wananchi? Kwa maoni yangu, sioni sababu ya Serikali kurudi nyuma, baada ya uamuzi wa Kuhamia Dodoma kwa miaka 35 kutofanikiwa. Serikali ichukue hatua mahususi ya kujenga miundombinu Mkoani Dodoma kwa nia ya kuhamia.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Wilaya yetu ya Kongwa, wananchi wanateseka mno kwa kukosa huduma za maji. Miradi ya Maji inayofadhiliwa na Benki ya Dunia, haijawasaidia Wananchi wa Wilaya ya Kongwa. Naiomba Serikali ione umuhimu wa kuwasaidia Wananchi wa Kongwa kupata maji safi na salama.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Serikali kwa uamuzi wa kushirikiana na wananchi katika kujenga shule za sekondari kila Kata nchini. Uamuzi huo umewawezesha watoto wengi kupata nafasi ya kuendelea na elimu ya sekondari.

Mheshimiwa Naibu Spika, ombi langu ni kwa Wilaya ya Bahi; Wilaya ya Bahi kuna upungufu mkubwa wa walimu katika shule za msingi pia sekondari. Serikali ione umuhimu wa kuwapeleka walimu wa kutosha katika Wilaya hiyo, kwani pamoja na upungufu uliopo wengine ni wagonjwa na wengine ni wazee sana, wamelemewa na kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. RUTH B. MSAFIRI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampongezsa mtoa hoja. Hoja imewasilishwa vizuri na imelenga Ilani ya Uchaguzi ambayo ni ahadi kwa wapiga kura.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na mengi niliyonayo, naomba nisaidiwe kupata majibu ya mgogoro wa ardhi kati ya wakazi wa Vijiji vya Ngenge, Rutoro na Ranchi ya Kagome. Kijiji cha Ngenge chenye usajili Na. 205 na Rutaro No. 577 vimemegwa sana na *Block No*. 10, 13, 14, 15 na 17. Kinachonisikitisha, tangu nilipopata hoja hii na kuanza kuifutalia tangu mwaka 2006 hadi sasa, sijapata jibu muafaka. Wanachi wanaendelea kuteswa na wawekezaji wa Ranchi katika Block nilizozitaja bila kujali maagizo ya Waziri aliyoyatoa kwa Mkuu wa Mkoa kwamba, Vijiji ambavyo vimepiwa na vina miundombinu ya kudumu havitaguswa, vitaendelea kuwepo na Ranchi zitakuwepo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kilichofanyika ni kweli wananchi wamebaki, lakini mashamba yao yenye migomba (ambalo ndilo zao la chakula kikuu), maeneo ya ardhi ambayo huwa wanalima maraharage kwenye Vitongoji vya Kyarutare, Kyobuheke na Nyakelela wamenyang'anywa. Maeneo hayo yameingizwa katika eneo la wawekezaji. Wawekezaji wanayachunga mashamba hayo, wameweka walinzi wenye mtutu, ambao wanawanyanyasa wananchi. Badala yake, wananchi wametakiwa waondoke hapo waende Bukoba Vijijini ilipo Block 291.

Hoja hii nimeifuatilia sana kwa Waziri aliyeanza nalo, Mheshimiwa Dr. Kawambwa. Mheshimiwa Diallo, yeye alinielekeza kwa *RC.* Hata hivyo, sikupata msaada wowote kwa Mheshimiwa Waziri aliyepita wala *RC,* ambaye hata sasa hatuna amani naye kwa sababu hatukubaliani juu ya hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata alipokuja Mheshimiwa Rais Kikwete tarehe 23 Januar, 2008, nililieleza suala hili na *RC* alikuwepo. Mheshimiwa Rais, alishangaa kuona *NARCO* imeshindwa kuiendeleza Ranchi hiyo, badala ya kuwafikiria waliopo imezua mgogoro nao. Hata hivyo, RC hajanipa jibu muafaka hadi sasa. Wananchi wanaendelea kubughudhiwa hata leo hii.

Lingine linalosikitisha; kasoro Block Na. 10 na 11 tu, ndizo zina ng'ombe wa mwekezaji, lakini zinazobaki Block 13, 14, 15 na 17 wamerejea wale wale Wanyarwanda (wahamiaji haramu), ndio wanaochunga ng'ombe humo. Wakati huo huo, wananchi wanafukuzwa. Hivi kweli hizi habari Serikali haizijui?

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Serikali ikubali ombi letu la kuwaacha wananchi waendelee kukaa pale, pia waongezewe eneo la kutosha kuishi na kufanya shughuli za kilimo na maendeleo; pia amani iwepo. Hapa nina maombi matatu; Wananchi waendee kubaki; Wananchi waongezewe eneo la kutosha sasa na baadaye; na wahamiaji haramu waondolewe na mifugo yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. ANDREW JOHN CHENGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchukua fursa hii, kumpongeza kwa dhati Waziri Mkuu, Mheshimiwa Mizengo Pinda,

kwa hotuba nzuri aliyoiwasilisha kwa umahiri mkubwa. Nawapongeza pia Mheshimiwa Philip Marmo, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Uratibu na Bunge); Mheshimiwa Celina Kombani, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa; na Mheshimiwa Aggrey Mwanri, Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa; pamoja na Wataalam wa Ofisi ya Waziri Mkuu na Taasisi zilizo chini yake wakiongozwa na Bwana Vincent Mrisho, Katibu Mkuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuunga mkono hoja ya Waziri Mkuu, napenda kuchangia kwa kifupi kama ifuatavyo:-

Naipongeza Serikali kwa jitihada inayoendelea kuchukua katika kutekeleza MKUKUTA. Suala la ukuaji wa uchumi hasa katika vipaumbele tunavyojiwekea, lazima tulifanye ajenda yetu ya kudumu. Maeneo ambayo yameonyesha ukuaji wa haraka na hivyo kuchangia katika ukuaji wa uchumi lazima Serikali iendelee kuyawekea mazingira mazuri ili yaweze kuchangia kwa kasi zaidi. Uanzishwaji wa *Export Processing Zones* na *Special Economic Zones* upewe uzito unaostahili. Tuonyeshe njia kwa vitendo kwa sababu maeneo hayo yana *potential* kubwa ya kukuza/kuongeza mauzo ya bidhaa yetu nje ya nchi na pia kukuza ajira. Sasa hivi tumekuwa tikilisema kwa nadharia zaidi kuliko vitendo, tuanze katika maeneo machache na yasimamiwe vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu kubwa ya fedha zilizotengwa na Serikali kwa mwaka ujao wa fedha (2008/09) katika Sekta ya Miundombinu, itatumika kulipia madeni kwa kazi zilizofanywa huko nyuma. Nashauri Serikali kupitia Wizara ya Miundombinu na Ofisi yako *(PMO),* iangalie uwezekano wa kuwa na maelewano na baadhi ya Mabenki ya Biashara hapa nchini ya kuwa na *facility* ambayo itatumiwa na *TANROADS* kulipia *certificates* ambazo zimeiva. Hatua hiyo, itaepusha malipo ya riba *(interest)* na adhabu *(penalty)*, kwa kuchelewesha malipo kwa kazi zilizofanywa na makandarasi. Mabenki yatakubali pendekezo hilo kwa sababu fedha za *Road Fund* ni *ring fenced;* ni fedha za uhakika ila zinatiririka kuingia katika Mfuko wa Barabara polepole. Nashauri tuwe wabunifu.

Pili, suala la *Sovereign Bonds* ni zuri, tatizo letu ni kasi ndogo ya utekelezaji. Kwa nini *Rating* tu ya Tanzania inachukua muda mrefu? Jibu Urasimu. Tubadilike, sambamba na mkakati huo wa *Sovereign Bonds,* nashauri kupitia *Finance Bill* ya mwaka huu; Sheria ya *Government Loans, Guarantees and Grants Act, 1974* kama ilivyorekebishwa, ifanyiwe marekebisho ili kushusha *threshold* ya *grant element* kwenye mikopo ambayo Tanzania inakopa ambayo kwa sasa hivi ni asilimia 50 au zaidi. Sharti hili lazima tuondokane nalo sasa kabla ya kuanza *road show* ya kutafuta mikopo kwa ajili ya miundombinu kupitia *Sovereign Bonds.*

Mheshimiwa Naibu Spika, Wananchi wa Bariadi wamekuwa na kilio cha muda mrefu cha kutaka Wilaya yao igawanywe kuwa Wilaya mbili. Ombi lao linakidhi vigezo vyote vilivyowekwa kwa maombi kama haya. Naimba Serikali iyapatie maombi ya Wananchi wa Bariadi uzito unaostahili.

Mheshimiwa Naibu Spika, jedweali Na. 16 ambalo ni miongozni mwa majedwali yanayoambatana na Hotuba ya Waziri Mkuu, limenishua sana kwa upande wa Mkoa wa Shinyanga, hususan *percentage* ya chini ya idadi ya wanafunzi waliofanya mtihani wa Darasa la Saba na waliofaulu, ikilinganishwa na mikoa mingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Serikali inipatie maelezo ya kuridhisha; tatizo ni nini, walimu wabovu au upungufu wa walimu?

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkoa wa Shinyanga ni miongoni mwa mikoa hapa nchini, iliyoitikia vizuri agizo la Serikali la ujenzi wa Shule za Sekondari za Kata. Hata hivyo, tatizo ambalo sasa limekuwa kero ni lile la idadi ya wanafunzi wa shule za msingi kwa uwiano wa mwalimu mmoja. Wakati mikoa kama Arusha, Kilimanjaro na kwingineko, uwiano ni mwalimu mmoja kwa wanafunzi 35 – 38, Shinyanga ni 1:63. Hii ni hatari sana. Naiomba Serikali iingilie kati ili kuondoa aibu hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya haya machache, namaliza kwa kusema naunga mkono hoja hii.

**MHE. ANTHONY M. DIALLO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Waziri Mkuu, atangaze kuanzishwa kwa Halmashauri mbili; ya Ilemela na Nyamagana katika mwaka huu wa fedha na kulisema alilolitamka katika hotuba yake ya bajeti, yaani utekelezaji utaanza mara muundo utakaopendekezwa na Tume iliyoundwa kujulikana.

Kwa vile bajeti inatokana na Mipango ya Kata na *OC*, ugawaji wa fedha za Bajeti ya Jiji utafanywa na Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa hata wakati bajeti hii inaendelea. Hili tamko litasaidia kutekeleza ahadi aliyoitoa Mheshimiwa Rais, wakati wa Kampeni na baada ya uchaguzi wakati wa ziara yake Mkoani Mwanza. *This is a political management issue especially* wakati tunafahamu tuna Uchaguzi wa Serikali za Mitaa mwaka kesho. Nitashukuru tamko hilo likitekekelezwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja ya Waziri Mkuu.

**MHE. FELIX N. KIJIKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya yote, napenda kumpongeza Waziri Mkuu, kwa hotuba nzuri aliyoitoa ambayo kwa hakika inagusa maisha ya kila Mtanzania.

Aidha, nawapongeza kwa dhati kabisa, Mawaziri wote wanaofanya kazi kwa kumsaidia Waziri Mkuu, ikiwa ni pamoja na Makatibu Wakuu wote. Kwa mantiki hiyo, napenda kutamka rasmi kuwa, naiunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

Baada ya utangulizi wangu huo, napenda kutoa ushauri na kuchangia katika baadhi ya maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, napenda kuzipongeza jitihada za Serikali za kuona umuhimu wa kuusaidia Mkoa wa Kigoma kwa kuanza harakati za kuukomboa Mkoa kwa matatizo ya muda mrefu. Pongezi hizo zinahusu jitihada katika yafuatayo:-

Naipongeza Serikali kwa kuweka msukumo mkubwa na kuhakikisha Wilaya ya Kibondo inapangiwa kununuliwa *generator* kwa ajili ya umeme kwa Mji wa Kibondo. Kwa niaba ya Wananchi wa Kibondo, naishukuru Serikali.

Naipongeza Serikali kwa kujali kilio cha watu wa Kigoma kuhusu usafiri wa barabara, tayari Serikali imeweka msukumo kwa hilo kwa kutenga fedha za kufanya upembuzi yakinifu, kazi ambayo imeanza tayari. Kwa hilo pia, natoa pongezi kwa Serikali lakini niombe kwamba, baada ya kazi ya upembuzi yakinifu kukamilika, basi kazi ya ujenzi wa barabara ianze.

Kuhusu maji hali ambayo ni mbaya sana, katika Wilaya ya Kibondo na hususan kwa wakazi wa Kibondo Mjini, Serikali itenge kiasi hicho cha shilingi 224,000,000 kwa mwaka 2006/07. Kiasi hicho cha fedha hakikutosha, hivyo, kwa makusudi mazima, naiomba Serikali kwa kutumia fedda za *Quick Win* ziongezwe ili kutoa huduma ya maji kwa wakazi wa Kibondo Mjini wapatao 15,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kipengele cha Elimu; Wilaya inayo mahitaji ya walimu kunakotokana na uchache wa walimu kwenye shule 129 za msingi za Wilaya nzima. Hata hivyo, upungufu unaohusu elimu nautoa kama ifuatavyo: shule za msingi zipo 129; walimu waliopo ni 1,086 pungufu 601; vyumba vya madarasa ni 1,046 pungufu 641; madawati yaliyopo 20,767 na pungufu ni madawati 3,306; vyoo vya matundu 1,106 pungufu 2,505; walimu waliopo ni 382 na pungufu ni 704; na maktaba zipo 2 na pungufu 132.

Mahitaji yaliyoainishwa hapo juu, yanatakiwa kupatiwa ufumbuzi kwa kuboresha hali ya Elimu katika Wilaya ya Kibondo.

Pamoja na jitihada za kuwapo na shule za kutosha, lakini bado lipo tatizo la mabweni ya kulala, kwa sababu wanafunzi wanapewa mimba kwa kutokuwa na mahali panapoaminika na kutoaminika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwepo na wimbi kubwa la kufanya biashara kwa kutumia dola badala ya Shilingi ya Tanzania. Hali hii imechangia kwa kiasi kikubwa, kuangusha thamani ya fedha ya Tanzania. Kwa mfano, hali hii inajitokeza kwenye upangaji wa nyumba, pamoja na kununua *airtime.* Kadiri hali hii inavyoruhusiwa kuendelea, mwisho manunuzi ya vitu vyote yatabadilika na kuwa katika Dola za Kimarekani.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali ya usafiri kutoka Dar es Salaam kwenda Kigoma kwa gari moshi ni mateso makubwa. Mbali na mateso kwa wasafiri, bado gari moshi imepangwa kufanya safari mara mbili kwa wiki hali ambayo haitoshelezi wasafiri. Matokeo ya utaratibu huu ni abiria kujazana kwenye mabehewa hadi vyooni. Utaratibu wa gari moshi kwa njia ya kati ni kila siku.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi karibuni tumeshuhudia tukio baya lililosababisha kuanguka kwa ndege ya Jeshi na kuua wananchi wasiokuwa na hatia. Imekuwa ni jambo la kawaida, kwa ndege zetu kuwa na hitilafu zinapokuwa angani ama wakati wa kuruka. Mfano hai ni Shirika la *Precision Air* ambalo mara kwa mara ndege zake zimekuwa zikiharibika. Ninashauri Serikali itoe msukumo wa makusudi, kuhakikisha mafundi wa ndege wanapelekwa kwenye mafunzo nyuo vinavyotambulika kuliko hali ilivyo sasa.

**MHE. ELIZABETH N. BATENGA:** Nampongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mawaziri, katika Ofisi ya Waziri Mkuu, Naibu Waziri, pamoja na Watendaji wote, kwa Hotuba ya Bajeti iliyowasilishwa hapa Bungeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, kilimo kimekuwa kikipewa jina na sifa nyingi; Sekta Kiongozi, Sekta Muhimu, Uti wa Mgongo (backborne, spinal cord) wa uchumi wetu, lakini kwa kiasi gani kilimo bora kinazingatiwa? Je, wapo wataalam wa kutoka hadi ngazi ya Kijiji? Je pembejeo zinazotakiwa zinawafikia wakulima kwa kiwango kinachotosha na kwa muda muafaka?

Je, Serikali inajihusisha vipi na kuhakikisha kwamba, wakulima wanapata bei nzuri kwa ajili ya mazao?

Wanawake ndio wazalishaji wakubwa katika Sekta ya Kilimo, lakini hawana utaalam; je, kuna utaratibu gani wa kuwapa mafunzo ili waweze kulima kwa ufanisi? Wanawake hawa wana majukumu mengi; kuzaa, kulea na kutunza/kulinda familia lakini pia wanakabiliwa na matatizo mengi kama vile kutopatikana kwa maji safi katika maeneo au masafa mafupi (si zaidi ya mita 400); mila na desturi ambazo hazimpi haki na heshima katika jamii; na kutokuwa na haki ya kumiliki mali au kushiriki kupanga matumizi ya fedha zinazotokana na mapato ya familia. Je, ni kwa kiasi gani mikakati inafanywa na serikali ili kupunguza tatizo la maji hususan maeneo ya Vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la Dodoma kuwa Makao Makuu ya Nchi halihitaji mjadala wowote zaidi ya kutungiwa sheria na kuweka mipango ya kujenga na kuhamia. Inaeleweka kuwa si rahisi kuhamisha Wizara zote kwa mara moja kutokana na hali ya uchumi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. MWAKA ABDULRAHMAN RAMADHAN:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa, napenda kumpongeza Waziri Mkuu, kwa hotuba yake.

Ninawapongeza Mawaziri na Naibu Mawaziri, Makatibu Wakuu, pamoja na Watendaji wote walioshiriki katika kuandaa Hotuba ya Bajeti ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchukua fursa hii, kuzipongeza Serikali zetu mbili (ya Muungano na ile ya Mapinduzi Zanzibar), kwa kuhamasisha wanachi wa chi hii ili kuanzisha *SACCOS* katika Kata/Shehia na Majimbo. Lengo kuu la *SACCOS* hizi ni kuwapatia mikopo kwa urahisi, kupitia katika mabenki yetu. Wananchi wengi wamehamasika na *SACCOS* nyingi zimeanzishwa, tatizo lililopo ni kuwa *SACCOS* nyingi hazijakidhi uwezo wa kukopa kutokana na hisa, pamoja na mitaji kuwa midogo. Masharti ya kukopa ni lazima *SACCOS* iwe na walau Sh. 5,000,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, ombi langu ni kwamba ni vizuri benki zetu zipunguze kima cha kuanza kupata mkopo toka Sh. 5,000,000 hadi 3,000,000. Hii itasaidia *SACCOS* zetu nyingi kuweza kupata mikopo na Wananchi/Wanachama wengi kufaidika na *SACCOS* hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie suala la Mkopo wa JK. Kwa upande wa Tanzania Bara, mikopo hii imeenda vizuri. Tunaomba Mpango huu ueleze utaratibu utakaotumika kupata mikopo hiyo kwa upande wa Tanzania Zanzibar. Aidha ni vizuri tukajifunza kutoka Tanzania Bara kuwa, kasoro zote zilizojitokeza, zisiweze kutokea kwa upande wa Tanzania Zanzibar.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala la Makao Makuu ya Serikali kuhamia Dodoma; kwa kweli hili suala ni la muda mrefu sasa, ambalo linapigiwa kelele sana ndani ya Bunge. Ushauri wangi ni kwamba, Ofisi ya Waziri Mkuu, ionyeshe mfano wa kuhamia Dodoma kikamilifu na Wizara nyingine nazo zifuate kikamilifu, ili tupunguze msongamano wa magari Dar es Salaam.

Mheshimiwa Naibu Spika, nazishukuru sana Serikali zetu mbili, kwa kusisitiza uwiano wa uwakilishi katika vyombo vya dola. Serikali hizo zimeamua kwa makusudi, kuhakikisha kuwa wanawake wanainuliwa kwa kuwekwa kwenye madaraka katika ngazi mbalimbali. Pia Serikali hizo zimesema kuwa, ifikapo mwaka 2010, vyombo vyote vya uwakilishi, yaani Bunge la Jamhuri ya Muungano Tanzania na Baraza la Wawakilishi Zanzibar, idadi ya uwakilishi itakuwa sawa baina ya wanawake na wanaume.

Mheshimiwa Spika, napenda kushauri kuwa, Serikali zetu ziweke bayana taratibu za kufikia nusu kwa nusu *(fifty fifty),* ili wanawake waweze kujua, bila maelezo ya kutosha. Kwa sasa toka Serikalini huenda mpango huu ukawashtukiza akina mama na kushindwa kupata wawakilishi wazuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. MHOGA S. RUHWANYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Msemaji wa Kambi ya Upinzani, kwa hotuba nzuri, yenye utafiti na inayohoji mambo ya msingi ya kitaifa na yanayotoa ushauri mzuri wa kizalendo kwa Serikali. Ombi langu ni

moja tu. Serikali ikubali ushauri au mapendekezo yanayotolewa na Kambi yetu au na mbunge yeyote, bila kujali anatoka katika Chama gani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Mheshimiwa Waziri Mkuu, ndiye msimamizi wa Serikali na Baraza lote la Mawaziri, naona bora nitoe wazo langu juu ya mabadiliko ya Baraza la Mawaziri. Kwa miaka miwili na nusu, tumeshuhudia mabadiliko madogo ya Baraza la Mawaziri mara tatu na Baraza lote kuvunywa mara moja.

Najua jambo hilo Rais alilifanya kwa nia njema, kwani lazima aridhike na wasaidizi wanaomsaidia na pindi anapoona kuna haja ya kubadili anafanya hivyo. Jambo hilo lina athari na faida zake. Nitatoa athari tu ninazofikiria.

Mheshimiwa Naibu Spika, athari ni za kiutekelezaji hasa katika mambo yanayohitaji maamuzi. Mara nyingi Wabunge wengi huilalamikia Serikali kuchelewa kufanya maamuzi mbalimbali. Mimi naona maamuzi mengi huchelewa kwa sababu ya mfano ufuatao: Ndani ya kipindi cha miaka miwili na nusu, aliyeteuliwa kuwa Naibu Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, akawa Naibu Waziri wa Uchumi na Mipango. Baadaye akawa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Bunge), sasa ni Waziri wa Mazingira. Kwa hali hii, kama Waziri huyo alikuta jambo lililohitaji maamuzi, lazima alifahamu kwa kina ndio aamue, lakini inaweza kutokea kabla hajatoa maamuzi akahamishwa; sasa atakayeingia nae lazima alifahamu jambo lile; hivyo hivyo kwa wengine, sasa lazima maamuzi yachelewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, athari nyingine ni za miradi kutoendelezwa. Nina mfano, Bajeti ya 2006/07, Mkoa wa Kigoma uliahidiwa umeme wa Gridi ya Taifa na Mheshimiwa Rais 29 Agosti, 2005. Akautaja Uwanja wa Centre Kigoma na Mbiga itapata umeme. Kwa kutekeleza ahadi hiyo, Mheshimiwa Msabaha, Waziri wa Nishati na Madini wa kipindi hicho, aliliambia Bunge hili Kigoma tutapata umeme wa Gridi ya Taifa na udhamini ulikuwa wa Benki ya Maendeleo ya Afrika *(ADB)*. Alituambia Mradi unatengewa shilingi 10.073,000,000, umeme utakuwa na KV 132 kutoka Tabara hadi Kigoma. Cha kusikitisha, baada ya yeye kuteuliwa kwenye Wizara nyingine, Mradi haukuendelea na wala hatukuelezwa ni sababu zipi za msingi zilizosababisha Mradi huu usiendelee.

Mheshimiwa Naibu Spika, aliingia Waziri mpya, Mheshimiwa Karamagi, naye kipindi cha Bajeti la 2007/08, alikuwa na Mpango Mpya bila maelezo ya Mradi wa kwanza. alikuja na KV 220, *Grid extention* Bulykulu – Geita, *then* upitie Kibondo mpaka Kigoma Mjini. Kwa hiyo, baada ya kumbana kwenye vifungu, ndio tukajibiwa kuwa, Mradi ule wa KV 132, Tabora - Kigoma halikuwa *viable* kwani umeme ni mdogo. Swali langu; hivi mpaka taarifa inaletwa Bungeni, upembuzi yakinifu ulikuwa haujafanyika?

Ilikuwaje Waziri Msabaha atuite Wabunge wa Kigoma wote na akatupa maelezo ya kina na kutuhakikishia Mradi ule utafaa na vilevile tulimwuliza itakuwaje ikiwa *ADB* hawatatoa pesa hiyo; akasema zitatumika za ndani.

Mheshimiwa Naibu Spika, Miradi yote hiyo iliishia kwenye makaratasi. Kwa hiyo, ahadi ya Bajeti ya 2006/07 na 2007/08, imebaki kuwa ni hadithi, sasa tunasikia Kigoma tutapata umeme kutoka Malagarasi chini ya *MCC*. Tunasubiri Waziri Mpya wa Wizara hiyo, atakuja na maelezo gani katika Bajeti yake ya 2008/09. Hii ni athari, kila Waziri kuja na Mradi wake.

Nashauri kuwe na mwelekeo, kwani upembuzi yakinifu unatumia pesa za wananchi na kama mradi haufai, tusiletewe Bungeni na kudanganywa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mabadiliko makubwa ya Baraza la Mawaziri, yalisababisha kupunguzwa kwa Baraza hilo; baadhi ya Wizara ziliunganishwa tena mfano, Mambo ya Ndani na Usalama wa Raia imekuwa moja; hatujaelewa utekelezaji wa bajeti umekuwaje? Idara kama ya Uvuvi kutolewa kwenye Wizara yake na kupelekwa Wizara ya Mifugo; je, utekelezaji wa bajeti utakuwaje?

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo lingine ni tabia ya Serikali, kupiga propaganda juu ya misaada au mikopo; mfano MMEM na MMES zinaitwa za Mkapa wakati ni mkopo kutoka Benki ya Dunia. Lazima wananchi waambiwe ukweli juu ya pesa zao za msaada na za mkopo, kwani zitalipwa kwa kodi zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, tangu nimeingia ndani ya Bunge la Jamhuri ya Muungano, nasikia habari za pesa za *MCC*, ambazo hutolewa kwa nchi za Kimaskini Duniani ili kufikia Malengo ya Milenia. Ndani ya Bunge hili, aliyekuwa Waziri Mkuu alituambia ni matokeo ya safari za Rais, akijibu hoja zilizomwandama Rais kusafiri kila mara nje ya nchi, zilifanya na pesa za *EU*.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa katika Kamati ya Mambo ya Nje, mwaka 2007 Bwana Mchomvu alikuja kutuelezea juu ya pesa za *MCC* na miradi itakayofadhiliwa na *MCC*. Swali nililomwuliza hizo pesa ni nyingine au ndio taarifa ile ile niliyoisikia toka mwanzo wa mwaka 2006?

Akajibu ndio hizo hizo cha kushangaza *sign* imewekwa mwezi Februari, 2008, Rais Bush alikuja, lakini propaganda imepigwa toka 2006. Tuache kuwapa matumaini Watanzania kwa kuwatajia ufadhili wa miradi yao wakati hata *sign* haijawekwa; je, wakighairi kabla ya kuweka *sign,* Serikali itaonekana inasema uongo; hiyo siyo aibu?

Mheshimwa Naibu Spika, nchi yetu ina matatizo mengi, tutafue njia ya kuyakabili. Tunavyo vyanzo vingi vya kutuongezea mapato, tuache kusamehe kodi, Makampuni ya Wawekezaji yanapata faida ndio maana hawaondoki. Tuangalie migodi yetu itatuongezea vipi mapato, bado hatujafaidi kuwa na rasilimali nyingi kama bahari, maziwa, ardhi yenye rutuba, madini na vingine vingi. Tunaweza kujitegemea kwani miradi mingi ya maendeleo inategemea wahisani kwa zaidi ya asilimia 97.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Hotuba ya Bajeti ya Waziri wa Fedha katika ukurasa wa 21 alisema, nanukuu: “Hata hivyo, upo wasiwasi kwamba, msaada na mikopo

kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo, haitapatikana kama ilivyoadhidiwa kutokana na sababu zilizo nje ya uwezo wa Serikali."

Mheshimiwa Naibu Spika, hii ni changamoto, tutafute vyanzo vyetu tutimize miradi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nasikitika, barabara ya Kigoma – Nyakanazi haikutajwa na Mheshimiwa Waziri Mkuu kwenye uk. 28. *Paragraph* ya 40 aliainisha barabara zilizo katika mpango wa ujenzi katika Bajeti ya 2008/09. Nadhani imesahaulika, tunaomba ijengwe kwani ni ahadi ya muda mrefu. Nitaomba jibu, Kigoma tunamatatizo makubwa, tumeandaa Mpango wa *Special Economic Zone* yetu lakini bila kuboresha Miundombinu hatutofanikiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri Mkuu, aingilie kati suala la Reli ya Kati ni aibu. Mwekezaji gani huyo anayeididimiza reli badala ya kuiinua? Tiketi hazipatikani, zinauzwa bei ya kuruka lakini treni inajaa, watoto wanawekwa hadi chini ya viti. Hali ni mbaya, Serikali iingilie kati. Mwaka 2006, Mheshimiwa Mramba kipindi hicho akiwa Waziri wa Miundombinu, alituita Wabunge wa Kigoma akatueleza wanatarajia kupata mwekezaji; *RITES,* ataiboresha lakini ameididimiza. Tumechoka na adha hii. Wenye uwezo wa kupanda ndege ni wachache mno.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika uk. 40, *paragraph* ya 59, Mheshimiwa Waziri Mkuu katika hotuba yake ametoa rai kwa wananchi na kuwaasa kutovamia ardhi, lakini wananchi hawawezi kuvamia ardhi kama watumishi wa Idara ya Ardhi katika Halmashauri zetu, hawatawadanganya na kuwapa vibali vya ujenzi. Hivyo si rahisi mwananchi kujenga bila vibali kutoka ardhi, watumishi nao watazamwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuwe na Mipango Miji tuepuke kero za bomoabomoa na fidia. Tatizo la fidia ni kubwa maeneo ya Kibamba, Dar es Salaam. Wananchi wanalalamika fidia ni ndogo, haiendani na mali, ukubwa wa ardhi na nyumba zao. Vile vile Serikali ifuatilie Mkoa wa Mara, nyaya za umeme zinapitishwa eneo la Musoma mpaka Tarime, *Nyamongo Gold Mine.* Maeneo ambayo umeme/nyaya hizo zinapita, wananchi wanatakiwa kuhama, lakini Diwani wao anadai yeye wala wananchi hawakushirikishwa; rejea kipindi cha kumekucha cha *ITV* tarehe 23 Juni, walionyesha mahojiano hayo. Tatizo kubwa, Mikataba ya Mahakimu wa Ardhi imekwisha, wananchi Kigoma wanateseka. Zipo taarifa kuwa, hili ni tatizo kubwa nchi nzima. Hakimu wa Ardhi wa Wilaya ya Kinondoni ndiye anayekata kesi za Kilimanjaro pia. Waziri Mkuu, atoe agizo kuhusu kuwapatia mikataba Mahakimu wa kesi za Ardhi ili kuondoa usumbufu na kusubiri kwa muda mrefu kesi zao kusikilizwa. Serikali ituambie inatumia vigezo gani kutoa mikataba hiyo na iharakishe wananchi wanateseka.

Mheshimiwa Naibu Spika, natarajia majibu wakati Waziri Mkuu akijibu hoja zetu.

**MHE. MARIAM S. MFAKI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naanza kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu, Waziri wa Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Naibu Waziri na Watendaji wa Wizara, wakiongozwa na Makatibu Wakuu wote wawili. Hotuba hii imezingatia maslahi ya wananchi kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuchangia yafuatayo:-

Suala la chakula ni muhimu kama alivyoeleza Mheshimiwa Waziri Mkuu na kuonyesha kwamba, Serikali imetenga Sh. 26.3 milioni, ambazo zitatumika kununua mahindi tani 100,000 na mtama tani 5,000 na kwa msisitizo kuwa chakula hicho kitanunuliwa kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri Mkuu, akifuatilie kitengo hicho cha maafa/ununuzi kwa karibu kwani kwa Mkoa wa Dodoma, sasa hivi maeneo mengi wameanza kuvuna na walanguzi wameanza kununua. Naomba Mpango huu uanze sasa kwa kushirikiana na Wakuu wa Mikoa. Naiomba Serikali ifanye uamuzi mapema na itoe fedha bila kuchelewa, vinginevyo, walanguzi watanunua na baadaye kuwauzia wananchi kwa bei kubwa na wakati huo wananchi hawatamudu kununua. Tahadhari ni kwamba, mavuno mwaka huu sio mengi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Serikali kwa kutenga fedha za kukamilisha upembuzi yakinifu ili hatimaye Barabara za Dodoma - Iringa na Dodoma – Babati ziweze kujengwa. Tunaomba usanifu ukamilike na kazi ya kujenga ianze.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Serikali kwa kuboresha maslahi Madiwani na naomba Wenyeviti wa Vijiji na Serikali za Mitaa nao wapewe posho, hali ya uchumi inaonekana inakuwa nzuri mwaka hadi mwaka. Sababu za kuwapa posho ni kuwawezesha.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ni vizuri ikatueleza kwa nini imeamua kuanzisha mjadala wa kuamua Makao Makuu ya Serikali yaendelee hapa Dodoma au sio? Vilevile ningependa kujua mjadala huu umepangiwa muda gani, pamoja na sheria hiyo inayotegemewa kutungwa?

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la Kilimo ni muhimu na kilimo hiki tulichonacho ni cha wakulima wadogo wadogo, ambao ndio wengi au hawana mtaji wa kununua matrekta ili yawasaidie.

Naiomba Wizara, badala kutumia fedha nyingi kwa semina, mikutano na mashamba darasa, zitumike kununua matrekta, matipa ya kusomba mbolea ya kumwaga mashambani na kwenye mitaro ya zabibu. Hii ingeweza kuleta tija kwa wananchi wengi na Serikali ingefaidika kwa wananchi hawa kufaidika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inao mkakati wa kuwashawishi wakulima wakubwa ili waanzishe mashamba makubwa. Naomba niishauri Serikali iwahamasishe wasomi waunde ushirika wa wakulima na wafugaji ili waweze kuzalisha chakula cha kutosha na mifugo bora ili wawauze, wananchi nao waweze kubadili mifugo yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Bajeti ya Maji isifutwe tena katika kipindi cha bajeti nyingine, kwani maji ni muhimu kwa viumbe hai vyote.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii asilimia mia kwa mia.

**MHE. EPHRAIM N. MADEJE:** Mheshimiwa Naibu Spika, pongezi zimfikie Waziri Mkuu, Mawaziri na Naibu Waziri, Katibu Mkuu na wale wote waliohusika na utayarishaji wa Bajeti na Hotuba hii nzuri.

Kwanza, naipongeza Wizara kwa kuweka mikakati ya kushughulikia matatizo ya kiutawala na miundombinu. Pili, naipongeza kwa kutambua umuhimu wa kuelekeza juhudi mahususi katika uendelezaji wa Mji wa Dodoma ili kuepuka matatizo yaliyojitokeza kwenye miji mingine kwa mfano, Dar es Salaam.

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wachache sana Dodoma Mjini wamenufaika na uwezeshaji wa wananchi kiuchumi. Hakuna hata mmoja kutoka kwenye Vijiji vya Wilaya ya Dodoma Mjini ambaye amepata mkopo huo na hakuna utaratibu uliowekwa kuwaingiza/kuwafikia Wanavijiji hao katika utaratibu mpya uliowekwa kuwalenga wakulima. Naomba wakulima hawa nao wapewe fursa hiyo.

Kuendelea kupuuza ujenzi wa Barabara ya Iringa – Dodoma - Babati kwa kiwango cha lami ni kujiumiza kiuchumi. Barabara hii ni Kongwe, ya Ki-mataifa *(Great North Road)* na Itasaidia sana *Economic Intergration* ya Mikoa ya Kusuni na Ile ya kaskazini ambayo ina shughuli nyingi sana za kiuchumi.

Kwa nini Baraba ya Ihumwa - Hombolo - Gawaye - Mayamaya hijaingizwa kwenye orodha ya barabara za Mkoa, pamnoja na kukidhi vigezo vyote? Barabara hii inaunganisha barabara kuu za Mogorogo - Dodoma na ile ya Dodoma - Arusha. Aidha, barabara hii inapita Hombolo ambapo kimejengwa Chuo cha Serikali za Mitaa cha Hombolo.

Mheshimiwa Naibu Spika, sikubaliani na suala la kuanzisha mjadala kuhusu Serikali kuhamia Dodoma kwa sababu zifuatazo: Mjadala ulikwishafanyika; ni Sera ya CCM kuhamishia Serikali Dodoma; na ni Sera ya Serikali kuhamishia Serikali Dodomana hata Wapinzani wanakubaliana.

Suala la kutunga sheria ni la kiutendaji na ni muhimu litekelezwe kama tulivyoahidi kwenye Ilani ya Uchaguzi. Mjadala pekee uwe ni wa kuwashirikisha wadau wote (hasa Manispaa ya Dodoma).

Ujenzi wa Maofisi na Nyumba za Serikali sasa uelekezwe Dodoma. Ni dhihaka kubwa kwa Serikali kuendelea kuimba wimbo wa kuhamia Dodoma na wakati huo huo, Serikali inatumia mabilioni katika ujenzi wa maofisi na nyumba za kukaa Mawaziri na Maofisa Dar es Salaam. Kwa maeneo mengine, Serikali inajiumbua yenyewe mbele ya wananchi wake!

Malalamiko ya Wananchi wa Dodoma Mjini dhidi ya utendaji wa baadhi ya Watendaji wa *CDA* hivi sasa yamekithiri. Eneo linalolalamikiwa sana ni katika upimaji na ugawaji wa viwanja; ni muhimu Ofisi ya Waziri Mkuu ichukue hatua kuchunguza hali hii, kwani panapofuka moshi hapakosi moto. Kuna umuhimu wa kuwashughulikia baadhi ya wafanyakazi, ambao wamekuwa wakilalaminiwa na wananchi. Inasemekana kutokana na wafanyakazi hawa kuwepo kwa miaka mingi, hivi sasa wamejenga kiburi, jeuri hata dharau kwa wale wanaowatumikia. Hatua zichukuliwe kuwaondoa watu hawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya ya Dodoma Mjini ina sura mbili; eneo la Mji Kati ambalo linahudumiwa na *DUWASA,* hakuna shida ya maji; na eneo la Vijiji visivyopoungua 40, ambavyo vingi vina matatizo makubwa ya maji. Idadi ya Vijiji 10 vimo kwenye Mradi wa *Rural Water and Sanitation Project.* Ahadi za Serikali kwa wananchi chini ya mradi huu, zimeleta matumaini makubwa kwa wanavijiji hao, lakini utekelezaji wake duni sasa unawakatisha tamaa. Naomba Serikali iongeze kasi katika kutekeleza Miradi hii vinginevyo, hali yetu itakuwa ngumu sana mwaka 2010.

Wilaya haina Mhandisi wa Maji na hili linaathiri utekelezaji wa Miradi; irekebishwe.

Naomba vijiji vyote vinavyopitiwa na nguzo/*line* ya *National Grid*, vipatiwe umeme kama tulivyoomba kwenye Wizara ya Nishati na Madini (Nkulabi, Mpunguzi, Matumbulu, Nala, Chigongwe na Msembeta).

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, ninaunga mkono hoja.

**MHE. FRED T. MPENDAZOE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nilipochangia kwenye hoja ya Waziri wa Fedha, nilielezea juu ya masuala yafuatayo:-

Katika Ripoti ya Mkaguzi Mkuu, upande wa Hesabu za Serikali za Mitaa, kiasi cha fedha zaidi ya shilingi bilioni saba kilitolewa na Serikali Kuu hazikutumika kwenye Halmashauri. Huu ni ushahidi kwamba, Miradi ya Maendeleo haikutekelezwa. Sababu zilizosababisha ni pamoja na upungufu wa wataalam na ugumu wa uibuaji wa Miradi kutokana na tatizo kubwa la kutofanyika kwa mikutano Vijijini.

Kuhusu suala la upungufu wa wataalam, niliomba Serikali itoe kipaumbele kutatua suala la upungufu wa wataalam Wilaya ya Kishapu, yenye upungufu wa wataalam 344. Je, Serikali inatatuaje tatizo hili?

Pia moja ya sababu za uibuaji hafifu wa Miradi ni kutokana na ukubwa wa Vijiji, Kata na Tarafa. Wilaya ya Kishapu ina Vijiji vingi ambavyo ni vikubwa, niliomba Serikali itoe kipaumbele kwa Wilaya ya Kishapu, ambayo tayari imepeleka maombi ya kugawanya Vijiji na Kata ambazo ni kubwa sana; Je, Serikali itaharakisha ugawaji wa Vijiji ambavyo ni vikubwa?

Nilipochangia pia nilieleza kwamba, katika Ripoti ya Mkaguzi Mkuu ilionyesha kwamba, Miradi ya Maendeleo yenye thamani ya shilingi bilioni sitini ilichelewa kukamilika. Kuchelewa kukamilika kwa miradi hiyo, kunawavunja moyo wananchi. Sababu zilizosababisha ni pamoja na kutopatikana kwa michango ya wananchi.

Wananchi hawakatai kuchangia, lakini utaratibu mbovu wa michango, ndiyo tatizo. *VEOs* na *WEOs,* hawasomi mapato na matumizi ya michango. Pia kuna ubadhirifu mkubwa wa michango; je, Serikali imechukua hatua gani juu ya *VEOs* na *WEOs* wa Wilaya ya Kishapu na Halmashauri nyingine, ambao wameonekana hawasomi mapato na matumizi ya michango iliyopata? Wilayani Kishapu kuna tatizo la kutosoma mapato na matumizi kwenye Kata nyingi na Vijiji vingi, naomba Serikali ifuatilie.

Ripoti ya Mkaguzi Mkuu wa Serikali pia imeeleza kwamba, baadhi ya Halmashauri hazitekelezi mapendekezo yaliyotolewa na Mkaguzi wa Serikali. Je, Ofisi ya Waziri Mkuu imechukua hatua gani mpaka sasa?

Ripoti ya Ukaguzi pia imeeleza kwamba, Serikali haizingatii bajeti iliyoidhinishwa na Bunge. Kumekithiri uhamishaji wa fedha kati ya vifungu na uchukuaji wa fedha kwenye benki zaidi ya zilizopo; je, Serikali imechukua hatua kwa Watendaji wangapi na ni Wizara zipi zilizoongoza katika tatizo hili?

Ukaguzi pia umeonyesha kwamba, kuna utunzaji hafifu wa taarifa unaoonyesha Deni la Taifa. Je, Serikali inachukua hatua gani kwa Watendaji katika kitengo kinachohusika na utunzaji wa Deni la Taifa?

**MHE. KHERI KHATIB AMEIR:** Mheshimiwa Naibu Spika, huu ni mwaka wa saba tangu kuwepo kwangu Bungeni ni kwa mara ya kwanza Hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, kugusia mambo ya Zanzibar angalau kwa kurasa zaidi ya tatu. Ni Hotuba makini na imegusa karibu kila eneo la nchi yetu.

Nampongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu, pamoja na Waheshimiwa Mawaziri, Katibu Mkuu na Watendaji wake wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama ujuavyo, mawazo ni kuchangiana, kwa hiyo basi, kuna sehemu ndogo ndogo na mimi nataka kuzigusia:-

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi sikuridhika kabisa fungu la bajeti liliyopewa Sekta ya Kilimo; asilimia sita ni kidogo sana, hasa tukifikiria kuwa mbele huko kuna tatizo la njaa inayoikabili dunia sio Tanzania tu. Tanzania tumekuwa na tatizo la ukame

katika kila kipindi cha kati ya miaka 4 – 6. Matatizo haya yanapojitokeza, huwa utanunua chakula kutoka Mataifa makubwa au hata kupatiwa msaada. Hivi sasa tahadhari zote zinatolewa, kwa tahadhari ya tatizo la chakula litakaloikabili dunia miaka ijayo hasa katika Afrika Kusini mwa Jangwa la Sahara na Tanzania ikiwemo; baya zaidi nchi zinazotusaidia au kutuuzia wao wenyewe wanazuia chakula kisiuzwe nje ya nchi zao; Watanzania tunafanya nini?

Kama hatutafanya jitihada za makusudi njaa itatumaliza. Tumeshuhudia wakati fulani, kuzika mizoga ya mifugo, safari hii tutazika mizoga ya watu (binadamu), chonde chonde bajeti hii ya kilimo iongezwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania ina uchumi wa kijiografia; kwa kutumia bandari zetu, Bandari ya Dar es Salaam ni kitovu na kielelezo cha kwanza cha uchumi wetu. Serikali ijitahidi kuona tunatumia ipasavyo zawadi hii tuliyopewa na Mungu. Hata hivyo, nakubaliana na rai inayotolewa ya kuimarisha bandari zetu hizi tatu; Dar es Salaam, Tanga na Mtwara. Usisahau kuwa, Bandari ya Zanzibar inahitajika sana kuwepo katika mpango huo.

Zanzibar ni sehemu ya Tanzania, kuendelea kushushia mizigo Kenya na kuileta Dar es Salaam ni uchache wa mawazo na busara haikutumika. Shusheni mizigo Tanga au Zanzibar, kwa ile mizigo iliyo kwenye Kanda ya Kaskazini; Dar es Salaam na Mtwara kwa ile mizigo iliyoko Kanda ya Kusini. Hili litasaidia sana kuleta ajira kwa wananchi wetu na litapunguza umaskini.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi yule mshauri mwelekezi amefikia hatua gani; mbona muda mwingi umepita, tatizo ni nini? Nashauri kama hili linaonekana gumu kwa nini hatuwatumii wataalam wetu wa hapa nchini kufanya kazi hiyo? Mheshimiwa Waziri Mkuu, tunakuomba hili ulifanyie kazi.

Tunapongeza hatua nzuri iliyofikiwa ya uchimbaji wa gesi Songosongo na tunapongeza Mpango Kabambe uliopangwa ili kusaidia uchumi wa Tanzania. Wazo la kutumika kwa gesi kuendeshea magari, kusaidia nishati ya kupikia na hata kuwauzia nchi jirani;i ni mpango mahususi wa kupongezwa. Ninashauri twende mbele zaidi ya hapa kwa uchimbaji na utafutaji, faraja ipo karibu na tutafanikiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunapokea kwa furaha msaada huo wa shilingi bilioni nne, fedha za *MCC* zilizoelekezwa kwa Miradi ya Zanzibar. Tumeelezwa katika taarifa aliyoitoa Naibu Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Omar Yussuf Mzee kuwa, kuna Miradi ya Barabara kama minne au mitano imeelekezwa Pemba; je, ni miradi gani imepelekwa Unguja na ni ipi?

Tunapongeza *TRA,* kwa dhati kabisa, kwa kazi nzuri wanayoifanya ya kukusanya mapato na kusaidia ukuaji wa Maendeleo Tanzania. Kukusanya zaidi ya milioni Sh. 330 kwa mwezi katika miaka hii ya 2006/07, kutoka makusanyo yaliyokuwa yanapatikana

katika miaka ya tisini ya bilioni 28 – 36 ni jambo la sifa kwa *TRA* na la kupigiwa mfano. Tatizo na doa kubwa walilonalo *TRA* ni kutoitendea haki Zanzibar na hilo halisameheki. Vipi Mheshimiwa Waziri Mkuu, hali hii itokee ya kusamehe asilimia 96 kama misamaha na pakusanywe asilimia nne tu ya makisio ya makusanyo.

Tatizo liko wapi; kwa nini *TRA* imeacha mwanya mkubwa hivi. Hii ni dalili inayoashiria rushwa. Tunataka maelezo ya kina, atakapokuja Mheshimiwa Waziri Mkuu, kufunga hoja yake hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. Ahsante.

**MHE. DORAH H. MUSHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa, namshukuru Mungu kwa kunipa uzima.

Pili, nampongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu na Mawaziri wake wote, pamoja na Wataalam wake, kwa Hotuba yao nzuri waliyoiwasilisha hapa Bungeni. Bila kuisahau Serikali yetu kwa uamuzi wake mzuri wa kuondoa kodi kwenye mafuta, ambayo imejibu kero mbalimbali za wanyonge ambao kipato chao ni cha chini.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nianze na suala la kilimo. Kwanza, ninamshukuru Mwenyezi Mungu, kwa sababu ametupendelea sana kutupa maeneo makubwa na ardhi yenye rutuba nzuri, lakini Watanzania hatuzingatii kilimo. Tunakimbilia biashara, vijana wengi wamekimbilia mijini kufanya biashara; wameacha mapori hayana kazi. Miji wanayoikimbilia ni Dar es Salaam ambako kuna msongamano wa watu na magari; vurugu tupu.

Mheshimiwa Naibu Spika, wazazi wetu hawakujua kufanya biashara nyingine yoyote isipokuwa kilimo. Maisha yetu yaliendeshwa na kilimo na tumesomeshwa na kilimo; kwa nini tunasahau tulikotoka? Kilimo ni uti wa mgogo wa Taifa letu. Tulihamasisha kujenga madarasa na zahanati na sasa tuhamasishe kilimo. Tunaomba Serikali iagize zana zote za kilimo ikiwa ni pamoja na matrekta, dawa za kuulia wadudu, mbolea na itufikie kwa wakati unaotakiwa.

Vilevile ianzishwe Benki ya Wakulima Vijijini; elimu ya Kilimo Bora itolewe, Elimu ya Ujasiriamali itolewe pia kwa vijana na akina mama kwa kuwa wakulima wengi wapo Vijijini. Mazingira mazuri yanaandaliwa ili kuwavutia wawekezaji wengi wa ndani na wa nje. Kwa kufanya hivyo, tutahamasisha watu wengi kupenda kilimo ikiwa ni pamoja na wafanyakazi, vijana, wafanyabiashara na hata wanasiasa. Hapo ndipo tutakapopata chakula cha kutosha na kingine tutakiuza nje ya nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkoa wa Manyara tunalima mazao mengi ya biashara na chakula, lakini barabara za kuunganisha Kata hadi Kata, Kijiji hadi Kijiji ni mbovu sana. Namshukuru Waziri Mkuu kwa kuongeza fungu la matengenezo ya barabara hizo kwenye Bajeti za Halmashauri. Matumaini yangu ni kuwa, Waheshimiwa Madiwani watatimiza wajibu wao kwa kuzisimamia vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, Barabara ya KIA - Mererani inatia aibu kwa wageni wanaotembelea Mererani kuona eneo hilo linalochimbwa *Tanzanite.* Pili, inachafua na kuharibu Mazingira ya Uwanja wa Ndege wa Kilimanjaro kwa sababu inapita pembeni kidogo ya uwanja huu.

Tatu, waathirika wakubwa wa barabara hii ni wanawake wajawazito na watoto wachanga. Ikitokea tatizo wakati wa kujifungua, mama huyo au mtoto kuwahishwa Hospitali kubwa kama *KCMC* au Mount Meru, barabaa hii haipitiki, inabidi mama apoteze uhai. Vifo vingi sana vya akina mama vimekuwa vikitokea na hakuna msaada wowote. Mimi binafsi, nilimpoteza mtoto wa ndugu yangu, alijifungua mapacha na kupoteza damu nyingi. Tukiwa kwenye harakati za kumpeleka Hospitali, alifariki dunia mikononi mwangu. Kauli ya kujenga barabara hii kwa kiwango cha lami ilikwishatolewa na Rais wa Awamu ya Tatu na vilevile wa Awamu ya Nne. Shida iko wapi? Tunaomba barabara ya KIA - Mererani ijengwe. Suala hili nimelizungumzia toka mwaka 2006 – 2008; nakaribia kumaliza kipindi cha miaka mitano; je, nitakuwa mgeni wa nani.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kila mwaka nikisimama nazungumzia barabara hii. Hakuna kinachoendelea, mpaka wapiga kura wetu wanasema Wabunge wa Viti Maalum hawasikilizwi. Nawaombeni hakikisheni tunasikilizwa kwa kujenga barabara hiyo. Kwa kuwa lengo la Serikali lilikuwa kupunguza idadi ya wasiokuwa na ajira kutoka asilimia 12.9 hadi 6.0 ifikapo 2010; kwa kuwa ndio mwisho wa MKUKUTA; Serikali ifanye jitihada za makusudi ili kuwavutia wawekezaji wengi wa nje na wa ndani. Itolewe elimu ya ujasiriamali kwa vijana na akina mama na pia waweze kuwatengenezea mazingira bora ili waweze kukopeshwa au kupewa mikopo na hatimaye kujiajiri wenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. HAMZA A. MWENEGOHA:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchukua nafasi hii, kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa hotuba nzuri sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni vyema nikaanza kuzungumzia Wilaya ya Morogoro Vijijini, ingawa Wilaya ni ya Vijijini, Makao yake Makuu yapo Morogoro Mjini. Baraza la Mogorogo Vijijini limeamua kwamba, Makao Makuu yawe Mvuha (Km 89).

Vyombo vya kuhama ni Halmashauri yote, Mheshimiwa *DC* atabaki Morogoro, kwani yeye mmoja anaweza kuhudumia Halmashauri na Manispaa bila matatizo. Tunaiomba Serikali itupe msaada wa kujenga Wilaya na Hospitali ya Wilaya.

Pamoja na ombi hilo, ninaleta ombi la ugawaji wa Wilaya katika Majimbo matatu. Mheshimiwa Waziri Mkuu, Wilaya hii ina eneo kubwa sana na lina jiografia mbaya, kwa jinsi milima mikubwa na mikali ilivyokuwa pingamizi kwa maendeleo inakuwa vigumu kwa Mbunge kutembelea Jimbo zima kwa mwaka. Hii ni kutokana na ukweli kwamba, maeneo mengi Mbunge analazimika kutembea kwa miguu toka Kijiji kimoja hadi kingine kwa kuwa hakuna barabara za kuunganisha Vijiji hivi; na Makao Makuu ya Kata nyingine hayafikiki kwa gari. Hivyo mbunge anawajibika kutembea

huko kwa miguu. Hivyo basi kuigawa Wilaya katika Majimbo matatu kutawapunguzia wabunge adha ingwaje haitakwisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo nina wajibu wa kulizungumzia ni Umeme Jimboni. Jambo la kwanza ni masikitiko makubwa, ambayo yamesababishwa na Uongozi wa *TAZARA.* Rais alipokuwa kwenye kampeni, Wananchi wa *Kisaki Station* waliomba ile jenereta kubwa ya *Kisaki Station* iweze kuwapatia umeme angalau pale Kijijini kwa kulipia. Kwa mshangao mkuwa, Uongozi wa *TAZARA* nilipowafuatilia, waliondoa lile jenereta kubwa na kupeleka jenerata dogo kabisa. Mheshimiwa Waziri Mkuu, kitendo hiki cha kushangaza sana, halafu wanaomba wananchi hawa hawa washiriki kwenye ulinzi wa reli yao ya *TAZARA!* Mheshimiwa Waziri Mkuu, tunaomba sana tena sana; *TAZARA* warudishe lile jenereta ili Wananchi wa *Kisaki station* nao wapate umeme wa kulipia.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikiendelea kuzungumzia suala la umeme, naomba kwanza, niishukuru Serikali kwa kutumia pesa za MCC kuvuta umeme hadi Matombo. Pamoja na shukrani hizo, napenda niiombe Serikali ipeleke umeme hadi Mvuha. Hapa ni urefu wa Km. 16 toka Kangazi, ulipoishia umeme kupimwa. Hali kadahlika, hapa ndiyo Makao Makuu ya Wilaya ya Morogoro Vijijini. Hapa Mvuha ndipo tunatarajia kujenga Hospitali ya Wilaya, Makao Makuu ya Halmashauri ya Morogoro Vijijini, Polisi Stesheni, ujenzi wa Mahakama ya Wilaya na kadhalika, kuwepo na umeme kutafanya Taasisi nyingine nazo zikue.

Mheshimiwa Naibu Spika, wawekezaji wa mashamba ya miwa wamepatikana, lakini bila umeme wao hawawezi kufanya jambo lolote la kuwekeza. Tunahitaji umeme kuanzia Matombo ili upitie Mvuha, Duthumi, Mngazi na Kisaki. Umeme utapeleka maendeleo na kuzuia vijana wasihame toka Vijijini kwenda Mijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nizungumizie Bwawa la Kidunda. Historia ya Bwawa hili ni ndefu sana; tangu mwaka 1959 lilianza kuingia kwenye Mipango ya Serikali ya kulijenga Bwabwa hili. Hatua zilionyesha matumaini ya ujenzi, lakini hivi sasa matumaini yamekatika kwani pesa za *MCC* hazipo katika mipango ya maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, watu wa Kata ya Selembala wamehamasishwa maendeleo kwa muda mrefu, sasa ni zaidi ya miaka miwili watu hawa wameambiwa wasiendeleze kitu chochote. Hivyo, hawalimi, hawajengi, hata Miradi ya *TASAF* ya Serikali imesimama hadi leo. Wananchi hawa sasa hawajui wafanye nini; ni vyema sana kama Serikali ingewaamulia jambo moja; kuwahamisha ama kuwaambia wabaki ili wafufue matumaini yao ya maendeleo. Watu hawa wana haki ya kuambiwa wazi hali halisi ilivyo sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuzungumzia Ahadi za Rais katika Wilaya ya Morogoro Vijijini. Wakati wa kampeni na wakati wa kushukuru, Mheshimiwa Rais aliahidi kwamba, Barabara ya Ubena – Ngerengere – Kiganila - Mvuha - Kisaki ingekuwa barabara ya changarawe na kupitika mwaka mzima. Hali kadhalika, pale ambapo alivuka chini, kwenye Mto Ruvu, Kijiji cha Kiganila, pangejengwa daraja.

Mheshimiwa Naibu Spika, daraja hili sasa ni muhimu sana kwa vile litawaunganisha watu wa Kidunda, Mkulazi na Ngerengere na kuweza kufika Makao Makuu ya Wilaya kwa urahisi zaidi na haraka zaidi. Hali kadhalika, daraja hili litarahisisha watu wa Selembala kuepuka kushambuliwa na mamba, hasa wakati bwawa litakapokuwa limejengwa. Daraja hili litarahisisha usafiri wa watalii kutoka Dar es Salaam kwenda *Selous Game Reserve* na kurudi. Hali kadhalika, wale wasafiri wa kawaida watafupisha safari zao za Dar es Salaam badala ya kupitia Morogoro.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii.

**MHE. DAMAS P. NAKEI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Waziri Mkuu na Mawaziri wote wa ofisi yake, kwa kazi nzuri wanazofanya na kwa Hotuba nzuri ya Bajeti, yenye matumaini makubwa kwa wananchi.

Naomba niseme tu kwa ujumla, nchi yetu inayo changamoto kubwa ya kuboresha hali ya uchumi na uondoaji umaskini. Naishauri Serikali, ihakikishe ujenzi wa uchumi wa nchi ni kipaumbele namba moja. Hii inahitaji Serikali kujizatiti *(committed)* kwa hali ya juu. Sote tujitahidi, kwa ushirikiano tutimize wajibu wetu

Mheshimiwa Naibu Spika, tunazo fursa nyingi *(opportunities)* katika maeneo mbalimbali; tunao utajiri wa madini, utalii na ardhi ya kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati umefika kama siyo kupita wa Serikali kuweka nguvu zake zote katika ujenzi wa barabara nchini. Bado tupo nyuma sana katika eneo hili la barabara. Serikali iwekeze katika barabara kwa gharama yoyote ile kuhakikisha barabara zote zinakuwa za kudumu na za lami. Barabara nzuri na za uhakika ni msingi muhimu katika kuondoa umaskini na kujenga uchumi. Uwekezaji katika maeneo mengine yoyote, unaguswa na miundombinu ya barabara. Nchi zote zilizoendelea; nenda Japan, America, Uingereza, Urusi na kadhalika, ishara ya nje ya kwanza unayoona kuwa ni nchi iliyoendelea ni barabara nzuri za hali ya juu. Mfano wa barabara mbovu au miundombinu mibovu ni Jiji la Dar es Salaam ni adha iliyoje na athari kiasi gani katika uchumi?

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, napenda kuipongeza na kuishukuru Serikali kwa ujenzi wa Barabara ya Minjingu – Babati – Singida kwa lami. Wakati wowote ujenzi unaanza; kwa kuwa ujenzi huu sasa unaanza utahusisha kazi kubwa ya uchimbaji wa udongo na changarawe *(earthworks),* kutakuwa na mashimo makubwa yaliyochimbwa njia yote.

Napenda kushauri kuwa, kuwepo mawasiliano ya kikazi kati ya Waziri wa Miundombinu na Waziri wa Maji ili pale inapowezekana (kuwa na *catchment* nzuri), mashimo yale ya changarawe *(borrowpits),* yaweze kuboreshwa na kuwa mabwawa au malambo ya maji kwa ajili ya mifugo na matumizi mengine hususan katika *stretch* ya Minjingu hadi Magugu na Babati. Hii inasaidia katika suala zima la *economies of scale* kwamba, tunapata barabara (*materials* zake) na bwawa la maji kwa ajili ya mifugo yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo ningependa kulisema ni kwamba, nchi yetu imebahatika kuwa na fedha za *millennium challenge*, lakini katika Jimbo langu la Babati Vijijini sijaona ni katika eneo gani nasi tunanufaika?

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la uongozi kuwa karibu na wananchi kuhusiana na ukaribu wa maeneo ya utawala; je, Serikali ina mpango gani au imefikia wapi katika maombi tuliyotoa Serikalini kuhusu kugawa Vijiji, Kata, Tarafa katika Jimbo la Babati Vijijini? Pia kulikuwa na maombi ya kugawa Jimbo la Babati Vijijini kuwa Babati Magharibi na Babati Mashariki, tumepitia hatua zote; Halmashauri na *RCC* ya Mkoa wa Manyara. Sasa ni hatua gani imefikiwa?

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ambalo ningependa kulizungumzia ni kuhusu migogoro mbalimbali. Kwanza, kuhusu Kiwanda cha Mbolea cha Minjingu. Tunaishukuru Serikali kwa hatua ya kuifanya Kiwanda hiki kuwa tegemeo kwa Serikali ili kiweze kutosheleza mahitaji ya mbolea nchini. Hapa pana tatizo la mipaka na mahusiano yanayohitajika ya ujirani mwema. Tunapenda pia tupate taarifa ya tathmini ya athari za mazingira *(Environmental Impact Assessment),* hususan kwa ajili ya kutunza mazingira. Je, Kiwanda kinazingatia matakwa ya kimazingira?

Mpaka wa Mkoa wa Manyara na Mkoa wa Arusha bado kuna utata wa ni wapi hasa mpaka ulipo. Tunaelekea kwenye Uchaguzi wa Serikali za Mitaa; je, Vijiji husika Mswakini, Olasiti na kadhalika, vitakuwa wapi? Serikali itusaidie kufikia uamuzi. Mpaka wa Vijiji vya Ayamango, Gedamar, Gijedbung na Tarangire – *TANAPA.* Hapa kuna mgogoro kati ya Vijiji tajwa na Hifadhi ya Taifa ya Tarangire. Naomba *TANAPA* irejee nia njema ya mazungumzo na pande zote husika ili kufikia ufumbuzi kwani kila mmoja hapa; Serikali na Wananchi ni wahusika wakuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hayo, naunga mkono hoja hii ya Ofisi ya Waziri Mkuu na Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa. Ahsante.

**MHE. ISSA KASSIM ISSA:** Suala la *Organization Islamic Conference (OIC),* lilizungumzwa sana wakati Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ilipoonyesha dhamira ya dhati ya kujiunga na Umoja huo, kwa maslahi ya kiuchumi; kwa sababu nchi Wanachama wa Umoja huo ni nchi huru zenye mamlaka kamili, yaani *(Sovereign State)*, uamuzi ulikuwa kwamba, Zanzibar haiwezi kujiunga peke yake lakini utafiti ufanywe kuona uwezekano wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kujiunga na Umoja huo.

Swali langu kwa Waziri Mkuu ni je, ule utafiti ulifikia wapi au maamuzi yale ya kufanya utafiti ilikuwa mbinu ya kuiua hoja ili Zanzibar mbali na neno "Kiislam" katika jina lake; Umoja wa *OIC* unajishughulisha zaidi na masuala ya uchumi na maendeleo ya nchi Wanachama wa Umoja huo. Nchi nyingi haziwezi kuitwa za Kiislam kwa mujibu wa Katiba za nchi hizo na mchanganyiko wa watu wenye imani totauti za kidini. Mfano mzuri ni nchi jirani yetu ya Uganda; ambayo ni Mwanachama kamili wa *OIC* na siku chache zilizopita, ilikuwa wenyeji wa Mkutano wa Wakuu wa Nchi za Umoja huo. Sio siri kuwa Zanzibar hivi sasa inakabiliwa na hali ngumu ya uchumi na hasa baada ya

kuanguka kwa Zao la Karafuu. Suala la *OIC* ni moja ya kero inayowaudhi sana Wazanzibari miongoni mwa kero za Muungano. Wenzetu Tanzania Bara mnavyo vyanzo vingi vya kiuchumi na Mapato ikilinganishwa na Zanzibar, pengine ndio sababu Serikali ya Jamhuri ya Muungano haioni haja ya kujiunga na *OIC*.

Wenzetu wa Zanzibar wanaona haja hiyo, tatizo ni nini Zanzibar wasiachwe wakajiunga na Umoja huo kwa maslahi ya kiuchumi. Naomba maelezo kutoka kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa maswali mawili; Je, ule utafiti ambao uliahidiwa ulifikia wapi? Je Ugumu ni nini au uko wapi kuiachia Zanzibar kujiunga na Mradi huo kwa sababu ikienda huko inapeperusha Bendera ya Tanzania? Naomba majibu Mheshimiwa Waziri atakapotoa majumuisho.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante na naunga mkono hoja kwa asilimia mia kwa mia.

**MHE. MAGALLE J. SHIBUDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, napenda kutumia fursa hii kupongeza maelezo yote ya Hotuba ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa Mizengo Peter Pinda.

Mimi nayaunga mkono maelezo yote ya Hotuba kwa hoja ya mapitio na mwelekeo wa kazi za Serikali na Makadirio ya Matumizi ya Fedha ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa na Ofisi ya Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, dhamira ya makadirio haya ni kufaulisha ustawi wa maendeleo ya jamii, kuhimiza uchumi endelevu na uwajibikaji makini. Yote haya ni uwajibikaji wa kusaka maisha bora kwa Watanzania wote. Jambo ambalo ndio dhamira ya Serikali ya Awamu ya Nne, pamoja na imani ya Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa dhamira ya Serikali ni ustawi na maendeleo ya jamii, kuendeleza uchumi na kufaulisha uwakilishi makini wa Bunge. Kwa kuwa Mbunge muda mwingi yupo katika kutekeleza majukumu ya Bunge katika fursa mbalimbali na ni muhimu atambue vikao vya Madiwani vyote kwa wakati muafaka na bila kubuni ili afikapo Bungeni asiulize suala la kuambiwa akaiulize Halmashauri yake.

Je, huu sio wakati muafaka na ni hatua endelevu ya kujenga ufungamano wa mawazo na kujenga mawasiliano hai kama sasa Makatibu wa Wabunge wataruhusiwa kuhudhuria Vikao vya Kamati za Madiwani za Halmashauri kwa niaba ya Mbunge wa Jimbo, kama Viongozi wengine wa Taasisi na Serikali ambayo huwakilishwa na mwakilishi kulipwa posho ya yule anayemwakilisha.

Naomba ombi hili litambue kuwa, Bajeti ya posho ya malipo kwa Mbunge daima ipo hivyo. Katibu kupokea badala ya Mbunge ni uendelevu wa kuboresha thamani ya Bunge na Ofisi ya Mbunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Wilaya ya Maswa ni moja ya Wilaya ambazo zina tatizo la Watendaji kutosoma mapato na matumizi ya michango ya

wananchi; na kwa kuwa hii ni kero ambayo inavunja ari ya hamasa ya wananchi kuchangia; na kwa kuwa ndani ya Serikali Kuu pana Sheria ya Kustaafisha Mtumishi ambaye ni vigumu kumtia hatiani; je, sasa sio wakati muafaka wa kutolewa Kanuni Elekezi ya kuwawajibisha wajanja potofu, Maofisa Watendaji wa Kata na Vijiji, ambao wamedhulumu michango ya wananchi kwa kuficha maelezo ya mapato na matumizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Maswa tunahitaji kuimarisha huduma ya afya ili tudhibiti vifo vya kukosa huduma stahiki Vijijini na kwamba huduma hiyo ipo katika Hospitali ya Wilaya; na kwa kuwa hoja hii niliieleza wakati wa Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Fedha ya 2008/09; na kwa kuwa mara ya kwanza nililieleza mwaka 2006; sasa naomba hatua elekezi za kutatua tatizo hili.

Mahitaji halisi kuwa ni magari manne kwa ukubwa wa mtandao wa Wilaya ya Maswa ambayo ni eneo la km 3400; naomba tupatiwe *ambulance* kuokoa maisha ya wagonjwa Vijijini Maswa.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo muhimu sana ambalo Maswa tunaomba Serikali ilizingatie na ambalo Rais aliahidi ni matengenezo ya barabara Vijijini. Kwa kuwa kuimarisha barabara ni uwezeshaji wa kufaulisha kushirikisha Vijiji kupata huduma bora ya Afya ipatikanayo Makao Makuu ya Wilaya; na kwa kuwa uimarishaji matengenezo ya barabara ni ufunguo wa kushirikisha kikamilifu juhudi za kiuchumi za biashara hivyo kuchochea mazao ya kilimo kulimwa zaidi; na kwa kuwa barabara ni changamoto kwa kupunguza bei za nafaka katika kipindi cha ukame na njaa na ni kivu.

Sasa naomba ushauri elekezi kwa Wizara ya Miundombinu iungane na Wizara ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa ili mtupatie Maswa shilingi bilioni 1.8 za kurekebisha maeneo korofi. Gharama hizi ni kwa ajili ya kuweka viraka vya kuunganisha mawasiliano. Jumla ya viraka ni km. 291.7.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Mheshimiwa Waziri Mkuu, amkumbushe Waziri wa Nishati na Madini, atimize hatua za kuanza kutatua matatizo ya umeme. Bila umeme, huduma za afya ni dhoofu na Mradi wa Elimu ya Sayansi nao hautekelezeki Vijijini. Bila umeme, uwekezaji Vijijini ili tuthaminishe kilimo cha pamba na pamba ipate bei bora ni ndoto.

Kwa hiyo, sasa naomba suala la umeme lipate kielelezo cha hatua kwa hatua, Serikali imeamua kutatua tatizo la hasara ya kukosekana umeme kwa msako wa maisha bora.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba vilevile Wizara ya Maji ikubali kujadili shida ya ukame wa maji ya binadamu na maji ya mifugo. Kwa kuwa programu saidizi za mfano wa *TASAF* hazikidhi makabiliano ya uzito wa gharama; sasa namwomba Waziri Mkuu, atoe ushauri elekezi wa kumwomba Waziri wa Maji apange fursa ya kujadili kwa kina, faida na hasara iwapo utatuzi hautaanza sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kumalizia mchango wangu wa kuishauri Serikali, kufungamana na matatizo ya Maswa kwa kuimarisha Utawala Bora.

Kwa masikitiko makubwa nasema, Mkuu wa Wilaya ya Maswa, ndugu yetu Captain James Yamungu ni kikwazo kwa ujezi wa Uongozi wa pamoja na Uongozi wa Maslahi ya Ustawi wa Maendeleo ya Jamii. Naomba uongozi ufuatiliwe na vyombo vya dola ili uwazi na ukweli ujulikane.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha. Naunga mkono hoja. Ahsante.

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kumpongeza Waziri Mkuu na Wasaidizi wake, kwa Hotuba nzuri na kazi kubwa waliyoifanya kwa manufaa ya Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Wananchi wa Jimbo la Simanjiro, naomba kuishauri Serikali itimize ahadi zake katika maeneo yafuatayo:-

Miundombinu: Barabara ya KIA hadi Mererani kujengwa kwa kiwango cha lami. Hii ni Ahadi ya Rais wa Awamu ya Tatu, Mheshimiwa Benjamin W. Mkapa na Ahadi ya Rais wa Awamu ya Nne, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete. Aidha, nashauri barabara tulizoziomba zipandishwe hadhi kuwa za Mkoa. Serikali ifanye hivyo.

Elimu: Tunaomba Serikali ituunge mkono katika ujenzi wa mabweni katika shule zetu kumi na nne za sekondari, kutokana na ukweli kuwa umbali kati ya Kijiji na Kijiji ni wastani wa km 50; hivyo, kujenga ulazima wa shule zote kuwa za bweni.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo lingine kubwa sana kwa Wilaya yetu kwa ujumla ni la maji. Tunaomba Serikali ianze sasa mradi kabambe wa kupeleka maji Makoa Makuu ya Wilaya, Orkesumet, utengewe fedha kukidhi haja/ahadi ya Viongozi wa Kitaifa na mahitaji ya Wananchi wa Simanjiro.

Aidha, tunaomba Miradi ya Mabwawa ya Maji tuliyoiibua na kuwasilisha Wizara ya Maji sasa itengewe fedha. Mabwawa hayo kulingana na vipaumbele ni Bwawa la Loonderkes (Kata ya Kitwai), Bwawa la Losokonoi (Kata ya Naberera), Bwawa la Endonyo-engijape (Kata ya Orkesumet), Bwawa la Loibor Siret na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la majosho ya kuogeshea mifugo ya *East Cost Fever (ECF)* ili kujengea mifugo yetu kinga dhidi ya Ugonjwa huo wa Ndigana.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuchangia suala la nishati ya umeme. Naishukuru Serikali ya CCM, kwa kutimiza ahadi yake ya kupeleka umeme Makao Makuu ya Wilaya yetu (Orkesumet). Aidha, nashauri Serikali irekebishe makosa ya

awali wakati wa utekelezaji wa mradi. Upungufu huo ni ule wa Kitongoji cha Engurash (Loiborsoit) na Ngage A na B.

Aidha, naishukuru Serikali kwa kuahidi kupitia Waziri wa Nishati na Madini kuwa, sasa Tarafa ya Msetu wa Tembo nayo imewekwa kwenye mpango wa mwaka huu. Upembuzi yakinifu ulikwishafanyika wa kupeleka umeme Vijiji vya Lendanai, Naberera na Namalulu; hivyo, tunaiomba Serikali ione uwezekano wa kutengea fedha angalau mwakani kutokana na umuhimu wa maeneo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaibua Miradi ya Umwagiliji katika Vijiji vya Ruvu Remit, Loibor Soit, Ngage, Lemkuna, Kiruani, Msitu wa Tembo na Kambi ya Chokaa na miradi hii ni ya muda mrefu; hivyo, wananchi wanasikiliza kauli ya Serikali kuhusu miradi hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja ya Waziri Mkuu kwa asilima mia moja.

**MHE. THOMAS A. MWANG'ONDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naanza kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa hotuba yake makini. Hata hivyo, pamoja na hotuba hii nzuri, ningependa niuelekeze mchango wangu kwenye mambo husika na Serikali hasa suala la barabara, hususan msongamano wa magari mijini *(heavy traffic).*

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali yetu kwa baadhi ya Mipango ya Mandeleo imekuwa inaonekana kutochukua tahadhari mapema. Mlinganisho wa ukuaji wa maendeleo kwa Miji ya Mbeya na Dar es Salaam ni mfano stahili na halisi, nikiwa kama Mkazi wa Jiji la Mbeya; hali ya msongamano wa magari niliyoiona Dar es Salaam inanitia hofu. Ziara zangu binafsi katika Majiji ya London na New York, zimenifundisha mengi; pale Dar es Salaam msongamano umefikia hatua ya kutisha, lakini bado hatuoni upanuzi wa barabara unaoendana sambamba na ongezeko la uingizaji wa magari nchini. Bado tunapoongeza barabara zetu sana sana zinakuwa ni za *dual lane* (zile zinazopishana mbili kwa mbili). Wenzetu katika Majiji ya New York na London, barabara ni nne kwa nne *(four lanes)* na barabara za ngazi *(fly-overs).*

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara nilizozitaja hapo juu si anasa; ni mojawapo ya njia pekee inayoweza kutusaidia kutatua tatizo la msongamano huu. Kwa upande wa Jiji kama la Mbeya, hali hii yaweza kutokea katika siku za usoni; ukuaji wake ni wa kasi. Naomba Ofisi ya Waziri Mkuu kwanza, itatue suala la msongamano huu katika Jiji la Dar es Salaam kwa namna tajwa hapo juu. Pili, mikoa yote iliyokwishapata hadhi ya jiji, hatua za tahadhari za upanuzi wa barabara kuu zake, zianze kuchukuliwa kabla nayo haijaingia katika tatizo hili lililoikumba Jiji la Dar es Salaam.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine linalonigusa na kunikera ni suala la Ustawi au Maendeleo ya Jamii yetu, hususan makundi ya watoto yatima na walemavu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nadiriki kutamka, kama ipo mipango ya kuhudumia makundi haya basi ipo katika mambo ya kinadharia zaidi kuliko matendo au utekelezaji.

Pale Dar es Salaam, makundi yanayoongoza kwa kujikimu kiuchumi kipitia njia ya kuomba fedha kwa wapita njia na wenye magari na hata kuhatarisha maisha yao.

Namwomba Mheshimiwa Waziri Mkuu, ahakikishe kwamba, njia ama pa kukimbilia kupata misaada ya uhakika kwa makundi haya panafahamika. Mipango iliyowekwa na Serikali pia ifanyiwe kazi, ihakikishwe utekelezaji wake unapata usimamizi stahili. Ni udhaifu ama kutokuwepo kwa utekelezaji huo ndio kumezaa watoto wezi na wahanga wa vitendo vya ngono kutokana na mazingira ya tabu wanayoishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni suala la umri wa kustaafu wanajeshi. Kutenda kosa si kosa ila kurudia kosa ndio kosa. Wanajeshi wetu kutokana na taratibu zetu, wale wa vyeo vya chini wamekuwa wakilazimika kustaafu wakiwa na umri mdogo kwa mujibu wa sheria. Matukio ya ujambazi katika miaka ya hivi karibuni, yamehusisha baadhi ya askari wetu kutoka Jeshi la Wananchi na lile la Polisi.

Naiomba Serikali, ikiangalie upya kipengele hiki cha kustaafu. Vijana hawa kutoka kwao mapema Jeshini, wanakuwa bado wana nguvu za kufanya kazi, huku wakiwa hawajajiandaa kustaafu, inapelekea kujiingiza kwao kwenye vitendo vya uhalifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nina mapendekezo yafuatayo: Umri wa kustaafu waongezwe hadi kufikia miaka 60; kuwe na ongezeko la marupurupu yanayoendana na ukuaji/mfumko wa bei *(inflation)* kwa askari wastaafu; na baadhi ya huduma za kijamii wastaafu hawa waendelee kuzipata bure kwa mfano, matibabu, elimu kwa familia zao na usafiri wa umma.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nihitimishe kwa kutamka kuwa, nina imani kubwa na Mheshimiwa Pinda na Serikali yetu. Namtakia kila la kheri Mheshimiwa Waziri Mkuu. Naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA:** Mheshimiwa Spika, katika Hotuba ya Waziri Mkuu, uk. Wa 6 na 7, Mheshimiwa Waziri Mkuu amezungumzia hali ya siasa nchini kwamba, nchi yetu ni shwari na inasifika sana duniani kwa kudumisha amani na utulivu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi sikubaliani na maneno hayo ya Waziri Mkuu, kwa sababu hali mbaya ya siasa iliyopo nchini na manung'uniuko ya watu kuhusu ufisadi ni mambo ambayo ni sawa na moto unaofukuta chini kwa chini unaporipuka ndio unaonekana juu. Ithibati ya hili ni semina ya Jumamosi tarehe 21 Juni, 2008, ambayo ilisema wazi wazi kwamba, yapo mambo mengi ambayo yanaashiria uvunjifu wa amani, likiwemo la hali tete ya Zanzibar.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la Muungano linatolewa maelezo kwamba, kero zake zinaendelea kutafutiwa ufumbuzi kwa vikao vinavyofanywa na Ofisi ya Waziri Mkuu, pamoja na Ofisi ya Waziri Kiongozi na pia kuna vikao vingine 11 vilivyokaa

kuzungumzia kero hizo. Nchi yetu ni ya Vyama Vingi; Ofisi ya Waziri Mkuu na Waziri Kiongozi zote ni kutoka Chama Tawala. Kwa lengo hilo, mazungumzo haya hayawawakilishi wote na wanalindana katika mazingira ya kisiasa.

Haiwezekani, miaka nenda miaka rudi, tunaelezwa matizo ya Muungano yanatafutiwa ufumbuzi lakini hakuna kinachotendeka. Ikiwa sasa ni miaka zaidi ya 30, kero hizi zinaongezeka siku hadi siku, kama vikao hivyo vinaleta ufumbuzi, leo tuambiwe ni kero ngapi za Muungano zimepata ufumbuzi na ngapi hazijapata ufumbuzi? Je, nitazungumza kwa *indefinite time?*

Mheshimiwa Naibu Spika, tumearifiwa katika Hotuba ya Bajeti ya Waziri Mkuu kwamba, kutakuwa na uteuzi wa Mshahauri mwelekezi, atakayeshauri kuhusu mgawanyo wa mapato yatokanayo na rasilimali za mafuta na kazi hii inatarajiwa kukamilishwa mwezi Agosti, 2008. Suala kubwa ambalo nataka Mheshimiwa Waziri Mkuu anijibu; huyo Mshauri Mwelekezi atashauri mapato yatokanayo na rasilimali ya mafuta tu; je, vipi kuhusu gesi?

Mshauri huyu atamaliza kazi Agosti, 2008. Je, *TPDC* yenyewe imepata wapi mamlaka ya kugawa Blocks Zanzibar?

Je, hii Sheria ya Kuanzishwa *TPDC* ilikuwa ya Muungano lini na huo mwezi Oktoba itakuwa imeshafanyiwa marekebisho?

Kwa masikitiko makubwa nimesoma hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, sikuona sehemu yoyote anapozungumzia ajali za baharini na namna gani mipango ya kuwaokoa wakati wa ajali. Tulilizungumza hili katika Bajeti ya 2007/08 kwa nguvu zetu zote, lakini bado hatkuna katika Mpango wa Bajeti ya mwaka huu. Kitu ambacho kimetajwa kuwa kifungu cha maafa 2001, kimetengewa 688.062.100 *only*. Sijaona fungu hilo la uokoaji. Wavuvi wetu, pamoja na wasafiri wengi wakipoteza maisha yao *(deaths)*. Kampuni ya Earnest wamechagulliwa na Serikali kufanya *auditing* na wakagundua zaidi ya Sh. 90 bilioni, makampuni mbalimbali wame-*forge* na kujichotea fedha hizo za umma. Kutokana na kauli aliyoitoa Mheshimiwa Waziri wa Fedha, pameingia dosari; kwa kauli yake ya kusema hizo pesa za *EPA* si mali ya Serikali bali ni mali ya wafanyabiashara. Ikiwa hivyo ndivyo, Waziri atueleze hao wafanyabiashara wamejiibia wenyewe?

*Task Force* gani iliyoundwa kwa kutatua au kufuatilia Sh. 4.47 bilioni zilizolipwa kwa watu (Makampuni) ya *MS Njake Enterprise* ya Arusha na Sh. 445 milioni zimelipwa kwa *M/S Ruaha Investiment* ya Dar es Salaam?

Mheshimiwa Naibu Spika, fedha hii vipi mbona Mheshimiwa Waziri ana majibu yasiyonufaisha au yasiyofafanua?

Mheshimiwa Naibu Spika, tunamwomba Waziri Mkuu, atupatie maelezo ya kina si ya kubabaisha.

**MHE. OMAR S. KWAANGW:** Mheshimiwa Naibu Spika, madhumuni ya mchango huu wa maandishi ni mawili; kusahihisha takwimu kama nilivyotamka kwenye mchango wangu wa kuzungumza *(Hansard)*. Naomba sehemu niliyozungumzia uimarishaji au ukarabari wa Hospitali ya Wilaya inayokabidhiwa Halmashauri ya Mji, nilitamka kwa bahati mbaya kwamba, tumeomba shilingi karibu milioni 1,940,000 *(Hansard)*, badala ya karibu bilioni 1,940,000,000.

Pale nilipozungumzia ujenzi wa Makao Makuu ya Halmashauri ya Mji, nilinukuu fungu 6402 – karibu 600,000 badala ya milioni 600 na kwamba, tuliomba bilioni moja na zaidi (Bilioni 1.1), badala ya milioni 1.1. Pia nilisema kwa makosa kuwa tulishapata karibu 400,000 badala ya kusema karibu milioni mia nne.

Ushauri wangu kuhusu Programu za Kuendeleza Kilimo; *ASDP, AMSDP, DADPS* na kadhalika. Ni muhimu kubadili Sera za Matumizi ya Fedha za Maendeleo kwa sababu ukiangalia *Action Program* zao, fedha zinazobaki pale Kijijini kwa maana ya kuendeleza ni kidogo sana. Karibu asilimia 80 ni fedha za Utawala; posho za semina na hasa hasa zinarudi tu kwa wataalam. Nashauri fedha za Utawala kama posho ziwe chini ya *OC* kama ilivyokuwa zamani kuwa fedha za maendeleo hazina uhusiano na *OC*. Utaratibu wa sasa, Mradi unaandikwa na gharama za *OC* hujumuishwa humo. Hili ndilo tatizo; Miradi kama hii ya kuendeleza kilimo ingekuwa inatoa vifaa vya kilimo/pembejeo ili vibaki na wakulima. Mashindano/maonyesho ya Kilimo yafanyike kila mwaka katika Kijiji au Kata. Wanaofanya vizuri wapewe zawadi kupitia miradi hii ya *ASDP, AMSDP, DADPS* na kadhalika. Mashamba ya Maonyesho iwe ni kwa kila mkulima na tujue idadi ya wakulima.

Kuhusu mbegu/mbolea za ruzuku, Serikali iende moja kwa moja kwa wakulima au vikundi vyao; Mpango wa Wakala haufai kwa sababu wakulima hawapati faida yoyote.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, naomba utaratibu ufanyike wa kutoa vitabu mahususi, vitakavyoonyesha fedha zote kwa kila Sekta zinazokwenda kwenye Halmashauri zetu. Kwa sasa si rahisi hata Mbunge kufahamu fedha zote zinazokwenda kwenye Halmashauri kwa kuwa kuna vyanzo vingi; Wizara ya Fedha, Wizara nyingine zote na Fedha za Wafadhili. Tunaomba muhtasari wa fedha kwa kila Mradi kwa kila Halmashauri ya Wilaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja kwa mara nyingine tena na naomba tupate fungu la kukarabari Hospitali ya Wilaya Babati.

**MHE. HASNAIN G. DEWJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichangie hoja iliyo mbele yetu. Napongeza sana hatua nzuri za Serikali kwa kuleta hapa Bungeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja, lakini ninayo machache ya kuchangia.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya ya Kilwa ina maeneo makubwa sana, kuna tatizo la kugawa maeneo makubwa kwa wawekezaji. Hii inaweza kuleta matatizo makubwa katika Wilaya yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, maeneo makubwa hayo hugawiwa wawekezaji kwa miaka 50. Ushauri wangu, tusije kugawa maeneo makubwa kwa ajili ya mibono *(jetropha).* Zao hilo linaweza kuleta njaa katika Wilaya hivi sasa wakulima wengi wadogo wanakwenda kusaidia kwenye mashamba hayo ya mibono na kufanya kuacha mashamba yao ovyo na kutolima na kwenda kujipatia pesa za kujikimu.

Hii inaweza kuleta njaa Wilayani na kufanya wakulima kwenda huko na Wilaya kukosa chakula. Naomba tuangalie upya mashamba ya mibono *(jatropha)* na ugawaji wa maeneo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya ya Kilwa kuna matatizo ya matreketa, hakuna hata zaidi ya matano. Suala hili linaifanya Wilaya kutozalisha zaidi chakula; tunaomba mikopo ya kupata matrekta.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kituo cha Kuzalisha Umeme cha Somanga Fungu; Mradi huu huko nyuma kwenye miezi 16 sasa, nina wasiwasi sana huu Mradi, kazi haijakamilika mpaka leo; je, Serikali inatoa kauli gani?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Kilwa ipo nyuma kimaendeleo, tunaomba sana kubadili Sera au kuwe na Sera ya Gesi nayo ipate mgao wa mrabaha kutokana na gesi asili. Ili Wilaya ipate maendeleo ya haraka, naomba sana kuwe na Sera hiyo. Nitashukuru kama tutafanikiwa. Kwa kuwa Kilwa ina vigezo vingi vya kuvutia watalii kama magofu, uvuvi, wanyama na Mapango ya Kipatimu, naiomba Serikali ifanye kila hali kuboresha Kiwanja cha Ndege cha Kilwa Masoko na barabara kutoka Dar es Salaam hadi Kilwa ikamilike haraka.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, narudia kuunga mkono hoja. Shukrani.

**MHE. TEDDY L. KASELLA-BANTU:** Mheshimiwa Naibu Spika,awali ya yote, nashukuru kwa kunipa nafasi nami nichangie hoja iliyopo mbele yetu. Kwa niaba ya Wananchi wa Jimbo la Uchaguzi la Bukene, maana mara baada ya kumaliza ziara yake Jimboni kwangu na Wilaya ya Nzega kwa ujumla na baada ya kunishangaa naomba daraja wakati barabara sina, Naibu Waziri wa wakati huo alipata au tuseme alipanda cheo na kuwa Waziri kamili, yaani sasa ndiye Waziri wa Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Mheshimiwa Celina Kombani. Hongera sana.

Mheshimiwa Waziri, mimi, pamoja na Wananchi wa Bukene, tunaamini na tuna uhakika tutafanya kazi pamoja kwa ushirikiano mkubwa. Tukianza na hilo la Daraja la Kilyalyoha, ambalo uliliona na ukamwambia mhandisi afanye gharama yake ili lishughulikiwe ipasavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mengine sitaki kuandika hapa ila najua Waziri analijua lile daraja likitengenezwa, litasaidia wakulima wote kupeleka mazao yao sokoni Isaka, Shinyanga, Mwanza, Tabora, Dar es Salaam, Burundi, Kenya na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, najua kuna fedha kutoka kilimo, ambazo zinatengeneza barabara kwa ajili ya kutoa mazao toka mashambani kupeleka sokoni. Naomba fungu hili la fedha, lisaidie kufanya kazi ya barabara hizi za Jimbo la Bukene na mengine, kutoa mazao mashambani kupeleka sokoni. Kwangu ni kutoa Semembela, Kahama ya Nhalanga, Ikindwa, Malolo, kupitia Darala la Kilyalyoha kwenda Mwamala, Buhondo, Isaka – Shinyanga/Mwanza, Kenya au Isaka Kahama Burundi au Dar es Salaam na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kijiografia la nchi hii ni kubwa mno na bado upo umuhimu wa kubuniwa kwa maeneo mapya ya kiutawala, hasa kwa maana ya kuanzisha mikoa mingine mipya, Wilaya nyingine mpya, Tarafa nyingine mpya, Kata nyingine mpya na hata maeneo mapya ya Vijiji na Mitaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kuna gharama katika hili, lakini kujipanga na kupanga mambo vizuri ni gharama za muhimu kama hitaji la msingi la kuchochea maendeleo ya kiuchumi na kijamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, zipo Wilaya na hata Kata katika Tanzania Bara, ambazo ukubwa wake unalingana au kuzidi ukubwa wa nchi fulani zilizopo katika Mabara ya Ulaya, Asia na Amerika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali itenge fedha kimakusudi kabisa ili kufanikisha zoezi muhimu la kubuni na kuanzisha maeneo madogo madogo zaidi ya kiutawala, kwa lengo la kuimarisha demokrasia (kwa kupeleka zaidi na zaidi ufanyaji maamuzi ya kiutawala karibu zaidi na maeneo waliko wananchi wengi zaidi).

Kwa misingi hiyo, isisahaulike Nzega ina Majimbo mawili; Nzega na Bukene na ina Kata 37. Sijui kama kuna Wilaya kubwa kama Nzega, nyingine zina Kata 5, 6 au 10. Hivyo, Nzega ina Kata 21 kuwa Wilaya peke yake, hivyo hivyo na Bukene Kata 16, sawa kwa kuanzia.

Mheshimiwa Naibu Spika, nafasi za kiutawala za Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya na Watendaji kama Mkatibu Tawala wa Mkoa na Wakurugenzi wa Halmashauri za Wilaya na Miji ni lazima sasa ziangaliwe upya, kwa lengo jema la kuchochea ufanisi, ufikiaji wa malengo na usisimuaji wa maeneo kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna suala la umeme Bukene na Ndala; ni jambo la kusikitisha sana unapoona Bajeti ya 2006/07 ilipita, tukaenda kutangaza kwa wananchi wakafurahi. Kwa sababu zisizozuilika hatukupata, 2007/08 tukapewa Sh. 50 milioni ambazo hazikufanya lolote na mwaka huu tumepangiwa Sh. 50 milioni. Hivi kweli ndio tunatekeleza Ahadi za Marais wetu? Hii ni Ahadi ya Rais Mkapa. Rais Kikwete alipopita akiomba kura 2005, aliahidi atatekeleza na kweli 2006/07 bajeti ikapitishwa.

Sasa kulikoni, mbona tunawadhalilisha Viongozi wetu? Mbona tunawajengea chuki viongozi wetu na katika Ilani ya uchaguzi na Ahadi za Rais Kikwete ipo?

Sasa ndio nini Hii? Sh. 50milioni watu wa *TANESCO* wanasema wafanye nini nazo ni kama mnatutania. Kumbuka katika Majimbo ya Mkoa wa Tabora, Rais alipata kura nyingi sana. Kwanza kabisa Igunga na pili Bukene. Pamoja na Mbunge wako, wananchi wanamwamini na wanampenda. Hebu fanyeni kweli acha utani. Gharama mpaka sasa ya kupeleka umeme imepanda hadi shilingi bilioni moja; sasa unapotoa 50 milioni za mwaka jana zipo. Kama zipo maana yake tuna Sh. 100,000,000; ina maana milioni 100. Naomba *TANESCO* nao waambiwe waanze, wasizitumie kwa shughuli nyingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna kitu huwa kinanishangaza; barabara "Truck Road" toka DSM – Kahama - Bukoba ni T3. Ukianzia DSM – Morogoro – Dodoma – Singida - Nzega unaona na ndio unapita T3. Sasa sheshe ikifika Nzega, T3 ipo ila sio lami inapitia Jimboni kwangu Nzega – Itobo – Igusule – Kagongwa - Kahama na kadhalika. Magari yote yanayotoka huku, yakifika *round about* yanaacha T3 (ambayo barabara siyo ya lami) yanafuata T8 ambayo yanaenda Mwanza, halafu huko mbele yanakwenda tena kupata T3. Sasa kulikoni? Mnyonge mnyongeni, haki yake mpeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa misingi hiyo, naomba kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Bukene ambao ni yaki yao, hako ka kipande kwa T3 toka Nzega, Itobo/Igusule/Kagongwa/Kahama kawekwe lami ipasavyo sio kutuonea na kutudhulumu haki yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, najua Mheshimiwa Waziri Mkuu ni mpole na mtenda haki, atatutendea haki ipasavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nikumbushie tu Mabwawa mawili; Bwawa la Umwagiliaji la Kahama ya Nhalanga. Mara nyingi na sasa nakumbushia tu ni Ahadi ya Hayati Edward Moringe Sokoine. Wataalam walishakuja kupima na kuweka *beacons* zao. Wananchi wa Bukene kama kawaida yao ni wakulima wazuri wa mpunga, karanga na bustani; wanasubiri sana kwa hamu na kwa matumaini makubwa, Ahadi hii kutekelezwa maana ni umri wa mtu. Ahadi ni ya 1984, tutekelezeeni nasi tutazalisha chakula chetu na cha biashara, hasa wakati huu ambapo dunia nzima ina upungufu wa chakula. Naamini hili tumepata, hasa tukizingatia wakati wenyewe wa upungufu wa chakula.

Mheshimiwa Naibu Spika, Bwawa la Itobo ni la historia; ni bwawa ambalo daktari wa kwanza Mwafrika, Dr. Mwaisela, alititia na umauti ukampata hapo.

Mheshimiwa Naibu Spika, bwawa hili lingefufuliwa kihistoria tukapata kitoweo cha samaki wazuri sana kwa Wananchi wa Bukene kwa lishe na biashara ili kujikwamua kiuchumi. Pia kumbukumbu ya Dr. Mwaisela ambaya kwa haraka haraka tu ana *Ward* pale Muhimbili Hospitali. Katika mizunguko yangu Jimbo langu la Bukene, Wenyeviti wa Vijiji, Vitongoji, nafikiri hata Kamati za Ardhi za Vijiji wanaomba *training;* semina,

warsha na kadhalika. Wanachaguliwa uongozi, nao wanahitaji kupigwa msasa ili wajue kazi na majukumu yao. Nawaombea ili waweze kutimiza vizuri majukumu yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Ofisi ya Waziri Mkuu na Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, wasiwaonee huruma wanaokula/iba fedha za umma/wananchi. Unakwenda mahali Watendaji kwa mfano, *VEO/WEO* wamekula pesa za michango ya wananchi. Kuna mahali nilikwenda waliniambia wananchi hawawataki, niondoke nao, mimi nikaripoti kwa mwajiri wao, lakini hatua zinachelewa sana hadi wanaringa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba wachukuliwe hatua haraka wafungwe/walipe, sio kuwaacha wanazurura au kuwahamishia sehemu nyingine. Waharibu hawa wanawavunja moyo wananchi kuchangia Miradi ya Maendeleo. Kufukuza *is the best*, ili iwe funzo kwa wengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakifukuzwa wachache wa kwanza na ikatangazwa kweli kweli, wananchi watafurahi na watajua na kuamini kabisa Serikali inafanya kazi yake ipasavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna suala la ulinzi shirikishi; sote tunajua ulinzi wa sungusungu tangu enzi za machifu. Ukisikia mwano lazima utoke kusaidia usalama wa mali na usalama wa raia wako.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba ulinzi wa sungusungu uangaliwe, wasiwavunje moyo wananchi, wanasaidia sana kwenye wizi wa ng'ombe na kadhalika. Kinachosikitisha, wapo wajanja wanaotokea Kagongwa, Isaka au Kahama Mkoa wa Shinyanga, hawa ni wajanja zaidi kuliko walinzi wa sungusungu toka Jimbo langu la Bukene, hasa Kata ya Igusulule. Wakiiba wanawageuzia kibao wananchi wangu eti wezi na hali walikuwa wakifuatilia ng'ombe/mali zilizoibiwa na kupelekwa huko.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba masuala haya yaangaliwe sana na kwa umakini ili watu wangu wasiwekwe au wasitishwe ndani upande wa pili na hivyo kuanza kuogopa kutenda haki na kusaidia ulinzi shirikishi kwa usalama wa raia na mali zao. Naomba Serikali itambue juhudi zao za hiari.

Mheshimiwa Naibu Spika, Polisi tuna *OCD* mmoja Nzega na gari moja bovu kwa Nzega na Bukene; Kata 37. Naomba tupewe pikipiki tano na mgao wake uwe kama ifuatavyo: Pikipiki moja kila Tarafa moja, tuna Tarafa nne kila Jimbo Tarafa mbili. Hivyo, Tarafa nne pikipiki nne; na Pikipiki moja kwa Makao Makuu ya Jimbo la Bukene, Bukene Mjini.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba angalau pikipiki tatu kwa Jimbo la Bukene. Tunaomba pia kuongezewa wafanyakazi/askari wenye utaalam mpya, kwani sasa hata wahalifu wamekuwa nao wataalam.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. DR. GUIDO G. SIGONDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali iwaongeze posho wastaafu hasa wale ambao hali yao ni ya kusikitisha kulingana na hali ya uchumi hivi sasa.

Serikali ifikirie namna ya kuwasaidia Godfrey Mwafongo, aliyekuwa Mwandishi Msaidizi wa Ikulu na Mshindo Mkeyenge, aliyewahi kufanya kazi Redio Tanzania na Ukuu wa Wilaya.

Wilaya ya Chunya ina ukubwa wa km za mraba 46 (karibu ya nusu ya Mkoa wa Mbeya), naomba ugawanywe kwa lengo la kusogeza huduma za maendeleo karibu na wananchi. Mfano, Jimbo la Songwe miundombinu yote ya Makao Makuu ya Wilaya. Boma lina nyumba ya Mkuu wa Wilaya na *DED.* Nyumba ya *DED, DSO,* Posta, Kituo cha Polisi, Kambi ya Magereza na kadhalika.

Serikali ifikirie kuanzisha Mfuko wa Maendeleo wa Jimbo *(CDF)*, kuwasaidia Waheshimiwa Wabunge Majimboni.

**MHE. SALIM HEMED KHAMIS:** Naipongeza Hotuba ya Waziri Mkuu, kwa kuwa imewagusa Watanzania wote katika nyanja mbalimbali, lakini hasa Mtanzania wa kipato cha chini. Pamoja na uzuri wa Hotuba hii, yapo mambo ambayo ningependa kuyajadili kwa kuamini kuwa, busara zake zinaweza kusaidia kutatua baadhi ya matatizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania imekuwa na Mahakama ya Kadhi kabla ya Uhuru, lakini bahati mbaya baada ya Uhuru Mahakama hiyo iliondolewa. Kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ibara ya 19; Serikali ya Tanzania haina dini lakini Watanzania wana dini zao na kwa mujibu wa ibara hiyo hiyo Watanzania wana uhuru wa kuabudu dini wanayoitaka. Dini zetu zina sheria zake, sera zake na mikakati yake na muumini anatakiwa siyo kuyaamini tu bali ni lazima kuyatekeleza kwa vitendo.

Waislamu wamekuwa wakidai Mahakama ya Kadhi irudishwe ili iwasimamie katika mambo yao ya mirathi, ndoa na takala na kadhalika. Inasikitisha kuwa Serikali inataka kuwauliza wale wasio Waislamu kama Mahakama hiyo iwepo au la. Serikali hii hii wakati Zanzibar inataka kujiunga na *OIC* ilizuiwa kwa mbinu kwa kuambiwa isubiri Tanzania ijiunge, jambo ambalo halijafanyika hadi leo, lakini wakati huo huo Watanzania wana uhusiano wa karibu sana Vatican.

Hivi sasa *Vatican* wanajenga Hospitali ya *Cancer Ocean Road Dar es Salaam.* Serikali haiwezi kuwa *double standard* kwa kuwaruhusu Vatican kuungana na waumini wao na kuanza kuwa na kigugumizi juu ya kuwaruhusu Waislam kuwa na Mahakama ya Kadhi. Waislamu hawawezi kuendelea kufanywa watoto wa kuku. Wakati umefika sasa wa Serikali kuamua kuanzisha Mahakama ya Kadhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inaonyesha haina Sera ya Mipango Miji. Watanzania ambao wamehamia maeneo mbalimbali, wanavunjiwa majumba yao kwa kisingizio cha utanuzi wa mji na kadhalika. Baya zaidi, bomoa bomoa hiyo haizingatii sheria na taratibu. Wengine wanapewa *notice* ya muda mfupi sana na wengine fidia wanayopewa hailingani na thamani ya majumba yaliyovunjwa.

Mivutano ya Kijamii katika Kijiji cha Kisingiri Kata ya Ilola – Jimbo la Solwa; Wananchi waliohoji juu ya mapato na matumizi ya Kijiji katika mkutano wa Kijiji walitengwa na Diwani. Waliwekwa chini ya karantini kwa siku 37 mpaka watakapolipa ng'ombe 20 au mbuzi 100. Chanzo cha tatizo ni baada ya wananchi hao kutaka kujua mapato na matumizi ya Kijiji kwa miaka miwili iliyopita; na mapato na matumizi ya Sungusungu. Majibu ya Viongozi hao ni kuwa wote waliouliza masuala hayo walikuwa ni Wapinzani hivyo, wasubiri mwaka 2010; majibu hayo yaliwakasirisha wananchi na wakaanza kuondoka na ndipo uamuzi wa kuwatenga ulipotolewa. Tunaomba maelezo ya Serikali juu ya tukio hili la aibu.

**MHE. EZEKIEL M. MAIGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, nampongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa kuandaa hobuta inayoloenga kutatua kero za wananchi. Hivyo, naunga mkono hoja hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali itusaidie kutatua matatizo yafuatayo:-

Wilaya ya Kahama igawanywe. Pamoja na mchakato unaoendelea Wilayani na Mkoani, naomba Serikali Kuu ituangalie; Kahama ina watu 750,000 ni idadi kubwa sana kubaki Wilaya moja.

Idadi ya watumishi wanaopangwa Kahama na Shinyanga ni ndogo ukiwianisha na idadi ya watu. Sababu kuu ya kutofanya vizuri katika elimu ni uhaba wa walimu. Naomba idadi ya walimu, madaktari, polisi na kadhalika iongezwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna barabara ya Kahama Mjini iliahidiwa na Mheshimiwa Rais kutiwa lami; Ahadi hii hatusikii mkakati wa utekelezaji.

Naomba vifaa vya Hospitali Kahama kama U*ltra-sound* na *X-ray* havitoshelezi mahitaji. Aidha, idadi ya *ambulance* zilizopo ni nne hazitoshi, tunahitaji walau mgao wa ambulance mpya tano.

Mheshimiwa Naibu Spika, mgao wa fedha za barabara kahama ni ndogo sana. Mwaka huu 2008/09, tumepangiwa Sh. 200m tu, pungufu hata ya mgao wa mwaka huu 2007/08. Tunaomba utafiti wa urefu wa barabara zetu ufanyike ili tupate mgao stahiki.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumeibuka wimbi la ujambazi, unaolenga watumishi hasa walimu. Tunaomba msaada wa haraka. Katika kipindi cha miezi sita iliyopita, walimu 43 wamevamiwa. Hakuna hata tukio moja ambalo lilizimwa au watuhumiwa kukamatwa. Polisi ni wachache, Vituo vya Polisi vichache, hata vifaa vya kazi hawana.

Tuonaomba sana usalama wa raia uimarishwe Kahama. Hivi sasa walimu hawafundishi, ninaamini hili litajitokeza katika matokeo ya mtihani mwaka huu.

Kwa kuwa mtandao wa barabara Kahama ni mkubwa sana na mgao wa *road fund* kwa Wilaya ni mdogo, Wilaya imependekeza barabara za Kahama – Ulowa (km 120), Kahama – Bulige (km 50) na Kahama – Busayi – Jomu ( hadi Bukwimba, Geita km 65) ziwe za Mkoa. Pamoja na mjadala unaoendelea Mkoani, naomba Serikali Kuu ituunge mkono na kutusaidia.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba tena nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri Mkuu na Waziri Kombani na Watendaji wote, chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu, kwa maandalizi ya Bajeti, nawatakia mafanikio katika utekelezaji na ninaunga mkono Bajeti.

**MHE. HASSAN C. KIGWALILO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninampongeza Mheshimiwa Mizengo Peter Pinda, kwa hotuba nzuri na kamilifu ambayo ninaiunga mkono kwa asilimia 100. Pia ninawapongeza Waziri, Mheshimiwa Celina Kombani na Naibu Waziri, Mheshimiwa Aggrey Mwanri, kwa kuteuliwa na Mheshimiwa Rais kushika nyadhifa hizo pia kwa mchango wao mkubwa kwa hotuba hiyo. Aidha, ninawapongeza Katibu Mkuu na Wataalam husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya yote, ninaipongeza sana Serikali kwa ushirikiano wao mzuri tulioupata katika Wilaya ya Liwale katika kufuatilia kwa karibu sana, Ahadi za Mheshimiwa Rais kwa Wilaya hiyo. Ahadi ya darala la Mto Ruhuu katika barabara ya kutoka Liwale kwenda Kijiji cha Lilombe (km 50 kutoka Liwale), ambalo lilikuwa linafikika kwa tabu sana hasa wakati wa masika, wakati mwingine hujifunga kabisa baada ya daraja la awali kuharibiwa na mafuriko zaidi ya miaka kumi iliyopita.

Leo nachukua fursa hii kuthibitisha kwamba, daraja hili lilikamilika na kufunguliwa/kuzinduliwa na Mheshimiwa Rais, Novemba, 2007. Daraja hilo ni ukombozi mkubwa kwa Wananchi wa Lilombe na Liwale kwa ujumla na linaendea kutumika. Hata mbio za Mwenge mwaka huu tarehe 18 Juni, 2008 umetumia daraja hilo na kulala Kijiji cha Lilombe na kukimbizwa kuelekea Wilaya jirani ya Nachingwea. Haijawahi kutokea kwa zaidi ya miaka 20 iliyopita, kabla ya daraja la awali kukumbwa na mafuriko. Ninamshukuru sana Mheshimiwa Rais na Serikali yake, kwa kukamilika kwa daraja hilo ambalo ni kiungo kikubwa kupitia Lilombe kwenda Wilaya jirani za Nachingwea na Tunduru.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ahadi nyingine ya Mheshimiwa Rais ni Barabara ya Nangurukulu kwenda Liwale hadi Nachingwea. Jitihada za Serikali, zinaendelea vizuri. Baadhi ya mabasi yanayotumia barabara hiyo ya Nangurukulu kutoka Dar es Salaam, yanafika Liwale saa tisa mchana. Kabla ya hapo, safari hiyo ilikuwa ya kubahatisha na kuchukua zaidi ya siku moja.

Hata hivyo, uwezekano huu ni wakati wa kiangazi tu kwani masika Nangurukulu – Liwale hujifunga kutokana na mvua nyingi. Kwa vile Ahadi ya Mheshimiwa Rais ni kufanya barabara hiyo itumike wakati wote; masika na kiangazi na ndio maombi yangu kama Mbunge wa Liwale na ni mategemeo ya Wananchi wa Liwale.

Barabara hiyo itakapokamilika itachangia kwa kiasi kubwa, maendeleo ya Wananchi wa Liwale. Barabara hiyo ni fupi mno kutoka Dar es Salaam kwenda Liwale, inapolazimika kupitia Lindi ina mzunguko wa zaidi ya kilomita 300 na hivyo, kuongeza gharama za usafiri kwa wafanyabiashara wanaposafirisha bidhaa ziendazo Liwale.

Hali hii husababisha kupanda kwa maisha ya Wananchi wa Liwale, jambo ambalo ni kikwazo kikubwa kwa dhamira ya Serikali ya kumfanya kila Mtanzania kuwa na maisha bora.

Kwa kutumia *TANROAD* Lindi, ninaomba ipewe uwezo wa kutosha ili irekebishe sehemu korofi kati ya Nangurukulu na Liwale, vilele kwa barabara ya Liwale hadi Nachingwea. Kutokana na ushirikiano mzuri kati ya Uongozi wa Mkoa, Wilaya ya Liwale na *TANROAD* Lindi, barabara hizo zinaweza kukamilika endapo *TANROAD* Lindi itawezeshwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaipongeza sana Serikali kwa kuchukua hatua kuboresha maslahi ya Madiwani, ambao ni kiungo muhimu sana cha kusimamia maendeleo ya Wananchi katika Kata zetu na Wilaya kwa ujumla. Ninashauri wapewe mishahara ya uhakika, kwani muundo uliopo wa Madiwani katika Halmashauri zetu ni Wenyeviti tu ndio wenye uhakika kuishi kwa posho kutokana na safari za kikazi. Madiwani wengine wote ni suala la bahati kupata safari watakazopata posho.

Hivyo ni dhahiri kwamba, Madiwani hawa hali zao kimaisha ni duni mno, naomba Serikali iendelee kubuni namna ya kuboresha maisha yao kwa uhakika zaidi; vinginevyo, uongozi wao utapuuzwa na baadhi ya Watumishi wa Halmashauri ambao kipato chao ni kikubwa kuliko Madiwani.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaipongeza Serikali kwa kupeleka watumishi wenye sifa kuongoza Idara mbalimbali, naomba zoezi hilo liendelee. Sambamba na jitihada hizo za kuboresha utumishi katika Halmashauri zetu, mbinu zifanywe za kuboresha uelewa wa Madiwani katika shughuli zao, wapewe mafunzo ya mara kwa mara kuongeza uelewa wao katika shughuli za maamuzi ya kidiwani na kuwajibika kikamilifu.

Kwa hali ilivyo sasa, baada ya kuboresha watumishi katika Halmashauri zetu, *gap* ya uelewa kati ya watumishi wa Halmashauri na Madiwani, itaendelea kuwa kubwa na hivyo kuweka uwezekano wa Madiwani kuburuzwa kwa maamuzi ya msingi kimaendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapendekeza pawe na utaratibu ulio wazi na mzuri ili *DCs* wetu waweze kufuatilia vizuri shughuli mbalimbali za maendeleo katika Wilaya zetu. Hali ilivyo katika baadhi ya Wilaya *DCs* wanapata vikwazo katika kufuatilia shughuli mbalimbali katika Halmashauri zetu, inaonekana wanaingilia shughuli za Halmashauri ambazo ni washirika wakubwa wa maendeleo na ndio Serikali katika Wilaya zetu.

Ninashauri maagizo yote yanayotolewa Serikali, pamoja viwango vya fedha za maendeleo zinazotumwa kwa Wakurugenzi, nakala zipelekwe kwa Wakuu wa Wilaya na Wabunge husika; kwani maagizo mengi yanayopelekwa katika Halmashauri zetu Wakuu wa Wilaya na Wabunge hawana taarifa kwa vile baadhi ya vikao muhimu vya Halmashauri hufanywa wakati wa Vikao vya Bunge na hivyo hushindwa kushiriki. Kwa Majimbo yaliyo mbali na Dodoma kama Liwale, dhahiri ni vigumu kushiriki vikao vyote. Hivyo, ninashauri Serikali itoe mwongozo mzuri kwa Wakurugenzi ili Halmashauri zetu zipange vikao wakati Wabunge hawapo Bungeni ili tuweze kushiriki kikamilifu kwenye vikao hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna baadhi ya mashirika yanayokopesha wafanyakazi, huwalaghai watumishi katika baadhi ya Halmashauri zetu ikiwemo ya Liwale kwamba, wanatoa mikopo nafuu; wateja wanapojiunga hatimaye wanajikuta wanakatwa fedha nyingi tofauti na makubaliano kabla ya kukopa. Moja ya Kampuni inayowashawishi watumishi Wilayani ni Kampuni ya *Bayport Financial Services Ltd.* Baadhi ya watumishi, imeshakuwa kero kubwa kwa maisha yao. Kampuni hiyo, mtumishi akikopa Sh. 400,000 mwisho wa makato hulipa Sh.1,303,094.80. Ninaambatanisha nakala ya baadhi ya wateja/watumishi waliokumbwa na Makampuni hayo ya kutoa mikopo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninashauri Serikali iangalie kwa karibu zaidi Makampuni haya yanayojihusisha na utoaji wa mikopo hasa huko Wilayani na Vijijini. Hali hii inatokana na ukweli kwamba, *NMB* tu ndio iliyoko kwenye Wilaya zetu na hivyo kutoa mianya kwa Makampuni kama haya kupenya huko Mawilayani.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninawasilisha na kuunga mkono tena hoja kwa asilimia mia moaja.

**MHE. BUJIKU P. SAKILA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza sana Waziri Mkuu na Wasaidizi wake wa Karibu, Waheshimiwa Mawaziri; Mheshimiwa Celina Kombani na Mheshimiwa Philip Marmo na Naibu Waziri, Mheshimiwa Aggrey Mwanri. Aidha, nawapongeza pia Makatibu na Watendaji wote wa Wizara na Idara zote katika Wizara na Ofisi husika, walioshiriki kwa njia moja au nyingine katika kufanikisha uandaaji wa hotuba hii, ambayo ni nzuri na imetokea kupokelewa na wananchi wengi kwa matumaini makubwa sana.

Nampongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu na Wasaidizi wake, kwa kuwa hii ni bajeti yao ya kwanza tangu waingie katika nyadhifa zao. Kukubalika kwa hoja hii ni moja ya kigezo kuwa, wanakubalika mbele ya umma. Aidha, hii inaonyesha kuwa wao pamoja na Watendaji husika wa Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa na Ofisi ya Bunge, wapo karibu na jamii. Wamefanikiwa kwa kiwango cha juu, kugusa kero zinazowagusa Watanzania wa ngazi mbalimbali katika Hotoba hii ya kwanza ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Serikali imekuja na maelezo muafaka ya jinsi kero mbalimbali zitakavyoshughulikiwa. Ni muafaka kwa kuwa hotuba hii imepokelewa vyema na wengi. Nami kwa niaba yangu binafsi na kwa niaba ya Wananchi wa Jimbo la Kwimba, naunga mkono hoja hii.

Katika Hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, inaonyesha kuwa wawekezaji wengi wapo katika mikoa michache miradi mingi ikiwa Dar es Salaam na Mwanza. Naipongeza Serikali kwa kufungua milango kwa wawekezaji wa nje na ndani. Uwekezaji katika miradi, huibua ajira na ajira huinua kipato cha waajiriwa na eneo husika. Miradi mingi kuwekwa maeneo fulani tu hujenga madaraja ya watu. Naiomba Serikali ibuni mbinu kuwashawishi wawekezaji wasambae na kadiri itakavyowezekana, waende na Vijijini.

Kwa mfano, kwenye Hotuba inaonekana kuna miradi 51, ukifuatilia miradi mingi inaweza kuwa mjini Mwanza na Wilaya zinazobaki zikawa na miradi 1, 2 au 3 kila moja. Hii ni dhahiri, itaendela kuvuta watu kwenda mijini na kuzidisha umaskini Vijijini kwa kuwa wanaoondoka Vijijini wengi huwa ni vijana ambao ndiyo nguvu kazi. Hivyo, wawekezaji katika Kilimo hususan katika Mikoa na Wilaya zilizo nyuma waungwe mkono na Serikali kwa kupewa ruzuku au kusamehewa kodi kama inavyokuwa kwa wawekezaji katika madini.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Serikali kwa Programu ya Uboreshaji wa Mfumo wa Serikali za Mitaa. Matunda yanaonekana, juhudi ziongezwe kuiimarisha Programu hii. Hatua zinazochukuliwa ziendelee kushuka chini zisiishie Wilayani.

Ruzuku ya Maendeleo ni utaratibu mzuri. Naomba utaratibu uangaliwe vizuri zaidi. Kuiadhibu Halmashauri kwa kosa la Watendaji lisilogusa Madiwani moja kwa moja ni kuwaadhibu wananchi. Bado ninaamini pamoja na kuwa rufaa tumekata na hatuna imani kama kweli itasikiliwa na kubadili maamuzi ya awali, kuinyima Ruzuku Halmashauri ya Wilaya ya Kwimba ni kuionea.

Kama tulivyokwishaeleza, ulikuwa upungufu ya Wizara husika na uamuzi wa wachache, kwa sababu wanazozijua wenyewe tukanyimwa ruzuku hiyo. Hata hivyo, aliyeshika mpini si wa kubishana naye utaishia kukatwa, tunasubiri hukumu yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza sana Serikali kwa kuona umuhimu wa maslahi ya Madiwani. Naomba utekelezaji wake usichelewe kwanza. Watafanya vizuri zaidi kwa nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Serikali ikubali kupandisha sifa ya kuwa Diwani hususan kwa elimu. Kwango cha Kidato cha Nne kiwe cha chini. Hii itakuwa na

maana zaidi ukizingatia kuwa Elimu ya Msingi ni ya kila mtu na kila mtu anaruhusiwa kujiendeleza; Kila Kata ina shule ya sekondari; na itasaidia kuongeza mijadala mizuri zaidi ya maendeleo katika Vikao vya Halmashauri.

Pamoja na kuboresha maslahi ya Madiwani, naiomba sana Serikali iangalie juu ya posho ya Madereva wa Wabunge. Ni jambo la msingi kwa Wabunge ambao kutokana na hadhi zao na mawazo mengi, kujiendesha wenyewe ni hatari hasa tunapoelekea kwenye uchaguzi na baada yake. Naomba sana Serikali izingatie ombi hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. MANJU S. O. MSAMBYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali yote, napenda nitamke kuwa naunga mkono hoja. Hata hivyo, ninayo maangalizo yafuatayo:-

Barabara ya Kigoma hadi Dodoma na hatimaye kuunganisha na Dar es Salaam kupitia Tabora, Igalula, Itigi na Manyoni, ipewe kipaumbele. Barabara hii itakuwa ni mtego wa kupata fedha nyingi zilizolala *DRC,* Burundi, Rwanda na hata Zambia. Tunalo Shirika la Reli, ambalo huduma zake zikisaidiwa na Barabara hii, uchumi wa Tanzania kwa ujumla na ule wa Wakazi wa Kigoma, Uvinza, Nguruka, Kaliua, Urambo, Tabora, Goweko, Itigi hadi Manyoni utakua. Kwa hali hiyo ni vyema Serikali ifanye kila liwezekanalo, kusimamia barabara hii ili kuwaondolea adha wakazi wa Kigoma na maeneo ambayo barabara inapita.

Daraja la Malagarasi litakuwa mkombozi kwa wakazi wa Mkoa wa Kigoma na Tabora. Tunaamini kuwa, Serikali ya Korea Kusini ni mdau makini wa maendeleo ya maeneo ambayo yatahudumiwa na daraja hilo.

Daraja la Malagarasi litahudumia wananchi walio wengi na kwa hali hiyo kukuza uzalishaji wa kilimo, uvuvi, ufugaji, urinaji asali na biashara kwa ujumla wake.

Waziri atakapojumuisha ni vyema kupitia Bunge hili, akatoa kauli ya kutambua mchango wa Serikali ya Korea Kusini kwa kutoa fedha za Daraja la Malagarasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, *TRC* imebadili jina na kuwa *TRL* chini ya muwekezaji mbia. Kweli hadi Menejimenti mpya inakabidhiwa Shirika hili, huduma zikiwa zimedorora. Hata hivyo, kudorora kulikokuwepo wakati ule, hakukuweza kufanya abiria kubebwa kama nyanya ndani ya tenga kama ilivyo sasa.

Safari za treni zimepunguzwa kutoka nne kwa wiki na kuwa mbili, hali hiyo inafanya abiria wakae hadi chooni. Tatizo linalosababisha huduma za shirika la reli kuwa mbovu ni Serikali kutotoa mchango wake katika ubia kama inavyoelezwa katika

Mkataba. Taarifa nilizonazo (kama ni sahihi) ni kwamba, siku 11 zilizopita Serikali imeanza harakati za kutoa mchango wake.

Hata hivyo, tatizo lingine ni urasimu wa Serikali yetu katika kusaidia kupata ufumbuzi jadidi wa kutatua matatizo ya Shirika la Reli *(TRL)*. Miezi ya hivi karibuni, Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano, alifanya ziara nchini India. Serikali ya India iliahidi kutoa $ 43 milioni kusaidia uimarishaji wa *TRL*.

Hii ni kwa sababu *RITES* ambayo imeingia ubia na Serikali ya Tanzania ni Kampuni ya India. Ieleweke wazi kuwa, kauli ya Serikali ya India ilitakiwa ifutwe na mawasiliano rasmi ya maombi toka Serikali yetu.

Vilevile iIeleweke kuwa Watendaji wanapata kigugumizi kufanya hilo. Hivi ni kwa sababu hawana maslahi binafsi? Naomba Mheshimiwa Waziri Mkuu aliangalie hili

Mheshimiwa Naibu Spika, naishukuru Serikali kwa juhudi zinazofanywa na ujenzi wa barabara hii. Barabara hii inatakiwa mbali na kuwa ya kichumi (Kilimo, Uvuvi na Biashara), pia ni barabara ya ulinzi na inatakiwa itoke Kalya na kuunganisha Mkoa wa Rukwa. Barabara hii nahitaji madaraja 67.

Napongeza juhudi za *TANROADS*, pamoja na Uongozi wa Mkoa chini ya Mkuu wa Mkoa, Col. Joseph Simbakalia. Barabara inakwenda lakini inasuasua kutokana na suala la madaraja.

Hata hivyo, naiomba Serikali ifanye chini juu, pale Mto Malagarasi Kijiji cha Ilapala, liwekwe daraja badala ya kuwekwa *panton* (kivuko) ambacho hakifanyi kazi wakati wa masika. Hii ni kwa sababu kivuko hicho kina injini chakavu ambazo haziendani na mkondo mkali wa mto.

Mheshimiwa Naibu Spika, uharamia umekithiri Ziwa Tanganyika. Majambazi wanaotoka *DRC* na pengine Burundi, wanawasumbua kwa kuwaibia zana za uvuvi wanavijiji wanaojishughulisha na uvuvi. Nashauri juhudi binafsi za ulinzi wa wavuvi na zile za Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Wilaya na Mkoa, zipatie nguvu ya zana za kisiasa za doria (boti ziendazo kasi).

Mheshimiwa Naibu Spika, huu ni wakati muafaka kwa Serikali itoe kauli kuhusu suala la Tanzania kujiunga na *OIC* kama ilivyoahidi mwaka 1993, baada ya kutingishwa na kundi la *G55*. Serikali wakati ule iliahidi kutoa mwongozo wa jinsi Tanzania itakavyojiunga na *OIC*. Inashangaza yamekuwa yakitolewa maneno ya kuhusisha *OIC*

na Uislam, lakini Uganda, Msumbiji na nchi ambazo sio za Kiislam ni wanachama. Hivi taasisi za dini kupinga Tanzania kujiunga na *OIC* ni kwa maslahi ya nani; dini, makanisa au nini?

Hivi kuna maslahi gani kwa madhehebu tofauti na Waislamu kuwa mstari wa mbele kupinga kuwapo Mahakama ya Kadhi? Mahakama ile ni kwa maslahi ya waislamu tu; kwa nini wasio Waislam waifanye Serikali kushindwa kutekeleza Ilani yake kuhusu suala hili?

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Serikali itoe kauli ili kepusha kuleta hoja binafsi Mkutano wa Kumi na Tatu.

**WAZIRI WA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kule Pemba kuna ngoma inaitwa Msewe na sehemu zingine kuna ngoma mbalimbali, ngoma hizi huchezwa mchana na nyingine huchezwa usiku ni kuwadhalilisha wananchi wa nchi hii kudhani kwamba kila wanapokutana usiku shughuli ni moja tu. Ndiyo maana tunasema kazi kubwa tunayoifanya ni kuelimisha wananchi. Lakini kudhani kwamba watu hawa wanapokutana madhali kuna giza basi shughuli ni kushughulikiana tu, si sahihi. (*Kicheko*)

**NAIBU SPIKA**: Waheshimiwa Wabunge muda wa maswali umeisha na maswali yameisha. Haya mengine mnayafanya kuyazulia tu. Tabia za watu ni za watu iwe kwenye ngoma, iwe kwenye mwenge, tabia za watu ni watu tu. Ni vizuri mkajichukulia suala hili kwa makini sana kwa sababu ni shida, kabisa. Baada ya kusema hivyo Waheshimiwa Wabunge mimi naomba niwapongeze kwa dhati Waheshimiwa Mawaziri kwa majibu yao mafupi yanayolenga kwenye hoja. Nyie wenyewe mnaona kabisa tukiwa namna hiyo mnakuta Bunge linakuwa changamfu sio anatuhutubia mtu mmoja mpaka tunalala usingizi. Sasa hii mimi nawapongeza sana kuna maendeleo makubwa kabisa na mfanye vizuri zaidi ya hapo. Kasoro ipo wauliza maswali wanauliza maswali wakati mwingine gazeti zima. Mnajua hatari ya kufanya hivyo. Wakati tunakaa hapa redio inatangaza moja kwa moja. Sasa swali lako likiwa refu mtangazaji atalisomaje lote swali refu mno? Maana unapouliza unasema naomba swali langu namba fulani lipatiwe majibu. Lakini mtangazaji analazimika kulisoma kusudi wananchi wajue uliuliza nini. Sasa wewe umeuliza *page* nzima mtangazaji atakuwa na muda kweli wa kusoma *page* hiyo na akaenda na wakati? Hiyo ndiyo hasara ya kuuliza maswali marefu na tunataka yaishe saa nne kwa sababu ikifika saa nne redio inazima. Kwa hiyo wanaouliza baada ya saa nne hawatangazwi *live*. Kwa hiyo, ndiyo maana tunataka ku-*stic* kwenye maswali mkiuliza mafupi, mkajibiwa kifupi na maswali ya nyongeza yakawa mafupi wote mtakuwa *covered*. Lakini nawapongeza Mawaziri kwa safari hii. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, matangazo ya wageni. Leo Naibu Spika hana matatizo ya kusoma vikaratasi ana karatasi rasmi. Wageni walioko Bungeni asubuhi hii. Kwanza kuna wageni wa Mheshimiwa Dr. Wilbrod Slaa, ambao ni Wajumbe 36 wa Kamati Kuu ya Taifa ya CHADEMA, wakiongozwa na Mwenyekiti wa Taifa Mheshimiwa Freeman Mbowe naomba wasimame wajumbe wote. Mzee wetu Mheshimiwa Edwin Mtei yupo, nadhani bado yupo safari. Halafu kuna Balozi Christopher Ngaiza, kuna Profesa

Mwesiga Baregu na baadhi ya Wakurugenzi wa Sekretarieti Kuu ya Chama. Wote hao wapo hapa mjini Dodoma kwa ajili ya Mkutano wa Kamati Kuu ya CHADEMA. Hawa wengine nimewataja hawakuonekana inaelekea bado wapo safarini wanakuja.

Tunao pia wageni wa Mheshimiwa Mtutura Abdallah Mtutura, ni Ndugu Said Zubeir Makandu, Mwenyekiti wa Taasisi isiyo ya Kiserikali inaitwa *HEDEFO*, karibu sana. Halafu tuna Ndugu Maulid Kalambo Maulid, Katibu wa Mbunge Tunduru. Karibuni sana wageni kutoka Tunduru.

Tuna wageni wa Mheshimiwa Charles Keenja, wako Madiwani 15 wa Kamati ya Mipango mji wakiongozwa na Mwenyekiti wao Mheshimiwa Diwani Rajabu Hasani na Mheshimiwa Diwani Ahmed Mwilima ambaye ni Naibu Meya wa Jiji la Dar es Salaam. Naomba Naibu Meya asimame na hawa wengine wote naomba wasimame, nadhani wengine wamechelewa kidogo. Halafu tuna wageni wa Mheshimiwa Fatma Othman Alli ni watoto wake watatu naomba wasimame na Madiwani sita kutoka Mkoa wa Mjini Magharibi Zanzibar, naomba wasimame walipo. Karibuni sana Waheshimiwa Madiwani. (*Makofi*)

Tuna wageni wa Mheshimiwa Celina Kombani Waziri katika Ofisi ya Waziri Mkuu anayehusika na Mambo ya TAMISEMI. Yupo Mr. S.K. Pongolani ambaye ni mume wake, karibu sana mkeo anafanya kazi nzuri. Pamoja naye ni watoto wake Shaban. Karibuni sana sisi Mheshimiwa Kombani tunamtegemea sana katika harakati zetu.

Mheshimiwa Hoogan ana wageni wake yupo Profesa Gati Andrew. C*an you please stand up, I don't who is?* Huyu ni *Director* kwenye Cancers African Studies Centres pia ni mzungumzaji wa lugha ya Kiswahili. Yupo yule pale karibu sana nasikia wewe ni mzungumzaji mzri wa Kiswahili. Halafu tuna wageni wa Mheshimiwa Benedict Ole Nangoro, ni wanafunzi 20 na walimu wawili kutoka shule ya sekondari ya Kiteto karibuni sana naomba msimame wote.

Tuna wageni wa Mheshimiwa Mwanawetu Zarafi, ni Bwana Suleman Bungala jina maarufu anaitwa Bwege ndiye mume wake. Bwana Bwege karibu sana mume wake na Mheshimiwa. Yupo Bwana Deo Chaurembo Mkurugenzi wa Siasa *CUF* Wilaya ya Kilwa, karibu sana na mdogo wake Salum Mayanga, karibuni sana. (*Makofi*)

Tunao wageni wengine ambao ni Wanafunzi wa Udaktari wa Binadamu kutoka *The Herbert Kairuki Memorial University Dar es Salaam* wako 35 wanaweza kusimama walipo. Ok karibuni sana Madaktari tunawategemea kwa siku zijazo karibuni sana. (Makofi)

Tuna wanafunzi 50 kutoka Shule ya Sekondari Jamhuri, Dodoma. Karibuni sana na Bunge lipo katika eneo lenu kwa hiyo ni haki yenu kuja kila wakati. Halafu tuna Ndugu Lucas Kisasa Katibu wa Yanga na nadhani wale wapenzi wa mnamjua huyu,

karibuni sana. Kwa hiyo, Kisasa unaona ulivyo na wanachama wengi humu ndani. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge nawashukuru kwa kuleta majina kwa utaratibu huu yanasomeka kwa urahisi. Sasa matangazo ya shuguli za leo kwa Kamati mbalimbali.

Mheshimiwa Issa Khatib Mwenyekiti wa Kamati ya Viwanda na Biashara anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati hiyo kwamba leo tarehe 27 kutakuwa na Kikao cha Kamati. Kikao hicho kitafanyika saa tano asubuhi katika ukumbi namba 227 jengo la utawala. Mheshimiwa Jenista Mhagama, Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii anawatangazia Waheshimiwa Wenyeviti, Makamu Wenyeviti na Waheshimiwa Wabunge wote walioandikiwa barua kuhudhulia mjadala baina ya Wajumbe wa Kamati za Kudumu za Bunge na Asasi za Kiraia. Mjadala huo utafanyika Jumapili tarehe 29/6/ kuanzia saa tano asubuhi katika Ukumbi wa Pius Msekwa. Kwa hiyo, mtakutana siku ya Jumapili saa tano.

Mheshimiwa Dr. Raphael Chegeni, Mwenyekiti wa *CPA, Tanzania Branch,* anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati ya Utendaji ya *CPA* tawi la Tanzania kuwa kutakuwa na Kikao cha Kamati katika chumba namba 219 ghorofa ya pili katika jengo la utawala leo saa saba mchana.

Kuna tangazo la kongamano, kesho Jumamosi tarehe 28 Juni, 2008kutakuwa na Kongamano kwa Waheshimiwa Wabunge wote litakaloanza saa tatu asubuhi katika Ukumbi wa Msekwa. Kongamano hilo linahusu usalama na ubora wa chakula kwa watunga sera na wenye kutoa maamuzi nchini. Waandaji wa kongamano hilo ni Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Viwango Tanzania. (Makofi)

Mheshimiwa Jenista Mhagama, Mwenyekiti wa Kamati ya Tafrija anaomba kuwatangazia wajumbe kwamba tarehe 28 Juni, 2008 kesho kutakuwa na burudani iliyoandaliwa kwa jina la usiku wa ki-Zanzibar itakayofanyika katika ukumbi wa tafrija za Bunge. *Basement Area* kuanzia saa moja jioni.

Waheshimiwa Wabunge wote mnakaribishwa ili waburudike na burudani zifuatazo. Kuna mziki wa dansi ya kiarabu, taarab, muziki mchanganyiko muziki wa zamani, Bongo flava na tenzi. Hapa si Wabunge tu na hata watu wa nje wanakaribishwa maana dansi hamuwezi kucheza peke yenu inabidi mcheze na watu wengine.

Baada ya kusema hivyo Waheshimiwa Wabunge tulikubaliana toka jana kwa sababu leo tunapenda kuhitimisha hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu na kama mnavyojua mmeshachangia kwa muda wa siku hizo tano na kwa Wabunge wengi sana wameandika michango yao kwa maandishi. Kwa sababu jioni tutaingia kwenye Kifungu kwa Kifungu na hiyo kunakuwa na Ofisi ya Waziri Mkuu yenyewe, Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za MIkoa na Serikali za Mitaa nafikiri kuna mafungu kama matatu.

Sasa ili kutoa muda mzuri kwa watu kupata nafasi nzuri kwa hiyo tunaingia moja kwa moja katika wachangiaji. Nafikiri tuanze na Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za MIkoa na Serikali za Mitaa.

**MWONGOZO WA SPIKA**

**MHE. MASOUD ABDALLA SALIM:** Mwongozo wa Spika.

**NAIBU SPIKA:** Mwongozo wa Spika, Mheshimiwa Masoud Abdalla Salim, Kanuni gani.

**MHE. MASOUD ABDALLA SALIM:** Mheshimiwa Naibu Spika, Kanuni ya 68 (7).

**NAIBU SPIKA:** Inasemaje?

**MHE. MASOUD ABDALLA SALIM:** Mheshimiwa Naibu Spika, Kanuni ya 68 (7), Mbunge anaweza kusimama wakati wowote ambapo hakuna Mbunge mwingine anayesema na kuomba Muongozo wa Spika kuhusu jambo ambalo limetokea Bungeni mapema ili Spika atoe ufafanuzi kama jambo hilo linaruhusiwa au haliruhusiwi kwa mujibu wa Kanuni na Taratibu za Bunge na majibu ya Spika yanatolewa papo hapo na baadae kadri atakavyoona inafaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati jana nikichangia hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu niligusia suala zima la bomoa bomoa Mjimwema Chang'ombe na baada ya hapo nilieleza kwamba kuna baadhi ya walionyanyaswa na Polisi na nilitakiwa kutoa uthibitisho na Waziri mhusika Mheshimiwa Marmo. Nilimpelekea majina kama alivyotaka, jina la mama aliyekuwa na kichanga na wale ambao walinyanyswa na Polisi. Hata hivyo akaniambia majibu hayatoshelezi na naaahidi kumpa mashirikiano ya hali ya juu. Naomba nimpe mashirikiano hayo kama ifuatavyo:-

**NAIBU SPIKA:** Ngoja kwanza Mheshimiwa Mbunge. Wakati unachangia jana uliombwa kuhusu utaratibu na muongozo wa Spika kwamba. Je, kuna ushahidi wa majina hayo? Kiti tukakwambia upeleke majina hayo kwa Waziri anayehusika wakati anajibu aweze kuwa ameyafanyia kazi majina hayo.

Sasa huwezi kuanza kujibu sasa hivi. Wewe subiri ajibu atakapokuwa hajajibu kwa kuridhisha ndiyo tunaingia kwenye vifungu baadaye jioni. Sasa huwezi kuanza kujibu sasa hivi itakuwa kama tunaingia kama *club* ya wazungumzaji tu.

Wewe jana ulizungumza nikakuagiza kwamba baada ya kutoa muongozo wa Spika kwa Waziri aliyekuwa anataka mwongozo kuhusu wewe kama una majina hayo mpelekee mtoa hoja.

Lengo letu lilikuwa akapate muda wa kutafuta majibu hayo. Wakati atakapokuwa anajibu kuanzia yoyote atakayeanza kujibu watajibu.

Wewe hujaridhika tutaingia kwenye vifungu wakati wa mchana utasimama kwamba sijaridhika na majibu kutokana na maelezo yako utakayokuwa nayo wakati huo. Kwa sasa ulivyopeleka umefanya vizuri. Tunaendelea. Katibu endelea na *Order Paper.*

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI)**: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa vile hii ni mara yangu ya kwanza kusimama hapa kwa ajili ya kuchangia hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu na kwa vile ningependa iingie katika rekodi, ningependa tena kwa mara ya pili kuchukua nafasi hii kumshukuru sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, ambaye alinipa mimi na wananchi wa Siha heshima kubwa ya kuwa Naibu Waziri katika Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI).

Naomba niseme hapa kwamba nitaendelea kushirikiana na Mheshimiwa Rais pamoja na Viongozi wote akiwemo Waziri Mkuu kutoa ushirikiano wangu na kumsaidia katika kazi zake kwa kadri Mwenyezi Mungu atakavyonijalia. Naomba nichukue fursa hii pia kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kuteuliwa kwake kuwa Waziri wetu Mkuu katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Ninapenda kusema kwamba tunamshukuru kwa kadri ambayo amekuwa anatulea tangu nilivyoingia katika Ofisi nimepata msaada mkubwa sana na amekuwa akinielekeza na kuniongoza. Ninachoweza kusema kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu nitaendelea kushirikiana naye kwa karibu sana na kumsaidia ili kazi yake iweze kuwa nyepesi.

Hivyo hivyo napenda kutoa salamu na shukrani zangu kwa Mheshimiwa Celina Kombani na kwa kweli kumpongeza kwa kuchaguliwa kuwa Waziri wa Nchi katika Ofisi ya Waziri Mkuu. Toka nimeingia katika Ofisi hii amenisaidia sana katika majukumu yangu na ameniliea vizuri na anaendelea kushirikiana na mimi.

Ninachoweza kumhakikishia Mheshimiwa Kombani ni kwamba nitaendelea kushirikiana naye kuhakikisha kwamba kazi ambazo anazifanya za kulijenga taifa letu zinafanyika kwa umakini mkubwa. Napenda kuwashukuru pia Katibu Mkuu Mama Maimuna Tarishi pamoja na Ndugu Mbonde Msaidizi wake pamoja na Wakuu wa Idara wote katika Wizara yetu ambao tumekuwa tukishirikiana katika majukumu mpya na katika upya wangu huu imenisaidia sana.

Kipekee napenda kuwashukuru wananchi wangu wa Siha pamoja na familia yangu ambayo walinienzi sana na kunipa fursa hii ya kuja hapa. Bila wananchi wa Siha

kufanya maamuzi ambayo waliyafanya mimi naamini kabisa kwamba isingeliwezekana nikawa nimesimama hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nimekuwa upande huu sasa na nimejaribu kuangalia mambo ambayo tumekuwa tunayafanya toka mwanzo tulipoanza na Wizara ya Fedha na mpaka tulipofika hapa tulipofika. Jambo moja kubwa sana ambalo limejitokeza katika mijadala yetu miwili, huu wa Waziri ya Fedha na huu wa Waziri Mkuu ni suala ambalo Wabunge wengi wamelizungumzia hapa la kuhakikisha kwamba tunakuwa na Bajeti ya kujitegemea. Mimi naamini kwamba kama tutakwenda hivyo tunavyokwenda itatusaidia sana katika nchi yetu kwa sababu hatuwezi tukakaa hapa tunawategemea Wahisani kwa ajili ya kuendeleza nchi yetu.

Mimi nafikiri ni vizuri sasa tukaingia kwenye huo mkondo wa kufikiri kwamba sisi wenyewe ndani tufanye nini ili kuweza kuwaletea Maendeleo kwa ajili ya nchi yetu. Badala ya kukaa tunawategemea wahisani. Kwa kuanza naomba nichukue fursa hii kuunga mkono Hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu asilimia mia moja na kwa vile muda niliopangiwa hapa ni mfupi sana nitaomba niende haraka yale masuala yanayohusu sekta nyingine na Wizara nyingine tumewaomba wale wenzetu watusaidie. Mheshimiwa Waziri Mkuu atakapokuja atazungumza zaidi lakini sisi tutajikita zaidi kwenye maeneo yanayotuhusu na mengine tumemwachia Mheshimiwa Waziri Mkuu ayajibu na Mheshimiwa Marmo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wa kwanza uliokuwa unahusu maslahi ya Madiwani na viongozi wengine wa ngazi za mwanzo na mawazo haya yaliletwa na Mheshimiwa George Lubeleje ambaye ni Mwenyekiti wa Katiba na Sheria, Mheshimiwa Jacob Shibiliti, Mheshimiwa Wilbrod Slaa, Mheshimiwa Kabuzi Rwilomba, Mheshimiwa George Simbachawene, Mheshimiwa Stephen Galinoma na Mheshimiwa Abbas Mtemvu na ningependa tu kusema kwamba suala hili la maslahi ya Madiwani linashughulikiwa kama ilivyoonyeshwa katika Hotuba ya Waziri Mkuu, ukurasa wa 62 aya ya 102 kwamba Serikali imekubali kuboresha maslahi ya madiwani kuhusu posho, matibabu, kiinua mgongo na kuwapatia vyombo vya usafiri na kutoa unafuu wa kodi. Kwa mwaka 2008/2009 jumla ya shilingi bilioni 4.8 zimetengwa kwa ajili ya posho ya mwezi kwa ajili ya Waheshimiwa Madiwani.

Aidha marekebisho ya Sheria yatafanyika ili kuwawezesha Waheshimiwa mbalimbali kulipwa posho zao za matatibu, kiinua mgongo na kuwapatia vyombo vya usafiri na kutoa unafuu wa kodi. Sheria ilivyokaa sasa hivi haituwezeshi kufanya hivyo lakini tunasema kwamba tutafanya haraka iwezekanavyo kuhakikisha kwamba sheria inakaa kwa namna ambayo Madiwani wanaweza wakapata hizi huduma. Suala la maslahi ya viongozi ambao wapo katika ngazi za vijiji na kuna kilio kikubwa sana hapa kwamba wenyeviti wa vijiji nao tungewaangalia na wale watendaji wengine walioko kwenye zile ngazi za chini kwa maana ya ngazi za msingi. Hili nalo linafanyiwa kazi na wakati mufaka utakapofika tutahakikisha kwamba tunatekeleza kama ilivyoelekezwa hapa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja ya pili ambayo ililetwa na Mheshimiwa George Malima Lubeleje ambayo inazungumzia Waheshimiwa Wabunge waelimishwe juu ya maboresho ya Serikali za Mitaa awamu ya kwanza na awamu ya pili. Katika awamu ya kwanza ya maboresho Serikali ilitoa elimu kwa wadau mbalimbali wakiwemo Waheshimiwa Wabunge. Katika awamu ya pili Serikali itaendelea kutoa elimu ya maboresho awamu ya kwanza na ya pili kwa Wabunge wote kadri ya uwezo wa fedha utakavyoruhusu. Tutaangalia uwezekano wa awamu hii ya pili kwa kufanya semina katika Bunge mwezi Novemba 2008. Huu ni ushauri ambao umetolewa hata tulipokutana katika Semina na ilishauriwa kwamba Wabunge waweze kupata semina kwa ajili ya maboresho, tunaangalia uwezekano huo na tunaangalia kipindi hiki cha Bajeti haionekani kama itawezekana lakini ahadi tunayoitoa hapa ni kwamba mwezi Novemba tutajitahidi kuhakikisha semina hii inafanyika.

Mheshimiwa George Lubeleje pia alizungumzia Mikoa iangalie uwezekano wa kujenga ofisi, nyumba mpya endapo gharama za kukarabati zinakaribia zile za ujenzi na Wabunge wengi wamezungumzia jambo hili. Tumelitafakari, tumeliangalia tumeona kwamba kweli takwimu zinaonyesha kwamba kuna maeneo ambayo watu tunakwenda tunakarabati nyumba lakini ukiangalia gharama za ukarabati zinazidi hata zile za kujenga nyumba mpya. Kwa hiyo, ushauri huu tumeukubali na tumeuchukua na tutaufanyia kazi. Serikali itenge fedha za ujenzi wa jengo la Mkuu wa Mkoa wa Dodoma.

Mawazo haya pia yameletwa na Mwenyekiti Mheshimiwa George Lubeleje. Katika mwaka wa fedha wa 2008/2009 Serikali imetenga kiasi cha shilingi bilioni 1.2 kwa ajili ya kuanza kujenga jengo la Ofisi ya Mkuu wa Mkoa na Serikali itaendelea kutenga fedha kwa ajili ya ujenzi huo. Mheshimiwa Lubeleje pia alizungumzia hali ya jengo la Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Pwani litazamwe upya ili kulingana na hali ya udongo. Tunachosema hapa ni kwamba tunafanya tathimini ya kitaalam ili kubaini tatizo lililopo. Matokeo ya tathimini hiyo yatasaidia Serikali katika kufanya uamuzi sahihi. Kwa hiyo hili tunalifanyia kazi tumeliona na tutapeleka wataalam pale ili waweze kufanya utafiti wa kufanya lakini baadaye tuhakikishe kwamba linatekelezwa. Mheshimiwa Lubeleje pia alisema Kamati inashauri mbinu za ushirikishaji wananchi katika shughuli za maendeleo. Huu ni mfumo ambao unatumika katika upangaji mipango, tunatumia mfumo huo huo kwa fursa na vikwazo kwa maendeleo. Hizi ni *O* and *OD* na mambo mengine kama hayo. Kwa hiyo hili tunalichukua moja kwa moja suala la *oppotunities and obsticles to development.*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sana anasema taarifa za Bajeti za Mikoa ziainishe mafanikio na matatizo. Ushauri huu tunauzingatia na tumeuchukua. Mheshimiwa Wilbrod Slaa, Mbunge wa Karatu na Mheshimiwa Jacob Shibiliti, Mbunge wa Misungwi amezungumzia ujazaji wa nafasi wazi za uongozi katika ngazi za vijiji na vitongoji. Jibu ni kwamba nafasi wazi zinapaswa kujazwa katika siku sitini toka Mkurugenzi wa Halmashauri kupokea taarifa ya kuwepo nafasi wazi. Hata hivyo Ofisi yangu itafuatilia kilichotokea maeneo hayo hadi uchaguzi ukachelewa kufanyika hadi sasa na kurekebisha kasoro hiyo. Kwa Mheshimiwa Slaa na Mheshimiwa Shibiliti tunataka tufuatilie jambo hili kuona kwamba nini kilichotokea mpaka ikawa hivyo lakini kama nilivyosema utaratibu unataka kwamba katika siku sitini uchaguzi uwe umeitishwa.

Mheshimiwa Slaa amezungumzia pia kuzuiliwa kwa shughuli za maendeleo kwenye vijiji vinavyoongozwa na vyama vya upinzani. Azma ya Serikali ni kusimamia maendeleo ya Watanzania bila kujali itikadi zao. Uchaguzi ukimalizika pale na kumpata Mwenyekiti pale, hatuna tena habari ya itikadi inakuwa imekwisha na tunachoangalia pale tunaangalia itikadi ya nchi kwa maana ya Ujamaa na Kujitegemea.

Kwa hiyo, kiongozi yoyote anapokuwepo pale, ndiyo katika Katiba ya Nchi hii tunazungumza habari za ujenzi wa Ujamaa na Kujitegemea. Kwa hiyo tunapoingia pale kazi inayofanyika pale ni kuhakikisha kwamba tunaleta maendeleo kwa ajili ya wananchi wetu kuhakikisha kwamba wanapata huduma muhimu. Hili jambo kama linafanyika kweli kama alivyosema Mheshimiwa Slaa tutalifanyia uchunguzi lakini tunataka kusema kwamba msimamo wetu ni huo kwamba kiongozi wetu akishachaguliwa pale anakuwa ni kiongozi kwa ajili ya Maendeleo ya watu wote bila kujali itikadi zao. *(Makofi)*

Serikali, ikipatia gari la wagonjwa kituo cha afya Malya. Hili wazo lilikuwa la Mheshimiwa Richard Ndassa wa Sumve. Majibu yake ni kwamba kituo cha afya cha Malya ni miongoni mwa vituo mbalimbali nchini vinavyohitaji magari ya wagonjwa. Katika mwaka wa fedha 2008/2009 Serikali ina mpango wa kununua magari 100 kwa ajili ya vituo vya afya na hospitali za Wilaya. Kutokana na ufinyu wa Bajeti Serikali imeshindwa kutenga fedha kwa madhumuni haya. Hivyo Halmashauri ya Wilaya ya Kwimba inashauriwa kutafuta vyanzo vingine vya fedha ili kununua gari hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Savelina Mwijage, Mbunge wa Viti Maalum, alizungumzia Hospitali ya Mkoa wa Kagera iboreshwe kwa kuongezewa fedha na vifaa. Ninaomba kujibu kama ifuatavyo. Upo mpango wa Serikali wa kuboresha Hospitali zote nchini. Kutokana na mpango huo Hospitali zote za Mikoa zitakuwa za Rufaa kwa Mikoa husika na za Wilaya zitakuwa za Rufaa kwa Wilaya husika. Kutokana na Mkakati huo wa Serikali uboreshaji uliopo ni pamoja na kuziongezea hospitali hizo fedha na vifaa. Kwa mwaka 2008/2009 Hospitali ya Mkoa wa Kagera imetengewa kiasi cha shilingi milioni 140.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Mwijage pia alizungumzia kuhusu hospitali ya mkoa ina upungufu wa madaktari na wataalam licha ya kuwepo kwa vifaa vya *X ray* na kadhalika. Majibu yake ni kwamba Serikali inao wajibu wa kuboresha vituo hivyo vya kutolea huduma za afya zikiwemo Hospitali za Mikoa. Kwa mujibu wa Ikama Hospitali za Mikoa kama Kagera inatakiwa iwe na Madaktari 19. Madaktari waliopo kwa sasa ni 14 na upungufu wa madaktari ni wa tano. Hivyo Hospitali ya Mkoa wa Kagera inaonekana kuwa na hali nzuri ikilinganishwa na Hospitali nyingine za Mkoa. Hata hivyo Ofisi yangu itawasiliana na Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii ili kupunguza tatizo la upungufu wa Madaktari katika Hospitali za Mikoa.

Mheshimwia Lucy Fidelis Owenya alizungumzia kuhusu mgawanyo wa rasilimali katika Mikoa uzingatie ukubwa wa Mikoa na Wingi wa watu. Ushauri huu umepokelewa na tutaendelea kuuzingatia katika utendaji wake.

Majengo mapya na marefu yaangaliwe ili yaendane na mfumo wa maji taka. Ushauri huu ulitolewa vilevile na Mheshimiwa Owenya na tunasema hapa kwamba sisi tunaukubali ushauri huu umezingatiwa na utafanyiwa kazi.

Serikali iangalie muudo wa Ofisi ya Elimu ya Mkoa, hili pia, Mheshimiwa Owenya kalizungumzia ili kuendana na majukumu ya sasa. Majibu yake ni kwamba, muundo wa Sekretarieti ya Mkoa, ulipitishwa na Serikali, Agosti mwaka 2007 ambapo sehemu ya Elimu Mkoa, itakuwa na Maafisa Elimu watano. Hata hivyo, baada ya Shule za Sekondari kukabidhiwa Halmashauri, Mikoa itakuwa na majukumu makubwa ya kuratibu uendeshaji wa Shule hizo. Hivyo, muundo wa Sekretarieti za Mkoa, utafanyiwa mapitio ili uendane na majukumu hayo mapya.

Mheshimiwa Naibu Spika, maombi ya Mbunge kuhusu vifaa vya ofisi yake, hayatekelezwi na fedha kubaki katika Ofisi ya Katibu Tawala. Wazo hili lililetwa na Mheshimiwa Khalifa Suleiman Khalifa, Mbunge wa Gando. Majibu yake ni kwamba, kiutaratibu, fedha za uendeshaji za Wabunge, hupitia katika mafungu ya Makatibu Tawala wa Mikoa na baadaye hupelekwa katika Ofisi za Makatibu wa Wilaya na Ofisi za Wabunge katika Wilaya hizo. Fedha hizi ni kwa ajili ya ununuzi wa *stationaries*, malipo ya ankara za maji, simu, samani na kadhalika. Katika mwezi huu wa Juni mwaka 2008, Katibu Tawala wa Wilaya ya Muheza, amepokea shilingi milioni 2.5 kwa ajili ununuzi wa samani za ofisi ya Mheshimiwa Mbunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kupandisha hadhi barabara ya Ugala - Kaliua ili iwe chini ya TANROADS, wazo hili limeletwa na Mheshimiwa Juma Kapuya wa Jimbo la Urambo na majibu yake ni kwamba kulingana na Sheria ya Barabara ya mwaka 2007, Halmashauri ya Wilaya ya Urambo, inabidi ifuate taratibu za kupandisha hadhi barabara kutoka daraja moja hadi lingine, utaratibu ambao Halmashauri inaufahamu na kuwasilisha mapendekezo yake kwenye vikao vinavyohusika.

Mheshimiwa Charles Mlingwa, alisema kwamba katika bajeti zijazo, Serikali itenge fedha za kutosha kwa ajili ya ujenzi wa barabara za lami na madaraja katika Manispaa ya Shinyanga kama ilivyoahidiwa katika Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2005. Majibu yake ni kwamba, Serikali inatambua umuhimu wa kuwa na barabara za lami katika Manispaa hii. Kwa kutambua umuhimu huo, mwaka 2005/2006, Serikali ilitoa shilingi milioni 465.7 ambazo zilitumika katika ukarabati wa barabara kwa kiwango cha lami katika Manispaa ya Shinyanga.

Aidha, kwa mwaka 2008/2009, Manispaa imetengewa shilingi milioni 150, kwa ajili ya ukarabati wa barabara kwa kiwango cha lami. Serikali itaendelea kutenga fedha kwa ajili ya Halmashauri ikiwemo Manispaa ya Shinyanga kulingana na hali ya fedha itakavyoruhusu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ujenzi kufanyika kwa mabwawa ya kutunza maji na *scheme* za umwagiliaji, wazo ambalo lililetwa na Mheshimiwa Jacob Shibiliti, Mbunge wa Misungwi. Majibu yake ni kwamba Serikali kupitia Mfuko wa Pamoja wa Mpango wa Maendeleo ya Sekta ya Kilimo, inatoa fedha kwa ajili utekezaji wa mipango ya maendeleo ya kilimo ya Wilaya. Hivyo, Halmashauri zinashauriwa kutenga fedha kwa ajili ya ujenzi wa mabwawa hayo katika Mpango wa Maendeleo ya Kilimo wa Wilaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga mkono hoja. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, sasa naomba niwaite Mawaziri wanaohusika kujibu hoja na baadaye Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Waheshimiwa Wabunge, mtakumbuka tumeongeza muda kwa Ofisi ya Waziri Mkuu, kwa sababu ya kuunganisha TAMISEMI na Ofisi ya Waziri Mkuu. Kwa hiyo, kwa kweli muda wa kujibu inabidi uwe saa mbili. Hizo saa mbili, tunazigawa na kila Mheshimiwa Waziri atakuwa na dakika thelathini na zitakazobaki, zitakuwa za Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Sasa namwita Mheshimiwa Waziri wa Nchi, TAMISEMI kwa dakika thelathini. (*Makofi*)

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU -TAMISEMI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchukua nafasi hii, kwanza kumshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kutufikisha siku hii ya leo.

Pia napenda kumshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, kwa imani kubwa aliyonionyesha kwa kuniteua kuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa. Naahidi kuwa nitafanya kazi kwa uwezo wangu wote na kwa kushirikiana na viongozi wenzangu ikiwa ni pamoja na ninyi Waheshimiwa Wabunge.

Aidha naomba kuchukua fursa hii, kumpongeza sana sana Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda, kwa kuteuliwa kwake kuwa Waziri Mkuu. Naomba nikiri kwa moyo dhati, ndugu zangu, yeye ndiye aliyenijengea uwezo wa kufika mahali nilipo. Naomba niseme kwamba, naahidi kumsaidia katika majukumu aliyokabidhiwa na Mheshimiwa Rais. Namshukuru na kumpongeza sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile, naomba kuchukua fursa hii, kumpongeza Mheshimiwa Aggrey Mwanri, kwa kuteuliwa kuwa Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa. Kwa kipindi kifupi, tumeshirikiana kwa karibu sana ndiyo maana mnaona anaweza kujibu maswali vizuri na kufanya kazi yake vizuri.

Pia bila kuwasahau wafanyakazi mbalimbali katika Ofisi yangu, akiwemo Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu, Wakuu wa Idara na wafanyakazi wote kwa ujumla, kwa ushirikiano ambao wananipa mpaka kazi yangu naiona nyepesi.

Mwisho napenda kuishukuru familia yangu, mume wangu na watoto. Vilevile sitawasahau wapiga kura wangu, wa Jimbo la Ulanga Mashariki, kwa kunivumilia kwa kipindi hiki ambacho mimi nipo katika kutimiza majukumu ya Kitaifa.

Mwisho, siwezi kusahau mikono yangu 21 ambayo ni Wakuu wa Mikoa, kwa kazi nzuri ambayo wanaifanya katika Mikoa yao ambapo inaniwezesha mimi kutekeleza majukumu yangu kuwa wepesi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichukue nafasi hii, kukushukuru wewe pamoja na Spika pamoja na Wabunge wote, kwa kuchangia hoja mbalimbali na kwa muda wa wiki moja nikiri kwamba nimejifunza mambo mengi ikiwa ni pamoja na misamiati mbalimbali pamoja na msamiati wa ku-*rewind*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli nilimwona Mheshimiwa Shoka na alinieleza alikuwa na maana gani na mimi nimemuelewa kwamba wakati wa kujibu maswali yake, tu-*rewind* kwanza ili tuwe tunamjibu maswali yake vizuri. Kwa hiyo, nilimuelewa. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema maneno hayo ya utangulizi, napenda kupongeza sana Hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu na niseme kwamba naunga mkono kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja zilizotolewa ni nyingi, nyingi tumezipeleka katika sekta husika ili na wenzetu waweze kubeba mzigo huu. Kwa hiyo, naomba sehemu zile ambazo hatutajibu, Waheshimiwa Wabunge, wajue kwamba tumewapelekea wenzetu sekta zinazohusika, watajibu na nina uhakika watazijibu kwa sababu tutawapelekea kimaandishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, niende moja kwa moja katika hoja namba moja ambayo ni kuanzisha maeneo mapya ya utawala katika Mikoa, Wilaya, Tarafa, Vijiji pamoja na Vitongoji, hoja hii ilichangiwa na Wabunge wengi ambao ni Mheshimiwa Samuel Chitalilo, Mheshimiwa Emmanuel Luhahula, Mheshimiwa Juma Kapuya, Mheshimiwa Richard Ndassa, Mheshimiwa Ahmed Shabiby, Mheshimiwa Mohamed Missanga, Mheshimiwa Dr. Luka Siyame, Mheshimiwa Anne Makinda, Mheshimiwa Jackson Makwetta, Mheshimiwa Kabuzi Rwilomba, Mheshimiwa James Musalika, Mheshimiwa Estherina Kilasi, Mheshimiwa John Lwanji, Mheshimiwa Zitto Kabwe, Mheshimiwa Aziza Sleyum Ally, Mheshimiwa Abdulkarim Shah, Mheshimiwa Tatu Ntimizi na Mheshimiwa Dr. Sigonda.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hoja hii, tunasema kwamba, Serikali kwa kweli inatambua sana kuna maeneo ambayo ni makubwa sana na Serikali imepokea maombi mengi sana kutoka katika Mikoa mbalimbali. Kama tulivyosema, kwa kweli kuanzisha Mkoa mmoja au Wilaya moja, ni gharama kubwa sana lakini Serikali inaangalia uwezekano wa kugawa maeneo haya mapya kulingana na uwezo wa kifedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme tu kwamba, maeneo tuliyogawa katika awamu ya tatu ambayo ni Mkoa mmoja na Wilaya 11, bado miundombinu haijakamilika. Kwa hiyo, Serikali iliona si vema kugawa maeneo mapya ya kiutawala wakati Wilaya nyingine zilikuwa bado hazijajengwa maboma na miundombinu haijakamilika.

Waheshimiwa Wabunge, mmemsikia Mheshimiwa Dunstan Mkapa, kutoka Nanyumbu, analalamika kwamba boma lake, halijakamilika. Kwa hiyo, tuliona kwa sababu Wilaya 11 bado hatujazikamilisha, tuliona si vema kugawa maeneo mapya bali tuyaimarishe yale yaliyopo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama mtaangalia kwenye bajeti, kwa mwaka huu, Serikali imetenga fedha nyingi kwenye Wilaya zile 11 ili kuhakikisha kwamba maboma yale na miundombinu mbalimbali inakamilika ili tuone uwezekano wa kugawa maeneo mengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, mchakato wa kuchambua maeneo hayo ya kiutawala, kwa ujumla unaendelea vizuri katika Ofisi yangu na umekamilika na unategemea kutolewa rasmi mwaka 2008. Nikisema maeneo ya utawala pia najumuisha vijiji, vitongoji pamoja na mitaa. Kwa hiyo, tutahakikisha kwamba zoezi hili tunalikamilisha kabla ya kufika mwaka 2009 wakati wa uchaguzi wa Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la pili lilikuwa ni kuhusu Wabunge kukosa kushiriki vikao vya Mabaraza, Kamati za Halmashauri, Bodi za Barabara kutokana na vikao hivyo kufanyika wakati wa Bunge. Waheshimiwa Wabunge, Serikali imekwishatoa maelekezo kwa barua iliyoandikwa tarehe 2/10/2007 kwenda kwa Makatibu Tawala wa Mikoa, kuzitaka Halmashauri kupanga ratiba za vikao vya mwaka mzima ambavyo vitazingatia ratiba za vikao vya Bunge. Tuliwaandikia wenzetu wa Bunge na Katibu wa Bunge akatupa ratiba ya vikao vya Bunge vya mwaka mzima. Kwa hiyo, tunaendelea kusisitiza kwamba wahakikishe kwamba vikao hivi vinafanyika wakati Mbunge anakuwa Jimboni na anakuwa *free*.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini nitoe angalizo kwamba, kwa mfano kwa kipindi hiki cha miezi mitatu, hatuwezi tukasema Halmashauri isiendeshe vikao kwa sababu Kamati ya Fedha na Mipango inatakiwa ikae kila mwezi, sasa tukisema kwamba miezi mitatu ipite bila kufanya vikao na tunajua kabisa Halmashauri zetu zinaenda kwa vikao, haitawezekana. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge, naomba mjipange.

Mheshimiwa Naibu Spika, mfano mzuri, ni Mheshimiwa Beatrice Shellukindo, juzi alikuwa kwenye kikao cha Fedha na Mipango katika Halmashauri yake. Kwa hiyo, naomba tujipange ili tuweze kuhudhuria vikao hivyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, suala hili lilichangiwa na Mheshimiwa Herbert Mntangi, Mheshimiwa Sevelina Mwijage na Mheshimiwa Mbarouk Mwandoro hawa ndiyo walichangia suala hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la tatu, ni Ofisi ya TAMISEMI kwamba itenge fedha za kutosha katika bajeti ya maendeleo. Kwa hili, tunasema kwamba nia ya Serikali, ni kuhakikisha kwamba madaraka yanakwenda kwa wananchi na madaraka hayo ni pamoja na rasilimali watu na rasilimali fedha. Ndiyo maana mnaona kwamba, bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI, inaongezeka mwaka hadi mwaka. Kwa mfano, bajeti ya maendeleo ya mwaka uliopita ilikuwa shilingi bilioni 328 lakini kwa mwaka huu imeongezeka imefikia shilingi bilioni 356. Kwa hiyo, Serikali itazidi kupanga fedha nyingi kwenda kwenye Halmashauri ili iweze kutekeleza miradi ya maendeleo. Wazo hili au mchango huu ulitolewa na Mheshimiwa Lubeleje.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la nne, ni fedha za ruzuku kwa Mikoa na Halmashauri na ziwasilishwe kunakohusika kwa wakati muafaka. Ni nia ya Serikali kupeleka fedha hizi kwa wakati muafaka lakini Waheshimiwa Wabunge, tukumbuke kwamba bajeti yetu ni *cash budget*, inakusanya na unatawanya. Kwa mfano, fedha za barabara ni mpaka ukusanye fedha za mafuta, ukishakusanya ndipo uzipeleke kwenye Halmashauri husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, niwashukuru sana wenzetu wa *TRA* na Wizara ya Fedha, kwa sasa wanakusanya kwa haraka sana na zikishapatikana mara moja zinapelekwa kwenye Halmashauri mbalimbali. Mfano mzuri, ni mwaka jana badala ya kutolewa mwezi wa tisa au kumi kama ilivyo kwa miaka mingine, fedha hizo ziliwahi mwezi wa nane na mwezi wa tisa mwanzoni baadhi ya fedha zilikuwa zimeshafika. Kwa hiyo, Serikali tunajitahidi kwa kila njia kuhakikisha kwamba fedha hizo zinafika kwa wakati ili ziweze kutimiza malengo ambayo yamepangwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja ya tano, ni kwamba ofisi ya TAMISEMI, ishirikiane na Wizara nyingine kuwadhibiti watumishi wabovu na wale wasiowajibika. Kwa mujibu wa kifungu namba 6(6) cha Sheria ya Utumishi wa Umma, Sheria Na.8, ya mwaka 2002, watumishi wote walioko katika Halmashauri isipokuwa Wakurugenzi, mamlaka zao za nidhamu, ni Halmashauri husika. Kwa hiyo, Wakuu wa Idara mpaka kwenda chini, mamlaka zao za nidhamu, ni Halmashauri za Wilaya. Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI, itaendelea kushirikiana na Wizara za Kisekta, kuhakikisha kwamba wataalamu walioko kwenye Halmashauri, wanazingatia maadili, taaluma, sera, sheria, kanuni na taratibu zinazohusika.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo kubwa ni kulindana katika Halmashauri, naomba kwa hili tusaidiane. Mara nyingi, unakuta mtumishi anakosa kwenye Halmashauri husika badala ya kusema kwamba wamchukulie hatua za nidhamu, wanakuja kutuomba sisi TAMISEMI tumhamishe. Ni Halmashauri gani ambayo inataka mtumishi mbovu? Kwa hiyo, niwaombe na niagize, Halmashauri zote wawachukulie hatua za nidhamu wale watumishi ambao hawatimizi wajibu wao. Suala la kulindana sio suala zuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, mara nyingi ukienda kwenye Halmashauri, wanasema tunamwonea huruma, unamwonea huruma mtu ambaye amekula hela za Halmashauri?

Wengine ukienda kwenye Halmashauri wanasema, Bwana Uislam imani, sasa Uislam imani, ni wa kumlinda mwizi?

Mheshimiwa Naibu Spika, ninachosema ni kwamba wachukuliwe hatua za kinidhamu kwenye Halmashauri husika na sio kumhamishia kwenye Halmashauri nyingine. Sisi kama TAMISEMI, makao makuu, hatuwezi tukajua kwamba mtumishi fulani kwenye Halmashauri fulani hana nidhamu au hatimizi wajibu wake mpaka mtuletee taarifa. Mkituletea taarifa, ndiyo tunaweza tukawa na uwezo wa kusema kwamba huyu achukuliwe hatua.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nasema kwamba suala la kulindana kwenye Halmashauri sio zuri. Waheshimiwa Wabunge, tushirikiane kwa kuwa ninyi ni Wajumbe kuhakikisha kwamba mtu anachukuliwa hatua za nidhamu katika Halmashauri husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la sita, ni suala la utekekezaji usio makini wa Sheria ndogo ndogo za Halmashauri kuhusu uendeshaji wa biashara ndogo ndogo mijini. Kuwepo kwa unyanyasaji unaotokana na maamuzi mabovu, ngazi za Halmashauri, miji Manispaa na Wilaya, mfano ni wa kuwandoa wamachinga. Suala hili lilichangiwa na Mheshimiwa Dr. Wilbrod Slaa na Jacob Shibiliti.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Sheria za Serikali za Mitaa, Mamlaka ya Miji, Sura Na.288, toleo la mwaka 2002, uendeshaji wa biashara kwenye mamlaka hizo, husimamiwa na kudhibitiwa na Halmashauri husika. Wafanyabiashara, wakiwepo wamachinga, baba na mama lishe, wanapobainika kufanya biashara kwenye maeneo yasiyoruhusiwa, ni kukiuka Sheria na Halmashauri husika huandaa taratibu za kuwaondoa kwenye maeneo haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, Halmashauri zinaagizwa kuweka utaratibu mzuri wa kuwaondoa wafanyabiashara wanaokiuka taratibu kwa kufanya biashara maeneo yasiyoruhusiwa ili kuepuka malalamiko yanayoweza kutokea wakati wa utekelezaji wa zoezi hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa pia niangalie kwa upande mwingine kwa wale watumishi ambao wanachukua vifaa vya baba lishe au mama lishe au wamachinga na kuvitumia, hii ni kinyume cha sheria na niziagize Halmashauri kwamba wafanyakazi wa aina hiyo, wachukuliwe hatua za kinidhamu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia niziagize Halmashauri kutenga maeneo kwa ajili ya wamachinga. Serikali ina nia nzuri sana ya kuwasaidia hao wamachinga ili nayo iwe ni *formal sector,* wakikaa sehemu mmoja, ni rahisi kuwasaidia lakini wakianza kutembea mitaani kila mtu na sehemu yake, si rahisi kuwasaidia. Kwa hiyo, Serikali ina nia nzuri kabisa kwamba wakae sehemu moja ili waweze kusaidiwa kwa kuwawekea miundombinu pamoja na kuwakopesha ili na wao wenyewe waingie katika sekta iliyo rasmi.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la saba, ni kushirikisha wadau mbalimbali katika maandalizi ya uchaguzi wa Serikali za Mitaa wa mwaka 2009 na uchaguzi wa Serikali za Mitaa, uratibiwe na Tume ya Taifa ya Uchaguzi badala ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa. Ushauri umezingatiwa katika Hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, aya ya 103.

Aidha vyama vya Siasa vimeandikiwa barua kuombwa kuwasilisha maoni yao ya jinsi ya kuboresha utekelezaji wa zoezi zima la uchaguzi. Tumeviandikia vyama mbalimbali vya siasa kwamba watuletee mapendekezo yao na upungufu ambao wameuona ili tuweze kurekebisha. Nitoe wito kwa vyama vya siasa, tunaomba zile barua mtuletee majibu. Kuna vyama vingine wametujibu kwamba sisi hatuwezi kujibu kwa sababu hatutaki nyie TAMISEMI msimamie hilo zoezi. Kwa hiyo, niwaombe tu ndugu zangu mlete ili tuweze kurekebisha ule upungufu ambao umejitokeza huko nyuma.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la nane, ni kujenga uwezo ngazi ya Kata, kijiji, kitongoji, ili wasimamie vizuri rasilimali ambazo zinaenda huko chini. Suala hili limechangiwa na Mheshimiwa Dr. Slaa, Mheshimiwa Arfi na Mheshimiwa Jacob Shibiliti. Ofisi yangu, imekuwa ikifanya mafunzo mbalimbali kwa viongozi wake, kuanzia ngazi ya chini mpaka ngazi za juu na katika mpango wa maboresho ya Serikali za Mitaa, awamu ya pili, suala hili limezingatiwa. Labda niongeze tu kwamba Chuo chetu cha Hombolo kipo pale kwa mdhumuni maalum ya kuimarisha na kujenga uwezo wa watumishi wa Serikali za Mitaa kuanzia ngazi ya chini mpaka ngazi ya juu. Ndiyo maana mwaka huu tumetenga fedha kwa ajili ya kupanua chuo chetu cha Hombolo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja namba tisa, ni kuanzisha vyanzo vya kudhibiti mapato ya Halmashauri, suala hili pia limetolewa na Mheshimiwa Dr. Slaa na Mheshimiwa Galinoma. Pamoja na utararibu uliopo sasa wa udhibiti wa matumizi, awamu ya pili ya maboresho, ina utaratibu mahususi wa kusimamia mapato na matumizi ya Halmashauri na mikakati hiyo ni pamoja na kuhakikisha Halmashauri inakuwa na watumishi wa kutosha wa Uhasibu na Ukaguzi wa Ndani, pia kuunda Kamati za Ukaguzi katika Halmashauri.

Waheshimiwa Wabunge, wenyewe mmeona kwamba kwa sasa hivi tumeajiri watumishi mbalimbali wakiwemo wa fedha ili kuweza kuimarisha au kusimamia mapato na matumizi katika Halmashauri zetu. Aidha, Serikali inaangalia uwezekano wa kuchukua baadhi ya vyanzo vya mapato vya Serikali Kuu kwenda kwenye Halmashauri, ili kuweza kuongeza kipato katika Halmashauri. Mfano mzuri, mwaka uliopita, katika bajeti iliyopita, Wizara mbalimbali zilichukua karibuni shilingi bilioni 286 kwenda kwenye Halmashauri za Wilaya. Kwa hiyo, hiyo ni hatua nzuri kwa kupeleka madaraka kwa wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja namba kumi, ni kuboresha vitendea kazi kwa Maafisa Watendaji. Nalo limetolewa na Wabunge mbalimbali. Tunasema kwamba azma ya Serikali, ni kuwawezesha watendaji wake kuwa na vitendea kazi vikiwemo vya usafiri. Juhudi mbalimbali zimefanyika katika Halmashauri na kuwawezesha watendaji wake kuwa na vyombo vya usafiri. Baadhi ya Halmashauri ambazo zimetimiza azma

hiyo, ni pamoja na Mfundi, Masasi pamoja na Mbinga ambazo zimewakopesha Watendaji wa Kata pikipiki. Tunawahimiza Halmashauri nyingine kuiga mfano wa Halmashauri za Mbinga, Masasi pamoja na Mufindi.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ni kufanya mapitio ya Sheria Na.7 na Sheria Na.8 ya Serikali za Mitaa ili kubainisha majukumu ya Wakuu wa Mikoa na Wilaya na Wakurugenzi wa Halmashauri kwa kuzingatia mabadiliko yaliyotokea. Hoja hii imetolewa na Mheshimiwa Dr. Slaa. Tunasema kwamba majukumu ya Mkuu wa Mkoa, Wilaya na Mkurugenzi wa Halmashauri yako wazi katika Sheria zilizopo sasa. Marekebisho ya Sheria Na.7 na Sheria Na.8 ya mwaka 1982, yamekuwa yakizingatia mabadiliko yanayoendelea. Kwa kuzingatia hili, Serikali imeanzisha Kamati za Ushauri katika ngazi za *DCC,* ili kuratibu shughuli zinazotendeka katika Wilaya kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la kumi na moja, ni kuhusu uchaguzi wa Serikali za Mitaa, uratibiwe na Tume ya Taifa ya Uchaguzi badala ya Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI na itumie Daftari la Kudumu la Wapiga Kura. Hoja hii imetolewa na Mheshimiwa Dr. Slaa. Utaratibu wa usimamizi wa uchaguzi wa Serikali za Mitaa, uko chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI kwa mujibu wa Sheria. Hata hivyo, watelezaji na wasimamizi wa uchaguzi huo, ni Wakurugenzi Watendaji wa mamlaka za Serikali za Mitaa. Hata hivyo, huo uchaguzi mkuu ambao huratibiwa na Tume ya Taifa ya Uchaguzi, wasimamizi wake ni wale wale watumishi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa na hii imefanyika kwa makusudi kwa sababu Serikali za Mitaa zimesambaa mpaka katika ngazi ya kijiji.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala kumi na mbili, ni kwamba Serikali iangalie uwezekano wa kuwa na mpango wa Kitaifa wa kuimarisha barabara vijijini kuanzia ngazi ya kitongoji hadi Mkoa. Hoja hii, imetolewa na Mheshimiwa Ndassa, Mheshimiwa Mramba, Mheshimiwa Zitto Kabwe, Mheshimiwa Mwinchumu Msomi na Mheshimiwa Daniel Mkapa. Tunachosema ni kwamba Serikali inakubaliana na ushauri huo lakini mpaka sasa hivi Ofisi yangu ina Programu ya Taifa ya Usafirishaji wa Serikali za Mitaa na Programu ya Usafiri na Usafirishaji Vijijini ili kuimarisha barabara vijijini kuanzia ngazi za vitongoji ili kuimarisha barabara za vijijini hadi Wilayani.

Mheshimiwa Naibu Spika, hiyo Programu ya Usafiri na Usafirishaji Vijijini, ilianza mwaka 1992 kwa majaribio ya Halmashauri nane na katika mwaka 2007/2008, programu ilipanuka hadi kufikia Halmashauri 27 na kwa mwaka huu programu imeelekezwa katika Halmashauri 55. Azma ya Serikali, ni kueneza programu hii katika nchi nzima. Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI kwa kutambua hili imeingia mkataba na Chuo cha Matumizi ya Nguvukazi katika ujenzi wa barabara ambacho kipo Mbeya ili kuwawezesha Wakandarasi wadogo wadogo na Wakandarasi wa Halmashauri kuzihudumia barabara hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la kumi na tatu, ni Sheria inayowazuia Wabunge wa Viti maalum kushiriki katika vikao vya Halmashauri vya Kamati ya Fedha na Mipango. Hoja hii imetolewa na Mheshimiwa Mwijage, Mheshimiwa Lediana Mng’ong’o na Mheshimiwa Meryce Emmanuel. Hoja hii, tunasema kwamba kwa mujibu

wa Sheria za Serikali za Mitaa, Sura ya 287 na 288, Halmashauri imepewa uwezo wa kuunda Kamati za Fedha na Mipango. Wajumbe wa Kamati ya Kudumu wanatajwa kwenye Kanuni za kudumu za Halmashauri. Kwa mujibu wa Waraka ambao tumetuma katika Halmashauri wa tarehe 3/11/2000, katika kipengele cha 5(d), Wajumbe wa Kamati ya Fedha na Mipango ni hawa wafuatao:-

Mwenyekiti wa Halmashauri, Makamu Mwenyekiti, wa Halmashauri, Wenyeviti wa Kamati za kudumu, Mbunge au Wabunge wa Majimbo wanaowakilisha Majimbo katika Halmashauri husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni hii, ni dhahiri kwamba msimamo wa Kisheria, Mbunge wa Viti Maalum, hatajwi kuwa Mjumbe wa Kamati ya Fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini naomba hapa nitoe rai kwa Waheshimiwa Madiwani Wanawake, katika Halmashauri, kugombea nafasi za Wenyeviti wa Kamati za Kudumu katika Halmashauri zao, ili kuongeza nguvu ya uwakilishi kwa upande wa wanawake. Sasa hivi pia kuna nafasi ya Naibu Meya na Makamu wenyeviti. Naomba wanawake katika Halmashauri mbalimbali, wagombee nafasi hii ili waweze kuingia au kuimarisha uwakilishi wa wanawake katika Halmashauri.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la kumi na nne, ni kwamba Serikali inapoangalia muundo wa Jiji wa Dar es Salaam, ihakikishe mitaro ya maji inafunikwa. Suala hili limetolewa na Mheshimiwa Lucy Owenya na Mheshimiwa Chaurembo. Tunachosema ni kwamba ushauri umezingatiwa, mifereji ya maji kando kando ya barabara imeachwa wazi ili kurahisisha kuhudimiwa kwa urahisi hasa ikizingatiw kwamba maeneo mengi kando kando ya barabara hayajasafishwa. Nitoe wito tu kwamba mitaro ile inapoachwa wazi, si kwa ajili ya kutupa takataka. Naomba tuwaelimishe wananchi kwamba mitaro ile ni ya maji na si madampo ya kutupia takataka.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la kumi na tano, ni kwamba kabla ya Serikali kujenga zahanati katika kila kijiji, ni vema ikaboresha zahanati zilizopo na kuhakikisha zinakarabatiwa na kuongeza watumishi. Tunaposema mpango wa *MMEM* umelenga kuimarisha vituo vya huduma za afya na kujenga vituo vya afya au zahanati mpya pale ambapo hakuna, lengo la mpango huu ni kuhakikisha vituo vilivyopo vinaboreshwa, vina watumishi wa kutosha wa fani mbalimbali na pale ambapo hakuna vinajengwa. Kwa mwaka 2008/09, Serikali imetenga bilioni 23 kwa ajili ya mpango huu na wenzetu Wizara ya Afya, pia wametenga fedha kwa ajili ya upanuzi wa vyuo mbalimbali pamoja na kuongeza udahili wa wanafunzi katika vyuo vya afya. Suala hili lilichangiwa na Wabunge wengi ambao kwa kweli kutokana na muda nimeshindwa kuwataja.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la kumi na sita, kwamba Serikali iangalie uwezekano wa Mji wa Makambako kuwa Halmashauri ya Mji. Suala hili limetolewa na Mheshimiwa Makwetta na ushauri huu umepokelewa na tunaomba suala hili lianzie kwenye Wilaya husika baadaye lije katika Ofisi yangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la kumi na saba, ni nafasi ya Mbunge na Mwenyekiti au *Mayor* wa Halmashauri kuhusu uendeshaji wa Halmashauri. Hapa tunasema kwamba kwa mujibu wa Sheria za Serikali za Mitaa, Mwenyekiti, *Mayor* huchaguliwa na Madiwani wote wa Halmashauri husika na kwa mantiki hii, Mwenyekiti au *Mayor* akichaguliwa na Madiwani wengi ikiwa ni pamoja na Mheshimiwa Mbunge, anakuwa Mwenyekiti wa Halmashauri yote zaidi ya kuwa Diwani wa Kata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maamuzi ya Halmashauri, hutolewa katika eneo la Halmashauri husika. Kwa mujibu wa Sheria za Serikali za Mitaa, Mheshimiwa Mbunge anapokuwa katika vikao vya Halmashauri, ni Mjumbe na anawajibika kwa kufuata na kuheshimu taratibu za mikutano ya Halmashauri ikiwa ni pamoja na taratibu za kufanya maamuzi katika Halmashauri na maamuzi yote yanafanywa ili kunufaisha wananchi wote kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la kumi na nane, limetolewa na Wabunge mbalimbali, ni suala la kuwepo kwa Akaunti nyingi za fedha katika Halmashauri ambapo kunasababisha usimamizi wa fedha kuwa mgumu. Ni kweli Serikali za Mitaa zinakuwa na akaunti nyingi kwa sababau ya kuwa na miradi mingi na pili kuzingatia masharti ya wahisani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa nini kunakuwa na akaunti nyingi, Halmashauri yenyewe inaweza kuwa na akaunti lakini miradi pia kwenye vijiji inatakiwa kufungua akaunti, hii ndiyo inafanya Halmashauri zionekane kwamba zina akaunti nyingi. Kama kweli tunataka kupeleka madaraka kwa wananchi, ni vema hizi akaunti kwenye vijiji mpaka kwenye kata, ziendelee ila sisi kama Serikali tutahakikisha kwamba tunadhibiti matumizi na mapato katika sehemu mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, masuala mengine ambayo yalikuwa ynahitaji sana utafiti kwa mfano yaliyotolewa na Mheshimiwa Nuru Bafadhili, Mheshimiwa Ania Chaurembo, Mheshimiwa Khamis ambao walinileteа *document* kwa ajili ya kufanyia kazi, tutayafanyia kazi na tutayajibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kusema kwamba naunga Mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

**WAZIRI WA NCHI OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, UTARATIBU, BUNGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa fursa hii, ya mimi kutoa mchango wangu katika hotuba ya bajeti ya Waziri Mkuu kwa mwaka wa fedha 2008/09.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, napenda kumpongeza sana Mheshimiwa Celina Kombani, kwa kuteuliwa kuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, *TAMISEMI* na Mheshimiwa Aggrey Mwanri kwa kuteuliwa kuwa Naibu Waziri wa Ofisi ya Waziri Mkuu *TAMISEMI*. Binafsi, napenda kuwahakikishia ushirikiano wangu wa dhati katika kutekeleza majukumu yetu kwa kumsaidia Mheshimiwa Waziri Mkuu kutekeleza majukumu yake vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, sitakuwa nimetenda haki iwapo sitatumia fursa hii pia kuwashukuru wananchi na viongozi wa Wilaya ya Mbulu, kwa ushirikiano walionipa na imani yao kubwa kwangu siku za nyuma na ushirikiano wetu na mshikamano wetu ulileta maendeleo yanayoonekana katika kila kijiji, Wilayani kwetu na pia kumekuwa na amani na utulivu baina ya wananchi muda wote, pamoja na kwamba baadhi ya viongozi wetu wa ngazi ya vijiji na vitongoji wametokana na vyama mbalimbali na katika ngazi za Halmashauri zaidi ya robo ya Madiwani wetu wanatoka katika Chama cha Siasa cha *CHADEMA*.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, napenda kusema mapema kuwa, naunga mkono hoja ya bajeti ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa mwaka wa fedha 2008/09.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nianze kutoa maelezo mafupi kwa kuanzia Makao Makuu Dodoma.

Mheshimiwa Naibu Spika, baadhi ya Wabunge, wametaka kufahamu ni hatua gani zimechukuliwa na Serikali kuhamisha Makao Makuu Dodoma na wengi wameshauri kwamba Serikali ihamie Dodoma kwa awamu kwa kuanza walau na Wizara sita na kuishauri Serikali itunge sheria ya kuhamia Dodoma na siyo mjadala.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja hizi zimetolewa na Waheshimiwa Wabunge wengi ikiwa ni pamoja na Mheshimiwa George Lubeleje, Mheshimiwa Dr. Wilbroad Slaa, Mheshimiwa Grace Kiwelu, Mheshimiwa Mariam Kasembe, Mheshimiwa Paschal Degera, Mheshimiwa Juma N'hunga, Mheshimiwa George Simbachawene na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ufupi kabisa, Serikali imeshatamka itaandaa mjadala wa wazi wa wadau wote kujadili suala la kuhamia Dodoma ambao utatoa mwelekeo mzuri wa jinsi Serikali itakavyoweza kutekeleza mpango wake wa kuhamia Dodoma ikiwa ni pamoja na kutunga sheria mpya.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wabunge pia wameomba Serikali kupanua miundombinu ya Manispaa ya Dodoma ili kumudu ongezeko la watu na magari kwa siku za usoni ili kuepukana na adha ya msongamano wa magari na watu kama inavyojitokeza hivi sasa katika Jiji la Dar es Salaam.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeanza ujenzi wa barabara kwa kiwango cha changarawe katika eneo la Kisasa na kuanza usanifu wa miundombinu katika eneo la makazi la Kizota yaani Area A na Chadulu, Area E, kwa lengo la kupanua miundombinu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mpango wa muda wa kati na mrefu, ni kutenganisha barabara za kutumiwa na mabasi pekee na barabara za magari ya kawaida ili kudhibiti, kutawanya vizuri mizunguko ya magari hapa Mjini Dodoma.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia imetolewa hoja kwamba maeneo ya wazi ya Manispaa ya Dodoma ambayo yana mandhari nzuri yamevamiwa kinyume na *master*

*plan*. Hoja hii imetolewa sana na Mheshimiwa Janet Kahama, napenda nimhakikishie Mheshimiwa Kahama kwamba maeneo ya wazi kwa kiwango kikubwa yamelindwa ili kukidhi malengo yale ya kuwa na uoto unaozunguka maeneo hayo mbalimbali ili kuboresha mwonekano wa Mji na kuburudisha wakazi wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, maeneo haya yameboreshwa na kuongezwa uoto wa kuwekewa huduma stahili kwa watumiaji wa maeneo hayo ya wazi kama ilivyofanywa kwa Nyerere *Square* na pia Uwanja wa Mashujaa na maeneo mengine kwa kuhusisha vikundi vya jamii na watoa huduma wa sekta binafsi pia.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini wakati mwingine maeneo ya wazi yametumika kutoa huduma ambazo hazikuwa zimeainishwa na haya ni makubaliano kati ya *CDA* na watoa huduma kama vile Mamlaka ya Mawasiliano yaani *TCRA*.

Mheshimiwa Naibu Spika, imetolewa hoja kwamba bustani ya miche ya maua ya *CDA,* imefifia na haina miti ya kuotesha. Hoja hii imetolewa pia na Mheshimiwa Janet Kahama na ninapenda kumfahamisha Mheshimiwa kwamba *CDA* imefufua bustani hiyo na sasa bustani hiyo hali yake inaridhisha kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nisingeweza kumaliza hoja hii ya Makao Makuu Dodoma bila kutaja lile suala la bomoabomoa ya hivi karibuni katika maeneo ya Chang'ombe na Mbwanga ambalo lilitolewa na Mheshimiwa Masoud Salim. Alitoa tuhuma nyingi kwa vyombo vya dola na kwamba kulikuwa na unyanyasaji na tulipomwomba uthibitisho na kwa kweli alitoa uthibitisho ambao haujatusaidia sana. Hata Katibu Tarafa tulipomtafuta atufanyie utafiti imeshindikana, pia Mtendaji wa Kata na hata Mabalozi, kwa sababu alitupa jina la Balozi anayeitwa William Charles ambaye hapatikaniki. Yule mama aliyesema kwamba alinyanyaswa, anaitwa Hujatu Abulalu, naye tumemtafuta hatumpati. Askari walionyanyasa, majina yale tumepeleka kwa *OCD* wa Dodoma, nayo hatuyapati.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nataka kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge na Bunge lako Tukufu kwamba zoezi hili kwa kweli lilifanyika kwa umakini sana chini ya uongozi wa Serikali ya Dodoma Mjini, chini ya Katibu Tarafa na Mkuu wa Wilaya na kwa kweli yale yaliyosemwa na Mheshimiwa Mbunge hapa hayana uthibitisho na tungeomba bado aondoe msemo wake kwa sababu hizi ni tuhuma nzito kabisa za kupotosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu majanga ya Kitaifa, Waheshimiwa Wabunge wameshauri Serika, kuwa wigo wa kushughulikia maafa upanuliwe zaidi na kuhakikisha majanga mengine kama ajali za barabarani na majini na kadhalika hazitokei. Pia Kitengo cha Maafa, kiongezwe nguvu ili kiweze kupambana na maafa mbalimbali yakiwemo ya wasafiri wa maboti kutoka Dar es Salaam kwenda Zanzibar, Pemba na Tanga.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imepokea ushauri huu na inaendelea kuufanyia kazi kwa lengo la kuzuia maafa, kujiandaa kukabili maafa na hatimaye kurudisha hali kuwa ya kawaida. Katika mwaka wa fedha 2008/09, Serikali imetoa shilingi milioni 453 kwa ajili ya kujenga uwezo wa Idara yetu ya Maafa na kwa mwaka

2008/09, mashirika mbalimbali ya kimataifa yametuahidi shilingi 256,270,800 kugharamia mradi wa kujenga uwezo wananchi kukabili maafa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa itoshe kutaja kwamba japokuwa nchi yetu ina Serikali mbili, kuna ushirikiano wa karibu sana katika eneo hili ambalo pia siyo la Muungano. Kitengo cha Maafa katika Ofisi ya Waziri Mkuu, tunaushirikiano wa karibu sana na Kitengo cha Maafa katika ofisi ya Waziri Kiongozi wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar.

Mheshimiwa Naibu Spika, ongezeko la vijana kujihusisha na dawa za kulevya, umetolewa ushauri kuwa elimu ya dawa za kulevya iwekwe kwenye *syllabus* za shule za msingi na sekondari. Vilevile Serikali iendelee kudhibiti biashara za dawa za kulevya na kuhakikisha kuwa inasimamia utekelezaji wa sheria zinazohusiana na dawa hizo. Hoja hiyo imetolewa na Mheshimiwa George Lubeleje, Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge, Katiba, Sheria na Utawala.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kulielezea Bunge lako kuwa, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi kwa kushirikiana na Tume yetu ya Uratibu na Udhibiti wa Dawa za Kulevya, watalifanyia kazi suala hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, yametolewa mapendekezo kuwa Serikali iandae mpango mahsusi wa kupambana na watumiaji wa dawa za kulevya nchini. Serikali iimarishe pia udhibiti wa matumizi ya dawa za kulevya kwa vijana ambao ndiyo wengi wanaoathirika. Maelezo ni kwamba Serikali inayo mipango mahsusi ya kupambana na watumiaji wa dawa za kulevya, mfano inatoa elimu kwa vijana kwa kupitia asasi za kiserikali zinazojihusisha na uelimishaji wa umma na hasa vijana ambao wako karibu sana na madhara ya madawa ya kulevya. Pia Tume yetu inaandaa sera ya kudhibiti dawa za kulevya, inatoa mwongozo kwa ajili ya kudhibiti dawa hizo katika ngazi mbalimbali na kumekuwa na nguvu za pamoja katika kudhibiti dawa hizi kati ya Tume ya Kudhibiti Dawa za Kulevya, Bandari, Polisi, *TRA* na *TFDA*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wabunge pia wameshauri kwamba itangazwe siku ya tarehe 14/7/, kuwa siku ya UKIMWI Tanzania ili kuienzi kampeni ya Rais ya kupima UKIMWI kwa hiari na vilevile Serikali iharakishe mchakato wa Muswada wa Mfuko wa UKIMWI. Ushauri huu umepokelewa lakini tukumbuke kwamba siku ya tarehe 14/7 ndiyo siku ambayo inatambuliwa Duniani. Sisi ni mwanachama wa Umoja wa Mataifa na kwa maagizo ya Umoja wa Mataifa, siku ya UKIMWI Duniani inajulikana. Hata hivyo, pendekezo hili linafanyiwa kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia *TACAIDS,* tayari imeanza mchakato wa kuanzisha Mfuko wa UKIMWI na pengine kabla ya mwisho wa mwaka huu, mfuko huo utakuwa umeanzishwa ili kusaidia pale ambapo kutakuwa na upungufu au wafadhili watakuwa wamepungua.

Mheshimiwa Naibu Spika, zipo baadhi ya Halmashauri ambazo hutumia fedha za UKIMWI bila kuzingatia miongozo na taratibu zilizowekwa. Fedha za UKIMWI, zinapopelekwa kwenye Halmashauri, zimegawanywa katika makundi matatu na miongozo yake ni kama ifuatavyo;-

Kwanza, ni fedha za *Global Funds*, mwongozo wa fedha hizi, hutayarishwa na TAMISEMI kwa kushirikiana na Wizara ya Afya na fedha hizo hupitia TAMISEMI na kupelekwa kwenye Halmashauri husika kwa shughuli za kudhibiti UKIMWI na katika ngazi hiyo kuna Kamati yetu ya Halmashauri ya Kudhibiti UKIMWI.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili kuna fedha za Mfuko wa Pamoja wa Wafadhili wa UKIMWI *(Basket Fund),* mwongozo wake hutayarishwa na *TACAIDS* na hutolewa na TAMISEMI, kwa Halmashauri kama moja ya miongozo ya bajeti. Fedha hizi zinapitia michakato ya Kamati mbalimbali na vikao vya maamuzi ya bajeti na matumizi ya Halmashauri ambapo Waheshimiwa Wabunge pia ni Wajumbe.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu, fedha za misaada zinazopokelewa kwenye asasi za kiraia, fedha hizi hupitia kwa wakala wa Mikoa ambao wanafanya kazi zote kwa ushirikiano na Halmashauri zetu. Sasa hivi fedha hizo zinaanza kupitia *TASAF*, ambapo pia wanafanya kazi kwa ushirikiano wa karibu sana na Halmashauri zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kulikuwa na suala la utoaji wa maamuzi ya Serikalini, suala hili limeletwa na Mheshimiwa Felix Mrema, Mbunge wa Arusha, Serikali itazingatia ushauri wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ruzuku kwa Vyama vya Siasa, ruzuku ya Serikali kwa Vyama vya Siasa, hutolewa kwa mujibu wa Sheria kwa Vyama vya Siasa vyenye sifa ya kupata ruzuku na vinavyotimiza masharti ya kupewa ruzuku ambayo ni pamoja na matumizi ya fedha hizi kukaguliwa na Mkaguzi aliyesajiliwa kila mwaka na taarifa za ukaguzi kuwasilishwa kwa Msajili. Kwa hivi sasa, vyama vyote vinavyopata ruzuku, vinatekeleza masharti ya kisheria. Aidha, Msajili anaendelea kusimamia kikamilifu matumizi ya fedha za ruzuku kuhakikisha zinatumika kwa malengo yaliyokusudiwa na kutolewa taarifa za matumizi yake kwa mujibu wa sheria zilizopo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa Wabunge, pia wameomba Serikali iangalie uwezekano wa kutoa posho kwa Madereva wa Bunge kama ilivyo kwa Madereva wa Wakuu wa Mikoa. Suala hili Serikali inaliangalia kwa karibu kwanza kwa kuangalia Kanuni zilizopo Serikalini lakini pia inawezekana tukatumia Sheria inayokuja ya Uendeshaji wa Shughuli za Bunge (*The Parliamentary Administarion Act*) ambayo tunatarajia itapitishwa na Bunge hili katika Mkutano wake huu wa 12. Hivyo, tunaomba sana Waheshimiwa Wabunge wavute subira.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushirikishwaji wa Wabunge katika Mikutano ya Halmashauri za Wilaya, nafikiri suala hili limeelezwa kwa umakini na TAMISEMI lakini hapa itoshe kusema kwamba Mheshimiwa Waziri Mkuu, ameshaandika barua kwa Wakuu wa Mikoa yote kuzielekeza mamlaka za Halmashauri zote kupanga Mkutano ya

Mabaraza ya Madiwani kwa utaratibu utakaowawezesha Wabunge wote kuhudhuria vikao hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la uwekezaji, kama unavyofahamu, Kituo cha Uwekezaji pamoja na Tanzania *Business Council,* sasa vimehamishiwa katika Ofisi ya Waziri Mkuu. Ushauri huu wa Mheshimiwa Mohamed Missanga, kuwa Serikali iandae haraka sana Sera ya *Public Private Partinership* ili kuharikisha uwekezaji pamoja na uboreshaji wa huduma mbalimbali nchini na hasa katika Mikoa yetu, umepokelewa na Serikali na unazingatiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu matumizi ya Stakabadhi ya Mazao Ghalani, Wabunge wengi wametoa ushauri ufuatao; kwanza mpango wa Stakabadhi Ghalani, haujaweza kufanikiwa Bukombe kwa sababu Mabenki hayatoi fedha na Mheshimiwa Mbunge aliomba tumsaidie. Pia mfumo wa Stakabadhi Ghalani, uenezwe nchi nzima. Pia mfumo wa Stakabadhi Ghalani, umegeuka kuwa tatizo, anayetaka kununua pamba ananyimwa pesa, Serikali iboreshe mfumo huu na kuondoa matatizo haya katika utekelezaji wake na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli benki ni kiungo muhimu katika utekelezaji wa mfumo huu wa Stakabadhi za Mazao Ghalani. Ili ushiriki wa benki uwe rahisi, ni muhimu kwa maandalizi ya awali kufanywa kwa makini kwa kuzingatia taratibu zote za msingi za ushiriki ili kuepusha migongano katika utekelezaji wa jambo hili muhimu. Hivyo, Serikali inawashauri sana Waheshimiwa Wabunge ambao maeneo yao yana matatizo kama haya, washirikiane na Halmashauri zao kuwasiliana na wataalamu wa Mfumo wa Stakabadhi Ghalani, kuondoa matatizo yanayoweza kujitokeza katika wa mfumo huu katika maeneo yao. Mfumo wa Stakabadhi ya Mazao Ghalani, umefanywa kwa majaribio katika baadhi ya maeneo nchini kupitia programu yetu ya uendelezaji wa mfumo wa masoko na mazao ya kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Prof. Raphael Mwalyosi, aliuliza swali moja la msingi sana, linalohusu soko la Mlangali katika Wilaya ya Ludewa, napenda kutoa maelezo kwamba soko hilo, lililojengwa kupitia Programu ya Maendeleo ya Mifumo ya Mifuko ya Mazao ya Kilimo (*IMSDP*) kama ilivyoainishwa kwenye hotuba ya Waziri Mkuu, aya ya 33.

Mheshimiwa Naibu Spika, soko hili, ujenzi wake ulikamilika Julai mwaka 2007 na Wakandarasi walitakiwa kufanya marekebisho madogo madogo katika sehemu zinazovuja, kazi ambayo wamekwishaifanya. Kwa hiyo, tunamshauri Mheshimiwa Mbunge na wananchi wa Ludewa na hasa wale wa Mlangali, watumie soko hili kikamilifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wabunge walishauri kuwa Serikali itazame muundo wa *TIC*, *TNBC* na Tume ya Mpango na *TIC* irudishwe kwenye Wizara ya Fedha na Uchumi, Tume ya Mpango iwe chini ya Ofisi ya Rais, awepo Waziri wa Nchi kusimamia, kuwepo kwake katika Wizara ya Fedha na Mipango, kunaipa Tume uzito kidogo.

Mheshimiwa Naibu  Spika, maelezo kuhusu suala hili ni kwamba kwanza mwenye mamlaka ya kuunda vyombo hivi, ni Mheshimiwa Rais, lakini kwa sasa hivi ninavyofahamu, kwa mapendekezo kutoka kwa wadau, ameona muundo huu unafaa ili majukumu ya Serikali yaweze kutekelezwa kwa urahisi na kwa ufanisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile ikumbukwe kwamba Tume ya Mipango haiko chini ya Wizara ya Fedha kwa sasa bali iko chini ya ofisi ya Rais na lengo ni kuwa na jopo la wataalamu waliobobea katika eneo la uchumi ambao wanatarajiwa kuishauri Serikali katika masuala yote na mchakato wa maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Riziki Omar Juma, Mbunge wa Viti Maalum, ameishauri Serikali ifuatilie malalamiko ya uboreshaji wa Daftari la Wapiga Kura Zanzibar. Daftari la Wapiga Kura Zanzibar, kwa utaratibu wetu wa sasa, linatayarishwa kwa mujibu wa Sheria ya Uchaguzi Zanzibar, hapa sisi tunafungwa mikono. Hivyo, malalamiko yote kama yapo ambayo yanahusu Daftari la Wapiga Kura Zanzibar, tunaomba wahusika wapeleke huko kunakohusika ili yashughulikiwe na Tume ya Uchaguzi Zanzibar.

Mheshimiwa Naibu Spika, ugawaji wa Majimbo ya Uchaguzi, Tume ya Uchaguzi katika kipindi cha mwaka 2008/2009, itafanya zoezi la Kikatiba la kuangalia upya mipaka yote ya Majimbo ya Uchaguzi na kugawa Majimbo yatakayohusika kwa kuzingatia matakwa ya Katiba na sheria ya Uchaguzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, marekebisho ya Tume ya Uchaguzi, kuna hoja pengine Tume ya Uchaguzi ingefanyiwa marekebisho lakini napenda kusema kwamba muundo wa sasa wa Tume ya Uchaguzi unakidhi matakwa ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977. Aidha, uhuru wa Tume, umeelezwa wazi katika Katiba hiyo na kwa sasa Serikali inachokifanya ni kuandaa Muswada wa Sheria ya Tume ambayo itafafanua mamlaka na majukumu zaidi. Hivyo, tunaomba Wabunge wavute subira pengine katika muda usiozidi mwaka mmoja, Sheria ya kufafanua mamlaka na majukumu ya Tume, tutaletewa hapa Bungeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mfumo wa Uwakilishi na Mgombea Binafsi, nisingependa kwenda kwenye undani wa suala hili kwa vile suala hili kwa sasa liko Mahakamani na taratibu zetu haziruhusu kulizungumzia Bungeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ofisi ya Waziri Mkuu kushirikiana na Ofisi Kiongozi Zanzibar, naomba niwahakikishie kwamba kuna ushirikiano wa karibu sana hata katika maeneo ambayo siyo ya Muungano lakini pia Ofisi ya Makamu wa Rais ndiyo kwa sasa inashughulikia masuala ya Muungano na Waziri Kiongozi kwa Shughuli za Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na anakuwa na mawasiliano ya karibu sana na Mheshimiwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna suala la mgawanyo wa miradi ya uwekezaji katika nchi yetu, Serikali yetu inatekeleza mpango wa ujenzi wa miundombinu ya

mawasiliano ya barabara, maji, nishati na inatekeleza programu maalum ya kuboresha mazingira ya kufanya biashara na kuwekeza ili kuchochea uwekezaji katika Mikoa iliyo nyuma kiuwekezaji na hii ndiyo maana Serikali kwa kupitia Baraza la Taifa la Biashara *(TNBC),* imeanzisha Mabaraza ya Biashara katika Mikoa yote 21, Tanzania Bara na jitihada ya kuanzisha Mabaraza ya Wilaya, zinaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mabaraza haya, yatachochea uwekezaji na kuibua fursa ya uwekezaji kwa Mikoa yote hususani Mikoa iliyo nyuma kiuwekezaji na pengine lengo la kuhamisha Baraza hili kuja kwenye Ofisi ya Waziri Mkuu, ni kwa kutambua tatizo hili kwa sababu ni mtambuka.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile Serikali kwa kupitia kituo cha Uwekezaji, tumefungua ofisi tatu za kanda za *TIC* ili kupeleka huduma karibu na wawekezaji. Pamoja na kuongeza ufanisi katika ngazi za chini, Serikali yetu imekuwa ikishirikiana na Mikoa yote kuwaunganisha wawekezaji wa ndani na wa nje kwa kupitia ziara na makongamano ya ndani na nje ya wafanyabiashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, natoa wito kwa Waheshimiwa Wabunge na viongozi wa Wilaya na Mikoa, wazidi kushirikiana na ofisi zetu za *TIC* na *TNBC* ili kuibua miradi na fursa za uwekezaji katika Mikoa yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu marekebisho ya Tume ya Uchaguzi, nimeshaelezea na Mheshimiwa Juma Said Omar, amehoji zaidi kuhusu Daftari la Wapiga Kura na hapa naomba nitoe maelezo kwamba japokuwa kwa sasa Serikali haioni sababu ya kufanya marekebisho ya muundo wa Tume ya Uchaguzi lakini tupo katika mchakato wa kuangalia upya sheria za uendeshaji wa uchaguzi kwa lengo la kuzifanyia marekebisho kama nilivyosema hapo awali ili kuboresha zaidi uendeshaji wa chaguzi zetu

Mheshimiwa Naibu Spika, Tume ya Uchaguzi Zanzibar, kama nilivyosema, Tume hiyo imeundwa na inaendesha shughuli zake kwa mujibu wa Katiba na Sheria za Uchaguzi Zanzibar.

Mheshimiwa Dr. Slaa, ametoa mchango wa maandishi kuhusu nyaraka nyeti ambazo ni za Serikali kutembezwa mitaani au kujadiliwa wazi Bungeni. Kwa kweli, Serikali imetumia busara nyingi sana tofauti na nchi nyingine duniani, ambapo Waziri yeyote akisema kwamba suala hili ni '*classified'* Spika huwa hana chaguo, kwa sababu duniani kote siri za Serikali huwa zinahifadhiwa. Hata hivyo, kwa vile Kanuni zetu ziko kimya, tumefanya semina baina ya viongozi wa Bunge, hasa Wenyeviti wa Kamati kule Zanzibar na viongozi wa Usalama, wametoa ufafanuzi kwenye nyaraka hizi na pia Wabunge wote wamepewa semina hapa Dodoma. Sasa Serikali inamshauri Mheshimiwa Dr. Slaa na Wabunge wote wavute subira ili tuweze kutoa maelezo zaidi kuhusu suala hili kwa sababu ni suala nyeti na pana kidogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, maeneo ambayo sisi watatu hatujayagusia, Kiongozi wetu, Mheshimiwa Waziri Mkuu, atayatolea maelezo na ufafanuzi. Hivyo, nami naomba kuunga mkono hoja hii, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kwa mamlaka ambayo ninayo kutokana na Kanuni kwamba ninaweza kuongeza muda, kwa hiyo, nitamuita mtoa hoja na atatoa majibu yake mpaka atakapomaliza ila isizidi saa 7.30, sasa namwita Mheshimiwa Waziri Mkuu.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nianze kwa kuwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wote, kwa namna ya pekee ambayo mmetusaidia kuchangia mawazo mbalimbali na hivyo kufanya kazi yetu kuwa nyepesi.

Naomba na mimi nikushukuru sana wewe Naibu Spika, kwa kuwa umeendesha vikao vyetu vizuri lakini niwashukuru wengine wote ambao nao kwa nyakati mbalimbali wamekuwa wakisaidia kuliongoza Bunge hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka jana, wakati kama huu, nilikuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, leo ni Waziri Mkuu. Wakati ule nilikuwa namsaidia Mheshimiwa Lowassa ambaye ndiye alikuwa kiongozi wangu. Kwa hiyo, nataka nitumie nafasi hii vile vile kumshukuru Rais na kuendelea kuwashukuru Wabunge, kwa imani kubwa mliyonipa. Lakini nisiache kumshukuru Mheshimiwa Lowassa kwa sababu nilijifunza mengi wakati wa uongozi wake. Nitamuomba tuendelee kusaidiana mawazo kutokana na uzoefu alioupata nyakati hizo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi hii ya Waziri Mkuu si nyepesi, ni nzito, wakati mwingine watu wanaponipa hongera na mimi huwa nawatazama kwa jicho baya sana, kwa kweli kazi hii ni ya kupeana pole tu na kwa sehemu kubwa inataka ushirikiano wa karibu sana kati ya Wabunge na mimi Waziri Mkuu ambaye ndiye nasimamia shughuli za Serikali hapa Bungeni. Kwa hiyo, kwa kweli nitaendelea kuwaomba kwa kadri itakavyowezekana, tushirikiane maana ndiyo namna pekee tunavyoweza kuendesha nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema haya machache, naomba sasa nijaribu na mimi kupitia hoja mbalimbali zilizojitokeza lakini kabla sijafanya hivyo, naomba kwanza kutambue wale wote waliochangia. Samahani sana, naona orodha nilisahau pale, kwa hiyo, naanza kwa kumtambua nao ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Herbert Mntangi, Mheshimiwa Fatma A. Mikidadi, Mheshimiwa Juma A. Kapuya, Mheshimiwa Charles O. Mlingwa, Mheshimiwa Godfrey W. Zambi, Mheshimiwa Janet B. Kahama, Mheshimiwa Jacob D. Shibiliti, Mheshimiwa Kabwe Z. Zitto, Mheshimiwa Brig. Gen. Hassan Ngwilizi, Mheshimiwa Mbaruk K. Mwandoro, Mheshimiwa Al- Shymaa J. Kwegyir, Mheshimiwa Profesa Idris A. Mtulia, Mheshimiwa Mwanchoum Abdulrahman Msomi, Mheshimiwa Anne S. Makinda, Mheshimiwa Mgana I. Msindai na Mheshimiwa Dr. Luka J. Siyame. *(Makofi)*

Wengine ni Mheshimiwa Victor K. Mwambalaswa, Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, Mheshimiwa Prof. Philemon Sarungi, Mheshimiwa Hemed Mohammed Hemed, Mheshimiwa John P. Lwanji, Mheshimiwa Gideon A. Cheyo, Mheshimiwa Dr. Cyril A. Chami, Mheshimiwa Emmanuel Luhahula, Mheshimiwa Profesa Raphael Mwalyosi, Mheshimiwa Charles Keenja, Mheshimiwa Juma Killimbah, Mheshimiwa Dr. Wilbrod P. Slaa, Mheshimiwa Kabuzi F. Rwilomba, Mheshimiwa Dr. Maua A. Daftari, Mheshimiwa Benson M. Mpesya, Mheshimiwa Sijapata F. Nkayamba, Mheshimiwa Bernadeta K. Mushashu, Mheshimiwa Dr. Raphael M. Chegeni, Mheshimiwa Savelina S. Mwijage, Mheshimiwa Balozi Abdi Hassan Mshangama na Mheshimiwa Dr. Samson Ferdinand Mpanda. *(Makofi)*

Wengine ni Mheshimiwa Mwantumu Bakari Mahiza, Mheshimiwa Haji Juma Sereweji, Mheshimiwa Mgeni J. Kadika, Mheshimiwa Ernest G. Mabina, Mheshimiwa Juma Said Omar, Mheshimiwa Paul P. Kimiti, Mheshimiwa Mwajuma Hassan Khamis, Mheshimiwa Khadija S. Al- Qassmy, Mheshimiwa Fatma O. Ali, Mheshimiwa Feteh Saad Mgeni, Mheshimiwa Ameir Ali Ameir, Mheshimiwa Janeth M. Massaburi, Mheshimiwa Bahati Ali Abeid, Mheshimiwa Benito Malangalila, Mheshimiwa Susan A. Lyimo, Mheshimiwa Yono S. Kevela, Mheshimiwa Pindi Chana, Mheshimiwa Vuai Abdallah Khamis, Mheshimiwa Maida H. Abdallah, Mheshimiwa Castor R. Ligallama na Mheshimiwa Dr. James A. Msekela. *(Makofi)*

Wengine ni Mheshimiwa Faida Mohamed Bakar, Mheshimiwa Joyce N. Machimu, Mheshimiwa Martha M. Mlata, Mheshimiwa Diana M. Chilolo, Mheshimiwa Dr. Aisha O. Kigoda, Mheshimiwa Margaret S. Sitta, Mheshimiwa James P. Musalika, Mheshimiwa Maria I. Hewa, Mheshimiwa Florence E. Kyendesya, Mheshimiwa Elietta N. Switi, Mheshimiwa Mwadini A. Jecha, Mheshimiwa Ali Khamis Seif, Mheshimiwa Lucas L. Selelii, Mheshimiwa Dr. Zainab A. Gama, Mheshimiwa Hadija Saleh Ngozi, Mheshimiwa Dr. Ali Tarab Ali, Mheshimiwa Dr. Omar M. Nibuka, Mheshimiwa William H. Shellukindo, Mheshimiwa Mohamed A. Said, Mheshimiwa Dr. Lucy S. Nkya, Mheshimiwa Magdalena H. Sakaya na Mheshimiwa Ussi A. Pandu. *(Makofi)*

Wengine ni Mheshimiwa Anastazia J. Wambura, Mheshimiwa Clemence B. Lyamba, Mheshimiwa Eng. Christopher Chiza, Mheshimiwa Kiumbwa Makame Mbaraka, Mheshimiwa Wilson Masilingi, Mheshimiwa Vedastus M. Manyinyi, Mheshimiwa Mossy Suleiman Mussa, Mheshimiwa Fuya G. Kimbita, Mheshimiwa Gaudence C. Kayombo, Mheshimiwa Omar A. Mzee, Mheshimiwa Ralnald A. Mrope, Mheshimiwa Vita Rashid Kawawa, Mheshimiwa Zaynab M. Vulu, Mheshimiwa Gaudentia M. Kabaka, Mheshimiwa Athumani S. Janguo, Mheshimiwa Ramadhan A. Maneno na Mheshimiwa Dr. Getrude Rwakatare. *(Makofi)*

Wengine ni Mheshimiwa Ludovick J. Mwananzila, Mheshimiwa Said Amour Arfi, Mheshimiwa Asha M. Jecha, Mheshimiwa Mohamed A. Abdulaziz, Mheshimiwa Profesa Feetham F. Banyikwa, Mheshimiwa Felister A. Bura, Mheshimiwa Ruth B. Msafiri, Mheshimiwa Andrew John Chenge, Mheshimiwa Anthony M. Diallo, Mheshimiwa Felix T. Kijiko, Mheshimiwa Elizabeth Batenga, Mheshimiwa Mwaka

Abdulrahaman Ramadhan, Mheshimiwa Mhonga Said Ruhwanya, Mheshimiwa Mariam S. Mfaki, Mheshimiwa Ephraim N. Madeje, Mheshimiwa Fred Mpendazoe Tungu, Mheshimiwa Kheri Khatib Ameir, Mheshimiwa Dorah H. Mushi, Mheshimiwa Hamza A. Mwenegoha, Mheshimiwa Damas P. Nakei, Mheshimiwa Issa K. Issa, Mheshimiwa Magale J. Shibuda, Mheshimiwa Christopher Ole-Sendeka, Mheshimiwa Thomas A. Mwang'onda, Mheshimiwa Mohamed H. Mnyaa, Mheshimiwa Omar Kwaangw' Mheshimiwa Hasnain Gulamabbas Dewji, Mheshimiwa Teddy L. Kassela – Bantu, Mheshimiwa Dr. Guido G. Sigonda, Mheshimiwa Salim Hemed Hamis, Mheshimiwa Ezekiel Maige, Mheshimiwa Hassan C. Kigwalilo, Mheshimiwa Bujiku Sakila na Mheshimiwa Manju Salum Msambya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hawa niliomaliza kuwataja, ni wale waliochangia moja kwa moja kwa kuzungumza humu ndani sasa naendelea na waliochangia kwa maandishi.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa kuweka rekodi sawasawa, nadhani uliomaliza kuwataja, ni wale waliochangia kwa maandishi, hawa unaotaka kuwataja sasa hivi ndiyo waliochangia kwa mdomo. (*Makofi*)

**WAZIRI MKUU:** Aaaah! *Yes,* sawasawa, nakushukuru sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naomba niwataje waliochangia kwa kuzungumza humu ndani nao ni Mheshimiwa George Lubeleje, Mheshimiwa Dr. Wilbrod P. Slaa, Mheshimiwa John Samwel Malecela, Mheshimiwa Jenista Mhagama, Mheshimiwa Diana M. Chilolo, Mheshimiwa Basil P. Mramba, Mheshimiwa Richard Ndassa, Mheshimiwa Samuel Chitalilo, Mheshimiwa Savelina S. Mwijage, Mheshimiwa Emmanuel Luhalula, Mheshimiwa Lucy F. Owenya, Mheshimiwa Kaika Telele, Mheshimiwa Manju Msambya, Mheshimiwa Peter Serukamba, Mheshimiwa Jackson Makwetta, Mheshimiwa Khalifa S. Khalifa, Mheshimiwa Kabuzi Faustine Rwilomba, Mheshimiwa Omar Kwaangw', Mheshimiwa Said Arfi, Mheshimiwa Ania Chaurembo, Mheshimiwa James Musalika na Mheshimiwa Estherina Kilasi. *(Makofi)*

Wengine ni Mheshimiwa Dunstan Mkapa, Mheshimiwa Ahmed Shabiby, Mheshimiwa George Simbachawene, Mheshimiwa Grace Kiwelu, Mheshimiwa Mudhihir Mudhihir, Mheshimiwa Hassan Khatib, Mheshimiwa Jacob Shibiliti, Mheshimiwa Lucas Selelii, Mheshimiwa Mohamed Missanga, Mheshimiwa Felix Mrema, Mheshimiwa Aziza Sleyum Ally, Mheshimiwa Said Nkumba, Mheshimiwa Dr. Harrison Mwakyembe, Mheshimiwa Dr. Binilith Mahenge, Mheshimiwa Lediana Mng'ong'o, Mheshimiwa Mariam Kasembe na Mheshimiwa Fatma Maghimbi. *(Makofi)*

Wengine ni Mheshimiwa James Lembeli, Mheshimiwa Vedastus Manyinyi, Mheshimiwa Nuru Awadhi Bafadhili, Mheshimiwa Mwanne Mchemba, Mheshimiwa Riziki Juma, Mheshimiwa Margreth Mkanga, Mheshimiwa Paschal Degera, Mheshimiwa Shoka Juma, Mheshimiwa Juma S. N'hunga, Mheshimiwa Mkiwa Adam Kimwanga, Mheshimiwa Dr. Chrisant Mzindakaya, Mheshimiwa Mzee Ngwali Zubeir, Mheshimiwa

Masoud Abdallah Salum, Mheshimiwa Halima Kimbau, Mheshimiwa Mohamed Rajab Soud, Mheshimiwa Abdul J. Marombwa, Mheshimiwa Abbas Z. Mtemvu na Mheshimiwa Idd Mohamed Azzan. *(Makofi)*

Wengine ni Mheshimiwa Abdulkarim Shah, Mheshimiwa Tatu Ntimizi, Mheshimiwa Issa Kassim Issa, Mheshimiwa Dr. Guido Sigonda, Mheshimiwa Stephen Galinoma, Mheshimiwa Profesa Philemon Sarungi, Mheshimiwa Martha Mlata, Mheshimiwa Beatrice Shellukindo, Mheshimiwa Haroub S. Masoud, Mheshimiwa Ponsiano Nyami, Mheshimiwa Laus Mhina, Mheshimiwa Aloyce B. Kimaro, Mheshimiwa Meryce Mussa Emmanuel, Mheshimiwa Dr. Zanaib A. Gama, Mheshimiwa Aggrey J. Mwanri, Mheshimiwa Celina O. Kombani na Mheshimiwa Philip S. Marmo. Jumla tulikuwa wachangiaji 205. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, inawezekana kabisa kuna majina pengine mawili/matatu, tutakuwa tumeyaruka, tunaomba radhi, lakini kama nitaletewa baadaye, nikikumbushwa, nitaweza kuya-*take up* bila matatizo yoyote.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa nipitie hoja mbalimbali na mimi nijaribu kutoa mchango katika eneo hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, iko hoja ilitolewa na Mheshimiwa Dr. Wilbrod Slaa ambaye ni Naibu Kiongozi wa Upinzani Bungeni, kwamba Waziri Mkuu akutane na Vyama vya Siasa ili kubadilishana mawazo. Ombi hilo nilishalipata na nilishawaahidi, tunapanga tarehe ili kukutana nao kwa sababu ni vizuri tukaendelea kushauriana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ingawa hili suala la kuhamia Dodoma limejibiwa na Mheshimiwa Marmo, nafikiri bado ni vizuri na mimi nikaongeza mawazo kidogo kutokana na uzito wa jambo lenyewe.

Kwanza, niombe radhi kama pengine mlipata tafsiri kwamba nakuja na agenda labda ya kujaribu kusema tusihamie Dodoma. *Actually,* mimi ni mpenzi sana wa kuhamia Dodoma kwa sababu nimetumia maisha yangu ya miaka saba hapa Dodoma. Isipokuwa niliamua tuweke agenda hii kwa nia nzuri tu. Uamuzi wa kuhamia Dodoma ulifanywa mwaka 1973 na tukapanga kwamba tutahamia Dodoma ndani ya kipindi cha miaka 10 na ikaandaliwa program, leo ni miaka 35. Nia bado iko pale pale. Lakini nilidhani pengine baada ya kipindi hiki, ni wakati mzuri wa watu kukaa chini na kujiuliza, hivi kasi hii tunayoenda nayo inatosha? Kama haitoshi, tatizo liko wapi? Tukibaini matatizo, tuna mpango gani sasa wa kuhamia Dodoma? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kujaribu kutafuta kumbukumbu mbalimbali, nimegundua kwamba tumekuwa na maswali 100 kutoka kwa Wabunge na yote ukitazama maudhui yake ni kuhoji *pace* ya kuhamia Dodoma na Serikali muda wote tumeweza kujibu maswali hayo lakini si maswali yaliyotutoa kwa kasi kubwa kutoka pale tulipokuwa kuja hapa tunapotaka tuwe. Ndiyo maana nikafikiria tuwe na kongamano Dodoma kwa wenyeji wetu, wale wadau wakubwa ambao tunajua wanaweza kutupa

mawazo, watupe. Twende Dar es Salaam, tukafanye kongamano lingine, tujaribu kujumuisha *private sector* na watu wale ambao tunafikiri wanaweza kuwa na mchango mkubwa katika eneo hili. Kisha nirudi Bungeni pengine kwa semina ya siku moja, tujaribu kwa pamoja ku-*sympathies* mawazo ili tuweze kusema *now we can move* kwa mpango ambao tunadhani tunakubaliana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nalisema hili kwa sababu suala la kuhamia Dodoma liko ndani ya Ilani ya Chama cha Mapinduzi. CCM kwenye Ilani yetu, tumesema kuhusu kuhamia Dodoma kwamba CCM itaendelea kusisitiza na kusimamia utekelezaji wa uamuzi wa kuhamishia Dodoma Makao Makuu ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika kipindi hiki cha 2005/2010. Hatua zifuatazo zitachukuliwa kwa lengo kuzidisha kasi ya kuhamia Dodoma. Kwanza, ni kutunga Sheria ya Kuitambua Rasmi Dodoma kuwa Makao Makuu ya Serikali na kuweka utaratibu wa Serikali kuhamia huko. Kujenga kwa kiwango cha lami barabara ambazo zinapita hapa Dodoma, moja ni ile ya *central corridor* lakini tuhakikishe na ile ya kutoka Babati - Dodoma – Iringa, inajengwa. Kuweka vivutio kwa sekta binafsi ili ishiriki katika uwekezaji kwenye ujenzi wa miundombinu inayohitajika katika ukuaji wa mji huu, na hilo lazima tujiulize, kuongeza kasi ya Wizara za Serikali kuhamia Dodoma kwa kuwa sasa Serikali inajenga nyumba za kuishi watumishi tutumie fursa hizo na nyingine zitakazokuwepo kutoa msukumo mpya ili azma hii ya Chama cha Mapinduzi na Serikali kwa ujumla iweze kufikiwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, pamoja na kumshukuru Mheshimiwa Marmo kwa hili, lakini nimeona niongeze na kusisitiza kwamba nia ni kutafuta namna ya kutoka hapa tulipo kwenda mbele zaidi pengine kwa kasi kubwa zaidi. (*Makofi*)

Vilevile, Mheshimiwa Dr. Wilbrod Slaa aliongelea kuhusu nafasi za uongozi kwa wanawake, alitaka kujua ni mpango gani wa Serikali uliopo wa kutekeleza Azimio la *AU,* la wanawake kufikia asilimia 50 ndani ya Bunge. Hili nalo ni moja ya changamoto tulizojiwekea kwenye Ilani ya Uchaguzi. Wale mnaopenda kuisoma, utaikuta katika Ibara ya 120, ukurasa wa 149. Hapa yapo mambo mawili ambayo nadhani tutaelewa. Liko lengo ndani ya *SADC countries* na liko lengo ndani ya Umoja wa Afrika. *SADC countries,* tulikubaliana angalau asilimia 30 ifikapo mwaka 2010 na *AU* ikasema twende mbele zaidi tufike asilimia 50. Sasa hali ikoje, kwa upande wa Tanzania kati ya Wabunge 324 hivi sasa 94 ni wanawake, wa Majimbo 19 na Viti Maalum wako 75. Hii ni asilimia karibu 30.4 hivi. Kwa hiyo, kwa maana ya lengo lililokuwa tumejiwekea ndani ya *SADC,* Tanzania ni moja kati ya nchi tatu ambazo tumefanya vizuri sana katika eneo hili. Nchi nyingine, *of course,* ni *Mozambique* na *South Africa,* ndiyo wanaongoza kwa maana ya kufikia lengo ndani ya nchi za *SADC* katika eneo letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, swali la Mheshimiwa Dr. Slaa, ni la msingi sana na lazima tujaribu kwenda kwa kasi inayotakiwa. Lakini ni lazima vile vile tuzingatie hali halisi. Kwa hiyo, itabidi tujaribu kufanya kazi hiyo kwa uangalifu mkubwa tukijua kabisa kwamba tuna vikwazo. Kwanza ni, uwezo wa jengo lenyewe la Bunge kama linaweza kubeba kiasi hicho cha Wabunge. Sasa jambo hili bado linazungumzwa, lakini lengo lipo pale pale, jitihada zitafanyika ili tuweze kuona kama tutafikia wapi

katika kutekeleza hiyo azma ya kuwa na asilimia 50. Lakini Ilani haizungumzii Bunge tu, Ilani inazungumzia hata ndani ya utendaji wa Serikali kwa ujumla, wanataka kasi ya kuwa na wajumbe akina mama iwe kubwa zaidi. Sasa nafikiri hili kwa upande wa Tanzania, tunajitahidi sana.

Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete, wakati amevunja Baraza la Mawaziri na kuliunda upya, moja ya kigezo alichokuwa ameweka ni kwamba miongoni mwa Manaibu Mawaziri lazima tupate asilimia 30 ya akinamama, na miongoni mwa Mawaziri, *full Ministers,* ni lazima theluthi moja wawe ni akina mama. Nadhani ni jambo jema na anaonyesha nia nzuri sana kwenye eneo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini wote ni mashahidi, juzi hapo aliapisha Majaji kumi na moja na saba miongoni mwao walikuwa ni akinamama. Kwa hiyo, jitihada hizi tutaendelea nazo. Najua hatujafika mwisho lakini nina hakika tutafika huko kama nia hii na dhamira hii itaendelea kuwepo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Dr. Wilbrod Slaa na hili Mheshimiwa Mama Mwantumu Mahiza amelichangia, aliuliza kwamba Serikali ina mpango gani wa kuanzisha mchakato wa kurekebisha Katiba ya nchi kwa kushirikisha wadau wote. Hoja hii imekuwa ikiibuliwa mara nyingi sana na hasa rafiki yangu Dr. Wilbrod Slaa na ndugu yangu Mheshimiwa Mohamed Rashid Hamad. Mimi nina mawazo tu kwamba suala la kubadili Katiba ni *on going* kutegemea kwa kweli na vikwazo na matatizo yanayobainishwa na kwa kipindi hicho yakaonekana yanahitaji mabadiliko ya Kikatiba. *(Makofi)*

Sasa rai hii inaweza kuwa imetokana na Bunge, inawezekana ikatokana tu na mijadala mbalimbali inayoendelea. Kwa hiyo, mimi sioni kwamba ni tatizo kubwa kwa maana ya kufanya marekebisho kama yapo maeneo ambayo wote kwa pamoja kama Taifa, tunaona ni vizuri yakafanyiwa marekebisho. Kubwa ni tunafanyaje? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nadhani hilo ndilo jambo peke yake unaweza ukaliona. Tunaweza tukapitisha mijadala kupitia ngazi mbalimbali na ikionekana kwa kweli kuna msingi, mimi sioni tatizo, *after all,* tumekuwa tukifanya mabadiliko haya kwa muda mrefu kidogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Dr. Wilbrod Slaa, vilevile amesema kwamba Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2010, upo karibu hivi wadau wameshirikishwa kwa kiasi gani? Ni kweli muda upo karibu, lazima tukubali hilo na ndiyo maana mnaona katika bajeti ya mwaka huu ambao tutaanza, tumelazimika kuweka fedha katika Tume ya Uchaguzi ili kazi hiyo kwa kweli ianze mapema na moja ya mambo ambayo mtayaona magumu, kwanza, ni uwekaji

wa mipaka ya Majimbo, Kata vilevile zitahitajika ku-*demarcate* vituo vya kupigia kura, lazima navyo vianze kuainishwa mapema, elimu kwa wapiga kura, nayo lazima ianze kutolewa mapema.

Mheshimiwa Naibu Spika, siyo hivyo tu, ni lazima vilevile mambo mengine ambayo yanahitajika kutolewa ufafanuzi na yenyewe yazingatiwe ndani ya muda huo tulionao. Moja, ni lile ambalo Mheshimiwa Philip Marmo, amelisema la kuwa na *independent candidate*. Sasa tukipata uamuzi *finally* kwamba Mahakama imeelekeza nini, ni mambo ambayo lazima uwepo utaratibu unaoweza kuwezesha jambo hili kufanyika bila matatizo yoyote.

Kwa hiyo, Mheshimiwa Dr. Wilbrod Slaa, nataka nikuhakikishie, *we are on need,* tunajipanga vizuri na tutawashirikisha wadau wote ambao tunaona ni vizuri wakashirikiana katika eneo hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa msingi huo huo, nitamwomba na Mheshimiwa Benson Mpesya ambaye alitoa rai yake kwamba angependa Jimbo lake ligawanywe, ni katika *process* hiyo na pengine ni wakati huu huu maana hatuna muda mrefu zaidi kabla hatujafunga ukurasa ili Tume ianzie kufanya *demarcation.*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Dr. Wilbrod Slaa vilevile alinibana sana kwenye taarifa ya Ihefu alisema Serikali itoe taarifa kuhusu matokeo ya Tume ya Rais ya Kuchunguza Uhamishaji wa Mifugo katika Bonde la Ihefu na sehemu nyingine. Nadhani kulikuwa na maelezo vilevile sijui kutoka kwa Mheshimiwa Mbunge gani ambaye alikuwa anauliza kwa nini hizi taarifa mbalimbali za Tume zinazaundwa huwa hatupati matokeo yake, inakuwaje?

Sasa mimi naomba kwanza niwatoe wasiwasi, taarifa zote ambazo zinaandaliwa kutokana na maamuzi ama ya Mheshimiwa Rais ama ya Baraza la Mawaziri au Waziri fulani, ni taarifa ambazo lengo lake ni kusaidia utendaji ndani ya Serikali na mara tu inapokuwa imekamilika, ndiyo maana lazima Mheshimiwa Rais au Waziri anayehusika, atumie taarifa hiyo kufanya marekebisho katika baadhi ya maeneo ambayo anaona ni lazima yafanyike.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ni kweli taarifa ya Jaji Chande ilikamilika tena mwaka jana akaikabidhi kwa Mheshimiwa Rais na sisi wengine tukapewa hiyo taarifa kwa lengo sasa la kutazama yale maeneo ambayo yanahitaji kufanyiwa kazi na moja ya eneo ambalo lilijitokeza mle dhahiri ni hali ya malipo au fidia kwa wafugaji ambao walilazimika kuondoka kwenye eneo lile. Sasa si kwamba tulilipuuza jambo hilo,

hata kidogo. Mimi kwa maelezo niliyonayo mpaka sasa nafikiri tumekwisha kutumia karibu bilioni sita katika kujaribu kutoa fidia kwa Watanzania waliokuwa wameathirika na zoezi hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kwa upande mwingine, lazima niseme kwamba, kuondolewa kwa watu pale Ihefu, jamani ni kwa faida ya Watanzania wote. Leo hali ya uoto imerudi, maji yapo ya kutosha maana yale ndiyo yanayo-*feed* Mto mkubwa ambao unapeleka maji Mtera. Kwa hiyo, wakati tunakubali kwamba kama kuna upungufu urekebishwe, usahihishwe lakini vilevile ni lazima tukubali kwamba hatua hiyo ilikuwa ni muhimu katika kurejesha hali ya umeme nchini Tanzania vizuri.

Mheshimwia Naibu Spika, Mheshimiwa Dr. Wilbrod Slaa, vilevile alitoa hoja yake kuhusu mauaji maalbino. Nilikwishakulisemea suala hili, tunaendelea kulaani kabisa kwa nguvu zote na mimi ninajua Waheshimiwa Wabunge, katika hili, tupo pamoja, tuendelee kusaidiana. Sisi kama Serikali, tutaendelea kutoa msukumo, tutajaribu kufanya kila litalowezekana kwa ajili ya upelelezi ili kuhakikisha jambo hili linasimamiwa kwa maana ya kukomesha kabisa mauaji ambayo hayana msingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa siyo Mheshimiwa Dr. Wilbrod Slaa peke yake, lakini yupo vilevile Mheshimiwa Hassan Rajab Khatib, Mbunge wa Amani na Mheshimiwa Nuru Awadhi Bafadhili ambaye naye alichangia katika eneo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine iliyochangiwa na Waheshimiwa hawa, inahusu muafaka wa CCM na *CUF*. Waheshimiwa Wabunge hawa waliuliza, Serikali inachukua hatua gani kuhusu kunusuru muafaka wa CCM na *CUF?* Mheshimiwa Rais aingilie kati suala la mpasuko wa kisiasa Zanzibar.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nirudie maneno ambayo tumekuwa muda wote tunayasema, Rais wetu mpendwa amejaribu kulieleza sana jambo hili na mimi ninaomba niseme.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaamini kwa dhati kabisa kwamba viongozi hao wa Chama cha *CUF* na Chama cha Mapinduzi, watarudi na kukaa kwenye meza, hata haya ambayo tunadhani magumu sana yanawezekana kutatuliwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini inaonekana kama vile kuna hali ya kukata tamaa, watu wanaona kwamba hakuna maana. Mimi nafikiri turudi kwenye mazungumzo ili tuweze kufanya hiyo kazi wote kwa pamoja. Nia na dhamira ya Rais na dhamira ya Watanzania, ni kuhakikisha kwamba Zanzibar kwa maana ya Unguja na Pemba wanaweze kuishi kwa amani, upendo na kwa kweli kwa namna ambayo watajisikia kwamba waishi katika hali nzuri. Sasa hili ni lazima tulifanye kwa utaratibu ambao

utasaidia kujenga imani pole pole ili jambo hili liweze kuwa la ukweli na uhakika, punde maamuzi yatakapokuwa yamefanyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, najua hapa lilikuja jambo hili baada ya kuambiwa kwamba inabidi tukapige kura za maoni ili tuone namna gani tuendelee mbele. Mimi kwa kweli sioni tunachoogopa nini kwenda kwenye kura ya maoni. Kama kweli tutakaa, tukapanga utaratibu mzuri wa namna ya kuendesha kura ya maoni, maana ni lazima tukubaliane, pande zote mbili na pande zote mbili tukainuka kwenda kuifanya kazi hiyo kwa dhamira moja, sioni tatizo hata kidogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kwa upande mwingine nimekuwa namwambia Mheshimiwa Hamad na mara moja moja Mheshimiwa Dr. Slaa. Nasema jamani, hivi nani asiyejua kwamba ukienda pale Zanzibar ukasema leo una-*impose* uamuzi mkubwa kama huu ambao tunauzungumza, utapata matatizo makubwa katika kutekeleza? Unahitaji kuandaa Watanzania vizuri na kwa mshikamano wa pamoja kati ya vyama vyote viwili ndipo mnaweza mkavusha jahazi hilo na mkaona mafanikio tunayoyataka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, liko suala la utoaji maamuzi linalojitokeza kutoka kwa Mheshimiwa Felix Christopher Mrema, kwamba Serikali inashindwa utoaji wa maamuzi ili kuwezesha utekelezaji wa haraka wa miradi hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nakubali kabisa. Nakubali kwa sababu sio siri hata ndani ya Serikali yenyewe wakati mwingine nawasikiliza mnaposema tunapeleka barua, tunapeleka maagizo, hujibiwi. Kwa hiyo, iko *relaxation* katika utumishi wa umma ambayo kwa kweli lazima kuhakikisha inaondoka. *(Makofi)*

Ndiyo haya yanayopelekea maamuzi wakati mwingine kuchelewa sana. Mtu amekalia tu jambo badala ya kufanyia uamuzi. Tusiogope kufanya uamuzi. Mimi nafikiri fanya uamuzi *wrong or right,* lakini toa uamuzi wako kuliko kukaa unacheleweshа jambo, halafu *it is interesting* kwamba mambo haya yanatokea wakati ndiyo tumejitahidi kweli kweli na vitu vinaitwa mikataba ya huduma kwa wateja. *(Makofi)*

*What is this?* Mbona ni *contradiction?* Mnaweza kuwaje na mikataba mizuri namna hiyo halafu bado mkawa ndiyo watu mnaochangia katika kuzorotesha utendaji ndani ya Serikali? *So, I think* ni jambo ambalo lazima tutalifanyia kazi kwa karibu zaidi ili tuhakikishe kwamba linafanywa kuwa ni jambo la msingi kabisa katika eneo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, liko jambo nafikiri Mheshimiwa Marmo ameligusia na lilitolewa hasa na Mheshimiwa Mohamed Rashid Mohamed. Anasema masuala nyeti hasa ya ufisadi, nadhani ufisadi imekuwa kila mahali, hata kwenye basi unaambiwa fisadi tu. Yenye athari kwa Taifa ni vyema yapelekwe kwenye Kamati ya Uongozi ya Bunge ambayo itashauri na kushirikisha Bunge. Mimi nadhani rai hii siyo mbaya, ni jambo

linazungumzika na pengine mkitumia vizuri fursa hiyo mnaweza mkapunguza hata baadhi ya migongano na mitafaruku ambayo pengine sio ya lazima sana.

Lakini nalo hili linataka kuwepo imani ya kweli miongoni mwenu. Hata kama ni kwenye hiyo Kamati ya Uongozi wa Bunge, mtu akishaanza kusema tu kwamba lakini Mheshimiwa Dr. Slaa, nikisema hili, najua atapeleka tu mahali fulani. *Then* utapata shida kusimamia utaratibu huu. Lakini kama wote kweli tutadhamiria kwa yale ambayo kimsingi tunakubali, lakini iwe siri yetu, *well and good*. Mimi nadhani ni jambo jema, linaweza likatazamwa na mimi nitajaribu kuzungumza na wenzangu tuone namna tunavyoweza kulisukuma.

Kuhusu maslahi ya Wabunge, hili wengi sana tumelizungumzia. Lakini Mheshimiwa Marmo amejaribu kulijibu vizuri tu na mimi nataka niungane naye kwamba pengine tukifaulu tukapata maamuzi ya Mawaziri juu ya ule Waraka tunaousubiri, inawezekana baadhi ya mambo kwa kweli yakafanyiwa haraka zaidi. Kwa sababu sielewi, sioni l*ogic* kabisa kwamba Mbunge huyu ambaye ni nguzo kati ya mihimili mitatu ya Serikali mmem-*facilitate* kwa kumpa mshahara, mnampa posho ili aweze kutimiza majukumu yake vizuri. Anakuja Dodoma hapa na dereva wake, lakini mnasema atakula alichonacho Mbunge. Hii kidogo, *it doesn't make sense. (Makofi)*

Mimi nadhani ni suala la kukaa chini tujaribu kutafuta *modality.* Mimi kwa imani kabisa naamini inawezekana. Inawezekana kwa sababu mkiwa na dhamira ya kumsaidia Mbunge, sioni kwa nini hili libakie ni mzigo wa Mheshimiwa Mbunge, *I don't think so.*

Mheshimiwa Naibu Spika, matumizi ya stakabadhi ya mazao ghalani. Hili nataka kwa kweli kulisisitiza tu. Najua Mheshimiwa Luhahula, hata rafiki yangu Mheshimiwa Dr. Mwakyembe kalisema. Lakini Lembeli vile vile alizungumza na inawezekana wako wengine vile vile wametoa mawazo yao juu ya jambo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi natoka Rukwa na Rukwa tunatumia mfumo huo. Kwa sababu sisi *basically* tunashughulika na kilimo cha mahindi na mpunga. Una manufaa makubwa sana. Ni utaratibu mzuri unaomwezesha mkulima kwanza kuwa na soko la uhakika, lakini wakati ule ule anakuwa na akiba kwa maana ya fedha ambazo zimeshikiliwa chini ya utaratibu huu na kwa wakati muafaka anapewa zile fedha ambazo kwa kweli zinamwondoa katika matatizo aliyokuwa anayaona. Lakini kubwa zaidi, mnaondoa tatizo la walanguzi, kwa sababu hawa ndiyo tatizo kubwa na hivi sasa wameshaanza kupeleka magari kule, wakanunue chakula bado kiko mashambani kwa bei ya kutupa. Suluhu pekee yake ni utaratibu huu ambao hata Mtwara kwa kiasi fulani imewasaidia sana. *(Makofi)*

Kwa hiyo mimi naomba nitoe wito kwa Wakuu wa Mikoa wote, hili jambo tulivalie njuga, litatusaidia sana. Linataka tu imani, lazima ujenge imani kwa wakulima ili muweze kufanikisha jambo hili vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika liko japo lingine hapa tete kidogo, lakini lazima tuliseme, nalo ni la Mahakama ya Kadhi. Wazo hili limetoka kwa Mheshimiwa

Msambya Mheshimiwa Hassan Rajab Khatib, Mheshimiwa Mohamed Hamisi Missanga, Mheshimiwa Juma Suleiman N'hunga na yeye vile alichangia kwenye eneo hili. Hii ni moja ya malengo ya Chama cha Mapinduzi. Tuliahidi kwamba jitihada zitafanyika ndani ya miaka mitano kulipatia suluhu au ufumbuzi suala hili. Sasa hata kwa lugha iliyomo kwenye ilani inaonyesha kabisa kwamba iko hali ya kutokukubaliana juu ya jambo hili. Ndiyo maana Chama kikasema, wacha nijaribu ndani ya miaka mitano kama naweza nikaondoa hiyo hali ya mtafaruku au hali ya kuvutana.

Sasa nilisema ni jambo tete. Ni tete kwa maana hasa kwamba kwa mujibu wa Katiba ya nchi yetu, tunaheshimu sana madhehebu haya ya dini. Kwa mfumo ulivyo, Katiba inasema wazi wazi masuala yote ya jamii yanayohusiana zaidi na madhehebu ya dini, *activities* za kidini dini hivi, haya yatashughulikiwa na madhehebu yanayohusika.

Ndiyo maana unapokuja kwenye eneo hili unapata shida kidogo kwamba aha, sasa *okay,* mnataka kuingiza jambo hili kwenye mfumo wa kisheria wa kikatiba? Wakatoliki nao wana *Canon Law* vile vile, watasema mkilikubali hilo na sisi tunaomba tuanzishe Mahakama ikubalike. Ndiyo maana unaona kidogo linakuwa tete. Sio kwamba kuna mtu anakataa tu, katika hali tuliyonayo sasa, ni dhahiri mambo haya hamuwezi mkayapuuza, yaani mkayarahisisha kiasi hicho. Inabidi wote tukubaliane kwamba *yes,* inahitaji maelezo.

Lakini kubwa na mimi nasema, nadhani hili ni suala la *time factor.* Tutafika mahali litaonekana sasa kwamba nadhani linawezekana na nitawaambia kwa nini. Hata kwa mfumo wa Mahakama hivi sasa, tumeshamega, tuna Mahakama ya Biashara. Hatukuwanayo hii. Sasa hivi tuna Mahakama ya Ardhi, haikuwepo, haya Mabaraza, tuna Mahakama ya Kazi *(Labour Disputes),* mwanzoni zote zilikuwa zinasimamiwa na mfumo mmoja wa Mahakama. Lakini Mahakama yenyewe imekuja, inaona hapana. Ukitaka hili liende vizuri, wape. Mnafanya s*pecialization* kwa namna moja au nyingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nasema, hata hili *at some stage* huko tunakokwenda watu mmeelewana, mmefika mahali haitawaletea *clashes* za namna yoyote, kama ilivyofanyika kwa Mahakama ya Biashara, Mahakama ya Kazi, Mahakama ya Ardhi, itafika mahali watu watasema aah, hata mkiliweka hilo tumeshaelewana, watu tumepata elimu ya kutosha. *Problem* sasa haijaandaliwa vizuri, elimu haijapatikana ya kutosha. Bado kuna hali ya kusigana sigana hivi miongoni mwa madhehebu haya ya dini *and this is not small issue* jamani. Mimi naomba niwasihi sana sio jambo dogo hili! Lazima sasa tuliandae vizuri ili tuweze kuona tunafanya nini. *(Makofi)*

Lakini kwa bahati nzuri jambo hili nadhani bado linashughulikiwa kwenye Tume nadhani ya *Law Reform Commission.* Nadhani hatimaye tutakuja kusikia wamesema nini. Lakini nataka tu ni-*express why?* Tunadhani ni jambo linataka maandalizi, *time* kidogo, hasa mnapokuwa nchi moja mnaheshimiana vizuri kiasi hiki. Unaweza ukakaa na Mohamed, ukakaa na Mudhihir, wakati mwingine hata *you don't even know his name* mradi ni Mtanzania tu. Sasa hiyo hali ni vizuri tukailea na kama inabidi twende huko, twende, lakini tumeelewana na *this is no longer a big issue.* Kwa hiyo, mimi nadhani

tutafika hapo na tunaweza kabisa tukatamba kwamba sasa tumekwenda huko. Naelewa Kenya wanao mfumo huo, lakini mfumo wa Kenya una historia yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, historia yake ni ya siku nyingi sana, kwa sababu ile Pwani ilikuwa ni sehemu ya utawala wa kiarabu ambao Makao yake Makuu ilikuwa ni Zanzibar. Kwa hiyo, wakati Mwingereza ana-*take over* wakati sasa Sultani anaombwa ku-*surrender* ile Pwani, akalazimika kumbana Mwingereza wakubaliane mambo fulani fulani. Kwa hiyo, moja ya jambo alilokubaliana naye ni uendelezaji wa mfumo wa Kadhi hasa pale Mombasa. *(Makofi)*

Kwa hiyo, ina historia yake kidogo, ingawa nimeona sasa wanajaribu kulitazama kama linaweza likapanuliwa likaingia kwenye mfumo kama tunavyoona kwenye *Judicial System* ambazo zina *hierarchies* zote tatu. Mimi nasema *it is a question of time.* Wenzetu walikuwa na hiyo *advantage,* sisi *unfortunately* hatukuwanayo. Inabidi sasa tuijenge katika mazingira ambayo tunatakiwa tuyajenge na wala hapa hakuna suala la jazba, hakuna suala la ukali, ni suala tu la watu kukaa kuzungumza na kuelimishana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niseme kidogo juu ya hili jambo la Jiji la Dar es Salaam. Nalisema hili kwa makusudi kwa sababu nilishakubali kwamba Dar es Salaam haiwezi kuwa *treated* sawa sawa na miji mingine. Matatizo yake ni mengi mno. Inahitaji kwa kweli *attention* ya namna yake.

Kwa hiyo, bado nataka nisisitize kwamba kwa hili tutakwenda nalo. Mimi niliwaahidi Madiwani Dar es Salaam kwamba nitajaribu kusimamia eneo hili vizuri ili tuone namna Serikali Kuu tunavyoweza ku-*cheap in* moja kwa moja badala ya kusema kwamba hizo ni shughuli za Manispaa ya Ilala au Kinondoni. *It is not possible!* Huwezi ukawa jicho la Serikali, halafu pale una Ofisi zote, Ofisi ya Ikulu, halafu unasema Manispaa hiyo itafanya kila kitu. Hakuna! Sisi kama Serikali tuweze kuleta hali ambayo ni nzuri zaidi badala ya haya ambayo sasa tunayaona yanaendelea. *(Makofi)*

Liko lingine ambalo nadhani nalo ni zuri, kuhusu uchunguzi wa maghorofa. Nakumbuka kama mwaka mmoja uliopita tulipata tatizo ya ghorofa pale Keko, likaporomoka chini. Juzi tena tukapata *incidence* nyingine ya namna hiyo. *It is very unfortunate,* katika hiyo ya juzi tumempoteza Mtanzania mmoja. Mungu amrehemu, amweke mahali pema pema Peponi. Lakini kifo kile katika mazingira ya kawaida hakikuwa cha lazima hata kidogo. Kitakuwa kimetokana na uzembe wa namna fulani ambao umepelekea jengo lile lika-*collapse*. Sasa taarifa ile nataka niwahakikishie kwamba ililetwa Serikalini, wakati ule Mheshimiwa Lowassa akiwa ndiyo Waziri Mkuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, uliundiwa utaratibu mzuri sana. Juhudi za kufanyia kazi matatizo yaliyokuwa yamejitokeza wakati ule ziliendelea na bado zinaendelea. Isipokuwa kama mnavyojua wote, unapokuwa na dudu kubwa kama Dar es Salaam ile na Manispaa zenye uongozi, kama kila mmoja ana lwake hivi, ndiyo maana yule Mhandisi siku ile alipokamatwa, mimi nikainama chini nikasema afadhali. Maana *you are*

*supposed to have made* utaratibu wako wa namna ya kufuatilia ujenzi wa majengo hayo. *You never did it!* Maana jengo lile linaonekana *from the beginning* kwamba halikuwa na viwango. Mtu makini angeweza kulipata hilo jambo, lakini hatukufanya hivyo. Kwa hiyo, ndiyo maana nasema, ni matatizo makubwa. Lakini naomba niseme kidogo *what happened* kwenye ile ripoti, maana ni vizuri mkajua tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika ripoti ile wanasema katika Manispaa ya Ilala, Kamati ile ilikagua majengo 505 ya ghorofa. Haya yako katika hatua mbalimbali za ujenzi. Lakini yako vile vile ambayo yalikuwa yamekamilika. Lile lililoporomoka mnajua nalo liko Ilala. Sasa nilipoliona nikawa nasema na hili walikagua? Sasa inawezekana, maana waliniambia Mzee tulilifanyia baada ya Tume. *I am not sure.* Inawezekana, lakini yalifanyiwa hivyo.

Sasa katika ukaguzi uliofanyika, walikuta mambo mengi tu mle, mapungufu mengi tu ambayo ndiyo hayo tulisema lazima yasimamiwe vizuri ili tuweze kuwa na uhakika kwamba ujenzi huo utakuwa wa manufaa kwa Watanzania. Sasa katika yale maghorofa 505, tuligundua kwamba majengo 147 hayakuwa na nyaraka ya kuruhusu ujenzi. *Can you imagine?* Maghorofa 147, Mswahili kasimama tu anajenga tu jengo hana kibali cha kumruhusu kujenga na mengine yameshajengwa yakakamilika. Majengo 81 yalijengwa bila kuzingatia masharti ya ujenzi na mengine 22 wenyewe hata hawakupatikana. Jitihada za kuwafuta haukupatikana.

Kwa hiyo, *you can see problem* ilivyo kubwa. Lakini *all that we can do as a Government* ni kukubali kwamba jambo hili tujaribu kukaa chini na kulitafutia ufumbuzi na mimi nimesema tutakaa na wataalam. Haya mambo ya kusema tu Mhandisi wa Manispaa, Mhandisi wa Manispaa, haitoshi. Tutakuja kupoteza maisha ya Watanzania wengi zaidi kuliko hata yaliyotupata juzi. Kwa hiyo, tutajitahidi tuone la kufanya kwenye eneo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niseme hili lingine, lakini nitalisema kwa kifupi tu. Humu limejitokeza katika sura ya pembejeo. Mheshimiwa Mhagama amelisema sana, Mheshimiwa Mzee Malecela mwenyewe, Mheshimiwa Omar Shaaban Kwaangw', Mheshimiwa Dunstan Mkapa, Mheshimiwa Said Nkumba kalisema sana, Mheshimiwa Lucas Lumambo Selelii rafiki yangu kalisema, Mheshimiwa Mrema, Mheshimiwa Mariam Kasembe na Mwanne Mchemba. Hii inaonyesha tu kwamba ni tatizo kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini tatizo hili ni kubwa kwa nini? Tatizo ni kubwa, kwanza, ni kwa sababu katika tani zile tunazohitaji hapa nchini karibu laki nne, kiwango cha mbolea inayopatikana kwa ujumla wake tu mara zote haifiki tani laki nne. Ukiweka sasa sharti la ruzuku, kile kinachopatikana kwa njia ya zuruku kinakuwa kidogo zaidi na hapo ndipo unakuta matatizo yanajitokeza, ujanja mawakala wake, kila mmoja anajaribu kutumia mwanya huo kufanya analoona yeye. Kwa hiyo, nataka niseme kwamba nadhani hili jambo tulitazame kwa upana wake kwa maana ya sekta ya kilimo. Lakini mimi naamini atakapokuja Mheshimiwa Wasira atajaribu pengine kutoa maudhui kwenye bajeti ya mwaka huu na kwa kweli namna tunavyojaribu kulikabili kwa maana ya kuweza

kuona kwamba *financial year* tuwe tumejipanga vizuri sio kwa pembejeo tu, lakini hata mfumo wa kilimo wenyewe. Lakini hata mfumo wenyewe wa kilimo. *(Makofi)*

Asilimia 70 hivi ya Watanzania bado tunatumia jembe la mkono tu, lakini mnataka mka-*feed* watu chungu mzima! Hamuwezi kwenda! Kwa hiyo, tunajaribu kupata mawazo kulia na kushoto tuone namna gani tutaweza kufanya hii kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya haya, sasa niliona niharakishe, maana mwalimu wakati ananifundisha shule alisema unakwenda kwenye mtihani unaanza na mepesi mepesi kidogo, halafu ndiyo unarudi kwa yale makubwa. Maana yale makubwa wakikwambia *time* unayaacha. Mnayaacha mradi yale mengi mepesi umeshayapitia tayari. *(Makofi)*

Sasa haya yaliyobaki ndiyo yenyewe hasa ambayo Mheshimiwa Dr. Slaa anayangoja kwa hamu kubwa sana. Nianze na hili ambalo Mheshimiwa Dr. Slaa alisema hapa Bungeni, kuhusiana na kesi ya Karatu. Akaishitaki CCM kwamba sasa mmegundulika wezi wakubwa nyie! Nikawa nacheka kichini chini nikasema hivi nani mwizi? CCM au wa CHADEMA hawa?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu gani? Kilichotokea kwenye kesi ile, waliolalamika ni wapigakura wa Chama cha Mapinduzi na ndiyo waliomshitaki Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Mheshimiwa Dr. Slaa akaona mh! Mwanasheria peke yake huyu, linaweza kuwa li-CCM CCM hivi, akajitokeza akasema naomba na mimi mniunganishe, tukasema njoo! Kwa hiyo, tukawa na watu wawili, Mwanasheria Mkuu wa Serikali na yeye mwenyewe Mheshimiwa Dr. Slaa. Lalamiko la hawa wananchi watatu dhidi ya ushindi wa Mheshimiwa Dr. Slaa ilikuwa *simple* tu, kwamba katika kuhesabu zile karatasi zinazowapa kura, walihesabu na kura ambazo hawa watatu waliamini ni za kughushi na zote zilihesabiwa zikampa ushindi Mheshimiwa Dr. Slaa. Wakasema, hapana bwana, mmetuonea sisi na tunaamini ziko nyingi tukizitafuta hizo, Mheshimiwa Dr. Slaa atadondoka. Ndiyo maana aliposema wezi CCM, nikasema aka mwenzangu! Wewe ulihesabiwa zote hizo, ndiyo mwenyewe hasa! *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nini kilitokea kwenye ile kesi? Jaji kawasikiliza wote vizuri sana na mwisho akasema, turudie. Wamehesabu zile kura wakawa wanatenga zile ambazo wanadhani ni za kughushi, wakaziweka pembeni. Wakasema haya mhesabu sasa hizo ambazo mnasema ni halali. Kwa hiyo, wakazihesabu hizo, tena bado ndugu yangu Mheshimiwa Dr. Slaa akashinda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ndiyo nikawa nasema, sasa wewe Mheshimiwa Dr. Slaa, umetunyanyasa kiasi hiki rafiki, bado unatu-*acuse* kwamba tumeiba, he! Kwa hiyo, nilitaka niseme tu kwamba uamuzi wa Mahakama ndiyo ulioamua hivyo.

Sasa nimeambiwa tutakata rufaa, wacha wajaribu. Maana ndiyo utaratibu wenyewe. Lakini kwa sasa mimi nasema nakupongeza sana Mheshimiwa Dr. Slaa, ushindi awamu ya kwanza hata baada ya *judgement* ya Mahakama ukashinda tena.

Ikitokea tena kwamba huko tunakufurumua tunakutoa, hiyo itakuwa ni jambo lingine. Lakini kwa sasa tunakubali. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili hili ni la *EPA*. Sasa *EPA* unaona ina mvuto mkubwa sana. Nami naelewa kwa nini? Naelewa kwa sababu kuna fedha pale ambazo Watanzania wanataka kujua zimetokatokaje Benki Kuu? Mimi nasema mradi zilikuwa Benki Kuu, maana hoja ni kwamba ziko ndani ya chombo cha Serikali, haiwezekani mtu ukaruhusu mtu mwingine yeyote akaja akazichukua hivi hivi akazipeleka tu anakoona *just like that,* haiwezekani! *(Makofi)*

Kwa hiyo, hoja hapa ni *where did that money gone?* Hizo pesa zimekwenda kwa nani? Akafanyie nini? Je, utaratibu ulifuatwa? Sasa mimi nadhani kwa hili wala hakuna sababu ya kulumbana. Mheshimiwa Rais ameshasema tumwachie. Ameunda ile timu, aliwaahidi miezi sita. Ikikamilika, *we are all anxiously waiting* kuona tutapata taarifa ya namna gani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mtazamo wangu, kwa maana ya tatizo hili, nadhani ni shauku. Shauku ni kubwa, watu wangependa mambo haya leo. Lakini wakati mwingine mambo mengine leo hivi hapana. Mimi nafikiri tufanye subira kidogo. Muda wenyewe kwanza umeshakwisha, sana sana atakachofanya kama utasema bado, utasema mzee labda unaruhusiwa kuongeza kidogo.

Lakini kubwa ni kwamba mwisho wa safari Mheshimiwa Rais mwenyewe ameji-*commit* kwamba atataka Watanzania wajue kumetokea nini. Hapo ndiyo sasa tunaweza tukaanza kuulizana maswali, ooh, sijui kwanza ni Mhindi! Mimi nadhani kubwa kwanza ni pesa zitafutwe, zirudi. Nadhani hiyo ndiyo hoja ninayoiona mimi kubwa sana. *(Makofi)*

Kwa hiyo, Mheshimiwa Dr. Slaa kwa sababu ulilizungumza sana hili kwenye hotuba yako na Mheshimiwa Arfi naye alikuja akalizungumza vile vile, lakini wako na Waheshimiwa Wabunge wengine ambao nao walizungumza. Naomba nitoe rai tu kwamba kwa muda mfupi uliobaki pengine tusubiri. Maana hata ukiiniuliza na mimi nitakuambia Mheshimiwa Dr. Slaa hata mimi sijui *what is going on.* *(Makofi)*

Rafiki yangu Mheshimiwa Mwanyika hapa, kila nikimbembeleza hivi kukoje? Anasema Mzee, wewe ngoja tu karibu mwishoni. Sasa nifanyeje?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nadhani tungoje litakalowezekana. Sasa ndani yake *of course* liko suala la Marehemu Dr. Ballali. Rafiki yangu Mheshimiwa Dr. Slaa anasema Serikali itoe taarifa kuhusu kifo cha Marehemu Dr. Ballali. Halafu kuna mahali, hakuishia hapo, kuna mahali alisema kutokutoa taarifa hii ni kama vile tunachezea chezea jambo hili la kifo cha Marehemu Dr. Ballali. Hakuishia hapo, akasema angetamani iundwe Kamati huru. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nikawa najiuliza, unataka kuunda Kamati ili kwenda kuchunguza kifo cha Dr. Ballali? Iundwe Kamati huru ya Serikali kuchunguza kifo cha

Dr. Ballali na taarifa yake iwasilishwe Bungeni! Sasa mimi sijui, lakini naelewa maana iko *connected,* alikuwa ni Gavana wa Benki Kuu, kwa hiyo, *presumable* atakuwa alikuwa anajua siri na mambo yanavyokwenda, *there is no doubt about that. (Makofi)*

Lakini hili wazo linaloendelea kusukumwa sukumwa hivi kana kwamba Dr. Ballali mchawi wake ni Serikali, mimi kidogo linanipa shida sana. Hilo ndilo linalonipa shida sana! Jamani huyu mtu amefariki, na jamii ndugu zake wote wanasema amefariki. Sasa kuendelea kutaka kumchokonoa Marehemu napata taabu kidogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu niseme, maana sielewi hasa kifo chake, hofu iko wapi? Kwa sababu jambo hili kwa wale ambao mna *interest* na kifo chake mngeweza pengine kutafuta utaratibu wa kusema kwamba tunaomba *postmortem if that was necessary.* Lakini kuiambia leo Serikali, yes, alikuwa mtumishi wetu, Gavana wa Benki Kuu, *there is no doubt about that.* Lakini *what happened* baada ya *crisis* ya *EPA* ilibidi huyu mtu ajiwajibishe kwa namna ile. Sasa mnataka hata baada ya pale! Mimi nafikiri tungoje taarifa ya mapesa yetu. Sasa kama watamtaja Marehemu Dr. Ballali humo, hawatamtaja, mimi *with all honest issue* ya Dr. Ballali kwangu mimi hainipi raha sana.

Lakini naona kama vile pengine labda mnadhani kuna jambo hivi! Sasa ndiyo maana mwisho nikasema, labda muwafuate wale ndugu zake, ndugu wa Marehemu, mjaribu kuwahoji hivi kwa kila mbinu wawaambie, *why? What was the course of the death?* Labda watawaambieni. Lakini Serikali *honestly* mnatubana kwa jambo ambalo kidogo *I don't think that you are being fair to us (Makofi)*

Kwa Marehemu huyu, kwanza ameshakufa, hata mkionekana mnataka kwenda ku-*probe, unless it is a criminal, something* labda mnaweza mka-*manage.* Lakini hii tunayozugumza, aah, mimi hapana bwana. Sielewi hasa msingi wake unataka nini?

Kwa hiyo, nadhani kwa sasa Serikali haioni hasa kama kuna sababu ama za kuunda Kamati au nini, maadam suala la *EPA* linafanyiwa kazi, *some how* kama anahusika atakuwa – *involved* tu *and that only we shall do* ni kusema tunamwombea kwa Mwenyezi Mungu, *full stop.* Lakini haka kaagenda haka, mimi sijui bwana. Ila uzuri wajanja sana. Wanasukuma sukuma agenda hii, lakini hawasemi tatizo liko wapi. Nadhani wanajua kabisa kwamba ukisema kitu ambacho huna uhakika nacho, si tutakugeuzia kibao! Mimi nasema kama ushahidi *other than what we know, fine this state is there,* mnaweza mkauleta watu wakautazama. Lakini tusitafute kisingizio kwenye Serikali huku, hapana.

Mheshimiwa Naibu Spika, liko hili suala la Kiwira. Kiwira nalo limevaliwa njuga na rafiki yangu Mheshimiwa Dr. Slaa. Akianza kulisemea huyu Mzee, mpaka unaogopa. Sasa nimejaribu kuuliza nikamwambia Mheshimiwa Ngeleja *what do we do* na jambo hili? Wakaniletea malezo marefu, marefu kweli kweli! Haya, wakaleta dudu hili, wakasema litakusaidia. Nikamwambia aka mwenzangu, mimi siwezi kuingia kwenye jambo *partially technical* kama hili la kwako.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nilitaka niombe, sijui kama taratibu zinaruhusu, lakini nilidhani pengine ili kuwapa *a fair picture* ya hii Kiwira mnayoizungumza, labda mturuhusu tu *as a Government,* Waziri wa Nishati na Madini - Mheshimiwa Ngeleja aje na Kauli ya Serikali *at an appropriate time* kama ndani ya kipindi hiki kadri mtakavyoona inafaa, ili pengine aweze kupata muda wa kujaribu kulizungumza hili jambo kwa upana wake ili kama kuna jambo baada ya pale ndiyo tutajua wenzetu sasa *what is it. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini Kiwira ile wakati inakuwa *privatized, it was a dead animal to be frank. Machinery* zake zilikuwa zimeoza, ziko katika hatua mbaya sana. Kwa hiyo, wakati mwingine ni vizuri pengine mkapata mwanya wa kujaribu kupata ripoti ambayo itakuwa ya kina kidogo kwa njia ya kauli ya Serikali ili muweze kuwa na *benefit* kujaribu kuona mnafanya nini. Lakini kwa maelezo niliyonayo hapa, *it looks very smooth exercise* ina maelezo yanayoonyesha hali ya kiwanda ilivyokuwa na kwa hiyo, walichokuwa na i*nterest* nacho ni kupata mwekezaji afufue kiwanda, *full stop.* Ndiyo *effort* ambayo sasa hivi inafanyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kama utaruhusu hilo, naomba niishie hapa ili mpate *the more detailed document* ambayo itawasaidia kujua nini cha kufanya. *(Makofi)*

Liko lingine ambalo ingawa wenzangu wamelihamishia kwa Mheshimiwa Ngeleja, nimeona hapana, nisije nikamwonea mdogo wangu Mheshimiwa Ngeleja, ni hili MEREMETA. MEREMETA ina mlolongo wa vikampuni pale, Mwananchi, *Tangold,* una *Green Finance Company* mle ndani. Sasa nilikuwa najaribu kutazama Kanuni zetu nione wapi naweza nikaficha hili jambo. Maana hata kwenye Sheria sisi huwa siku zote kuna *lee-way* fulani. Sasa mle sikuona, lakini nikasema kwa mazingira ya jambo lenyewe, naomba niseme na mimi nina hakika hata Mheshimiwa Dr. Slaa analijua kwa kiasi fulani. Kwa maelezo niliyoyaona kwenye maelezo yake, anajua kabisa kwamba suala la MEREMETA limejikita ndani ya Jeshi la Wananchi wa Tanzania. Haukuwa mradi hivi mnaukuta uraiani huko ambako tungeweza tukasema jambo lolote tunalotaka kulisema, *this is a unique situation. (Makofi).*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nilitaka tu niseme, mimi kusimama hapa nianze kusema *this is what it was and this is what…,* hapana. Napata taabu, sitaweza. Sitaweza *for a simple reason* tu kwamba ni jambo ambalo lina uhusiano wa karibu sana na masuala ya ulinzi na usalama wa nchi yetu. Mengine yote niko radhi, ila kwa hili na kwa sababu nalijua na mimi, kwa kweli inafika mahali nasema hapana, nadhani iwe *protected* na tui-*protect* Serikali na tu-*protect* jambo hili ambalo linahusiana na ulinzi na usalama.

Sasa itakuwa ni juu ya Mheshimiwa Naibu Spika na Waheshimiwa Wabunge. Kama mtaona hiyo inatosha, vyema. Mkiona munisulubishe kwa sababu sijasema yote, *well and good* vilevile. Mimi nitakuwepo pale kwa ajili hiyo. Kwa kifupi naomba tu niseme hivyo kwa mazingira ambayo yanahusiana na jambo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme kidogo lingine la jumla ambalo sikutaka Maliasili wahangaike nalo sana. Utaona kwenye mjadala lilijitokeza suala la simba walawatu Manyoni. *It's a serious one, very very serious,* watu wanakamatwa *every now and then.* Sasa nikadhani hili si la kiutekelezaji tu, *actually* kama nchi, lazima tuwe *concerned* na jambo hili.

Kwa hiyo, nilitaka niliseme, *we are going to take action on this one.* Nitajaribu kuzungumza na Maliasili, tutajaribu ku-*reinforce* maaskari wa kutosha wa wanyamapori wajaribu kwenda Manyoni *Camp there for a while* kujaribu kutafuta hawa simba walawatu kwanini wanasababisha vifo vya watanzania wenzetu? Utakuta mara nyingi atakuwa ni simba mzee ama simba mwenye watoto. Mara nyingi ndio hawa wanaopenda kupata wanyama kwa urahisi na binadamu aki-*happen* kuwa *available,* masikini anapoteza maisha yake.

Sasa hili nadhani ni jambo kubwa *I have to do something,* lakini tuta-*connect* vilevile na maeneo mengine ambayo tunajua kuna hatari za wanyama hawa kama Bunda, najua Tunduru kule kwa sababu nilikwenda mwenyewe. Lakini nadhani *there is a need* ya kulitazama hili eneo kwa upana wake na tuone the *kind of action* ambayo tunaweza tukaichukua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ambalo sikutaka kuachia sana wenzangu wa Miundombinu ni Tabora *crisis,* maana naona mmeona mfululizo hapa na mimi nina hakika Tabora hawawezi kuniacha, watanikaba koo tu. Wanalalamikia barabara zote zinazoingia Tabora na kutoka kwamba jamani, yaani katika Mikoa yote mnayoiona ninyi, Tabora mmeona ndio mnyonge hata barabara moja ya lami wasiwe nayo! Sasa wengine wameiweka *in a very good way, politely,* wengine wakali, lakini *you can appreciate.*

Mheshimiwa Naibu Spika, nilitaka tu niseme kwamba *definitely* ni jambo ambalo hamuwezi mkalifanya dogo. *It's a concern* kwa wananchi wa Tabora na tuna kila sababu ya kulishughulikia.

Lakini nilitaka tu niseme kwamba ukienda kwenye Ilani ya Uchaguzi, maana ni lazima uanzie pale, utakuta barabara karibu zote wanazozitaja Wabunge wa Tabora, safari hii zote ziko kwenye *feasibility studies* pamoja na ile wanaita *detail design studies* kwa sababu ndiyo tulikuwa tumepangiana hivyo. Tulikuwa na barabara tumalize tulizozikuta kwenye awamu iliyopita, tuanze miradi mipya, halafu tu *take up* kundi la tatu la miradi ambalo tutakuwa tunakamilisha *study* zake. Sasa kama mlivyoona, nadhani wote walikuwa wanasema hapana Mzee, hatuwezi kufika 2010 bila barabara. Nami niseme nini? Maana kwenye bajeti, haikuwa imepangwa kwa maana hiyo, nayo ni ngumu vilevile. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sasa tunachoweza kusema ni kwamba ile barabara ya Kigoma – Kidahwe kilometa zile 30, nadhani wenzangu wa kigoma wanajua kwamba ujenzi pale unaendelea, hiyo barabara ina-*lead* kuja Tabora. Sasa Kidahwe – Uvinza pale tuna kilometa 130 na ni moja kati ya barabara ambayo chini ya Ilani ya *CCM* ile ibara ya 44(a) na yenyewe ilitakiwa kuja *by way of feasibility study.* Lakini pale tumebahatika,

angalau tumepata dola milioni 40 kutoka *Abudhabi Fund,* kwa hiyo, pale itatusaidia kidogo Kidahwe mpaka Uvinza.

Bahati nyingine, ni kwa sababu Malagarasi tunajua tayari imekuwa *taken up* na tumepeta fedha hizo kutoka *Korea Exim Bank.* Lakini *good enough* pale *on either side* ya *bridge* tuna kilometa 48 za lami. Kilometa 48 sio haba, maana ni zaidi ya hata ile ya Rukwa kwenye barabara yangu pale, nusu kilomita huku, nusu kilomita huku, haisaidii. Lakini hapa angalau sio mbaya sana. Kwa hiyo, baada ya hizo *approaches,* baada ya hicho kipande cha lami kuelekea Kaliuwa, Urambo na Tabora, huko ndiko kwenye *gape* kwa sababu hatuna *financing.* Walitenga tu shilingi bilioni mbili kwa ajili ya hiyo *feasibility study,* lakini wanaona pengine wazee mngeharakisha bwana Tabora hakukaliki huko. Halafu tena ile barabara ya Tabora – Itigi - Manyoni na yenyewe haina fedha kwa sababu iko bado kwenye utaratibu wa *feasibility study. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa tumejaribu kuzungumza na wenzetu Serikalini humu na kwa kweli tumepeana tu kazi kwamba hebu angalieni kama kutatokea pengine mfadhili mmoja alichelewa chelewa hivi ku-*submit* maombi yetu, akiyaleta, basi angalau tutafute barabara hata moja tu inayoingia Tabora, ama ya Nzega – Tabora ama ile nyingine… aah, *good news, that's very good.*

Nilikuwa nimeanza kuogopa, nisiliseme lakini hapa naambiwa leo asubuhi wameamua kutenga *ten billion* kwa ajili ya Tabora – Itigi. Kwa hiyo, angalau barabara moja inaweza kuwa *taken up* kutokana na nadhani hawa watakuwa ni wale *late bringers* wa fedha ambazo zinaingia pale. Kwa hiyo, tukipata hata hiyo, lakini mjue *ten billion* hazitoshi, lakini kwa kuanza, nadhani ni jambo jema kwa sababu inabakia ni deni kwa *financial year* inayokuja. Kwa hiyo, hizo ni jitihada ambazo nadhani zitasaidia kidogo kupunguza matatizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo naomba niseme, maana nalo hili lilijitokeza vilevile, ni suala la kiwanda cha Mgololo. Kiwanda cha Mgololo, nacho kilishafika mahali *almost* ilikuwa ni kama kimekufa tu.

Sasa nalo hili nadhani kidogo linataka maelezo mengi ili muweze kuona Serikali imefanya nini, kwa sababu ile *process* yote ya *privatization* mpaka inafika mwisho ni kweli kama alivyokuwa anasema Mheshimiwa Dr. Slaa. Unakuta sehemu nyingine unataka kujua, huyu mnayemwita, mbia huyu wa *zero zero zero point* ngapi, *what is this?* Huyo mwingine, Mzungu sijui wa wapi mwenye hisa zote hizi, huyu naye nani? Anaingiaje kwenye mradi kama huu? *It's a valid issue* ambayo inabidi mtu apate maelezo.

Kwa hiyo, nilikuwa nafikiri kwamba kwa hili tutamtaka Waziri wa Viwanda na Biashara, maana hata kwa majibu yake hawezi kulijibu hili kwa sababu linataka maelezo marefu kidogo. Kwa hiyo, nilikuwa naomba, kwa hili vilevile tuwatake tu watoe kauli moja Bungeni, itakayotoa ufafanuzi wa kina ili baada ya pale muweze kuwa na nafasi ya kuuliza vizuri zaidi kama bado kutakuwa na mapengo ambayo yanaonekena hayajajibika inavyotakiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, *RICHMOND* sina hakika kama nina haja ya kulieleza, lakini najua katika michango lilijitokeza. Nami naomba niendelee kusema kwamba *RICHMOND is a question of time* tu hapa Bungeni. Mimi nimeshajipanga *I am ready* kutoa maelezo ambayo yanaweza kusaidia kuonyesha tu *where we are* katika *process* ya ushauri ambao tulikuwa tumeupata kutoka Bunge letu la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Nilishamwomba Mheshimiwa Spika, wakati wowote aki-*feel* kwamba tutoe kauli, nitatoa tu kwa sababu ipo tayari na ina maelezo. Ila tu niseme kwamba kwa sababu majibu mengine ni *on going,* wanaendelea huko wananiletea wanaendelea huko wananiletea, lakini ni vizuri hata hapa nilipofika mkaambiwa, kwamba tumefika hapa ili iweze kuwasaidieni ni nini cha kufanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimalizie la mwisho. Sasa sijui kama nitalipata hapa! Liko suala moja ambalo nilikuwa nimeletewa mwishoni na Mama Kombani, ambalo nilifikiri nalo ni vizuri tukalisemea kidogo. Samahani sana, tatizo la wachangiaji wengi na mambo mengi, ndio hilo.

Haya kuna hoja ambayo ilitolewa na Mheshimiwa Godfrey Zambi, Mbozi Mashariki. Serikali kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu, inagharamia ujenzi wa Ofisi za Wabunge, hivyo Ofisi ya Waziri Mkuu, igharimie pia uendeshaji wa Ofisi hizo kwa chai kahawa na sukari. Haya bwana tunakubali. Bahati nzuri tulishalianza kidogo kidogo, kwa hiyo, tutajitahidi kuona *what we can put* kwenye Mikoa pale *in the mean time* wakati mambo yenyewe bado yanaendelea. Lakini tulishaanza Mkoa wa Mbeya, kwa mfano tumewatengea Shilingi milioni 14 pale na hiyo ni pesa kwa ajili ya kuhudumia ofisi za Wabunge wa Mkoa wa Mbeya.

Kwa hiyo, tutaangalia na Mikoa mingine tulikuwa tumepanga nini. Lakini hili nataka niseme *at the end of this all,* lazima turudi kwenye ule ule Muswada tuone namna utakavyo-*open up windows* za namna nzuri zaidi za kuweza kuwahudumia Waheshimiwa Wabunge. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Zambi, vilevile amesema ofisi za Wabunge zitajengwa katika Majimbo yapi kwa mwaka 2007/2008 na 2008/2009? Ni jambo la kweli kabisa, lazima tujue, sasa ngoja niwasomee kabisa maana sina namna nyingine.

*"Ofisi za Wabunge awamu ya kwanza 2007/2008 zitajengwa katika Majimbo yafuatayo kwa Tanzania Bara: Lulindi - Masasi, Kilwa Kusini, Mpanda Mashariki, Kalambo - Sumbawanga, Kigoma Kaskazini, Kasulu Magharibi, Buyuni - Kibondo, Mbinga Magharibi, Karagwe, Buchosa Sengerema, Busanda Geita, Busega - Magu, Bukene - Nzega, Urambo Mashariki, Iramba Magharibi, Ikungi - Singida, Msala - Kahama, Kisesa Meatu, Bagamoyo, Kibiti - Rufiji, Kondoa, Kibakwe - Mpwapwa, Bahi, Ulanga Magharibi, Mikumi - Kilosa, Morogoro, Rorya, Mbozi Magharibi, Itigi - Manyoni, Uyui - Tabora, Kwimba na Muleba."*

Haya ni Majimbo 32. Kwa upande wa Zanzibar, Majimbo yafuatayo yatahusika: Chaani Kaskazini, Donge Kaskazini 'B', Koani Kati, Makunduchi Kusini, Micheweni, Kojani, Chake Chake na Mkoani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mwaka 2008/2009, bado Majimbo hayajaainishwa. Maana yake ni nini? Maana yake ni kwamba awamu ya kwanza ni hiyo, inabidi kwenye awamu ya pili twende tena na vigezo vingine tuone namna ya kulifanya hilo. Kwa hiyo, tunaendelea ingawa *phace* kama mlivyoona hata kwenye taarifa yetu *it's not so encouraging.* Lakini hapo katikati ilibadilika baada ya kuonekana gharama zimepanda sana, *we need more money.* Lakini bado kuna *issue* ya ramani vilevile. Nadhani itabidi kui-*resolve* hii *issue* mapema ili tuweze kujua ni ramani gani hasa itumike na itazaa gharama kiasi gani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nitakuwa nimesahau jambo lingine, nitaomba radhi, lakini naomba nimalizie hili la mwisho. Kama nilivyozungumza hili la wanyama kama simba kule Manyoni, Tunduru na maeneo mengine, liko vilevile suala ambalo, haya nimekubali, nimesahihishwa jimbo linaitwa Buyungu Kibondo sio Buyuni. Haya nimekubali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hili jambo nalo kwa upande wa Mkoa wa Mara na *specifically* Tarime na Rorya, maana pale sasa ni Wilaya mbili, suala la usalama mpakani pale. *It is a very serious issue* na Serikali hatuna budi kuliona hili kwamba sio jambo ambalo linaweza likawa tena dogo. Sasa yako mawazo pale kwamba pengine iko haja kwa muda hivi pengine kutumia hata *beyond police* wa kawaida. Kwa sababu hawa wanaokuja kuvuka mpaka na kuanza kuiba mifugo yetu sio watu wanaokuja na mishale na mapanga hapana, wanakuja na bunduki tena bunduki kubwa. Sasa nikifika hapo huo si wizi tena wa kawaida.

Kwa hiyo, tumekubaliana kwamba tutajitahidi tutakaa chini na Mambo ya Ndani, tutajaribu vilevile kushirikisha na Jeshi tuone wanaweza kuwa na mawazo gani juu ya jambo hili, halafu *at the shortest possible time* tuone namna tunavyoweza tukaimarisha ulinzi pale mpakani ili kupunguza hii kero ambayo kwa kweli imezagaa na inasumbua sana Watanzania wengi pale mpakani. Kuja pale na kupora ng'ombe 300 sio jambo dogo! Maana yake ni kwamba umefanya kazi kubwa kweli kweli na kwamba uliowakuta pale wanyonge, wameshindwa kuhimili mapigo na sio ajabu wengi walikimbia tu wakaacha hilo jambo likawa limechukuliwa na watu wengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuyasema haya, naomba basi nirudie kukushukuru, niwashukuruni sana Waheshimiwa Wabunge, kwa ujumla wenu.

Ooh, kafanya vizuri sana huyu, sijui nani huyu, Mheshimiwa Mwanne? Nilitaka kusahau jambo moja kubwa, maadamu bado nina muda, naomba nizungumzie suala la *TRL.* Kampuni ya Reli ambayo imebinafsishwa sio muda mrefu na namna inavyotoa huduma na matatizo ambayo Watanzania sasa wanayapata kutokana na hiyo huduma

inayotolewa imeleta matatizo makubwa sana. Sasa wakati mwingine labda ni kusema tu yale ambayo yatasaidia mkajua *situation* ikoje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kampuni ya *RITES* ndiyo iliyopewa hilo jukumu la kuendesha reli hii. Imepewa hiyo kazi mwaka jana na tuliwaambia *don't worry* nyie watu wa *TRL,* mkija hapa mambo bomba. Tuna vichwa vya treni zaidi ya 90 na wakasema hata mabehewa yako, unajua vitu vingine hivi tunajiponza sisi wenyewe tu. Siku ile nimekwenda kuzungumza na wafanyakazi pale *I was shocked,* kwamba *what was found here* ilikuwa ni *engine* 50 badala ya zile zilizokuwa zimetajwa kwenye maelezo. Sasa kosa ni la nani? *The whole study* inakuwa *based on a wrong basis,* lakini tukasema potelea mbali tutajitahidi, poeni. Hawa walitakiwa wapate mkopo kutoka *IFC,* masharti wala hayakuwa makubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza walitaka tufungue *some kind of an account* hivi, tu-*deposit* pale kama *two million US Dollars* kuonyesha *seriousness* kwa upande wa Serikali. Nami nikasema, *why didn't we do that?* Sharti la pili ilikuwa ni kupata maoni ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ili ule mkopo wa *over 30 million US Dollars* uweze kutoka. Wenzangu Waheshimiwa Wabunge, mambo mengine haya tunatafuta wachawi, lakini wachawi wakati mwingine ni sisi wenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa *what happened* katika *situation* ile? Kule kuja kupata hiyo *AG's opinion,* ile *document* ilipopelekwa pale Hazina ili ipate baraka zile za kiuchumi baadaye ije kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali, *it took more than three months. Yes!* Ndio ikaja kwa ndugu yangu hapa Mheshimiwa Mwanyika – Mwanasheria Mkuu wa Serikali, ndio akaitoa haraka haraka juzi ndio wamekubali watu wa *IFC.* Wametoa mkupuo wa kwanza wa dola milioni 14 ili zikawekezwe sasa kwenye yale maeneo ambayo tungekuwa tumeshapata vichwa na mabehewa na *spare parts.*

Kwa hiyo, tuna *14 million US Dollars* ndio zimekwenda kwa wale *suppliers.* Lakini *this thing could have been done much earlier* bila wasiwasi. Kwa hiyo, wakati mwingine sijui ni mambo mengi au ndio ile tuliyoulizwa huko nyuma, lakini *it's an area that we need to look into. Speed* yetu ya kufanya maamuzi wakati mwingine inahitaji mambo mengi ya msingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeshapata *opinion* ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, *fine,* lakini Mheshimiwa Rais alipokuwa India ni juzi au hivi karibuni, amekutana na Waziri Mkuu pale, Waziri Mkuu akaelezwa tatizo akasema tunaweza kuisaidia Tanzania kupata nguvu kubwa yaku-*speed up* namna yaku- *revamp* hiyo reli *(Makofi).*

Mheshimiwa Naibu Spika, walikuwa tayari wame-*offer* nadhani kama dola 47,000,000. Tulichoambiwa tufanye sisi ni kupeleka tu hiyo *formal request* kupitia kwa Balozi wao hapa Dar es Salaam, basi hicho tu. Juzi amekuja huyu Mwakilishi wa Rais, yule *Chairman* wao walikuja na rafiki yangu, Juma Kaboyonga *in my Office* na yule meneja wananiambia *PM,* tunakuomba usukume hiyo barua iende kwa Balozi wa India.

Sasa huyu sitaki kumtetea maana mimi sina *interest* pale ya namna yoyote. Lakini ninachotaka kusema katika mazingira haya na mnataka tum-*condemn* huyu *TRL* wa sasa. Mimi nadhani tungeanza na hawa hawa wanaotucheleweshea mambo yasiende vizuri. Kwa hiyo, nimeagiza juzi kwamba jamani kaeni kwenye Bodi yenu, nadhani walikutana jana, nikawaambia kaeni, *make this formally to the Ministry* ya Miundombinu *and I want a copy* ili nione, hivi wewe unaambiwa lete tu ombi, unapata taabu gani wewe Mtanzania?

*I hope I will get that letter* mapema ili tuweze ku-*deal* nayo. Kwa hiyo, hilo tuta-*deal* nalo hivyo. Lakini *in the mean time* nai-*appreciate,* ila tatizo ninaloliona pale ni kubwa sana, mabehewa hayatoshi, na kweli hayatoshi. Sasa juzi niliwaambia baadhi ya watu kwamba jamani hebu tuvute subira, *may be with a $ 14,000,000* na huyu baba wa India aki-*offload* hizo *may be* tunaweza tuka-*speed up* tukapata kitu kizuri.

Lakini vilevile nilikuwa nimeagiza tuunde Kamati ndogo pale ambayo iliundwa nikawaambia kaeni chini, hebu pitieni huo mkataba wenyewe, *see if you are comfortable with it.* Kazi hiyo kama wameimaliza, lakini sijapata *feedback.* Lakini najua walikuwa wameanza kuifanya. Nilitaka nijiridhishe tu kama kweli jambo hilo linakwenda vizuri au hapana. Kwa hiyo, hili la reli tunaendelea kulishughulikia na ninafikiri tutalimaliza. *(Makofi/Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine jamani ni daraja la Kigamboni. Daraja la Kigamboni nalo, wakati mwingine ukiwa Serikalini vingine unaona aibu hata kusema sema hivi. Lakini nalo tumechelewa chelewa ni sisi wenyewe tu. Lakini niseme tu la uhakika kwamba walikuja kuniona juzi *NSSF,* Wizara ya Miundombinu kupitia Katibu Mkuu wake, pamoja na Waziri wa Kazi Maendeleo ya Vijana, tumezungumza.

Mheshimiwa Naibu Spika, *issue* pale wala sio kubwa kwa sababu hata kwenye ilani lilishasemwa tayari kwamba *NSSF* ndio watakaosimamia zoezi zima la kujenga daraja la Kigamboni. Kitu kinachotakiwa pale ni kuiambia *NSSF go ahead* ili uweze kutuletea sasa orodha ya watu ambao unasema baada ya kutangaza tumewapata hawa, wamechujwa, *these are the names* ambao tunafikiri wanaweza wakatusaidia, *just that.*

Kwa hiyo, jana waliponiona hapa nikasema bwana we ngoja mimi nijaribu kutafuta *shortcut.* Kwa hiyo, nimemwomba Rais, nimemwandikia dokezo kumsihi tu kwa sababu jambo lenyewe halina utata mkubwa. Nakubali tuwape *go ahead* waka-*process* hilo jambo ili *process* ianze. Kwa hiyo, mimi naamini nalo tutalifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, *feasibility study* zile zilizofanyika zinasema mpango huo *economically* ni *viable* kabisa wala hawana tatizo katika hili. *TPA* wanamezea sana mate kwamba tupeni sisi kama ninyi mnaona mnachelewa. Lakini *TPA, NSSF* wote wetu na pengine tulidhani *NSSF* pengine anaweza akasaidia zaidi. Kwa hiyo, tutangoja kidogo, lakini *we are pushing it* ili tuweze kupata maamuzi ya msingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi vikaratasi vya mwisho, univumilie. Haya, liko suala la maji, sijui ndio la mwisho hili? Hili la maji naomba nimuachie Waziri wa Maji

na Umwagiliaji, atakuwa na mambo mengi ya kueleza. Mimi niseme tu mtazamo wangu kama mmoja wa viongozi Serikalini kwa maana ya kukubaliana na Waheshimiwa Wabunge, kwamba ni kweli eneo la maji linahitaji msukumo mkubwa kabisa. Ni vizuri vile vile tukasema hata hizi taratibu zetu za namna ya kuchimba visima, maana wote tumeathirika, hata mimi nimekubwa na jambo hilo, *process* yake ni ndefu sana na wenye vitendea kazi vya kuweza kutawanya kuchimba visima nchi nzima nao hawapo wa kutosha. Ni jambo ambalo lazima tuliangalie tuone *what do we do.*

Lakini liko ombi la jumla ambalo nimelipata kutoka kwenu katika michango kwamba *for the next financial year,* hebu tujiulize kama maji hayawezi kuwa *uplifted* yakapata *priority* kubwa zaidi kutokana na fedha zetu wenyewe, badala pengine ya kutegemea hawa wakubwa kutoka nje! Mimi nadhani ni jambo zuri na ni jambo la msingi kabisa. Maji ni ajenda moja kubwa sana, naamini tutalipa uzito unaostahili ili tuweze kuwa na kitu cha kusema. Maana vinginevyo Mheshimwia Dr. Slaa pale akija Jimboni kwangu, taabu! Kwa hiyo, lazima tujitahidi sana tuone ni nini la kufanya. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, liko suala lingine hapa ambalo nimeombwa. Sasa hili na mimi linanigusa, kwa hiyo ni lazima ku-*declare interest* mapema. Tuna barabara ambayo inatoka Nyakanazi ambayo inatuunganisha na ile *central corridor.* Inakuja Kigoma, ukitoka nayo pale ukute ndege, basi ikurushe ikulete Dar es Salaam, ukisema unatembea kwa gari mpaka Dar es Salaam utaipata joto ya jiwe. Kwa hiyo, tunachojaribu kusema pale ni nini?

Kwanza ni kufanya jitihada za kuimarisha reli, lakini lazima vilevile tutazame kiwanja kile cha Kigoma, kama mnataka mambo haya yaende vizuri. Maana ukiwa na *facility* hiyo ya barabara ya lami ya kwamba utajaribu kuipitisha Tabora na mkawa angalau na ndege za uhakika, kidogo adha ya reli inaweza ikapungua. Kwa hiyo, itabidi nasi tuendelee kulisukuma hili kwa kadiri itakavyowezekana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Mabina na Mzee wa Misungwi, maji yenu nimeyasikia na mimi. Nilisikia jana na juzi wakati mnasema lakini siwezi kulisemea kwa sababu linaji-*focus* zaidi kwenye miradi ambayo iko chini ya Wilaya ya Misungwi pamoja na hiyo ya Geita. Lakini nadhani Waziri atakapokuja kutoa hoja zake, basi ni vizuri tuone katika eneo hilo atatusaidiaje ili tuweze ku-*make some progress*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ambalo hatuwezi kuacha kulisemea ni Simanjiro. Simanjiro, mimi kwasababu nimekwenda pale, maana matatizo ya maji tunayo kila mahali, lakini *what I saw in Simanjiro* pale Orkesbet, inatisha kabisa. Hawana maji ya uhakika! Nilipokwenda pale ndio nikaambiwa twende tukupeleke kwenye kisima ambacho ng'ombe wanakunywa maji. Nilidhani kisima hivi cha maana maana hivi. Wakanipeleka *not far from the town area.* Sio kisima kile!

Mheshimiwa Naibu Spika, Watanzania pale wamejitahidi, wamechimba shimo refu sana kwenda chini ndio wanatega maji ya mvua na kidogo mengine yanatoka

ardhini. Ng'ombe wote wanaingia pale kwa foleni, kwa sabau ile *room* ni ndogo sana na kuna kupeana zamu. Sasa nikasema, kwa Simanjiro kwa kweli *something must be done.*

Nafikiri tutaliangalia tuone *what we can do.* Tulijaribu ku-*save a little bit of some money* kwaajili ya Simanjiro pale lakini itajikita zaidi kwenye *feasibility study* kwa maana ya kui-*up-grade* kuifanya iwe *modern* zaidi tuone gharama za sasa zitakuwaje. Lakini kwa kweli pana tatizo kubwa. Naamini tutayakabili yote haya kwa kadiri itakavyowezekana. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema haya, naomba basi nimalizie tu kwamba nawashukuru sana kwa michango yenu mizuri. *We are sorry* kwa yale ambayo pengine hatukuyasema sema hapo kwa sababu hatukupata muda wa kutosha, tutayazingatia *in the process* ya utumishi na utendaji wetu wa kazi kwa karibu kabisa ili tuweze wote kwa pamoja kufanikisha kazi iliyo mbele yetu kutekeleza ilani ya Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, mtakubaliana na mimi kwamba Mheshimiwa Waziri Mkuu, amejitahidi sana kujaribu kuingia kwa undani sana kwenye hoja ambazo mmekuwa mmezizungumza, lakini hiyo haiondoi kwamba tukirudi tutaingia kwenye fungu baada ya kifungu.

Sasa kuna mambo ambayo ningependa kuyaweleza kwanza. Hili suala la *TRL* kulikuwa na hoja ambayo ilitolewa na Mheshimiwa Arfi, katika Bunge la Kumi na Mbili, April 2008 nadhani Serikali bado mnatakiwa kujibu utekelezaji wa hoja yake. Bado hiyo haiwezi kuwa imejibiwa saa hizi, inatakiwa kujibiwa rasmi. Kwa hiyo, wanaohusika mjue kuwa mnatakiwa kujibu rasmi hoja ile ya Mheshimiwa Mbunge. Kwa hiyo, mtaeleza yote hayo katika maelezo yake.

Lakini ya pili, Mheshimiwa Waziri Mkuu, alipozungumza, aliuliza kama suala la Kiwira, linaweza kuja kwenye kauli za Mawaziri. Ndiyo! Hiyo ni utaratibu kabisa ambao utakuwa umeandikwa vizuri na kwa muda unaokubalika na na kwa ushahidi wote unaostahili, inaweza kuja kwa utaratibu wa Kanuni zetu. Ni kitu ambacho kinaweza kuingia mara baada ya maswali kuulizwa, wakati wote hiki kipindi ni cha kauli za Mawaziri. Lakini mnatoa taarifa mapema kwa Spika, halafu iwe imeandikwa na inasomwa kama ilivyoandikwa na kusambazwa kwa Wabunge kama inavyostahili. Hiyo ni Kanuni.

Lakini wakati huo huo tunayo sheria Na.3 ya mwaka 1988 inayohusu haki, kinga na madaraka ya Bunge. Sheria hiyo inasema: *"Si ruhusa kuongelea mambo ya ulinzi na usalama, labda kama Rais, ataridhia kwa maandishi."* Kwa hiyo, hiyo sheria mtaisoma.

Baada ya kusema haya, kwa sababu muda wetu umefika, tunakushukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu, hukuzidisha muda, tutarudi mchana. Ni mategemeo yangu kwamba Waheshimiwa Wabunge, mtakuwa na vile vitabu vyote vinavyohusika na kazi ya leo. Kuna kitabu cha pili, kuna kitabu cha tatu na nafikiri na cha nne. Nategemea mtakuwanavyo.

Nisingependa kuona Waheshimiwa Wabunge wakisema ndiyoo! Ndiyoo! Ndiyoo! Wala mtu hasomi, anaweza kuzunguka kwenye kiti anasema ndiyo, ndiyo, aah! Huo siyo mradi wa hapa. Vitabu hivyo kila Mbunge anavyo na tunashauri kwamba vibakie hapa Bungeni, kipindi chote cha miezi miwili tutakayokuwepo kwasababu kila siku tutakuwa tunavipitia vile vitabu.

Kwa hiyo, nategemea mchana mnakuja navyo na wale watakaokuwa na hoja yoyote ile wajiandae vizuri, tutakapofika nitawakumbusha kuhusu kanuni zinazohusika, nitazitumia vizuri. Nami nakwenda ku-*refresh* sasa hivi. Nitazitumia vizuri sana. Kwa hiyo, tusigombane hapo. *(Makofi/Kicheko)*

Baada ya kusema hayo, nasitisha shughuli za Bunge mpaka saa 11:00 jioni.

*(Saa 07:03 mchana Bunge lilifungwa mpaka saa 11:00 jioni)*

*(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)*

**NAIBU SPIKA:** Tulimaliza Shughuli za Bunge kwa maana ya kujibu maswali ambayo Mheshimiwa mtoa hoja alikuwa ameulizwa na kutoa ufafanuzi. Sasa hatua tunayokuja nayo ni ile ya kuingia kwenye kujadili kwa maana ya kupitisha bajeti kwa Kamati ya Matumizi. Sasa zoezi hili linatawaliwa na Kanuni kuanzia ya 100 mpaka Kanuni ya 106. Kanuni ya 100 inatueleza kwamba tutapitia Kifungu hadi Kifungu na kila Kifungu kwa Kanuni ya 101 kitapitiwa kwa kupigiwa kura.

Sasa kuna kazi mbili hapa tunazozifanya. Kwa mfano, uchukue hii hotuba ya Waziri Mkuu ina mafungu zaidi ya sita. Sasa kuna fungu moja, ni la Ofisi yake kama Waziri Mkuu. Pale hamuulizi swali ile mnayosema kufanya lolote. Fungu 37 mnaweza kuingia kwenye mshahara kwa sababu hilo ndio fungu la kazi. Halafu kuna fungu lingine la TAMISEMI, pale mnaweza pia kushughulika na kutoa mshahara wa Waziri. Sasa mshahara wa Waziri, Waheshimiwa siyo kila kitu utasema, pale unatakiwa kwa mujibu wa kifungu hiki ni kwamba, kifungu cha 101 (3) Mbunge atakayeamua kutumia kifungu chenye mshahara wa Waziri ataruhusiwa tu iwapo ataomba ufafanuzi wa suala mahsusi la kisera na atazungumzia zaidi ya mambo mawili ya aina hiyo.

Sasa hapa kuna mambo mengine ni ya kisera tu, huwezi kusema una fungu fulani utamwuliza, halipo, lakini kisera tu. Mambo ya kisera pale mtaweza kusema mambo yote ya sera. Wengi wanachanganya, kuna mambo ya maendeleo, kipo kitabu cha mafungu ya maendeleo, kule katika kifungu cha maendeleo unaweza kushughulika na miradi. Huo mradi wako kama haupo, tena huwezi kutuambia sisi tuweke pale, hatuwezi. Sana sana unaweza kuzungumzia ubora, udhaifu wa utekelezaji, sana sana unaweza kusema, lakini

wakati fulani niliahidiwa hivi, lakini kwamba utapewa fedha kwamba sasa itaingia, haitaingia, kwa hiyo, mradi inakwenda kule kwenye kitabu cha nne.

Halafu kuna zoezi lingine sasa la kutoa shilingi. Suala la kutoa shilingi kwa kweli ni hoja, utoaji wa shilingi ni hoja kabisa. Kwa hiyo, Mbunge anatoa shilingi kusudi aweze kueleza kwa urefu zaidi kuhusu jambo lile analotaka tumwelewe na sisi wote tutaacha kazi nyingine tutamsikiliza yeye. Yule anayetoa shilingi akishajieleza, ni ruhusa kuungwa mkono na watu kwa mjadala.

Kama mtu katoa habari fulani na mwingine anafikiri anataka kumsaidia yule kumchangia au kusema sivyo, mnaruhusiwa kujadili. Mtoa shilingi atapata dakika tano, wengine watakaokuwa wanamsaidia kujadili ni dakika tatu. Baada ya mjadala huo tutaendeleza huo mjadala, halafu tutamwita mtu kutoka Serikalini, Waziri wa Serikali ajibu hoja zile zilizotolewa na wote wengine. Baada ya hapo, ni yule mtoa shilingi ndio atakayefunga mjadala. Akishafunga mjadala, yule aliyetoa shilingi kama hakuondoa shilingi yake, basi itabidi tupige kura. Tukipiga kura, ikatokea kwamba ile kura imeshinda, basi tutaendelea na vifungu vingine huku tukiwa tunasema leo bajeti imepita bila shilingi moja. Kama mtoa shilingi kashindwa, basi tunaendelea na safari.

Sasa maana ya kwamba bajeti ya Waziri fulani imetoka bila shilingi, siyo kwamba haitaendelea, lakini ni dalili ya kuonyesha kwamba kuna kasoro katika utendaji wa kazi katika Wizara ile. Ni *implication* kubwa, inaonyesha kasoro kwamba kuna walakini kidogo. Zikitoka shilingi kama nyingi nyingi, hapo kwa kweli mara nyingine inakuwa tena hata aliyemchagua atakuwa hana imani na huyu ndugu.

Kwa hiyo, tumesema kwamba katika kutoa fungu ni dakika tano, kwa wale watakaochangia hoja, aliyetoa shilingi ni dakika tatu. Kama utaomba ufafanuzi wa kawaida, tutakuruhusu mara mbili tu unatoa ya kwanza wanakujibu, unatoa ya pili wanakujibu, baada ya hapo, hutaruhusiwa. Haya ni kwa mujibu wa Kanuni zote tulizonazo hapa. Kwa hiyo, naomba msome hizo Kanuni na mfuate. Tutakwenda taratibu ili kuruhusu nafasi.

## KAMATI YA MATUMIZI

## MATUMIZI YA KAWAIDA

**MWENYEKITI:** Tutakapofika katika Mikoa tutakwenda Mkoa kwa Mkoa kwa maana ya fungu la Mkoa kwa Mkoa, vinginevyo tutalala humu humu.

### Fungu 25 – Waziri Mkuu

Kifungu 1001 – *Administration and General*. ... Tshs. 3,280,014,000/=

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 27 – Msajili wa Vyama vya Siasa**

Kifungu 1001 – *Admistration and General* ... Tshs. 19,901,907,000/=

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 37 – Ofisi ya Waziri Mkuu**

Kifungu 1001 – *Administration and General*... ... Tsh.6,338,480,900/=

**MWENYEKITI:** Tutapata majina ya wote, Mheshimiwa *Dr*. Wilbrod Slaa, Mheshimiwa *Dr*. Zainab Gama, Mheshimiwa Juma Killimbah, Mheshimiwa Jacob Shibiliti, Mheshimiwa John Cheyo, Mheshimiwa Vedastus Manyinyi, Mheshimiwa Mohamed Mnyaa, Mheshimiwa Shoka Khamis, Mheshimiwa Omar Kwaangw', Mheshimiwa Salim, Mheshimiwa Issa, Mheshimiwa Manju Msambya, Mheshimiwa Lucas Selelii, tunaanza na Mheshimiwa *Dr*. Wilbrod Slaa, siyo kama nimewaita, nitafuata hivyo hivyo nitawachanganya tu.

**MHE. DR. WILBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, niko kwenye *Vote* 37, *program* ya 10 *Sub-vote* 1001, *Sub-vote* ndogo zaidi 250100 - Mshahara wa Waziri. Sijui kama ndio Waziri Mkuu lakini ndio mshahara wa Waziri. Mheshimiwa Waziri Mkuu asiwe na wasiwasi sina shida sana na mshahara wake baada ya majibu aliyoyatoa, tena kwa ustaarabu mkubwa, sina nia ya kukamata shilingi, lakini naomba nipate ufafanuzi. *(Makofi)*

Kimsingi, Waziri Mkuu ninakubaliana na majibu kama alivyosema atapeleka masuala kama ya *EPA* na nini kwenye Kamati ya Uongozi ya Bunge. Nakubaliana na ninadhani basi, tutafuata katika *line* hiyo. Lakini nilipenda niweke rekodi tu vizuri kwamba katika masuala ya *MEREMETA* na *TANGOLD* japo ilikuwa imepewa Jeshi MEREMETA na Waziri Mkuu anisaidie kama hilo siyo sahihi.

Suala la MEREMETA kuchimba madini pamoja na kwamba inachimbwa na Jeshi la Wananchi, haiwezi kufanana na wala kulinganishwa na siri za Jeshi. Kwa hiyo, kunapokuwa na ubadhilifu ambao ndio jambo tunalofuatilia tutategemea Serikali itupe majibu. Sasa kama kuna kitu ambacho kinataka usiri katika hiyo, ndio maana nilisema kwamba tunaruhusu tuko tayari, tutakubali kujadili kwenye Kamati ya Bunge. Lakini nilitaka kuweka rekodi tu kwamba katika suala tunalozungumzia hatuzungumzii mambo na utendaji wa Jeshi, tunazungumzia ubadhirifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa suala ambalo ninataka nipate ufafanuzi wa kina, nilikuwa nimemwandikia Mheshimiwa Waziri Mkuu katika mchango wa maandishi, yeye hakujibu, alijibu Mheshimiwa Marmo, ni kuhusu kinachoitwa nyaraka nyeti za Serikali na kwamba Wabunge wanatembea na hizo nyaraka nyeti za Serikali na mimi ni mmojawapo na sihitaji kuzificha, ziko hapa. Kwa hiyo, kama Mheshimiwa Marmo yuko

tayari kuagiza Polisi kesho, niko tayari, nitakamatwa na niko tayari nikamatwe, lakini nataka kusema nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachotaka kusema na ambalo naomba Mheshimiwa Waziri Mkuu anisaidie, kwa sababu ni suala la sera, hivi ni kweli kwamba panapokuwa na nyaraka za Serikali kimsingi zinaonyesha kabisa ubadhirifu, wizi, mkataba mbovu, bado ikapigwa mhuri wa siri na ikaitwa kwamba ni nyaraka nyeti na kwa hiyo, watu wasipate? Nilitaka ufafanuzi wa hilo, wa kina, kwa sababu ninaamini hata mbele ya Mwenyezi Mungu ukificha kitu hicho wewe mtumishi wa Serikali mbele ya Mungu utakuwa pia na dhambi kwa sababu wizi hauwezi kuhalalishwa kwa usiri, ubadhilifu hauwezi kuhalalishwa kwa usiri, matumizi mabovu ya rasilimali ya Taifa hayawezi kuhalalishwa kwa usiri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa Waziri Mkuu anisaidie, mimi ninafahamu ile sheria, ninaifahamu *classify documents:* Je, nyaraka hizi za fedha, mikataba iko kwenye sehemu ya *classify documents?* Kama nimeomba kwa njia ya kawaida sipewi, ninaomba Serikali, sipati; Watanzania wenye dhamira safi wanasema hii hapa. Hivi kweli katika hatua hiyo tutaziitaje kwamba ni nyaraka nyeti? Naomba jibu la ufafanuzi katika hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru.

**NAIBU SPIKA:** Upande wa Serikali, Waziri Mkuu au Waziri wa Nchi.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba nitoe maelezo machache kuhusu masuala ya ndugu yangu Mheshimiwa *Dr.* Wilbrod Slaa kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza suala la siri ya Serikali haihitaji maelezo ya kina, lakini dosari iliyopo au mapungufu yaliyoko hapa kwenye Kanuni yetu, Kanuni zetu hazisemi wazi nyaraka zipi za siri za Serikali zinazojadiliwa Bungeni moja kwa moja.

Kwa hiyo, hapa ni busara ya Spika na mila na desturi ya Mabunge mbalimbali duniani. Sisi ni wajumbe wa *Commonwealth* (Jumuiya ya Madola). Katika Jumuiya ya Madola, *information* yoyote ambayo ni *classified,* haijadiliwi Bungeni. Sasa utapiga mstari wapi? Sasa hii inategemeana na busara ya anayehusika na kwa kweli katika nchi yetu tumetumia busara sana katika kuvumilia nyaraka nyingi ambazo zinaletwa hapa Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi wengine ambao ni Wakatoliki tunajua siri maana yake ni nini. Mapadre wanajua siri maana yake ni nini. Lakini *Dr.* Wilbrod Slaa ameonyesha nyaraka nyingi sana hapa, lakini ni mjanja kweli kweli kwa sababu anafahamu kwamba anavunja sheria na kwa vile anavunja sheria, huwa anajikinga sana. Mfano mmoja ni taarifa ya Kikao cha Bodi ya Benki Kuu iliyofanyika tarehe sita mwezi huu, sijui alipataje nyaraka zile za siri za Benki Kuu na ni kikao kizito sana kilichokuwa

kinajadili taarifa nzito sana za ndani ya Benki Kuu. Lakini amekata maeneo yote, amekata kila upande wala hujui imetoka wapi na wala hakuna mhuri wa siri, isipokuwa anamwandikia rafiki yake mmoja *NB,* tafadhali nimeondoa *source* kwa usalama wa maofisa wetu. *(Makofi)*

Nirudie, anasema nimeondoa *source* kwa usalama wa maofisa wetu, inaonekana hawa watu hata wana maofisa wao, sijui ndio maofisa wa *CHADEMA* au maofisa wao ndani ya Benki Kuu au ndani ya Serikali, lakini hii yote ni kuficha kwamba kuna jinai hapa. Kuna makosa ya jinai hapa!

Kwa hiyo, wala Mheshimiwa *Dr*. Wilbrod Slaa hastahili kufundishwa nini nyaraka ya siri au zikiwa siri kwa sababu mwenyewe anaelewa ndio maana huwa anakata kila wakati sehemu zote. Hapa ametuthibitishia kabisa kwamba kwa kikao kile cha Bodi ya Benki Kuu ya tarehe sita ameondoa *source* kwa usalama wa maofisa wetu, anajua kwamba lazima wawe salama kwa sababu wanavunja sheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa haitaji kufundishwa nini maana ya siri. Lakini duniani kote mimi sijasikia Wabunge wanavua nchi yao ikawa uchi kabisa, sijawahi kusikia. Nenda Uingereza, nenda Canada, nenda Marekani, nenda Australia, bahati mbaya Mheshimiwa Ndesamburo hayupo. Juzi tulikuwa Australia, Waziri wa Fedha akishasema kwamba hii ni *classified information,* Spika, Mwenyekiti hana namna tena na wote tena wapinzani kule ni wengi zaidi kuliko hapa, wote wanakubaliana kwa manufaa na kwa uzalendo wa nchi yao na inakuwa ndio mwisho. *(Makofi)*

Kwa hiyo, mimi bado ninaamini sisi kama Bunge ambalo ni mwanachama wa *CPA*, mwanachama CCM, Mwanachama wa Jumuiya ya Madola, nadhani wakati umefika sasa tuanze kuzingatia *precedence* ya kwamba *classified documents* zijadiliwe Bungeni. Bado ninarejea, Mheshimiwa Mbunge yeyote hasa Mheshimiwa *Dr*. Wilbrod Slaa ambaye ametuthibitishia hapa anayefahamu kabisa kwamba ni kosa la jinai kulea nyaraka hizi hapa, hata kidogo hataki kufundishwa, hastahili kufundishwa nyaraka zipi ni za siri na hazitakiwi zijadiliwe wazi Bungeni hapa kwa sababu Bunge hili linasikilizwa na linaangaliwa siyo tu nchini Tanzania, bali duniani kote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. DR. WILBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nafikiri amenichokoza zaidi. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwamba Mheshimiwa Marmo amenukuu na waraka wa mwisho niliompatia ni wa tarehe 6 Juni, Watanzania wenye dhamira safi wanasema kwamba waraka huu unaeleza kitendo ambacho kimefanyika kinahusu *EPA* ambayo hata Kamati ya Mwanyika haikupewa, kuna ubadhirifu zaidi katika *EPA* kwenye ukaguzi wa mwaka 2006/2007 kwa kuwa ameisema ninaisema mimi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kama haikupelekwa na mfumo wa Serikali ukianguka na ndio maana nimesema hakuna cha siri tena kwenye nyaraka za aina hiyo, kwa sababu mfumo wa Serikali ukishaanguka, njia za kawaida za kusaidia Serikali

zitatafutwa. Ndio maana nasema ni vyema wala nilipoiondoa haina maana ya kwamba nilikuwa sijui kwamba ni jinai au sio jinai.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakuna jinai pale isipokuwa watu wetu wangenyanyasika na nimeondoa na itakapotakiwa, ninatoa na popote pale itakapotakiwa, akitaka Waziri Mkuu, akitaka Mwanasheria Mkuu nitampa, lakini inapoanguka *system* ya Serikali ndio sababu hizi nyaraka zinatoka. Tulichoomba asubuhi kwa ufafanuzi ni kwamba, tusaidieni ni namna gani taarifa hizi zinapotoka zifanyiwe kazi na zikifanyiwa kazi sisi wazalendo, hata sisi tunajua kwamba ile ambayo haitaki kwenda hadharani, hatutatoa, lakini kama haifanyiwi kazi, mambo yanafichwa, Taifa linaumia hatutakaa kimya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, katika Bunge la mfumo wa Vyama vingi duniani kote na hasa Jumuiya ya Madola, tunazo Kamati tatu ambazo kwa makusudi zinaongozwa na Upinzani, ni Kamati ya Mashirika ya Umma, Kamati ya Hesabu za Serikali na Kamati ya Hesabu za Serikali za Mitaa. Sababu yake ni kwamba hawa wawe na uwezo wa kihalali wa kufikia mambo fulani fulani ndani ya vyombo vinavyohusika. Tunasema utaratibu ulio halali wa kufikia vitu fulani fulani kwa mfano anaweza huyo mtu wenu akapiga hadithi huko akasema bwana kule kitu fulani fulani, kwa kweli Kamati haizuii kwenda kuandika barua na kusema tunahitaji *document* ya namna hii inayofanana na hii, wakapewa kwa utaratibu unaohusika.

Kwa hiyo, hiyo ndio njia mojawapo ya kuweza kutengeneza Serikali ibakie katika utaratibu wake, lakini bado Wabunge na wananchi wasikose kujua maovu yanayotendeka ndani, huo ndio utaratibu. Lakini wakati huo huo, basi na ndani ya Serikali lipo tatizo, kwa hiyo, inabidi pia na nadhani Waziri Mkuu kwa sababu wewe ni Msimamizi Mkuu wa Serikali ndani ya Serikali, halipo tatizo. Kwa hiyo, sio kwamba tusilete, ni watu kwa sababu kama ilivyoelezwa, nchi yoyote heshima yake ni siri zake zinazokuwa zinasimamiwa kwa utaratibu unaohusika. Kwa hiyo, hili nadhani tunaendelea, kwa maana hiyo tumemaliza. Sasa tunakuja kwa Mheshimiwa *Dr*. Zainab Gama.

**MHE. DR. ZAINAB A. GAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. *Vote* 37 *Program* ya 10 *Sub-vote* 1001 *item* 250100 - Mshahara wa Waziri.

**MWENYEKITI:** Tupunguze muda kwa kurudia *item*, tuko katika *vote* hiyo hiyo.

**MHE. DR. ZAINAB A. GAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri Mkuu alipokuwa anajaribu kujibu hoja za Waheshimiwa Wabunge, aliionyesha ilani, akaonyesha kipengele Na.120 na akasema ilani ile iliahidi kwamba wanawake watafikia asilimia 50 kwa 50 na mimi ninaomba *specifically* nizungumze ndani ya Bunge, ninaamini ilani ile ilifanywa na wataalam wenye kujua na ikashawishi wanawake wengi wakaipigia kura CCM. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini katika maelezo yake hakueleza utekelezaji huo ikifika 2010 itakuwaje. Imeelezwa juu juu 30. Namwomba Mheshimiwa Waziri Mkuu aniambie maana yake tukichelewa mwaka 2008 mwaka 2009 kazi ya kubadilisha Katiba na mambo mengine itakuwa ngumu. Naomba Waziri Mkuu anisaidie taratibu na mikakati ikoje ili ahadi ile ambayo wanawake wengi wa Tanzania waliipigia CCM kwa ahadi ile itekelezeke.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe maelezo kidogo ya ufafanuzi kuhusiana na hoja aliyoitoa Mheshimiwa *Dr*. Zainab Gama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilijaribu kutoa maelezo kuonyesha jitihada za ujumla ndani ya nchi yetu kwa maana kwamba ilani iliagiza hivyo na nikaonyesha hata katika kipindi hiki hatua ambazo tumeshapiga kwa maana kwamba *SADC Countries* walitaka iwe *30 percent*. Sisi tumeshafikia na Mheshimiwa *Dr*. Zainab Gama ukanishangilia, nikasema *AU* ime-*set* kiwango hicho cha asilimia 50 ambacho na sisi ndio tumejaribu kukiahidi kwenye ilani, nikasema jambo hili linaendelea kufanyiwa kazi na nikasema yako mambo lazima vilevile tutakapokuwa tunalifikiria hilo, hivyo vikwazo navyo tuviangalie. Nikatoa mfano mmoja tu kwamba, jengo letu hili mkienda kwa *formular* ya 50, 50 kwa maana ya Majimbo tuliyonayo, hamuwezi kuenea humu ndani ya jengo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ni lazima kuwepo na kitu kingine kitakachojaribu kusema tukienda kwa utaratibu huu unafanyaje ili jengo liweze ku-*accommodate* Wabunge wote kwa *ratio* ya 50, 50.

Lakini dhamira ya Serikali iko pale pale na bahati nzuri nimekuwa ninaona hata Wabunge wakina mama wanakutana wanajaribu kuzungumza, yote ile ni katika mchakato wa kujaribu kuelekea kwenye asilimia 50 kwa 50. Sasa nilidhani maelezo yale pengine yamejitosheleza na nikadhani yangetosha. Kwa kifupi, ninaweza nikasema bado dhamira iko pale pale, lakini lazima tuangalie na vikwazo vyake ambavyo lazima tuviondoe. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa *Dr*. Zainab Gama wewe una *formular*? *(Kicheko)*

**MHE. DR. ZAINAB A. GAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, siwezi kusema nina *formular* kwa sababu nitakwenda nje ya utaratibu. Mimi ninachotaka kumwomba Waziri Mkuu ni kwamba atuthibitishie wanawake kama jambo hili litawezekana mwaka 2010 kama Katiba ilivyosema.

**MWENYEKITI:** Nadhani alichokisema Waziri Mkuu inatosha, isipokuwa nilipenda tu kusahihisha kwamba ilipokuwa ile *SADC Development Declaration* ilikuwa nchi hizo ziwe zimefika asilimia 30 mwaka 2005 na sasa baada ya hapo wote wanaelekea mwaka 2010 kwa asilimia 50, 50 ile ilikuwa tumefikia mwaka 2005 na Bunge na Serikali yetu hasa Chama cha Mapinduzi kilijitahidi kweli kufikia asiliamia 30. Sasa tafsiri, Kiswahili kina maana nyingi.

Kwa hiyo, kwa kweli isingekuwa ni juhudi ya Chama cha Mapinduzi, asilimia 30 tulikuwa hatuwezi kufikia, lakini ilifanya tukalazimisha wengine waliokuwa *number two* wakaingia *number one* katika kura za maoni. Kwa hiyo, sasa hivi dunia nzima inaelekea huko kwa asilimia 50 ifikapo 2010 na kuendelea. *(Makofi)*

**MHE. JUMA H. KILLIMBAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Nami niko hapo hapo *Vote 37 Program 10 Sub-vote 1001*.

Mheshimiwa mwenyekiti, katika mchango wangu wa maandishi nilioutoa kupitia hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, nilikuwa nimezungumzia kwamba iko barabara moja inayomilikiwa na Halmashauri. Barabara yenyewe ni ile ya Ntwike, Nsunsu, Mingela, Tulya, Doromoni, Migilango, Luoni, Kidaru kisha unapandisha unakwenda Kiomboi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara hii wakazi wanakaa kule wanakadiriwa kufikia 60,000.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU:** Taarifa!

**MWENYEKITI:** Kuhusu taarifa!

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU:** Kuhusu Taarifa. Fungu hili ni la Waziri anayehusika na Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa. Kwa hiyo, fungu analoongea Mheshimiwa Juma H. Killimbah, bado.

**MWENYEKITI:** Nami nilikuwa nataka kumwambia hivyo hivyo baadaye kwamba hii ni Ofisi ya Waziri Mkuu, barabara wala nini haviko huko.

Waheshimiwa Wabunge, nilishawaambia kwamba, tunayo mafungu mengi hapa. Ipo hii ya Waziri Mkuu kwa maana ya Ofisi ya Waziri MKuu, halafu lipo la TAMISEMI na huyu hapa hahusiki sana, utakwenda kwenye barabara ukitaka zaidi.

**MHE. JUMA H. KILLIMBAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sawa!

**MWENYEKITI:** Tunaendelea na Mheshimiwa Jacob Dalali Shibiliti.

**MHE. JACOB D. SHIBILITI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kifungu cha 37 *Program* 10 kifungu kidogo sana 250100 - Mshahara wa Waziri.

Wakati nachangia, nilizungumzia suala la jumla upande wa maji, lakini nikagusia kwamba asilimia 28 tu kwa Wilaya yetu ya Misungwi, wakati mwenendo wa nchi ni kufikia asilimia 65 vijijini na asilimia 90 mjini. Hali hii ni mbaya sana. Nilitegemea Mheshimiwa Waziri atoe tamko au mwelekeo halisi kutokana na hali hiyo ambayo ni mbaya zaidi ambayo itapelekea aidha, hospitali yetu kufungwa kutokana na hali ambayo ni mbaya mno, shule ya walemavu ya Mitindo kufungwa kwa sababu hali ni mbaya mno.

Ningependa Mheshimiwa Waziri Mkuu awaeleze kitu wananchi wa Misungwi kuhusu suala la maji, ni tatizo kubwa sana.

**MWENYEKITI:** Hawezi kueleza yeye, siyo kazi yake.

Tulipata nafasi ya kuongea kila kitu ili Waziri anayehusika aweze kupata hizo *note,* sasa mkimwuliza huyu masuala ya maji hajui! Kwa hiyo, siyo hivyo. Tunaendelea. Mheshimiwa John M. Cheyo!

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwanza kabisa, nataka kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa vile alivyojibu maswali mbalimbali na hoja mbalimbali na nilikuwa safarini, lakini nimemsikiliza kwa kina kabisa.

Jambo ambalo nataka kurejea ni juu ya Meremeta. Kwa jibu la Mheshimiwa Waziri Mkuu ametuelekeza kwamba hili jambo linahusu Jeshi. Ni kweli Meremeta ya kwanza ilihusu Jeshi, Meremeta ya pili ambayo imeendeshwa na *Task Force* ya Serikali, ambayo imekuwa *reported* na haijakanushwa katika toleo la 93 tarehe 16/4/2008 katika gazeti la Mwanahalisi, kwa mfano, mimi nazungumza tu *what is fact*.

**MWENYEKITI:** Naomba tutumie muda vizuri.

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, inaonyesha kuna fedha ambayo iko *TANGOLD* ambapo kuna *balance* ya zaidi ya Shilingi bilioni 11 ambayo imekwenda *Meremeta* na *Meremeta* hiyo inaonyeshwa katika takwimu ambazo zipo, kwamba yenyewe na hili jambo sitaki kulizungumza lakini naamini umekutana nalo. *Meremeta* ile imepokea fedha kutoka Benki Kuu na siyo hivyo tu, *Meremeta* hiyo ina Ma-*signatories* ambao hawafanani kabisa na Watanzania. Kuna akina Anthony Bura, Robert Jafferis, Ian Bevenage, Deogras Geys na watu kama hao. Sasa hao hawahusiki na Meremeta ya zamani.

Mimi ningeshauri na ningeomba Mheshimiwa anikubalie jambo hili lifanyiwe uchunguzi wa kina kwa sababu katika baadhi ya *account* hizo pameonyeshwa na imeandikwa kwamba kuna fedha takriban dola 467,000 zimeondoka *TANGOLD* iliyo na uhusiano na *Meremeta* na zimekwenda kwa *account* ya mtu ambaye ametajwa. Sasa naona kulihusisha Jeshi na *Meremeta* ya sasa sio sawa. Ni vizuri tukasema Jeshi lilipochoka na *Meremeta*, lilisema chukueni hiki kitu chenu *(Meremeta)* na Serikali ndiyo ime-*fumble* na hii *Meremeta* kiasi cha kuwa ndani humu kuna fedha ya Serikali ambayo imepotea. Kwa hiyo, hili limeulizwa pia hata na Kamati ya Madini ambayo sitaki kuingia kule.

Mimi namshauri Waziri Mkuu kuwatendea haki wananchi wa Tanzania, kama kuna Shilingi bilioni 12 *TANGOLD* na Hazina mwenyewe, tunazihitaji hizo kwa ajili ya kuchimba visima vya maji na mambo mengine. Kwa hiyo, ningependa kusikia msimamo wa Waziri Mkuu juu ya *Meremeta* ya pili, siyo *Meremeta* ya Jeshi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri wa Nchi!

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kusikia kwamba Mheshimiwa Cheyo alimfuatilia sana Mheshimiwa Waziri Mkuu wakati akitoa maelezo mafupi sana kuhusu suala zima la Meremeta, lakini yenye kutoa picha halisi kuhusu suala hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukifuatilia mchakato wa jambo hili, hakuna Meremeta ya pili, kwa kweli *Meremeta, Tangold, Greenfinance* hayo yote tunaweza kusema kwamba ni mchakato mmoja lakini kwa hatua tofauti.

Kama Mheshimiwa Cheyo amefuatilia vyema maelezo ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ni kwamba kwa kweli yeye mahali alipofikia amefungwa mikono na akasema pengine jambo hili lijadiliwe mahali hasa ikiwa ni lazima sana iwe kwenye Kamati kwa sababu *Meremeta, Tangold* na *Greenfinance,* huu ni mchakato mmoja, lakini katika hatua tofauti. Tungemwomba na tungeomba Waheshimiwa Wabunge wote watuelewe hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kwa vile ulinisaidia pale kumweleze Mheshimiwa Dr. Willbrod Slaa kuhusu namna bora zaidi ya kupata nyaraka za Serikali na mimi narejea palepale kwamba kuna utaratibu wa kupata nyaraka za Serikali. Tunafahamu kuwa Wabunge wana dhamana kubwa ya wananchi na maombi yao huwa hayapuuzwi. Kwa hiyo, tunaomba watumie utaratibu wa kawaida wa kumwendea Waziri au Katibu Mkuu ili wapate nyaraka ambazo wanazihitaji kuliko utaratibu huu uliopo.

Hapo hapo nafikiri niongezee pia kuwa Dr. Willbrod Slaa amesema kwamba Watanzania wengi wanapendelea utaratibu huu, sijui amewahesabu wangapi kwa sababu kama hii ya Bodi ya Benki Kuu ni suala la wiki moja iliyopita, sasa sijui amewahesabu wangapi. Lakini bado tunasema kwamba sio vyema kutafuta nyaraka kinyemela. Waheshimiwa Wabunge watumie utaratibu wa kawaida kuomba nyaraka na kama kuna umuhimu wa kujadili nyaraka hizi kwenye ngazi ya Kamati, basi Ofisi ya Spika na Ofisi ya Kiongozi wa Shughuli za Serikali Bungeni wataamua itakavyoonekana inafaa. Lakini kwa kweli njia sasa ambayo inatumika inatudhalilisha na siyo njia nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Kama tulielewana Mheshimiwa Cheyo, una lingine zaidi?

Kwa sababu tumesema tunayo Sheria yetu wenyewe Na.3 ya mwaka 1988 ya Haki na *Privileges* za Wabunge kwamba mambo yote yenye Ulinzi na Usalama hayatajadiliwa kwetu sisi hapa mpaka yaletewe idhini ya Mheshimiwa Rais atakayesema zungumzeni, hiyo moja.

Kama kuna *element* ya *EPA* ndani ya hivyo hiyo Kamati ambayo Rais anaishughulikia inasikia haya mnayosema. Naomba tusiendelee kubishana, maana sasa msifikiri kama Waziri alisema amefungwa, *so, what do you say*?

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu ninachosema ni kwamba hili siyo jambo la Jeshi. *This is what I am trying to say.* Hakuna *evidence* yoyote ambayo Mheshimiwa Marmo ambaye amezungumza inayotuonyesha uhusiano kati ya *Meremeta* hii na Jeshi na mimi sitaki kusoma.

Lakini kitu kimoja kwamba kama kweli wao wanaamini yaliyozungumzwa kwenye Mwanahalisi yalikuwa yanagusa mahali ambapo ni nyeti kama vile Jeshi, mbona Serikali haikukanusha jambo hili? *(Makofi)*

Ingekuwa imekanusha ikaweka ukweli ni *a, b, d* au *d* na mimi ninaushahidi wa kuonyesha kwamba hata Gavana anasema walioshiriki ndani ya *Meremeta* ya pili siyo kwa niaba ya *BOT on their person capacity* kama watu binafsi.

Kwa hiyo, ndiyo maana nasema kwamba nitaridhika kama nitaambiwa jambo hili lichunguzwe ili tupate maelezo ya kina. Lakini kuhusisha *Meremeta* ya pili na *Tangold* ni kulionea Jeshi letu la wananchi.

**MWENYEKITI:** Hilo la pili lilianza lini? Wapi utajua ya kwanza imeishia wapi na ya pili ?

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *around* 2003/2004 ndiyo mwaka ule.

**MWENYEKITI:** Halafu *reference* ya magazeti naomba isiingie ndani ya Bunge hili. Lakini ya pili, kama ni shida yetu kama ni *Meremeta, when* una-*distinguish* lini ya kwanza iliishia wapi na ya pili ilianzia wapi ? Tutajuaje?

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama Mheshimiwa Waziri anataka kupata hiyo *information* anayo *source* na anaweza akaenda hata akazungumza na *Treasury Registry has all the sources* ile ya pili iliyokuwa inaendeshwa na *Task Force* na ambayo kama unataka ninaweza kuitaja hiyo *Task Force* lakini sitaki kwenda mbali. Anajua.

Mimi kitu ambacho sitaki ni kumhusisha Waziri Mkuu kutoliambia Bunge hali halisi. Tutakuwa na Mawaziri wangapi ambao tunawaweka kitimoto hapa? Mimi afadhali kama hili jambo haliko wazi ni afadhali Serikali ikubali iende ikaliangalie hili jambo na *source* ya *information* wanazo na wanafahamu na hakuna sababu ya kutuwashawasha sisi kama vile ni makaa, watueleze tu ukweli au kama hawataki kutueleza ukweli waseme wataeleza ukweli huo katika Kamati, nitakubali. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri Mkuu.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, unajua unapofikia maeneo fulani unapata shida kidogo kusema tuseme nini. Kwa sababu *process* ya kuanzishwa kwa *Meremeta* kuna-*involve* vyombo vingi sana, ndiyo maana unakuta hakuna cha *Meremeta* moja wala mbili.

Kwa mfano, humu ndani utakuta kuna *Trinex*, kuna *DEDCO Bank*, kuna *Presidential Taskforce* unayoisema, kuna *Tangold, Deep Green Finance,* kuna *Randgold all these things together* walikuwa wana-*deal* na jambo hili moja tu. Sasa na Mheshimiwa Cheyo anasema tuambie hilo walilokuwa wana-*deal* nalo ni lipi na mimi nasema *no way, we cant do that, please*! *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Tunaendelea na Mheshimiwa Vedastusi Mathayo Manyinyi.

**MHE. VEDASTUSI M. MANYINYI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Katika hicho kifungu cha *Vote 37, Program* ya 10 *Sub-vote* ya 1001.

**MWENYEKITI:** Ninaomba Waheshimiwa Wabunge kwenye *vote* hii muendelee kusema tu kwa sababu muda huu ni mwingi.

**MHE. VEDASTUSI M. MANYINYI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kuna hii hoja niliileta kwa maandishi ambayo inataka ufafanuzi. Serikali inapokuwa imetoa ahadi kwa wananchi wake, wananchi wanakuwa na shauku kubwa ya kusubiri ile ahadi iliyotolewa na Serikali.

Sasa mimi nakumbuka mwaka jana tena ilikuwa kipindi hiki cha bajeti kuna suala ambalo tulilizungumzahumu Bungeni linalohusiana na usafiri wa baiskeli na kwa kuona umuhimu wa usafiri huo ukizingatia kwamba maeneo yetu mengi hayafikiki, mwisho Serikali ilikubali kwamba italeta sheria Bungeni ifanyiwe marekebisho na ianze kutumika na ilivyofika katika Bunge la Januari mwaka huu hoja hiyo tena ikaja, nakumbuka aliyekuwa Waziri wa Usalama wa Raia akasema kwamba hebu sasa hivi wanamalizia ule mchakato wa kuangalia maeneo mengine yamewekwaje na hatimaye iweze kuletwa hapa.

Sasa mimi ningependa kufahamu. Ukiangalia toka mwaka jana hadi leo, basi ni vizuri Mheshimiwa Waziri Mkuu angetoa tamko kwamba kwa namna ambavyo Serikali imeliona suala hilo halifai ili wananchi waweze kufahamu kuliko kila mara wanapokuwa na ahadi hiyo kwamba Bunge hili Sheria hiyo itafanyiwa marekebisho au itazungumzwa na lakini cha ajabu ni kwamba leo ni mwaka wa pili hakuna kilichoendelea.

Naomba maelezo ya Mheshimiwa Waziri Mkuu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, ningependa kutoa maelezo mafupi kuhusu maelezo ya Mheshimiwa Manyinyi, Mbunge wa Musoma Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kulikuwa na ahadi kwamba tutabadilisha Sheria ya *Traffic*, Sheria ya Usalama wa Barabarani ili kuwezesha angalau pikipiki na bajaji zitumike kama vyombo vya moto vya kubebea abiria. Mchakato wa sheria hii umefikia hatua nzuri, waraka wa Baraza la Mawaziri umeshakamilika, nadhani umeshapitishwa na Baraza la Mawaziri. Nadhani wakati wowote kuanzia sasa mabadiliko ya Sheria yataletwa hapa Bungeni kama siyo Novemba, basi mapema mwaka ujao. Tunamwomba Mheshimiwa Manyinyi pamoja na Waheshimiwa Wabunge wengine wavute subira.

**MHE. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja niliyohitaji kuizungumza naona imeshaongelewa na Waheshimiwa Wabunge wawili, nayo ni hoja ya *Meremeta.* Kwa hiyo, sina haja ya kuendelea tena.

**MHE. SHOKA KHAMIS JUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Nami nipo hapo hapo kwenye mshahara wa Waziri, lakini sina haja ya kuuchukua. Ni suala la sera.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati nilipokuwa nikichangia, nilizungumzia hapa kuhusiana na wavuvi ambao huwa wanavua katika Bahari ya Hindi na Wavuvi wale wamezuiwa kuvua kwa kutumia nyavu za *ringnet*, kuzama kwa kutumia miwani, kuzamia kwa kutumia *oxygen* pamoja kuogelea kwa viatu, halafu wamezuia na nyavu za *ringnet* zisivulie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa suala hili nilizungumza kwa urefu na nikasema kuwa litawaumiza sana wananchi wetu kwa sababu watu wetu wa sehemu za mwambao wengi wao ni wavuvi. Kwa hiyo, nikamwomba Mheshimiwa Waziri, wakati atakapofanya majumuisho atufafanulie kuhusiana na suala hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni hivyo tu.

**MWENYEKITI:** Utapata ufafanuzi katika Wizara inayohusika. Hii ni utendaji kabisa wa Wizara hiyo. Tunaendelea na Mheshimiwa Salim Hemed Khamis!

**MHE. SALIM HEMED KHAMIS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Katika mchango wangu wa maandishi nilitaka nielezwe na Serikali juu ya unyanyaswaji uliofanywa na Serikali katika Kijiji cha Chang'ombe katika zoezi zima la bomoa bomoa.

Maelezo yangu yalifanana sana na mchango wa Masoud Abdallah Salim kwa jana ambayo yeye alichangia kwa kusema, maelezo ambayo Waziri Marmo aliyaita kuwa ni tuhuma nzito na upotoshaji.

Nataka kusema kwamba, suala zima hili sio tuhuma, wala sio upotoshaji na Mheshimiwa Masoud Abdallah Salim amefanikiwa kupata nyaraka zote na vielelezo ambavyo vinaeleza kadhia hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika vielelezo hivyo tunalo jina la Balozi anayeitwa William Charles, Mama aliyekuwa na kichanga hicho anaitwa Hujat Abuu Lalu na wanakijiji wengine wawili walionyanyaswa na Polisi mmoja anaitwa Chonya Mbatiani na mwingine Patric Mpilimi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu huyo mama aliyekuwa na Kichanga tuna taarifa zake vilevile kwa urefu, tunayo taarifa ya siku aliyolazwa, aina ya *operation* aliyofanyiwa, tarehe aliyoruhusiwa kutoka hospitali, tarehe ya kutoa nyuzi, cheti cha kuzalia, kati ya Kliniki na tunayo mpaka picha ya mama mwenyewe hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa hizi zinatosha kabisa kuiarifu Serikali ili ifuatilie wahusika, sisi hatuwajibiki mpaka sasa kuwatafuta wahusika, Serikali ina mkono mrefu na ninasikitika sana kwa maelezo ya Mheshimiwa Waziri Marmo kwamba hawa hakuwaona, siamini. Hawajawatafuta na wananchi hao wapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tena maelezo ya Serikali kuhusu unyanyasaji huu uliofanywa na Serikali kwa makusudi kwa wananchi ambao hawakuwa na hatia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, napenda nitoe maelezo kuhusiana na maswali aliyouliza Mheshimiwa Salim na yale ya Mheshimiwa Masoud Salim pia kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpaka sasa hivi sisi bado tunadhani tuhuma hizi bado ni tuhuma nzito sana na ni lazima Serikali izifanyie kazi. Hii ni Serikali iliyochaguliwa na wananchi na tusingependa wananchi wanyanyaswe na vyombo vya dola na ndiyo maana jana tulipoleta taarifa hizi tuliwatuma watu wetu huko sehemu za Chang’ombe, Mbwanga na Nkuhungu kumtafuta huyo Balozi William Charles ili atuonyeshe huyu mama anayeitwa Hujat Abuu Lalu, lakini hatukuweza kuwaona wote.

Leo tulipokuwa tunajibu hoja za Waheshimiwa Wabunge, nilidhani Mheshimiwa Masoud Salim angekuwa maeneo haya kwa sababu Katibu Tarafa wa Chang’ombe alikuwa hapa ilikuwa afuatane na Mheshimiwa Masoud atuonyeshe huyo Balozi na atuonyeshe huyu mama ili angalau suala hili tulifuatilie kama kweli kulikuwa na unyanyasaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba *operation* hii ya kuokoa Mji wa Dodoma *Master Plan* yake au Mpango Kabambe

usiharibiwe, ni *operation* iliyofanyika kwa umakini sana iliyoandaliwa katika ngazi ya Mkoa, Wilaya, Kata na Tarafa.

Wakati wa *operation* alikuwepo *OCD* mwenyewe wa Dodoma na kulikuwa na *FFU* ambao muda wate walikuwa wamesimama na kuangalia kuhakikisha kwamba wavamizi wanabomoa mabanda yao na wanaondoka katika maeneo waliyoyavamia. Hakuna Askari hata mmoja aliyemkaribia mwananchi. Hizi ndizo taarifa tulizonazo na ndiyo taarifa ya Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Wilaya ya Dodoma Mjini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ndiyo maana tunataka kulifuatilia suala hili kwa karibu sana. Namwomba Mheshimiwa Mbunge hata jioni hii tuko tayari kuongozana naye tufuatane na Katibu Tarafa na Mtendaji wa Kata ya Chang'ombe kwenda kwa huyu mama au mzazi ambaye wakati huo alikuwa na kichanga cha siku 20 tumwone na pia tuwatafute hawa wanaoitwa Askari Polisi ambao majina yao yametajwa, la sivyo hatungeweza kufanyia kazi. Kutajwa tu mtu jina na Dodoma ni Mji mkubwa siyo kijiji wala Mtaa, huwezi kupiga kelele kwamba jamani Hajut Abuu Lalu yuko wapi? Nani atakuitikia?

Kwa hiyo, tunamwomba sana Mheshimiwa Mbunge na pengine Mheshimiwa Masoud kama atakuwa kwenye maeneo haya, baada ya kupindi hiki kuna Katibu Tarafa yuko hapa, Mkurugenzi Mkuu wa *CDA* yuko hapa ili tuandamane mpaka maeneo hayo tumwone huyo mama ili tulitatue hili tatizo kwa kweli ili kusiwe na tafsiri tofautitofauti baina yetu na Waheshimiwa Wabunge. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nadhani tunachokubaliana hapa kwamba hatuwezi kujibu hii kesi, kwa hiyo, tutumie nafasi ya vyombo vilivyopo na ninyi wenzetu kwa sababu mna ushahidi huo wote upatikane ili kusudi *statement* itolewe katika Bunge hili kwamba hicho kitu kilikuwepo ama hakikuwepo.

Kwa hiyo, namwita Mheshimiwa Issa Kassim Issa.

**MHE. ISSA KASSIM ISSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. *Sub-Vote 37*

**MWENYEKITI:** Endelea tu!

**MHE. ISSA KASSIM ISSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ilikuwa ni suala la umeme Zanzibar. Tulimtaka Mheshimiwa Waziri Mkuu anieleze, kwa nini Bara imepandishwa 21.7 na Zanzibar asilimia 168 na pili kuhusu habari ya mchango wangu wa maandishi na ukaweza kumsisitiza kwamba atakapokuja hapa kutoa majumuisho anieleze suala la *OIC:* Je, ule utafiti ambao uliahidiwa ulifikia wapi? Swali la kwanza.

Je, ugumu ni nini au uko wapi kuachia Zanzibar kujiunga na mradi huo kwa sababu ukienda huko itapeperusha bendera ya Tanzania. Naomba maelezo ya kina kutoka kwa Waziri Mkuu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa swali la kwanza la Mheshimiwa Mbunge kuhusu gharama ya umeme Zanzibar, tunaahidi kwamba wakati Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini atakapokuja hapa kutoa hoja yake ya bajeti, pengine atalitolea maelezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini tukumbuke kwamba masuala ya Nishati na Madini siyo masuala ya Muungano, kwa hiyo, inawezekana kabisa wenzetu wa Zanzibar kwa kuona mazingira halisi ya Zanzibar wanaweza wakapandisha *tarrif* ya umeme. Kwa hiyo, tunamwomba Mheshimiwa Mbunge avute subira.

Suala la *OIC* kwa hakika Zanzibar haiwezi kujiunga na *OIC* kwa sababu Zanzibar siyo nchi. Wananchama wa *OIC* ni nchi. Mapendekezo ya Kamati ile ilikuwa ni kwamba, iwapo kuna dhamira ya kujiunga na *OIC*, basi Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ijiunge kama nchi kwa sababu ya hali halisi ya chombo kile. Sasa baada ya Zanzibar kujitoa katika *OIC,* inaonekana hakukuwa na msukumo wowote wala umuhimu wa jambo hili kwa wakati huo.

Iwapo Mheshimiwa Mbunge atapenda kulifufua, basi tutalipeleka Wizara yetu ya Mambo ya Nje ili waanze mchakato wa kuona kama inafaa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kama nchi ijiunge na *OIC* au lah!

**MHE. ISSA KASSIM ISSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, bado nipo pale pale kwenye suala la umeme; msigune wananchi ndio wanaopata tabu.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, naomba sana mniambie mimi, maana mnajibu hata watu wakikohoa tu mnajibu.

**MHE. ISSA KASSIM ISSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la umeme Zanzibar ambayo ni sehemu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kulikuwa na kikao rasmi na makubaliano baina ya Waziri Mkuu aliyeondoka kwenye madaraka na Waziri Kiongozi wa Zanzibar kwamba, hili suala limalizike; bei iliyokubaliwa ya asilimia 21.7 iwe hiyo hiyo kwa Zanzibar. Zanzibar hawajapandisha umeme kwa gharama hii, isipokuwa *TANESCO* pamoja na *EWURA* ndiyo waliopandisha bei. Tunataka ufafanuzi ikiwa sote ni Watanzania.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo la ndugu yangu huwa wakati mwingine akizungumza naogopa kweli, ana sauti kali kweli kweli. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niseme kwamba, anachosema ni kweli; gharama zilipanda kwa upande wa Bara kwa asilimia 21.7 na Zanzibar ikaenda mpaka karibu mia moja na zaidi huko, ingawa kwa maana ya viwango vya tozo vyenyewe bado lile ongezeko linaonekana kubwa sana, lakini halikuwa kubwa unapolinganisha na tozo ya asilimia 21.7. Sasa kilichotokea baada ya kupata maelezo kutoka Serikali ya Mapinduzi

ya Zanzibar, Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete, akaagiza kwamba ni vizuri wakaendelea kulipa kama Bara; tunaelewana? Walipe asilimia 21.7, lakini ukishafanya hivyo ulikuwa unaacha pengo katika mfumo wa *bills* wa bilioni 1.5. Sasa nani anagharamia hiyo tofauti inayotokana na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, kulipa kwa asilimia hii inayofanana na ya Bara?

Kwa hiyo, tukaomba Wizara ilifanyie kazi jambo hili, baadaye tukawasilisha kwa Mheshimiwa Rais. Ikaonekana kwamba, wenye umeme ni Zanzibar, hawa wachangie zaidi kidogo kuliko sisi katika kufidia ile gharama ya 300 kwa bilioni 1.2.

Kwa hiyo, Mheshimiwa Mwenyekiti, nilichofanya nilimpelekea Waziri Kiongozi; mwenzangu unaonaje *formula* hiyo? Sijapata majibu, kwa hiyo, natarajia kwamba, atakapokuwa amerejesha maelezo yake, tutaona tunafanya nini. Ukweli ni kwamba, kwa ku-*drop* hiyo *percentage* ni lazima mtafute bilioni 1.5 na ndiyo maana nasema maadam lipo kwa Mheshimiwa Waziri Kiongozi; tufanye subira. Tunajua Tanzania hii ni moja tu na wasikivu sana, lazima kutakuwa na njia ya kuweza kulimaliza. *(Makofi)*

**MHE. OMAR S. KWAANGW':** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Nataka nipate ufafanuzi juu ya Sera za Matumizi ya Serikali. Ukisoma nyaraka za Serikali; Sera za Matumizi zinazofuatwa ni za miaka iliyopita, hata mwaka huu wamesema hazitabadilika sana. Ukiangalia Sera za Matumizi, kwa mfano, kwenye Miradi ya Maendeleo inayokwenda mpaka kule vijijini, chini ya *programmes* nyingi kama za kilimo na nini, karibu asilimia sabini zinarudi kwenye mambo ya utawala, kinachobaki pale ni kidogo mno ni kama hakuna, pale chini kwenye Sera za Matumizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile tatizo hili la kupeleka maboresho naona kama linaishia zaidi kwenye Halmashauri zetu; ni lini Serikali itahakikisha kwamba, Sera zetu za Matumizi zinaweza kujibu kwamba tupeleke mambo haya ya Utawala Bora kwa wananchi wenyewe? Wananchi nao wawe wanapewa maboresho hayo ili waweze kufahamu namna ya matumizi, kwa sababu sasa hivi wanapouliza taarifa ya fedha zinazotoka iwe Serikalini, kwenye Halmashauri au kwa Wafadhili; taarifa hazitoki. Nadhani tatizo ni Sera za Matumizi; je, Serikali inaweza ikaangalia Sera zake za Matumizi katika maeneo haya? (*Makofi*)

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyojibu asubuhi kwamba, katika Programu ya Pili ya Maboresho ya Serikali za Mitaa, tutajikita zaidi katika kuboresha Watendaji wa Vijiji, Kata mpaka ngazi ya Vitongoji, kwa hiyo, hilo linazingatiwa.

**MHE. OMAR S. KWAANGW':** Mheshimiwa Mwenyekiti, sijapata ufafanuzi wa kutosha juu ya Sera za Matumizi; asilimia nyingi ya fedha za Miradi ya Maendeleo ambazo zinapelekwa, karibu asilimia sabini au themanini zinarudi kwenye mambo ya utawala, kinachobaki pale ni kidogo. Naomba ufafanuzi wa hilo.

**MWENYEKITI:** Utawala upi huo; yaani zinarudi wapi Mkoani, Wilayani au wapi?

**MHE. OMAR S. KWAANGW':** Kwa ujumla kwenye miradi yote kwa mfano, siku hizi kuna utaratibu, fedha za miradi au miradi inajumuisha na matumizi ya kawaida. Sasa unapochanganya kwenye miradi, unapokwenda pale, karibu asilimia kubwa inarudi kwenye mambo ya utawala. Kwa hiyo, unakuta inakuja kuelezwa tu kwamba, wananchi hawa wamefundishwa habari ya kilimo bora na nini, baada ya wao kuondoka hakuna kinachobaki pale ni yale maelezo tu, lakini fedha karibu asilimia themanini zimerudi kwenye mambo ya utawala, posho na vitu vingine. (*Makofi*)

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inapopeleka fedha katika Halmashauri mbalimbali, inatoa miongozo na katika miongozo hiyo ni pamoja na asilimia gani iende katika ngazi ya kijiji au kwenye mradi na asilimia gani iwe kwa ajili ya *supervision.*

Miradi yote; *PADEP*, MMEM, MMES, *TASAF* ni asilimia kumi tu inabaki kwenye Wilaya kwa ajili ya *supervision,* asilimia tisini yote inakwenda kwenye mradi husika. Kwa hiyo, pale inabaki fedha ya *supervision* tu, hata kwenye miradi mikubwa ya barabara, sisi kama Wizara pale Wizarani inabaki asilimia kumi tu kwa ajili ya *inspection, supervision* na mambo ya *evaluation*. Kwa hiyo, hata kwenye Wilaya pia asilimia kumi ndio inabaki, Mhandisi aende kuangalia kama barabara inatengenezwa vizuri, shule inajengwa vizuri na kadhalika.

**MHE. MANJU S. O. MSAMBYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Nami nipo kwenye kasma hiyo hiyo na ninayo mambo mawili; la kwanza ni la Mahakama ya Kadhi na la pili ni la Tanzania kujiunga na *OIC*.

Waziri Mkuu, asubuhi wakati wa majumuisho ametueleza hili la Mahakama ya Kadhi, ambalo linakaribia umri wa miaka kumi na tatu tangu limeanza kuzungumzwa Bungeni humu. Akatoa mifano ya Mahakama ya Ardhi, Biashara na Kazi na wakati anaelekea kuzungumzia masuala ya barabara za Tabora akawaambia Wabunge wa Tabora, akatumia maneno ya Kiingereza, asingeweza ku-*belittle* suala la Barabara ya Tabora, ndiyo maana ameliweka kwenye makundi ya mwisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa suala hili kwanza, nilipata picha kwamba, suala la Mahakama ya Kadhi ndio liliwekwa kwenye makundi ambayo yamekuwa *belittled*. Mheshimiwa Waziri Mkuu, ametuambia hapa kwamba, hata Wakatoliki wanayo *Canon Law*. Sina matatizo na *Canon Law* ya Wakatoliki, lakini niseme Mahakama ya Kadhi inazungumzwa kwa miaka yote hii, inaundiwa Tume na Tume; bado hapa tunaambiwa tena tuachie hii Tume ya Jaji Mashuhuri Mwesiumo imalize kazi yake. Hivi hizi Mahakama nyingine ninazozitaja za Ardhi, Kazi na Biashara ziliundiwa Tume gani?

Sasa nilikuwa nataka Mheshimiwa Waziri Mkuu, atueleze kwa nini hili linasuasua, kama nilivyoeleza katika mchango wangu; suala la Mahakama ya Kadhi ni la kushughulikia masuala ya Waislam na si vinginevyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili la *OIC* nadhani Mheshimiwa Marmo …

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Msambya, *OIC* tumeshaliongea sasa hivi, haturudii Kanuni inakataa.

**MHE. MANJU S. O. MSAMBYA:** Sikuliongea mimi lakini.

**MWENYEKITI:** Hukuliongea wewe lakini limezungumzwa sasa.

**MHE. MANJU S. O. MSAMBYA:** Haya tuburuze.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri swali la kwanza.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilisema pale kwamba, nafikiri ngoja niinukuu vizuri; ukienda kwenye Ibara ya 19(2) inasema hivi: "Kazi ya kutangaza dini, kufanya ibada na kueneza dini itakuwa ni huru na jambo la hiari la mtu binafsi na shughuli na uendeshaji wa Jumuiya za Dini zitakuwa nje ya shughuli za mamlaka ya nchi." *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilichokuwa najaribu kusema ni kwamba, kama utaratibu huu tunaoufikiria unakwenda kujikita katika mfumo wa dhehebu linalohusika, kwa maana ya vyombo ndani ya utaratibu wa dhehebu hilo, watu wanaweza kuona namna gani waoanishe sheria na taratibu za rufaa mbele ya safari. Tatizo linakuwa ambapo utaratibu huo unataka kujengwa ndani ya mfumo wa Serikali, kwa maana ya kuingiza kwenye Katiba au kutunga sheria ambayo inatawala jambo ambalo kwa misingi ya sasa, inaonekana inasaidia dhehebu fulani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo nikasema katika mazingira tuliyonayo ya kuishi kindugu Waislam na Wakristo ni lazima tujitahidi kupima kwa uangalifu mambo ambayo kwa nia nzuri tu, yanaletwa Serikalini lakini mnadhani yanaweza kuwaletea hali ya kutoelewana. Kwa hiyo, nikasema utafiti utakapokamilika kwa sababu najua jambo hili linazungumzwa, ambapo hizo hisia, hiyo hali ya kutokuaminiana, hiyo hali ya kudhani kwa nini mmelifanya hili itaondoka na jambo hili linaweza kujengwa kwa utaratibu wa Kisheria na Kikatiba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana nikasema jambo hili bahati nzuri lipo kwenye Tume na nikasema basi tungoje tuone Tume itakuwa na maoni gani. Ndiyo maana nikasema kwa lugha nzito kidogo kwamba, jambo hili si dogo na wala sikuwa na maana ya kuli-*belittle* na wala ulivyo-*connect* pale sidhani kama nilikuwa na maana hiyo, *is a serious issue* kwa maana kwamba, ukilizungumza wapo wanaosikiliza, wanasema mnakwenda wapi, ndiyo maana nikasema tuwe *careful*. Naona kama vile tulivyoondoa

Mahakama za Ardhi, Kazi na Biashara, hili nalo litafika mahali litaweza kuondolewa na kutengenezewa mfumo ambao unakubalika ndani ya nchi, ndicho nilichosema. *(Makofi)*

**MHE. MANJU S. O. MSAMBYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, nilitaka kufahamu hao watu wanaosema tunakwenda wapi ni akina nani? Pili, kama wapo wanaolizungumza na tupo tunaolitaka tunapata hisia kwamba, suala hili liliwekwa kwenye Ilani ili kuomba na kutongoza kura za Waislam.

**MWENYEKITI:** Naomba uondoe maneno hayo. *(Makofi)*

**MHE. MANJU S. O. MSAMBYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naondoa, *okay*, kushawishi kura za Waislam, maana wanafikiri kusema kutongoza ni matusi si matusi ni Kiswahili safi tu.

**MHE. LUCAS L. SELELII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi, nami nipo kifungu hicho hicho na nina mambo mawili. La kwanza, namshukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa niaba ya wenzangu wa Mkoa wa Tabora, Kigoma na Rukwa, kwa jinsi alivyoiona kwa jicho zuri barabara yetu ya Itigi - Tabora – Manyoni. Namshukuru sana kwa busara hiyo aliyoitumia, ambayo na sisi tumefarijika sana na naamini Wananchi wa Tabora, Rukwa na Kigoma vilevile wamefarijika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda tu kwa sababu itasemwa kwenye Wizara ya Miundombinu nakubali, lakini najua barabara hii ya kutoka Itigi – Tabora – Ipole, tayari imeshafanyiwa *design* toka mwaka 1994 lakini katika maelezo ya Waziri Mkuu inaonekana kwamba, ndiyo tunaelekea kuifanyia *design*. Tunavyojua, tayari imeshafanyiwa *design* na *design* hiyo ipo tayari, kinachotafutwa ni pesa kwa ajili ya ujenzi wa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa swali langu katika hilo ni kwamba, kwa sababu hii barabara mwaka juzi na mwaka jana tumeizungumza sana na Wizara ilisema itakuwa ni *trunk road,* lakini katika vikao vyetu Mkoani bado haijawa *trunk road;* je, hizi fedha alizoahidi Mheshimiwa Waziri Sh. 10bn tutazipata kupitia Wizarani au kwa *RAS*; na ni *RAS* yupi wa Mkoa wa Tabora, Kigoma au Rukwa ili tuweze kufuatilia vizuri? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Ndiyo maana lita-*fit* kwenye Wizara ya Ujenzi na Mawasiliano. La pili?

**MHE. LUCAS L. SELELII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nina mawili.

**MWENYEKITI:** Lingine ni nini tena? Hebu tuendelee upesi. *(Kicheko)*

**MHE. LUCAS L. SELELII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, leo umekuwa mkali sana. Nilipochangia kwa maandishi, nilimwomba Mheshimiwa Waziri Mkuu aweze kulifafanulia Bunge lako, juu ya vipengele ambavyo vipo kwenye orodha ya Ripoti ya *Richmond* na alipokuwa anajibu alisema kwamba, ripoti hiyo ipo tayari na ataijibu. Kipo kipengele kimoja kwenye Mkataba cha *Capacity Charge,* ambacho kinaumiza sana

wananchi kwa sababu wanalipa fedha nyingi kwa makampuni haya ya jenereta kwa karibu Sh. 20bn na karibu Sh. 240bn kwa mwaka. Je, hili nalo hawezi kulifafanua tukaelewa kwamba, kipengele hicho kimeshafanyiwa kazi ili angalau wananchi waweze kupata nafuu au Serikali iweze kupata fedha za kufanya maendeleo katika kipengele cha umeme?

**MWENYEKITI:** Atajibu pamoja na taarifa yake atakayokuwa anajibu.

**MHE. CHACHA Z. WANGWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti - kuhusu utaratibu.

**MWENYEKITI:** Unatumia Kanuni gani?

**MHE. CHACHA Z. WANGWE:** Nitatumia kifungu cha 103.

**MWENYEKITI:** Soma hicho kifungu kinasema nini.

**MHE. CHACHA Z. WANGWE:** Kifungu cha 103 kinasema kwamba, hoja ya kuondoa shilingi kwenye makadirio.

**MWENYEKITI:** Ndiyo.

**MHE. CHACHA Z. WANGWE:** Na kinasema kwa kuzingatia utaratibu wa majadiliano yaliyowekwa na Kanuni hizi…

**MHE. CHACHA Z. WANGWE:** Soma Kanuni hizo zote.

**MHE. CHACHA Z. WANGWE:** **"**Kwa kuzingatia utaratibu wa majadiliano yaliyowekwa na Kanuni hizi, Mbunge yeyote anaweza kuomba ufafanuzi wa maelezo zaidi katika kifungu chochote cha fungu linalohusika, wakati kifungu hicho kitakapofikiwa na Kamati ya Matumizi."

**MWENYEKITI:** Tatizo liko wapi, ndiyo tunavyofanya sasa?

**MHE. CHACHA Z. WANGWE:** Tatizo ambalo mimi nataka kulizungumzia ni kuhusu Waziri Mkuu alivyosema kuhusu …

**MWENYEKITI:** Kuhusu nini?

**MHE. CHACHA Z. WANGWE:** Kuhusu Tarime.

**MWENYEKITI:** Hapana wewe haupo katika wale waliosimama. *(Kicheko)*

**MHE. CHACHA Z. WANGWE:** Ndiyo lakini kifungu kinaniruhusu.

**MWENYEKITI:** Hakikuruhusu. Mheshimiwa kaa chini. *(Kicheko)*

**MHE. CHACHA Z. WANGWE:** Kifungu kinaniruhusu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Chacha kifungu unachosema ndiyo haya tunayoyafanya sasa. Ilipofika *programme* ya 10 katika Ibara ya 37, ndiyo maana wenzio wote walisimama na ndio hao tunakwenda nao, wewe hukuwemo, kwa hiyo tunaendelea.

**MHE. CHACHA Z. WANGWE:** Kuhusu utaratibu. Nionyeshe hicho kifungu ambacho kinasema ni lazima wote tusimame kwa wakati mmoja. *(Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Chacha, naomba ukae.

**MHE. CHACHA Z. WANGWE:** Nionyeshe kifungu.

**MWENYEKITI:** Bahati mbaya hujui *the seriousness* ya kubishana na Kiti, *is a very serious thing*. Sasa umesema kifungu…

**MHE. CHACHA Z. WANGWE:** *I know my rights here*.

**WABUNGE:** Aaah!

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Chacha, usitufikishe mahali pabaya, nataka kukwambia bahati mbaya hujui Kanuni. Hii ningeisoma mimi ungesema nimeisoma nyingine, umesoma mwenyewe, hili zoezi tunalolifanya ndilo hili ulilosoma hapa, tutapitia kupata ufafanuzi kifungu hadi kifungu, ilipofika 37 *programme* ya 10, ambapo ni mahali pa kisera wenzio wote walisimama, tukawaorodhesha, ndiyo hawa tunaozungumza nao. Unachokisema wewe, upo *out of order*, ndiyo hiyo ninayokwambia.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 1002 – *Finance and Accounts* … … ..... ... .... Sh. 507,122,900

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 1003 – *Policy and Planning* … … … … ..... ... .... Sh. 2,122,415,000

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Chacha, hii inahusu *Policy and Planning*.

**MHE. CHACHA Z. WANGWE:** Ndiyo hicho hicho.

**MWENYEKITI:** Ndiyo!

**MHE. CHACHA Z. WANGWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nilikuwa napenda kupata ufafanuzi zaidi kwa mujibu wa Kifungu cha 103 kwamba, Waziri Mkuu kwanza, namshukuru kwa kuzungumzia Tarime na kusema kwamba, tatizo lililopo Tarime ni baya sana.

Namshukuru kwa ku-*acknowledge* hivyo, lakini sikuelewa pale alipotamka kwamba, ana mpango wa kupeleka *operation* ya kijeshi ili kuweza kutatua tatizo hilo; kwa sababu Mbunge mwenzangu wa Rorya alizungumza kwamba, ng'ombe 300 waliibiwa katika Jimbo lake wakati ambapo Waziri Mkuu hajazungumzia watu waliouawa Tarime katika kipindi hiki hiki. Watu wengi zaidi ya thelathini waliuawa na majambazi wanaoshirikiana na Polisi. Nasema hivyo kwa sababu hata Mbunge mwenzangu wa Rorya amethibitisha kwamba…

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge, naomba unisikilize; ni kifungu gani unachoki-*refer* hapa? Hii ni *Policy* sio Polisi; ni *Policy and Planning*. *(Kicheko)*

**MHE. CHACHA Z. WANGWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nafahamu umesoma kuliko mimi, maana ya *Policy* ni Sera na mimi nazungumzia suala la kisera sio Polisi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge, hapa unazungumzia Idara ndogo kabisa ya Mipango pale Waziri Mkuu. Umechelewa, wenzako walipokuwa wanauliza, pale palikuwa panamzungumzia Waziri Mkuu kwa maana ya *Policy* na nchi nzima. Sasa sio hapa, sana sana unaweza kuleta maelezo binafsi au unaweza kusubiri Wizara ya Usalama wa Raia, *that is the only place*, ulishachelewa kwenye maswali ya jumla ambapo ndiyo pangekuwa *the relevant place*, huku umechelewa.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 1004 – *Internal Audit* … … … … … … ..... ... .... Sh. 96,392,200
Kif. 1005 – *Information, Education and Communication* … … ..... ... ....… … Sh. 192,085,800
Kif. 1006 – *Procurement Management Unit* … ..... ..... Sh. 108,946,500

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 2001 – *Civil Affairs and Contingencies* … … ..... Sh. 688,062,100

**MHE. CHACHA Z. WANGWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu hiki kinazungumzia masuala ya *Civil Affairs and Contingencies*.

**MWENYEKITI:** Kinaitwa *National Festivals and Celebrations*.

**MHE. CHACHA Z. WANGWE:** *Sub-vote* 2001.

**MWENYEKITI:** Ndiyo, soma *title* yake.

**MHE. CHACHA Z. WANGWE:** *Civil Affairs and Contingencies*.

**MWENYEKITI:** Usiishie hapo tu, anza *National Festival and Celebrations, Civil Affairs and Contingencies*.

**MHE. CHACHA Z. WANGWE:** Nazungumzia kifungu cha 25100.

**MWENYEKITI:** Kifungu 25100 kinasema nini?

**MHE. CHACHA Z. WANGWE:** Kinasema *Basic Salaries and Pensionable Posts*.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge, naona hii kazi inakushinda, naomba ukae chini. Hiki hapa kinahusiana na mshahara wa msimamizi wa kitengo hicho basi. Huyu ni mtu mdogo kabisa wa kitengo hicho cha *Festivals and Celebrations* basi, siyo hayo yote.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 2002 – *National Festival*… … … … … ..... ... .... Sh. 1,509,612,400
Kif. 3001– *Parliamentary and Political Affairs* … .. . Sh. 235,884,100
Kif. 5001 – *Coordination of Government Business* … Sh. 2,720,593,000
Kif. 7001– *Government Printer* … … … … ..... ... .... Sh. 1,818,167,900

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 42 – Mfuko wa Bunge**

Kif. 1001 – *Administration and General* … … … Sh. 7,837,045,700
Kif. 2001 – *National Assembly*… … … … … .... Sh. 40,567,939,300

**Fungu 56 – Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa**

Kif. 1001 – *Administration and General* .. ... ... Sh. 2,456,740,500

**MHE. CHACHA Z. WANGWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nazungumzia *programme* 10, *Subvote* 1001 -*Administration and General*. Katika *Administration* inayoendelea Mkoa wa Mara…

**MWENYEKITI:** Nenda kwenye kifungu kidogo, maana huwezi kuongea kila kitu hapo.

**MHE. CHACHA Z. WANGWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu kidogo 250100 - *Basic Salaries and Pensionables*. Nashukuru hakuna *objection*. Katika *operation* ambayo ameizungumzia Waziri Mkuu kwamba, baada ya kuwa amesikiliza maelezo ya Mbunge wa Jimbo la Rorya ambalo ni la CCM kwamba, kuliuawa ng'ombe 300, Mheshimiwa Waziri Mkuu alisema atapeleka *operation* ya kijeshi pale.

Ninaona ni bora nijikite katika eneo la Katiba, maana hapo ndipo tulipokubaliana, tuangalie Katiba inasema nini kuhusu kutangaza hali ya hatari. Ningependa kujua kama Mheshimiwa Waziri Mkuu ana mamlaka ya kutangaza hali ya hatari kwa watu wa Tarime na kupeleka *operation* ya kijeshi, wakati Katiba katika Ibara ya 32 inatuambia kwamba; "Bila ya kuathiri Katiba hii au Sheria iliyotungwa na Bunge kwa ajili hiyo, Rais aweza kutangaza hali ya hatari katika Jamhuri ya Muungano na akishafanya hivyo, bado Katiba inamhitaji ya kwamba, Rais atatuma mara nakala ya Tangazo hilo kwa Spika wa Bunge, ambaye baada ya kushauriana na Kiongozi wa Shughuli za Serikali Bungeni, ataitisha Mkutano wa Bunge ndani ya siku zisizozidi kumi na nne, ili kuitafakari hali ya mambo na kuamua kupitisha au kutopitisha azimio litakaloungwa mkono kwa kura za Wajumbe wasiopungua theluthi mbili ya Wajumbe wote, kuunga mkono tangazo la hali ya hatari lililotolewa na Rais."

Sasa mimi ninaona ya kwamba, hatua ambazo zinachukuliwa kuhusu hali ya Tarime ambako watu wengi wamekufa siyo za Kikatiba, kwa sababu kwanza, Mheshimiwa Mbunge mwenzangu wa Rorya, alitamka bunduki ambazo zimebainika kwamba, zinafanya kazi pale ni SMG na risasi zake na hizo ni bunduki *standard* za Serikali. Kwa hiyo, inamaanisha kwamba, hizo bunduki zinatoka kwenye *armoury* za Serikali. Kwa hiyo, *investigation* ilitakiwa ifanyike kuona Polisi waliopo Mara hususan Tarime, wanahusika vipi katika kuruhusu ng'ombe waibiwe na kwenda Kenya. Polisi wa Kenya vilevile wawajibishwe kwa sababu tuna Mkataba wa Afrika Mashariki, lakini pia tuko *bound* na *International Conservation.* Tuelewe ya kwamba, hiyo *syndicate* ambayo inashirikiana na hao Polisi kuwanyanyasa wananchi ni ipi na imechukuliwa hatua gani kabla ya kutoa amri ya hali ya hatari na kupeleka Jeshi katika eneo lile kwenda kukandamiza watu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina ushahidi kwamba, juzi tu ameuawa mtu na Polisi pale bila sababu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge, jielekeze kwenye *issue*.

**MHE. CHACHA Z. WANGWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *issue* ndiyo hiyo, inaonyesha Polisi *brutality in Tarime* kwamba, watu wanaweza kufa hadi 30, lakini Mheshimiwa Waziri Mkuu hawezi kuongelea ila anaongelea ng'ombe ambao wameibiwa katika Jimbo la Rorya, anapeleka *operation* ya kijeshi.

Kwa hiyo, napenda kujua ana *mandate* gani ya kupeleka *operation* ya Kijeshi Tarime na hizo *operations* zimekuwa ni *on going, anyway* kwa sababu juzi juzi wamepeleka *operation* kwamba Kampuni ya Barrick ilikuwa inaibiwa mawe, wakapeleka Polisi kwa helikopita na magari; wakawakamata watu wengi sana na wakafanya maafa makubwa sana pale.

Sasa ningependa kujua kama hiyo ni *administration* tuliyokubaliana Kikatiba na kama siyo ni kwa nini eneo la Tarime linatangaziwa *operations almost* kila mwaka; na wakati ambapo katika maelezo niliyokuwa nayatoa kwa Serikali juzi katika Hotuba ya Waziri wa Fedha na Uchumi, Mheshimiwa Waziri Mkuu alikuwa hapa anasikiliza na ni Serikali yake angeweza kujibu pia kwamba …

*(Hapa kengele ililia kuashiria muda wa mzungumzaji kwisha)*

**MWENYEKITI:** Maelezo ya Serikali.

**WAZIRI MKUU:** Rafiki yangu Chacha Wangwe looh!

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa ni Mheshimiwa Chacha Wangwe, basi inabidi nijaribu kulieleza tena jambo hili. Nilisema kwamba, suala la mpaka ambao unagusana na Rorya na Tarime, kwa muda mrefu kumejitokeza matatizo mengi yanayohusiana au kutishia usalama wa raia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilichosema pale ni kwamba, kama Serikali, hatuwezi kunyamaza kimya. Ndiyo maana nikasema, nitapeleka timu ya wataalam mchanganyiko; Polisi, Jeshi na wengine, kushauriana ni namna gani tunaweza kusaidia kudhibiti wimbi la uhalifu unaoendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Chacha Wangwe, ndiye aliyekuja kuniambia juu ya raia wake wanaouawa kule. Sasa jambo hili nilidhani pengine angesema ninashukuru, mkienda kule angalie mpaka huo na hapa na pale. Sasa limegeuka tena limekuwa *issue* kwa Waziri Mkuu wake. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sijatangaza hali yoyote ya hatari hapa, kwa sababu mimi ni Mwanasheria na ninajua utaratibu wake. Kwa hiyo, naomba sana hili asinielewe vibaya ni kwa ajili ya kusaidia Jimbo lake, lakini vilevile Jimbo la Rorya na Wananchi wa Rorya kwa ujumla. *(Makofi)*

**MHE. CHACHA Z. WANGWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa maelezo ambayo yamenihakikishia kwamba, kumbe Waziri Mkuu anaheshimu Katiba ya Nchi. Kwa nini zoezi lile lirudiwe kwa mara ya pili, wakati Waziri Mkuu aliyeacha madaraka hivi karibuni alikuwepo kule tarehe 26 Novemba, 2006 na akazungumza na viongozi wote na tukakubaliana kwamba kuna hatua kadhaa zinazopaswa kuchukuliwa, ikiwa ni pamoja na ku- *reinforce* zile *demarcations,* pamoja na kutengeneza *rural roads* na mambo kama hayo?

Je, ile *recommendation* yake iko wapi, kwa sababu angeweza kuanzia pale, sasa hawezi kuanza *fresh* wakati yeye alifanya kazi kwa makubaliano na wananchi wote wa Tarime ambao waliafiki kwamba hizo ndizo hatua ambazo zingeweza kutatua huo mgogoro?

La pili, nilizungumzia *land issue* kwamba, *scientifically* tumekwishagundua ya kwamba ni tatizo la ugomvi wa ardhi. Ugomvi huo umesababishwa na *Policy* za Serikali za kuhamisha watu kutoka kwenye maeneo yao na kuwapeleka vijijini na baadaye kuwarudisha bila mpango. Suala hilo alipolizungumzia Mheshimiwa Waziri Mkuu katika Hotuba yake alisema ya kwamba, anawaonya wananchi ambao wanaenda kukaa katika maeneo yaliyopimwa. Mheshimiwa Waziri hajazungumzia kuhusu wananchi ambao ardhi zao zimechukuliwa na Serikali kwa nguvu na kuwasababishia upungufu wa ardhi na hatimaye kuwapa msongamano kama watu wa Tarime na hatimaye wakaanza ku-*crush* na hali hiyo ikaleta maafa. Ningependa Mheshimiwa Waziri Mkuu anipe ufafanuzi zaidi.

**MWENYEKITI:** Mnajua kama Tume itaundwa, Waheshimiwa Wabunge hamzuiliwi kwenda kuisaidia kufanya hayo unayoyasema sasa, kwa sababu hilo ulilolisema limetokea jana. Kwa hiyo, ndiyo maana Serikali imesema itaunda Tume ya Wataalam, Waheshimiwa Wabunge saidieni katika kutoa changamoto zenu. Namwita Mheshimiwa Dr. Festus Limbu.

**MHE. CHACHA Z. WANGWE:** Mwongozo wa Spika. *(Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Chacha Wangwe, Mwongozo wa nini wakati sasa hivi umekaa na nimempa nafasi Mbunge mwingine, hajaanza hata kusema wewe unataka Mwongozo juu yake. Mheshimiwa Dr. Festus Limbu. *(Kicheko)*

**MHE. DR. FESTUS B. LIMBU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia katika vifungu. *Programme 10, Sub-Vote* 1001, *item* 250100 - Mshahara wa Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni jambo la kufurahia kwamba, nchi yetu sasa imepunguza utegemezi kutoka asilimia 42 kwenda asilimia 34. Bajeti inayokwenda kwenye Mikoa kwa ajili ya Maendeleo; asilimia 80 ni fedha za wafadhili na asilimia 20 ndiyo fedha zetu za ndani. Kuna Mikoa kama Shinyanga fedha za ndani ni asilimia 12, Ruvuma fedha za ndani ni asilimia 15, Rukwa fedha za ndani ni asilimia 16 na Mwanza fedha za ndani ni asilimia 20.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nauliza Mheshimiwa Waziri akubaliane na mimi kwamba kuna haja katika bajeti ijayo, kupunguza matumizi kwenye matumizi ya kawaida ya Serikali ili yaweze kwenda kwenye Maendeleo Mikoani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU –TAMISEMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali azma yake ni nzuri sana ya kutaka kujitegemea kwa asilimia 100. Kwa hiyo, tunaenda hatua kwa hatua. Wazo lake ni zuri tunalipokea na tutalifanyia kazi, kwa sababu Serikali ina nia nzuri tu ya kuhakikisha kwamba, angalau tunajitegemea kwa asilimia kubwa. *(Makofi)*

**MHE. CHACHA Z. WANGWE:** Kuhusu utaratibu.

**MWENYEKITI:** Kifungu gani?

**MHE. CHACHA Z. WANGWE:** Kifungu cha 68.

**MWENYEKITI:** Soma.

**MHE. CHACHA Z. WANGWE:** Mbunge anaweza kusimama wakati wowote na kusema maneno kuhusu utaratibu, ambapo Mbunge yeyote ambaye wakati huo atakuwa anasema atanyamaza na kukaa chini na Spika atamtaka Mbunge aliyedai utaratibu, ataje Kanuni au sehemu ya kanuni iliyokiukwa.

**MWENYEKITI:** Sasa Kanuni iliyokiukwa ni ipi?

**MHE. CHACHA Z. WANGWE:** Imekiukwa Kanuni ya Nane inayosema, uadilifu kwa Kiongozi wa Bunge. Kwa sababu hiyo, Kanuni inasema hivi, unajua wengine wanaweza kucheka; watu wanakufa, wengine wanaweza ku-*afford* kucheka lakini *is my people who are dying. (Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Endelea bwana, nimeshasema kila saa mnam-*address* Mwenyekiti siyo watu wengine. Ni kifungu gani?

**MHE. CHACHA Z. WANGWE:** Kifungu cha nane kinasema: "Kwa kuzingatia matakwa na masharti yaliyowekwa na kiapo cha kazi zake na kwa madhumuni ya utoaji wa maamuzi na uendeshaji wa shughuli za Bunge kwa haki bila upendeleo Spika, (a) ataendesha shughuli za Bunge na kutoa maamuzi kwa haki, uadilifu na bila chuki wala upendeleo wowote, kwa kuongozwa na Katiba, Sheria za Nchi, Kanuni za Nchi, Kanuni nyingine zilizopo, maamuzi ya Maspika na Mabunge yaliyotangulia na pia kwa kuzingatia uzoefu, pamoja na mila na desturi za Mabunge mengine yanayofuata utaratibu wa Kibunge unaofanana na utaratibu wa Bunge la Tanzania."

Kwa maana hiyo, ninamaanisha ya kwamba, Mwenyekiti umemzuia Waziri Mkuu kunijibu swali langu wakati ambapo yupo hapa na mimi sikukuuliza wewe nimemwuliza yeye! Sasa hiyo inaonekana ya kwamba, unamlinda zaidi ya mahitaji. Ningependa anijibu swali langu. *(Makofi/Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge, kama tungeendesha Bunge unavyotaka wewe wala lisingefika kokote. Ukikuta Mwenyekiti anakaa hapa, anasikiliza neno hadi neno, hata vibarua vya wanaoleta hapa sisomi kwa sababu nataka kusikiliza. Hatuwezi kurudia, anasema tumeunda Kamati ya Watalaam, nikakwambia hayo unayoyasema yapeleke kwenye Kamati hiyo.

Kwa hiyo, nimekujibu; nimependelea chama gani au nani niliyempendelea? Ndiyo utaratibu na huwezi kurudia mara mbili na huu ni uamuzi wa Spika, umemalizika. Tunaendelea na Mheshimiwa Juma Killimbah. (*Makofi*)

**MHE. JUMA H. KILLIMBAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Nipo *Vote* 56, *program* 10, *subvote* 1001, *item* 250100 - Mshahara wa Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilipochangia kwa maandishi, nilitoa mchango wangu kuhusiana na suala la Barabara ya Halmashauri ile ya Twike, Sunzu, Mingela, Tulya, Dolomoni, Midilango, Luwono, Kidalu na kisha unakwenda mpaka Makao Makuu ya Wilaya, Kiomboi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimewahi kueleza mara kadhaa, toka mwaka 2006/2007 na sasa ni mwaka 2008, majibu ambayo yamekuwa yakitolewa na Waziri wa Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, kuhusiana na suala la barabara hii ambayo ina wakazi zaidi ya 60,000, ambayo inamilikiwa na Halmashauri ni palizi la ng'ombe. Sasa nataka ufafanuzi katika maelezo yangu niliyoyaandika hawajanijibu; je, wale wananchi walioko kule pamoja na sehemu ile ya biashara ya Ziwa Kitangiri, tunawasaidia vipi kuhusiana na hii barabara? *(Makofi*)

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumjibu Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo: Barabara ya Ndwike, Sekenke, Tulya hadi Kiomboi, kwa mwaka 2008/2009 imepangiwa shilingi milioni 28. Kwa mujibu wa bajeti ya hivi sasa, Wilaya ya Iramba imepangiwa shilingi 434,540,000.

Kwa hiyo, kama Mheshimiwa Mbunge anaona kwamba, hizi shilingi milioni 28 hazitoshi kwa barabara hii, naomba aende kwenye Halmashauri yake, waangalie umuhimu wa barabara hii ili katika hizi shilinig 434,540,000 waiongozee zaidi barabara hii kulingana na umuhimu wake. Sisi tukishapeleka fedha kwenye Halmashauri, wanaopanga vipaumbele ni Halmashauri yenyewe husika. Kwa kuwa Mheshimiwa Mbunge ni Mjumbe kwenye Halmashauri, naomba aishauri Halmashauri yake. Ahsante.

**MHE. JUMA H. KILLIMBAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, anachozungumza Mheshimiwa Waziri, pengine labda amekuwa akielezwa au amekuwa akipata taarifa za kuandikiwa na Mkurugenzi kutoka kule Iramba. Ninachosema ni kwamba, shilingi milioni 28 zitaisaidia nini barabara yenye mito, mabonde na inatisha?

Sasa nilichokuwa nataka kama inawezekana, kwa sababu hayo anayoyasema ya kuongea kwenye Halmashauri yote nimeshapitia na imeshindikana; ninataka kauli yake

yeye mwenyewe Waziri, anieleze kwamba hiyo barabara ina umuhimu nasema ina watu 60,000 na wale watu ni wapiga kura na walikipigia kura Chama cha Mapinduzi kikashinda. Kwa hiyo, ninachosema ni kwamba, wale watu tunawaambia nini kuhusiana na hii badala ya kusema nirudi kwenye Halmashauri, suala hili limeshindikana kwenye Halmashauri.

**MWENYEKITI:** Anaweza kujibu, kwa hiyo, ulitaka waseme kwamba hela zipo nyingi au?

**MHE. JUMA H. KILLIMBAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachotaka kwanza, aweze tu kunihakikishia maana anasema kwamba, fedha zinapelekwa zaidi ya shilingi milioni 500 za barabara; sasa nataka maelekezo yake yeye mwenyewe Waziri kwamba, hii barabara iwe ni *special case,* ipewe kipaumbele katika matengenezo. Akatoa maelekezo hayo kwamba, Mkurugenzi atafanya hivyo.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Halmashauri zote ni *full autonomy*. Sisi tukianza kuziingilia kwamba hakikisha barabara hii unaifanyia matengenezo, tutakuwa tumeingilia uhuru wa Halmashauri husika. Ndiyo maana nimesema kwamba, hata wananchi wake wananisikia kwamba, fedha tulizopanga kama wanaona ni muhimu sana na shilingi milioni 28 hazitoshi ni vyema wakazipangia fedha nyingi.

Mimi nazishauri Halmashauri kwamba, tusiwe tunapanga fedha kidogo kidogo; barabara hii milioni 50, barabara ile milioni 20 na ile milioni tano, wakati *value for money* haiwezi ikaonekana. Kwa hiyo, wao ndiyo wanaoweza kupanga kwamba, mwaka huu tutatengeneza barabara hii kwa shilingi milioni 300, tuna mifano mizuri kwa mfano Igunga, mwaka jana walikuwa na shilingi milioni 500 za barabara lakini wana daraja moja ambalo lina wakazi 100,000. Wao walichofanya wali-*sacrifice* barabara nyingine wakasema lazima tujenge Daraja la Mbutu. Kwa hiyo, Halmashauri zenyewe ndizo zinazopanga. *(Makofi*)

**MHE. DR. ZAINAB A. GAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Umesema tusirudie kusema vifungu, kwa hiyo ni kifungu hicho hicho. Katika Bajeti ya 2006/2007, niliinuka nikaulizia kuhusu utekelezaji wa Ahadi za Rais na bahati nzuri anazifahamu wakanijibu. Ahadi ya Rais ni amri watatekeleza. Kwenye Bajeti ya 2007/2008, nilichangia nikauliza amri ile imekwenda wapi mbona mpaka leo bado? Nikajibiwa tutaendelea. Safari hii Bajeti hii ya 2008/2009, Ahadi ya Rais sijaiona popote ilipoonyeshwa itatekelezwa.

**MWENYEKITI:** Ilikuwa Ahadi gani jamani?

**MHE. DR. ZAINAB A. GAMA:** Ahadi ya Rais alisema mbele ya mkutano wa hadhara kwamba, nitahakikisha Mji wa Kibaha hautakuwa maficho ya Mkoa wa Dar es Salaam, nitaleta viwanda, hiyo ahadi ya kwanza.

Ahadi ya pili, alipokuwa Rais akasema nitahakikisha barabara za Mji wa Kibaha; ahadi ya tatu alipokuja kama Rais tena akasema Kituo cha Afya cha Mkoani atahakikisha anakipa fedha ili kiweze kuwa Hospitali ya Wilaya na wakati huo huo alishangaa akasema, ninashangaa mji wenyewe upo wapi kwamba usiendelee, Rais akashangaa sisi ndiyo tukashangaa kabisa.

Sasa mimi nataka niulize, namwomba dada yangu wala sitaki kushika shilingi ni mwenzangu, aniambie Ahadi hizi zitatekelezwa lini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine namwomba dada yangu kwa sababu *speech* ya Waziri Mkuu ilikuwa nzuri sana, kuhusu masuala ya ardhi na kwangu ni mfano wa kwanza wa mgogoro unaosababishwa na matumizi mabaya ya ardhi; akasema watu wanaovamia ovyo kwangu ni mfano; je, Mheshimiwa Waziri, utakuja ili nikuonyeshe maeneo hayo na nikuonyeshe wananchi waliokuwa na mgogoro Sofu, tujue tunalimaliza namna gani tatizo hilo? Ahsante.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Ahadi za Rais zinatekelezwa kwa miaka mitano na zinatekelezwa kwa awamu. Sasa kuhusu suala lake la Barabara za Kibaha; kweli walituomba *special request* kwa ajili ya kuweka lami. Kulingana na ufinyu wa bajeti, suala lao bado tunaliangalia na bado tunalitafutia fedha. Kwa hiyo, *Kibaha Town Council* kwa mwaka huu kwenye Mfuko wa Barabara wametengewa shilingi milioni 260. Kwa hiyo, bado tunalifanyia kazi kwa sababu wameomba karibu bilioni 1.5. Ukitoa bilioni 1.5 kwa Halmashauri moja kwa kweli Halmashauri nyingine hazitapata chochote.

Kuhusu Mji wa Kibaha kupelekewa viwanda na kadhalika, hiyo ni mipango mikakati ya Wilaya husika, wengine wanatafuta wawekezaji wenyewe, siyo lazima uletewe kutoka Serikali Kuu. Najua Mheshimiwa Mbunge ni mchacharikaji mzuri sana, kwa hiyo, kama ameona kuna mwekezaji ambaye anataka kuwekeza Kibaha ni vyema tukashirikiana kuwavutia wawekezaji ili wajenge viwanda pale Kibaha.

Kuhusu suala la Hospitali, nafikiri dada yangu angeshukuru kwamba, kwa mwaka huu tumeivalia njuga Hospitali ya Tumbi ili iweze kupanuliwa na tumetenga shilingi bilioni 1.5 kwa ajili ya upanuzi wa Hospitali. Kwa hiyo, hiyo ni hatua mojawapo ya kupunguza adha ya wagonjwa kutibiwa katika hospitali au katika Mkoa wa Pwani kwa ujumla.

Kuhusu suala la viwanja, labda Mheshimiwa Dr. Gama hakubaliani na Halmashauri yake, lakini mipango yote ya viwanja katika Halmashauri ya Mji wa Kibaha vimepitishwa na vikao husika vya Mipango Miji na vimebarikiwa na Baraza la Madiwani. Sasa sijui kwa nini Mheshimiwa Mbunge hakubaliani nao? Ndio lile lile linalosema kwamba, sisi kama Serikali Kuu, tusingependa kuziingilia sana Halmashauri. Wakipanga mipango, wapange kulingana na Halmashauri husika. Sisi tusingependa kuwaingilia sana. Tunaingilia tu pale ambapo tunaona kwamba, wanakwenda kinyume cha sheria. (*Makofi*)

**MHE. DR. ZAINAB A. GAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Wakati Rais anatoa Ahadi alijua Dr. Gama yupo na wataalam wako, lakini akasema nitahakikisha. Neno "nitahakikisha" ukilibadili wananchi wa kule hawatamwelewa Rais. Naomba hilo lichukuliwe kwa uzito wake.

La pili, nasikitika sana, kama ningekuwa sikubaliani na Halmashauri yangu, Halmashauri isingekwenda kuweka alama X, imeweka alama X yule mhusika akafuta akaendelea. Mimi na Halmashauri ni kitu kimoja. Mwanasheria wetu alikwenda Mahakamani, kesi inashindwa kuendelea kwa sababu Mwanasheria yule mmemchukua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kidogo ananipa msisimko kwamba, sikubaliani na Halmashauri yangu kwenye jambo hilo, nimemwomba yeye aje tusaidiane aone yale maeneo tu atushauri. Hicho ndicho nilichomwomba na si kwamba sielewani, mimi naelewana nao sana na tunafanya kazi vizuri sana.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nikubaliane naye tu kwamba, tutakwenda kuangalia hilo suala. *(Makofi)*

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. La kwanza, tulipokuwa tunawasilisha Hotuba ya Kambi ya Upinzani, tulizungumzia sana juu ya kurekebishwa Sheria Namba Saba na Nane ambazo pia zinaainisha kazi mbalimbali za *DCs, Regional Commissioners* na mambo kama hayo.

Nataka kuulizia zaidi juu ya uhusiano kati ya Waheshimiwa Wabunge na Maafisa mbalimbali wa Halmashauri hasa Maafisa Watendaji wa Kata na Tarafa na vitu kama hivyo. Mara nyingi sana wala si katika Jimbo langu tu, unaenda kufanya ziara Afisa Kata haji, huna njia ya kumwajibisha, ukimwambia Mtendaji na yeye hachukui hatua. Sasa Serikali inasema nini juu ya hili kwa sababu Katibu Kata au Afisa Kata ni kiungo kikubwa sana cha Mbunge? Hilo la kwanza.

La pili, nimefurahia sana katika jibu lake amezungumzia juu ya kuwawajibisha watu wabovu katika Halmashauri zetu, lilikuwa jibu sahihi na hongera sana. Naona kuna tatizo, hapo katika Halmashauri inaonekana kuna ku-*recall due authority,* yaani ni kama vile tuna pande mbili; upande wa *DC* ambaye naye anaweza kutoa amri kutoka juu mpaka Kitongoji, kwa kisingizio cha Afisa Msimamizi wa Usalama. Mara nyingi hawa wanaonekana kama vile wanajuana; ni Serikali hawawajibishwi na *Director*. Isingekuwa vizuri akatamka kwamba, Watendaji wote tangu Kitongoji, Kata ukiacha Tarafa, wapo chini ya *Director* na kama *DC* ana matatizo nao ni vizuri akapitia kwa *DED.*

La mwisho, mamlaka ya kukamata. Mimi nimetoka kijijini hivi karibuni, wananchi wengi wanamsifu sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa kukemea kamata kamata ya Afisa Kata na hao Maafisa Vijiji. Wanamsifu sana kwamba, angalau sasa wanaweza wakalala wakapumzika. Tabia hii kwa *DCs* bado ipo; ni lini tutaongoza nchi yetu kwa kuwashawishi watu *rather than* Wazungu wanasema *cohesive means* kwamba

ni kamata tu, ukifanya nini haelewi yeye anasema kamata. Mimi sisemi kwamba sote ni wabaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Kamati ya *PAC,* nataka kutoa shukrani nyingi kwa vile tulivyopokelewa na *Regional Commissioner* wa Shinyanga, *DC* wa Bariadi, *DC* wa Mugumu na Maafisa wote ambao walishirikiana na Kamati. Bado kuna watu ambao hawaoni kwamba, kazi ya Mbunge ni ya maana; naomba tamko lake au msimamo wake juu ya mambo hayo. Ahsante sana.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati najibu swali langu asubuhi kuhusu majukumu ya Mkuu wa Mkoa, Mkuu wa Wilaya na Mkurugenzi wa Halmashauri, nimesema yapo wazi katika Sheria hizo ambazo Mheshimiwa Mbunge naye amezitaja na yanaendelea kubadilishwa kulingana na wakati. Kama yeye anaona kwamba, zimepitwa na wakati na zinahitaji pia kurekebishwa; tumezirekebisha mwaka 2006. Kwa hiyo, kama yeye anaona kwamba kuna kitu kinamkera anataka kubadilisha ni vyema Waheshimiwa Wabunge, tukakubaliana wakalileta hapa, sisi hatuna matatizo tunaweza tukabadilisha kama Wabunge wanaona kwamba ni wakati muafaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, Watendaji wa Kata kazi zao ni nini? Naomba niwafahamishe Waheshimiwa Wabunge kwamba, Mbunge kama anataka kwenda kwenye kazi maalum kwenye Kata Fulani, inabidi amuarifu kwanza Mtendaji wa Kata, kwamba naingia kwenye Kata yako. Mara nyingi utakuta pengine Mtendaji wa Kata hana habari kwamba, Mbunge anakuja katika sehemu yake. Hapa mara nyingi ndiyo unakuta pengine anaweza akawa amesafiri au lingine lolote linaweza likatokea. Watendaji wa Kata katika Kata zao, wanawajibika moja kwa moja kuwapokea na kuwatembeza Waheshimiwa Wabunge sehemu mbalimbali katika Kata husika, wakiwemo Waheshimiwa Madiwani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la *DC* vs *DED* kwamba, *DC* naye anatoa maagizo na kuwawajibisha Watendaji; ninachosema ni kwamba, *DC* yupo pale kwenye Wilaya kama Mwakilishi wa Rais, kama anaona Mtendaji fulani hatendi au hawajibiki vizuri, lazima atatoa agizo. Agizo lile linafanyiwa kazi na Mkurugenzi ambaye ni Mamlaka ya Nidhamu. Kwa hiyo, Mkuu wa Mkoa anaweza akaenda mahali akamkuta Mtendaji wa Kata au wa Kijiji ame-*mess up* anaagiza kwamba, huyu achukuliwe hatua za kinidhamu. Mkurugenzi ndiye anayemwajibisha yule mfanyakazi husika.

Kuhusu suala la kamata kamata na michango; nafikiri Mheshimiwa Waziri Mkuu, alitoa agizo zuri tu alisema jamani Watendaji tuangalie wakati muafaka wa kuwachangisha wananchi. Tukasema tuangalie wakati wa kuwachangisha na wakati wa mavuno; sio wakati wa njaa unamkamata mtu. Kwa hiyo, naendelea kusisitiza kauli ya Waziri Mkuu kwamba, jamani watu hao tuwachangishe kwa wakati muafaka, lakini michango ipo pale pale. Jamani, Serikali peke yake haiwezi kufanya kitu, baadhi ya vitu inabidi wananchi wachangie na mimi nawashukuru sana wananchi wetu, tukishawaelewesha mara nyingi wanatekeleza bila matatizo yoyote. Ahsante.

**MHE. OMAR S. KWAANGW':** Mheshimiwa Mwenyekiti, *Vote* hiyo hiyo na *item* 250100; kulingana na Sera ya Taifa ya Afya, kila Mkoa unapaswa kuwa na Hospitali ya Mkoa. Mkoa wa Manyara ni Mkoa ambao hauna Hospitali ya Mkoa, lakini nimeshukuru kwamba, mwaka huu fungu limetengwa kwa ajili ya ujenzi wa Hospitali ya Mkoa na katika mchango nilieleza na nilitoa shukrani hizo.

Vilevile nilieleza kwamba, tunalo tatizo la Hospitali ya Wilaya ambayo sasa imekabidhiwa Halmashauri ya Mji kuweza kubeba ule uwezo wa kuhimili wananchi wengi ambao wamekuja kwa ajili ya Mkoa wa Manyara. Kwa hiyo, nikaomba walau Serikali itenge fungu kidogo la kuiimarisha ile Hospitali. Sasa hivi akija kiongozi yeyote hata Mheshimiwa Waziri mwenyewe, hatuna *ICU* wala chumba cha maiti. Tumesema tangu mwaka jana na mwaka huu na Halmashauri yangu ya Mji imeomba. Nataka tu ufafanuzi kama Serikali ipo tayari ku-*support* katika kipindi hiki ambacho tunasubiri huo ujenzi utakapokamilika kwa sababu itakuwa miaka mingi.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli Mheshimiwa Omar Kwaangw' aliomba fedha kwa ajili ya kuiimarisha Hospitali ya Halmashauri ya Wilaya ya Mji wa Babati. Kulingana na ufinyu wa Bajeti uliopo, sasa hivi tumeshindwa kabisa kuwatengea fedha kwa ajili ya hiyo Hospitali. Hii ni kwa sababu Mkoa wa Manyara walikuwa na vitu vingi sana ambavyo wameomba kama *special request* na tumeviingiza katika Bajeti hii.

Kwa hiyo, kwenye Hospitali ya Babati tulishindwa; tumewapangia vitu vingi na Manyara Bajeti imeongezeka kutoka shilingi bilioni 11 mpaka shilingi bilioni 17 ili tumalize kujenga miundombinu ule Mkoa mbalimbali. Kwa suala la Hospitali, tulishindwa kwa sababu maombi yao yalikuwa ni mengi sana yalifikia bilioni nyingi ambayo Serikali isingeweza ku-*afford.*

**MHE. OMAR S. KWAANGW':** Mheshimiwa Mwenyekiti, naelewa *situation* ya Serikali, lakini yapo mafungu mengine kwa mfano *Basket Funds;* hayawezi kufanya hata *rehabilitation* katika maeneo fulani fulani. Hilo naomba anisaidie jibu.

Vilevile mwaka huu fedha hazijapatikana za kutosha kwa ajili ya Hospitali; je, mbona hajaeleza sasa tunakokwenda tutafanya nini? Nataka kujua haya mafungu mengine si yanaweza kusaidia hata kupunguza tatizo?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, vipaumbele vya Wilaya vinafanywa na Wilaya husika. Fedha za *Basket Fund* wanazo wao, kama wanaona kwamba kipaumbele ni ukarabati wa Hospitali hiyo, wanaweza wakatumia fedha hizo sisi hatuna matatizo yoyote.

**MHE. SALIM HEMED KHAMIS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Nataka kuongelea suala la mgogoro uliopo hivi sasa kati ya Wananchi wa Kijiji cha Nanyanje na Mkuu wa Mkoa wa Lindi. Tatizo hili ni la muda mrefu na niliwahi

kumpelekea aliyekuwa Waziri wa Elimu, Mheshimiwa Margaret Sitta, lakini ufumbuzi haukupatikana.

Katika bajeti hii suala hilo limechangiwa na Wabunge wawili; Mheshimiwa Mwanawetu Zarafi na Mheshimiwa Mudhihir, lakini kila mmoja kati ya hao alikuwa na msimamo wake. Ukweli ni kwamba, Wananchi wa Nanyanje walikubaliana kujenga shule yao ya msingi na vijiji vyote katika katika Kata hiyo vilikubaliana na mihutasari ya vikao ipo. Tatizo ni kwamba, shule hii ambayo sasa hivi ina kidato cha pili, imehamishiwa katika shule nyingine ya Chikonje bila ridhaa ya wananchi hao. Katika shule hiyo niliyoizungumza ya Nanyanje ambayo imesajiriwa rasmi na ina fedha za *TASAF,* ambazo zinahamishwa katika shule mpya ya Chikonje kuna tatizo ambalo linakua na Serikali inatakiwa kuwa na tahadhari kubwa ya tatizo hili. Hii ni kwa sababu, kadiri muda unavyokwenda, ndiyo hasira za wananchi zinakua.

Ninataka nipate mwelekeo wa Serikali kuhusu tatizo hili; ni kwa nini shule hiyo ihamishwe kwenda Chikonje wakati walikubaliana, wakahamasishana shule ikajengwa na kusajiliwa; kwa sababu ambazo hazieleweki ikapelekwa sehemu nyingine ambako wananchi wa kule hawapo tayari? Kwa hiyo, naomba nipate maelezo ya Serikali kuhusu hili ili hali isije ikabadilika baadae.

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Diwani wa Kata ya Chikonji aliwashawishi Madiwani wenzie wakaanza ujenzi wa Shule ya Sekondari ya Kata ya Chikonji katika Kijiji cha Nanyanje. Kata hii ina vijiji vingine vitatu, baada ya shule kuandikishwa ikaonekana dhahiri kwamba ni mbali sana kwa wanafunzi kutoka kwenye vijiji vyote vile kwenda kwenye Kijiji cha Nanyanje. Kwa hiyo, Kata ya Chikonji ikaamua kujenga shule ya pili ya sekondari.

Hakuna shule iliyohamishwa na zipo Kata nyingi sana hapa Tanzania ambazo zina shule za sekondari zaidi ya moja na Wizara yangu itaendelea kuziunga mkono sekondari zote hizi mbili katika Kata ya Chikonji.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 1002 - *Finance and Accounts* ... .... … … ..... Sh.296, 973,000
Kif. 1003 - *Policy and Planning Division* ... ... … … .....Sh.746, 803,200
Kif. 1004 - *Management Information Systems Division*.... … … ..... ... .... .... .... Sh.235, 424,400
Kif. 1005 - *Legal Service Division* ... ... … … ..... ... ....Sh.298, 483,400
Kif. 1006 - *Internal Audit Unit* ... ... ... … … ..... ... ....Sh.170, 600,600
Kif. 2001 - *Regional Admin. Coordination Division* .... … … ..... ... .... … … ..... ... ....Sh. 454, 560, 100
Kif. 2002 - *Local Government Coordination Division*... … … ..... ... .... … … ..... ... ... Sh. 16,966,108,600
Kif. 2003 - *Sector Coordination Division* ... .... … … Sh. 65,974,210,200

Kif. 3001- *Organization Development Division* … … Sh. 6,128,264,00

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 61 – Tume ya Uchaguzi**

Kifungu 1001 – *Administration and General* … …Sh. 11,678,741,000

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 91 – Tume ya Kuzuia Madawa ya Kulevya**

Kif. 1001 – *Administration and General* … … … … ... Sh. 1,136,100,000

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 92 - *TACAIDS***

Kif. 1001 – *Policy, Planning and National Response* … Sh. 335,900,000
Kif. 1002 – *Finance Admin and Resource Mobilization* ... … … ..... ... .... … … Sh. 2,470,157,000
Kif. 1003 – *Monitoring, Evaluation, Research and MIS* ... … … ..... ... .... … … ..... ... Sh. 235, 350,000
Kif. 1004 – *Advocacy Information Education and Comm* ….. … … ..... ... .... ..... ... Sh. 400,300,000
Kif. 1005 – *District and Community Response* … … …Sh.312,575,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Fungu 70 - Mkoa wa Arusha … … … … ... ....Sh. 40,502,916,000

*(Fungu lililotajwa hapo juu lilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Fungu 71- Mkoa wa Pwani … … … … … ..... ... ....Sh.36,233,531,000

**MHE. JUMA H. KILLIMBAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna marekebisho, amesema 36,233,531,000. Hapa inaonekana 480 lakini yeye amesema 531.

**MWENYEKITI:** Ukishaisoma ile inakuja *Less Appropriation-in-AID 51,000.* Kwa hiyo, *figure* yenyewe ni ile ya juu sio *net vote* ni *total vote*.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Fungu 72 - Mkoa wa Dodoma … … ... … .... Sh. 43,350,072,000
Fungu 73 - Mkoa wa Iringa … … … … ..... .. Sh. 53, 215,367,000
Fungu 74 - Mkoa wa Kigoma … … … … …. Sh. 39,013,000,000
Fungu 75 - Mkoa wa Kilimanjaro … … … … … Sh. 60,384,175,000
Fungu 76 - Mkoa wa Lindi… … .... … … ..... .Sh. 28,045,191,000
Fungu 77 - Mkoa wa Mara … … … … … … … . Sh. 47,586,742,000
Fungu 78 - Mkoa wa Mbeya… … … … … .... Sh. 73,098,212,000
Fungu 79 - Mkoa wa Morogoro… … ... … …. ....Sh. 54,553,902,000
Fungu 80 - Mkoa wa Mtwara … … … … ... ....Sh. 34,822,958,000
Fungu 81 - Mkoa wa Mwanza… … … … ... .... Sh. 75,926,850,000
Fungu 82 - Mkoa wa Ruvuma… … … .. ... ....Sh. 39,746,060,000

*(Mafungu yaliyotajwa hapo juu yalipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Fungu 83 - Mkoa wa Shinyanga … …. … ... Sh. 62,188,894,000

**MHE. EMMANUEL J. RUHAHULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati nachangia kwa maandishi na wakati nachingia kwa kuzungumza, nilitoa ushauri kwamba, mgawanyo wa fedha hizi uwe unafuatana na idadi ya watu. Sijui utaratibu wanaoutumia, kwa mfano, nilijaribu ku-*highlight* Mkoa wa Shinyanga na idadi yetu ni milioni 3.4.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa unazungumzia kifungu gani; *Vote 83, sub-vote* na programu gani?

**MHE. EMMANUEL J. RUHAHULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Shinyanga na nilitaka kuisemea jumla yote sijui kama nipo sahihi?

**MWENYEKITI:** Hauko sahihi, si mahali pake.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Fungu 84 - Mkoa wa Singida … … … .... ..... ... Sh.34,261,852,000
Fungu 85 - Mkoa wa Tabora… … … ... ..... .... Sh. 41,639,942,000
Fungu 86 - Mkoa wa Tanga… … … ... ...... ... Sh. 56,696,331,000
Fungu 87 - Mkoa wa Kagera … … … .... ..... .Sh. 53,374,264,000

Fungu 88 - Mkoa wa Dar es Salaam… .... ..... Sh. 60,185,390,000
Fungu 89 - Mkoa wa Rukwa… … .... ..... ...... Sh. 31,592,921,000
Fungu 95 - Mkoa wa Manyara … … … ..... ...... Sh. 32,940,284,000

*(Mafungu yaliyotajwa hapo juu yalipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**MIPANGO YA MAENDELEO**

**Fungu 27 – Msajili wa Vyama vya Siasa**

Kifungu 1001 - *Administration and General* ... ... Sh. 178,954,200

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 37- Ofisi ya Waziri Mkuu**

Kifungu 1001 - *Administration and General* ... .... Sh.5, 596,000,000
Kifungu 1003 - *Policy and Planning* … … … .. ... ... Sh. 2,417,735,904
Kifungu 1005 - *Information, Education and Comm…* … … .... ..... .... .... Sh. 90,000,000
Kifungu 2001- *Civil Affairs and Contingencies* … … Sh. 286,270,800
Kifungu 5001 - *Coordination of Government Business* … … … ..... ... .... .... ...... .... Sh. 5,257,477,700
Kifungu 7001 - *Government Printer* … … … … … Sh. 1,791,621,096

*(Vifungu viliyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 42 – Mfuko wa Bunge**

Kifungu 1001 - *Administration and General* ... ... ..Sh. 355,232,900
Kifungu 2001 - *National Assembly* … … … … … …Sh. 8,682,273,000

*(Vifungu viliyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 56 – Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa**

Kifungu 1001 - *Administration and General* . ... ... Sh. 290,000,000

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu 1003 – *Policy and Planning Division* … … … Sh. 1,512,500,000

**MHE. CHARLES N. KEENJA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Nipo kwenye kifungu kidogo cha kwanza pale 4285. Huu ni Mradi wa Jiji la Dar es Salaam na mwaka jana fedha zilitolewa.

**MWENYEKITI:** Usome huo Mradi unaitwaje?

**MHE. CHARLES N. KEENJA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, unaitwa *Dar es Salaam Rapid Transport Programme*. Mwaka jana fedha zilitolewa chini ya Jiji la Dar es Salaam kama inavyoonekana kwenye ukurasa wa 272, lakini wakati huu naona umehamishiwa Wizarani. Napenda kujua kwa nini ilitokea hivyo?

Pengine nichukue nafasi hii kukumbusha kwamba, kuna shughuli nyingine zinazofanyika Dar es Salaam ambazo vilevile zinasimamiwa na Wizara na zinatuletea madhara makubwa sana. Kwa mfano, Soko la Kariakoo na Usafiri Dar es Salaam (UDA); kwa nini Wizara hii ambayo ndiyo inasimamia *D & D* inakuwa na hii *tendency* ya ku-*centralize* baadhi ya hizi shughuli?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, natoa sababu kwa nini mwaka jana Mradi huu ulikuwa chini ya Mkoa wa Dar es Salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ilikuwa chini ya Mkoa wa Dar es Salaam kwa sababu fedha zote zilizotolewa mwaka jana, zilikuwa ni kwa ajili ya kuwafidia wananchi ambao wataathirika na Mradi huo. Mradi huu kwa sasa ni Wakala wa Serikali na utaanza mwaka huu. Kwa hiyo, Wakala wa Serikali yeyote inakuwa chini ya Serikali Kuu, ndiyo maana upo chini ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 2002 – *Local Government Coordination Division* .... ..... .... … … ..... ... .... Sh. 28, 398,003,100

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 2003 – *Sector Coordination Division* … …. …. Sh. 40,081,377,000

**MHE. SUZAN J. LYIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Nipo kwenye *Sub-Vote* 4313 na 4390. *Programme* ya *Primary Education* na ile ya *Secondary Education*, zipo pia katika Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi. Naomba kujua *operationalisation* ya hizi fedha, lakini pia nataka nipate ufafanuzi ni kwa nini *Sub-Vote*

4313 ya *PADEP* inaonekana ni 4313 lakini kwenye *Ministry of Education and Vocational Training* inaonekana kama *Sub-Vote* 4321?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha hizi za *Primary Education Development Programme* zipo katika Wizara yetu, kwa ajili ya *Supervision, Evaluation and Monitoring*.

Fedha nyingine zote za Mradi huu zimeenda moja kwa moja kwenye Halmashauri, kama atakavyoona kwenye zile Bajeti za Mikoa kuna *education transfer* hizo zinaenda kwenye Halmashauri na hizi zinabaki Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, kwa ajili ya *Coordination, Supervision* na *Evaluation*.

**MWENYEKITI:** Na zile zinakaa Wizarani; Mheshimiwa Waziri wa Elimu *if you have that?*

**WAZIRI WA ELIMU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha ambazo zipo kwenye Wizara ya Elimu kwa ajili *ya PADEP* ni zile za *Quality Assurance* kama *inspection* na kadhalika. Fedha zote hizi huwa zinapelekwa kwenye ofisi zetu zile za *Inspection* na nyingine ambazo zipo Wizara ya Elimu ni zile za *Monitoring and Evaluation.*

**MHE. SUZAN J. LYIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa ufafanuzi, lakini bado nilikuwa naomba kujua kwa nini *Sub-Vote* ya *PADEP* katika Wizara ya Elimu, inatofautiana na ile ya Wizara ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, lakini ile ya sekondari zote ni sawa, naomba nipate maelezo.

**MWENYEKITI:** Sasa hilo ni swali zito kabisa maana mpaka tutafute kile kitabu kingine tuingie huko tukaone, maana hatujaona, tumelisikia.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 3001 – *Organisational Development Division* ….. …. …. … … ..... ... .... ... Sh. 2,776,825,000

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 61 - Tume ya Uchaguzi**

Kif. 1001- *Administration and General* … …. ….. Sh. 596,362,400

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 91- Tume ya Kudhibiti Madawa ya Kulevya**

Kif. 1001 - *Administarion General* …… … ..... ... .... … … Sh. 0

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 92- *Tanzania Commission for AIDS (TACAIDS)***

Kif. 1001 - *Planning and National Response* … … Sh. 5,201,550,000

Kif. 1002 - *Finance, Admnistration. and Resource Mobilization* …. … … ..... Sh. 2,002, 399,000
Kif. 1003 - *Monitoring, Evaluation, Research and MIS* … … ..... ... .... … … ..... ... Sh. 3,801,905,000
Kif. 1004 - *Advocacy, Information, Education and Comm*. …. ….. …… … … ..... ... Sh. 3,727,050,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

Kif. 1005 - *District and Community Response* … Sh. 21,964,025,000

**MHE. DR. WILBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika *Sub-Vote* 1005, kifungu kidogo 5492 - *Tanzania Multisectoral AIDS Project*, zimetengwa shilingi 8,181,025,000; hizi ni hela nyingi; zinatakiwa kufanya kazi katika Wilaya zetu mbalimbali. Katika Bunge lako hili, umeombwa Mwongozo Maalum wa matumizi ya fedha za UKIMWI. Nikirejea kwenye maelezo aliyowahi kutoa Mheshimiwa Marmo kwamba, ukweli ni kwamba maelekezo haya hayapo kwenye taarifa mbalimbali zilizopo. Fedha hizi zinatumika visivyo na sisi tunaopita kwenye taarifa mbalimbali, tumeona kwamba, zinatumika kweli. Kwa mfano, wakati unazungumzia UKIMWI, lakini vinanunuliwa viti vya shilingi milioni moja kwenye Ofisi ya Mkurugenzi na kadhalika.

Mahali pengine pia watu wamegawana fedha, mahali pengine zinaishia kwenye semina na *workshop*, wakati yale maeneo *specific* ya UKIMWI hayaonekani; sasa je, Serikali ipo tayari fedha hizi nyingi sana ziwezi kuwafikia waathirika; watoto yatima na hasa kupata uwezekano wa kununua dawa wenyewe (wenye matatizo haya)? Serikali ipo tayari kutoa Mwongozo ulio wazi kuhusu hili, unaoeleweka kwa Watendaji Wilayani na Wabunge wapate nakala ili tuweze kufuatilia?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba nitoe maelezo kama ifuatavyo: Hapa kuna mgawanyo wa mamlaka ya kusimamia fedha hizi; *TACAIDS* ni kitabu kidogo sana ambacho kazi yake ni pamoja na kutafuta fedha

hizi, lakini zinapogawanywa kwenye Wilaya mbalimbali, mamlaka zinazohusika kufuatilia fedha hizi ni Halmashauri za Wilaya. Tukumbuke kwamba, katika Halmashauri zetu za Wilaya kuna Kamati Maalum ya Kudhibiti UKIMWI, ambayo Mwenyekiti wake ni Makamu Mwenyekiti wa Halmashauri. Kwa hiyo, tunadhani Halmashauri zinawajibika kufuatilia kwa karibu sana fedha hizi na ninaomba Waheshimiwa Wabunge, wakiwa pia ni Wajumbe wa Mabaraza haya, watusaidie kwa sababu kwa muundo wa *TACAIDS* hauna wawakilishi kwenye ngazi ya Wilaya.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, Kanuni yetu ya 104(1) inasema kwamba, iwapo zimesalia dakika kumi kabla ya kufikia muda wa kuahirisha Kikao cha Bunge na Kamati ya Matumizi bado haijamaliza kupitisha mafungu, Mwenyekiti anaweza kuongeza muda usiozidi dakika 30 bila kuihoji Kamati ili kumaliza shughuli ya kupitia mafungu yaliyobaki.

Waheshimiwa Wabunge, kwa sababu Kitabu cha Nne hatujakifikia, kwa hiyo, natumia kifungu hiki naongeza dakika 30.

**MHE. DR. WILBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ndiyo mamlaka iliyo kubwa kuliko zote. Halmashauri zetu zimetawanyika kwenye kona mbalimbali, Mabaraza ya Madiwani yanatakiwa yapewe mwongozo ili yaweze kusimamia na nimeeleza hapa. Sisi kwa niaba ya Bunge hili, ninasema hivi kwa sababu sasa nipo kwenye Kamati ya *LAAC*; ndiyo tunaosimamia na ndiyo tulioona matatizo; sasa tunapoiomba Serikali itoe Mwongozo; hivi inapata tatizo gani kukubali kwamba, itatoa Mwongozo kwa sababu tulichokuta ni kwamba hakuna Mwongozo wowote!

Halmashauri zote tulizozikagua zina matumizi mabovu. Fedha za umma zinazotakiwa kwenda kusaidia; hazisaidii. Hapa tunapoomba nia njema ya Ofisi hii inayoratibu, kwa sababu tunaongea na Waziri ambaye ndiye kazi yake kuratibu, hivi tatizo ni nini; tukisema kwamba tunaomba Mwongozo uandaliwe na ujulikane kwa Wakurugenzi, ujulikane kwa Kamati zenyewe hizo tunazoziita Kamati za UKIMWI za Wilaya; ujulikane mpaka chini na Wabunge pia wajue ili waweze kufuatilia hivi tatizo hapa ni nini. Nilifikiri ni jambo rahisi tu kwamba, tunaweza kusimamia mabilioni haya kwa urahisi kwa kutoa tu Mwongozo.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kukiri kwamba, mwanzoni hizo fedha za *AIDS* zilikuwa zinaenda Wilayani bila Mwongozo wowote, kwa sasa tunatoa Mwongozo kwa kila fedha zinazoenda kwenye Halmashauri.

Kwa hiyo, sina uhakika kwamba Ofisi yangu haikutoa Mwongozo kwenye hela hizi za *AIDS,* lakini kila fedha zinazotolewa na Serikali Kuu zikipelekwa kwenye Wilaya, zina Mwongozo Maalum. Kwa hiyo, nikubaliane tu na Mheshimiwa Mbunge kwamba, kama Mwongozo haujatolewa kwa fedha za *AIDS,* tutatoa Mwongozo huo. *(Makofi)*

**MHE. RUTH B. MSAFIRI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuuliza kuhusu *Vote 92, Sub-Vote 1005, Vote* ndogo 5495 -

*HIV/AIDS Prevention Project.* Katika *Vote* hii, moja ya eneo katika Mkoa wa Kagera ambalo lina matatizo ya athari kubwa za *UKIMWI* ni pamoja na ya Muleba,

**MWENYEKITI:** Tunazungumzia *Global Fund.*

**MHE. RUTH B. MSAFIRI:** Ndiyo Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye *HIV/AIDS Prevention Project*; pesa zinazopelekwa Wilayani. Ninachopenda kusema hapa ni kutokana na majibu ambayo ameyatoa Waziri anayehusika hivi sasa kwamba, pesa zinazotolewa zinazokwenda Wilayani, zamani walikuwa hawatoi Mwongozo.

Naomba sasa watoe Mwongozo kwa sababu ndani ya maeneo yanayotakiwa, watakapokuwa wamepeleka Mwongozo wapeleke pamoja na maeneo yanayotakiwa kufikiwa elimu hii. Maeneo haya ni pamoja na visiwa vyangu nilivyonavyo, ambavyo kuna Kata mbili za Kiserikali, kuna vijiji vinane vya Kiserikali, lakini kote huko hawajawahi kupata elimu hii na athari hii inaendelea kuwa kubwa. Kwa hiyo, nilipenda niliseme hilo ili wanapotoa Mwongozo wazingatie hayo maeneo, kwa sababu nimekuwa nikifuatilia *TACAIDS* lakini mara zote nimekuwa sipati majibu sahihi.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyokwishajibu, nasema ushauri huo tunauzingatia na tutahakikisha kwamba, tunatoa miongozo kwa fedha zote za aina hiyo.

*(kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Fungu 70 - Mkoa wa Arusha … … … … ..... ... Sh. 17,243,981,000
Fungu 71 - Mkoa wa Pwani … … … … ….. ....Sh. 14,707,072,000
Fungu 72 - Mkoa wa Dodoma … … ..... ... ....Sh.18,736,714,000
Fungu 73 - Mkoa wa Iringa … … … ..... ... ...Sh.20,309,699,000
Fungu 74 - Mkoa wa Kigoma … … … … ... ....Sh. 16,856,566,000
Fungu 75 - Mkoa wa Kilimanjaro … … …... ... Sh. 17884582000
Fungu 76 - Mkoa wa Lindi … … … … … ..... ... ....Sh.13,158,634,000

*(Mafungu yaliyotajwa hapo juu yalipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Fungu 77- Mkoa wa Mara … … … … … ..... ... ....Sh.18,933,133,000

**MHE. CHACHA Z. WANGWE:** Ahsante Mheshimiwa Mwenyekiti. Nipo katika *Vote* 77, *Sub-Vote* 1001 - *Administration and General*.

**MWENYEKITI:** *Sub-Vote* 1001 halafu *item* namba ngapi?

**MHE. CHACHA Z. WANGWE:** 6532 - *Self Help Scheme*. Ningependa nipate ufafanuzi; kwa nini Serikali imeweka vizuizi ili nafaka zisiende katika Wilaya ya Tarime na Rorya kwa sababu sasa hivi tunaelewa kwamba Katiba …

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Chacha Wangwe, naomba sana tunapoingia kwenye vifungu *we are talking about an item* tunayoipitisha. Hapa ni *Self Help Scheme,* sasa inahusiana vipi na ni shilingi milioni 20 tu halafu ipo chini ya *administration*? Wewe ungeuliza hiki kifungu maana yake ni nini, halafu atakapokujibu swali la pili ndiyo utauliza hicho unachotaka kuuliza kama kitakuwa *relevant*.

**MHE. CHACHA Z. WANGWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, labda *interpretation*, kwa sababu *Self Help Scheme* ninavyo-*interpret* mimi ni jinsi Wananchi wa Mara wanavyojisaidia katika maisha yao. Kwa hiyo, nataka nipewe *explanation* kwa nini wanawazuia kupata chakula?

**MWENYEKITI:** Wewe waulize hiki kifungu maana yake nini.

**MHE. CHACHA Z. WANGWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimekubali wanieleze maana …

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *Self Help Scheme* ni fedha za maendeleo ambazo Mkuu wa Mkoa akienda kutembelea katika Miradi mbalimbali na wananchi wanahitaji msaada, anaweza akajitolea mifuko kumi ya simenti, mabati au vitu vingine vyovyote ambavyo ni katika Miradi ya Maendeleo.

**MHE. CHACHA Z. WANGWE:** Sawa kabisa na hiyo ndiyo ninayomaanisha.

**MWENYEKITI:** Hapana, hapana, Mheshimiwa unaitwa kwanza. *(Kicheko)*

**MHE. CHACHA Z. WANGWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti nakushukuru. Naona hicho kifungu ni *relevant* kwa sababu namzungumzia Mkuu wa Mkoa, ambaye alitoa amri tarehe 14 Juni, 2008, akipiga marufuku nafaka kwenda katika Wilaya za Tarime na Rorya.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa siyo *relevant* kabisa, tatizo huelewi; hapa tupo kwenye *development* hatupo kwenye sera. Wenzako walipokuwa wanauliza kwenye Mshahara wa Waziri wa Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, yote haya ungeyauliza. Kwa hiyo, hapa si mahali pake, kumbuka kwamba kuna vifungu vile vinavyosema Mshahara wa Waziri, tunamwajibisha Waziri kwa nafasi yake, kwa hiyo, hili ungeliuliza kwa wakati ule ungeruhusiwa.

**MHE. CHACHA Z. WANGWE:** *Message sent.* *(*K*icheko)*

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati*

*ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Fungu 78 - Mkoa wa Mbeya … … … … … …Sh. 24,281,039,000
Fungu 79 - Mkoa wa Morogoro … … … … … Sh. 19824634000
Fungu 80 - Mkoa wa Mtwara … … … … … …Sh.13,208,014,000
Fungu 81 - Mkoa wa Mwanza … … … … … …Sh.28,538,228,000
Fungu 82 - Mkoa wa Ruvuma … … … … … …Sh.15,560,134,000
Fungu 83 - Mkoa wa Shinyanga … … … … … Sh. 28,103,250,000
Fungu 84 - Mkoa wa Singida … … … … … …Sh.14,416,984,000
Fungu 85 - Mkoa wa Tabora … … … … … …Sh.18,357,819,000
Fungu 86 - Mkoa wa Tanga … … … … … …Sh.20,518,262,000
Fungu 87 - Mkoa wa Kagera … … … … … …Sh.22,946,136,000
Fungu 88 - Mkoa wa Dar es Salaam… … … … …Sh. 14,038,082,000
Fungu 89 - Mkoa wa Rukwa … … … … … …Sh.14,725,503,000
Fungu 95 - Mkoa wa Manyara … … … … …Sh.17,344,943,000

*(Mafungu yaliyotajwa hapo juu yalipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

*(Bunge lilirudia)*

**T A A R I F A**

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa Taarifa kwamba, Kamati ya Matumizi baada ya kujadili taarifa ya Mapitio na Mwelekeo wa Kazi za Serikali, imeyapitia Makadirio ya Matumizi ya Fedha za Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa na Asasi zilizo chini yake na yale ya Ofisi ya Bunge, kwa Mwaka wa Fedha wa 2008/2009, kifungu kwa kifungu na kuyapitisha bila mabadiliko. Hivyo basi, naomba sasa Bunge lako Tukufu liyakubali Makadirio haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

**WAZIRI WA MAENDELEO YA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Makadirio ya Matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu na Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kwa Mwaka 2008/2009 yalipitishwa na Bunge)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kwa hatua hii, sasa tumemaliza kazi ya kupitia vifungu kwa vifungu. Kwa hiyo, Ofisi ya Waziri Mkuu, pamoja na *Vote*s zote zilizopitiwa; wamekubaliwa Matumizi yao, ninawapongeza.

Kwa kuwa tunao Wakuu wa Mikoa hapa ni vizuri wamesikia na kama tunavyosema, sasa hivi Kamati za Bunge zipo tatu zinaitwa *Watchdog Committees*, zinaingia kwa undani kabisa; tuna Kamati ya Hesabu za Serikali, Kamati ya Hesabu za Serikali za Mitaa na Kamati ya Mashirika ya Umma.

Kwa mujibu wa mabadiliko ya Kanuni zetu, Kamati hizi sasa zinaongozwa na Kambi ya Upinzani. Kwa hiyo, tumeongeza nguvu za *accountability*, msije mkakuta mnapata matatizo kama matumizi ya fedha hizi yatakuwa katika utaratibu ambao si wenyewe.

Kwa hiyo, ni vizuri mfahamu hivyo; Bunge sasa hivi limejipanga vizuri, halitaacha kitu chochote kitakachokuwa hakifanani na *value for money*. Mategemeo yetu ni kwamba, hiyo kazi mtaifanya vizuri.

Waheshimiwa Wabunge, kama tulivyosema kwa vifungu vingine, kwa mtu yeyote anayependa kujiandaa vizuri, atumie Kanuni zetu vizuri. Ukitumia vyema Kanuni, utakuwa katika nafasi nzuri ya kuweza kuhoji na kutaka ufafanuzi vizuri.

Zipo nafasi nyingi mpaka na kuondoa shilingi ambayo hamjawahi kuitumia, lakini ni lazima kuwe na maandalizi mazuri. Usisimame hapa ndani ukafikiria, ni lazima Kanuni iangaliwe vizuri na kufuata utaratibu kama inavyostahili.

Waheshimiwa Wabunge, sina shughuli nyingine, kesho kuna semina saa 3.00 asubuhi, nafikiri Ukumbi wa Msekwa na jioni kutakuwa na tafrija ya Usiku wa Zanzibar.

Baada ya kusema hivyo, naahirisha Bunge mpaka Siku ya Jumatatu, Saa Tatu Asubuhi.

*(Saa 02.08 usiku Bunge liliahirishwa mpaka Siku ya Jumatatu, Tarehe 30 Juni, 2008, Saa Tatu Asubuhi)*